KISA
CHA
UKOMBOZI
Safari ya neema, dhabihu, na ushindi
wa milele katika Kristo.
Kwa maana jinsi hii
Mungu aliupenda ulimwengu,
hata akamtoa Mwanawe pekee,
ili kila mtu amwaminiye asipotee,
bali awe na uzima wa milele."
YOHANA 3:16
MaarifaMtandaoni.com
RohoYaUnabii.Org

Tunamshukuru Mungu kwa kuwezesha kazi, pia tunawashukuru, Wasomaji,Watafsiri, Wahariri, Wahakiki, Wanaufundi, na

Wote wanaochangia kazi hii kwa maombi , hali na mali Wana ufundi, wahariri na wengineo, kimetafsiriwa kutoka The REDEMPTION STORY na ROHOyaUNABII.Org

1. Nhandi Masunga-Bariadi, Tanzania
2. Emmanuel Oola-Rorya, Tanzania
3. Daniel Masaka-Kisii, Kenya
4. Sharon Ondieki -Nairobi, Kenya
5. Judi Mmari Mugane-Siha, Tanzania
6. John Mugane-Boston, Marekani
7. David Masaka-North Carolina, Marekani
8. Sandra Barron-North Carolina, Marekani

Mbarikiwe, Grace Momadi-Masaka-Jersey, Marekani 1st Edition, 2026 Jersey, Marekani

KISA CHA UKOMBOZI

KISA CHA UKOMBOZI

YALIYOMO

I. **SURA YA 1—ANGUKO LA LUSIFA 3**

II. **SURA YA 2—UUMBAJI.....8**

III. **SURA YA 3—MATOKEO YA UASI 14**

IV. **SURA YA 4—MAJARIBU NA ANGUKO 22**

V. **SURA YA 5—MPANGO WA WOKOVU 32**

VI. **SURA YA 6—KAINI NA ABELI NA SADAKA ZAO 42**

VII. **SURA YA 7—SETHI NA HENOKO 47**

VIII. **SURA YA 8—GHARIKA 52**

IX. **SURA YA 9—MNARA WA BABELI 62**

X. **SURA YA 10—IBRAHIMU NA UZAO WA AHADI 64**

XI. **SURA YA 11—NDOA YA ISAKA 73**

XII. **SURA YA 12—YAKOBO NA ESAU 76**

XIII. **SURA YA 13—YAKOBO NA MALAIKA 83**

XIV. **SURA YA 14—WANA WA ISRAELI 89**

XV. **SURA YA 15—NGUVU ZA MUNGU ZILIZOFUNULIWA 101**

XVI. **SURA YA 16—KUONDOKA KWA ISRAELI UTUMWANI 108**

XVII. **SURA YA 17—SAFARI ZA ISRAELI 115**

XVIII. **SURA YA 18—SHERIA YA MUNGU 125**

XIX. **SURA YA 19—PATAKATIFU 139**

XX. **SURA YA 20—WAPELELEZI NA RIPOTI YAO 146**

XXI. **SURA YA 21—DHAMBI YA MUSA 152**

XXII. **SURA YA 22—KIFO CHA MUSA 157**

XXIII. SURA YA 23—KUINGIA KATIKA NCHI YA AHADI 162

XXIV. SURA YA 24—SANDUKU LA MUNGU NA HATIMA YA ISRAELI 170

XXV. SURA YA 25—UJIO WA KWANZA WA KRISTO.....183

XXVI. SURA YA 26—HUDUMA YA KRISTO 189

XXVII. SURA YA 27—KUSALITIWA KWA KRISTO.....195

XXVIII. SURA YA 28—JARIBIO LA KRISTO 200

XXIX. SURA YA 29—KUSULUBIWA KWA KRISTO 207

XXX. SURA YA 30—UFUFUO WA KRISTO.....216

XXXI. SURA YA 31—KUPAA KWA KRISTO 226

XXXII. SURA YA 32—PENTEKOSTE 228

XXXIII. SURA YA 33—UPONYAJI WA KIWETE.....235

XXXIV. SURA YA 34—UAMINIFU KWA MUNGU CHINI YA MATESO 241

XXXV. SURA YA 35—MPANGILIO WA INJILI.....246

XXXVI. SURA YA 36—KIFO CHA STEFANO.....249

XXXVII. SURA YA 37—KUONGOKA KWA SAULI.....255

XXXVIII. SURA YA 38—HUDUMA YA AWALI YA PAULO 263

XXXIX. SURA YA 39—HUDUMA YA PETRO 268

XL. SURA YA 40—PETRO AOKOLEWA KUTOKA GEREZANI 279

XLI. SURA YA 41—KATIKA MAENEO YA NGAMBO 288

XLII. SURA YA 42—MIAKA YA HUDUMA YA PAULO ….....297

XLIII. SURA YA 43—USHAHIDI KIFO CHA PAULO NA PETRO 302

XLIV. SURA YA 44—UASI MKUU 307

XLV. SURA YA 45—SIRI YA KUASI 312

XLVI. **SURA YA 46—WANAMATENGENEZO WA AWALI 321**

XLVII. **SURA YA 47—LUTHER NA MATENGENEZO MAKUU 326**

XLVIII. **SURA YA 48—KUENDELEA KWA MATENGENEZO.....332**

XLIX. **SURA YA 49—KUSHINDWA KUSONGA MBELE 339**

L. **SURA YA 50—UJUMBE WA MALAIKA WA KWANZA.....342**

LI. **SURA YA 51—UJUMBE WA MALAIKA WA PILI.....350**

LII. **SURA YA 52—KILIO CHA USIKU WA MANANE.....355**

LIII. **SURA YA 53—PATAKATIFU.....361**

LIV. **SURA YA 54—UJUMBE WA MALAIKA WA TATU.....365**

LV. **SURA YA 55—JUKWAA IMARA 370**

LVI. **SURA YA 56—UDANGANYIFU WA SHETANI 373**

LVII. **SURA YA 57—UMIZIMU 378**

LVIII. **SURA YA 58—KILIO KIKUU.....384**

LIX. **SURA YA 59—KUFUNGWA KWA MLANGO WA REHEMA 387**

LX. **SURA YA 60—WAKATI WA TAABU YA YAKOBO 391**

LXI. **SURA YA 61—UKOMBOZI WA WATAKATIFU 394**

LXII. **SURA YA 62—TAJI KWA WATAKATIFU 398**

LXIII. **SURA YA 63—MILENIA** **400**

LXIV. **SURA YA 64—UFUFUO WA PILI 403**

LXV. **SURA YA 65—KUTAWAZWA KWA KRISTO 406**

LXVI. **SURA YA 66—MAUTI YA PILI 412**

LXVII. **SURA YA 67—DUNIA MPYA.....415**

SURA YA 1–ANGUKO LA LUSIFA

Lusifa mbinguni, kabla ya uasi wake, alikuwa malaika mkuu na aliyeinuliwa, anayefuatia kwa heshima ya Mwana mpendwa wa Mungu. Uso wake, kama wa wale malaika wengine, ulikuwa mpole na wenye kuonyesha furaha. Paji la uso wake lilikuwa juu na pana, likionyesha akili yenye nguvu. Umbo lake lilikuwa kamilifu; mwonekano wake adhimu na wa fahari. Nuru ya pekee ilimulika kwenye uso wake na nuru hii ilipomulika kumzunguka, ilikuwa na uzuri zaidi kuliko ilivyowazunguka malaika wengine; lakini Kristo, Mwana mpendwa wa Mungu, alikuwa na ukuu juu ya jeshi lote la malaika. Alikuwa Umoja na Baba kabla ya malaika kuumbwa. Lusifa alimwonea wivu Kristo, na polepole akajitwalia mamlaka ya kutoa amri na maagizo ambayo yalikuwa juu ya Kristo pekee. **{SRSw 13.1}**

Muumba mkuu alikusanya jeshi lote la mbinguni, ili apate kumtunukia heshima ya pekee Mwana Wake mbele ya malaika. Mwana alikuwa ameketi juu ya kiti cha enzi pamoja na Baba, na umati wa malaika watakatifu wa mbinguni ulikusanyika kuwazunguka. Kisha Baba alijulisha mkutano huu kwamba Yeye Mwenyewe aliamuru kwamba Kristo, Mwanawe, awe sawa na Yeye Mwenyewe; ili kwamba popote palipokuwa uwepo wa Mwanawe, palikuwa kama uwepo Wake Mwenyewe. Neno la Mwana lilipaswa kutiiwa kwa utayari kama Neno la Baba. Alikuwa amemkabidhi Mwanawe, mamlaka ya kuamuru jeshi la mbinguni. Hasa, Mwana Wake alipaswa kufanya kazi katika muungano pamoja Naye katika uumbaji uliotazamiwa wa dunia na kila kiumbe kilicho hai ambacho kingepaswa kuwepo juu ya dunia. Mwanawe angetimiza mapenzi Yake na makusudi Yake lakini hangefanya jambo lolote peke yake. Mapenzi ya Baba yangetimizwa ndani Yake. **{SRSw 13.2}**

Lusifa alimwonea wivu na kijicho Yesu Kristo. Hata hivyo, wakati malaika wote walipopiga magoti mbele ya Yesu kukubali na kukiri kwamba alikuwa Mkuu wao, na Mwenye mamlaka ya juu na mtawala halali, yeye pia alipiga magoti pamoja nao; lakini moyo wake ulikuwa umejaa wivu na chuki. Kristo alikuwa ameshirikishwa katika mashauri ya siri ya Mungu kuhusu mipango Yake, ilhali Lusifa hakufahamishwa mipango hiyo. Hakuielewa, wala hakuruhusiwa kujua makusudi ya Mungu. Lakini Kristo alitambuliwa na kukubaliwa kama mkuu Mwenye Enzi Kuu wa mbinguni, akiwa na uwezo na mamlaka yaliyo sawa na yale ya Mungu Mwenyewe. Lusifa alijiona mwenyewe kuwa malaika kipenzi, yaani aliyependwa sana mbinguni miongoni mwa malaika. Alikuwa amepewa cheo cha juu sana, lakini jambo hilo halikumfanya awe na moyo wa shukrani wala kumtukuza Muumba wake. Badala yake, alipania kufikia cheo cha Mungu Mwenyewe. Aliitukuza nafasi yake ya juu. Alijua kwamba malaika walimheshimu sana. Alikuwa amepewa utume jukumu la kutekeleza utume maalumu. Alikuwa karibu sana na Muumba Mkuu, na miale ya nuru ya utukufu isiyokoma, iliyomzunguka Mungu wa milele ilikuwa ikimwangazia kwa namna ya pekee. Alikumbuka jinsi malaika walivyotii amri zake kwa hiari na kwa furaha. Je, mavazi yake hayakuwa na mng'ao na ya kupendeza? Kwa nini basi Kristo apewe heshima kubwa kuliko yeye? **{SRSw 14.1}**

Aliondoka karibu na uwepo wa Baba akiwa hajaridhika na akiwa amejaa wivu dhidi ya Yesu Kristo. Akiyaficha makusudi yake halisi, aliwakusanya jeshi la malaika. Alianza kuzungumzia jambo lililomhusu yeye mwenyewe. Kama yule asiyekuwa na furaha, aliyeumia moyoni na mwenye chuki moyoni, alieleza jinsi Mungu alivyompa Yesu upendeleo/kipaumbele na kumpuuza yeye. Aliwaambia kwamba tangu wakati huo uhuru mtamu ambao malaika walikuwa wamefurahia ulikuwa umefikia mwisho. Kwa maana je, hawakuwa wamewekewa

mtawala ambaye tangu hapo walipaswa kumpa heshima ya utumwa? Aliwaambia kwamba alikuwa amewaita ili kuwahakikishia kwamba hatakubali tena, kuvamiwa kwa haki zake na zao; kwamba hatasujudu tena mbele ya Kristo kamwe; kwamba angejichukulia heshima ambayo ilipaswa kupewa yeye, na kwamba angekuwa kamanda/kiongozi wa wote ambao wangekubali kumfuata na kutii sauti yake. **{SRSw 14.2}**

Kulikuwa na mabishano na kutoridhika miongoni mwa malaika. Lusifa na wale waliomuunga mkono walikuwa wakijitahidi kufanyia matengenezo utawala wa Mungu. Walikuwa hawajaridhika na hawakuwa na furaha kwa sababu hawakuweza kuichunguza hekima ya Mungu isiyochunguzika wala kuelewa makusudi Yake ya kumtukuza Mwana Wake na kumpa mamlaka na uwezo usio na mipaka. Waliasi dhidi ya mamlaka ya Mwana. **{SRSw 15.1}**

Malaika waliokuwa waaminifu na wakweli walijaribu kumrudisha malaika huyu mkuu mwenye uasi kwenye mapenzi ya Muumba wake. Walitetea na kuhalalisha tendo la Mungu la kumpa Kristo heshima, na kwa hoja zenye nguvu walijaribu kumshawishi Lusifa kwamba hakuwa amepungukiwa heshima yoyote aliyokuwa nayo hapo awali, hata baada ya Baba kutangaza heshima aliyompa Mwana Wake. Walieleza wazi kwamba Kristo alikuwa Mwana wa Mungu, aliyekuwapo pamoja Naye kabla malaika hawajaumbwa; na kwamba daima alikuwa amesimama upande wa kulia wa Mungu. Mamlaka Yake yenye upole na upendo haikuwa imewahi kutiliwa shaka hapo awali; na kwamba Hakuwa ametoa amri yoyote ambayo jeshi la mbinguni halikufurahia kutimiza. Walimsihi kwamba, kwa Kristo kupokea heshima maalumu kutoka kwa Baba mbele ya malaika hakukuondoa heshima ambayo Lusifa alikuwa amepewa hapo awali. Malaika walilia machozi. Kwa shauku walijaribu kumshawishi Lusifa akane/aachane na mpango wake mbaya na ajisalimishe kwa Muumba wao; kwa maana hadi wakati huo kila kitu

kilikuwa katika amani na maelewano, na ni nini kingeweza kusababisha sauti hii ya kutokubaliana, upinzani na uasi? **{SRSw 15.2}**

Lusifa alikataa kusikiliza. Kisha akawageukia wale malaika waaminifu na wakweli, na kuwashutumu kuwa ni watumwa. Malaika hao waliokuwa waaminifu kwa Mungu walibaki wakishangaa walipoona kwamba Lusifa alikuwa amefanikiwa katika juhudi zake za kuchochea uasi. Aliwaahidi serikali mpya na bora zaidi kuliko ile waliyokuwa nayo wakati huo, ambayo ndani yake wote wangekuwa na uhuru. Idadi kubwa ya malaika walionyesha nia yao ya kumkubali Lusifa kama kiongozi na mkuu wao. Alipoona kwamba juhudi zake zilikuwa zikifanikiwa, alijisifu moyoni mwake kwamba bado angeweza kuwaleta malaika wote upande wake, na kwamba angekuwa sawa na Mungu Mwenyewe, na sauti yake ya mamlaka ingesikika ikiamuru jeshi lote la mbinguni. Malaika waaminifu walimwonya tena na kumweleza matokeo ambayo yangempata ikiwa angeendelea na njia hiyo; kwamba Yeye aliyewaumba malaika alikuwa na uwezo Wake kuangusha mamlaka yao yote na kuwaadhibu kwa namna ya pekee kwa ujasiri wao na uasi wao mkubwa. Wazo kwamba malaika (kiumbe) angeweza kupinga sheria ya Mungu ambayo ilikuwa takatifu kama Mungu Mwenyewe ni jambo la kushtua! Waliwaonya waasi wazibe masikio yao dhidi ya hoja za udanganyifu za Lusifa, na wakamshauri yeye pamoja na wote walioathiriwa naye wamwendee Mungu na kukiri kosa lao, na hata tu kukiri lile wazo la kuihoji mamlaka Yake. **{SRSw 16.1}**

Wengi wa wale waliomuunga mkono Lusifa, na hata kumwonea huruma, walikuwa tayari kusikiliza ushauri wa malaika waaminifu, na kutubu kwa kutoridhika kwao, na kupokelewa tena na kuaminiwa na Baba na Mwana Wake mpendwa. Lakini mwasi huyo mkuu akatangaza kwamba alikuwa anaijua sheria ya Mungu, na kwamba ikiwa angejitiisha katika utiifu wa kitumwa, heshima yake ingeondolewa.

Alisema kwamba asingepewa tena utume wake mkubwa (mission). Aliwaambia kwamba yeye pamoja nao, tayari walikuwa wamekwenda mbali sana kiasi kwamba wasingeweza kurudi nyuma, na kwamba angekabiliana na matokeo yake; kwa maana kamwe asingesujudu kwa ibada ya utumwa mbele ya Mwana wa Mungu. Alisema Mungu asingewasamehe, na sasa walipaswa kudai uhuru wao na kutwaa kwa nguvu nafasi na mamlaka ambayo hawakupewa kwa hiari. [Hivyo ndivyo ilivyokuwa kwamba Lusifa, “mbeba nuru,” Kiumbe aliyeshiriki utukufu wa Mungu na aliyekuwa mhudumu wa kiti Chake cha enzi, akawa Shetani kwa kuvunja sheria, “adui.” [wakati Mungu anaitunza sheria Yake Mwenyewe]— **Patriarchs and Prophets, 40.]** **{SRSw 16.2}**

Malaika waaminifu waliharakisha kwenda kwa Mwana wa Mungu na kumjulisha kuhusu yaliyokuwa yakitokea miongoni mwa malaika. Walimkuta Baba akiwa katika mashauri pamoja na Mwana Wake mpendwa, wakitafuta njia ambayo ingeleta ufumbuzi wenye msaada na faida zaidi kwa malaika waaminifu, kwamba mamlaka iliyotwaliwa bila ruksa na Shetani ingeweza kukomeshwa kabisa milele. Mungu Mkuu angeweza mara moja kumtupa mdanganyifu huyo mkuu kutoka mbinguni; lakini huo haukuwa mpango Wake. Alitaka kuwapa waasi nafasi sawa ya kujipima nguvu na uwezo wao dhidi ya Mwana Wake Mwenyewe na malaika Wake waaminifu. Katika vita hii, kila malaika angechagua upande anaotaka kuwa na kuonekana wazi kwa wote. Isingekuwa salama kuwaacha wale waliojiunga na Shetani katika uasi wake, waendelee kukaa mbinguni. Walikuwa wamejifunza somo la uasi halisi dhidi ya sheria isiyobadilika ya Mungu, na hali hiyo isingeweza kutibika. Kama Mungu angetumia nguvu Zake kumwadhibu mara moja kiongozi huyo mkuu wa uasi, malaika waliokuwa hawajaridhika moyoni, wasingeweza kujitokeza wazi na kujulikana; kwa hiyo Mungu alichukua njia nyingine, kwa sababu alitaka kuonyesha wazi mbele ya jeshi lote la mbinguni haki na hukumu Yake. **{SRSw 17.1}**

Vita Mbinguni

Uasi dhidi ya serikali ya Mungu ulikuwa uhalifu mkubwa kupita aina yoyote ya uhalifu. Mbinguni kote kulionekana kuwa na msukosuko na mkanganyiko. Malaika walipangwa katika makundi, kila kundi likiwa na malaika mkuu wa kuliongoza. Shetani alikuwa akipigana dhidi ya sheria ya Mungu kwa sababu alikuwa na tamaa ya kujikweza na hakutaka kujitiisha chini ya mamlaka ya Mwana wa Mungu, Amiri Mkuu wa mbinguni. **{SRSw 17.2}**

Jeshi lote la mbinguni liliitwa kusimama mbele za Baba, ili kila kesi ijulikane vyema. Shetani bila aibu alieleza kutoridhika kwake kwa sababu Kristo alikuwa amependelewa kuliko yeye. Alisimama kwa kiburi na kudai kwamba alipaswa kuwa sawa na Mungu na kwamba alipaswa kushirikishwa katika mashauri pamoja na Baba ili ajue makusudi Yake. Mungu alimjulisha Shetani kwamba ni kwa Mwana Wake pekee yake, Ndiye Angefunua makusudi Yake ya siri, na alidai kwamba familia yote ya mbinguni, hata Shetani mwenyewe, imtii kwa uaminifu usio na masharti na usiohojiwa; lakini kwamba yeye (Shetani) alikuwa amejionyesha kuwa hastahili tena nafasi mbinguni. Ndipo Shetani kwa kujivuna na kushangilia, aliwasonda wale malaika waliomuunga mkono, ambao walikaribia nusu ya malaika wote wa mbinguni, na akasema: “Hawa wako pamoja nami! Je, mtawafukuza hawa pia na kuacha pengo kubwa hivyo mbinguni?” Kisha akatangaza kwamba alikuwa tayari kupinga mamlaka ya Kristo na kutetea nafasi yake mbinguni kwa nguvu na uwezo, nguvu dhidi ya nguvu. **{SRSw 18.1}**

Malaika wema walilia waliposikia maneno ya Shetani na majivuno yake. Mungu alitangaza kwamba waasi hawezi kuishi tena mbinguni. Uwepo wao na hali ya maisha ya juu na furaha vilifungamanishwa kwa sharti la kutii sheria ambayo Mungu alikuwa ameitoa ili kuongoza

viumbe wenye akili wa cheo cha juu. Lakini hakukuwa na mpango wa kuwaokoa wale ambao wangethubutu kuvunja sheria Yake Mwenyezi Mungu. Shetani alizidi kuwa jasiri katika uasi wake, na akaonyesha dharau yake kwa sheria ya Muumba. Hili Shetani hakuweza kulivumilia. Alidai kwamba malaika hawakuhitaji sheria, bali walipaswa kuachwa huru kufuata mapenzi yao wenyewe, ambayo daima yangewaongoza kufanya mambo kwa usahihi; kwamba sheria ilikuwa kizuizi cha uhuru wao-kuwabana wasiwe huru; na kwamba kuondoa sheria lilikuwa mojawapo ya malengo makuu ya msimamo wake. Alifikiri kwamba hali ya malaika ilihitaji kuboreshwa. Lakini haya hayakuwa mawazo ya Mungu, ambaye Ndiye aliyeweka sheria na kuwainua malaika kuwa na hadhi kubwa. Furaha ya jeshi la malaika ilitegemea utii wao kamili kwa sheria. Kila mmoja alikuwa amepewa kazi yake maalumu, na kabla Shetani hajaanza uasi, kulikuwa na mpangilio mkamilifu na utendaji wenye maelewano mbinguni. **{SRSw 18.2}**

Ndipo kukawa na vita mbinguni. Mwana wa Mungu, Mkuu wa mbinguni, pamoja na malaika Wake waaminifu walipigana dhidi ya mwasi mkuu na wale waliojiunga naye. Mwana wa Mungu na malaika wakweli/waadilifu waliokuwa waaminifu walishinda; na Shetani pamoja na wafuasi wake walifukuzwa kutoka mbinguni. Jeshi lote la mbinguni lilimtambua na kumwabudu Mungu wa haki. Hakukuwa tena na doa lolote la uasi mbinguni. Kila kitu kilirudi kuwa na amani na maelewano kama hapo awali. Malaika mbinguni waliomboleza kwa ajili ya hatima ya wale waliokuwa wenzi wao katika furaha na baraka. Kupotea-kuondoka kwao kulihisiwa mbinguni. **{SRSw 19.1}**

Baba alishauriana na Mwana Wake kuhusu kutekeleza mara moja mpango wao wa kumuumba mwanadamu ili akae duniani. Angemweka mwanadamu katika kipindi cha angalizo (probation) ili kupima uaminifu wake kabla hajaonekana kuwa salama milele. Ikiwa angepitia

jaribu/mtihani ambao Mungu aliona unafaa kumpima, hatimaye angekuwa sawa na malaika. Angekuwa na kibali cha Mungu, angezungumza na malaika, nao wangezungumza naye. Mungu hakuona inafaa kuwaweka wanadamu katika hali ambayo wasingeweza tena kuasi [aliwapa uchaguzi]. **{SRSw 19.2}**

SURA YA 2–UUMBAJI

Sura hii imejengwa katika Mwanzo 1.

Baba na Mwana walishiriki katika kazi ile kuu na ya ajabu waliyokuwa wameikusudia—ya kuumba ulimwengu. Dunia ilitoka katika mkono wa Muumba ikiwa nzuri sana. Kulikuwa na milima, vilima na tambarare; na katikati yake kulikuwa na mito na mabwawa ya maji. Dunia haikuwa tambarare kubwa moja lisilo na mabadiliko, bali hali ya kufanana kwa mandhari ilivunjwa na vilima na milima, sio mirefu na yenye miamba mikali/rafu kama ilivyo sasa, bali ikiwa na

umbo la kawaida na zuri. Miamba mirefu na iliyo wazi haikuonekana juu yake, bali ilikuwa chini ya uso wa ardhi, ikifanya kazi kama mifupa ya dunia. Maji yaligawanywa kwa mpangilio mzuri. Vilima, milima na tambarare nzuri sana zilipambwa kwa mimea, maua na miti mirefu yenye fahari ya kila aina, ambayo ilikuwa mikubwa mara sana kuliko leo na yenye uzuri zaidi kuliko miti ilivyo sasa. Hewa ilikuwa safi na yenye afya, na dunia ilionekana kama ikulu bora na tukufu. Malaika walitazama na kufurahia kazi za ajabu na nzuri za Mungu. **{SRSw 20.1}**

Baada ya dunia kuumbwa, pamoja na wanyama waliokuwa juu yake, Baba na Mwana walitimiza kusudi lao, ambalo lilikuwa limepangwa kabla ya kuanguka kwa Shetani, ya kumfanya mwanadamu kwa mfano wao. Walikuwa wamefanya kazi pamoja katika kuumba dunia na kila kiumbe hai kilichomo ndani yake. Na sasa Mungu akamwambia Mwana Wake: “Na tumfanye mtu kwa mfano wetu.” Adamu alipotoka katika mkono wa Muumba wake alikuwa na kimo cha heshima na mwili uliokuwa na uwiano mzuri. Alikuwa mrefu zaidi ya mara mbili ya urefu wa watu wanaoishi duniani sasa, na mwili wake ulikuwa na uwiano kamili. Sura yake ilikuwa kamilifu na nzuri. Rangi yake haikuwa nyeupe wala ya manjano iliyofifia, bali ilikuwa yenye wekundu, iking’aa kwa rangi tajiri ya afya njema. Hawa hakuwa mrefu kama Adamu kabisa. Kichwa chake kilifika juu kidogo ya mabega yake. Hawa pia alikuwa mwenye ubora, uwiano mkamilifu na mzuri sana. **{SRSw 20.2}**

Wanandoa hawa wasio na dhambi hawakuvaa mavazi yaliyotengenezwa na mwanadamu. Walikuwa wamevikwa kwa nuru na utukufu, kama vile malaika wanavyovaa. Walipokuwa wakiishi katika utii kwa Mungu, duara hili la nuru liliwazunguka. Ingawa kila kitu ambacho Mungu alikuwa amefanya kila kilichowezekana ili kuwa kikamilifu na kizuri, na hakukuwa na kitu kilichoonekana kukosekana

duniani ambacho Mungu alikuwa ameumba ili kumfanya Adamu na Hawa wawe na furaha, bado alionyesha upendo Wake mkuu kwao kwa kupanda bustani maalumu kwa ajili yao. Sehemu ya muda wao ilipaswa kutumika katika kazi yenye furaha ya kuitunza bustani hiyo, na sehemu nyingine katika kupokea ziara za malaika, kusikiliza mafundisho yao, na kutafakari kwa furaha. Kazi yao haikuwa ya kuchosha bali ilikuwa ya kupendeza na yenye kuwapa nguvu. Bustani hii nzuri ilikuwa makao yao. **{SRSw 21.1}**

Katika bustani hiyo Bwana aliweka miti ya kila aina kwa ajili ya manufaa na uzuri. Kulikuwa na miti iliyobeba matunda mengi yenye harufu nzuri, yaliyopendeza kwa macho na matamu kwa ladha, ambayo Mungu alikuwa ameyakusudia kuwa chakula cha wale wawili watakatifu. Kulikuwa pia na mizabibu mizuri iliyokua wima, ikiwa imebeba mzigo wa matunda yake, tofauti na kitu chochote ambacho mwanadamu ameona tangu anguko. Matunda yake yalikuwa makubwa sana na ya rangi mbalimbali; mengine kama meusi, mengine ya zambarau, mekundu, ya waridi na ya kijani hafifu. Ukuaji huu mzuri na wenye matunda mengi kwenye matawi ya mzabibu uliitwa zabibu. Mizabibu hiyo haikutambaa chini, bali ilisimama wima, ingawa haikushikiliwa na nguzo au miti maalumu; lakini uzito wa matunda uliinamisha matawi yake. Ilikuwa kazi ya furaha ya Adamu na Hawa kutengeneza vivuli vya kupendeza kutoka kwenye matawi ya mizabibu na kuyaongoza, wakitengeneza makao yaliyotokana na miti hai mizuri ya asili na majani yake, yakiwa yamebeba matunda yenye harufu nzuri. **{SRSw 21.2}**

Dunia ilikuwa imevikwa kijani kibichi kizuri, huku maelfu ya maua yenye harufu nzuri ya kila aina na rangi yakichanua kwa wingi pande zote zilizowazunguka. Kila kitu kilikuwa kimepangwa kwa ustadi na kwa utukufu. Katikati ya bustani kulikuwa na mti wa uzima, ambao

utukufu wake ulizidi miti mingine yote. Matunda yake yalionekana kama tufaha za dhahabu na fedha, na yalikuwa ya kudumisha uzima wa milele (hali ya kutokufa). Majani yake yalikuwa na uwezo wa kuponya**.** **{SRSw 22.1}**

Adamu na Hawa katika Edeni

Jozi hii ya wanadamu hawa wawili watakatifu, ilikuwa na furaha kubwa sana katika Edeni. Walikuwa wamepewa mamlaka yasiyo na mipaka juu ya kila kiumbe hai. Simba na mwana-kondoo walicheza kwa amani na bila madhara karibu nao, au walilala miguuni pao. Ndege wa kila aina ya rangi na manyoya waliruka kati ya miti na maua na kuwazunguka Adamu na Hawa, huku muziki wao mtamu ukisikika katikati ya miti kwa ulinganifu mzuri, ukiwa kama sifa kwa Muumba wao. **{SRSw 22.2}**

Adamu na Hawa walivutiwa sana na uzuri wa makao yao ya Edeni. Walifurahia ndege, ambao walikuwa waimbaji wadogo karibu nao, wakiwa wamevalia manyoya yenye kung'aa na yenye kupendeza, wakitoa sauti zao za furaha na nyimbo tamu. Wanandoa hao watakatifu waliungana nao na kuinua sauti zao katika nyimbo zenye ulinganifu wa upendo, sifa na ibada kwa Baba na Mwana Wake mpendwa, kwa sababu ya ishara za upendo zilizowazunguka. Walitambua mpangilio na upatano wa uumbaji, ambao ulionyesha hekima na maarifa yasiyo na mwisho. Kila wakati waligundua uzuri mpya na utukufu mwingine wa ziada katika makao yao ya Edeni, jambo lililojaza mioyo yao upendo mkubwa zaidi na kuleta kutoka midomoni mwao maneno ya shukrani na heshima kwa Muumba wao. **{SRSw 22.3}**

SURA YA 3—MATOKEO YA UASI

Katikati ya Bustani, karibu na Mti wa Uzima, ulisimama mti wa ujuzi wa mema na mabaya. Mti huu uliwekwa hasa na Mungu kuwa ahadi ya utii wao, imani, na upendo Kwake. Katika mti huu Bwana aliwaamuru wazazi wetu wa kwanza wasile, wala wasiuguse, wasije wakafa. Aliwaambia kwamba wangeweza kula miti yote katika bustani isipokuwa mmoja, lakini wakila mti huo bila shaka watakufa. **{SRSw 24.1}**

Adamu na Hawa walipowekwa kwenye bustani nzuri walikuwa na kila kitu kwa ajili ya furaha yao ambayo wangeweza kutamani. Lakini

Mungu alichagua, katika mipango Yake ya hekima yote, kupima uadilifu wao kabla ya kuwafanya kuwa salama milele. Walipaswa kupata kibali Chake, na alipaswa kuzungumza nao na wao pamoja Naye. Hata hivyo hakuweka uovu nje ya uwezo wao [walikuwa huru kuchagua, ndiyo sheria ya upendo]. Shetani aliruhusiwa kuwajaribu. Kama wangestahimili na kupasi jaribu hilo daima wangepata kibali mbele za Mungu na malaika wa mbinguni. **{SRSw 24.2}**

Shetani alisimama kwa mshangao kwa hali yake mpya. Furaha yake ilitoweka. Aliwatazama malaika waliokuwa pamoja naye, ambao mwanzoni walikuwa na furaha sana, lakini walikuwa wamefukuzwa kutoka mbinguni pamoja naye. Kabla ya kuanguka kwao hapakuwa na kivuli cha kutoridhika kilichokuwa kimeharibu furaha yao kamili. Sasa yote yalionekana kubadilika. Nyuso ambazo zilikuwa zimeakisi sura ya Muumba wao zilikuwa na huzuni na kukata tamaa. Ugomvi, mifarakano, na lawama kali zilikuwa miongoni mwao. Kabla ya uasi wao mambo haya yalikuwa hayajulikani mbinguni. Shetani sasa aliona matokeo ya kutisha ya uasi wake. Alitetemeka kwa kushtuka na kuogopa kukabiliana na siku zijazo na kutafakari mwisho wa mambo haya. **{SRSw 24.3}**

Saa ya nyimbo za shangwe na furaha za kumsifu Mungu na Mwanawe mpendwa ilikuwa imefika. Shetani alikuwa ameongoza kwaya ya mbinguni. Alikuwa mtoaji wa noti ya kwanza [mtoaji wa sauti]; Kisha jeshi lote la malaika lilikuwa limeungana naye, na aina tukufu za muziki zilisikika mbinguni ili kumsifu Mungu na Mwanawe mpendwa. Lakini sasa, badala ya ala za muziki mtamu zaidi, mifarakano na maneno ya hasira yanaangukia kwenye sikio la kiongozi mkuu wa waasi. Shetani aliwaza kwamba, Je, yuko wapi? Je, hiyo sio ndoto ya kutisha? Je, ametupwa kutoka mbinguni? Je, milango ya mbinguni haifunguki tena ili kumkubali? Saa ya ibada inakaribia, wakati ambapo

malaika waangavu na watakatifu wanasujudu mbele za Baba. Shetani hakuweza tena kuungana katika wimbo wa mbinguni. Hawezi kusujudu tena kwa heshima na kicho kitakatifu mbele ya uwepo wa Mungu wa milele. **{SRSw 25.1}**

Kama angeweza kuwa tena kama alivyokuwa wakati alipokuwa msafi wa moyo, mwadilifu, na mwaminifu, kwa furaha angesalimisha madai ya mamlaka yake. Lakini alikuwa amepotea! Bila ukombozi, kwa uasi wake wa kiburi na ujuvi! Na hii haikuwa yote; Alikuwa amewaongoza malaika wengine kwenye uasi katika hali ile ile aliyopotea yeye mwenyewe, malaika ambao hawakuwahi kufikiria kutilia shaka mapenzi ya mbinguni au kukataa utii wa sheria ya Mungu mpaka alipoiweka akilini mwao, akiwasilisha mbele yao ili wafurahie wema mkuu zaidi, wa juu zaidi na wa uhuru zaidi uliotukuka. Huu ulikuwa ni ujanja/hila ambapo alikuwa amewadanganya. Jukumu sasa liko juu yake ambalo angetamani kuachiliwa. **{SRSw 25.2}**

Roho hizi zilikuwa na msukosuko na matumaini yaliyokatishwa tamaa. Badala ya mema zaidi, walikuwa wakipitia matokeo ya kusikitisha ya kutotii na kutozingatia sheria. Kamwe hawa viumbe wasio na furaha wasingeongozwa tena na utawala mpole wa Yesu Kristo. Kamwe roho zao hazingechochewa tena na upendo wa kina, wa dhati, amani, na furaha ambayo uwepo Wake uliwahi kuwavuvia, kuwarudisha Kwake kwa utii wenye furaha na heshima ya uchaji-Mungu na kicho. **{SRSw 25.3}**

Shetani Atafuta Kurejeshwa

Shetani alitetemeka alipotazama kazi yake. Alikuwa peke yake katika kutafakari yaliyopita, ya sasa, na mipango yake ya baadaye. Umbo lake lenye nguvu lilitikisika kama vile dhoruba. Malaika kutoka mbinguni alikuwa akipita. Alimwita na kusihi mahojiano na Kristo. Hii

ilikuwa nafasi aliyopewa. Kisha akahojiana na Mwana wa Mungu kuwa alitubu uasi wake na akatamani tena kibali cha Mungu. Alikuwa tayari kuchukua tena nafasi/mahali ambapo Mungu alikuwa amemkabidhi hapo awali, na kuwa chini ya amri na Uongozi Wake yenye hekima. Kristo alilia kwa ole wa Shetani lakini akamwambia, kama nia ya Mungu, kwamba hangeweza kamwe kupokelewa mbinguni. Mbingu haipaswi kuwekwa hatarini. Mbingu zote zingeharibiwa ikiwa angepokelewa tena, kwa maana dhambi na uasi ulianzia kwake -ndani yake. Mbegu za uasi bado zilikuwa ndani yake. Kwa uasi wake, hakuwa na nafasi kwake, na alikuwa amejiangamiza bila tumaini, na siyo yeye mwenyewe tu, bali hata na jeshi la malaika pia, ambalo lingekuwa na furaha mbinguni kama angebaki thabiti. Sheria ya Mungu ingeweza kuhukumu lakini isingeweza kusamehe. **{SRSw 26.1}**

Hakutubu uasi wake kwa sababu aliona wema wa Mungu alioutumia vibaya. Lilikuwa ni jambo ambalo lilikuwa halijawezekana kwake bado, kwamba upendo wake kwa Mungu ulikuwa umeongezeka sana tangu anguko lake kiasi kwamba upendo wake ulete utii wenye unyenyekevu na wa furaha kwa sheria Yake Bwana ambayo ilikuwa imedharauliwa. Unyonge/uharibifu aliougundua katika kupoteza nuru tamu ya mbinguni, na hisia ya hatia ambayo ilijisukuma kwake, na hali ya kukata tamaa aliyopitia kwa kutopata matarajio yake kutimizwa, ilikuwa sababu ya majonzi yake. Kuwa kamanda au kiongozi nje ya mbingu kulikuwa tofauti sana na jinsi alivyokuwa na heshima mbinguni. Hasara aliyokuwa ameipata ya kupoteza haki na fursa zote za mbinguni ilionekana kuwa kubwa sana kiasi cha kushindwa kuvumilika. Alitaka kurejesha haya aliyopoteza. **{SRSw 26.2}**

Badiliko hili kubwa la nafasi halikuwa limeongeza upendo wake kwa Mungu, wala kwa sheria Yake yenye hekima na haki. Shetani alipothibitisha kabisa kwamba hakukuwa na uwezekano wowote wa

kurejeshwa katika kibali cha Mungu, alidhihirisha uovu wake kwa chuki iliyozidi na hasira kali sana. **{SRSw 27.1}**

Mungu alijua kwamba uasi huo uliodhamiriwa haungebaki bila kufanya kazi. Shetani angebuni njia za kuwaudhi malaika wa mbinguni na kuonyesha dharau kwa mamlaka Yake. Kwa vile hangeweza kupata kuingia ndani ya malango ya mbinguni, angengoja tu mlangoni, na kuwadhihaki malaika na kutafuta ugomvi nao walipokuwa wakiingia na kutoka. Angetafuta kuharibu furaha ya Adamu na Hawa. Angejitahidi kuwachochea waasi, akijua kwamba hilo lingesababisha huzuni mbinguni. **{SRSw 27.2}**

Njama Dhidi ya Familia ya Mwanadamu

Wafuasi wake walikuwa wakimtafuta, na alijiinua, akiwa na sura ya ukaidi, akawajulisha juu ya mipango yake ya kuwaondoa kwa nguvu kutoka kwa Mungu Adamu na mwenzi wake Hawa. Kama angeweza kwa njia yoyote kuwahadaa wasitii, Mungu angefanya njia fulani ambapo wangeweza kusamehewa, na kisha yeye mwenyewe na malaika wote walioanguka wangekuwa katika njia ya haki kushiriki nao rehema ya Mungu. Ikiwa hii ingeshindikana, wangeweza kuungana na Adamu na Hawa, kwa maana mara tu watakapoivunja sheria ya Mungu wangekuwa raia wa ghadhabu ya Mungu, kama wao wenyewe. Uasi wao ungewaweka, pia, katika hali ya uasi, na wangeweza kuungana na Adamu na Hawa, wakaimiliki Edeni, na kuishikilia kama makao yao. Na kama wangeweza kuupata Mti wa Uzima katikati ya bustani, walifikiri, nguvu zao zingekuwa sawa na zile za Malaika Watakatifu, na hata Mungu Mwenyewe hangeweza kuwafukuza. **{SRSw 27.3}**

Shetani alifanya mashauriano na malaika wake waovu. Hawakuwa na mshikamano kwa urahisi kushiriki katika kazi hii hatari na ya kutisha. Aliwaambia kwamba hatamkabidhi yeyote kati yao kukamilisha kazi hii,

kwa kuwa alifikiri kwamba yeye peke yake alikuwa na hekima ya kutosha kuendeleza kazi muhimu sana. Aliwataka wazingatie suala hilo huku akiwaacha na kujitenga ili kutafakari na kukamilisha juu ya mipango yake. Alitaka kuwasisitiza kwamba hili lilikuwa tumaini lao la mwisho na la pekee. Kama wangeshindwa hapa, matarajio yote ya kurejesha na kutawala mbingu, au sehemu yoyote ya uumbaji wa Mungu, yasingekuwa na tumaini. **{SRSw 28.1}**

Shetani alienda peke yake kukamilisha mipango ambayo kwa hakika ingehakikisha anguko la Adamu na Hawa. Alikuwa na hofu kwamba makusudi yake yanaweza kushindwa. Na tena, hata kama angefanikiwa kuwaongoza Adamu na Hawa kutotii amri ya Mungu, na hivyo kuwa waasi wa sheria Yake, na na yeye mwenyewe asipate faida yoyote, hali yake mwenyewe isingeboreka; Hatia yake ingeongezeka tu. **{SRSw 28.2}**

Alitetemeka alipofikiria kuwazamisha wanandoa hao watakatifu na wenye furaha katika mateso na majuto ambayo aliyokuwa akiyapata yeye mwenyewe. Alionekana katika hali ya kusitasita kufanya uamuzi: wakati mwingine alikuwa thabiti na mwenye kuamua, kisha wakati mwingine alikuwa akisita na kuyumbayumba. Malaika wake walikuwa wakimtafuta, kiongozi wao, ili kumjulisha uamuzi wao. Wangeungana na Shetani katika mipango yake, na kubeba jukumu pamoja naye na kushiriki matokeo. **{SRSw 28.3}**

Shetani alitupilia mbali hisia zake za kukata tamaa na udhaifu, na, kama kiongozi wao, alijiimarisha kwa kujikakamua ili kujipa ushupavu katika jambo hilo na kufanya yote awezayo kukaidi mamlaka ya Mungu na Mwanawe. Aliwafahamisha mipango yake. Kama angekuja kwa ujasiri mbele ya Adamu na Hawa na kutoa malalamiko dhidi ya Mwana wa Mungu, wasingemsikiliza hata kwa muda mfupi, bali wangekuwa tayari kwa shambulio hilo. Na kama angejaribu kuwatisha kwa sababu

ya nguvu zake, ambazo hivi karibuni alikuwa nazo kama malaika mwenye cheo cha juu, hangefanikiwa chochote. Aliamua kwamba hila na udanganyifu vinaweza kufanya kile ambacho nguvu, au mabavu yasingeweza kufanya. **{SRSw 29.1}**

Adamu na Hawa Walionywa

Mungu alikusanya jeshi la malaika kuchukua hatua za kuzuia uovu uliokuwa unatishia kutokea. Iliamuliwa katika Baraza la Mbinguni kwa malaika waende Edeni na kumwonya Adamu kwamba alikuwa hatarini kutoka kwa adui. Malaika wawili waliharakisha kwenda kuwatembelea wazazi wetu wa kwanza. Wanandoa hao watakatifu waliwapokea kwa furaha na unyenyekevu wa kutokuwa na hatia, wakimshukuru kwa shukrani nyingi Muumba wao kwa kuwazungushia kwa wingi wa fadhila Zake. Kila kitu cha kupendeza na cha kuvutia kilikuwa chao kufurahia, na kila kitu kilionekana kuratibiwa vyema, kulingana na matakwa yao; na kile walichokithamini zaidi ya baraka nyingine zote, kilikuwa ni ushirika wa Mwana wa Mungu na Malaika wa Mbinguni, kwa maana walikuwa na mengi ya kuhusiana nao katika kila ziara, ya uvumbuzi wao mpya wa uzuri wa asili katika makazi yao ya kupendeza ya Edeni, na walikuwa na maswali mengi ya kuuliza kuhusiana na mambo mengi ambayo hawakuyaelewa vizuri. **{SRSw 29.2}**

Malaika kwa neema na upendo waliwapa habari waliyotaka. Pia waliwapa historia ya kusikitisha ya uasi na kuanguka kwa Shetani. Kisha wakawajulisha waziwazi kwamba Mti wa Ujuzi uliwekwa katika bustani kuwa ni kiapo cha utii wao na upendo kwa Mungu; kwamba hali ya juu na yenye furaha ya Malaika Watakatifu iliifadhiwa kwa sharti la utii; kwamba wao pia walikuwa katika hali kama hiyo; Kwamba wangeweza kutii sheria ya Mungu na kuwa na furaha isiyoelezeka, au kutotii na kupoteza hali yao ya juu na kutumbukia katika kukata tamaa bila tumaini. **{SRSw 29.3}**

Waliwaambia Adamu na Hawa kwamba Mungu asingewalazimisha kumtii—kwamba hakuwa ameondoa uwezo wao wa kwenda kinyume na mapenzi Yake; Kwamba walikuwa viumbe wenye maamuzi ya kimaadili, walio huru kutii au kutotii. Kulikuwa na katazo moja tu ambalo Mungu alikuwa ameona linafaa kuliweka juu yao. Ikiwa wangevunja mapenzi ya Mungu bila shaka wangekufa. Waliwaambia Adamu na Hawa kwamba malaika aliyetukuka zaidi, aliyemfuata Kristo kwa cheo, alikataa kutii sheria ya Mungu ambayo alikuwa Ameiweka kutawala viumbe vya mbinguni; Kwamba uasi huu ulikuwa umesababisha vita mbinguni, ambayo ilisababisha waasi kufukuzwa kutoka humo, na kila malaika alifukuzwa kutoka mbinguni ambaye alikuwa ameungana naye katika kuhoji mamlaka ya Yehova Mkuu; na kwamba adui huyu aliyeanguka sasa alikuwa adui kwa wote waliohusika na maslahi ya Mungu na Mwanawe mpendwa. **{SRSw 30.1}**

Waliwaambia kwamba Shetani alikusudia kuwadhuru, na ilikuwa ni lazima walindwe, kwa maana wangeweza kukutana na adui aliyeanguka; Lakini asingeweza kuwadhuru ikiwa wangetii amri ya Mungu, kwa maana kama ingehitajika, kila malaika kutoka mbinguni angewasaidia badala ya kumruhusu Shetani awadhuru kwa njia yoyote ile. Lakini kama wangekataa kutii amri ya Mungu, basi Shetani angekuwa na uwezo wa kuwaudhi, kuwasumbua, kuwafadhaisha na kuwapa shida daima. Kama wangebaki imara dhidi ya uzushi wa kwanza wa Shetani, wangekuwa salama kama malaika wa mbinguni. Lakini kama wangejisalimisha kwa mjaribu, Mungu ambaye hakuwaonea huruma malaika waliotukuka walipokosa, asingewaonea huruma wanadamu pia. Wangepaswa kupata adhabu ya kosa lao, kwa kuwa sheria ya Mungu ilikuwa takatifu kama Yeye mwenyewe, na alihitaji utii kamili kutoka kwa wote mbinguni na duniani. **{SRSw 30.2}**

Malaika walimtahadharisha Hawa asitengane na mume wake katika kazi yake, kwa maana angeweza kukutana na adui huyu aliyeanguka. Ikiwa wangetenganishwa kutoka kwa kila mmoja, wangekuwa katika hatari kubwa kuliko pale wote wawili wanapokuwa pamoja. Malaika waliwaagiza wafuate kwa ukaribu maagizo ambayo Mungu alikuwa amewapa kuhusiana na Mti wa Ujuzi, kwa kuwa kwa utii kamili walikuwa salama, na adui huyu aliyeanguka asingeweza kuwa na uwezo wa kuwadanganya. Mungu asingemruhusu Shetani kufuata wanandoa hawa watakatifu kwa majaribu ya mara kwa mara. Angeweza kuwapata tu kwenye mti wa ujuzi wa mema na mabaya. **{SRSw 31.1}**

Adamu na Hawa waliwahakikishia malaika kwamba hawatavunja amri iliyo wazi ya Mungu, kwa kuwa ilikuwa ni furaha yao kubwa kufanya mapenzi Yake. Malaika waliungana na Adamu na Hawa katika nyimbo takatifu za muziki wenye upatanifu, na nyimbo zao zilipokuwa zikisikika katika Edeni yenye furaha, Shetani alisikia sauti za nyimbo zao za furaha na ibada kwa Baba na Mwana. Na Shetani aliposikia nyimbo hizo, husuda yake, chuki, na uovu wake wa kutisha viliongezeka, na akaonyesha wasiwasi wake kwa wafuasi wake ili kuwachochea (Adamu na Hawa) waasi na mara moja wajiletee ghadhabu ya Mungu juu yao, na kubadilisha nyimbo zao za sifa kuwa chuki na laana dhidi ya Muumba wao. **{SRSw 31.2}**

SURA YA 4—MAJARIBU NA ANGUKO

Sura hii imejengwa katika Mwanzo 3.

Shetani alichukua umbo la nyoka na akaingia katika Bustani ya Edeni. Nyoka alikuwa kiumbe mzuri mwenye mabawa, na alipokuwa akiruka angani, mwonekano wake ulikuwa unang’aa, ukifanana na

dhahabu iliyosuguliwa vizuri/iliyochomwa. Hakuwa akitembea ardhini bali alikuwa akihama kutoka sehemu moja hadi nyingine angani na kula matunda kama mwanadamu. Shetani aliingia ndani ya nyoka na kuchukua nafasi yake katika Mti wa Ujuzi na akaanza kula tunda kwa raha/utulivu. **{SRSw 32.1}**

Hawa, bila kujua mwanzoni, alitengana na mumewe katika kazi yake. Alipofahamu ukweli kwamba alihisi kwamba kunaweza kuwa na hatari, lakini tena alijiona yuko salama, hata kama asingebaki karibu na mume wake. Aliamini kuwa alikuwa na hekima na nguvu ya kujua kama uovu ukija, na kuukabiliana nao. Hili Malaika walikuwa wamemtahadharisha asifanye. Hawa alijikuta akitazama kwa udadisi mshangao na kuvutiwa na matunda ya mti uliokatazwa. Aliona tunda hilo lilikuwa la kupendeza sana, na akaanza kujifikiria mwenyewe kwa busra yake, kwanini Mungu alikuwa amekataza kabisa kulila au kuligusa. Sasa ilikuwa fursa ya Shetani. Alizungumza naye kana kwamba alikuwa na uwezo wa kutabiri mawazo yake: ***Ati! Hivi ndivyo alivyosema Mungu, Msile matunda ya miti yote ya bustani?*** Kwa hivyo, kwa maneno laini na ya kupendeza, na kwa sauti ya muziki, alizungumza na Hawa anayeshangaa. Alishtuka kusikia nyoka akiongea. Aliutukuza uzuri wake na uzuri kupita kiasi, jambo ambalo halikumpendeza Hawa. Lakini alistaajabu, kwa kuwa alijua kwamba kwa nyoka, Mungu hakuwa amempa uwezo wa kusema. **{SRSw 32.2}**

Udadisi wa Hawa uliamshwa. Badala ya kukimbia kutoka mahali hapo, alisikiliza sauti ya nyoka. Haikuingia akilini mwake kwamba huenda ilikuwa adui aliyeanguka, akitumia nyoka kama chombo cha kuwasiliana. Shetani ndiye aliyezungumza, na sio nyoka. Hawa alidanganywa, alipendezwa, na akavutiwa. Kama angekutana na mtu mwenye amri, akiwa na umbo kama malaika na anafanana nao, angekuwa makini zaidi na kujilinda. Lakini sauti hiyo ngeni, ingemfanya

Hawa aende haraka kwa mume wake ili kumuuliza kwa nini kiumbe mwingine alikuwa akiongea naye kwa uhuru namna hiyo. Lakini aliingia kwenye mabishano na nyoka. Alijibu swali lake, ***"Matunda ya miti ya bustanini twaweza kula; lakini matunda ya mti ulio katikati ya bustani Mungu amesema, Msiyale wala msiyaguse, msije mkafa. Nyoka akamwambia mwanamke, Hakika hamtakufa, kwa maana Mungu anajua ya kwamba siku mtakayokula matunda ya mti huo, mtafumbuliwa macho, nanyi mtakuwa kama Mungu, mkijua mema na mabaya.*** **{SRSw 33.1}**

Shetani alitaka kuwasadikisha kwamba kwa kula matunda ya mti uliokatazwa wangepokea aina mpya na bora zaidi ya maarifa kuliko yale waliyokuwa nayo hapo awali. Hii imekuwa kazi yake ya pekee, yenye mafanikio makubwa, tangu kuanguka kwake—kuwaongoza watu kuingia katika siri za Mwenyezi na kutoridhika na yale ambayo Mungu amefunua, na kutokuwa makini kutii yale Aliyoamuru. Angewaongoza kutotii amri za Mungu, na kisha kuwafanya waamini kwamba wanaingia katika uwanja wa ajabu wa maarifa. Hii ni dhana ya kufikirika tu, na udanganyifu mbaya. Wanashindwa kuelewa kile ambacho Mungu amefunua, na kupuuza amri Zake zilizo wazi na kutamani hekima, bila ya Mungu, na kutafuta kuelewa kile ambacho amekuwa radhi kuwazuia wanadamu. Wanafurahishwa na mawazo yao ya kuendelea na kuvutiwa na falsafa yao isiyo na maana, lakini wanapapasa-papasa katika giza la usiku wa manane kuhusiana na ujuzi wa kweli. Wanajifunza kila wakati na hawawezi kupata maarifa ya Ukweli. **{SRSw 33.2}**

Haikuwa mapenzi ya Mungu kwamba wanandoa hawa wasio na dhambi wawe na ujuzi wowote wa uovu. Alikuwa amewapa mema kwa hiari lakini alizuia mabaya. Hawa alifikiria maneno ya nyoka mwenye hekima, na akapokea madai hayo mapana, ***"kwa maana Mungu anajua ya kwamba siku mtakayokula matunda ya mti huo, mtafumbuliwa***

macho, nanyi mtakuwa kama Mungu, mkijua mema na mabaya- alimfanya Mungu kuwa mwongo. Shetani alisisitiza kwa ujasiri kwamba Mungu alikuwa amewadanganya ili kuwazuia wasitukuzwe katika ujuzi sawa na yeye mwenyewe. Mungu alisema: ***"kwa maana siku utakapokula matunda ya mti huo utakufa hakika. Nyoka akamwambia mwanamke, Hakika hamtakufa.***" **{SRSw 34.1}**

Mjaribu alimhakikishia Hawa kwamba mara tu atakapokula tunda hilo, angepokea maarifa mapya na ya hali ya juu ambayo yangemfanya kuwa sawa na Mungu. Alivuta usikivu wake. Alidai kuwa yeye mwenyewe alikula kutoka kwenye mti huo kwa na akauona sio tu usio na madhara kabisa bali ni mtamu na wa kusisimua, na akamwambia (Hawa) kwamba ni kwa sababu ya sifa zake za ajabu za kutoa hekima na uwezo, ndio maana Mungu alikuwa amewakataza kuuonja au hata kuugusa, kwa kuwa alijua sifa zake za ajabu. Alisema kwamba kula kwake matunda ya mti waliokatazwa ndiyo sababu iliyompa uwezo wa kusema. Alidokeza kwamba Mungu hatatekeleza Neno Lake. Ilikuwa tu tishio kuwatisha na kuwaepusha na wema mkubwa. Aliwaambia zaidi kwamba hawawezi kufa. Je! hawakuwa wamekula mti wa uzima ambao unaendeleza kutokufa? Alisema kwamba Mungu alikuwa akiwadanganya ili kuwaepusha na hali ya juu ya uchangamfu na furaha iliyotukuka zaidi. Mjaribu alichuma tunda na kulipitisha kwa Hawa. Alilichukua mkononi mwake. Sasa, alisema mjaribu, wewe ulikatazwa hata kuligusa usije ukafa. Alimwambia kwamba hatatambua maana ya uovu na kifo katika kula kuliko kugusa au kushughulikia matunda. Hawa alitiwa moyo kwa sababu hakuhisi dalili za mara moja za kukasirika kwa Mungu. Alifikiri maneno ya mjaribu kwa hekima na sahihi. Alikula, na alifurahishwa na tunda. Ilionekana kuwa tamu kwa ladha yake, na alifikiria kwamba aligundua ndani yake matokeo ya ajabu za matunda. **{SRSw 34.2}**

Hawa Anakuwa Mjaribu

Kisha akachuma tunda na kula, na akafikiria alihisi nguvu ya kuhuisha ya maisha mapya na yaliyoinuliwa kama matokeo ya ushawishi wa kusisimua wa tunda lililokatazwa. Alikuwa katika msisimko wa ajabu na usio wa kawaida huku akimtafuta mumewe huku mikono yake ikiwa imejaa tunda lililokatazwa. Alimsimulia mazungumzo ya busara ya nyoka na alitaka kumwongoza mara moja kwenye Mti wa ujuzi. Alimwambia alikuwa amekula tunda hilo, na badala ya kuhisi kifo chake, aligundua ushawishi wa kupendeza na wa kusisimua. Mara tu Hawa alipokosa kutii akawa chombo chenye nguvu ambacho kilisababisha kuanguka kwa mume wake. **{SRSw 35.1}**

Niliona huzuni ikija juu ya uso wa Adamu. Alionekana akiwa na hofu na mshtuko. Mapambano yalionekana kuendelea akilini mwake. Alimwambia Hawa alikuwa na hakika kabisa kwamba huyu ndiye adui ambaye walikuwa wameonywa dhidi yake, na ikiwa ni hivyo, kwamba ni lazima afe. Alimhakikishia kwamba hakuhisi madhara yoyote bali ushawishi wa kupendeza sana, na akamsihi ale. **{SRSw 35.2}**

Adamu alielewa vyema kwamba msaidizi wake alikuwa amevunja katazo pekee lililowekwa juu yao kama jaribio la uaminifu na upendo wao. Hawa alitoa sababu kwamba, nyoka huyo alisema kwamba hawatakufa hakika, na maneno yake lazima yawe ya kweli, kwa kuwa hakuhisi dalili zozote za kuchukizwa na Mungu, bali mvuto wenye kupendeza, kama alivyowazia kwamba malaika walihisi. **{SRSw 36.1}**

Adamu alijuta kwamba Hawa alikuwa ameondoka upande wake, lakini sasa tendo lilifanyika. Lazima atenganishwe na yeye ambaye jamii yake aliipenda sana. Je, angewezaje kuwa na hali hiyo? Upendo wake kwa Hawa ulikuwa na nguvu, na kwa kuvunjika moyo kabisa aliamua kushiriki hatima yake. Alitoa sababu kwamba Hawa alikuwa sehemu

yake mwenyewe, na ikiwa lazima Hawa afe, angekufa pamoja naye, kwa kuwa hangeweza kustahimili wazo la kujitenga naye. Alikosa imani katika Muumba wake mwenye rehema na fadhili. Hakufikiri kwamba Mungu, ambaye alikuwa amemuumba kutoka katika mavumbi ya ardhi na kuwa hai, umbo zuri, na alikuwa amemuumba Hawa kuwa msaidizi wake, angeweza kumjaliza mahali pake. Baada ya yote, je, maneno ya nyoka huyu mwenye hekima hayawezi kuwa sahihi? Hawa alikuwa mbele yake, mzuri na mrembo, akiwa hana hatia, kama kabla ya kitendo hiki cha kutotii. Alionyesha upendo mkubwa zaidi kwake kuliko kabla ya kutotii kwake, kama athari za tunda alilokula. Hakuona ndani yake dalili za kifo. Alikuwa amemwambia juu ya ushawishi wa furaha wa matunda, upendo wake mkuu kwake, na aliamua kuthubutu matokeo. Alilitwaa tunda hilo na kulila haraka, na kama Hawa, hakuhisi madhara yake mara moja. **{SRSw 36.2}**

Hawa alijiona kuwa na uwezo wa kuamua kati ya mema na makosa/mabaya. Tumaini la kupendeza la kuingia katika hali ya juu zaidi ya ujuzi lilimfanya afikiri kwamba nyoka huyo alikuwa rafiki yake wa pekee [special friend], aliyependezwa sana na ustawi wake. Lau angemtafuta mumewe, nao wangemshirikisha Muumba wao kwa kumwelezea maneno ya nyoka, yangetolewa mara moja kutoka kwa majaribu yake ya kijanja. Bwana asingewataka wachunguze tunda la Mti wa ujuzi, kwa maana basi wangeanikwa wazi kwa barakoa ya Shetani [alikuwa amejifunika uso kama malaika wa nuru]. Alijua kwamba wangekuwa salama kabisa ikiwa hawangegusa matunda. **{SRSw 36.3}**

Uhuru wa Mwanadamu wa Kuchagua

Mungu aliwaelekeza wazazi wetu wa kwanza kuhusiana na Mti wa ujuzi, na walikuwa na habari kamili kuhusiana na anguko la Shetani, na hatari ya kusikiliza mapendekezo yake. Hakuwanyima uwezo wa kula tunda lililokatazwa. Aliwaacha kama viumbe huru wa kiadili kuamini

Neno Lake, kutii amri Zake, na kuishi, au kumwamini mjaribu, kutotii, na kuangamia. Wote wawili walikula, na hekima kuu waliyopata ilikuwa ujuzi wa dhambi na hisia ya hatia. Nuru ya Mungu iliyofunika juu yao ilitoweka upesi, na chini ya hisia ya hatia na kupoteza kifuniko chao cha Kiungu, mshituko uliwakamata, na walijaribu kufunika hali zao za utupu- zilizokuwa wazi. **{SRSw 37.1}**

Wazazi wetu wa kwanza walichagua kuamini maneno ya nyoka, kama walivyofikiri; Hata hivyo hakuwa amewapa ishara za upendo wake. Hakuwa amefanya lolote kwa ajili ya furaha na manufaa yao, ilhali Mungu alikuwa amewapa kila kitu ambacho kilikuwa kizuri kwa chakula na cha kupendeza kwa macho/uoni. Kila mahali jicho linaweza kupumzika lilikuwa tele na uzuri; Hata hivyo Hawa alidanganywa na nyoka, kufikiri kwamba kulikuwa na jambo ambalo lingewafanya wawe na hekima, hata kama Mungu. Badala ya kuamini na kumweleza Mungu vidokezo walivyopewa na ShetaniBaada ya kosa la Adamu mwanzoni alifikiria kwamba alihisi kupanda kwa uwepo mpya na wa juu zaidi. Lakini upesi wazo la kosa lake lilimtia hofu. Hewa, ambayo ilikuwa ya joto kidogo na hata joto, ilionekana kuwa baridi. Wanandoa wenye hatia walikuwa na hisia ya dhambi. Walihisi hofu ya siku zijazo, hisia ya kutaka, uchi wa nafsi. Upendo mtamu na amani na furaha iliyojaa furaha ilionekana kuondolewa kutoka kwao, na mahali pake uhitaji wa kitu ulikuja juu yao ambao hawakuwahi kupata hapo awali. Kisha kwa mara ya kwanza walielekeza mawazo yao kwa nje. Hawakuwa wamevaa bali walikuwa wamefunikwa na nuru kama vile malaika wa mbinguni. Nuru hii iliyokuwa imewafunika ilikuwa imeondoka. Ili kupunguza hisia zao za kupungukiwa na ukosefu na utupu/uchi ambao waliutambua wanao sasa, umakini wao ulielekezwa kutafuta kufunika hali zao, kwani wangewezaje kukutana na jicho la Mungu na malaika bila nguo? **{SRSw 38.1}**

Uhalifu wao sasa ulikuwa mbele yao katika nuru Yake wa kweli. Ukiukaji wao wa amri ya Mungu iliyo wazi huchukua tabia iliyo wazi zaidi. Adamu alishutumu upumbavu wa Hawa kwa kuondoka upande wake na kudanganywa na nyoka. Wote wawili walijipendekeza kwamba Mungu, ambaye alikuwa amewapa kila kitu ili kuwafurahisha, bado angeweza kuwasamehe kutotii kwao kwa sababu ya upendo Wake mkuu kwao na kwamba adhabu yao isingekuwa ya kutisha hata kidogo. **{SRSw 38.2}**

Shetani alishangilia katika mafanikio yake. Sasa alikuwa amemjaribu mwanamke huyo kutomwamini Mungu, kuhoji hekima Yake, na kutafuta kupenya mipango Yake ya hekima yote. Na kupitia kwake pia alikuwa amesababisha kupinduliwa kwa Adamu, ambaye, kwa matokeo ya upendo wake kwa Hawa, aliasi amri ya Mungu na akaanguka pamoja naye. **{SRSw 38.3}**

Habari za anguko la mwanadamu zilienea mbinguni—kila kinubi kilinyamazishwa. Malaika walitupa taji zao kutoka vichwani mwao kwa huzuni. Mbingu zote zilikuwa katika fadhaa na mzozo. Malaika walihuzunishwa na kutokuwa na shukrani kwa msingi wa mwanadamu kwa malipo ya fadhila nyingi ambazo Mungu alikuwa ametoa. Baraza lilifanyika ili kuamua nini kifanywe kwa wanandoa hao wenye hatia. Malaika waliogopa kwamba wangenyoosha mkono na kula mti wa uzima, na hivyo kuendeleza maisha ya dhambi milele. **{SRSw 39.1}**

Bwana aliwatembelea Adamu na Hawa, na kuwajulisha matokeo ya kutotii kwao. Waliposikia njia kuu ya Mungu walijaribu kujificha kutokana na ukaguzi Wake, ambao walifurahia, huku katika kutokuwa na hatia na utakatifu, kukutana nao. ***"Bwana Mungu akamwita Adamu, akamwambia, Je, Uko wapi? Akasema, Nalisikia sauti Yako bustanini, nikaogopa kwa kuwa mimi ni uchi; nikajificha. Akasema, Ni nani aliyekuambia ya kuwa u uchi? Je! Umekula wewe matunda ya mti***

niliyokuagiza usiyale?" Swali hili liliulizwa na Bwana, sio kwa sababu alihitaji kupata habari, bali kwa ajili ya kuwasadikisha wenzi hao wenye hatia kile ambacho walikifanya. Je, ulipataje aibu na woga? Adamu alikiri kosa lake, si kwa sababu alikuwa ametubu kwa ajili ya kutotii kwake, bali kwa kumtupia Mungu lawama, kama sababishi ya kutenda kwake dhambi. Adamu akasema, ***Huyo mwanamke uliyenipa awe pamoja nami ndiye aliyenipa matunda ya mti huo, nikala. Bwana Mungu akamwambia mwanamke, Nini hili ulilolifanya? Mwanamke akasema, Nyoka alinidanganya, nikala. Mwanzo 3:12-13*** **{SRSw 39.2}**

Laana

Bwana akamwambia yule nyoka**: Bwana Mungu akamwambia nyoka, Kwa sababu umeyafanya hayo, umelaaniwa wewe kuliko wanyama wote, na kuliko hayawani wote walioko mwituni; kwa tumbo utakwenda, na mavumbi utakula siku zote za maisha yako; Mwanzo 3:14** Kwa vile nyoka alikuwa ameinuliwa juu ya wanyama wa mwituni, alipaswa kushushwa hadhi chini yao wote, na kuchukiwa na mwanadamu, kwa vile yeye ndiye chombo kilichotumika na Shetani katika utendaji. ***Akamwambia Adamu, Kwa kuwa umeisikiliza sauti ya mke wako, ukala matunda ya mti ambao nalikuagiza, nikisema, Usiyale; ardhi imelaaniwa kwa ajili yako; kwa uchungu utakula mazao yake siku zote za maisha yako; michongoma na miiba itakuzalia, nawe utakula mboga za kondeni; kwa jasho la uso wako utakula chakula, hata utakapoirudia ardhi, ambayo katika hiyo ulitwaliwa; kwa maana u mavumbi wewe, nawe mavumbini utarudi. Mwanzo 3:17-19*** **{SRSw 39.3}**

Mungu aliilaani ardhi kwa sababu ya dhambi yao katika kula mti wa ujuzi, na akatangaza; ***kwa uchungu utakula mazao yake siku zote za maisha yako."*** Alikuwa amewagawia wema, lakini alizuia uovu. Sasa

anatangaza kwamba watakula, yaani, wanapaswa kuujua uovu siku zote za maisha yao. **{SRSw 40.1}**

Kuanzia wakati huo, jamii ya wanadamu wote wangeanza kupatwa na majaribu ya Shetani. Maisha ya taabu na mahangaiko ya kudumu yaliwekwa kwa Adamu, badala ya kazi ya furaha, na urahisi ambayo alikuwa nayo hapo awali. Angeweza kukatishwa tamaa, kuwa na huzuni, na maumivu, na hatimaye kufikia uharibifu-mauti. Waliumbwa kwa mavumbi ya ardhi, na mavumbini watarudi. **{SRSw 40.2}**

Walifahamishwa kwamba wangelazimika kupoteza makazi yao ya Edeni. Walikuwa wamejisalimisha kwa udanganyifu wa Shetani na kuamini neno la Shetani, kwamba Mungu angesema uwongo. Kwa kosa lao walikuwa wamemfungulia njia Shetani kupata njia kwa urahisi zaidi, na haikuwa salama kwao kubaki katika bustani ya Edeni, wasije katika hali yao ya dhambi wapate kuufikia mti wa uzima na kuendeleza maisha ya dhambi. Walisihi waruhusiwe kubaki Edeni, ingawa walikiri kwamba walikuwa wamepoteza haki zote kwa Edeni yenye furaha. Waliahidi kwamba katika wakati ujao wangejitoa kwa Mungu kwa utii kamili. Walifahamishwa kwamba katika Anguko lao kutoka kutokuwa na hatia hadi hatia hawakupata nguvu bali udhaifu mkubwa. Hawakuweza kudumisha uaminifu wao walipokuwa bado katika hali ya utakatifu na furaha ya kutokuwa na dhambi. Kwa hiyo, sasa wakiwa katika hali ya dhambi na hatia, wangekuwa na nguvu kidogo zaidi ya kubaki waaminifu na watiifu kwa Mungu. Walijaa huzuni kubwa, maumivu ya moyo, na majuto makali kwa kile walichokifanya. Sasa walielewa wazi kwamba adhabu ya dhambi ni kifo. **{SRSw 40.3}**

Malaika waliagizwa kulinda mara moja njia ya Mti wa Uzima. Ilikuwa ni mpango wa Shetani kwamba Adamu na Hawa wamwasi Mungu, kupokea kipaji Chake, na kisha kushiriki katika mti wa uzima, ili waweze kuendeleza maisha ya dhambi milele. Lakini Malaika

Watakatifu walitumwa kuweka njia yao kwenye Mti wa Uzima. Karibu na malaika hawa waliangaza miale ya mwanga kila upande, ambayo ilikuwa na mwonekano wa panga zinazometa-meta. **{SRSw 41.1}**

SURA YA 5—MPANGO WA WOKOVU

Mbinguni palijaa huzuni ilipobainishwa kwamba mwanadamu alikuwa amepotea na ulimwengu ule ambao Mungu alikuwa ameuumba ulipaswa kujazwa na wanadamu waliohukumiwa kwa taabu, magonjwa, na kifo, na hapakuwa na njia ya kuokolewa kwa mkosaji. Familia nzima ya Adamu lazima ife. Nilimwona Yesu Mwenye upendo na mwema na nikaona mwonekano wa huruma na huzuni juu ya uso Wake. Muda si

muda nilimwona akikaribia nuru angavu iliyomfunika Baba. Alisema malaika wangu aliyeandamana nami, Yuko katika mazungumzo ya karibu na baba Yake. Wasiwasi wa malaika ulionekana kuwa wa kina kikubwa, wakati Yesu alipokuwa akiwasiliana na Baba Yake. Mara tatu alifunikwa ndani ya nuru mtukufu iliyomzunguka Baba, na mara ya tatu alipotoka kwa Baba, sura (nafsi) Yake ilionekana. Uso Wake ulikuwa mtulivu, usio na mifadhaiko na mashaka yote, na uling'aa kwa wema na uzuri, ambao maneno hayawezi kueleza. **{SRSw 42.1}**

Kisha aliwajulisha jeshi la malaika kwamba njia ya kuokolewa ilikuwa imefanywa kwa mwanadamu aliyepotea. Aliwaambia kwamba alikuwa akimsihi Baba Yake, na kwamba amejitoa kutoa maisha Yake kuwa fidia, kuchukua hukumu ya kifo juu Yake Mwenyewe, ili kupitia Yeye na haki Yake, mwanadamu apate msamaha; ili kwa njia ya damu Yake, na utii kwa sheria ya Mungu, wangeweza kupata kibali cha Mungu na kuletwa tena katika bustani nzuri na kula matunda ya mti wa uzima. **{SRSw 42.2}**

Mwanzoni malaika hawakuweza kufurahi, kwa kuwa Kiongozi wao hakuwaficha chochote, lakini aliwafunulia mpango wa wokovu mbele yao. Yesu aliwaambia kwamba Yeye angesimama kati ya ghadhabu ya Baba Yake na mtu mwenye hatia, kwamba atabeba uovu na dharau, na ni wachache wangempokea kama Mwana wa Mungu. Karibu wote wangemchukia na kumkataa. Angeuacha utukufu Wake wote mbinguni, akionekana duniani kama mwanadamu, akijinyenyekeza kama mwanadamu, akijifunza kwa uzoefu Wake Mwenyewe na majaribu mbalimbali ambayo mwanadamu angepatwa nayo, ili apate kujua jinsi ya kuwasaidia wale wanaojaribiwa; na kwamba hatimaye, baada ya utume Wake kama mwalimu ungekamilika, angewekwa mikononi mwa wanadamu na kuvumilia karibu kila ukatili na mateso ambayo Shetani na malaika zake wangeweza kuwatia moyo watu waovu

kuwatendea; kwamba angekufa kifo cha kikatili zaidi, kwa kutundikwa kati ya mbingu na dunia kama mwenye dhambi mwenye hatia; Kwamba angeteseka kwa masaa ya kutisha ya uchungu, ambayo hata malaika hawakuweza kutazama, bali wangefunika nyuso zao wasione. Sio tu uchungu wa mwili ambao angeweza kuteseka, bali pia uchungu wa kiakili, ambao mateso ya mwili hayangeweza kulinganishwa kwa njia yoyote. Uzito wa dhambi za ulimwengu wote, ungekuwa juu Yake. Aliwaambia angekufa na kufufuka tena siku ya tatu, na angepanda Kwenda kwa Baba Yake ili kumwombea mtu aliyepotoka, mwenye hatia. **{SRSw 43.1}**

Njia Moja Inayowezekana ya Wokovu

Malaika walisujudu mbele Yake. Walitoa maisha yao. Yesu aliwaambia kwamba kwa kifo Chake angewaokoa wengi, kwamba maisha ya malaika hayangeweza kulipa deni. Maisha Yake pekee yangeweza kukubaliwa na Baba Yake kama fidia ya mwanadamu. Yesu pia aliwaambia kwamba watakuwa na sehemu ya kutenda, kuwa pamoja Naye na katika nyakati tofauti kumtia nguvu; kwamba angechukua asili ya mwanadamu iliyoanguka, na nguvu Zake hazingekuwa sawa na zao; kwamba wangekuwa mashahidi wa unyonge Wake na mateso Yake makubwa; na kwamba pale watakaposhuhudia haya mateso Yake na chuki ya watu Kwake, wangechochewa na hisia za ndani kabisa, na kwa upendo wao Kwake wangetaka kumwokoa na kumkomboa kutoka kwa wauaji Wake; lakini kwamba hawapaswi kuingilia kati ili kuzuia chochote wanachopaswa kutazama; na kwamba wachukue sehemu katika ufufuo Wake; kwamba mpango wa wokovu ulibuniwa, na Baba Yake, Naye alikuwa amekubali mpango huo. **{SRSw 43.2}**

Kwa huzuni takatifu Yesu aliwafariji na kuwapa moyo malaika na kuwajulisha kwamba baadaye wale ambao angewakomboa watakuwa pamoja Naye, na kwamba kwa kifo Chake, awakomboe wengi na

kumwangamiza yeye ambaye alikuwa na nguvu za kifo. Na Baba Yake angempa ufalme na ukuu wa ufalme chini ya mbingu yote, na angeumiliki milele na milele. Shetani na wanadamu wenye dhambi wangeangamizwa, kamwe wasisumbue mbingu au dunia mpya iliyotakaswa. Yesu aliamuru jeshi la mbinguni lipatanishwe na mpango ambao Baba Yake alikuwa ameukubali na kufurahi kwamba kupitia kifo Chake, mwanadamu aliyeanguka angeweza tena kuinuliwa ili kupata kibali kwa Mungu na kufurahia mbinguni. **{SRSw 44.1}**

Kisha furaha, furaha isiyoelezeka, ikajaza mbingu. Na jeshi la mbinguni likaimba wimbo wa sifa na ibada. Waligusa vinubi vyao na kuimba noti ya juu zaidi kuliko walivyokuwa wamefanya hapo awali, kwa ajili ya rehema kubwa na unyenyekevu wa Mungu katika kumtoa Mpendwa Wake, awe mwanadamu na kuja hapa chini, na kisha afe kwa ajili ya jamii ya waasi. Sifa na ibada zilimiminwa kwa ajili ya kujikana nafsi na dhabihu ya Yesu; Kwamba angekubali kuondoka kifuani mwa Baba Yake na kuchagua maisha ya mateso na uchungu, na kufa kifo cha aibu ili kuwapa wengine uzima. **{SRSw 44.2}**

Malaika akasema, “Mnadhani ya kwamba Baba alimtoa Mwanawe mpendwa bila mapambano? La, la. Hakika kulikuwa na pambano kwa Mungu wa mbinguni, iwapo angemwacha mwanadamu mwenye hatia aangamie, au kumtoa Mwanawe mpendwa afe kwa ajili yake. Malaika walipendezwa sana na wokovu wa mwanadamu kiasi kwamba wangeweza kupatikana miongoni mwao wale ambao wangetoa utukufu wao na kutoa uhai wao kwa ajili ya mwanadamu anayeangamia, “lakini,” akasema malaika wangu aliyeandamana nami, “hilo lisingefaa kitu. Uasi huo ulikuwa mkubwa sana kiasi kwamba uhai wa malaika haungelipa deni hilo. Hakuna chochote ila kifo na maombezi ya Mwanawe ndio vingelipa deni na kumwokoa mtu aliyepotea kutokana na huzuni na taabu zisizo na tumaini.” **{SRSw 45.1}**

Lakini kazi ya Malaika waliyopewa, ni kupanda na kushuka, wakiwa na zeri ya kutia nguvu kutoka utukufuni ili kumfariji Mwana wa Mungu katika mateso Yake na kumhudumia. Pia, kazi yao ingekuwa kulinda na kuwaweka raia walio chini ya neema dhidi ya malaika waovu na giza linalotupwa karibu nao kila mara na Shetani. Niliona kwamba haikuwezekana kwa Mungu kubadilisha au kuigeuza sheria Yake ili kuokoa mtu aliyepotea, anayeangamia; Kwa hiyo alimruhusu Mwanawe mpendwa kufa kwa ajili ya kosa la mwanadamu. **{SRSw 45.2}**

Shetani alifurahi tena pamoja na malaika wake kwamba kwa kusababisha anguko la mwanadamu, angeweza, kumshusha Mwana wa Mungu kutoka katika cheo Chake kilichotukuka. Aliwaambia malaika wake kwamba wakati Yesu anapaswa kuchukua asili ya mwanadamu aliyeanguka, angeweza kumshinda na kuzuia utimilifu wa mpango wa wokovu. **{SRSw 45.3}**

Nilionyeshwa Shetani kama alivyokuwa hapo awali, malaika mwenye furaha, aliyetukuka. Kisha nikaonyeshwa jinsi alivyo sasa. Bado ana umbo la kifalme. Sifa zake na sehemu za uso wake bado ni nzuri, kwa kuwa yeye ni malaika aliyeanguka. Lakini mwonekano wa usemi wa uso wake umejaa wasiwasi, masumbufu, kutokuwa na furaha, uovu, chuki, uovu, udanganyifu, na kila uovu. Paji la uso ambalo hapo awali lilikuwa la heshima/uungwana na ubora sana, nililiona haswa. Paji la uso wake lilianza kutoka kwa macho yake hadi kupungua. Niliona kwamba kwa muda mrefu alikuwa amejiinamia kwa uovu kiasi kwamba kila sifa nzuri iliharibiwa, na kila sifa mbaya ilikuzwa. Macho yake yalikuwa ya hila, ya ujanja, na yalionyesha kupenya sana. Umbo lake lilikuwa kubwa, lakini nyama ilining'inia kwenye mikono na uso wake. Nilipomtazama, kidevu chake kilikuwa kimeegemea kwenye mkono wake wa kushoto. Alionekana kuwa na mawazo mazito. Tabasamu lilikuwa juu ya uso wake, ambalo lilinifanya nitetemeke, kwa kuwa

lilikuwa limejaa uovu na ujanja wa kishetani. Tabasamu hili ndilo analovaa kabla hajathibisha kumpata mhanga wake, na anapomnasa mmhanga katika mtego wake, tabasamu hili linakuwa la kutisha. **{SRSw 45.4}**

Katika unyenyekevu na huzuni isiyoelezeka Adamu na Hawa waliondoka kwenye bustani nzuri ambamo walikuwa wamefurahi sana hadi walipokosa kutii amri ya Mungu. Hali ya anga ilibadilika. Haikuwa tena ile ile isiyobadilika kama ilivyokuwa kabla ya uvunjaji wa sheria. Mungu aliwavika mavazi ya ngozi ili kuwalinda kutokana na hali ya ubaridi na kisha joto ambalo walikuwa wanakabiliana nalo. **{SRSw 46.1}**

Sheria ya Mungu Isiyobadilika

Mbingu zote ziliomboleza kwa sababu ya kutotii na kuanguka kwa Adamu na Hawa, ambayo ililileta ghadhabu ya Mungu juu ya jamii yote ya wanadamu. Walikatiliwa mbali na kuwasiliana na Mungu, na waliangukia katika taabu isiyo na matumaini. Sheria ya Mungu isingeweza kubadilishwa ili kukidhi ulazima wa mwanadamu, kwa kuwa katika mpangilio wa Mungu haikupaswa kamwe kupoteza nguvu zake wala kuacha sehemu ndogo zaidi ya madai yake. **{SRSw 46.2}**

Malaika wa Mungu waliagizwa kuwatembelea wanandoa hao walioanguka na kuwajulisha kwamba ingawa hawakuweza tena kuhifadhi mali yao takatifu, makazi yao ya Edeni, kwa sababu ya uvunjaji wao wa sheria ya Mungu, lakini hata kama hali yao ilikuwa hivyo hawakupaswa kukata tamaa kabisa. Kisha wakafahamishwa kwamba Mwana wa Mungu, ambaye alikuwa amezungumza nao katika Edeni, alikuwa amesukumwa na huruma alipokuwa akiona hali yao ya kutokuwa na tumaini, na alikuwa amejitolea kuchukua juu yake adhabu inayostahili kwao, na kufa kwa ajili yao ili mwanadamu aishi tena, kwa njia ya imani katika upatanisho ambao Kristo alipendekeza kufanya kwa

ajili yake. Kupitia Kristo mlango wa tumaini ulifunguliwa, kwamba mwanadamu, ijapokuwa dhambi yake ni kubwa, hapaswi kuwa chini ya udhibiti kamili wa Shetani. Imani katika sifa za Mwana wa Mungu ingempandisha mwanadamu kiasi kwamba angeweza kupinga hila za Shetani. Angepewa rehema, kisha kupitia maisha ya toba na imani katika upatanisho wa Mwana wa Mungu, angeweza kukombolewa kutoka katika uvunjaji wake wa sheria ya Baba, na hivyo kuinuliwa hadi mahali ambapo jitihada zake za kushika sheria Yake zingeweza kukubaliwa. **{SRSw 46.3}**

Malaika waliwaelezea huzuni iliyokuwa ikihisiwa/kuonekana mbinguni ilipotangazwa kwamba walikuwa wamevunja sheria ya Mungu, jambo lililofanya iwe lazima kwa Kristo kutoa dhabihu kuu ya maisha Yake ya thamani. **{SRSw 47.1}**

Wakati Adamu na Hawa walipotambua jinsi sheria ya Mungu ilivyokuwa imetukuka na takatifu, ambayo kuvunjwa kwake kulihitaji dhabihu ya gharama kubwa sana kuwaokoa na uzao wao kutokana na uharibifu mkubwa, waliomba wao wenyewe wafe, au kuwaacha wao na uzao wao wavumilie adhabu ya uasi wao; badala ya kwamba Mwana mpendwa wa Mungu kutoa dhabihu hii kuu. Uchungu wa Adamu uliongezeka. Aliona kwamba dhambi zake zilikuwa za ukubwa mkubwa kiasi cha kuhusisha matokeo ya kutisha. Na je, ni lazima iwe hivyo kwa Kiongozi wa heshima, ambaye alikuwa ametembea naye na kuzungumza naye akiwa katika hali yake takatifu na kutokuwa na hatia, ambaye malaika walimheshimu na kumwabudu, Je, ilimpasa ashushwe kutoka katika nafasi Yake iliyotukuka ili afe kwa sababu ya kosa lake? **{SRSw 47.2}**

Adamu alijulishwa kwamba uhai wa malaika usingeweza kulipa deni. Sheria ya Yehova, msingi wa serikali Yake mbinguni na juu ya nchi, ilikuwa takatifu kama Mungu Mwenyewe; Na kwa sababu hii

maisha ya malaika hayangeweza kukubaliwa na Mungu kama dhabihu kwa ajili ya uvunjaji wake. Sheria Yake ni muhimu zaidi machoni Pake kuliko malaika watakatifu walio karibu na kiti Chake cha enzi. Baba hakuweza kukomesha au kubadilisha hata kanuni moja ya sheria Yake ili kukutana na mwanadamu katika hali yake ya kuanguka. Lakini Mwana wa Mungu, ambaye alikuwa ameungana na Baba, Aliyemuumba mwanadamu, angeweza kufanya upatanisho kwa ajili ya mwanadamu kukubalika kwa Mungu, kwa kutoa maisha Yake dhabihu na kubeba ghadhabu ya Baba Yake. Malaika walimjulisha Adamu kwamba, kwa vile kosa lake lilileta kifo na unyonge, uzima na kutokufa vingewekwa kwenye nuru kupitia dhabihu ya Yesu Kristo. **{SRSw 48.1}**

Mtazamo Wa Wakati Ujao

Adamu alifunuliwa matukio muhimu ya baadaye, tangu kufukuzwa kwake kutoka Edeni hadi Gharika, na kuendelea hadi ujio wa kwanza wa Kristo duniani; Upendo Wake kwa Adamu na uzao wake ungemwongoza Mwana wa Mungu kujishusha chini, kuchukua asili ya kibinadamu, na hivyo kuwainua, kupitia kujinyenyekeza Kwake Mwenyewe, wote ambao wangemwamini. Sadaka hiyo ilikuwa ya thamani ya kutosha kuokoa ulimwengu wote; Lakini ni wachache tu ambao wangefaidika wenyewe kwa wokovu ulioletwa kwao kupitia dhabihu hiyo ya ajabu. Wengi hawangezingatia masharti yanayotakiwa kwao ili waweze kuwa washiriki wa wokovu Wake mkuu. Wangependelea dhambi na uvunjaji wa sheria ya Mungu badala ya toba na utii, wakitegemea kwa imani juu ya sifa za dhabihu iliyotolewa. Dhabihu hii ilikuwa ya thamani isiyo na kikomo kiasi cha kumfanya mtu ambaye angejinufaisha nayo, kuwa wa thamani zaidi kuliko dhahabu safi, hata mtu kuliko kabari ya dhahabu ya Ofiri. **{SRSw 48.2}**

Adamu alichukuliwa mpaka katika vizazi vilivyofuata na kuona ongezeko la uhalifu, hatia na unajisi, kwa sababu mwanadamu

angekubali mielekeo yake yenye nguvu ya kiasili ya kukiuka sheria takatifu ya Mungu. Alionyeshwa laana ya Mungu ikiegemea zaidi na zaidi juu ya jamii ya wanadamu kwa uzito mkubwa, juu ya wanyama, na juu ya ardhi, kwa sababu ya kuendelea kwa makosa ya mwanadamu. Alionyeshwa kwamba uovu na vurugu zingeongezeka kwa kasi; Bado katikati ya wimbi la taabu na ole wa mwanadamu, kungekuwa na wachache ambao wangehifadhi maarifa ya Mungu na wangebaki bila kuchafuliwa katikati ya kuzorota kwa maadili. Adamu alifanywa kuelewa dhambi ni nini—yaani uvunjaji wa sheria. Alionyeshwa kwamba kuzorota kwa maadili, kiakili, na kimwili kungetokea kwa jamii ya wanadamu kutokana na makosa, hadi ulimwengu ungejawa na taabu za kibinadamu za kila aina. **{SRSw 49.1}**

Siku za mwanadamu zilifupishwa na mwenendo wake wa dhambi katika kukiuka sheria ya haki ya Mungu. Hatimaye jamii ya wanadamu ilishuka thamani sana kiasi kwamba ilionekana kuwa duni na karibu kukosa thamani kabisa. Kwa ujumla hawakuwa na uwezo wa kufahamu fumbo la Kalvari, Ukweli mkuu na ulioinuliwa wa upatanisho, na mpango wa wokovu, kwa sababu ya kufuata tamaa za mwili. Hata hivyo, ijapokuwa udhaifu huo, na kudhoofika kiakili, kiadili, na nguvu za kimwili za wanadamu, Kristo, aliendekea kuwa Mkweli kwa kusudi ambalo aliondoka mbinguni, anaendelea kupendezwa na walio dhaifu, walioshuka thamani, na walioharibika, na huwaalika wanadamu kuficha udhaifu wao na mapungufu makubwa ndani Yake Yeye. Ikiwa watakuja Kwake, atawatimizia mahitaji yao yote. **{SRSw 49.2}**

Sadaka ya Dhabihu

Wakati Adamu, kulingana na maagizo maalum ya Mungu, alipotoa sadaka kwa ajili ya dhambi, ilikuwa kwake sherehe yenye maumivu makubwa sana (chungu sana). Mkono wake ulipaswa kuinuliwa ili kutoa uhai, ambao Mungu pekee angeweza kutoa, na kutoa sadaka kwa ajili ya

dhambi. Ilikuwa ni mara yake ya kwanza kushuhudia kifo. Alipokuwa akimtazama mnyama aliyekuwa akivuja damu akihema kwa uchungu wa kifo, alipaswa kutazamia kwa imani Mwana wa Mungu, ambaye huyo mnyama alimtangulia, ambaye angekufa kuwa dhabihu ya mwanadamu. **{SRSw 50.1}**

Sadaka hii ya sherehe/kaida, iliwekwa na Mungu, na ilipaswa kuwa ukumbusho wa daima kwa Adamu wa hatia yake, na pia kukiri kwa toba ya dhambi yake. Kitendo hiki cha kuchukua uhai kilimpa Adamu hisia ya ndani zaidi na kamilifu zaidi ya kosa lake, ambalo hakuna chochote kingeweza kufanya upatanisho isipokuwa kifo cha Mwana mpendwa wa Mungu. Alistaajabia wema usio na kikomo na upendo mwanana usio na kifani ambao ungetoa fidia kama hiyo kuokoa wenye hatia. Adamu alipokuwa akimwua mnyama asiye na hatia, ilionekana kwake kwamba alikuwa akimwaga damu ya Mwana wa Mungu kwa mkono wake mwenyewe. Alijua kwamba kama angebaki imara kwa Mungu, na Kweli kwa sheria Yake takatifu, kusingekuwa na kifo cha mnyama wala mwanadamu. Hata hivyo katika sadaka za dhabihu, zilizokuwa zikielekeza kwenye dhabihu kuu na kamilifu ya Mwana mpendwa wa Mungu, kulionekana nyota ya matumaini ya kuangazia wakati ujao wa giza na wa kutisha, na kuiondolea kutokuwa na tumaini kabisa na uharibifu. **{SRSw 50.2}**

Hapo mwanzo mkuu wa kila familia alichukuliwa kuwa mtawala na kuhani wa nyumba yake mwenyewe. Baadaye, jamii ilipoongezeka juu ya dunia, watu walioteuliwa na Mungu walifanya ibada hii kuu ya dhabihu kwa ajili ya watu. Damu ya wanyama ilipaswa kuhusishwa katika akili za wenye dhambi na damu ya Mwana wa Mungu. Kifo cha mnyama kilikuwa ni ushahidi kwa wote kwamba adhabu ya dhambi ilikuwa kifo. Kwa tendo la dhabihu, mwenye dhambi alikiri hatia yake na kudhihirisha imani yake, akitarajia dhabihu kuu na kamilifu ya

Mwana wa Mungu, ambayo sadaka ya wanyama ilimwakilisha. Bila upatanisho wa Mwana wa Mungu hakuwezi kuwa na mawasiliano ya baraka au wokovu kutoka kwa Mungu kwenda kwa mwanadamu. Mungu alikuwa na wivu kwa heshima ya sheria Yake. Ukiukaji wa sheria hiyo ulisababisha utengano wa kutisha kati ya Mungu na mwanadamu. Adamu katika kutokuwa na hatia alipewa ushirika, moja kwa moja, huru, na furaha, na Muumba wake. Baada ya kosa lake Mungu angewasiliana na mwanadamu kupitia Kristo na malaika [maombi, asili, njozi, ndoto, Roho Mtakatifu, na miujiza mara zingine]. **{SRSw 50.3}**

SURA YA 6—KAINI NA ABELI NA SADAKA ZAO

Sura hii imejengwa katika Mwanzo 4:1-15.

Kaini na Abeli, wana wa Adamu, walikuwa tofauti sana katika tabia. Habili alimcha Mungu. Kaini alithamini hisia za uasi na kunung'unika dhidi ya Mungu kwa sababu ya laana iliyotamkwa juu ya Adamu na kwa sababu ardhi ililaaniwa kwa ajili ya dhambi yake. Ndugu hawa walikuwa wameagizwa kuhusiana na utoaji uliofanywa kwa ajili ya wokovu wa wanadamu. **{SRSw 52.1}**

Walitakiwa kutekeleza mfumo wa utii wa unyenyekevu, wakionyesha kicho kwa Mungu na imani yao na utegemezi wao juu ya Mkombozi aliyeahidiwa, kwa kuwaua wazaliwa wa kwanza wa kundi la mifugo na kuwaleta kwa uzito pamoja na damu kama sadaka ya kuteketezwa kwa Mungu. Dhabihu hii ingewaongoza kuendelea kukumbuka dhambi yao na Mkombozi ajaye, ambaye alipaswa kuwa dhabihu kuu kwa ajili ya mwanadamu. Kaini alileta sadaka yake kwa Bwana kwa manung'uniko na ukafiri moyoni mwake kuhusiana na Dhabihu iliyoahidiwa. Hakuwa tayari kufuata kikamilifu mpango wa utii na kupata mwana-kondoo na kumpa mazao ya ardhi. Alichukua tu ardhi na kupuuza hitaji la Mungu. Mungu alikuwa amemjulisha Adamu kwamba bila kumwaga damu hakuwezi kuwa na ondoleo la dhambi. Kaini hakujali kuleta hata mazao yaliyo bora zaidi. Habili alimshauri ndugu yake asije mbele za Bwana bila damu ya dhabihu. Kaini, kama mmzaliwa wa kwanza (mkubwa), hakutaka kumsikiliza ndugu yake. Alidharau shauri lake, na kwa shaka na manung'uniko kuhusiana na ulazima wa sadaka ya sherehe ya dhabihu, aliwasilisha sadaka yake. Lakini Mungu hakuikubali. **{SRSw 52.2}**

Habili alileta wazaliwa wa kwanza wa kundi lake na mafuta, kama Mungu alivyoamuru; Na kwa imani kamili ya Masihi ajaye, na kwa kicho na unyenyekevu, alitoa sadaka. Mungu alipokea sadaka yake. Nuru ilimulika kutoka mbinguni na kuteketeza sadaka ya Abeli. Kaini hakuona udhihirisho wowote kwamba sadaka yake umekubaliwa.

Akamkasirikia Bwana na kaka yake. Mungu alishuka kumtuma malaika kwa Kaini ili kuzungumza naye. **{SRSw 53.1}**

Malaika akamwuliza sababu ya hasira yake, na kumjulisha kwamba ikiwa atafanya vizuri na kufuata maagizo ambayo Mungu ametoa, atamkubali na kuipokea sadaka yake. Lakini ikiwa hatajisalimisha kwa unyenyekevu kwa mipango ya Mungu, na kumwamini na kumtii, hawezi kukubali sadaka yake. Malaika anamwambia Kaini kwamba haikuwa dhuluma kwa upande wa Mungu, au upendeleo ulioonyeshwa kwa Abeli, lakini kwamba ilikuwa ni kwa sababu ya dhambi yake mwenyewe na kutotii amri ya Mungu iliyo wazi kwamba hangeweza kupokea sadaka yake—na kama angefanya vyema angekubaliwa na Mungu, na anapaswa kumsikiliza ndugu yake, na anapaswa kuongoza, kwa sababu alikuwa ndiye mkubwa. **{SRSw 53.1}**

Lakini hata baada ya kufundishwa hivyo kwa uaminifu, Kaini hakutubu. Badala ya kukubali na kuchukia kutokuamini kwake, bado alilalamikia dhuluma na upendeleo wa Mungu. Na katika wivu na chuki yake anashindana na Habili na kumlaumu. Habili kwa upole anaonyesha kosa la ndugu yake na kumwonyesha kwamba kosa liko ndani yake mwenyewe. Lakini Kaini anamchukia ndugu yake tangu wakati ambapo Mungu alimtolea ishara za kukubalika kwake. Ndugu yake Habili anatafuta kutuliza ghadhabu yake kwa kusisitiza huruma ya Mungu katika kuokoa maisha ya wazazi wao wakati angeweza kuwaletea kifo cha papo hapo. Anamwambia Kaini kwamba Mungu anawapenda, au asingemtoa Mwanawe, asiye na hatia na mtakatifu, kuteseka na ghadhabu ambayo mwanadamu, kwa kutotii kwake, alistahili kuteseka. **{SRSw 53.3}**

Mwanzo wa Kifo

Wakati Abeli anaona mpango wa Mungu ni wa haki na kuutekeleza, Kaini anakasirika, na hasira yake huongezeka na kuwaka juu ya Abeli hadi kwa hasira yake anamuua nduguye. Mungu anauliza juu ya Kaini kwa ndugu yake, na Kaini anasema uwongo wenye hatia: ***Akasema, Sijui, mimi ni mlinzi wa ndugu yangu? Mwanzo 4:9*** Mungu anamjulisha Kaini kwamba alijua kuhusu dhambi yake—kwamba alikuwa amelifahamu kila tendo lake, na hata mawazo ya moyo wake, na kumwambia; ***Akasema, Umefanya nini? Sauti ya damu ya ndugu yako inanililia kutoka katika ardhi. Basi sasa, umelaaniwa wewe katika ardhi, iliyofumbua kinywa chake ipokee damu ya ndugu yako kwa mkono wako; utakapoilima ardhi haitakupa mazao yake; utakuwa mtoro na mtu asiye na kikao duniani.*** **Mwanzo 4:10-12** **{SRSw 54.1}**

Laana juu ya ardhi mwanzoni ilikuwa imehisiwa kwa kiwango kidogo; Lakini sasa laana maradufu ilikaa juu yake. Kaini na Abeli wanawakilisha tabaka mbili za wanadamu, wenye haki na waovu, waumini na wasioamini, ambao wanaopaswa kuwepo tangu anguko la mwanadamu hadi ujio wa pili wa Kristo. Kaini kwa kumuua ndugu yake Abeli kunawakilisha waovu ambao watawaonea wivu wenye haki na kuwachukia kwa sababu wao ni bora kuliko wao. Watawaonea wivu wenye haki na watawatesa na kuwaua kwa sababu matendo yao mema yanahukumu mwenendo wao wa dhambi. **{SRSw 54.2}**

Maisha ya Adamu yalikuwa ya huzuni, unyenyekevu, na toba ya daima. Alipokuwa akiwafundisha watoto wake na wajukuu kumcha Bwana, mara nyingi alishutumiwa vikali kwa ajili ya dhambi yake ambayo ilisababisha taabu nyingi sana juu ya uzao wake. Alipoondoka Edeni nzuri, wazo la kwamba lazima afe lilimchemsha moyo kwa hofu. Alikiona kifo kama msiba wa kutisha. Kwanza alifahamishwa na Ukweli wa kutisha wa kifo katika familia ya kibinadamu na mtoto wake mwenyewe Kaini akimuua ndugu yake Abeli. Akiwa amejawa na

majuto ya uchungu zaidi kwa kosa lake mwenyewe, na kunyimwa mwanawe Abeli, na kumtazama Kaini kama muuaji wake, na kujua laana ambayo Mungu alitamka juu yake, moyo wa Adamu uliinama kwa huzuni. Kwa uchungu zaidi alijilaumu kwa kosa lake kuu la kwanza. Aliomba msamaha kutoka kwa Mungu kupitia dhabihu iliyoahidiwa. Alikuwa amehisi ghadhabu ya Mungu kwa ajili ya uhalifu wake uliofanywa katika Paradiso. Alishuhudia ufisadi wa jumla ambao hatimaye ulimchochea Mungu kuwaangamiza wakaaji wa dunia kwa mafuriko. Hukumu ya kifo iliyotamkwa juu yake na Muumba wake, ambayo mwanzoni ilionekana kuwa ya kuogofya sana kwake, baada ya kuishi mamia ya miaka, ilionekana kuwa jambo la haki na huruma kwa Mungu kufanya, ili kukomesha maisha yenye huzuni ya kutisha. **{SRSw 55.1}**

Adamu aliposhuhudia dalili za kwanza za kuoza kwa asili katika jani linaloanguka na katika maua yaliyoinama, aliomboleza kwa kina/undani zaidi kuliko watu ambao sasa wanaomboleza juu ya wafu wao. Maua yaliyonyauka hayakuwa sababu ya kina ya huzuni, kwa sababu ni laini na dhaifu; Lakini miti mirefu, yenye heshima, yenye nguvu ilipoanza kuachia majani yake na kuoza, iliwasilisha mbele yake mvunjiko wa jumla wa asili nzuri, ambayo Mungu alikuwa ameiumba kwa manufaa ya pekee ya mwanadamu. **{SRSw 55.2}**

Kwa watoto wake na kwa watoto wao, kwa kizazi cha tisa, alifafanua ukamilifu wa makazi yake ya Edeni, na pia anguko lake na matokeo yake ya kutisha, na mzigo wa huzuni uliletwa juu yake kwa sababu ya mpasuko katika familia yake ambao uliishia katika kifo cha Habili. Aliwasimulia mateso ambayo Mungu alikuwa amemletea, ili kumfundisha ulazima wa kuambatana kabisa na sheria Yake. Aliwatangazia kwamba dhambi ingeadhibiwa kwa namna yoyote ile.

Aliwasihi wamtii Mungu, ambaye angeshughulika nao kwa rehema ikiwa wangempenda na kumcha. **{SRSw 55.3}**

Malaika waliwasiliana na Adamu baada ya anguko lake, na wakamjulisha kuhusu mpango wa wokovu, na kwamba jamii ya wanadamu haikuwa nje ya uwezekano wa kukombolewa. Ingawa utengano wa kutisha ulikuwa umetukia kati ya Mungu na mwanadamu, lakini mpango ulikuwa umefanywa kupitia dhabihu ya Mwana Wake mpendwa ambao kupitia huo mwanadamu angeweza kuokolewa. Lakini tumaini lao pekee lilikuwa kupitia maisha ya toba ya unyenyekevu na imani katika mpenyo na mpango uliotolewa. Wale wote ambao wangeweza kumkubali Kristo kama Mwokozi wao pekee, wangeweza kuletwa tena katika kibali cha Mungu kupitia sifa, haki na wema wa Mwanawe. **{SRSw 56.1}**

SURA YA 7—SETHI NA HENOKO

Sura hii imejengwa katika Mwanzo 4:25, 26; 5:3-8, 18-24; Yuda 14, 15.

Sethi alikuwa mtu mwenye tabia njema, na alipaswa kuchukua nafasi ya Habili katika kutenda haki. Hata hivyo alikuwa mwana wa Adamu, kama Kaini mwenye dhambi, na alirithi kutoka kwa asili ya Adamu bila kuwa na wema wa asili zaidi kuliko alivyokuwa nao Kaini. Alizaliwa katika dhambi, lakini kwa neema ya Mungu, katika kupokea maagizo ya uaminifu ya Baba yake Adamu, alimheshimu Mungu katika kufanya mapenzi Yake. Alijitenga na wazao wapotovu wa Kaini, na kufanya kazi, kama Habili angefanya kama angeishi, kugeuza mawazo ya watu wenye dhambi kumheshimu na kumtii Mungu. **{SRSw 57.1}**

Henoko alikuwa mtu mtakatifu. Alimtumikia Mungu kwa moyo mmoja. Alitambua upotovu wa familia ya kibinadamu na akajitenga na wazao wa Kaini, na akawakemea kwa uovu wao mkubwa. Kulikuwa na wale duniani waliomkiri Mungu, waliomcha na kumwabudu. Hata hivyo Henoko mwenye haki alihuzunishwa sana na uovu unaoongezeka wa wanadamu wasiomcha Mungu, hata asingeshirikiana nao kila siku, akihofia kwamba angeathiriwa na ukafiri wao na kwamba mawazo yake yasingeweza kamwe kumchukulia Mungu kwa kicho/heshima hiyo takatifu ambayo ilistahili. tabia iliyoinuliwa. Nafsi yake ilifadhaika aliposhuhudia kila mara kukanyaga kwao mamlaka ya Mungu. Alichagua kujitenga nao, na alitumia muda wake mwingi katika faragha, ambao aliutumia kutafakari na kusali. Alingoja mbele za Mungu na akaomba kujua mapenzi Yake kikamilifu zaidi, ili aweze kuyatimiza. Mungu alizungumza na Henoko kupitia malaika Wake na kumpa maagizo ya Kiungu. Alimjulisha kwamba Yeye hatamvumilia

mwanadamu daima katika uasi wake sikuzote—kwamba kusudi Lake lilikuwa kuharibu jamii yenye dhambi kwa kuleta Gharika ya maji juu ya dunia. **{SRSw 57.2}**

Bustani safi na ya kupendeza ya Edeni, ambayo wazazi wetu wa kwanza walifukuzwa, ilibakia hadi Mungu alipokusudia kuiangamiza dunia kwa Gharika. Mungu alikuwa ameipanda bustani hiyo na kuibariki hasa, na katika majaliwa Yake ya ajabu aliitoa kutoka duniani, na atairudisha duniani tena ikiwa imepambwa kwa utukufu zaidi kuliko ilivyokuwa kabla haijaondolewa duniani. Mungu alikusudia kuhifadhi kielelezo cha kazi Yake kamilifu ya uumbaji bila laana ambayo kwayo alikuwa ameilaani dunia. Bwana alifungua kikamilifu zaidi kwa Henoko mpango wa wokovu, na kwa Roho ya unabii akamwonyesha kupitia vizazi ambavyo vilipaswa kuishi baada ya Gharika, na kumwonyesha matukio makubwa yanayohusiana na ujio wa pili wa Kristo na mwisho wa ulimwengu. **(Yuda 1:14.)** **{SRSw 58.2}**

Henoko alifadhaika kuhusiana na wafu. Ilionekana kwake kwamba wenye haki na waovu wangeenda mavumbini pamoja, na huo ndio ungekuwa mwisho wao. Hakuweza kuona wazi maisha ya watu baada ya kaburi. Katika maono ya kinabii aliagizwa kuhusiana na Mwana wa Mungu, ambaye angekufa kama dhabihu ya mwanadamu, na alionyeshwa ujio wa Kristo katika mawingu ya mbinguni, akisindikizwa na jeshi la malaika, kuwapa uzima wafu wenye haki na kuwakomboa kutoka kwenye makaburi yao. Pia aliona hali potovu ya ulimwengu wakati ambapo Kristo angetokea mara ya pili—kwamba kungekuwa na kizazi chenye majivuno, chenye majivuno, ujuvi, ukaidi na chenye kujifanyia mapenzi yake, kilichojiwekwa katika uasi dhidi ya sheria ya Mungu na kumkana Bwana Mungu wa pekee na Bwana wetu Yesu Kristo, na kikikanyaga damu Yake na kudharau upatanisho Wake. Aliwaona wenye haki wakiwa wamevikwa taji ya utukufu na heshima

huku waovu wakitengwa na uwepo wa Bwana na kuteketezwa kwa moto. **{SRSw 58.3}**

Henoko aliwafunza watu kwa uaminifu yote ambayo Mungu alikuwa amemfunulia kwa roho ya unabii. Wengine waliamini maneno yake na wakageuka kutoka katika uovu wao na kumcha na kumwabudu Mungu. **{SRSw 59.1}**

Henoko Anyakuliwa

Henoko aliendelea kukua zaidi katika mambo ya mbinguni huku akiwasiliana na Mungu. Uso wake ulikuwa unang'aa kwa nuru takatifu ambayo ingebaki juu ya uso wake, huku akiwaelekeza wale ambao wangesikia maneno yake ya hekima. Mwonekano wake wa mbinguni na wa hadhi/heshima uliwashangaza watu. Bwana alimpenda Henoko kwa sababu alimfuata kwa uthabiti na kuchukia uovu na kutafuta maarifa ya mbinguni kwa bidii, ili afanye mapenzi Yake kikamilifu. Alitamani kuungana kwa ukaribu zaidi na Mungu, ambaye alimcha, kumheshimu, na kumwabudu. Mungu hangemruhusu Henoko afe kama wanadamu wengine, bali aliwatuma malaika Wake wampeleke mbinguni bila kuona kifo. Mbele ya wenye haki na waovu, Henoko aliondolewa kutoka kwao. Wale waliompenda walifikiri kwamba Mungu angeweza kumwacha katika baadhi ya sehemu zake za faragha, lakini baada ya kumtafuta kwa bidii, na kutoweza kumpata, waliripoti kwamba hayupo, kwa maana Mungu alikuwa amemchukua. **{SRSw 59.2}**

Bwana hapa anafundisha somo la umuhimu mkubwa zaidi kwa kunyakuliwa kwa Henoko, mzaliwa wa Adamu aliyeanguka, kwamba wote watapokea thawabu, ambao kwa imani wangeitegemea dhabihu iliyoahidiwa na kutii amri Zake kwa uaminifu. Makundi mawili yamewakilishwa hapa tena ambayo yangekuwepo hadi Ujio wa Pili wa Kristo—wenye haki na waovu, waasi na waaminifu. Mungu

atawakumbuka wenye haki, wanaomcha Yeye. Kwa sababu ya Mwana Wake mpendwa atawaheshimu na kuwapokea na kuwapa uzima wa milele. Lakini waovu, wanaokanyaga mamlaka Yake, Yeye atawakatilia mbali na kuwaangamiza duniani, nao watakuwa kana kwamba hawakuwapo. **{SRSw 59.3}**

Baada ya kuanguka kwa Adamu kutoka katika hali ya furaha kamilifu hadi hali ya taabu na dhambi, kulikuwa na hatari ya mwanadamu kuvunjika moyo na kuuliza, "**Tumepata faida gani kwa kuyashika maagizo Yake, na kwa kwenda kwa huzuni mbele za Bwana wa majeshi? Malaki 3:14** kwa kuwa laana nzito iko juu ya jamii ya wanadamu, na kifo ni fungu letu sote? Lakini maagizo ambayo Mungu alimpa Adamu, na ambayo yalirudiwa na Sethi na kuonyeshwa kikamilifu na Henoko, yaliondoa giza na utusitusi, na kumpa mwanadamu tumaini, kwamba kama vile kupitia Adamu kifo mauti ilikuja, kwa njia ya Yesu, Mkombozi aliyeahidiwa, kungekuja uzima na kutokufa. **{SRSw 60.1}**

Katika kisa cha Henoko waumini waliokata tamaa walifundishwa kwamba, ingawa waliishi kati ya watu wafisadi, uovu uliokithiri na wenye dhambi, ambao walikuwa katika uasi wa wazi na wa kuthubutu dhidi ya Mungu, Muumba wao, lakini kama wangemtii Yeye na kuwa na imani katika Mkombozi aliyeahidiwa, wangeweza kutenda haki kama Henoko mwaminifu, kukubaliwa na Mungu, na hatimaye kuinuliwa kwenye kiti Chake cha enzi cha mbinguni. **{SRSw 60.2}**

Henoko, alijitenga na ulimwengu, na kutumia muda wake mwingi katika sala na ushirika na Mungu, anawakilisha watu waaminifu wa Mungu katika siku za mwisho, ambao watakuwa tofauti na ulimwengu. Udhalimu utatawala kwa kiwango cha kutisha juu ya dunia. Wanadamu watajitoa wenyewe kufuata kila fikira za mioyo yao potovu na

kutekeleza falsafa yao ya udanganyifu na kuasi mamlaka ya Mbingu ya Juu. **{SRSw 60.3}**

Watu wa Mungu watajitenga na mazoea yasiyo ya haki ya wale walio karibu nao, watatafuta usafi wa mawazo na upatanifu mtakatifu kwa mapenzi Yake hadi sura Yake ya Kiungu itakapoonyeshwa ndani yao. Kama Henoko, watachukua muda kupata stahiki za kunyakuliwa kwenda mbinguni. Ingawa wanajitahidi kufundisha na kuonya ulimwengu, hawatapatana na roho na desturi za wasioamini bali watawahukumu kwa mazungumzo yao matakatifu na kielelezo cha Kiungu. Kunyakuliwa kwa Henoko kwenda mbinguni kabla tu ya uharibifu wa ulimwengu kwa gharika inawakilisha kunyakuliwa kwa waadilifu wote walio hai kutoka duniani kabla ya kuharibiwa kwa moto. Watakatifu watatukuzwa mbele ya wale ambao wamewachukia kwa utii wao wa uaminifu kwa amri za haki za Mungu. **{SRSw 61.1}**

SURA YA 8—GHARIKA

Sura hii imejengwa katika Mwanzo 6; 7; 8 na 9:8-17.

Wazao wa Sethi waliitwa wana wa Mungu; Uzao wa Kaini, wana wa wanadamu. Wana wa Mungu walipochanganyikana na wana wa wanadamu, wakawa wapotovu, na kwa kuoana nao, wakapotea, kwa njia ya ushawishi wa wake zao, na kupoteza tabia yao ya kipekee, takatifu, na kuunganishwa na wana wa Kaini katika ibada yao ya sanamu. Wengi walitupilia mbali hofu ya Mungu na kukanyaga amri Zake. Lakini kulikuwa na wachache waliotenda haki, ambao walimcha na kumheshimu Muumba wao. Nuhu na familia yake walikuwa miongoni mwa watu wachache wenye haki. Uovu wa mwanadamu ulikuwa mkubwa sana, na uliongezeka kwa kiwango cha kutisha sana, hata Mungu alijuta kwamba alikuwa amemfanya mwanadamu juu ya dunia, kwa kuwa aliona kwamba uovu wa mwanadamu ulikuwa mkubwa, na kwamba kila mawazo katika fikra za moyo wake yalikuwa mabaya/uovu tu daima. **{SRSw 62.2}**

Zaidi ya miaka mia moja kabla ya gharika Bwana alimtuma malaika kwa Nuhu mwaminifu ili kumjulisha kwamba hatakuwa na huruma tena juu ya jamii iliyopotoka uovuni. Lakini hakutaka wasijue mpango Wake. Angemfundisha Nuhu na kumfanya mhubiri mwaminifu, kuonya ulimwengu juu ya uharibifu wake unaokuja, ili wakazi wa dunia wasiwe na udhuru. Nuhu alipaswa kuwahubiria watu, na pia kuandaa safina kama vile Mungu alivyomwelekeza kwa ajili ya kumwokoa yeye mwenyewe na familia. Hakupaswa kuhubiri tu, bali mfano wake katika kujenga safina ulikuwa kuwasadikisha wote kwamba aliamini kile alichohubiri. **{SRSw 62.3}**

Nuhu na familia yake hawakuwa peke yao katika kumcha na kumtii Mungu. Lakini Nuhu alikuwa mchamungu na mtakatifu kuliko yeyote duniani, na ndiye ambaye maisha yake Mungu aliyahifadhi ili kutekeleza mapenzi Yake katika kujenga safina na kuuonya ulimwengu juu ya maangamizi yake yanayokuja. Methusela, babu wa Nuhu, aliishi hadi mwaka uleule wa gharika; Na kulikuwa na wengine walioamini mahubiri ya Nuhu, na kumsaidia katika kujenga safina, ambao walikufa kabla ya gharika ya maji kufika juu ya nchi. Nuhu, kwa mahubiri yake na mfano wake katika kujenga safina, aliuhukumu ulimwengu. **{SRSw 63.1}**

Mungu aliwapa wote waliochagua fursa ya kutubu na kumgeukia. Lakini hawakuamini mahubiri ya Nuhu. Walidhihaki maonyo yake na kukejeli ujenzi wa chombo hicho kikubwa kwenye nchi kavu. Jitihada za Nuhu za kuwarekebisha wanadamu wenzake hazikufaulu. Lakini kwa zaidi ya miaka mia moja alivumilia katika jitihada zake za kuwageuza wanadamu kwenye toba na kwa Mungu. Kila pigo lililopigwa kwenye safina lilikuwa likihubiria watu. Nuhu alielekeza, alihubiri, alifanya kazi, huku watu wakitazama kwa mshangao na kumwona kuwa mwenye mtu shupavu, mwenye msimamo uliopitiliza. **{SRSw 63.2}**

Kujenga Safina

Mungu alimpa Nuhu vipimo kamili vya safina na maelekezo ya wazi kuhusiana na ujenzi wake katika kila jamb kwa kinagaubaga. Katika mambo mengi haikujengwa kama chombo/meli bali ilitayarishwa kama nyumba/makazi, msingi wake kama mashua ambayo ingeelea juu ya maji. Hakukuwa na madirisha kwenye pande za safina. Ilikuwa na orofa tatu juu, na mwanga waliopokea ulikuwa unatokae kwenye dirisha lililokuwa juu. Mlango ulikuwa pembeni. Vyumba tofauti vilivyotayarishwa kwa ajili ya mapokezi ya wanyama mbalimbali vilitengenezwa kiasi kwamba dirisha lililokuwa juu lilitoa mwanga kwa

wote. Safina ilitengenezwa kwa mti wa mtiriza au mvinje (cypress or gopher), ambao haungeweza kuoza kwa mamia ya miaka. Lilikuwa ni jengo la uimara mkubwa, ambalo hakuna hekima ya mwanadamu ingeweza kubuni. Mungu alikuwa mbunifu, na Nuhu mjenzi Wake Bwana mkuu. **{SRSw 63.3}**

Baada ya Nuhu kufanya yote katika uwezo wake kufanya kila sehemu ya kazi kuwa sahihi, haikuwezekana kwamba yenyewe ingeweza kustahimili jeuri ya dhoruba ambayo Mungu katika hasira yake kali alikuwa anaileta juu ya dunia. Kazi ya kukamilisha jengo ilikuwa mchakato wa polepole. Kila kipande cha mbao kilikuwa kilipimwa vizuri ili kiweze kutosha vyema (kufit), na kila muunganiko/mshono ulifunikwa na lami. Chochote kile ambacho mwanadamu angeweza kukifanya, kilifanywa, ili kuifanya kazi iwe kamilifu; Hata hivyo, baada ya yote, Mungu pekee Ndiye angeweza kuhifadhi mjengo huu juu ya mawimbi yenye hasira, kwa nguvu za miujiza Yake. **{SRSw 64.1}**

Yaonekana umati wa watu mwanzoni ulipokea onyo la Nuhu, lakini hawakumgeukia Mungu kwa ukamilifu, kwa toba ya kweli. Kulikuwa na muda waliopewa kabla ya gharika kuja, ambamo walipaswa kuwekwa kwenye chini ya angalizo—kuthibitishwa na kujaribiwa. Walishindwa kuvumilia jambo hilo. Uharibifu wa maadili ulioenea ulifanya washindwe, na hatimaye walijiunga na wengine ambao walikuwa wapotovu katika kumkejeli na kumdhihaki Nuhu mwaminifu. Hawakuacha dhambi zao bali waliendelea na mitala na kujifurahisha kwa kuendekeza tamaa zao potovu. **{SRSw 64.2}**

Kipindi cha rehema yao kilikuwa kinakaribia mwisho wake. Wakaaji wasioamini, wenye kutoa dhihaka wa ulimwengu, walipaswa kuwa na ishara maalum ya uwezo wa Mwenyezi Mungu. Nuhu alikuwa amefuata kwa uaminifu maagizo ambayo Mungu alikuwa amempa.

Safina ilikamilika kama vile Mungu alivyoelekeza. Alikuwa ameweka kiasi kikubwa cha chakula kwa ajili ya mwanadamu na mnyama. Na baada ya hayo kukamilika, Mungu alimwamuru Nuhu mwaminifu, **Bwana akamwambia Nuhu, Ingia wewe na jamaa yako yote katika safina; kwa maana nimekuona wewe u mwenye haki mbele Zangu katika kizazi hiki. Mwanzo 7:1** **{SRSw 64.3}**

Wanyama wanaingia kwenye safina

Malaika walitumwa kukusanya wanyama kutoka msituni ambao mashambani Mungu alikuwa amewaumba. Malaika waliwatangulia wanyama hawa, na wanyama wakawafuata, wawili kwa wawili, dume na jike, na wanyama safi saba-saba. Wanyama hawa, kuanzia wale wakali zaidi, hadi wale wapole na wasio na madhara, kwa amani na kwa taadhima waliingia ndani ya safina. Anga ilionekana kufunikwa na ndege wa kila aina. Walikuja wakiruka kuelekea safina, wawili na wawili, dume na jike, na ndege safi saba-saba. Ulimwengu ulitazama kwa mshangao—wengine kwa woga, lakini walikuwa wamekasirishwa sana na uasi kiasi kwamba udhihirisho huu wa ishara kuu na za nguvu za Mungu ulikuwa na ushawishi wa kitambo tu juu yao. Kwa muda wa siku saba wanyama hawa walikuwa wakiingia ndani ya safina, na Nuhu alikuwa akiwapanga mahali palipotayarishwa kwa ajili yao. **{SRSw 65.1}**

Na wakati jamii ile iliyokuwa inaenda kuhukumiwa na kuharibiwa ilipoona jua likiangaza katika utukufu wake na dunia ikiwa imevaa uzuri wake unaokaribia ule wa Edeni, walifukuza hofu zao zilizokuwa zinaendelea kuinuka kwa furaha yenye kelele na fujo, na kwa matendo yao ya ukatili, walionekana kuhamasisha kutembelewa na ghadhabu ya Mungu iliyoamshwa tayari. **{SRSw 64.2}**

Kila kitu kilikuwa tayari sasa kwa kufungwa kwa safina, jambo ambalo Nuhu asingeweza kufanya kutoka ndani. Malaika anaonekana na

umati wa watu wanaodhihaki, akishuka kutoka mbinguni, akiwa amevikwa mwangaza kama umeme. Anafunga mlango huo mkubwa wa nje, na kisha anapanda juu tena, kuelekea mbinguni. **{SRSw 64.3}**

Kwa siku saba familia ya Nuhu ilikuwa ndani ya safina kabla ya mvua kuanza kunyesha juu ya nchi. Wakati huu walikuwa wakipanga kukaa kwao kwa muda mrefu wakati maji yatakapokuwa juu ya nchi. Na hizi zilikuwa siku za furaha yenye kukufuru ya umati wa watu wasioamini. Walifikiri, kwa sababu unabii wa Nuhu haukutimizwa mara moja baada ya kuingia ndani ya safina, kwamba alidanganyika na kwamba haiwezekani ulimwengu uangamizwe kwa Gharika. Kabla ya hili hapakuwa na mvua juu ya nchi. Ukungu ulikuwa umeinuka kutoka kwenye maji, ambayo Mungu alisababisha kushuka usiku kama umande, kuinawirisha na kuikuza mimea na kusababisha kustawi. **{SRSw 65.4}**

Ijapokuwa walikuwa wameshuhudia maonyesho hayo mazito ya uwezo wa Mungu—miujiza na mambo yasiyo ya kawaida ya wanyama kuondoka msituni na mashambani, na kuingia ndani ya safina, na malaika wa Mungu aliyevikwa mwangaza na ukuu wa kutisha akishuka kutoka mbinguni na kufunga mlango; Hata hivyo waliifanya mioyo yao kuwa migumu na kuendelea kufurahi kwa kelele na kuleta mchezo kuhusiana na maonyesho ya ishara ya nguvu za Mwenyezi Mungu. **{SRSw 66.1}**

Dhoruba inapasuka

Lakini siku ya nane mbingu zilifunikwa na giza. Radi za ngurumo na miale zilianza kumtisha mwanadamu na mnyama. Mvua ilishuka kutoka kwenye mawingu juu yao. Hili lilikuwa jambo ambalo hawakuwahi kulishuhudia, na mioyo yao ilianza kuzirai kwa hofu. Wanyama walikuwa wakizunguka-zunguka kwa hofu kuu, na sauti zao zisizo na upatanifu zilionekana kuomboleza hatima yao wenyewe na

hatima ya mwanadamu. Dhoruba iliongezeka kwa vurugu hadi maji yalionekana kutoka mbinguni kama maporomoko makubwa ya maji. Mipaka ya mito ilipasuka, na maji yakakimbilia kwenye mabonde. Misingi ya kilindi kikuu pia ilivunjwa. Mikondo ya maji ilipasuka kutoka ardhini kwa nguvu isiyoelezeka, ikirusha mawe makubwa mamia ya futi angani, na kisha ingejizika ndani kabisa ya ardhi. **{SRSw 66.2}**

Watu waliona kwanza uharibifu wa kazi za mikono yao. Majengo yao ya kifahari, bustani zao zilizopangwa vizuri na vichaka vya miti ya kawaida na miti ya matunda, ambapo walikuwa wameweka sanamu zao, yaliharibiwa na umeme kutoka mbinguni. Magofu yao yalitawanyika kila mahali. Walikuwa wameweka madhabahu katika vichaka, na kuziweka wakfu kwa sanamu zao, ambapo walitoa dhabihu za kibinadamu. Hivi vitu ambavyo Mungu alivichukia viling'olewa katika ghadhabu Yake mbele yao, na wakafanywa kutetemeka mbele ya uwezo wa Mungu aliye hai, Muumba wa mbingu na nchi, na wakafanywa kujua kwamba ni machukizo yao na dhabihu za kutisha, za ibada ya sanamu ambazo zilichochea kwa uharibifu wao. **{SRSw 67.1}**

Vurugu za dhoruba ziliongezeka, na zikachangamana na vipengele vilivyokuwa katika vita, vilio vya watu ambao walikuwa wamedharau mamlaka ya Mungu. Miti, majengo, mawe, na ardhi vilirushwa kila upande. Hofu ya mwanadamu na mnyama ilikuwa zaidi ya maelezo. na hata Shetani mwenyewe, ambaye alilazimishwa kuwa katikati ya vipengele hivi vya mapambano, aliogopa uwepo wake mwenyewe. Alikuwa amefurahi kudhibiti jamii yenye nguvu sana, na aliwataka waishi ili kutekeleza machukizo yao, na kuongeza uasi wao dhidi ya Mungu wa Mbinguni. Alitamka mashtaka dhidi ya Mungu, akimshtaki kwa dhuluma na ukatili. Wengi wa watu, kama Shetani, walimtukana Mungu, na kama wangeweza kutekeleza uasi wao, wangemng'oa kutoka kwenye kiti Chake cha enzi cha haki. **{SRSw 67.2}**

Ingawa wengi walikuwa wakimtukana na kumlaani Muumba wao, wengine walikuwa na hofu, wakinyoosha mikono yao kuelekea safina, wakiomba wakubaliwe. Lakini hii ilikuwa haiwezekani. Mungu alikuwa amefunga mlango, mlango pekee wa kuingilia, na kumfungia Nuhu ndani na wasiomcha Mungu nje. Yeye peke yake Ndiye angeweza kufungua mlango. Hofu na toba yao ilichelewa sana. Walilazimika kujua kwamba kulikuwa na Mungu aliye hai ambaye alikuwa mkuu kuliko mwanadamu, ambaye walikuwa wamemkaidi na kumtukana. Walimwita kwa bidii, lakini sikio Lake halikuwa wazi kwa kilio chao. Wengine katika hali yao ya kukata tamaa walitaka kuingia ndani ya safina, lakini muundo/mjengo huo imara ulipinga juhudi zao zote. Wengine waling'ang'ania safina hadi wakachukuliwa na mawimbi makali ya maji, au kushikilia kwao kulivunjwa na mawe na miti iliyorushwa kila upande. **{SRSw 67.3}**

Wale ambao walikuwa wamepuuza onyo la Nuhu na kumdhihaki huyu mhubiri mwaminifu wa haki, walitubu kwa kuchelewa sana kutokuamini kwao. Safina ilitikiswa sana na kurushwa huku na kule. Wanyama ndani walionyesha, kwa kelele zao mbalimbali, hofu isiyo na mipaka kama wanyama mwitu; Hata hivyo, katikati ya vita vyote vya hali ya hewa, mawimbi ya maji, na kurushwa kwa miti na miamba, safina hiyo ilitembea kwa usalama. Malaika wabobezi na wenye ufanisi na nguvu waliiongoza safina na kuihifadhi isiharibike. Kila wakati wa dhoruba hiyo ya kutisha katika siku arobaini mchana na usiku, kuhifadhiwa kwa safina ulikuwa muujiza wa nguvu za Mwenyezi Mungu. **{SRSw 68.1}**

Wanyama walioathiriwa na tufani nje ya safina, walikimbilia kwa mwanadamu, wakichagua jamii ya wanadamu, kana kwamba walitarajia msaada kutoka kwao. Baadhi ya watu waliwafunga watoto wao, na wao wenyewe juu ya wanyama wenye nguvu, wakijua kwamba wangekuwa

wanakabili maisha kwa ustahimilivu, na wasingechoka kirahisi, hivyo wangepanda hadi sehemu za juu zaidi ili kuepuka maji yanayoinuka. Dhoruba haikupunguza ghadhabu yake—maji yaliongezeka haraka kuliko mwanzoni. Wengine walijifunga kwenye miti mirefu juu ya sehemu za juu kabisa za ardhi, lakini miti hii iling'olewa na mizizi pia, na kubebwa kwa jeuri angani na ilionekana kana kwamba imerushwa kwa nguvu, kwa mawe na ardhi, na maji yakavimba na kuwa mawimbi yanayochemka. Juu ya vilele vya juu zaidi wanadamu na wanyama walijitahidi kushikilia msimamo wao hadi wote walipotupwa pamoja kwenye maji yenye povu, ambayo karibu yafikie sehemu za juu zaidi za ardhi. Urefu wa juu zaidi mwishowe ulifikiwa, na mwanadamu na mnyama waliangamia kwa maji ya Gharika. **{SRSw 68.2}**

Nuhu na familia yake walitazama kwa wasiwasi kupungua kwa maji. Alitamani kwenda juu ya nchi tena. Alituma kunguru ambaye aliruka na kurudi kutoka na kutoka kwa safina. Hakupokea taarifa alizotaka, na akatoa njiwa, ambaye, bila kuona pa kutua, ilirudi tena kwenye safina. Baada ya siku saba njiwa alitumwa tena, na akarudi, kisha jani la mzeituni lilipoonekana kinywani mwake, palikuwa na shangwe kubwa kwa familia hii ya watu wanane, ambayo ilikuwa imefungwa kwa muda mrefu ndani ya safina. **{SRSw 69.1}**

Tena malaika alishuka na kufungua mlango wa safina. Nuhu angeweza kuondoa paa la safina, lakini hakuweza kufungua mlango ambao Mungu alikuwa ameufunga. Mungu alizungumza na Nuhu kupitia kwa malaika aliyefungua mlango, na akaamuru familia ya Nuhu itoke nje ya safina na kuleta kila kitu kilicho hai. **{SRSw 69.2}**

Dhabihu ya Nuhu na ahadi ya Mungu

Nuhu hakumsahau Mungu, ambaye alikuwa amewahifadhi kwa ukarimu sana, lakini mara moja alisimamisha madhabahu na kuchukua

kila mnyama safi, na kila ndege safi, na kutoa sadaka ya kuteketezwa juu ya madhabahu, akionyesha imani yake katika Kristo aliye dhabihu kuu, na kudhihirisha shukrani zake kwa Mungu kwa uhifadhi wao wa ajabu. Sadaka ya Nuhu ilikuja mbele za Mungu kama harufu nzuri. Alikubali sadaka na kumbariki Nuhu na familia yake. Hapa somo linafundishwa wote ambao wanapaswa kuishi duniani, kwamba kwa kila udhihirisho wa rehema na upendo wa Mungu kwao tendo la kwanza la wote linapaswa kuwa, kumtolea shukrani za shukrani na ibada ya unyenyekevu. **{SRSw 69.3}**

Na ili mtu asiogope kutishwa na mawingu na mvua zinazonyesha, na awe katika hofu ya daima, akiogopa mafuriko mengine, Mungu kwa neema anahimiza familia ya Nuhu kwa ahadi. "***Na agano Langu nitalithibitisha nanyi; wala kila chenye mwili hakitafutwa tena kwa maji ya gharika; wala hakutakuwa tena gharika, baada ya hayo, kuiharibu nchi. Mungu akasema, Hii ndiyo ishara ya Agano nifanyalo kati Yangu na ninyi, na kila kiumbe hai kilichoko pamoja nanyi, kwa vizazi vyote hata milele; Mimi nauweka upinde Wangu winguni, nao utakuwa ni ishara ya agano kati Yangu na nchi. Hata itakuwa nikitanda mawingu juu ya nchi, upinde utaonekana winguni, Nami nitalikumbuka Agano Langu, lililoko kati Yangu na ninyi, na kila kiumbe hai katika wote wenye mwili, wala maji hayatakuwa gharika tena kuwaharibu wote wenye mwili. Basi huo upinde utakuwa winguni; Nami nitauangalia nipate kulikumbuka agano la milele lililoko kati ya Mungu na kila kiumbe hai katika wote wenye mwili kilichoko katika nchi. Mwanzo 9:11-16" Mungu akamwambia Nuhu, Hii ndiyo ishara ya agano nililoliweka kati Yangu na wote wenye mwili walioko katika nchi." Mwanzo 9:11-17*** **{SRSw 70.1}**

Ni kujishusha chini kwa kiasi gani kwa upande wa Mungu! Ni huruma iliyoje kwa mwanadamu aliyekosea, kuweka upinde wa mvua

mzuri, wa aina mbalimbali mawinguni, ishara ya agano la Mungu Mwenyezi na mwanadamu! Upinde huu wa mvua ulipaswa kuthibitisha uhalisia na Ukweli kwa vizazi vyote kwamba Mungu aliwaangamiza wakaaji wa dunia kwa Gharika, kwa sababu ya uovu wao mkubwa. Ilikuwa ni mpango Wake kwamba watoto wa vizazi vijavyo watakapoona upinde katika wingu na kuuliza sababu ya upinde huu wenye utukufu unaovuka mbingu, wazazi wao wangeweza kuwaeleza uharibifu wa ulimwengu wa kale kwa Gharika, kwa sababu watu walijitoa wenyewe kwa kila namna. Uovu, na kwamba mikono ya Yeye Aliye Juu ilikuwa imeukunja upinde na kuuweka mawinguni kama ishara kwamba hataleta tena gharika ya maji juu ya nchi. **{SRSw 70.2}**

Ishara hii katika mawingu, huthibitisha imani ya wote, na kusimika mani yao kwa Mungu, kwa kuwa ni ishara ya rehema ya Mungu na wema kwa mwanadamu; Kwamba ingawa Mungu alikuwa amechokozwa na kuiangamiza dunia kwa gharika, lakini rehema Yake bado inaizingira dunia. Mungu anasema atakapoutazama upinde katika wingu atakumbuka. Yeye anataka tuelewe kwamba hatasahau kamwe, lakini anazungumza na mwanadamu kwa lugha ya mtu mwenyewe, ili mwanadamu apate kumwelewa vyema zaidi. **{SRSw 71.1}**

SURA YA 9—MNARA WA BABELI

Sura hii imejengwa katika Mwanzo 11:1-9.

Baadhi ya wazao wa Nuhu walianza kuasi mapema. Baadhi walifuata mfano wa Nuhu na kutii amri za Mungu; Wengine walikuwa wasioamini na waasi, na hata hawa hawakuamini sawa kuhusiana na Gharika. Wengine hawakuamini uwepo wa Mungu, na katika akili zao wenyewe walichangia mafuriko kutokana na sababu za asili. Wengine waliamini kwamba Mungu alikuwepo na kwamba aliharibu jamii ya kabla ya gharika kwa mafuriko; Na hisia zao, kama za Kaini, ziliongezeka katika uasi dhidi ya Mungu kwa sababu aliwaangamiza watu kutoka duniani na kulaani dunia mara ya tatu kwa gharika. **{SRSw 72.1}**

Wale ambao walikuwa maadui wa Mungu walihisi kila siku kukasirishwa na mazungumzo ya haki na maisha ya Kiungu ya wale waliopenda, kutii, na kumwinua Mungu. Wasioamini walishauriana kati yao na wakakubali kujitenga na waumini, ambao maisha yao ya haki yalikuwa ni kizuizi cha daima juu ya mwendo wao mbaya. Walisafiri umbali kutoka kwao na kuchagua uwanda mkubwa wa kukaa. Wakajijengea mji, kisha wakapata wazo la kujenga mnara mkubwa wa kufika mawinguni, ili wakae pamoja katika mji na mnara, wala wasitawanyike tena. **{SRSw 72.2}**

Walifikiri kwamba wangejilinda wenyewe ikiwa kuna Gharika nyingine, kwa maana wangejenga mnara wao kwa urefu zaidi kuliko maji yaliyokuwapo wakati wa gharika, na ulimwengu wote ungewaheshimu, na wangekuwa kama miungu na kutawala watu. Mnara huu ulihesabiwa kuwainua wajenzi wake, na ulikusudiwa kugeuza usikivu wa wengine ambao wangeishi juu ya dunia kutoka kwa Mungu ili kuungana nao katika ibada yao ya sanamu. Kabla ya kazi ya ujenzi kukamilika, watu walikaa kwenye mnara huo. Vyumba vilipambwa kwa uzuri, urembo, na kutengwa kwa ajili ya sanamu zao. Wale ambao hawakumwamini Mungu walifikiri ikiwa mnara wao ungeweza kufika mawinguni, wangeweza kugundua sababu za Gharika. **{SRSw 72.3}**

Walijiinua dhidi ya Mungu. Lakini Bwana hangewaruhusu kukamilisha kazi yao. Walikuwa wamejenga mnara wao kwa urefu wa juu wakati Bwana alipotuma malaika wawili kuwavuruga katika kazi yao. Watu walikuwa wameteuliwa kwa kusudi la kupokea neno kutoka kwa watenda kazi walio juu ya mnara, wakiita nyenzo kwa ajili ya kazi yao, ambayo wa kwanza angewasiliana na wa pili, na yeye hadi wa tatu, mpaka neno au ujumbe ufikie wale walio chini. Neno lilipokuwa likipita kutoka kwa mtu mmoja hadi mwingine katika kushuka kwake, malaika walichanganya lugha yao, na neno lilipowafikia watenda kazi juu ya ardhi, walileta vifaa ambavyo havikuhitajika au hawakutumwa kuleta. Na baada ya mchakato mgumu wa kupata vifaa kwa wafanya kazi juu ya mnara, haikuwa kile walichotaka. Wakiwa wamevunjwa moyo na kukasirika, waliwakemea wale ambao walidhani walikuwa na makosa. **{SRSw 73.1}**

Baada ya hayo hapakuwa na maelewano katika kazi yao. Wakiwa na hasira kati yao, na hawakuweza kujua sababu sababishi ya kutokuelewana na maneno ya ajabu kati yao, waliacha kazi na kujitenga na kutawanyika katika dunia yote. Hadi wakati huu watu walikuwa

wakizungumza lugha moja tu. Umeme kutoka mbinguni, kama ishara ya ghadhabu ya Mungu, ulivunja sehemu ya juu ya mnara wao, na kuutupa chini. Hivyo Mungu alimwonyesha mwanadamu mwasi kwamba Yeye Ndiye mkuu (SUPREME). **{SRSw 73.2}**

SURA YA 10—IBRAHIMU NA UZAO WA AHADI

Sura hii imejengwa katika Mwanzo 12:1-5; 13; 15; 16; 17; 21 na 22:1-19.

Bwana alimchagua Ibrahimu kutekeleza mapenzi Yake. Aliagizwa kuliacha taifa lake lililoabudu sanamu na kujitenga na jamaa zake. Bwana alikuwa amejidhihirisha kwa Ibrahimu katika ujana wake na akampa ufahamu na kumhifadhi mbali na ibada ya sanamu. Alipanga kumfanya kuwa kielelezo cha imani na kujitoa kwa kweli kwa watu wake ambao baadaye walipaswa kuishi duniani. Tabia yake iliwekwa alama kwa uadilifu, ukarimu, na ukaribishaji wageni. Alipewa heshima kama mkuu kati ya watu. Heshima na upendo wake kwa Mungu, na utii wake wa nguvu katika kutekeleza mapenzi Yake, ulipata kwake heshima ya watumishi na majirani zake. Mfano wake wa kumpendeza Mungu na mwenendo wa haki, uliounganishwa na maagizo Yake ya uaminifu kwa watumishi wake na nyumba yake yote, uliwaongoza kumcha, kumpenda, na kumheshimu Mungu wa Ibrahimu. **{SRSw 75.1}**

Bwana alimtokea Ibrahimu na kumuahidi kwamba uzao wake utakuwa kama nyota za mbinguni kwa idadi. Pia alimjulisha, kupitia sura ya hofu ya giza kuu iliyomjia, utumwa mrefu, wa utumishi wa wazao wake huko Misri (miaka 400). **{SRSw 75.2}**

Hapo mwanzo Mungu alimpa Adamu mke mmoja, hivyo kuonyesha utaratibu wake. Hakuwahi kubuni kwamba mwanadamu awe na wingi wa wake. Lameki alikuwa wa kwanza kuondoka katika jambo hili kutokana na mpangilio wa Mungu wenye hekima. Alikuwa na wake wawili, jambo ambalo lilizua mifarakano katika familia yake. Wivu na wivu wa wote wawili ulimfanya Lameki akose furaha. Watu walipoanza kuzidi juu ya uso wa nchi, na mabinti wakazaliwa kwao, waliwachukua wake wowote waliyowachagua. Hii ilikuwa moja ya dhambi kuu za wakaaji wa ulimwengu wa kale, ambazo zilileta ghadhabu ya Mungu juu yao. Desturi hii ilitekelezwa baada ya Gharika, na ikawa ya kawaida sana hata watu waadilifu walianguka katika mazoea na kuwa na wake wengi. Hata hivyo haikuwa dhambi kidogo kwa sababu walipotoshwa na kuondoka katika jambo hili kwenye utaratibu wa Mungu. **{SRSw 75.3}**

Bwana alisema juu ya Nuhu na familia yake, waliookolewa katika safina; **kwa maana nimekuona wewe u mwenye haki mbele Zangu katika kizazi hiki. Mwanzo 7:1** Nuhu alikuwa na mke mmoja tu, na nidhamu ya familia yao iliyoungana ilibarikiwa na Mungu. Kwa sababu wana wa Nuhu walikuwa waadilifu walihifadhiwa ndani ya safina pamoja na baba yao mwadilifu. Mungu hajaidhinisha mitala hata katika tukio moja. Ni kinyume na mapenzi Yake. Alijua kwamba furaha ya mwanadamu ingeharibiwa kwa jambo hilo. Amani ya Abrahamu iliharibiwa sana na ndoa yake isiyo na furaha, na Hagari. **{SRSw 76.1}**

Kusitasita Juu ya Ahadi ya Mungu

Bwana akamwambia Abramu, alipokwisha kutengana na Lutu, **“Inua sasa macho yako, ukatazame kutoka hapo ulipo, upande wa kaskazini, na wa kusini na wa mashariki na wa magharibi; maana nchi hii yote uionayo, nitakupa wewe na uzao wako hata milele. Na uzao wako nitaufanya uwe kama mavumbi ya nchi; hata mtu akiweza kuyahesabu mavumbi ya nchi, uzao wako nao utahesabika.**

Mwanzo 13:14-16 Baada ya mambo hayo Neno la Bwana likamjia Abramu katika njozi, likinena, Usiogope, Abramu, Mimi ni ngao yako, na thawabu yako kubwa sana... Abramu akasema, Tazama, hukunipa uzao, na mtu aliyezaliwa nyumbani mwangu ndiye mrithi wangu. Mwanzo 15:1,3. **{SRSw 76.2}**

Kwa vile Ibrahimu hakuwa na mwana, mwanzoni alifikiri kwamba mtumishi wake mwaminifu, Eliezeri, angekuwa mwana wake kwa kuasili, na mrithi wake. Lakini Mungu alimjulisha Ibrahimu kwamba mtumishi wake hapaswi kuwa mwanawe na mrithi, bali kwamba ni kweli anapaswa kupata mwana. **Akamleta nje, akasema, Tazama sasa mbinguni, kazihesabu nyota, kama ukiweza kuzihesabu. Akamwambia, Ndivyo utakavyokuwa uzao wako. Mwanzo 15:5** **{SRSw 77.1}**

Ikiwa Ibrahimu na Sara wangengoja kwa imani yenye kumtumaini Mungu ili kutimiza ahadi ya kwamba wangepata mwana, kutokuwa na furaha kungeepukwa. Waliamini kwamba ingekuwa kama vile Mungu alivyoahidi, lakini hawakuamini kwamba Sara katika uzee wake angekuwa na mwana. Sara alipendekeza mpango ambao alifikiri ahadi ya Mungu inaweza kutimizwa. Alimsihi Ibrahimu amchukue Hajiri kama mke wake. Katika hili wote wawili walikosa imani na tumaini kamilifu katika uwezo wa Mungu. Kwa kusikiliza sauti ya Sara na kumchukua Hajiri kama mke wake Ibrahimu alishindwa kustahimili jaribu la imani yake katika uwezo usio na kikomo wa Mungu, na akajiletea yeye na Sara kutokuwa na furaha kabisa. Bwana alikusudia kuthibitisha imani thabiti na tegemeo la Ibrahimu juu ya ahadi alizompa. **{SRSw 77.2}**

Majivuno ya Hajiri

Hajiri alikuwa na kiburi na majivuno, na alitenda kwa kiburi mbele ya Sara. Alijikomba na kujidanganya kwamba angekuwa mama wa taifa kubwa ambalo Mungu alikuwa ameahidi kumfanya Ibrahimu. Naye Ibrahimu alilazimika kusikiliza malalamiko kutoka kwa Sara kuhusiana na mwenendo wa Hajiri, akimshtaki Ibrahimu kwa makosa katika jambo hilo. Ibrahimu alihuzunishwa na kumwambia Sara kwamba Hajiri ni mtumishi wake, na kwamba anaweza kuwa na udhibiti wake, lakini anakataa kumfukuza, kwa maana atakuwa mama wa mtoto wake, ambaye anafikiri ahadi hiyo inapaswa kutimizwa. Anamjulisha Sara kwamba yeye hangemchukua Hajiri kwa mke wake kama lisingekuwa ombi lake maalum. **{SRSw 77.3}**

Abraham pia alilazimika kusikiliza malalamiko ya Hajiri ya unyanyasaji kutoka kwa Sara. Ibrahimu yuko katika mfadhaiko. Ikiwa anatafuta kurekebisha makosa ya Hajiri na anaongeza wivu na kutokuwa na furaha kwa Sara, mke wake wa kwanza na aliyependwa sana. Hajiri anakimbia uso wa Sara. Malaika wa Mungu alikutana naye na kumfariji na pia kumkemea kwa ajili ya mwenendo wake wa kiburi, katika kumtaka arudi kwa bosi wake na kujisalimisha chini ya mikono yake. **{SRSw 78.1}**

Baada ya kuzaliwa kwa Ishmaeli, Bwana alijidhihirisha tena kwa Ibrahimu, akamwambia;**"Agano Langu nitalifanya imara kati ya Mimi na wewe, na uzao wako baada yako, na vizazi vyao, kuwa Agano la milele. Mwanzo 17:7** Tena Bwana alirudia kwa njia ya malaika wake ahadi Yake ya kumpa Sara mwana, na kwamba anapaswa kuwa mama wa mataifa mengi. Ibrahimu alikuwa bado hajaelewa ahadi ya Mungu. Mara moja akili yake ilitulia juu ya Ishmaeli, kana kwamba kupitia kwake mataifa mengi yaliyoahidiwa, na akasema, kwa upendo wake kwa mwanawe. **"Lau kwamba Ishmaeli angeishi mbele yako." Mwanzo 17:18** **{SRSw 78.2}**

Tena ahadi hiyo inarudiwa kwa hakika zaidi kwa Ibrahimu: Mungu akasema, Sivyo, lakini Sara mkeo atakuzalia mwana wa kiume, nawe utamwita jina lake Isaka. **Nami nitafanya agano Langu imara kwake kuwa Agano la milele kwa ajili ya uzao wake baada yake. Mwanzo 17:19** Malaika wanatumwa mara ya pili kwa Ibrahimu wakielekea kuiangamiza Sodoma, na wanarudia ahadi hiyo kwa uwazi zaidi kwamba Sara atakuwa na mwana. **{SRSw 78.3}**

Mwana Aliyeahidiwa

Baada ya kuzaliwa kwa Isaka furaha kuu iliyodhihirishwa na Ibrahimu na Sara ilimfanya Hajiri kuwa na wivu sana. Ishmaeli alikuwa ameagizwa na mama yake kwamba alipaswa kubarikiwa hasa na Mungu, kama mwana wa Ibrahimu, na kuwa mrithi wa kile alichoahidiwa. Ishmaeli alishiriki hisia za mama yake na alikasirika kwa sababu ya furaha iliyoonyeshwa wakati wa kuzaliwa kwa Isaka. Alimdharau Isaka, kwa sababu alifikiri alipata upendeleo kabla yake. Sara aliona tabia iliyodhihirishwa na Ishmaeli dhidi ya mwanawe Isaka, na aliguswa moyo sana. Alimsimulia Ibrahimu mwenendo wa dharau wa Ishmaeli kwake na kwa mwanawe Isaka, akamwambia; **Mfukuze mjakazi huyu na mwanawe, maana mwana wa mjakazi hatarithi pamoja na mwanangu, Isaka. Mwanzo 21:10** **{SRSw 79.1}**

Ibrahimu alihuzunika sana. Ishmaeli alikuwa mwanawe, aliyependwa naye. Je, angewezaje kumfukuza? Aliomba kwa Mungu katika mshangao wake, kwa maana hakujua ni njia gani ya kuchukua. Bwana alimjulisha Ibrahimu, kwa njia ya malaika wake, kusikiliza sauti ya Sara mkewe, na kwamba hapaswi kuruhusu mapenzi yake kwa mwanawe au kwa Hajiri kuzuia kufuata kwake matakwa Yake Bwana. Kwa maana hii ndiyo njia pekee ambayo angeweza kufuata ili kurejesha maelewano na furaha tena kwa familia yake. Ibrahimu alikuwa na ahadi ya kufariji kutoka kwa malaika, kwamba Ishmaeli, ingawa alitengwa na

nyumba ya baba yake, hapaswi kufa wala kuachwa na Mungu, kwamba atahifadhiwa kwa sababu alikuwa mwana wa Ibrahimu. Mungu pia aliahidi kumfanya Ishmaeli kuwa taifa kubwa. **{SRSw 79.2}**

Ibrahimu alikuwa na tabia bora ya uungwana na wema, ambayo ilidhihirika katika kusihi kwake kwa bidii kwa watu wa Sodoma. Roho yake yenye nguvu iliteseka sana. Aliinama kwa huzuni, na hisia zake za ubaba ziliguswa sana alipomfukuza Hajiri na mwanawe Ishmaeli kutangatanga kama wageni katika nchi ngeni. **{SRSw 80.1}**

Kama Mungu angeidhinisha ndoa ya wake wengi (mitala), asingemwelekeza Ibrahimu kuwafukuza Hajiri na mwanawe. Angeweza kuwafundisha wote somo katika hili, kwamba haki na furaha ya uhusiano wa ndoa inapaswa kuheshimiwa na kulindwa daima, hata kwa dhabihu kubwa. Sara alikuwa mke wa kwanza na mke wa pekee na wa kweli wa Ibrahimu. Alikuwa na haki, kama mke na mama, ambayo hakuna mwingine angeweza kuwa na haki hiyo katika familia. Alimheshimu mume wake, akimwita Bwana, lakini alikuwa na wivu kwamba upendo wa mumewe ungegawanywa kwa Hajiri pia. Mungu hakumkemea Sara kwa mwendo aliofuata. Ibrahimu alikemewa na malaika kwa kutoamini nguvu za Mungu, ambayo ilimfanya amchukue Hajiri kama mke wake na kufikiria kwamba kupitia kwake ahadi hiyo ingetimizwa. **{SRSw 80.2}**

Jaribio Kuu la Imani

Tena Bwana aliona inafaa kujaribu imani ya Ibrahimu kwa jaribio la kutisha zaidi. Kama angevumilia jaribu la kwanza na kungoja kwa subira ahadi hiyo itimie kwa Sara, na asingemchukua Hajiri kama mke wake, asingepitia jaribu kubwa kuliko yote yaliyowahi kutolewa kwa mwanadamu. Bwana akamwambia Ibrahimu,"**Umchukue mwanao, mwana wako wa pekee, umpendaye, Isaka, ukaende zako mpaka**

nchi ya Moria, ukamtoe sadaka ya kuteketezwa huko juu ya mlima mmojawapo nitakaokuambia. Mwanzo 22:2 {SRSw 80.3}

Ibrahimu hakumtilia Mungu shaka wala kusitasita, lakini asubuhi na mapema aliwachukua watumishi wake wawili na Isaka, mwanawe, na kuni kwa ajili ya sadaka ya kuteketezwa, kisha akaenda mahali ambapo Mungu alikuwa amemwambia. Hakufunua hali halisi ya safari yake kwa Sara, akijua kwamba mapenzi yake kwa Isaka yangemfanya asimwamini Mungu na kumzuia mwana wake. Ibrahimu hakuruhusu hisia za ubaba zimtawale na kumpelekea kumwasi Mungu. Amri ya Mungu ilikuwa imekusudiwa kutoa mguso makini kwa nafsi yake. **"Umchukue mwanao"** Kisha, kana kwamba alikuwa akiuchunguza moyo wake Ibrahimu kwa undani zaidi, aliongeza, **mwana wako wa pekee, umpendaye, Isaka, ukaende zako mpaka nchi ya Moria, ukamtoe sadaka ya kuteketezwa. {SRSw 80.4}**

Kwa siku tatu baba huyu alisafiri pamoja na mwanawe, akiwa na wakati wa kutosha wa kufikiri na kumtilia shaka Mungu kama angelikuwa na ajenda ya kutilia Mungu shaka. Lakini hakumtilia shaka Mungu. Hakufikiri tena kwamba ahadi hiyo ingetimizwa kupitia kwa Ishmaeli, kwa kuwa Mungu alimwambia waziwazi kwamba kupitia Isaka, ndiyo ahadi hiyo ingetimizwa. **{SRSw 81.1}**

Ibrahimu aliamini kwamba Isaka alikuwa mwana wa ahadi. Pia aliamini kwamba Mungu alimaanisha yale aliyosema tu alipomwambia aende kumtolea kama sadaka ya kuteketezwa. Hakutetereka katika ahadi ya Mungu bali aliamini kwamba Mungu, ambaye katika majaliwa Yake alimpa Sara mwana katika uzee wake, na ambaye alikuwa amemtaka achukue uhai wa mwana huyo, angeweza pia kutoa uhai tena na hata kumleta Isaka kutoka kwa wafu. **{SRSw 81.2}**

Ibrahimu aliwaacha watumishi wake njiani na akapendekeza kwenda peke yake na mwanawe kuabudu umbali fulani kutoka kwao. Hangeruhusu watumishi wake waandamane nao, ili kwamba upendo wao kwa Isaka usiweze kuwaongoza kumzuia asitekeleze yale ambayo Mungu alikuwa amemwamuru kufanya. Alichukua kuni kutoka kwa mikono ya watumishi wake na kuiweka juu ya mabega ya mwanawe. Pia alichukua moto na kisu. Alikuwa amejiandaa tayari, kutekeleza utume wa kutisha aliopewa na Mungu. Baba na mwana waliendelea pamoja. **{SRSw 81.3}**

Kisha Isaka akasema na Ibrahimu baba yake, akinena, **Babangu! Naye akasema, Mimi hapa, mwanangu. Akasema, Tazama! Moto upo, na kuni zipo, lakini yuko wapi mwana-kondoo kwa sadaka ya kuteketezwa? Ibrahimu akasema, Mungu atajipatia mwana-kondoo kwa hiyo sadaka, mwanangu. Basi wakaendelea wote wawili pamoja.Mwanzo 22:7, 8** Baba huyu aliyeteseka moyoni kwa kuwa alimpenda mtoto wake, alitembea kwa uthabiti kando ya mtoto wake. Walipofika mahali ambapo Mungu alikuwa amemwonyesha Ibrahimu, alijenga huko madhabahu na kuweka kuni kwa utaratibu, tayari kwa ajili ya dhabihu, na kisha akamjulisha Isaka juu ya amri ya Mungu ya kumtoa kama sadaka ya kuteketezwa. Alirudia tena ahadi ambayo Mungu alikuwa amempa mara kadhaa, kwamba kupitia Isaka awe taifa kubwa, na kwamba katika kutekeleza amri ya Mungu katika kumtoa dhabihu, Mungu angetimiza ahadi Yake, kwa maana aliweza kumfufua kutoka kwa wafu. **{SRSw 82.1}**

Ujumbe wa Malaika

Isaka alimwamini katika Mungu. Alikuwa amefundishwa utii kamili kwa baba yake, na alimpenda na kumheshimu Mungu wa baba

yake. Angeweza kumpinga baba yake ikiwa angechagua kufanya hivyo. lakini baada ya kumkumbatia baba yake kwa upendo, alijisalimisha kufungwa na kuwekwa juu ya kuni. Na wakati mkono wa baba yake ulivyoinuliwa ili kumwua mwanawe, malaika wa Mungu, ambaye alikuwa ameweka alama ya uaminifu wote wa Ibrahimu kwenye njia ya Moria, akamwita kutoka mbinguni, akasema, **Ibrahimu! Ibrahimu! Naye akasema, mimi hapa.** **{SRSw 82.2}**

Akasema, Usimnyoshee kijana mkono wako, wala usimtendee neno; kwa maana sasa ninajua ya kuwa unamcha Mungu, iwapo hukunizuilia mwanao, mwanao wa pekee. Ibrahimu akainua macho yake, akaangalia, na tazama, kondoo mume yuko nyuma yake, amenaswa pembe zake katika kichaka. Basi Ibrahimu akaenda akamtwaa huyo kondoo, akamtoa awe sadaka ya kuteketezwa badala ya mwanawe. Mwanzo 22:11-13 **{SRSw 83.1}**

Ibrahimu sasa alikuwa amepasi jaribu hilo kikamilifu na kwa ustadi, na kwa uaminifu wake alifidia ukosefu wake wa kumtumaini Mungu kikamilifu jambo ambalo lilimfanya amchukue Hajiri kama mke wake. Baada ya kuona imani na ujasiri wa Ibrahimu, Mungu alirudia ahadi Yake kwake. **Malaika wa Bwana akamwita Ibrahimu mara ya pili kutoka mbinguni akasema, Nimeapa kwa Nafsi Yangu asema Bwana, kwa kuwa umetenda neno hili, wala hukunizuilia mwanao, mwanao wa pekee, katika kubariki, nitakubariki, na katika kuzidisha, nitauzidisha uzao wako kama nyota za mbinguni, na kama mchanga ulioko pwani; na uzao wako utamiliki mlango wa adui zao; na katika uzao wako mataifa yote ya dunia watabarikiwa; kwa sababu umetii sauti Yangu. Mwanzo 22:15-18** **{SRSw 83.2}**

SURA YA 11—NDOA YA ISAKA

Sura hii imejengwa katika Mwanzo 24.

Wakanaani walikuwa waabudu sanamu, na Bwana alikuwa ameamuru kwamba watu Wake wasioane nao, ili wasije wakaongozwa katika ibada ya sanamu. Abrahamu alikuwa mzee, na alitarajia kufa hivi karibuni. Isaka alikuwa bado hajaoa. Ibrahimu aliogopa ushawishi mbaya uliomzunguka Isaka, na alikuwa na shauku ya kuchaguliwa mke ambaye hangemwondoa kwa Mungu. Alikabidhi jambo hili kwa mtumishi wake mwaminifu, mwenye uzoefu, ambaye alisimamia juu ya masuala yote. **{SRSw 84.1}**

Ibrahimu alimtaka mtumishi wake atoe kiapo kizito mbele za Bwana kwamba hatachukua mke kwa ajili ya Isaka wa Wakanaani, bali kwamba angeenda kwa jamaa za Ibrahimu, ambaye alimwamini Mungu wa kweli, na kumchagulia Isaka mke. Alimwonya ajihadhari na

asimpeleke Isaka katika nchi aliyotoka, kwa maana karibu wote waliathiriwa na ibada ya sanamu. Ikiwa hangeweza kupata mke wa Isaka ambaye angewaacha jamaa zake na kuja pale alipokuwa, basi angekuwa huru na kiapo alichokuwa amempa. **{SRSw 84.2}**

Jambo hili muhimu halikuachwa kwa Isaka, ili ajichagulie mwenyewe, bila ya baba yake. Ibrahimu alimwambia mtumishi wake kwamba Mungu angemtuma malaika Wake mbele yake ili kumwelekeza katika chaguo lake. Mtumishi ambaye alikabidhiwa jukumu hili alianza safari yake ndefu. Alipoingia katika jiji ambalo jamaa za Ibrahimu walikaa, aliomba kwa bidii kwa Mungu ili kumwelekeza katika chaguo lake la mke kwa Isaka. **{SRSw 84.3}**

Aliomba apewe ushahidi fulani, ili asikose katika suala hilo. Alipumzika karibu na kisima, ambacho kilikuwa mahali pa mkusanyiko mkubwa zaidi. Hapa aliona hasa adabu na mwenendo wa adabu wa Rebeka, na ushahidi wote aliokuwa amemwomba Mungu alipokea kwamba Rebeka ndiye ambaye Mungu alikuwa amependezwa kumchagua kuwa mke wa Isaka. Alimwalika mtumishi nyumbani kwa baba yake. Kisha akamsimulia baba yake Rebeka na ndugu yake ushahidi aliokuwa amepokea kutoka kwa Bwana kwamba Rebeka awe mke wa mwana wa bwana wake Isaka. Kisha mtumishi wa Ibrahimu akawaambia, **Basi, kama mnataka kumfanyia rehema na kweli bwana wangu, niambieni, na kama sivyo, niambieni; ili nigeuke upande wa kuume au wa kushoto. Mwanzo 24:49** Baba na ndugu walijibu, **wakasema, Neno hili limetoka kwa Bwana, wala sisi hatuwezi kukuambia neno jema wala baya. Tazama, huyo Rebeka yuko mbele yako, umchukue, ukaende zako awe mke wa mwana wa bwana wako, kama alivyosema Bwana. Ikawa mtumishi wa Ibrahimu aliposikia maneno yao, akainama hata nchi mbele za Bwana. Mwanzo 24:50-52** **{SRSw 85.1}**

Baada ya yote kupangwa, ridhaa ya baba na ndugu ilikuwa imepatikana, kisha Rebeka akafuatwa ili kuulizwa maoni yake kama angeenda na mtumishi wa Ibrahimu umbali mkubwa kutoka kwa familia ya baba yake, ili awe mke wa Isaka. Aliamini kutokana na mambo na hali ya yale yaliyotukia kwamba mkono wa Mungu ulikuwa umemchagua kuwa mke wa Isaka, “naye akasema, Nitaenda.” **{SRSw 85.2}**

Mikataba ya ndoa wakati huo kwa kawaida ilifanywa kwa ujumla na wazazi; Hata hivyo hapakuwa na kulazimishwa kuwaoa wale wasiowapenda. Lakini watoto walikuwa na imani katika uamuzi wa wazazi wao, wakafuata mashauri yao, na waliwekeza upendo wao kwa wale ambao wazazi wao wenye uzoefu wa kumcha Mungu, waliwachagulia. Ilionekana kuwa ni kosa kuwa uhalifu kufuata njia iliyo kinyume na hii. **{SRSw 85.3}**

Mfano wa Utiifu Kamili

Isaka alikuwa amezoezwa katika kumcha Mungu kwa maisha ya utii. Na alipokuwa na umri wa miaka arobaini alikubali kuwa mtumishi wa baba yake mwenye kumcha Mungu, na mwenye uzoefu, amchagulie mke. Aliamini kwamba Mungu angeelekeza kuhusu kupata kwake mke. **{SRSw 86.1}**

Kisa cha Isaka kimeachwa kikiwa kumbukumbu kama kielelezo cha watoto kuiga katika vizazi vijavyo, hasa wale wanaodai kumcha Mungu. **{SRSw 86.2}**

Njia ambayo Ibrahimu alifuata katika malezi ya Isaka, ambayo ilimfanya apende maisha ya utii wa hali ya juu, imeandikwa kwa manufaa ya wazazi, na inapaswa kuwaongoza wazazi kuamuru nyumba zao baada yao. Wanapaswa kuwaelekeza watoto wao kujisalimisha, na kuheshimu, mamlaka yao. na wanapaswa kuhisi kwamba jukumu liko

juu yao la kuongoza hisia za watoto wao, ili ziwekwe kwa watu ambao uamuzi wao ungewaonyesha kuwa ni wenzi wanaofaa kwa wana wao na binti zao. **{SRSw 86.3}**

SURA YA 12—YAKOBO NA ESAU

Sura hii imejengwa katika Mwanzo 25:19-34 na 27:1-32.

Mungu anajua mwisho tangu mwanzo. Yeye Alijua, kabla ya kuzaliwa kwa Yakobo na Esau, ni tabia gani ambayo wote wawili wwangeendeleza. Alijua kwamba Esau asingekuwa na moyo wa kumtii. Alijibu sala iliyotolewa kwa moyo wa kutaabika, ya Rebeka na kumjulisha kwamba atakuwa na watoto wawili, na mkubwa amtumikie mdogo. Aliwasilisha historia ya wakati ujao ya wanawe wawili mbele yake, kwamba wangekuwa mataifa mawili, mmoja mkuu kuliko mwingine, na mkubwa anapaswa kumtumikia mdogo. Mzaliwa wa kwanza alikuwa na haki ya faida za kipekee na haki maalum, ambazo hazikuwa za washiriki wengine wa familia. **{SRSw 87.1}**

Isaka alimpenda Esau kuliko Yakobo, kwa sababu Esau alimpa mawindo. Alifurahishwa na roho yake ya ushujaa, ya ujasiri

iliyoonyeshwa katika kuwinda wanyama wa mwitu. Yakobo alikuwa mwana kipenzi cha mama yake, kwa sababu tabia yake ilikuwa ya upole na iliyoratibiwa vyema ili kumfurahisha mama yake. Yakobo alikuwa amejifunza kutoka kwa mama yake yale ambayo Mungu alikuwa amemfundisha, kwamba mkubwa huyo amtumikie mdogo zaidi, na mawazo yake ya ujana yalimfanya ahitimishe kwamba ahadi hiyo isingeweza kutimizwa wakati Esau bado ana haki alizopewa mzaliwa wa kwanza. Na Esau aliporudi kutoka mawindoni, akiwa amechoka kwa njaa, Yakobo alitumia fursa hiyo kugeuza hitaji la Esau kwa manufaa yake mwenyewe, na akapendekeza kumlisha kwa chakula cha dengu ikiwa angekataa madai yote ya haki yake ya mzaliwa wa kwanza, na Esau akauza haki yake ya mzaliwa wa kwanza kwa Yakobo. **{SRSw 87.2}**

Esau alichukua wake wawili waabudu sanamu, ambayo ilikuwa huzuni kubwa kwa Isaka na Rebeka. Ijapokuwa ilikuwa hivyo, Isaka alimpenda Esau kuliko Yakobo. na alipofikiri kwamba alikuwa karibu kufa alimwomba Esau amandalie nyama, ili ambariki kabla hajafa. Esau hakumwambia baba yake kwamba alikuwa ameuza haki yake ya mzaliwa wa kwanza kwa Yakobo na akathibitisha kwa kiapo. Rebeka alisikia maneno ya Isaka, naye akakumbuka Maneno ya Bwana, “Mkubwa atamtumikia mdogo,” na alijua kwamba Esau alikuwa ameichukulia kwa wepesi haki yake ya mzaliwa wa kwanza na akamuuzia Yakobo. Alimshawishi Yakobo amdanganye baba yake na kwa ulaghai, apokee baraka za baba yake, ambazo alifikiri hazingeweza kupatikana kwa njia nyingine yoyote. Mara ya kwanza Yakobo hakuwa tayari kutekeleza udanganyifu huu, lakini hatimaye alikubali mipango ya mama yake. **{SRSw 88.1}**

Rebeka alifahamu upendeleo wa Isaka kwa Esau, na aliridhika kwamba kufikiri hakungebadili kusudi lake. Badala ya kumtumaini

Mungu, mpangaji wa mambo yote, alidhihirisha ukosefu wake wa imani kwa kumshawishi Yakobo amdanganye Baba yake. Njia ya Yakobo katika hili haikukubaliwa na Mungu. Rebeka na Yakobo walipaswa kumngoja Mungu alete makusudi yake mwenyewe kwa njia yake mwenyewe, na kwa wakati wake, badala ya kujaribu kuleta matukio yaliyotabiriwa kwa msaada wa udanganyifu. **{SRSw 88.2}**

Ikiwa Esau angepokea baraka za baba yake, ambazo ziliwekwa juu ya mzaliwa wa kwanza, mafanikio yake yangeweza kutoka kwa Mungu peke yake; na angembariki kwa ufanisi, au kuleta juu yake shida, kulingana na mwenendo wake. Ikiwa angempenda na kumheshimu Mungu, kama Habili mwadilifu, angekubaliwa na kubarikiwa na Mungu. Ikiwa, kama Kaini mwovu, hakuwa na heshima kwa Mungu wala kwa amri Zake, lakini alifuata njia yake mwenyewe potovu, asingepokea baraka kutoka kwa Mungu bali angekataliwa na Mungu, kama vile Kaini. Ikiwa njia ya Yakobo ingekuwa ya haki, ikiwa angempenda na kumcha Mungu, angebarikiwa na Mungu, na mkono wa Mungu unaofanikisha ungekuwa pamoja naye, hata kama asingepata baraka na upendeleo/kibali ambacho kwa ujumla alipewa mzaliwa wa kwanza. **{SRSw 88.3}**

Miaka ya Yakobo ya Uhamishoni

Rebeka alitubu kwa uchungu kwa ajili ya shauri lisilofaa ambalo alimpa Yakobo, kwa maana ilikuwa ni njia ya kumtenganisha naye milele. Alilazimika kukimbia ili kuokoa maisha yake kutokana na ghadhabu ya Esau, na mama yake hakuuona uso wake tena. Isaka aliishi miaka mingi baada ya kumpa Yakobo baraka, na akasadiki, kwa mwenendo wa Esau na Yakobo, kwamba baraka hiyo ilikuwa ya Yakobo. **{SRSw 89.1}**

Yakobo hakuwa na furaha katika uhusiano wake wa ndoa, ingawa wake zake walikuwa dada. Alifanya mkataba wa ndoa na Labani kwa binti yake Raheli, ambaye alimpenda. Baada ya kutumikia Raheli kwa miaka saba, Labani alimdanganya na kumpa Lea. Yakobo alipotambua udanganyifu uliokuwa umefanywa juu yake, na kwamba Lea alikuwa ametenda sehemu yake katika kumdanganya, asingeweza kumpenda Lea. Labani alitaka kuendelea kujipatia huduma za uaminifu za Yakobo kwa muda mrefu zaidi, kwa hiyo akamdanganya kwa kumpa Lea, badala ya Raheli. Yakobo alimkemea Labani kwa kudharau hisia zake, kwa kumpa Lea, ambaye hakuwa amempenda. Labani alimsihi Yakobo asimwache Lea, kwa maana hii ilionekana kuwa fedheha kubwa, si kwa mke tu, bali kwa familia nzima. Yakobo aliwekwa katika mtihani mkubwa, lakini aliamua kumshikilia Lea, na pia kumwoa dada yake. Lea alipendwa kwa kiwango kidogo sana kuliko Raheli. **{SRSw 89.2}**

Labani alikuwa mbinafsi katika mambo yake na Yakobo. Alifikiria tu kujinufaisha mwenyewe kupitia kazi ya uaminifu ya Yakobo. Angekuwa amemwacha Labani mjanja muda mrefu kabla, lakini aliogopa kukutana na Esau. Alisikia malalamiko ya wana wa Labani, wakisema, "**Yakobo amechukua mali yote ya baba yetu; na kwa mali ya baba yetu amepata fahari hii yote. Yakobo akaona uso wa Labani, ya kuwa hakumtazama vema kama jana na juzi. Mwanzo 31:1-2** **{SRSw 90.1}**

Yakobo alihuzunika. Hakujua ni njia gani ya kugeukia. Alipeleka jambo lake kwa Mungu na kuomba mwongozo kutoka Kwake. Bwana kwa rehema akajibu maombi yake yenye mfadhaiko na huzuni**. Bwana akamwambia Yakobo, Urudi mpaka nchi ya baba zako na kwa jamaa zako, Nami nitakuwa pamoja nawe. Mwanzo 31:3** **{SRSw 90.2}**

Yakobo akatuma watu, akawaita Raheli na Lea waje nyikani kwenye wanyama wake. Akawaambia, Naona uso wa baba yenu, kwamba hanitazami vema kama jana na juzi. Lakini Mungu wa baba yangu amekuwa pamoja nami. Nanyi mmejua ya kwamba kwa nguvu zangu zote nimemtumikia baba yenu. Na baba yenu amenidanganya, akabadili mshahara wangu mara kumi; lakini Mungu hakumwacha kunidhuru. Mwanzo 31:4-7 Yakobo aliwasimulia ndoto aliyopewa ya Mungu, kumwacha Labani na kwenda kwa jamaa zake. Raheli na Lea walionyesha kutoridhika kwao na utendaji wa baba yao. Yakobo aliporudia makosa yake kwao na akapendekeza kumwacha Labani, Raheli na Lea wakamwambia Yakobo; **Je! Imetubakia sehemu au urithi katika nyumba ya baba yetu? Hakutufanya kama wageni, maana ametuuza, naye amekula fedha zetu kabisa? Maana mali yote ambayo Mungu amemnyang'anya baba yetu, mali hiyo ndiyo yetu na ya wana wetu. Basi yoyote Mungu aliyokuambia, uyafanye. Mwanzo 31:14-16** **{SRSw 90.3}**

Kurudi Kanaani

Kwa kutokuwepo kwa Labani, Yakobo alichukua familia yake na vyote alivyokuwa navyo, na kumwacha Labani. Baada ya kuendelea na safari yake siku tatu, Labani alipata habari kwamba alikuwa amemwacha, na alikasirika sana. Naye akamfuata, akidhamiria kumrudisha kwa nguvu. Lakini Bwana alimhurumia Yakobo, na Labani alipokuwa karibu kumpata, alimpa ndoto ya kutosema mema au mabaya kwa Yakobo. Hiyo ni, hapaswi kumlazimisha kurudi, au kumhimiza kwa vivutio vya kupendeza, udanganyifu au kujikomba. **{SRSw 91.1}**

Labani alipokutana na Yakobo aliuliza kwa nini aliiba bila kujua na akawachukua binti zake kama mateka waliochukuliwa kwa upanga. Labani akamwambia, **Ninao uwezo mkononi mwangu wa kukufanyia madhara; lakini Mungu wa baba yako usiku huu ameniambia,**

akisema, Ujihadhari, usimwambie Yakobo neno la heri wala la shari. Mwanzo 31:29 Kisha Yakobo akamweleza Labani mwenendo usio na ukarimu aliokuwa amefuata kwake, kwamba alikuwa akijitafutia tu faida yake mwenyewe. Alimsihi Labani kuhusu unyoofu wa mwenendo wake akiwa pamoja naye, akasema, **Kilichoraruliwa na hayawani sikukuletea, mimi mwenyewe nimetwaa hasara yake, wewe umekidai katika mkono wangu, ikiwa kilichukuliwa mchana, au ikiwa kilichukuliwa usiku. Hii ilikuwa hali yangu; mchana jua likanipata, na baridi usiku, usingizi ukanitoka machoni mwangu. Mwanzo 31:39-40** {SRSw 91.2}

Yakobo akasema, Miaka hii ishirini nimekaa nyumbani mwako; nilikutumikia miaka kumi na minne kwa binti zako wawili, na miaka sita kwa wanyama wako, nawe umebadili mshahara wangu mara kumi. Kama Mungu wa baba yangu, Mungu wa Ibrahimu na Hofu ya Isaka, hangalikuwa pamoja nami, hakika sasa ungalinifukuza mikono mitupu. Mateso yangu na kazi za mikono yangu Mungu ameziona, akakukemea usiku huu. Mwanzo 31:41-42 {SRSw 91.3}

Kisha Labani akamhakikishia Yakobo kwamba alikuwa na nia kwa binti zake na watoto wao, kwamba hangeweza kuwadhuru. Alipendekeza kufanya agano kati yao. Na Labani akasema, Haya! Na tufanye agano, mimi na wewe, liwe kwa ushahidi kati ya mimi na wewe. Yakobo akatwaa jiwe akalisimamisha kama nguzo. Mwanzo 31:44-45 {SRSw 92.1}

Na Labani akasema, **Mungu awe shahidi kati ya mimi na wewe, wakati tusipoonana. Ukiwatesa binti zangu, na ukitwaa wake zaidi ya binti zangu, wala hapana mtu pamoja nasi, tazama, Mungu ni shahidi kati ya mimi na wewe. Mwanzo 31:49-50** {SRSw 92.2}

Yakobo alifanya agano zito mbele za Bwana kwamba hatachukua wake wengine zaidi ya wale aliochukua kutoka kwa Labani. **Labani akamwambia Yakobo, Tazama chungu hii utazame na nguzo niliyoitia kati ya mimi na wewe. Chungu hii na iwe shahidi, na nguzo hii na iwe shahidi, ya kuwa mimi sitapita chungu hii kuja kwako, wala wewe hutapita chungu hii na nguzo hii uje kwangu, kwa madhara. Mungu wa Ibrahimu, na Mungu wa Nahori, Mungu wa baba yao, ahukumu kati yetu. Yakobo akaapa kwa babaye Isaka Mwanzo 31:51-53** **{SRSw 92.3}**

Yakobo alipoendelea na safari yake, malaika wa Mungu walikutana naye. Naye alipowaona, alisema, “Hili ni jeshi la Mungu.” Aliwaona malaika wa Mungu katika ndoto, wakipiga kambi karibu naye. Yakobo alituma ujumbe wa unyenyekevu, wa upatanisho kwa ndugu yake Esau. Wale wajumbe wakarudi kwa Yakobo wakisema, **Tulifika kwa ndugu yako, Esau, naye anakuja kukulaki, na watu mia nne pamoja naye.** Ndipo Yakobo akaogopa sana, na kufadhaika sana, akawagawanya watu waliopo pamoja naye, na kondoo, na ng'ombe, na ngamia, wawe matuo mawili. Akasema, **Akija Esau kwa kundi la kwanza, akalipiga, kundi litakalosalia litaokoka.** **{SRSw 92.4}**

Yakobo akasema, Ee Mungu wa baba yangu Ibrahimu, na Mungu wa baba yangu Isaka, Bwana, uliyeniambia, Rudi uende mpaka nchi yako, na kwa jamaa zako, Nami nitakutendea mema; mimi sistahili hata kidogo hizo rehema zote na kweli yote uliyomfanyia mtumwa wako; maana nalivuka mto huo wa Yordani na fimbo yangu tu, na sasa nimekuwa matuo mawili. Uniokoe sasa na mkono wa ndugu yangu, mkono wa Esau, maana mimi namwogopa, asije akanipiga, na mama pamoja na wana. Nawe ulisema, Hakika nitakutendea mema, Nami nitafanya uzao wako

uwe kama mchanga wa bahari, usiohesabika kwa kuwa mwingi. Mwanzo 32:6-12 {SRSw 93.1}

SURA YA 13—YAKOBO NA MALAIKA

Sura hii imejengwa katika Mwanzo 32:24-33:11.

Makosa ya Yakobo katika kupokea baraka za ndugu yake kwa ulaghai yaliletwa tena kwa nguvu mbele yake, na aliogopa kwamba Mungu angemruhusu Esau kuchukua uhai wake. Katika dhiki yake aliomba kwa Mungu usiku kucha. Malaika aliwakilishwa kwangu kama amesimama mbele ya Yakobo, akiwasilisha kosa lake mbele yake katika tabia yake ya kweli. Malaika anapogeuka kumwacha, Yakobo alimshika, na hakumwacha aende zake. Alimsihi kwa machozi. Alimsihi kwamba ametubu kabisa dhambi zake na makosa dhidi ya kaka yake, ambayo yalikuwa njia ya kumtenganisha na nyumba ya baba yake kwa miaka

ishirini. Alithubutu kudai ahadi za Mungu na ishara za kibali Chake kwake mara kwa mara kwa kutokuwepo kwake kutoka kwa nyumba ya baba yake. **{SRSw 94.1}**

Usiku kucha Yakobo alishindana mweleka na malaika, akiomba baraka. Malaika alionekana kupinga maombi yake, kwa kuendelea kumkumbusha dhambi zake mara kwa mara, wakati huohuo akijaribu kujitenga naye. Yakobo aliazimia kumshikilia malaika, si kwa nguvu za kimwili, bali kwa nguvu ya imani hai. Katika dhiki yake Yakobo alirejelea toba ya nafsi yake, unyenyekevu wa kina aliokuwa ameuhisi kwa makosa yake. Malaika aliyatazama maombi yake kwa kutojali, akiendelea kufanya jitihada za kujitoa kutoka kwa mshiko wa Yakobo. Angeweza kutumia nguvu zake zisizo za kawaida na kutumia nguvu Zake kwa Yakobo, lakini hakuchagua kufanya hivyo. **{SRSw 94.2}**

Lakini alipoona kwamba hakumshinda Yakobo, ili kumsadikisha juu ya nguvu zake zisizo za kawaida, aligusa paja lake, ambalo mara moja lilitoka mahali pake-aliteguka. Lakini Yakobo asingeacha jitihada zake za dhati kwa ajili ya maumivu ya mwili. Lengo lake lilikuwa kupata baraka, na maumivu ya mwili hayakutosha kugeuza akili yake kutoka kwa lengo lake. Azimio lake lilikuwa na nguvu zaidi katika dakika za mwisho za pambano kuliko mwanzoni. Imani yake ilizidi kuwa ya bidii na ya kudumu hadi mwisho kabisa, hata hadi kupambazuka. Asingemwacha malaika aende zake mpaka ambariki. **Akasema, Niache, niende, maana kunapambazuka. Akasema, Sikuachi, usiponibariki. Kisha malaika akauliza, Akamwuliza, Jina lako nI nani? Akasema, Yakobo. Akamwambia, Jina lako hutaitwa tena Yakobo, ila Israeli, maana umeshindana na Mungu, na watu, nawe umeshinda. Mwanzo 32:26-28** **{SRSw 95.1}**

Imani Ishindayo Mwanzo 32 -34.

Imani ya Yakobo ya uvumilivu ilishinda. Alimshikilia malaika huyo mpaka akapata baraka aliyotaka, na uhakikisho wa msamaha wa dhambi zake. Kisha jina lake lilibadilishwa kutoka kuwa Yakobo, mdanganyifu, hadi kuwa Israeli, ambayo inaashiria mkuu wa Mungu. **Yakobo akamwuliza, akasema, Niambie, tafadhali, Jina Lako? Akasema, Kwa nini waniuliza Jina Langu? Akambariki huko. Yakobo akapaita mahali pale, Penueli, maana alisema, Nimeonana na Mungu uso kwa uso, na nafsi yangu imeokoka. Mwanzo 32:29-30** Ni Kristo aliyekuwa pamoja na Yakobo usiku ule, ambaye alipigana naye mieleka, na ambaye alimshikilia kwa kutochoka mpaka alipombariki. **{SRSw 95.2}**

Bwana alisikia dua za Yakobo, na akabadilisha makusudi ya moyo wa Esau. Hakuidhinisha njia yoyote mbaya ambayo Yakobo alifuata. Maisha yake yalikuwa ya mashaka, fadhaa, na majuto kwa sababu ya dhambi yake, hadi pale aliposhindana kwa bidii na malaika, na ushahidi aliopata pale kwamba Mungu alikuwa amesamehe dhambi zake. **{SRSw 96.1}**

Naam, alikuwa na uwezo juu ya malaika Akashinda; alilia, na kumsihi; Alimwona huko Betheli, naye akasema nasi huko; Naam, Bwana, Mungu wa majeshi; Bwana ndilo kumbukumbu Lake. Hosea 12:4-5 {SRSw 96.2}

Esau alikuwa akija kumkabili Yakobo na jeshi, kwa kusudi la kumuua ndugu yake. Lakini Yakobo alipokuwa akipigana mieleka na malaika usiku ule, malaika mwingine alitumwa kwenda kugusa moyo wa Esau katika saa zake za kulala. Katika ndoto yake alimwona Yakobo akiwa uhamishoni kutoka katika nyumba ya baba yake kwa miaka ishirini, kwa sababu aliogopa maisha yake yatakuwa hatarini. Naye akaona huzuni yake kumkuta mama yake amekufa. Aliona katika ndoto yake unyenyekevu wa Yakobo na malaika wa Mungu karibu naye.

Aliota kwamba walipokutana hakuwa na nia ya kumdhuru. Esau alipoamka alisimulia ndoto yake kwa watu wake mia nne na kuwaambia kwamba wasimdhuru Yakobo, kwa maana Mungu wa baba yake alikuwa pamoja naye. Na watakapokutana na Yakobo, asiwepo hata mmoja wao anayepaswa kumdhuru. **{SRSw 96.3}**

Yakobo akainua macho yake, akaona, na tazama, Esau anakuja na watu mia nne pamoja naye. Akagawanya watu wakwe katika makundi 4, Lea, na Raheli, na wale vijakazi wawili, wana wao. Akawaweka hao vijakazi na wana wao mbele, na Lea na wanawe nyuma yao, na Raheli na Yusufu mwisho. Akapita mwenyewe mbele yao, akainama mpaka nchi mara saba, hata alipomkaribia ndugu yake. Esau akaja mbio kumlaki, akamkumbatia, na kumwangukia shingoni, akambusu; nao wakalia. Mwanzo 33:1-4 Yakobo alimsihi Esau akubali sadaka ya amani, ambayo Esau alikataa, lakini Yakobo akamhimiza: **Pokea, tafadhali, mbaraka wangu, ulioletewa, kwa sababu Mungu amenineemesha, na kwa sababu ninavyo hivi vyote Akamshurutisha, naye akapokea. Mwanzo 33:11** **{SRSw 96.4}**

Somo Muhimu

Yakobo na Esau wanawakilisha makundi mawili: Yakobo, mtu Mwenye Haki, na Esau, mtu Mwovu. Dhiki ya Yakobo alipojua kwamba Esau alikuwa akija dhidi yake pamoja na watu mia nne, inawakilisha taabu ya wenye haki wakati amri itakapotolewa ya kuuawa kwao, kabla tu ya kuja kwa Bwana. Waovu wanapokusanyika juu yao, watajawa na uchungu, kwa maana, kama Yakobo, hawawezi kuona njia yoyote ya kuokoa maisha yao. Malaika alisimama mbele ya Yakobo, naye akamshika malaika na kumshikilia na kushindana naye usiku kucha. Vivyo hivyo wenye haki, katika wakati wao wa taabu na uchungu, watashindana mieleka katika maombi na Mungu, kama Yakobo

alivyoshindana na malaika. Yakobo katika dhiki yake aliomba usiku kucha kwa ajili ya ukombozi dhidi ya mkono wa Esau. Wenye haki katika uchungu wao wa kiakili watamlilia Mungu mchana na usiku kwa ajili ya ukombozi dhidi ya mkono wa waovu wanaowazunguka. **{SRSw 97.1}**

Yakobo alikiri kutostahili kwake: **mimi sistahili hata kidogo hizo rehema zote na kweli yote uliyomfanyia mtumwa wako; maana nalivuka mto huo wa Yordani na fimbo yangu tu, na sasa nimekuwa matuo mawili. Mwanzo 32:10** Wenye haki katika dhiki yao watakuwa na hisia ya kina ya kutostahili kwao na kwa machozi mengi watakubali kutostahili kwao kabisa na, kama Yakobo, wataomba ahadi za Mungu kupitia Kristo, zilizofanywa kwa wadhambi wanaomtegemea, wasiojiweza, na wanaotubu kama hao. **{SRSw 97.2}**

Yakobo akamshika Malaika huyo kwa uthabiti katika dhiki yake na hakumruhusu aende zake. Alipokuwa akiomba dua kwa machozi, Malaika Huyo alimkumbusha makosa yake ya zamani na akajaribu kujiondoa kutoka kwa Yakobo, ili kumjaribu na kumthibitisha. Vivyo hivyo wenye haki, katika siku ya taabu yao, watajaribiwa,watathibitishwa, na kujaribiwa, kudhihirisha nguvu zao za imani, uvumilivu wao na imani isiyotikisika katika uwezo wa Mungu wa kuwakomboa. **{SRSw 97.3}**

Yakobo hakukubali kuambiwa ageuke au aende. Alijua kwamba Mungu alikuwa na huruma, na aliomba rehema Yake. Alirejelea huzuni yake ya zamani kwa sabau ya makosa yake, na toba yake, na akasisitiza ombi lake la kuokolewa kutoka mkononi wa Esau. Hivyo kusihi kwake kuliendelea usiku kucha. Alipoyakumbuka makosa yake ya zamani alikaribia kukata tamaa. Lakini alijua kwamba lazima apate msaada kutoka kwa Mungu, la sivyo angeangamia. Alimshikilia Malaika huyo

kwa nguvu na kusisitiza ombi lake kwa kilio cha uchungu, cha dhati, hadi akashinda. **{SRSw 98.1}**

Ndivyo itakavyokuwa kwa wenye haki. Wanapopitia matukio ya maisha yao ya zamani, matumaini yao yatakaribia kuzama. Lakini wanapotambua kwamba ni suala la uhai au mauti, watamlilia Mungu kwa dhati na bidii, na kumwomba Yeye kuhusiana na huzuni yao ya zamani, na toba ya unyenyekevu kwa dhambi zao nyingi, na kisha watataja ahadi Yake. **"Au azishike nguvu Zangu, Afanye amani Nami; Naam, afanye amani Nami." Isaya 27:5** Hivyo maombi yao ya dhati yatatapelekwa kwa Mungu mchana na usiku. Mungu asingesikia maombi ya Yakobo na kwa rehema kumuokoa maisha yake kama asingetubu makosa yake hapo awali katika kupata baraka kwa ulaghai. **{SRSw 98.2}**

Wenye haki, kama Yakobo, watadhihirisha imani isiyobadilika, isiyolegea na azimio la dhati, lisilokubali kukataliwa. Watahisi kutostahili kwao lakini hawatakuwa na makosa yaliyofichwa ya kufunuliwa. Kama watakuwa na dhambi ambazo hajizaungamwa na hazijatubiwa, zitakapotokeza mbele yao wakati huo, huku wakiteswa kwa woga na uchungu, kwa hisia kali ya kutostahili kwao, wangelemewa. Kukata tamaa kungekata imani yao ya dhati, na wasingeweza kuwa na ujasiri wa kumsihi Mungu hivyo kwa bidii kwa ajili ya ukombozi, na nyakati zao za thamani zingetumika katika kuungama dhambi zilizofichwa na kuomboleza hali yao ya kutokuwa na tumaini. **{SRSw 98.3}**

Kipindi cha rehema ni wakati unaotolewa kwa wote kujiandaa kwa ajili ya siku ya Mungu. Iwapo yeyote atapuuza maandalizi na kutozingatia maonyo ya uaminifu yanayotolewa, hatakuwa na udhuru. Kupambana mielekea kwa bidii kwa Yakobo,na kushindana na Malaika

kunapaswa kuwa kielelezo kwa Wakristo: Yakobo alishinda kwa sababu alikuwa akivumilia na kuazimia. **{SRSw 99.1}**

Wote wanaotamani baraka za Mungu, kama vile Yakobo, na kushikilia ahadi, kama alivyofanya, na kuwa na bidii dhati na uvumilivu kama alivyokuwa, watafanikiwa kama alivyofaulu. Kuna matumizi madogo sana ya imani ya kKweli na uzito mdogo sana wa ukweli unaokaa juu ya waumini wengi wanaodai kuwa ni wavivu katika mambo ya kiroho. Hawako tayari kufanya juhudi, kujikana nafsi, kuteseka mbele za Mungu, kuomba kwa muda mrefu na kwa bidii kwa ajili ya baraka, na kwa hiyo hawapati. Imani hiyo ambayo itaishi wakati wa shida lazima iwekwe katika mazoezi ya kila siku katika sasa. Wale ambao hawafanyi juhudi kubwa sasa za kutumia imani isiyochoka na yenye ustahimilivu, hawatakuwa tayari kabisa kutumia imani hiyo ambayo itawawezesha kusimama katika siku ya taabu. **{SRSw 99.2}**

SURA YA 14—WANA WA ISRAELI

Sura hii imejengwa katika Mwanzo 37; 39; 41-48; Kutoka 1-4.

Yusufu alisikiliza maagizo ya baba yake na alimcha Bwana. Alikuwa mtiifu zaidi kwa mafundisho ya haki ya baba yake kuliko ndugu zake wote. Alithamini maagizo yake na, kwa uadilifu wa moyo, alipenda kumtii Mungu. Alihuzunishwa na mwenendo mbaya wa baadhi

ya ndugu zake na kwa upole akawasihi wafuate njia ya haki na kuacha matendo yao maovu. Hii iliwakasirisha zaudu tu dhidi yake. Chuki yake ya dhambi ilikuwa ile ambayo asingeweza kuvumilia kuona ndugu zake wakitenda dhambi dhidi ya Mungu. Aliliweka jambo hilo mbele ya baba yake, akitumaini kwamba mamlaka yake yangeweza kuyarekebisha. Ufichuaji huu wa makosa yao uliwakasirisha ndugu zake dhidi yake. Walikuwa wameona upendo mkubwa wa baba yao kwa Yusufu, na walikuwa wakimwonea wivu. Wivu wao ulikua na kuwa chuki, na hatimaye kuua. **{SRSw 100.1}**

Malaika wa Mungu alimwagiza Yusufu katika ndoto ambazo alikuwa amezisimulia bila hatia kwa ndugu zake; **Tazama, sisi tulikuwa tukifunga miganda shambani, kumbe! Mganda wangu ukaondoka ukasimama, na tazama, miganda yenu ikazunguka ikainama mbele ya mganda wangu. Ndugu zake wakamwambia, Je! Kweli wewe utatumiliki sisi? Nawe utatutawala sisi? Wakazidi kumchukia kwa ajili ya ndoto yake, na kwa maneno yake. Mwanzo 37:7-8** **{SRSw 100.2}**

Akaota tena ndoto nyingine, akawaambia ndugu zake, akasema, Angalieni, nimeota ndoto nyingine; na tazama, jua na mwezi na nyota kumi na moja zikaniinamia. Akawaambia baba yake na ndugu zake; baba yake akamkemea akamwambia, Ni ndoto gani hii uliyoiota? Je! Mimi na mama yako na ndugu zako tutakuja tukusujudie hata nchi? Ndugu zake wakamhusudu; bali baba yake akalihifadhi neno hili. Mwanzo 37:9-11 **{SRSw 101.1}**

Yusufu Huko Misri

Ndugu za Yusufu walikusudia kumuua, lakini hatimaye walijiridhisha kumuuza kama mtumwa, ili kumzuia kuwa mkuu kuliko wao wenyewe. Walifikiri walikuwa wamemweka mahali ambapo

hawangesumbuliwa tena na ndoto zake, na ambapo hakutakuwa na uwezekano wa kutimizwa kwa hizo ndoto. Lakini njia ile ile waliyoichukua Mungu aliigeuza ili kutimiza kile ambacho walikusudia kisitokee kamwe—kwamba yeye angekuwa na mamlaka juu yao. **{SRSw 101.2}**

Mungu hakumwacha Yusufu aende Misri peke yake. Malaika walitayarisha njia kwa ajili ya mapokezi yake. Potifa, ofisa wa Farao, nahodha wa walinzi, alimnunua kutoka kwa Waishmaeli. Bwana alikuwa pamoja na Yusufu, naye akamfanikisha na kumpa kibali kwa bwana wake, hata kila alichokuwa nacho aliweka chini ya uangalizi wa Yusufu. "**Akayaacha yote aliyokuwa nayo mkononi mwa Yusufu; wala hakujua habari za kitu chochote chake, ila hicho chakula alichokula tu. Mwanzo 39:6"** Ilichukuliwa kuwa chukizo kwa Mwebrania kuandaa chakula kwa ajili ya Mmisri. **{SRSw 101.3}**

Yusufu alipojaribiwa kukengeuka kutoka kwenye njia ya haki, ili kuivunja sheria ya Mungu na kuthibitisha kwamba si kweli kwa bwana wake, alipinga kwa uthabiti na kutoa ushahidi wa kuinua uwezo wa kumcha Mungu katika jibu lake kwa mke wa bwana wake. Baada ya kusema juu ya imani kubwa ya bwana wake ndani yake, kwa kumkabidhi yote aliyokuwa nayo, alisema kwa mshangao. **Nifanyeje ubaya huu mkubwa nikamkose Mungu? Mwanzo 39:9** Hangeshawishiwa kukengeuka kutoka kwenye njia ya haki na kukanyaga sheria ya Mungu kwa vivutio au vitisho vyovyote. **{SRSw 101.4}**

Na aliposhtakiwa, na kosa baya kuwekwa juu yake kwa uongo, hakukatishwa tamaa wala kuvunjika moyo. Akiwa na dhamiri ya kutokuwa na hatia na haki, aliendelea kumtumaini Mungu. Na Mungu, ambaye hadi sasa alikuwa amemsaidia, hakumwacha. Alikuwa amefungwa kwa pingu na kuwekwa katika gereza lenye huzuni. Hata

hivyo Mungu aligeuza hata msiba huu kuwa baraka. Alimpa kibali kwa mlinzi wa gereza, na muda mfupi Yusufu akapewa kusimamia wafungwa wote. **{SRSw 102.1}**

Hapa kuna mfano kwa vizazi vyote ambavyo vinapaswa kuishi juu ya dunia. Ingawa wanaweza kukabiliwa na majaribu, lakini wanapaswa kutambua kwamba kuna ulinzi ulio karibu, na itakuwa ni kosa lao wenyewe ikiwa hawatahifadhiwa. Mungu atakuwa msaada wa karibu, na Roho Wake ni ngao. Ingawa wamezungukwa na majaribu makali zaidi, kuna chanzo cha nguvu ambacho wanaweza kukitegemea na kushinda. **{SRSw 102.2}**

Jinsi shambulio lilivyokuwa kali juu ya maadili ya Yusufu. Lilitoka kwa mtu mwenye ushawishi, ambaye angeweza kumpotosha kwa kirahisi sana. Hata hivyo lilipingwa mara moja na kwa uthabiti. Aliteseka kwa ajili ya wema wake na uadilifu wake, kwa maana yeye ambaye angempotosha alilipiza kisasi juu ya wema wa Yusufu, ambao asingeweza kuupotosha, na kwa ushawishi wake ukamfanya atupwe gerezani, kwa kumshtaki kwa kosa baya. Hapa Yusufu aliteseka kwa sababu hakutaka kuacha uadilifu wake. Alikuwa ameweka sifa na shauku yake katika mikono ya Mungu, na ijapokuwa aliteswa kwa muda, ili atayarishwe kujaza nafasi muhimu, Mungu aliilinda kwa usalama sifa hiyo ambayo ilitiwa rangi nyeusi na mshtaki mwovu, na baadaye, katika wakati wake mzuri, akaifanya ing'ae. Mungu alilifanya hata gereza kuwa njia ya kuelekea kwenye kupanda kwake juu. Utu wema utaleta thawabu yake wenyewe. Ngao iliyofunika moyo wa Yusufu ilikuwa ni hofu ya Mungu, ambayo ilimfanya kuwa mwaminifu na mwenye haki kwa Bwana wake na mwaminifu kwa Mungu. **{SRSw 102.3}**

Ingawa Yusufu aliinuliwa kuwa mtawala juu ya nchi yote, lakini hakumsahau Mungu. Alijua kwamba alikuwa mgeni katika nchi ngeni, mtu aliyetenganishwa na baba yake na ndugu zake, jambo ambalo mara

nyingi lilimletea huzuni, lakini aliamini kabisa kwamba mkono wa Mungu ulikuwa umemshindia njia yake ,na kumweka katika nafasi muhimu. Na, akimtegemea Mungu daima, alitekeleza majukumu yote ya ofisi yake, kama mtawala juu ya nchi ya Misri, kwa uaminifu. **{SRSw 103.1}**

Yusufu alitembea na Mungu. Asingeweza kushawishiwa kukengeuka kutoka kwenye njia ya haki na kukiuka sheria ya Mungu, kwa ushawishi, vivutio vyovyote au vitisho. Kujitawala nafsi na subira yake katika dhiki na uaminifu wake usioyumba, vimeachwa kuwa kumbukumbu kwa manufaa ya wote ambao baadaye wanapaswa kuishi duniani. Ndugu za Yusufu walipokiri dhambi yao mbele yake, yeye aliwasamehe kwa moyo mkunjufu na alionyesha kwa matendo yake ya ukarimu na upendo kwamba hakuwa na hisia za kinyongo kwa ajili ya mwenendo wao wa kikatili walioufanya zamani kwake. **{SRSw 103.2}**

Siku za Mafanikio

Wana wa Israeli hawakuwa watumwa. Hawakuwahi kuuza mifugo wao, mashamba yao, na wao wenyewe kwa Farao kwa ajili ya chakula, kama Wamisri wengi walivyofanya. Walikuwa wamepewa sehemu ya ardhi ya kukaa, pamoja na mifugo yao na ng'ombe, kwa sababu ya huduma ambayo Yusufu alikuwa nayo kwa ufalme. Farao alithamini hekima yake katika usimamizi wa mambo yote yanayohusiana na ufalme, hasa katika maandalizi ya miaka mingi ya njaa iliyokuwa inakuja juu ya nchi ya Misri. Alihisi kwamba ufalme wote uliwiwa kwa ajili ya ustawi wake kwa usimamizi wa busara wa Yusufu; na, kama ishara ya shukrani zake, alimwambia Yusufu, “**nchi ya Misri iko mbele yako, palipo pema pa nchi uwakalishe baba yako na ndugu zako; na wakae katika nchi ya Gosheni. Tena ukijua ya kuwa wako watu hodari miongoni mwao, uwaweke wawe wakuu wa wanyama wangu.” Mwanzo 47:6** **{SRSw 103.3}**

Yusufu akawakalisha babaye na nduguze, na kuwapa milki katika nchi ya Misri, katika mahali pazuri pa nchi, katika nchi ya Ramesesi, kama Farao alivyoamuru. Naye Yusufu akawalisha babaye na nduguze na nyumba yote ya babaye, kwa kadiri ya hesabu ya watoto wao. Mwanzo 47:11-12 {SRSw 104.1}

Hakuna kodi ambayo mfalme wa Misri, aliwadai baba na ndugu wa Yusufu, na Yusufu aliruhusiwa kuwaandalia chakula kwa wingi. Mfalme akawaambia viongozi wake, Je, sisi hatuna deni kwa Mungu wa Yusufu, na kwake, kwa ugavi huu wa chakula huria? Je, si kwa sababu ya hekima yake tulimehifadhi ghalani chakula kwa wingi sana? Wakati nchi zingine zinaangamia, sisi tuna chakula cha kutosha! Usimamizi wake ulikuwa umetajirisha sana ufalme. **{SRSw 104.2}**

Yusufu akafa, na ndugu zake wote, na watu wote wa kizazi kile. Na wana wa Israeli walikuwa na uzazi sana, na kuongezeka mno, na kuzidi kuwa wengi, nao wakaendelea na kuongezeka nguvu; na ile nchi ilikuwa imejawa na wao. Basi akainuka mfalme mpya kutawala Misri, asiyemjua Yusufu. Akawaambia watu wake, Angalieni, watu wa wana wa Israeli ni wengi tena wana nguvu kuliko sisi. Haya! Na tuwatendee kwa akili, wasije wakaongezeka; tena, ikitokea vita, wao nao wasije wakashikamana na adui zetu na kupigana nasi, na kutoka katika nchi hii. Kutoka 1:6-10 {SRSw 104.3}

Ukandamizaji

Mfalme huyu mpya wa Misri aligundua kwamba wana wa Israeli walikuwa na manufaa mkubwa kwa ufalme. Wengi wao walikuwa

mafundi wenye uwezo na uelewa, na hakuwa tayari kupoteza kazi yao. Mfalme huyu mpya aliwahesabu wana wa Israeli pamoja na kundi hilo la watumwa waliokuwa wameuza makundi yao ya mifugo yao, mali zao, na wao wenyewe kwa ufalme. **Basi wakaweka wasimamizi juu yao wawatese kwa mizigo yao. Nao wakamjengea Farao miji ya kuwekea akiba, Pithomu na Ramesesi. Kutoka 1:11** **{SRSw 105.1}**

Lakini kwa kadiri ya walivyowatesa ndivyo walivyoongezeka na kuzidi kuenea. Nao walichukiwa kwa sababu ya wana wa Israeli. Wamisri wakawatumikisha wana wa Israeli kwa ukali; wakafanya maisha yao kuwa uchungu kwa kazi ngumu; kazi ya chokaa na ya matofali, na kila namna ya kazi ya mashamba; kwa kazi zao zote walizowatumikisha kwa ukali. Kutoka 1:12-14 **{SRSw 105.2}**

Waliwalazimisha wanawake wao kufanya kazi shambani, kana kwamba ni watumwa. Hata hivyo idadi yao haikupungua. Mfalme na wakuu wake walipoona kwamba wanaongezeka mara kwa mara, walishauriana pamoja ili kuwalazimisha kutimiza kiasi fulani fulani cha kazi kila siku. Walifikiria kuwatiisha kwa kazi ngumu, na walikuwa na hasira kwa sababu hawakuweza kupunguza idadi yao na kuvunja roho yao ya kujitegemea na kuwa huru. **{SRSw 105.3}**

Na kwa sababu walishindwa kutimiza kusudi lao, waliifanya mioyo yao kuwa ngumu kwenda mbele zaidi. Mfalme aliamuru kwamba watoto wa kiume wauawe mara tu wanapozaliwa. Shetani ndiye aliyekuwa mwanzilishi na mtendaji katika mambo haya. Alijua kwamba mkombozi alipaswa kuinuliwa miongoni mwa Waebrania ili kuwaokoa kutokana na ukandamizaji. Alifikiri kwamba ikiwa angeweza kumshawishi mfalme ili kuwaangamiza watoto wa kiume, kusudi la Mungu lingeshindwa. Wanawake walimcha Mungu na hawakufanya kama mfalme wa Misri alivyowaamuru, bali aliwaokoa watoto wa kiume, na wakawa hai. **{SRSw 105.3}**

Wanawake hawakuthubutu kuwaua watoto wa Kiebrania, na kwa sababu hawakutii amri ya mfalme, Bwana aliwapa mafanikio. Mfalme wa Misri alipofahamishwa kwamba amri yake haikutiiwa, alikasirika sana. Kisha akafanya amri yake kuwa ya dharura na inayojumuisha kwa mapana. Aliwaagiza watu wake wote kuweka lindo kali, akisema, **Kila mtoto mwanamume atakayezaliwa mtamtupa mtoni, na kila mtoto mwanamke mtamhifadhi hai. Kutoka 1:22** **{SRSw 106.1}**

Musa

Wakati amri hii ya kikatili ilipokuwa inatekelezwa kikamilifu, Musa alizaliwa. Mama yake alimficha kwa muda mrefu Kadiri alivyoweza kwa usalama, na kisha akatayarisha chombo kidogo cha nyasi, na kukipaka lami ili maji yasiingie kwenye kikapu kile, na kukiweka kwenye ukingo wa maji, huku dada yake akizunguka karibu na maji kana kwamba hakuwa na habari. Alikuwa akitazama kwa hamu kuona itakuwaje kwa mdogo wake. Malaika pia walikuwa wakitazama, ili kwamba madhara yoyote yasimpate mtoto mchanga asiyejiweza, ambaye alikuwa amewekwa pale na mama mwenye upendo mwenye kujitoa kwaajili ya utunzaji wa Mungu kwa maombi yake ya bidii na dhati yaliyochanganyika na machozi. **{SRSw 106.2}**

Na malaika hawa walielekeza nyayo za binti ya Farao hadi mtoni, karibu na mahali pale ambapo mtoto mdogo mgeni na asiye na hatia alikuwa amelala. Usikivu wake ulivutiwa na chombo kidogo cha ajabu, na akamtuma mmoja wa wajakazi wake amletee. Na alipoondoa kifuniko cha chombo hiki kidogo kilichojengwa kwa namna ya pekee, alimwona mtoto mchanga mzuri, **na tazama, mtoto yule analia. Basi akamhurumia, Kutoka 2:6** Alijua kwamba mama Mwebrania mwenye huruma alikuwa ametumia njia hii ya pekee ili kuhifadhi maisha ya mtoto wake mchanga anayependwa sana, na aliamua mara moja kwamba atakuwa mwanawe. Yule dada wa Musa akajitokeza mara

moja na kuuliza, **Je! Niende nikamwite mlezi katika wanawake wa Kiebrania, aje kwako, akunyonyeshee mtoto huyu? Binti Farao akamwambia, Haya! Enenda. Kutoka 2:7,8** **{SRSw 106.3}**

Kwa furaha dada huyo alikimbia kwa mama yake na kumweleza habari za furaha na kumwongoza kwa haraka kwa binti ya Farao, ambapo mama alipewa mtoto yule ili amnyonyeshe, na alilipwa mshahara mzuri kwa ajili ya kulea mtoto wake mwenyewe. Kwa shukrani mama huyu akaanza kazi yake yenye furaha sasa kwa usalama. Aliamini kwamba Mungu alikuwa amehifadhi maisha yake. Kwa uaminifu alitumia fursa hiyo ya thamani ya kumlea mwanawe kwa ajili ya maisha yenye manufaa. Alikuwa makini zaidi katika mafundisho yake kuliko yale ya watoto wake wengine; kwa maana aliamini kuwa alihifadhiwa kwa kazi fulani kubwa. Kwa mafundisho yake ya uaminifu aliingiza katika akili yake changa hofu ya Mungu na upendo kwa ile Kweli na haki. **{SRSw 107.1}**

Hakukomea hapa katika jitihada zake bali aliendelea kumwomba kwa bidii kwa Mungu kwa ajili ya mwana wake ili ahifadhiwe kutokana na kila ushawishi mbovu. Alimfundisha mwanawe kusujudu na kumwomba Mungu, Mungu aliye hai, kwa kuwa Yeye pekee Ndiye angeweza kumsikia na kumsaidia katika dharura yoyote. Alijitahidi kumfundisha uovu wa ibada ya sanamu. Alijua kwamba muda si mrefu angetenganishwa na ushawishi wake na kuachwa kwa mama yake wa kifalme aliyeasiliwa, ili kuzungukwa na ushawishi ambao uliratibiwa kumfanya asiamini kuwepo kwa Muumba wa mbingu na dunia. **{SRSw 107.2}**

Mafundisho aliyopokea kutoka kwa wazazi wake yalikuwa ya kuimarisha akili yake na kumkinga ili asije akajivuna na kupotoshwa na dhambi na kuwa na kiburi katikati ya fahari na ubadhirifu wa maisha ya kifalme. Alikuwa na akili safi na moyo wa uelewa, na kamwe

hakupoteza hisia za uchamungu alizopokea katika ujana wake. Mama yake alimhifadhi kwa muda mrefu kama alivyoweza, lakini alilazimika kutengana naye alipokuwa na umri wa miaka kumi na miwili hivi, na ndipo akawa mwana wa binti Farao. **{SRSw 108.1}**

Hapa Shetani alishindwa. Kwa kumshawishi Farao ili kuwaangamiza watoto wa kiume, alifikiri angezuia makusudi ya Mungu na kumwangamiza yule ambaye Mungu angemwinua ili kuwakomboa watu Wake. Lakini amri hiyohiyo, ya kuwaua watoto wa Kiebrania ikawa ndiyo ndiyo njia ambayo Mungu aliitumia ili kumweka Musa katika familia ya kifalme, ambako alikuwa na faida za kuwa mtu msomi na mwenye uwezo mkubwa wa kuwaongoza watu Wake kutoka Misri. **{SRSw 108.2}**

Farao alitarajia kumwinua mjukuu wake aliyeasiliwa kwenye kiti cha enzi. Alimfundisha kusimama mbele ya majeshi ya Misri na kuwaongoza vitani. Musa alipendwa sana na jeshi la Farao na aliheshimiwa kwa sababu aliendesha vita kwa ustadi na hekima ya hali ya juu. **Musa akafundishwa hekima yote ya Wamisri, akawa hodari wa maneno na matendo. Matendo ya Mitume 7:22** Wamisri walimwona Musa kuwa mtu asiye wa kawaida. **{SRSw 108.3}**

Maandalizi Maalum kwa Ajili ya Uongozi

Malaika walimfundisha Musa kwamba Mungu alikuwa amemchagua kuwakomboa wana wa Israeli. Viongozi miongoni mwa wana wa Israeli pia walifundishwa na malaika kwamba wakati wa ukombozi wao ulikuwa umekaribia, na kwamba Musa alikuwa mtu ambaye Mungu angemtumia kukamilisha kazi hii. Musa alifikiri kwamba wana wa Israeli wangepaswa kupigana vita, na kwamba angesimama mbele ya jeshi la Waebrania, ili kuendesha vita dhidi ya majeshi ya Misri na kuwakomboa ndugu zake kutoka katika nira ya

uonevu. Akiwa na mtazamo huu, Musa alilinda hisia zake, ili zisije zikamfungamanisha sana na mama yake wa kumlea au juu ya Farao, isije ikawa vigumu zaidi kwake kubaki huru, kufanya mapenzi ya Mungu. **{SRSw 108.4}**

Bwana alimhifadhi Musa asiharibiwe na ushawishi mbaya uliomzunguka. Kanuni za Ukweli, alizopokea katika ujana wake kutoka kwa wazazi wanaomcha Mungu, hakuzisahau kamwe. Na wakati alipohitaji zaidi kulindwa dhidi ya ushawishi mbaya wa maisha kifalme, ndipo mafundisho ya ujana wake yalipozaa matunda. Kumcha Mungu kulikuwa mbele zake. Na upendo wake kwa ndugu zake ulikuwa na nguvu sana, na heshima yake kwa imani ya Kiebrania ilikuwa kubwa sana, hata asingeficha asili yake kwa heshima ya kuwa mrithi wa familia ya kifalme. **{SRSw 109.1}**

Musa alipokuwa na umri wa miaka arobaini, "**akatoka kuwaendea ndugu zake, akatazama mizigo yao. Akamwona Mmisri anampiga Mwebrania, mmojawapo wa ndugu zake. Basi akatazama huko na huko, na alipoona ya kuwa hapana mtu, akampiga Mmisri yule, akamficha ndani ya mchanga. Akatoka siku ya pili, na tazama, watu wawili wa Waebrania walikuwa wakipigana. Akamwambia yule aliyemdhulumu mwenzake, Mbona unampiga mwenzako? Yule akasema, Ni nani aliyekuweka wewe kuwa mkuu wetu, na mwamuzi juu yetu? Je! Wataka kuniua mimi kama ulivyomwua yule Mmisri? Musa akaogopa, akasema, Kumbe! Jambo lile limejulikana. Basi Farao alipopata habari, akataka kumwua Musa; lakini Musa akakimbia mbele ya Farao, akakaa katika nchi ya Midiani" Kutoka 2:11-15**

Bwana akaongoza njia yake, naye akapata makao kwa Yethro, mtu aliyemwabudu Mungu. Alikuwa mchungaji, pia kuhani wa Midiani. Binti zake walichunga mifugo yake. Lakini mifugo ya Yethro

ikakabidhiwa chini ya uangalizi wa Musa, ambaye alimwoa binti ya Yethro na kukaa Midiani miaka arobaini. **{SRSw 109.2}**

Musa alifanya haraka mno katika kumuua Mmisri. Alifikiri kwamba watu wa Israeli walielewa kwamba usimamizi maalum wa Mungu ulikuwa umemwinua ili kuwakomboa. Lakini Mungu hakupanga kuwakomboa wana wa Israeli kwa vita, kama Musa alivyofikiri, bali kwa uweza Wake mkuu, ili utukufu umwendee Yeye peke yake. Mungu aliruhusu tendo la Musa katika kumuua Mmisri ili kuleta kusudi Lake. Alikuwa amemleta Musa katika familia ya kifalme ya Misri, ambako alikuwa amepata elimu kamili; Na bado hakuwa tayari kwa Mungu kumkabidhi kazi kubwa aliyomwinua ili kuitimiza. Musa hakuweza kuondoka mara moja katika Ikulu ya mfalme na anasa alizopewa kama mjukuu wa mfalme ili kutimiza kazi ya pekee ya Mungu. Ilimpasa awe na muda wa kupata uzoefu na kuelimishwa katika shule ya dhiki na umaskini na ufukara/uhitaji. Alipokuwa akiishi maisha ya upweke, Bwana alimtuma malaika Wake hasa kumfundisha kuhusu wakati ujao. Hapa alijifunza kikamilifu zaidi somo kuu la kujidhibiti na unyenyekevu. Alichunga mifugo ya Yethro, na alipokuwa akifanya kazi zake za unyenyekevu kama mchungaji, Mungu alikuwa akimtayarisha kuwa mchungaji wa kiroho wa kondoo Wake, yaani watu Wake Israeli. **{SRSw 110.1}**

Musa alipoongoza kundi la watu jangwani, akafika kwenye mlima wa Mungu, hata Horebu; **Malaika wa Bwana akamtokea, katika mwali wa moto uliotoka katikati ya kijiti Kutoka 3:2 Bwana akasema, Hakika nimeyaona mateso ya watu Wangu walioko Misri, Nami nimekisikia kilio chao kwa sababu ya wasimamizi wao; maana nayajua maumivu yao; Nami nimeshuka ili niwaokoe na mikono ya Wamisri, niwapandishe kutoka nchi ile, hata nchi njema, kisha pana; nchi ijaayo maziwa na asali; hata mahali pa Mkanaani,**

na Mhiti, na Mwamori, na Mperizi, na Mhivi, na Myebusi. Basi, tazama, kilio cha wana wa Israeli kimenifikilia; tena nimeyaona hayo mateso ambayo Wamisri wanawatesa. Haya, basi, nitakutuma sasa kwa Farao, ili upate kuwatoa watu Wangu, hao wana wa Israeli, katika Misri. Kutoka 3:7-10 **{SRSw 110.2}**

Wakati ulikuwa umefika kabisa ambapo Mungu angemtaka Musa abadilishe fimbo ya mchungaji kuwa fimbo ya Mungu, ambayo angeifanya kuwa na nguvu katika kutimiza ishara na maajabu, katika kuwaokoa watu Wake dhidi ya ukandamizaji, na kuwahifadhi wanapofuatwa na adui zao. **{SRSw 111.1}**

Musa alikubali kutekeleza kazi hiyo. Kwanza alimtembelea baba mkwe wake na kupata kibali chake kwa ajili yake na familia yake kurudi Misri. Hakuthubutu kumwambia Yethro utume na ujumbe wake kwa Farao, asije akawa hataki kumwacha mke wake na watoto wake wamsindikize kwenye kazi hiyo hatari. Bwana akamtia nguvu na kuondoa hofu yake kwa kumwambia, **Haya, nenda, karudi Misri; kwa kuwa wale watu wote waliokutaka uhai wako wamekwisha kufa. Kutoka 4:19** **{SRSw 111.2}**

SURA YA 15—NGUVU ZA MUNGU ZILIZOFUNULIWA

Sura hii imejengwa katika Kutoka 5:1-12:28.

Kwa miaka mingi wana wa Israeli walikuwa katika utumwa kwa Wamisri. Ni familia chache tu zilizoshuka hadi Misri, lakini zilikuwa zimekua umati mkubwa wa watu. na kuzungukwa na ibada ya sanamu,

wengi wao walikuwa wamepoteza maarifa ya Mungu ya Kweli na walikuwa wamesahau sheria Yake. Nao wakaungana na Wamisri katika ibada yao ya jua, mwezi, na nyota, na wanyama na sanamu, kazi ya mikono ya wanadamu. **{SRSw 112.1}**

Kila kitu kilichowazunguka wana wa Israeli kilikuwa kimepangwa ili kuwafanya wamsahau Mungu aliye hai. Hata hivyo kulikuwa na wale kati ya Waebrania waliohifadhi maarifa ya Mungu ya Kweli, Muumba wa mbingu na nchi. Walihuzunika kuona watoto wao wakishuhudia haya kila siku, na hata kujihusisha na machukizo ya watu waabudu sanamu waliowazunguka, na kusujudu kwa miungu ya Kimisri, iliyotengenezwa kwa mbao na mawe, na kutoa dhabihu kwa vitu hivi visivyo na maana. Waumini walihuzunika, na katika dhiki zao walimlilia Bwana kwa ajili ya kukombolewa kutoka kwa nira ya Misri, ili awatoe Misri, ambapo wangeondolewa kwenye ibada ya sanamu na ushawishi wa ufisadi uliowazunguka. **{SRSw 112.2}**

Lakini wengi wa Waebrania waliridhika kubaki katika utumwa badala ya kwenda katika nchi mpya na kukabiliana na matatizo yaliyohusiana na safari hiyo. Kwa hiyo Bwana hakuwakomboa kwa udhihirisho wa kwanza wa ishara na maajabu yake mbele ya Farao. Alitumia matukio ili kuendeleza kikamilifu roho ya kidhalimu ya Farao, na ili apate kudhihirisha uwezo Wake mkuu kwa Wamisri, na pia mbele ya watu Wake, ili kuwafanya wawe na tashwishwi ya kuondoka Misri na kuchagua huduma ya Mungu. **{SRSw 112.3}**

Ingawa wengi wa Waisraeli walikuwa wamepotoshwa na ibada ya sanamu, lakini wale waliomwamini walisimama imara. Hawakuwa wameficha imani yao, bali waliikiri waziwazi mbele ya Wamisri kwamba walimtumikia Mungu wa pekee wa kweli na Aliye hai. Waliendelea kueleza uthibitisho wa kuwepo kwa Mungu na nguvu kutoka uumbaji hadi wakati ujao. Wamisri walipata fursa ya

kufahamiana na imani ya Waebrania na Mungu wao. Walikuwa wamejaribu kuwapotosha waabudu waaminifu wa Mungu wa kweli, na walikasirishwa kwa sababu hawakufaulu, ama kwa vitisho, ahadi ya thawabu, au kwa kutendewa kikatili. **{SRSw 113.1}**

Wafalme wawili wa mwisho waliokuwa wamekalia kiti cha enzi cha Misri walikuwa wadhalimu na walikuwa waliwatendea Waebrania kwa ukatili. Wazee wa Israeli walijitahidi kuimarisha imani iliyokuwa ikidhoofishwa ya Waisraeli, kwa kurejelea ahadi iliyotolewa kwa Ibrahimu, na Maneno ya unabii ya Yusufu kabla tu ya kufa kwake, yakitabiri kukombolewa kwao kutoka Misri. Wengine walisikiliza na kuamini. Wengine waliangalia hali yao ya kusikitisha, na hawakutaka kuwa na tumaini. **{SRSw 113.2}**

Israeli Waliathiriwa na Mazingira Yao

Wamisri walikuwa wamejifunza matarajio ya wana wa Israeli na kudhihaki matumaini yao ya ukombozi na kusema kwa kuwatupia dharau juu ya uwezo wa Mungu wao. Waliwaelekeza kwenye hali yao wenyewe kama watu, kama taifa la watumwa tu, na kuwaambia kwa dhihaka, Ikiwa Mungu wako ni mwenye haki na mwenye rehema, na ana uwezo juu ya miungu ya Misri, kwa nini Yeye Bwana hawafanyi ninyi kuwa watu huru? Kwa nini asidhihirishe ukuu na uwezo Wake, na kukuinua? **{SRSw 113.3}**

Kisha Wamisri wakawaelekeza Waisraeli kwa watu wao wenyewe, ambao waliabudu miungu ya chaguo lao wenyewe, ambayo Waisraeli waliita miungu ya uwongo. Walisema kwa furaha kwamba miungu yao imewafanikisha, na kuwapa chakula na mavazi na utajiri mwingi, na kwamba miungu yao pia ilikuwa imewapa Waisraeli mikononi mwao ili kuwatumikia, na kwamba walikuwa na uwezo wa kuwakandamiza na kuharibu maisha yao, ili wasiwe watu -(wa kipekee, au taifa).

Walidhihaki wazo la kwamba Waebrania wangekombolewa dhidi ya utumwa. **{SRSw 114.1}**

Farao alijigamba kwamba angependa kuona Mungu wao akiwakomboa kutoka mikononi mwake. Maneno haya yaliharibu matumaini ya wengi wa wana wa Israeli. Ilionekana kwao kabisa kama ukweli, yale mfalme na washauri wake waliyosema. Walijua kwamba walitendewa kama watumwa, na kwamba lazima wavumilie kiwango hicho cha ukandamizaji ambao wasimamizi wao wa kazi na watawala wangeweza kuweka juu yao. Watoto wao wa kiume walikuwa wanawindwa na kuuawa. Maisha yao wenyewe yalikuwa mzigo, na walikuwa wakimwamini, na kumwabudu, Mungu wa Mbinguni. **{SRSw 114.2}**

Kisha wakalinganisha hali yao na ile ya Wamisri. Hawakuamini hata kidogo katika Mungu Aliye hai ambaye alikuwa na uwezo wa kuokoa au kuharibu. Baadhi yao waliabudu sanamu, sanamu za mbao na mawe, huku wengine wakichagua kuabudu jua, mwezi, na nyota; Hata hivyo walikuwa wamefanikiwa na matajiri. Na baadhi ya Waebrania walifikiri kwamba ikiwa Mungu alikuwa juu ya miungu yote asingewaacha kama watumwa wa taifa la ibada ya sanamu. **{SRSw 114.3}**

Watumishi waaminifu wa Mungu walielewa kwamba ilikuwa ni kwa sababu ya kutokuwa waminifu kwao kwa Mungu kama watu, na tabia yao ya kuoana na mataifa mengine, na hivyo kuongozwa katika ibada ya sanamu, kwamba Bwana aliwaruhusu waingie Misri. Na wakatangaza kwa uthabiti kwa ndugu zao kwamba Mungu angewatoa hivi karibuni kutoka Misri na kuvunja nira yao ya kidhalimu. **{SRSw 114.4}**

Wakati ulikuwa umefika ambapo Mungu angejibu maombi ya watu Wake waliodhulumiwa, na kuwaleta kutoka Misri kwa maonyesho makubwa ya uwezo Wake kiasi kwamba Wamisri wangelazimishwa kukiri kwamba Mungu wa Waebrania, ambaye walikuwa wamemdharau, alikuwa juu ya miungu yote. Sasa angewaadhibu kwa ajili ya ibada yao ya sanamu na kwa kiburi chao cha kujivunia rehema walizopewa na miungu yao isiyo na maana. Mungu angelitukuza Jina Lake Mwenyewe, ili mataifa mengine yasikie juu ya uwezo Wake na kutetemeka kwa matendo Yake makuu, na kwamba watu Wake, kwa kushuhudia matendo Yake ya miujiza, wanapaswa kuachana kabisa na ibada yao ya sanamu ili kumpa ibada safi. **{SRSw 115.1}**

Katika ukombozi wa Israeli kutoka Misri, Mungu alionyesha wazi rehema Yake ya pekee kwa watu Wake mbele ya Wamisri wote. Mungu aliona inafaa kutekeleza hukumu Zake juu ya Farao, ili apate kujua kwa uzoefu wa kusikitisha, kwa kuwa asingesadikishwa vinginevyo, kwamba uwezo Wake ulikuwa bora kuliko wengine wote. Ili Jina Lake liweze kutangazwa duniani kote, angetoa uthibitisho wa mfano na wa maonyesho kwa mataifa yote ya uwezo Wake wa Kiungu na haki. Ilikuwa ni mpango wa Mungu kwamba maonyesho haya ya nguvu yanapaswa kuimarisha imani ya watu Wake, na kwamba vizazi vyao vimuabudu kwa uthabiti Yeye peke yake ambaye alikuwa amefanya maajabu hayo ya rehema kwa niaba yao. **{SRSw 115.2}**

Musa alitangaza kwa Farao, baada ya kuwataka watu kutengeneza matofali bila kupewa malighafi ya majani, kwamba Mungu, ambaye alijifanya hamjui, angemlazimisha kukubali madai Yake na kukiri mamlaka Yake kama Mtawala Mkuu. **{SRSw 115.3}**

Mapigo

Muujiza ya fimbo kuwa nyoka na mto kugeuzwa kuwa damu haukuugusa moyo mgumu wa Farao, bali uliongeza tu chuki yake kwa Waisraeli. Kazi ya waganga ilimfanya aamini kwamba miujiza hii ilifanywa kwa uchawi, lakini alikuwa na ushahidi mwingi kwamba hii haikuwa hivyo wakati pigo la vyura lilipoondolewa. Mungu angeweza kuwafanya Wamisri kutoweka na kurudi mavumbini kwa muda mfupi, lakini hakufanya hivi, isije, baada ya kuondolewa, mfalme na Wamisri wangesema kwamba ilikuwa ni matokeo ya uchawi, kama kazi ya wachawi. Walikufa, na kisha wakawakusanya pamoja katika lundo. Miili yao waliiona mbele yao, wakati ilipokuwa inaharibu anga (kwa harufu nk). Hapa mfalme na Misri yote walikuwa na ushahidi ambao falsafa yao ya bure haikuweza kupinga, kwamba kazi hii haikuwa uchawi bali hukumu kutoka kwa Mungu wa mbinguni. **{SRSw 116.1}**

Waganga hawakuweza kuzalisha chawa. Bwana asingewaruhusu kuifanya ionekane kwa macho yao wenyewe, au kwa Wamisri, kwamba wangeweza kutokeza tauni ya chawa. Angeondoa visingizio vyote vya kutokuamini kwa Farao. Aliwalazimisha hata waganga wenyewe kusema, ***Jambo hili ni chanda cha Mungu.*** **Kutoka 8:19 SRSw 116.2}**

Kisha likaja pigo la makundi ya nzi. Hawakuwa nzi wale wanaotusumbua bila madhara katika baadhi ya misimu ya mwaka, bali nzi walioletwa Misri walikuwa wakubwa na wenye sumu. Kuuma kwao kulimtia maumivu makali mwanadamu na mnyama. Mungu aliwatenganisha watu Wake na Wamisri na hakuruhusu nzi kuonekana katika pwani zao. **{SRSw 116.3}**

Kisha Bwana akatuma pigo la tauni nzito juu ya mifugo yao, na wakati huo huo akahifadhi mifugo ya Waebrania, kwamba hakuna hata mmoja wao aliyekufa. Kisha likaja pigo la jipu juu ya mwanadamu na mnyama, na waganga hawakuweza kujikinga nayo. Kisha Bwana akatuma juu ya Misri pigo la mvua ya mawe lililochanganyika na moto,

na umeme na radi. Wakati wa kila pigo ulitangazwa kabla halijaja, ili isisemwe kuwa ilitokea kwa bahati. Bwana alionyesha kwa Wamisri kwamba dunia yote ilikuwa chini ya amri ya Mungu wa Waebrania—kwamba ngurumo, mvua ya mawe, na dhoruba hutii sauti Yake. Farao, mfalme mwenye kiburi ambaye mara moja aliuliza, **Bwana ni nani, hata niisikilize sauti Yake?** alijinyenyekeza na kusema, **Mimi nimekosa wakati huu; Bwana ni Mwenye haki, na mimi na watu wangu tu waovu. Kutoka 9:27** Alimsihi Musa awe mwombezi wake kwa Mungu, ili ngurumo na umeme wa kutisha vikome. **{SRSw 117.1}**

Kisha Bwana alituma pigo la kutisha la nzige. Mfalme alichagua kupokea mapigo badala ya kujisalimisha kwa Mungu. Bila majuto aliona ufalme wake wote chini ya muujiza wa hukumu hizi za kutisha. Kisha Bwana akapeleka giza juu ya Misri. Watu hawakunyimwa nuru tu, bali angahewa ilikuwa ya kukandamiza sana, hivyo kwamba kupumua kulikuwa kugumu; Hata hivyo Waebrania walikuwa na anga safi na mwanga katika makao yao. **{SRSw 117.2}**

Pigo moja tena la kutisha zaidi ambalo Mungu alilileta juu ya Misri, kali zaidi kuliko yoyote kabla yake. Ilikuwa ni mfalme na makuhani waabudu sanamu waliopinga ombi la mwisho la Musa. Watu walitamani kwamba Waebrania waruhusiwe kuondoka Misri. Musa aliwaeleza Farao na watu wa Misri, pia kwa Waisraeli, asili na matokeo ya pigo la mwisho. Katika usiku ule, wa kutisha sana kwa Wamisri na wa utukufu sana kwa watu wa Mungu, ilikuwa ni agizo kuu la Pasaka lililoanzishwa. **{SRSw 117.3}**

Ilikuwa ngumu sana kwa mfalme wa Misri na watu wenye kiburi na waabudu sanamu kujisalimisha kwa matakwa ya Mungu wa Mbinguni. Polepole sana mfalme wa Misri alijinyenyekeza. Akiwa chini ya mateso makali, alikubali kidogo; Lakini mateso yalipoondolewa, alirudisha nyuma kila alichokubali. Kwa hiyo, pigo baada ya pigo

lililetwa juu ya Misri, na hakujitoa zaidi ya vile alivyolazimishwa na maonyesho ya kutisha kwa ghadhabu ya Mungu. Mfalme, hata alidumu katika uasi wake baada ya Misri kuharibiwa. **{SRSw 118.1}**

Musa na Haruni walimweleza Farao asili na matokeo ya kila pigo ambalo lingefuatabaada ya kukataa kwake kuwaacha Israeli waende zao. Kila alipoona mapigo haya yanakuja sawasawa na alivyoambiwa yatakuja; Hata hivyo hakukubali. Kwanza, aliwapa tu ruhusa ya kutoa dhabihu kwa Mungu katika nchi ya Misri; Kisha, baada ya Misri kuteseka kwa ghadhabu ya Mungu, alikubali kwamba wanaume peke yao waende. Baada ya Misri kuangamizwa karibu na pigo la nzige, basi alikubali kwamba watoto wao na wake zao waende pia, lakini hakuruhusu mifugo yao kwenda. Kisha Musa akamwambia mfalme kwamba malaika wa Mungu angemuua mzaliwa wao wa kwanza. **{SRSw 118.2}**

Kila pigo lilizidi kuwa karibu na kali zaidi, na hii ilikuwa ya kutisha zaidi kuliko yoyote kabla yake. Lakini mfalme mwenye kiburi alikasirika sana, na hakujinyenyekeza. Na Wamisri walipoona matayarisho makubwa yakifanywa kati ya Waisraeli kwa ajili ya usiku ule wa kutisha, walidhihaki ishara ya damu kwenye miimo yao ya milango. **{SRSw 118.3}**

SURA YA 16—KUONDOKA KWA ISRAELI UTUMWANI

Sura hii imejengwa katika Kutoka 12:29-15:19.

Wana wa Israeli walikuwa wamefuata maagizo waliyopewa na Mungu; Na wakati malaika wa mauti alipokuwa akipita nyumba kwa nyumba kati ya Wamisri, wote walikuwa tayari kwa safari yao, na kumngojea mfalme mwasi na watu wake wakuu wawaamuru waende zao. **{SRSw 119.1}**

Hata ikawa, usiku wa manane Bwana akawapiga wazaliwa wa kwanza wote katika nchi ya Misri, tangu mzaliwa wa kwanza wa Farao aliyeketi katika kiti chake cha enzi, hata mzaliwa wa kwanza wa mtu aliyefungwa katika nyumba ya wafungwa; na wazaliwa wa kwanza wote wa wanyama. Farao akaondoka usiku, yeye na watumishi wake wote, na Wamisri wote; pakawa na kilio kikuu katika Misri; maana hapakuwa na nyumba hata moja asimokufa mtu. Akawaita Musa na Haruni usiku, akasema, Ondokeni tokeni katika watu wangu, ninyi na wana wa Israeli; enendeni, kamtumikieni Bwana kama mlivyosema. Twaeni kondoo zenu na ng'ombe zenu kama mlivyosema, enendeni zenu, mkanibariki mimi pia. Wamisri nao wakawahimiza watu, kuwatoa katika nchi kwa haraka, maana walisema, Tumekwisha kufa sote. Kutoka 12:29-33 {SRSw 119.2}

“Watu wakauchukua unga wa mikate yao kabla haijatiwa chachu, na vyombo vyao vya kukandia wakavitia ndani ya nguo zao mabegani. Wana wa Israeli wakafanya kama neno lile la Musa; wakataka kwa Wamisri vyombo vya fedha na vyombo vya dhahabu, na mavazi. Bwana akawajalia kupendelewa na Wamisri hata wakawapa kila walichokitaka. Nao wakawateka Wamisri nyara.” Kutoka 12:34-36 {SRSw 119.3}

“Bwana alimfunulia Abrahamu hayo miaka mia nne hivi kabla ya kutimizwa; Bwana akamwambia Abramu, Ujue hakika ya kwamba uzao wako utakuwa mgeni katika nchi isiyo yake, watawatumikia watu wale, nao watateswa muda wa miaka mia nne. Hata na taifa lile, watakaowatumikia, nitawahukumu; baadaye watatoka na mali mengi.” Mwanzo 15:13-14 {SRSw 120.1}

“Na kundi kubwa la watu waliochangamana mno wakakwea pamoja nao; na kondoo na ng'ombe, wanyama wengi sana.” Kutoka 12:38 Wana wa Israeli walitoka Misri na mali zao, ambazo hazikuwa za Farao, kwa maana hawakuwahi kumuuzia. Yakobo na wanawe walichukua mifugo yao na ng’ombe pamoja nao mpaka Misri. Wana wa Israeli walikuwa wengi sana, na mifugo yao na ng'ombe walikuwa wameongezeka sana. Mungu alikuwa amewahukumu Wamisri kwa kuwapelekea mapigo juu yao, na kuwafanya waharakishe watu Wake kutoka Misri pamoja na vyote walivyokuwa navyo. {SRSw 120.2}

“Ilikuwa hapo Farao alipokwisha kuwaacha watu hao waende zao, Mungu hakuwaongoza kwa njia ya nchi ya Wafilisti, ijapokuwa ilikuwa ni ya karibu; maana Mungu alisema, Wasije wakaghairi watu hawa hapo watakapokutana na vita, na kurudi Misri; lakini Mungu akawazungusha hao watu kwa njia ya bara kando ya Bahari ya Shamu; wana wa Israeli wakakwea kutoka nchi ya Misri hali wamevaa silaha. Musa akaichukua ile mifupa ya Yusufu pamoja naye; maana, alikuwa amewaapisha sana wana wa Israeli, akisema, Mungu hana budi atawajilia ninyi; nanyi mtaichukua mfupa yangu kutoka hapa pamoja nanyi.” Kutoka 13:17-19 {SRSw 120.3}

Nguzo ya Moto

“Nao wakasafiri kutoka Sukothi, wakapiga kambi Ethamu, kwenye mpaka wa ile jangwa. Bwana Naye akawatangulia mchana

ndani ya wingu mfano wa nguzo, ili awaongoze njia; na usiku, ndani ya moto mfano wa nguzo, ili kuwapa nuru; wapate kusafiri mchana na usiku; ile nguzo ya wingu haikuondoka mchana, wala ile nguzo ya moto haikuondoka usiku, mbele ya hao watu." Kutoka 13:20-22 **{SRSw 121.1}**

Bwana alijua kwamba Wafilisti wangepinga kupita kwao katika nchi yao. Wangesema juu yao, kwamba wameiba kutoka kwa mabwana zao huko Misri, na wangefanya vita nao. Hivyo Mungu, kwa kuwaleta kwa njia ya bahari, alijidhihirisha kuwa Mungu Mwenye huruma na vilevile Mungu wa hukumu. Bwana akamjulisha Musa kwamba Farao angewafuata, naye akamwelekeza mahali pa kuweka kambi mbele ya bahari. Alimwambia Musa kwamba angeheshimiwa mbele ya Farao na jeshi lake lote. **{SRSw 121.2}**

Baada ya Waebrania kuondoka Misri siku kadhaa, Wamisri walimwambia Farao kwamba walikuwa wamekimbia na hawatarudi tena kumtumikia. Na wakaomboleza kwa sababu walikuwa wamewaruhusu kuondoka Misri. Ilikuwa ni hasara kubwa sana kwao kunyimwa huduma zao, na walijuta kwamba walikuwa wamekubali kuwaacha waende zao. Ijapokuwa yote waliyokuwa wameteseka kutokana na hukumu za Mungu, walikuwa wagumu sana kwa uasi wao wa mara kwa mara hivi kwamba waliamua kuwafuata wana wa Israeli na kuwarudisha kwa nguvu Misri. Mfalme alichukua jeshi kubwa sana na magari mia sita, akawafuatia, na kuwafikia wakiwa wamepiga kambi kando ya bahari. **{SRSw 121.3}**

"Hata Farao alipokaribia, wana wa Israeli wakainua macho yao, na tazama, Wamisri wanakuja nyuma yao; wakaogopa sana; wana wa Israeli wakamlilia Bwana. Wakamwambia Musa, Je! Kwa sababu hapakuwa na makaburi katika Misri umetutoa huko ili tufe jangwani? Mbona umetutendea haya, kututoa katika nchi ya Misri?

Neno hili silo tulilokuambia huko Misri, tukisema, Tuache tuwatumikie Wamisri? Maana ni afadhali kuwatumikia Wamisri kuliko kufa jangwani. Musa akawaambia watu, Msiogope, simameni tu, mkauone wokovu wa Bwana atakaowafanyia leo; kwa maana hao Wamisri mliowaona leo hamtawaona tena milele. Bwana atawapigania ninyi, nanyi mtanyamaza kimya." Kutoka 14:10-14 {SRSw 121.4}

Ni upesi kiasi gani Waisraeli hawakumwamini Mungu! Walikuwa wameshuhudia hukumu Zake zote juu ya Misri ili kumlazimisha mfalme kuwaacha Waisraeli waondoke, lakini imani yao katika Mungu ilipojaribiwa, walinung'unika, bila ya kujali walikuwa wameona uthibitisho kama huo wa uwezo Wake katika ukombozi wao wa ajabu. Badala ya kumtumaini Mungu katika shida yao, walimnung'unikia Musa mwaminifu, wakimkumbusha maneno yao ya kutokuamini ambayo walitamka huko Misri. Walimshtaki kuwa ndiye aliyesababisha dhiki yao yote. Aliwahamasisha kumtumaini Mungu na kuzuia maneno yao ya kutokuamini, na walipaswa kuona kile ambacho Bwana angewafanyia. Musa alimlilia Bwana kwa bidii ili kuwakomboa watu Wake wateule. **{SRSw 122.1}**

Ukombozi katika Bahari ya Shamu

Bwana akamwambia Musa, Mbona unanililia Mimi? Waambie wana wa Israeli waendelee mbele. Nawe inua fimbo yako, ukanyoshe mkono wako juu ya bahari, na kuigawanya; nao wana wa Israeli watapita kati ya bahari katika nchi kavu. ***Kutoka 14:15-16*** Mungu angemfanya Musa aelewe kwamba angefanya kazi kwa ajili ya watu wake—kwamba hitaji lao ingekuwa fursa Yake. Wanapopaswa kwenda mbali kama walivyoweza, lazima awabidishe bado wasonge mbele; Kwamba atumie fimbo ambayo Mungu alikuwa amempa kugawanya maji. **{SRSw 122.2}**

Nami, tazama, nitaifanya mioyo ya Wamisri kuwa migumu, nao wataingia na kuwafuatia, Nami nitajipatia utukufu kwa Farao, na kwa jeshi lake lote, kwa magari yake na kwa wapanda farasi wake. Na Wamisri watajua ya kuwa Mimi Ndimi Bwana, nitakapokwisha kujipatia utukufu kwa Farao, na magari yake, na farasi zake. Kisha Malaika wa Mungu, aliyetangulia mbele ya jeshi la Israeli, akaondoka akaenda nyuma yao; na ile nguzo ya wingu ikaondoka hapo mbele yao, ikasimama nyuma yao; ikafika kati ya jeshi la Misri na jeshi la Israeli; napo palikuwa na lile wingu na lile giza, lakini lilitoa nuru wakati wa usiku; na hawa hawakuwakaribia hawa usiku kucha. Kutoka 14:17-20 **{SRSw 123.1}**

Wamisri hawakuweza kuwaona Waebrania, kwa maana wingu la giza nene lilikuwa mbele yao, wingu ambalo lilikuwa taa/nuru kwa Waisraeli. Hivyo ndivyo Mungu alivyoonyesha uwezo Wake wa kuwathibitisha watu Wake, kama wangemtumaini baada ya kuwapa ishara kama hizo za utunzaji na upendo Wake kwao, na kukemea kutokuamini kwao na manung'uniko yao. Musa; ***akanyosha mkono wake juu ya bahari; Bwana akaifanya bahari irudi nyuma kwa upepo wa nguvu utokao mashariki, usiku kucha, akaifanya bahari kuwa nchi kavu, maji yakagawanyika. Wana wa Israeli wakaenda ndani kati ya bahari katika nchi kavu; nayo maji yalikuwa ukuta kwao mkono wa kuume, na mkono wa kushoto. Kutoka 14:21-22*** Maji yaliinuka na kusimama kama kuta zilizoganda, pande zote mbili wakati Israeli walipotembea katikati ya bahari kwenye ardhi kavu. **{SRSw 123.2}**

Jeshi la Misri lilikuwa llikishangilia usiku ule kwamba wana wa Israeli walikuwa tena katika uwezo wao. Walifikiri hakuna uwezekano wa Waisraeli kuokoka; Kwa maana mbele yao ilitanda Bahari ya Shamu, na majeshi yao makubwa yalikuwa karibu nyuma yao. Asubuhi, walipofika baharini, tazama, palikuwa na njia kavu, maji yaligawanyika,

na kusimama kama ukuta wa pande zote mbili, na wana wa Israeli walikuwa katikati ya bahari, wakitembea juu ya nchi kavu. Walingoja kwa muda kuamua ni njia gani wangechukua. Walikatishwa tamaa na kukasirika kwa vile Waebrania walikuwa karibu ya uwezo wao kuwadhuru, na walikuwa na uhakika nao, ila njia isiyotarajiwa ilifunguliwa kwa ajili yao baharini. Waliamua kuwafuata. **{SRSw 124.1}**

Na wale Wamisri wakawafuatia, wakaingia ndani kati ya bahari, farasi zote za Farao, na magari yake, na wapanda farasi wake. Ikawa katika zamu ya alfajiri, Bwana akalichungulia jeshi la Wamisri katika ile nguzo ya moto na ya wingu, akalifadhaisha jeshi la Wamisri. Akayaondoa magurudumu ya magari yao, hata yakaenda kwa uzito; na Wamisri wakasema, Na tukimbie mbele ya Israeli; kwa kuwa Bwana anawapigania, kinyume cha Wamisri. Kutoka 14:23-25 **{SRSw 124.2}**

Wamisri walithubutu kujitosa katika njia ambayo Mungu alikuwa amewaandalia watu Wake, na malaika wa Mungu walipita Katikati ya jeshi lao na kuhamisha magurudumu ya magari yao. Walipatwa na taabu. Mwendo wao ulikuwa wa polepole sana, na walianza kuwa na shida. Walikumbuka hukumu ambazo Mungu wa Waebrania alikuwa amewaletea huko Misri ili kuwalazimisha kuwaachia Israeli waende zao, na walifikiri kwamba Mungu angewaweka wote mikononi mwa Waisraeli. Waliamua kwamba Mungu alikuwa akiwapigania Waisraeli, na waliogopa sana na walikuwa wakigeuka kuwakimbia, wakati ***"Bwana alipomwambia Musa, Nyosha mkono wako juu ya bahari, ili maji yarudi tena juu ya Wamisri, juu ya magari yao, na juu ya farasi zao."*** **Kutoka 14:26** **{SRSw 124.3}**

Musa akaunyosha mkono wake juu ya bahari, na kulipopambazuka, bahari ikarudi kwa nguvu zake; Wamisri wakakimbia mbele yake; na Bwana akawakukutia mbali hao Wamisri

kati ya bahari. Yale maji yakarudi yakafunikiza magari na wapanda farasi, hata jeshi lote la Farao lililoingia katika bahari nyuma yao; hakusalia hata mtu mmoja. Lakini wana wa Israeli wakaenda katika nchi kavu katikati ya bahari; na hayo maji yalikuwa ni kuta upande wao wa kuume, na upande wao wa kushoto. Ndivyo Bwana alivyowaokoa Israeli siku ile mikononi mwa Wamisri; Waisraeli wakawaona Wamisri ufuoni kwa bahari, wamekufa. Israeli akaiona ile kazi kubwa aliyoifanya Bwana juu ya Wamisri, ndipo hao watu wakamcha Bwana, wakamwamini Bwana, na Musa mtumishi Wake. Kutoka 14:27-31 **{SRSw 125.1}**

Waebrania waliposhuhudia kazi ya ajabu ya Mungu katika kuwaangamiza Wamisri, waliungana katika wimbo uliovuviwa, wenye ufasaha wa hali ya juu na sifa za shukrani. **{SRSw 125.2}**

SURA YA 17—SAFARI ZA ISRAELI

Sura hii iimejengwa katika Kutoka 15:23-18:27.

Wana wa Israeli walisafiri jjangwani na kwa siku tatu hawakuweza kupata maji mazuri ya kunywa. walikuwa wanateseka na kiu, ***Ndipo watu wakamnung'unikia Musa, wakisema, Tunywe nini? Naye akamlilia Bwana; Bwana akamwonyesha mti, naye akautia katika hayo maji, maji yakawa matamu. Basi akawawekea amri na hukumu huko, akawaonja huko; akawaambia, Kwamba utaisikiza kwa bidii sauti ya Bwana, Mungu wako, na kuyafanya yaliyoelekea mbele Zake, na kutega masikio usikie maagizo yake, na kuzishika amri Zake, mimi sitatia juu yako maradhi yoyote niliyowatia Wamisri; kwa kuwa Mimi ndimi Bwana nikuponyaye. Kutoka 15:24-27*** **{SRSw 126.1}**

Wana wa Israeli walionekana kuwa na moyo mbaya wa kutokuamini. Hawakuwa tayari kuvumilia magumu jangwani. Walipokutana na matatizo katika njia hiyo, waliyaona kuwa ni mambo yasiyowezekana kutatulika. Imani yao kwa Mungu ilidhoofika, na hawakuweza kuona chochote mbele yao ila kifo. ***Na mkutano mzima wa wana wa Israeli ukawanung'unikia Musa na Haruni, huko barani; wana wa Israeli wakawaambia, Laiti tungalikufa kwa mkono wa Bwana katika nchi ya Misri, hapo tulipoketi karibu na zile sufuria za nyama, tulipokula vyakula hata kushiba; kwani mmetutoa huko na kututia katika bara hii, ili kutuua kwa njaa kusanyiko hili lote. Kutoka 16:2-3*** **{SRSw 126.2}**

Kwa kweli hawakuwa wameteseka na uchungu wa njaa. Walikuwa na chakula cha wakati huo, lakini waliogopa kukosa riziki katika siku zijazo. Hawakuweza kuona jinsi jeshi la Israeli lilivyopaswa kujikimu, katika safari zao ndefu jangwani, juu ya chakula rahisi walichokipata wakati huo, na katika kutokuamini kwao, waliona watoto wao wakiwa

na njaa. Bwana alikuwa tayari kwamba wapungukiwe katika chakula chao, na kwamba wakabiliane na matatizo, ili mioyo yao imgeukie Yeye ambaye hadi sasa alikuwa amewasaidia, ili wapate kumwamini. Alikuwa tayari kuwa msaada wa wakati huo kwao. Ikiwa, kwa uhitaji wao, wangemwita, angewadhihirishia ishara za upendo Wake na utunzaji wa daima. **{SRSw 127.1}**

Lakini walionekana kuwa hawataki kumwamini Bwana zaidi ya vile wangeweza kushuhudia mbele ya macho yao ushahidi wa kudumu wa uwezo Wake. Kama wangekuwa na imani ya kweli na imani thabiti kwa Mungu, usumbufu na vizuizi, au hata mateso ya kweli, yangebebwa kwa furaha, baada ya Bwana kufanya kwa namna hiyo ya ajabu kwa ajili ya ukombozi wao kutoka utumwani. Zaidi ya hayo, Bwana aliwaahidi kama wangetii amri Zake, hakuna ugonjwa ambao ungekaa juu yao, kwa maana alisema, ***Mimi Ndimi Bwana nikuponyaye*.** **Kutoka 15:26** **{SRSw 127.2}**

Baada ya ahadi hii ya hakika kutoka kwa Mungu, kule kutoamini kwao ilikuwa uhalifu ndani yao kutazamia kwamba wao na watoto wao wanaweza kufa kwa njaa. Walikuwa wameteseka sana huko Misri kwa kutozwa ushuru/suluba kupita kiasi katika kazi. Watoto wao walikuwa wameuawa, na katika kujibu maombi yao ya uchungu, Mungu alikuwa amewakomboa kwa rehema. Aliahidi kuwa Mungu wao, kuwachukua Kwake kama watu na kuwaongoza kwenye nchi kubwa na nzuri. **{SRSw 127.3}**

Lakini walikuwa tayari kuzimia kwa mateso yoyote ambayo walipaswa kuvumilia katika njia ya kuelekea nchi hiyo. Walikuwa wamevumilia mengi katika utumishi wa Wamisri, lakini sasa hawakuweza kuvumilia mateso katika utumishi wa Mungu. Walikuwa tayari kuacha mashaka ya huzuni na kuzama kwa kuvunjika moyo walipojaribiwa. Walinung'unika dhidi ya mtumishi aliyejitolea wa

Mungu Musa na kumshtaki kwa majaribu yao yote, na wakaonyesha tamaa mbaya ya kwamba wangebaki Misri, ambapo wangeweza kuketi karibu na vyungu vya nyama na kula mkate kwa wingi. **{SRSw 128.1}**

Somo kwa Siku Zetu

Kutokuamini na manung'uniko ya wana wa Israeli yanaonyesha watu wa Mungu sasa duniani. Wengi hutazama nyuma yao, na kustaajabia kutokuamini kwao na manung'uniko ya mara kwa mara, baada ya Bwana kuwafanyia mengi sana, kwa kuwapa ushahidi wa mara kwa mara wa upendo Wake na utunzaji Wake. Wanafikiri kwamba hawakupaswa kuthibitika kutokuwa na shukrani. Lakini wengine ambao hufikiria hivyo, kunung'unika na kukubaliana na mambo ambayo hayana matokeo. Hawajijui. Mungu huwathibitisha mara kwa mara, na hujaribu imani yao katika mambo madogo; na hawavumilii jaribu hilo kuliko Israeli wa kale. **{SRSw 128.2}**

Wengi wana mahitaji yao ya sasa; Hata hivyo hawatamtumaini Bwana kwa siku zijazo. Hudhihirisha kutokuamini na kuzama katika hali ya kudhoofika na huzuni kwa uhitaji unaotarajiwa siku za mbeleni. Wengine wanajiletea matatizo ya kudumu, wakiwawaza kwamba wasije wakaingia katika kupungukiwa riziki na kisha watoto wao wakateseka. Wakati matatizo yanapotokea au yanapoletwa katika maeneo magumu—wakati imani yao na upendo wao kwa Mungu unapojaribiwa—husinyaa na kujiepusha na majaribu na kunung’unika kwa mchakato ambao Mungu amechagua kuwatakasa. Upendo wao hauthibitishi kuwa safi na mkamilifu, kubeba vitu vyote. **{SRSw 128.3}**

Imani ya watu wa Mungu wa Mbinguni inapaswa kuwa na nguvu, hai, na ya kudumu—kiini cha mambo yanayotarajiwa. Ndipo lugha yao itakuwa itakuwa, ***Ee nafsi yangu, umhimidi Bwana. Naam, vyote vilivyo ndani yangu Vilihimidi Jina Lake takatifu. Zaburi 103:1 Naam,***

nimwimbie Bwana, Kwa kuwa amenitendea kwa ukarimu. Zaburi 13:6 **{SRSw 129.1}**

Kujinyima kunachukuliwa na wengine kuwa mateso ya kweli. Tamaa potovu huendekezwa. Na kujizuia juu ya matumbo yasiyofaa kungesababisha hata wengi wanaodai kuwa Wakristo sasa kuanza kurudi nyuma, kana kwamba njaa halisi ingekuwa matokeo ya mlo wa kawaida. Na, kama wana wa Israeli, wangependelea utumwa, miili yenye magonjwa, na hata kifo, badala ya kunyimwa vyungu vya nyama. Mkate na maji ni yote ambayo yameahidiwa kwa masalio wakati wa taabu. **{SRSw 129.2}**

Manna

"Na ulipoinuka ule umande uliokuwa juu ya nchi, kumbe! Juu ya uso wa bara kitu kidogo kilichoviringana, kidogo kama sakitu juu ya nchi. Wana wa Israeli walipokiona, wakaambiana, Nini hiki? Maana hawakujua ni kitu gani. Musa akawaambia, Ndio mkate ambao Bwana amewapa ninyi, mle. Neno hili ndilo aliloagiza Bwana, Okoteni ninyi kitu hicho kila mtu kama ulaji wake ulivyo; kichwa pishi,kama hesabu ya watu wenu ilivyo; ndivyo mtakavyotwaa, kila mtu kwa ajili ya hao walioko hemani mwake." Kutoka 16:14-16 **{SRSw 129.3}**

"Wana wa Israeli wakafanya hivyo, wakaokota wengine zaidi, wengine kupungua. Nao walipoipima kwa pishi, yeye aliyekuwa ameokota kingi hakubakiwa na kitu, na yeye aliyekuwa ameokota kichache hakupungukiwa; wakaokota kila mtu kama ulaji wake ulivyokuwa. Musa akawaambia, Mtu awaye yote asikisaze hata asubuhi. Lakini hawakumsikiza Musa; wengine miongoni mwao wakakisaza hata asubuhi, nacho kikaingia mabuu na kutoa uvundo; Musa akawakasirikia sana. Basi wakaokota asubuhi baada ya asubuhi,

kila mtu kama ulaji wake ulivyokuwa; na hapo jua lilipokuwa ni kali, kikayeyuka." Kutoka 16:17-21 **{SRSw 129.4}**

"Basi ikawa siku ya sita wakaokota kile chakula sehemu maradufu, kila mtu pishi mbili; na wazee wote wa mkutano wakaenda na kumwambia Musa. Akawaambia, Ndilo Neno alilonena Bwana Kesho ni starehe takatifu, Sabato takatifu kwa Bwana; okeni mtakachooka, na kutokosa mtakachotokosa; na hicho kitakachowasalia jiwekeeni kilindwe hata asubuhi. Basi wakakiweka hata asubuhi, kama Musa alivyowaagiza; nacho hakikutoa uvundo wala kuingia mabuu. Musa akasema, Haya, kuleni hiki leo; kwa kuwa leo ni Sabato ya Bwana; leo hamtakiona nje barani. Siku sita mtaokota; lakini siku ya saba ni Sabato, siku hiyo hakitapatikana." Kutoka 16:22-26 **{SRSw 130.1}**

Bwana leo ni Mwenye kujali kwa kiwango kikubwa kuhusiana na Sabato Yake kama pale alipotoa maagizo maalum yaliyotangulia kwa wana wa Israeli. Aliwataka kuoka kile ambacho wangeoka, na kuchomeka (yaani, kuchemsha) kile ambacho wangekichoma, siku ya sita, kuwaandalia Sabato iliyobaki. **{SRSw 130.2}**

Mungu alidhihirisha utunzaji na upendo Wake mkuu kwa watu Wake katika kuwapelekea mkate kutoka mbinguni. **Mwanadamu akala chakula cha malaika. Zaburi 78:25**; yaani chakula walichopewa na malaika. Muujiza wa mara tatu wa mana—kiwango maradufu katika siku ya sita, na kutokuwepo kabisa siku ya saba, na kubaki kwake salama katika Sabato, na katika siku nyingine ingekuwa isiyofaa kutumika—ilikusudiwa kuwavutia, utakatifu wa Sabato. **{SRSw 130.3}**

Baada ya kupatiwa chakula kwa wingi, waliona aibu juu ya kutokuamini kwao na manung'uniko yao, na kuahidi kumtumaini Bwana

kwa ajili ya wakati ujao, lakini upesi walisahau ahadi yao na wakashindwa katika jaribio la kwanza la imani yao. **{SRSw 131.1}**

Maji Kutoka Kwenye Mwamba

Walisafiri kutoka jangwa la Sini, wakapiga kambi Refidimu, na hapakuwa na maji ya kunywa. ***Kwa hiyo hao watu wakateta na Musa, wakasema, Tupe maji tunywe. Musa akawaambia, Kwani kuteta na mimi? Mbona mnamjaribu Bwana? Watu wakawa na kiu huko; nao wakamnung'unikia Musa, wakasema, Mbona umetupandisha kutoka Misri, kutuua sisi na watoto wetu na wanyama wetu kwa kiu? Musa akamlilia Bwana, akisema, Niwatendee nini watu hawa? Bado kidogo nao watanipiga kwa mawe. Kutoka 17:2-4*** **{SRSw 131.2}**

"Bwana akamwambia Musa, Pita mbele ya watu, ukawachukue baadhi ya wazee wa Israeli pamoja nawe; na ile fimbo yako ambayo uliupiga mto kwayo, uitwae mkononi mwako, ukaende. Tazama, nitasimama mbele yako huko, juu ya lile jabali katika Horebu; nawe utalipiga jabali, na maji yatatoka, watu wapate kunywa. Musa akafanya hivyo mbele ya wazee wa Israeli. Akapaita mahali pale jina lake Masa, na Meriba; kwa sababu ya mateto ya wana wa Israeli, na kwa sababu walimjaribu Bwana, wakisema, Je! Bwana Yu kati yetu au sivyo" Kutoka 17:5-7 **{SRSw 131.3}**

Mungu aliwaelekeza wana wa Israeli kupiga kambi mahali pale, ambapo hapakuwa na maji, ili kuwathibitisha/kuwatahini, ili kuona kama wangemtazama katika dhiki zao, au kunung'unika kama walivyofanya hapo awali. Kwa kuzingatia yale ambayo Mungu alikuwa amewafanyia katika ukombozi wao wa ajabu, walipaswa kumwamini katika dhiki yao. Walipaswa kujua kwamba Yeye asingeruhusu waangamie kwa kiu, ambaye alikuwa ameahidi kujichukulia kama watu Wake. Lakini badala ya kumsihi Bwana kwa unyenyekevu awape

mahitaji yao, walinung'unika dhidi ya Musa, na kumtaka maji. **{SRSw 131.4}**

Mungu alikuwa akiendelea kudhihirisha uwezo Wake kwa namna ya ajabu mbele yao, ili kuwafanya waelewe kwamba faida zote walizopokea zilitoka Kwake; kwamba Yeye angeweza kuwapa, au kuwaondolea, kulingana na mapenzi Yake Mwenyewe. Wakati fulani walikuwa na hisia kamili ya hili, na walijinyenyekeza sana mbele za Bwana; Lakini walipokuwa na kiu au walipokuwa na njaa, walimshtaki Musa, kana kwamba wametoka Misri ili kumpendeza. Musa alihuzunishwa na manung'uniko yao ya kikatili. Aliuliza kwa Bwana nini anapaswa kufanya, kwa maana watu walikuwa tayari kumpiga mawe. Bwana akamwambia aende kuupiga mwamba kwa fimbo ya Mungu. Wingu la utukufu Wake lilipumzika moja kwa moja mbele ya Mwamba. ***Akapasua miamba jangwani; Akawanywesha maji mengi kama maji ya vilindi. Akatokeza na vijito gengeni, Akatelemsha maji kama mito. Zaburi 78:15-16*** **{SRSw 132.1}**

Musa aliupiga mwamba, lakini Kristo Ndiye aliyesimama karibu naye na kusababisha maji kutiririka kutoka kwenye mwamba huo. Watu walimjaribu Bwana katika kiu yao, wakasema, Ikiwa Mungu ametutoa hapo, kwa nini hatupi maji, pamoja na mkate. Kwamba kama angeonyesha uhalifu wa kutokuamini na kumfanya Musa aogope kwamba Mungu angewaadhibu kwa ajili ya manung'uniko yao mabaya. Bwana aliijaribu imani ya watu Wake, lakini hawakuvumilia jambo hili. Walinung'unika kwa ajili ya chakula na maji, na wakamlalamikia Musa. Kwa sababu ya kutokuamini kwao, Mungu aliwaruhusu adui zao kufanya vita nao, ili awadhihirishe watu Wake kwamba nguvu zao zinatoka wapi. **{SRSw 132.2}**

Kuokolewa Kutoka kwa Waamaleki

"Musa akamwambia Yoshua, Tuchagulie watu, ukatoke upigane na Waamaleki; kesho nitasimama juu ya kilele kile, na ile fimbo ya Mungu nitakuwa nayo mkononi mwangu. Basi Yoshua akafanya kama Musa alivyomwambia, akapigana na Amaleki; na Musa na Haruni na Huri wakapanda juu ya kile kilima. Ikawa, Musa alipouinua mkono wake, Israeli walishinda; na alipoushusha mkono wake, Amaleki walishinda. Lakini mikono ya Musa ilikuwa mizito; basi wakatwaa jiwe, wakaliweka chini yake akalikalia. Haruni na Huri wakaitegemeza mikono yake, mmoja upande huu na mmoja upande huu; mikono yake ikathibitika hata jua lilipokuchwa. "Kutoka 17:9-12 **{SRSw 133.1}**

Musa aliinua mikono yake kuelekea mbinguni, akiwa na fimbo ya Mungu katika mkono wake wa kuume, akiomba msaada kutoka kwa Mungu. Kisha Israeli wakashinda na kuwarudisha nyuma adui zao. Musa aliposhusha mikono yake, ilionekana kwamba Israeli walipoteza upesi kila walichopata, na walikuwa wakishindwa na adui zao. Musa tena aliinua mikono yake kuelekea mbinguni, na Israeli wakashinda, na adui akarudishwa nyuma. **{SRSw 133.2}**

Kitendo hiki cha Musa, akiinua mikono yake kuelekea kwa Mungu, kilikuwa ni kuwafundisha Israeli kwamba ikiwa wangemfanya Mungu kuwa tumaini lao na kushikilia nguvu Zake na kuinua kiti Chake cha enzi, Yeye angewapigania na kuwatiisha adui zao. Lakini ikiwa wangeacha kushikilia nguvu Zake na kutumaini uwezo wao wenyewe, wangekuwa dhaifu zaidi kuliko adui zao, ambao hawakuwa na ujuzi wa Mungu, na adui zao wangewashinda. Kisha "Yoshua akamshinda Amaleki na watu wake kwa makali ya upanga." **{SRSw 133.3}**

"BWANA akamwambia Musa, Andika habari hii katika kitabu iwe ukumbusho, kisha ihubiri masikioni mwa Yoshua; ya kuwa nitaufuta ukumbusho wa Amaleki kabisa, usiwe tena chini ya mbingu." Kutoka 17:14 **{SRSw 134.1}**

Ziara ya Yethro

Kabla ya Musa kuondoka Misri alikuwa amemrudisha mke wake na watoto, kwa baba mkwe wake. Na baada ya Yethro kusikia juu ya ukombozi wa ajabu wa Waisraeli kutoka Misri, alimtembelea Musa jangwani, na akamletea mke wake na watoto wake. "Musa akatoka kwenda kumlaki baba mkwe wake, akamsujudia, akambusu; wakaombana ustawi wao; wakaingia ndani ya hema. kwa ajili ya Israeli, na taabu zote zilizowajia njiani, na jinsi Bwana alivyowaokoa. **{SRSw 134.2}**

"Yethro alifurahi kwa ajili ya wema wote BWANA aliowatendea Israeli, kwa alivyo waokoa mikononi mwa Wamisri. Kisha Yethro akasema, Na ahimidiwe BWANA aliyewaokoa na mikono ya Wamisri, na mkono wa Farao; aliyewaokoa watu hao watoke mikononi mwa Wamisri. Sasa najua ya kuwa BWANA ni mkuu kuliko miungu yote; naam, katika jambo hilo walilowatenda kwa unyeti. Yethro mkwewe Musa akamletea Mungu sadaka ya kuteketezwa na dhabihu; na Haruni akaja, na wazee wote wa Israeli, wale chakula pamoja na mkwewe Musa mbele za Mungu." Kutoka 18:9-12 **{SRSw 134.3}**

Jicho la utambuzi la Yethro upesi liliona kwamba mizigo juu ya Musa ilikuwa kubwa sana, kwani watu walileta mambo yao yote ya shida kwake, na akawaagiza kuhusu sheria na sheria ya Mungu. Akamwambia Musa, ***Sikiza sasa neno langu, nitakupa shauri, na Mungu na awe pamoja nawe; uwe wewe kwa ajili ya watu mbele ya Mungu, nawe umletee Mungu maneno yao; nawe utawafundisha zile amri na sheria, nawe utawaonyesha njia ambayo inawapasa kuiendea,***

na kazi ambayo inawapasa kuifanya. Zaidi ya hayo utajipatia katika watu hawa watu walio na uwezo, wenye kumcha Mungu, watu wa kweli, wenye kuchukia mapato ya udhalimu; ukawaweka juu yao, wawe wakuu wa maelfu, na wakuu wa mia, na wakuu wa hamsini, na wakuu wa kumi; nao wawaamue watu hawa sikuzote; kisha, kila neno lililo kubwa watakuletea wewe, lakini kila neno dogo wataliamua wenyewe; basi kwako wewe mwenyewe utapata nafasi zaidi, nao watauchukua huo mzigo pamoja nawe. Kwamba utafanya jambo hili, na Mungu akikuagiza hivyo, basi utaweza kusimama wewe, na watu hawa wote nao watakwenda mahali pao kwa amani. **{SRSw 135.1}**

Basi Musa akasikiza neno la mkwewe, akayafanya yote aliyokuwa amemwambia. Musa akawachagua watu wenye uwezo katika Israeli yote, akawaweka wawe vichwa juu ya watu, wakuu wa maelfu, na wakuu wa mia, na wakuu wa hamsini, na wakuu wa kumi. Nao wakawaamua watu sikuzote; mashauri magumu wakamletea Musa, lakini kila neno dogo wakaliamua wenyewe. Kisha Musa akaagana na mkwewe; naye akaenda zake, mpaka nchi yake mwenyewe. Kutoka 18:19-27 **{SRSw 135.2}**

Musa hakuwa juu ya kufundishwa na baba mkwe wake. Mungu alikuwa amemwinua sana na kufanya maajabu kwa mkono wake. Hata hivyo Musa hakuwaza kwamba Mungu alikuwa amemchagua kuwafundisha wengine, na alikuwa ametimiza mambo ya ajabu kwa mkono Wake, na kwa hiyo hakuhitaji kufundishwa. Alisikiliza kwa furaha mapendekezo ya baba-mkwe wake, na akakubali mpango wake kama mpango wa busara. **{SRSw 136.1}**

SURA YA 18—SHERIA YA MUNGU

Sura hii imejengwa katika Kutoka 19 na 20.

Baada ya wana wa Israeli kuondoka Refidimu, walifika kwenye ***"jangwa la Sinai, wakatua katika lile jangwa; Israeli wakapiga kambi huko wakiukabili mlima. Musa akapanda kwa Mungu, na BWANA akamwita toka mlima ule, akisema, Utawaambia nyumba ya Yakobo, na kuwaarifu wana wa Israeli, Maneno haya; Mmeona jinsi nilivyowatendea Wamisri, na jinsi nilivyowachukua ninyi juu ya mbawa za tai, nikawaleta ninyi kwangu Mimi. Sasa basi ikiwa mtaitii sauti Yangu kweli kweli, na kulishika agano langu, hapo ndipo mtakapokuwa tunu kwangu kuliko makabila yote ya watu; maana dunia yote pia ni mali Yangu, nanyi mtakuwa Kwangu ufalme wa makuhani, na taifa takatifu. Hayo ndiyo Maneno utakayowaambia wana wa Israeli. Musa akaenda akawaita wazee wa watu, akawafunulia maneno hayo yote, BWANA aliyokuwa amemwagiza. Watu wote wakaitika pamoja wakisema, Hayo yote aliyoyasema BWANA tutayatenda. Naye Musa akamwambia BWANA Maneno ya hao watu. Kutoka 19:2-8*** **{SRSw 137.1}**

Hapa watu waliingia katika agano takatifu na Mungu na wakamkubali kuwa Mtawala wao; kwa jambo hilo wakawa watu wa pekee chini ya mamlaka Yake ya Kiungu. "**BWANA akamwambia Musa, Tazama, Mimi Naja kwako katika wingu zito ili watu hawa wasikie nitakaposema nawe, nao wapate kukuamini wewe nawe hata milele." Kutoka 19:9** Wakati Waebrania walipokutana na matatizo njiani, walikuwa na tabia ya kunung'unika dhidi ya Musa na Haruni na kuwashutumu kwamba walikuwa wamewaongoza kutoka Misri ili kuwaangamiza. Mungu alitaka kumheshimu Musa mbele yao ili wapate kuyaamini maagizo Yake na kujua kwamba alikuwa ameweka Roho Wake juu yake. **{SRSw 137.2}**

Matayarisho ya kumkaribia Mungu

Kisha Bwana akampa Musa maagizo ya wazi kuhusu kuwaandaa watu ili Mungu awakaribie, wapate kuisikia sheria Yake ikitamkwa, si kwa njia ya malaika, bali na Yeye Mwenyewe. ***"BWANA akamwambia Musa, Enenda kwa watu hawa, ukawatakase leo na kesho, wakazifue nguo zao, wawe tayari kwa siku ya tatu; maana siku ya tatu BWANA atashuka katika mlima wa Sinai machoni pa watu hawa wote." Kutoka 19:10-11*** **{SRSw 138.1}**

Watu walitakiwa kujiepusha na kazi na shughuli za kidunia, na kuwa na mawazo ya ibada na kujitoa kwa Mungu. Mungu aliwataka pia wafue mavazi yao. Yeye si tofauti leo kuliko alivyokuwa wakati huo. Yeye ni Mungu wa utaratibu, na anawataka watu Wake duniani sasa kudumisha tabia za usafi wa hali ya juu. Wale wanaomwabudu Mungu wakiwa na mavazi machafu na miili isiyo safi hawaji mbele Zake kwa namna inayokubalika. Yeye Hafurahishwi na kukosa kwao heshima kwa Yeye, wala hatakubali ibada ya waabudu wachafu, kwa sababu wanamdharau (wanamtukana) Muumba wao. Muumba wa mbingu na dunia aliona usafi kuwa wa maana sana hata akasema, ***wakazifue nguo zao.*** **{SRSw 138.2}**

"Nawe utawawekea mipaka watu hawa pande zote, ukisema, Jihadharini, msipande mlima huu, wala msiuguse, hata mapambizo yake; kila mtu atakayeugusa mlima huu, bila shaka atauawa. Mkono wa mtu awaye yote usimguse mtu huyo, ila hakika yake atapigwa kwa mawe, au kupigwa kwa mkuki; kwamba ni mnyama au kwamba ni mwanadamu, hataishi. Hapo panda itakapotoa sauti kwa kufuliza ndipo watakapoukaribia mlima." Kutoka 19:12-13 Amri hii ilikusudiwa kugusa akili za watu hawa waasi kwa heshima kubwa kwa Mungu, Mwanzilishi na mwenye mamlaka ya sheria zao. **{SRSw 138.3}**

Udhihirisho wa Mungu Katika Ukuu wa Kutisha

"Ikawa siku ya tatu, wakati wa asubuhi, palikuwa na ngurumo na umeme, na wingu zito juu ya mlima, na sauti ya baragumu iliyolia sana. Watu wote waliokuwa kituoni wakatetemeka." Kutoka 19:16 Jeshi la malaika waliokuwa wakiandamana **na** Ukuu wa Mungu liliwaita watu kwa sauti inayofanana na ile ya tarumbeta, ambayo ilizidi kuongezeka hadi dunia nzima ikatetemeka. **{SRSw 139.1}**

"Mlima wa Sinai wote pia ukatoa moshi, kwa sababu BWANA alishuka katika moto; na ule moshi wake ukapanda juu kama moshi wa tanuu, mlima wote ukatetemeka sana". Kutoka 19:18 Ukuu wa Mungu ulishuka katika wingu pamoja na msafara wa utukufu wa Malaika, ambao walionekana kama miali ya moto. **{SRSw 139.2}**

"Na hapo sauti ya baragumu ilipozidi kulia sana, Musa akanena, naye Mungu akamwitikia kwa sauti. BWANA akaushukia mlima, juu ya kilele cha mlima; BWANA akamwita Musa aende hata kilele cha mlima; Musa akapanda juu. Ndipo BWANA akamwambia Musa, Shuka chini, uwaonye watu wasije wakapasua njia waje kwa BWANA kutazama, kisha wengi miongoni mwao wakaangamia. Makuhani nao, wamkaribiao BWANA, na wajitakase, BWANA asije akawafurikia." Kutoka 19:19-22 **{SRSw 139.3}**

Hivyo Bwana, katika utukufu wa kutisha, alitamka sheria Yake kutoka Sinai, ili watu waamini. Kisha alifuatisha utoaji wa sheria Yake pamoja na maonyesho ya hali ya juu ya mamlaka Yake, ili wapate kujua kwamba Yeye Ndiye Mungu pekee wa kweli na aliye hai. Musa hakuruhusiwa kuingia ndani ya wingu la utukufu, bali alikaribia tu na kuingia katika giza nene lililolizunguka. Naye akasimama kati ya watu na Bwana. **{SRSw 140.1}**

Sheria ya Mungu Yatangazwa

Baada ya Bwana kuwapa ushahidi kama huo wa uwezo Wake, aliwaambia Yeye ni nani: ***Mimi ni BWANA, Mungu wako, niliyekutoa katika nchi ya Misri, katika nyumba ya utumwa. Kutoka 20:2*** Mungu huyo huyo alitukuza nguvu Zake kati ya Wamisri sasa alitamka sheria Yake; **{SRSw 140.2}**

Kutoka 20:3-17

3 *Usiwe na miungu mingine ila mimi.* **{SRSw 140.3}**

4 *Usijifanyie sanamu ya kuchonga, wala mfano wa kitu cho chote kilicho juu mbinguni, wala kilicho chini duniani, wala kilicho majini chini ya dunia.*

5 Usivisujudie wala kuvitumikia; kwa kuwa mimi, BWANA, Mungu wako, ni Mungu Mwenye wivu; nawapatiliza wana maovu ya baba zao, hata kizazi cha tatu na cha nne cha wanichukiao,

6 nami nawarehemu maelfu elfu wanipendao, na kuzishika amri Zangu. **{SRSw 140.4}**

7 Usilitaje bure jina la BWANA, Mungu wako, maana BWANA hatamhesabia kuwa hana hatia mtu alitajaye Jina Lake bure. **{SRSw 140.5}**

8 *Ikumbuke siku ya Sabato uitakase.*

9 Siku sita fanya kazi, utende mambo yako yote;

10 lakini siku ya saba ni Sabato ya BWANA, Mungu wako, siku hiyo usifanye kazi yo yote, wewe, wala mwana wako, wala binti yako, wala mtumwa wako, wala mjakazi wako, wala mnyama wako wa kufuga, wala mgeni aliye ndani ya malango yako.

11 Maana, kwa siku sita BWANA alifanya mbingu, na nchi, na bahari, na vyote vilivyomo, akastarehe siku ya saba; kwa hiyo BWANA akaibarikia siku ya Sabato akaitakasa. **{SRSw 140.6}**

12 *Waheshimu baba yako na mama yako; siku zako zipate kuwa nyingi katika nchi upewayo na BWANA, Mungu wako*. **{SRSw 141.1}**

13 *Usiue*. **{SRSw 141.2}**

14 *Usizini*. **{SRSw 141.3}**

15 *Usiibe*. **{SRSw 141.4}**

16 *Usimshuhudie jirani yako uongo*. **{SRSw 141.5}**

17 *Usiitamani nyumba ya jirani yako, usimtamani mke wa jirani yako; wala mtumwa wake, wala mjakazi wake, wala ng'ombe wake, wala punda wake, wala cho chote alicho nacho jirani yako*. **{SRSw 141.6}**

Amri ya kwanza na ya pili zilizonenwa na Yehova ni kanuni dhidi ya ibada ya sanamu; Kwa maana ibada ya sanamu, ikiwa itafanywa, itawaongoza watu mbali sana katika dhambi na uasi, na kusababisha kutolewa kwa dhabihu za kibinadamu. Mungu alitaka kulinda dhidi ya njia ndogo zaidi ya machukizo kama hayo. Amri nne za kwanza zilitolewa ili kuwaonyesha wanadamu wajibu wao kwa Mungu. Ya nne ni kiungo cha kuunganisha kati ya Mungu mkuu na mwanadamu. Sabato, hasa, ilitolewa kwa manufaa ya mwanadamu na kwa heshima ya Mungu. Amri sita za mwisho zinaonyesha wajibu wa mwanadamu kwa wanadamu wenzake. **{SRSw 141.7}**

Sabato ilipaswa kuwa ishara kati ya Mungu na watu Wake milele. Kwa namna hiyo ilikuwa ishara—wote ambao wangeishika Sabato walionyesha kwa kuishika kwamba walikuwa waabudu wa Mungu aliye hai, Muumba wa mbingu na nchi. Sabato ilipaswa kuwa ishara kati ya

Mungu na watu Wake kwa muda wote ambao angekuwa na watu duniani wa kumtumikia. **{SRSw 141.8}**

"Watu wote wakaona umeme na ngurumo na sauti ya baragumu, na ule mlima kutoka moshi; na watu walipoona hayo wakatetemeka, wakasimama mbali. Wakamwambia Musa, Sema nasi wewe, nasi tutasikia, bali Mungu asiseme nasi, tusije tukafa. Musa akawaambia watu, Msiogope, maana Mungu amekuja ili awajaribu, na utisho Wake uwe mbele yenu, ili kwamba msifanye dhambi." Kutoka 20:18-20 **{SRSw 142.1}**

"Basi hao watu wakasimama mbali, naye Musa akalikaribia lile giza kuu Mungu alipokuwapo. BWANA akamwambia Musa, Waambie wana wa Israeli hivi, Ninyi wenyewe mmeona ya kuwa nimenena nanyi kutoka mbinguni. Kutoka 20:21-22. Uwepo wa utukufu wa Mungu katika Sinai, pamoja na mitikisiko ya nchi iliyosababishwa na uwepo Wake, ngurumo za kutisha na miale ya umeme iliyoandamana na kutembelewa huku kwa Mungu, vilizigusa sana akili za watu kwa hofu na kicho kwa ukuu Wake mtakatifu. Kwa hiyo kwa kawaida walirudi nyuma kutoka mbele za uwepo huo wa kutisha wa Mungu, wakihofia kwamba wasingeweza kustahimili utukufu Wake mkuu. **{SRSw 142.2}**

Hatari ya ibada ya sanamu

Tena, Mungu angewalinda wana wa Israel kutokana na ibada ya sanamu. Akawaambia, Msifanye miungu mingine pamoja Nami; miungu ya fedha, wala miungu ya dhahabu, msijifanyie. Kutoka 20:23 Walikuwa katika hatari ya kuiga mfano wa Wamisri, na kujitengenezea sanamu za kumwakilisha Mungu. **{SRSw 142.3}**

Bwana akamwambia Musa, Tazama, Mimi namtuma Malaika aende mbele yako, ili akulinde njiani na kukupeleka mpaka mahali pale nilipokutengezea. ***Jitunzeni mbele Yake, mwisikize sauti yake; wala msimtie kasirani; maana,***

hatawasamehe makosa yenu; kwa kuwa Jina Langu limo ndani Yake. Lakini ukiisikiza sauti Yake kweli, na kuyatenda yote ninenayo Mimi; ndipo mimi nitakuwa ni adui wa adui zako, na mtesi wa hao wakutesao. Kwa kuwa Malaika Wangu atatangulia mbele yako, na kukufikisha kwenye Mwamori, na Mhiti, na Mperizi, na Mkanaani, na Mhivi, na Myebusi; nami nitawakatilia mbali. Kutoka 23:20-23. Malaika aliyetangulia Israeli alikuwa Bwana Yesu Kristo. ***Usiisujudie miungu yao, wala kuitumikia; wala usitende mfano wa matendo yao; bali utaiangamiza kabisa, na nguzo zao utazivunja vipande vipande. Nanyi mtamtumikia BWANA, Mungu wenu, Naye atakibarikia chakula chako, na maji yako; Nami nitakuondolea ugonjwa kati yako. Kutoka 23:24-25*** **{SRSw 142.4}**

Mungu aliwataka watu Wake waelewe kwamba Yeye pekee Ndiye anayepaswa kuwa kitu cha kuabudiwa; Na watakapoyashinda mataifa ya waabudu sanamu waliowazunguka, hawakupaswa kuhifadhi sanamu zozote za ibada zao, bali walipaswa kuziharibu kabisa. Miungu mingi ya kipagani ilikuwa ya thamani kubwa na ilitengenezwa kwa ustadi na uzuri mkubwa, jambo ambalo lingeweza kuwajaribu wale waliokuwa wamezoea kuona ibada za sanamu zilizokuwa za kawaida sana nchini Misri, hata kuziheshimu kwa kiwango fulani sanamu hizo zisizo na uhai wala akili. Bwana alitaka watu Wake wajue kwamba ilikuwa ni kwa sababu ya ibada ya sanamu ya mataifa hayo, ambayo yalikuwa yamewaongoza katika kila aina ya uovu, ndipo angewatumia Waisraeli kama vyombo Vyake vya kuwaadhibu na kuiharibu miungu yao. **{SRSw 143.1}**

Nitatuma utisho wangu utangulie mbele yako, nami nitawafadhaisha watu wote utakaowafikilia, nami nitawafanya hao adui zako wote wakuonyeshe maungo yao. Nami nitapeleka mavu mbele yako, watakaomfukuza Mhivi, na Mkanaani, na Mhiti, watoke

mbele yako. Sitawafukuza mbele yako katika mwaka mmoja; nchi isiwe ukiwa, na wanyama wa bara wakaongezeka kukusumbua. Nitawafukuza kidogo kidogo mbele yako, hata utakapoongezeka wewe, na kuirithi hiyo nchi. Nami nitakuwekea mpaka wako tangu Bahari ya Shamu hata bahari ya Wafilisti, tena tangu jangwani hata huo Mto; kwa kuwa nitawatia wenyeji wa nchi mkononi mwako; nawe utawafukuza mbele yako. Usifanye maagano pamoja nao, wala pamoja na miungu yao. Wasikae katika nchi yako, wasije wakakufanya kunitendea Mimi dhambi; kwa sababu ukiitumikia miungu yao, jambo hili halikosi litakuwa ni tanzi kwako. Kutoka 23:27-33 Ahadi hizi za Mungu kwa watu Wake zilikuwa katika sharti la utii wao. Ikiwa wangemtumikia Bwana kikamilifu, angewafanyia mambo makuu. **{SRSw 143.2}**

Baada ya Musa kupokea hukumu kutoka kwa Bwana, na kuziandika kwa ajili ya watu, pia ahadi, kwa sharti la utii, Bwana akamwambia. ***Kweeni wewe, na Haruni, na Nadabu, na Abihu, na watu sabini wa wazee wa Israeli, mkamfikilie BWANA; mkasujudie kwa mbali; na Musa peke yake ndiye atakayekaribia karibu na BWANA; lakini hao hawatakaribia karibu; wala hao watu hawatakwea pamoja naye. Musa akaenda akawaambia watu Maneno yote ya BWANA, na hukumu zake zote; watu wote wakajibu kwa sauti moja, wakasema, Maneno yote aliyoyanena BWANA tutayatenda. Kutoka 24:1-3*** **{SRSw 144.1}**

Musa alikuwa ameandika, si zile Amri Kumi, bali hukumu ambazo Mungu angetaka wazizingatie, na ahadi kwa sharti kwamba wangemtii. Alisoma hizi kwa watu, na wakajifunga kwa ahadi kutii Maneno yote ambayo Bwana alikuwa amesema. Kisha Musa akaandika ahadi yao nzito katika kitabu na kutoa dhabihu kwa Mungu kwa ajili ya watu. ***Kisha akakitwaa kitabu cha agano akakisoma masikioni mwa watu;***

wakasema, Hayo yote aliyoyanena BWANA tutayatenda, nasi tutatii. Musa akaitwaa ile damu, akawanyunyizia watu, akasema, Hii ndiyo damu ya agano alilolifanya BWANA pamoja nanyi katika Maneno haya yote. Kutoka 24:7-8 Watu walirudia ahadi yao adhimu/nzito kwa Bwana kufanya yote aliyosema, na kuwa watiifu. **{SRSw 144.2}**

Sheria ya milele ya Mungu

Sheria ya Mungu ilikuwepo kabla ya mwanadamu kuumbwa. Malaika walitawaliwa nayo. Shetani alianguka kwa sababu alikiuka kanuni za serikali ya Mungu. Baada ya Adamu na Hawa kuumbwa, Mungu aliwajulisha sheria Yake. Wakati huo haikuandikwa, bali ilirudiwa kwao na Yehova. **{SRSw 145.1}**

Sabato ya Amri ya Nne ilianzishwa katika Edeni. Baada ya Mungu kuumba ulimwengu na kumuumba mwanadamu juu ya dunia, aliifanya Sabato kwa ajili ya mwanadamu. Baada ya dhambi ya Adamu na kuanguka hakuna kitu kilichochukuliwa (kubadilishwa) kutoka kwa sheria ya Mungu. Kanuni za Amri Kumi zilikuwepo kabla ya anguko na zilifaa kwa hali ya viumbe watakatifu. Baada ya kuanguka kwa mwanadamu, kanuni za amri hizo hazikubadilishwa, lakini maagizo ya ziada yalitolewa ili kukidhi hali ya mwanadamu aliyeanguka dhambini. **{SRSw 145.2}**

Kisha mfumo ulianzishwa unaohitaji dhabihu ya wanyama, ili kumkumbusha mwanadamu aliyeanguka jambo ambalo nyoka alimfanya Hawa asiliamini—kwamba adhabu ya kutotii ni kifo. Kuvunjwa kwa sheria ya Mungu kulifanya iwe lazima kwa Kristo kufa kama dhabihu, na hivyo kufungua njia ya mwanadamu kuokoka kutoka katika adhabu, huku heshima ya sheria ya Mungu ikidumishwa. Mfumo wa dhabihu ulikuwa wa kumfundisha mwanadamu unyenyekevu, kwa kuzingatia hali yake ya kuanguka, na kumwongoza katika toba na kumtumaini

Mungu pekee, kwa njia ya Mkombozi aliyeahidiwa, ili apate msamaha kwa makosa yake ya zamani dhidi ya sheria ya Mungu. Kama sheria ya Mungu isingevunjwa, kusingekuwa na kifo kamwe, na kusingekuwa na haja ya kanuni za ziada ili kukidhi hali ya mwanadamu aliyeanguka. **{SRSw 145.3}**

Adamu aliwafundisha watoto wake sheria ya Mungu, ambayo sheria ilikabidhiwa kwa waumini kupitia vizazi vilivyofuata. Uvunjaji wa daima wa sheria ya Mungu ulileta mafuriko ya maji juu ya dunia. Sheria hiyo ilihifadhiwa na Nuhu na familia yake, ambao kwa ajili ya kutenda haki waliokolewa katika safina kwa muujiza wa Mungu. Nuhu aliwafundisha watoto wake Amri Kumi. Bwana alihifadhi watu kwa ajili Yake Mwenyewe kutoka kwa Adamu kwenda chini, ambaye ndani yake kulikuwa na sheria Yake. Anasema juu ya Ibrahimu, yeye ***"alisikia sauti Yangu, akayahifadhi maagizo Yangu, na amri Zangu, na hukumu Zangu, na sheria Zangu." Mwanzo 26:5*** **{SRSw 145.1}**

Bwana akamtokea Ibrahimu, akamwambia; **{SRSw 145.2}**

Mimi ni Mungu Mwenyezi, uende mbele Yangu, ukawe mkamilifu. Nami nitafanya agano langu kati ya Mimi na wewe, Nami nitakuzidisha sana sana. Mwanzo 17:1-2 Agano Langu nitalifanya imara kati ya Mimi na wewe, na uzao wako baada yako, na vizazi vyao, kuwa agano la milele, kwamba nitakuwa Mungu kwako na kwa uzao wako baada yako. Mwanzo 17:7 **{SRSw 145.3}**

Kisha akamtaka Ibrahimu na uzao wake, tohara, ambayo ilikuwa ni mduara uliokatwa katika ngozi ya mwili, kama ishara kwamba Mungu alikuwa amewakata na kuwatenganisha na mataifa yote kama hazina Yake ya pekee. Kwa ishara hii waliweka ahadi ya dhati kwamba hawataoana na mataifa mengine, kwa kuwa kwa kufanya hivyo wangepoteza heshima yao kwa Mungu na sheria Yake takatifu, na

wangekuwa kama mataifa ya waabudu sanamu yaliyowazunguka **{SRSw 145.4}**

Kwa kitendo cha tohara walikubali kwa dhati kutimiza kwa upande wao, masharti ya agano yaliyofanywa na Ibrahimu, kuwa tofauti na mataifa yote na kuwa wakamilifu. Ikiwa wazao wa Ibrahimu wangejitenga na mataifa mengine, hawangeshawishiwa kuingia katika ibada ya sanamu. Kwa kujitenga na mataifa mengine, kishawishi kikubwa cha kushiriki katika mazoea yao ya dhambi na kumwasi Mungu kingeondolewa kutoka kwao. Walipoteza kwa kiasi kikubwa tabia yao ya kipekee, takatifu kwa kuchanganyika na mataifa yanayowazunguka. Ili kuwaadhibu, Bwana alileta njaa juu ya nchi yao, ambayo iliwalazimu kushuka hadi Misri kuhifadhi maisha yao. Lakini Mungu hakuwaacha walipokuwa Misri, kwa sababu ya agano Lake na Ibrahimu. Yeye aliruhusu wawe chini ya kongwa la Wamisri, ili wamgeukie katika dhiki yao, wachague serikali Yake ya haki na rehema, na kutii matakwa Yake. **{SRSw 146.1}**

Kulikuwa na familia chache tu ambazo zilishuka kwanza na kuishi Misri. Hizi ziliongezeka hadi umati mkubwa. Wengine walikuwa waangalifu kuwafundisha watoto wao katika sheria ya Mungu, lakini wengi wa Waisraeli walikuwa wameshuhudia ibada nyingi sana za sanamu kiasi kwamba walikuwa wamechanganya mawazo ya sheria ya Mungu. Wale waliomcha Mungu walimlilia kwa uchungu wa roho wavunje nira yao ya utumwa mzito na kuwatoa katika nchi ya utumwa wao, ili wawe huru kumtumikia. Mungu alisikia kilio chao na akamwinua Musa kama chombo Chake cha kutimiza ukombozi wa watu Wake. Baada ya wao kuondoka Misri, na maji ya Bahari ya Shamu kugawanywa mbele yao, Bwana aliwathibitisha kuona kama wangemtumaini Yeye aliyewachukua, taifa kutoka kwa taifa lingine, kwa ishara, majaribu, na maajabu. Lakini walishindwa kuvumilia jambo

hilo. Walinung'unika dhidi ya Mungu kwa sababu ya matatizo katika njia na walitaka kurudi tena Misri. **{SRSw 146.2}**

Ziliandikwa katika Mbao za Mawe

Ili wasiwe na udhuru, Bwana mwenyewe alijinyenyekeza na kushuka juu ya Sinai, akiwa amefunikwa na utukufu na kuzungukwa na malaika Zake, na kwa namna ya hali ya juu na ya kutisha alitangaza sheria Yake ya Amri Kumi. Hakuwaamini kufundishwa na mtu yeyote, hata na malaika Wake, bali alinena sheria Yake kwa sauti inayoonekana na kusikika na watu wote. Hata hivyo, bado hakuitegemea kumbukumbu ya watu wanaosahau kwa urahisi maagizo Yake, bali aliyaandika kwa kidole Chake kitakatifu juu ya mbao za mawe. Alitaka kuondoa uwezekano wote wa kuchanganya maagizo Yake na mapokeo ya wanadamu au kuchanganya matakwa Yake na desturi za watu. **{SRSw 148.1}**

Kisha akaja tena karibu na watu Wake, ambao walipotoshwa kwa urahisi, na hakutaka kuwaacha na maagizo kumi tu ya Amri Kumi. Alimwamuru Musa aandike, kama alivyopaswa kumwamuru, hukumu na sheria, akitoa maelekezo ya kinagaubaga kuhusiana na yale aliyotaka wayatekeleze, na hivyo kuzilinda zile Amri kumi alizokuwa amezichonga juu ya mbao za mawe. Maelekezo haya mahususi na matakwa yalitolewa ili kumvuta mwanadamu aliyekosea kwenye utii wa sheria ya maadili, ambayo yeye huwa na mwelekeo wa kuivunja. **{SRSw 148.2}**

Kama mwanadamu angeshika sheria ya Mungu, kama alivyopewa Adamu baada ya kuanguka kwake, iliyohifadhiwa katika safina na Nuhu, na kuzingatiwa na Ibrahimu, kusingekuwa na ulazima wa kuamuru tohara na kuichonga amri juu ya mbao za mawe na kuilinda kwa maelekezo ya uhakika katika maagizo na sheria za Musa. **{SRSw 148.3}**

Hukumu na Sheria

Musa aliandika hukumu hizi na sheria kutoka katika kinywa cha Mungu alipokuwa pamoja Naye katika Mlima. Ikiwa watu wa Mungu wangetii kanuni za Amri Kumi, kusingekuwa na haja ya maelekezo maalum aliyopewa Musa, ambayo aliandika katika kitabu, kuhusiana na wajibu wao kwa Mungu na kwa mtu mwingine. Maelekezo ya uhakika ambayo Bwana alimpa Musa kuhusiana na wajibu wa watu Wake wao kwa wao, na kwa mgeni, ni kanuni za Amri Kumi zilizorahisishwa na kutolewa kwa namna ya uhakika, ambavyo wasingehitaji kukosea. **{SRSw 149.1}**

Bwana alimwagiza Musa kwa hakika kuhusiana na dhabihu za sikukuu ambazo zilipaswa kukoma wakati wa kifo cha Kristo. Mfumo wa dhabihu uliwakilisha sadaka ya Kristo kama Mwana-Kondoo asiye na dosari. **{SRSw 149.2}**

Bwana alianzisha kwanza mfumo wa utoaji wa dhabihu na Adamu baada ya kuanguka kwake, ambayo aliwafundisha wazao wake. Mfumo huu ulipotoshwa kabla ya Gharika, na wale waliojitenga na wafuasi waaminifu wa Mungu na kushiriki katika ujenzi wa Mnara wa Babeli. Walitoa dhabihu kwa miungu ya [kutengeneza] yao wenyewe badala ya Mungu wa mbinguni. Walitoa dhabihu si kwa sababu walikuwa na imani katika Mkombozi ajaye, bali kwa sababu walifikiri kuifurahisha miungu yao kwa kutoa wanyama wengi juu ya madhabahu za sanamu zilizochafuliwa. Ushirikina wao uliwaongoza kwenye ubadhirifu mkubwa. Waliwafundisha watu kwamba kadiri dhabihu inavyokuwa yenye thamani zaidi ndivyo inavyoifurahisha zaidi miungu yao ya sanamu, na ndivyo ustawi na utajiri wa taifa lao ungekuwa mkubwa

zaidi. Kwa hiyo, wanadamu mara nyingi walitolewa dhabihu kwa sanamu hizi zisizo na maana. Mataifa hayo yalikuwa na sheria na kanuni za kudhibiti vitendo vya watu, ambavyo vilikuwa vya kikatili sana. Sheria zao zilitungwa na wale ambao mioyo yao haikulainika kwa neema; Na ingawa wangefanya uhalifu wa kudhalilisha zaidi na ukapuuzwa, kosa dogo lingetoa adhabu ya kikatili zaidi kutoka kwa wale walio na mamlaka. **{SRSw 149.2}**

Musa alikuwa na hayo katika mtazamo alipowaambia Israeli, ***Angalieni nimewafundisha amri na hukumu, vile vile kama BWANA, Mungu wangu, alivyoniamuru, ili mzitende katika nchi mwingiayo ili kuimiliki. Zishikeni basi, mkazitende, maana hii ndiyo hekima yenu na akili zenu, machoni pa mataifa watakaozisikia amri hizi zote, nao watasema, Hakika taifa hili kubwa ni watu wenye hekima na akili. Kwa maana liko taifa gani kubwa, lililo na Mungu aliye karibu nao, kama BWANA, Mungu wetu, alivyo, kila tumwitapo? Tena liko taifa gani kubwa, lililo na amri na hukumu zenye haki kama Torati hii yote, ninayoiweka mbele yenu leo. Kumbukumbu la Torati 4:5-8*** **{SRSw 150.1}**

SURA YA 19—PATAKATIFU

Sura hii imejengwa katika Kutoka 25 hadi 40.

Hema la kukutania ilitengenezwa kulingana na Amri ya Mungu. Bwana aliwainua wanadamu na kuwasitahilisha kwa uwezo uliozidi ule wa kawaida ili kufanya kazi ya werevu zaidi. Si Musa wala wafanyakazi hao walioachwa kupanga umbo na uundaji wa jengo hilo. Mungu Mwenyewe Ndiye aliyepanga mpango huo na kumpa Musa, kwa maelekezo maalum kuhusu ukubwa na umbo lake na vifaa vya kutumika, na akabainisha kila samani ambayo ilipaswa kuwa ndani yake. Aliwasilisha mbele ya Musa kielelezo kidogo cha Patakatifu pa mbinguni na kumwamuru afanye vitu vyote kulingana na muundo alioonyeshwa mlimani. Musa aliandika maagizo yote katika kitabu na kuwasomea watu wenye ushawishi mkubwa zaidi. **{SRSw 151.1}**

Ndipo Bwana akawataka watu walete sadaka ya hiari, wamfanyie Patakatifu, ili akae kati yao. "***Basi mkutano wote wa wana wa Israeli wakaondoka hapo mbele ya Musa. Wakaja kila mtu ambaye moyo wake ulimhimiza, na kila mtu ambaye roho yake ilimfanya kuwa apende, nao wakaleta sadaka za kumpa BWANA, kwa kazi ya hema ya kukutania, na kwa utumishi wake, na kwa hayo mavazi matakatifu. Nao wakaja, waume kwa wake, wote waliokuwa na moyo wa kupenda, wakaleta vipini, na hazama, na pete za muhuri, na vikuku, na vyombo vyote vya dhahabu; kila mtu aliyetoa toleo la dhahabu la kumpa BWANA. Kutoka 35:20-22*** **{SRSw 151.2}**

Maandalizi makubwa na ya gharama kubwa yalihitajika. Nyenzo za thamani na za gharama kubwa zilipaswa zikusanywe. Lakini Bwana

alikubali tu sadaka za hiari. Kujitolea kwa kazi ya Mungu na dhabihu kutoka moyoni kulihitajika kwanza katika kuandaa mahali kwa ajili ya Mungu. Na wakati jengo la Patakatifu lilipokuwa likiendelea, na watu walikuwa wakileta sadaka zao kwa Musa, na alikuwa akiwakabidhi watenda kazi, watu wote wenye hekima waliofanya kazi hiyo walichunguza vitu na kuamua kwamba watu walikuwa wameleta malighafi za kutosha, na hata zaidi, kwa kuvitumia. Musa akatangaza katika kambi yote, akisema, ***Wasifanye kazi tena, mtu mume wala mwanamke, kwa ajili ya matoleo kwa mahali Patakatifu. Basi watu wakazuiwa wasilete tena. Kutoka 36:6*** **{SRSw 152.1}**

Imerekodiwa kwa Vizazi vya Baadaye

Manung'uniko ya mara kwa mara ya Waisraeli, na kutembelewa na ghadhabu ya Mungu kwa sababu ya makosa yao, yameandikwa katika historia takatifu kwa manufaa ya watu wa Mungu ambao baadaye walipaswa kuishi juu ya dunia, lakini zaidi hasa kuthibitisha onyo kwa wale ambao wanapaswa kuishi nyakati za mwisho. Pia matendo yao ya kujitolea, nguvu zao na ukarimu wao katika kuleta matoleo yao ya hiari kwa Musa yameandikwa kwa manufaa ya watu wa Mungu. Mfano wao katika kuandaa nyenzo kwa ajili ya Hema la kukutania kwa furaha sana ni mfano kwa wote wanaopenda kweli-kweli ibada ya Mungu. Wale wanaothamini baraka za uwepo mtakatifu wa Mungu, wakati wa kuandaa jengo ili aweze kukutana nao, wanapaswa kudhihirisha shauku kubwa na bidii katika kazi takatifu kwa kadiri wanavyothamini baraka zao za mbinguni kuliko starehe zao za kidunia. Wanapaswa kutambua kwamba wanatayarisha nyumba kwa ajili ya Mungu. **{SRSw 152.2}**

Ni jambo lenye umuhimu fulani kwamba jengo linaloandaliwa mahsusi ili Mungu akutane na watu Wake, lipangwe kwa uangalifu—lifanywe liwe la kustarehesha, nadhifu, na linalofaa, kwa kuwa linapaswa kuwekwa wakfu kwa Mungu na kuwasilishwa Kwake, na

anapaswa kuombwa kukaa ndani ya nyumba hiyo na kuifanya kuwa takatifu kwa uwepo Wake mtakatifu. Inatosha kutoa kwa hiari kwa Bwana ili kukamilisha kazi hiyo kwa wingi, na kisha watenda kazi waweze kusema, msilete tena sadaka zaidi. **{SRSw 153.1}**

Kulingana na Kielelezo

Baada ya ujenzi wa Hema ya kukutania kukamilika, Musa aliichunguza kazi yote, na kuilinganisha na kielelezo, na maagizo aliyokuwa amepokea kutoka kwa Mungu, na akaona kwamba kila sehemu yake ilikubaliana na mfano huo; Naye akawabariki watu. **{SRSw 153.2}**

Mungu alimpa Musa mfano wa Sanduku la Agano, lenye maelekezo maalum ya jinsi ya kulitengeneza. Sanduku hilo lilitengenezwa ili kuhifadhi mbao za mawe ambazo Mungu aliziandika kwa kidole Chake, Amri Kumi. Lilikuwa kama Sanduku, na lilifunikwa na dhahabu safi ndani na nje. Lilipambwa kwa taji za dhahabu kuzunguka juu yake. Kifuniko cha Sanduku hilo takatifu kilikuwa Kiti cha Rehema, kilichotengenezwa kwa dhahabu safi. Katika kila mwisho wa kiti hicho kulikuwa na makerubi wa dhahabu safi. Nyuso zao zilielekezwa kwa kila mmoja, na walikuwa wakitazama kwa heshima kuelekea kiti cha rehema, kuwakilisha malaika wote wa mbinguni wanaotazama kwa shauku na heshima sheria ya Mungu iliyowekwa katika Sanduku la Agano katika Patakatifu pa mbinguni. Makerubi hawa walikuwa na mbawa. Bawa moja la kila malaika lilinyoshwa juu, huku bawa lingine la kila malaika likifunika mwili wake. Sanduku la Patakatifu pa duniani lilikuwa mfano wa Sanduku la kweli lililo mbinguni. Huko, karibu na sanduku la mbinguni, wanasimama malaika hai katika kila upande wa sanduku, kila mmoja akiwa na bawa moja likifunika kiti cha rehema na lingine likiwa limefunikwa mwili wake kwa unyenyekevu. **{SRSw 153.3}**

Katika sanduku la duniani Musa alipaswa kuweka mbao za mawe. Hizi ziliitwa mbao za ushuhuda; na sanduku likaitwa Sanduku la ushuhuda kwa sababu lilikuwa na ushuhuda wa Mungu katika Amri Kumi. **{SRSw 154.1}**

Vyumba Viwili

Hema yya kukutania ilikuwa na sehemu mbili zilizotenganishwa kwa pazia. Samani zote za Hema hiyo zilitengenezwa kwa dhahabu safi, au zilifunikwa kwa dhahabu. Mapazia ya hema ya kukutania yalikuwa ya rangi mbalimbali, yakiwa yamefumwa na kupangwa kwa uzuri mkubwa sana, na katika mapazia haya zilifumwa nyuzi za dhahabu na fedha, makerubi, ambao walipaswa kuwakilisha jeshi la malaika ambao wanahusiana na kazi ya Patakatifu pa mbinguni na ambao ni Malaika wanaohudumia watakatifu hapa duniani. **{SRSw 154.2}**

Ndani ya pazia la pili liliwekwa sanduku la ushuhuda, na pazia zuri na la thamani kubwa lilining'inizwa mbele ya sanduku hilo takatifu. Pazia hili halikufika hadi juu ya jengo. Utukufu wa Mungu, ambao ulikuwa juu ya kiti cha rehema, ungeweza kuonekana kutoka sehemu zote mbili, lakini kwa kiwango kidogo sana kutoka kutoka sehemu ya kwanza. **{SRSw 154.3}**

Moja kwa moja mbele ya Sanduku, lakini ikitenganishwa na pazia, palikuwa na Madhabahu ya Dhahabu ya uvumba. Moto juu ya madhabahu hii uliwashwa na Bwana Mwenyewe, na ulithaminiwa kwa utakatifu kwa kuongezewa uvumba mtakatifu, ambao ulijaza Patakatifu kwa wingu lake lenye harufu nzuri mchana na usiku. Harufu yake ilienea kwa umbali mkubwa kuzunguka Hema ya kukutania. **{SRSw 154.4}**

Kuhani alipotoa uvumba mbele za Bwana, alielekeza macho yake kwa kiti cha rehema. Ingawa hakuweza kukiona kwa macho, alijua kiko

pale; na uvumba ulipoinuka kama wingu, utukufu wa Bwana ulishuka juu ya kiti cha rehema na kujaza Patakatifu pa Patakatifu, na mara nyingi ulijaza vyumba vyote viwili kiasi kwamba kuhani hakuweza kuhudumu na alilazimika kusimama kwenye mlango wa Hema ya kukutania. Kuhani katika mahali Patakatifu, akielekeza maombi yake kwa imani kwenye kiti cha rehema, ambacho hakuweza kukiona, anawakilisha watu wa Mungu wakielekeza maombi yao kwa Kristo mbele ya Kiti cha Rehema katika Patakatifu pa mbinguni. Hawawezi kumtazama mpatanishi wao kwa jicho la kawaida, lakini kwa jicho la imani wanamwona Kristo mbele ya Kiti cha Rehema na kuelekeza maombi yao Kwake, na kwa uhakikisho wanadai sifa stahili za upatanishi Wake. **{SRSw 155.1}**

Vyumba hivi vitakatifu havikuwa na madirisha ya kupitisha mwanga. Kinara kilitengenezwa kwa dhahabu safi kabisa na kiliwekwa kuwaka usiku na mchana, na kilitoa mwanga kwa vyumba vyote viwili. Nuru ya taa juu ya kinara iliakisi juu ya mbao zilizofunikwa kwa dhahabu, kando ya jengo, na juu ya samani takatifu na juu ya mapazia ya rangi nzuri na makerubi Waliotengenezwa kwa nyuzi za dhahabu na fedha, ambazo zilionekana kuwa za utukufu zaidi ya maelezo. Hakuna lugha inayoweza kuelezea uzuri, utukufu na utakatifu ambao vyumba hivi viliwasilisha. Dhahabu katika Patakatifu iliakisi rangi za mapazia, ambayo yalionekana kama rangi tofauti za upinde wa mvua. **{SRSw 155.2}**

Mara moja tu kwa mwaka kuhani mkuu aliweza kuingia katika Patakatifu pa Patakatifu, baada ya maandalizi makini na mazito. Hakuna jicho la mwanadamu ila lile la kuhani mkuu lingeweza kutazama ukuu mtakatifu wa sehemu hiyo, kwa sababu palikuwa makao ya pekee ya utukufu unaoonekana wa Mungu. Kuhani mkuu sikuzote aliingia humo kwa kutetemeka, huku watu wakingoja kurudi kwake kwa ukimya mzito.

Maombi yao ya dhati yalikuwa yakimwendea Mungu kwa ajili ya baraka Yake. Mbele ya kiti cha rehema Mungu alizungumza na Kuhani Mkuu. Ikiwa angekaa kwa wakati usio wa kawaida katika Patakatifu pa Patakatifu, mara nyingi watu waliogopa, wakiogopa kwamba kwa sababu ya dhambi zao au dhambi fulani ya kuhani, utukufu wa Bwana ungeweza kumuua. Lakini wakati sauti ya mlio wa njuga kwenye mavazi yake iliposikika, walifarijika sana. Kisha alitoka nje na kuwabariki watu. **{SRSw 155.3}**

Baada ya kazi ya hema kumalizika, ***Ndipo lile wingu likaifunikiza hema ya kukutania, na huo utukufu wa BWANA ukaijaza maskani. Wala Musa hakuweza kuliingia hema la kukutania, kwa sababu lile wingu lilikaa juu yake, na huo utukufu wa BWANA ukaijaza maskani. Na hapo lile wingu lilipoinuliwa kutoka juu ya maskani, wana wa Israeli wakaenda mbele katika safari zao zote Kutoka 40:34-36*** **{SRSw 156.1}**

Hema ya kukutania ilijengwa kwa namna ambayo ingeweza kuvunjwa na kubebwa pamoja nao katika safari zao zote. **{SRSw 156.2}**

Wingu Linaloongoza

Bwana aliwaongoza Waisraeli katika safari zao zote jangwani. Ilipokuwa kwa manufaa ya watu na kwa utukufu wa Mungu kwamba waweke hema zao mahali fulani na wakae hapo, Mungu alionyesha mapenzi Yake kwao kwa nguzo ya wingu iliyotulia moja kwa moja juu ya hema ya kukutania. Na hapo ilibaki mpaka Mungu alipowataka wasafiri tena. Kisha wingu la utukufu likainuliwa juu zaidi ya hema ya kukutania, kisha wakasafiri tena. **{SRSw 156.3}**

Katika safari zao zote walifuata utaratibu kamili. Kila kabila lilikuwa na bendera yenye alama ya nyumba ya baba yao juu yake, na kila kabila liliamriwa kupiga kambi karibu na bendera yao wenyewe. Na

waliposafiri makabila mbalimbali yalitembea kwa utaratibu, kila kabila chini ya bendera yao wenyewe. Walipopumzika kutoka kwenye safari zao, Hema ya kukutania ilisimamishwa, na kisha makabila mbalimbali yakapiga hema zao kwa utaratibu, katika nafasi ile ile Mungu alioamuru kuizunguka hema ya kukutania kwa umbali fulani. **{SRSw 157.1}**

Watu waliposafiri, Sanduku la Agano lilichukuliwa mbele yao.

"Na wingu la BWANA lilikuwa juu yao mchana hapo waliposafiri kwenda mbele kutoka kambini. Ilikuwa, hapo Sanduku liliposafiri kwenda mbele, ndipo Musa akasema, Inuka, Ee BWANA, adui Zako na watawanyike; na wakimbie mbele Zako hao wakuchukiao. Tena hapo liliposimama, akasema, Ee BWANA, uwarudie maelfu kumi ya maelfu ya Israeli". Hesabu 10:34-36 **{SRSw 157.2}**

SURA YA 20—WAPELELEZI NA RIPOTI YAO

Sura hii imejengwa katika Hesabu 13, 14.

Bwana alimwamuru Musa atume watu kuipeleleza nchi ya Kanaani, ambayo angewapa wana wa Israeli. Kiongozi wa kila kabila alipaswa kuchaguliwa kwa kusudi hili. Wakaenda, na baada ya siku arobaini, wakarudi kutoka katika upelelezi wao, wakafika mbele ya Musa na Haruni na kusanyiko lote la Israeli, wakawaonyesha matunda ya nchi. Wote walikubali kwamba ilikuwa nchi nzuri, na walionyesha matunda mengi ambayo walikuwa wameleta kama ushahidi. Kishada kimoja cha zabibu kilikuwa kikubwa sana kiasi kwamba watu wawili walikibeba kati yao juu ya fimbo. Pia walileta tini na makomamanga, ambayo yalikua huko kwa wingi. **{SRSw 158.1}**

Baada ya kusema juu ya rutuba ya nchi, wote wapelelezi wawili, walizungumza kwa kukatisha tamaa sana juu ya uwezo wao wa kuimiliki. Walisema kwamba watu waliokuwa wakikaa katika nchi walikuwa na nguvu sana, na miji ilikuwa imezungukwa na kuta kubwa na za juu; Na, zaidi ya haya yote, waliona wana wa majitu Anaki huko. Kisha walieleza jinsi watu walivyokuwa karibu na Kanaani, na kutowezekana kwao kuwa na uwezo wa kuimiliki. **{SRSw 158.2}**

Watu waliposikiliza taarifa hii walionyesha kukatishwa tamaa kwao kwa lawama na maombolezo. Hawakungoja na kutafakari na kufikiria kwamba Mungu, ambaye alikuwa amewatoa huko mbali hadi sasa, bila shaka angewapa nchi. Lakini walikubali kukata tamaa mara moja. Walimwekea mipaka na hawakumtumaini Mungu, Yeye ambaye hadi sasa alikuwa amewaongoza. Walimkashifu Musa na kulalamika kwa manung'uniko, basi, huu ndio mwisho wa matumaini yetu yote. Hii ndiyo nchi ambayo tumekuwa tukisafiri kutoka Misri ili kuichukua. **{SRSw 158.3}**

Kalebu na Yoshua walitaka kusikilizwa, lakini watu walisisimka sana kiasi kwamba hawakuweza kujitawala nafsi zao ili kuwasikiliza watu hawa wawili. Baada ya kutulia kidogo, Kalebu alijitosa kuzungumza. Akawaambia watu, ***Na tupande mara, tukaitamalaki; maana twaweza kushinda bila shaka. Hesabu 13:30*** Lakini wale watu waliopanda pamoja naye wakasema, ***Hatuwezi kupanda tupigane na watu hawa; kwa maana wana nguvu kuliko sisi. Hesabu 13:31*** Nao wakaendelea kurudia taarifa yao mbaya, na wakasema kwamba watu wote walikuwa wa kimo kikubwa sana***. "Kisha, huko tuliwaona Wanefili, wana wa Anaki, waliotoka kwa hao Wanefili; tukajiona nafsi zetu kuwa kama mapanzi; nao ndivyo walivyotuona sisi". Hesabu 13:33*** **{SRSw 159.1}**

Israeli Yanung'unika Tena

Mkutano wote wakapaza sauti zao wakalia; watu wakatoka machozi usiku ule. Kisha wana wa Israeli wote wakamnung'unikia Musa na Haruni; mkutano wote wakawaambia, Ingekuwa heri kama tungalikufa katika nchi ya Misri, au, ingekuwa heri kama tungalikufa katika jangwa hili. Mbona BWANA anatuleta mpaka nchi hii ili tuanguke kwa upanga? Wake zetu na watoto wetu watakuwa mateka; je! Si afadhali turudi Misri? Wakaambiana, Na tumweke mtu mmoja awe akida, tukarudi Misri. Ndipo Musa na Haruni wakaanguka kifudifudi mbele ya mkutano wa kusanyiko la wana wa Israeli. Hesabu 14:1-5 **{SRSw 159.2}**

Waisraeli walitoa malalamiko yao dhidi ya Musa na kumtuhumu Mungu Mwenyewe kwa kuwafanyia hila kwa kuwaahidi nchi ambayo hawangeweza kuimiliki. Roho yao ya uasi ilifikia kiwango cha juu kiasi kwamba, wakisahau mkono wenye nguvu wa uweza wa Mungu ambao uliwatoa katika nchi ya Misri na hadi sasa ulikuwa ukiwapelekea kwa miujiza, waliamua kuchagua kiongozi atakayewaongoza kurudi Misri,

mahali walipokuwa watumwa na kuteseka kwa shida nyingi. Walimteua kiongozi kwa ajili yao, wakimfukuzilia mbali Musa, kiongozi wao mvumilivu na mwenye kuteseka; na walimung'unikia Mungu kwa uchungu mkubwa. **{SRSw 160.1}**

Musa na Haruni walijitupa kifudifudi mbele za Bwana mbele ya umati wote wa jamii, kuomba rehema za Mungu kwa ajili ya watu waasi. Lakini huzuni yao na maumivu yao yalikuwa makubwa mno kuweza kuyatamka. Walibakia kifudifudi katika hali ya ukimya kabisa. Kalebu na Yoshua walirarua mavazi yao kama ishara ya huzuni kubwa.

"Wakanena na mkutano wote wa wana wa Israeli wakasema, Nchi ile tuliyopita kati yake ili kuipeleleza, ni nchi njema mno ya ajabu. Ikiwa BWANA anatufurahia, atatuingiza katika nchi hii atupe iwe yetu, nayo ni nchi yenye wingi wa maziwa na asali. Lakini msimwasi BWANA, wala msiwaogope wale wenyeji wa nchi, maana wao ni chakula kwetu; uvuli uliokuwa juu yao umeondolewa, Naye BWANA yu pamoja nasi; msiwaogope." Hesabu 14:7-9 **{SRSw 160.2}**

"Uvuli uliokuwa juu yao umeondolewa "Yaani, Wakanaani walikuwa wamejaza kipimo cha uovu wao, na ulinzi wa Kiungu uliondolewa kutoka kwao, na walijiona salama kabisa na hawakuwa tayari kwa vita; na, kwa agano la Mungu, nchi imehakikishwa kuwa yetu. Badala ya maneno haya kuwa na athari iliyokusudiwa juu ya watu, waliongeza uasi wao uliodhamiriwa. Wakawa kwa hasira na kulia kwa kilio kikuu na cha hasira kwamba Kalebu na Yoshua wanapaswa kupigwa mawe, jambo ambalo lingefanywa kama Bwana asingeingilia kati kwa ishara kubwa ya utukufu Wake wa kutisha katika hema ya kukutania mbele ya wana wa Israeli wote. **{SRSw 160.3}**

Maombi ya Musa ya Ushindi

Musa aliingia ndani ya Hema ili kuzungumza na Mungu. “**BWANA akamwuliza Musa, Je! Watu hawa watanidharau hata lini? Wasiniamini hata lini? Nijapokuwa nimefanya ishara hizo zote kati yao. Nitawapiga kwa tauni, na kuwaondolea urithi wao, Nami nitakufanya wewe kuwa taifa kubwa, kisha yenye nguvu kuliko wao. Musa Awaombea Watu kwa Mungu. Basi Musa akamwambia BWANA, Ndipo Wamisri watasikia habari hiyo; kwa kuwa Wewe uliwaleta watu hawa kwa uweza wako, kutoka kati yao; kisha watawaambia wenyeji wa nchi hii; wamesikia wao ya kuwa wewe BWANA u kati ya watu hawa; maana, Wewe BWANA waonekana uso kwa uso, na wingu lako lasimama juu yao, kisha Wewe watangulia mbele yao, katika nguzo ya wingu mchana, na katika nguzo ya moto usiku. Basi kama Wewe ukiwaua watu hawa mfano wa mtu mmoja, ndipo mataifa yaliyosikia habari za sifa Zako watakaponena na kusema, Ni kwa sababu Yeye BWANA hakuweza kuwaleta watu hao kuwatia katika nchi aliyowaapia, kwa ajili ya hayo amewaua nyikani.” Hesabu 14:11-16** **{SRSw 161.1}**

Musa akakataa kabisa wazo la kuangamizwa kwa Israeli na yeye kufanywa taifa kubwa zaidi kuliko Israeli. Mtumishi huyu mpendwa wa Mungu anadhihirisha upendo wake kwa Israeli na kuonyesha shauku yake kwa utukufu wa Muumba wake na heshima ya watu Wake. Kama ulivyowasamehe watu hawa, tangu huko Misri hata sasa, Umekuwa mwenye subira na mwenye rehema hadi sasa kwa watu hawa wasio na shukrani; ingawa hawastahili, rehema Yako ni ile ile. Anamsihi, Je, hutawasamehe, basi, mara hii, na kuongeza mfano huu mmoja wa uvumilivu wa Kiungu kwa mingi ambayo tayari umewapa? **{SRSw 161.2}**

“BWANA akasema, Mimi nimewasamehe kama neno lako lilivyokuwa; lakini hakika Yangu, kama niishivyo, tena kama dunia

hii nzima itakavyojawa na utukufu wa BWANA; kwa sababu watu hawa wote, ambao wameuona utukufu Wangu na ishara Zangu, nilizozitenda huko Misri, na huko jangwani, pamoja na haya wamenijaribu mara hizi kumi, wala hawakuisikiza sauti Yangu; hakika yangu hawataiona hiyo nchi niliyowaapia baba zao, wala katika hao wote walionidharau hapana atakayeiona; lakini mtumishi Wangu Kalebu, kwa kuwa alikuwa na roho nyingine ndani yake, naye ameniandama kwa moyo wote, nitamleta yeye mpaka nchi hiyo aliyoingia; na uzao wake wataimiliki." Hesabu 14:20-24 {SRSw 162.1}

Kurudi Jangwani

Bwana aliwaambia Waebrania warudi na kuingia jangwani kwa njia ya Bahari ya Shamu. Walikuwa karibu sana na nchi nzuri, lakini, kwa uovu wa uasi wao, waliutelekeza ulinzi wa Mungu. Kama wangepokea taarifa ya Kalebu na Yoshua, na kuondoka mara moja, Mungu angeliwapa nchi ya Kanaani. Lakini walikuwa wasiokuwa na imani na walionyesha roho ya kiburi dhidi ya Mungu kiasi kwamba walijiletea laana wasiingie kamwe kuingia Nchi ya ahadi. Ilikuwa kwa huruma na rehema kwamba Mungu aliwatuma warudi kupitia Bahari ya Shamu, kwa maana walipokuwa wakichelewa na kunung'unika, Waamaleki na Wakanaani, walijua ni wapelelezi na walijitayarisha kuwapiga vita wana wa Israeli. {SRSw 162.2}

"Kisha BWANA akanena na Musa na Haruni, na kuwaambia, Je! Nichukuane na mkutano mwovu huu uninung'unikiao hata lini? Nimesikia manung'uniko ya wana wa Israeli, waninung'unikiayo." Hesabu 14:26-27 Bwana aliwaambia Musa na Haruni waambie watu kwamba atawafanyia kama walivyosema. Walikuwa wamesema, "Ingekuwa heri kama tungalikufa katika nchi ya Misri,

au, ingekuwa heri kama tungalikufa katika jangwa hili." Hesabu 14:2 **{SRSw 163.1}**

Sasa Mungu alisikiliza matakwa yao . Aliwaambia watumishi Wake waambie kwamba watakufa jangwani**,** kuanzia wenye miaka ishirini na kuendelea, kwa sababu ya uasi wao na kunung'unika dhidi ya Bwana. Ni Kalebu na Yoshua pekee ndiyo watakaokwenda katika nchi ya Kanaani. ***"Lakini Watoto wenu, ambao mlisema watakuwa mateka, ndio nitakaowaleta na kuwatia ndani, nao wataijua nchi mliyoikataa ninyi."*** **Hesabu 14:31** **{SRSw 163.1}**

Bwana alitangaza kwamba wana wa Waebrania wangezunguka jangwani kwa miaka arobaini, kuanzia wakati walipoondoka Misri, kwa sababu ya uasi wa wazazi wao, hadi wazazi wote watakapokufa. Hivyo ndivyo wangevumilia na kuchukuliana na mambo magumu na kuteseka kutokana na uovu wao kwa miaka arobaini, kulingana na idadi ya siku walizokuwa wakiipeleleza nchi, siku moja kwa kila mwaka. **"Nanyi mtakujua kufarikana Kwangu. Hesabu 14:34** Walipaswa kutambua kikamilifu kwamba ilikuwa ni adhabu kwa ajili ya ibada zao za sanamu na manung'uniko ya uasi ambayo yalimlazimisha Bwana kubadilisha kusudi Lake juu yao. Kalebu na Yoshua waliahidiwa thawabu badala ya jeshi lote la Israeli, kwasababu wale wa mwisho walikuwa wamepoteza madai yote ya kibali na ulinzi wa Mungu. **{SRSw 163.2}**

SURA YA 21—DHAMBI YA MUSA

Sura hii imejengwa katika Hesabu 20.

Tena kusanyiko la Israeli lililetwa jangwani, mahali pale ambapo Mungu aliwajaribu mara baada ya kuondoka Misri. Bwana aliwapa maji kutoka kwenye mwamba, ambayo yaliendelea kutiririka mpaka muda mfupi kabla hawajafika tena kwenye mwamba huo, ndipo Bwana akafanya ule mto wa maji uache kutiririka ili kuwajaribu watu Wake tena, ili kuona kama wataweza kuvumilia jaribu la imani yao au watanung'unika tena dhidi Yake**. {SRSw 164.1}**

Wakati Waebrania walipokuwa na kiu na hawakuweza kupata maji, walikosa subira na hawakukumbuka nguvu za Mungu ambazo, karibu miaka arobaini kabla, ambazo ziliwaletea maji kutoka kwenye mwamba. Badala ya kumtumaini Mungu, wakamlalamikia Musa na Haruni, wakawaambia; **Ingalikuwa heri kama tungalikufa wakati ule ndugu zetu walipokufa mbele za BWANA! Hesabu 20:3** Yaani, walitamani kuwa miongoni mwa wale waliokuwa wameangamizwa na pigo katika uasi wa Kora, Dathani, na Abiramu. **{SRSw 164.2}**

Waliuliza kwa hasira, **"Mbona mmewaleta kusanyiko la BWANA hata jangwa hili ili tufe huku, sisi na wanyama wetu? Na mbona mmetupandisha kutoka Misri ili kutuleta hata mahali hapa pabaya? Si mahali pa mbegu, wala tini, wala mizabibu, wala makomamanga; wala hapana maji ya kunywa." Hesabu 20:4-5 {SRSw 164.3}**

"Musa na Haruni wakatoka pale palipokuwa mkutano, wakaenda hata mlangoni pa hema ya kukutania, wakaanguka

kifudifudi; utukufu wa BWANA ukawatokea. BWANA akasema na Musa, akinena, Twaa ile fimbo, ukawakusanye mkutano, wewe na Haruni ndugu yako, ukauambie mwamba mbele ya macho yao utoe maji yake, nawe utawatokezea maji katika mwamba, na hivyo utawanywesha maji mkutano na wanyama wao. Musa akaitwaa hiyo fimbo kutoka mbele za BWANA kama alivyomwamuru." Hesabu 20:6-9 {SRSw 165.1}

Musa Akosa Uvumilivu

"Musa na Haruni wakawakusanya kusanyiko mbele ya mwamba, akawaambia, Sikieni sasa, enyi waasi; je! Tuwatokezee maji katika mwamba huu? Musa akainua mkono wake akaupiga ule mwamba kwa fimbo yake mara mbili; maji yakatoka mengi, mkutano wakanywa na wanyama wao pia. BWANA akamwambia Musa na Haruni, Kwa kuwa hamkuniamini mimi, ili kunistahi mbele ya macho ya wana wa Israeli, basi kwa sababu hiyo, hamtawaingiza kusanyiko hili katika ile nchi niliyowapa." Hesabu 20:10-12 {SRSw 165.2}

Hapa Musa alitenda dhambi. Alichoshwa na manung'uniko ya mara kwa mara ya watu dhidi yake, na kwa amri ya Bwana, akachukua fimbo, na, badala ya kuuambia mwamba, kama Mungu alivyomwamuru, aliupiga kwa fimbo mara mbili, baada ya kusema, **"je! Tuwatokezee maji katika mwamba huu?" Hesabu 20:10** Hapa alizungumza kwa midomo yake bila kufikiria. Hakusema, Mungu atawapa sasa ushahidi mwingine wa nguvu Zake na kuleta maji kutoka kwenye mwamba huu. Hakutaja nguvu na utukufu kwa Mungu kwa kufanya maji yatiririke tena kutoka kwenye mwamba wa gumegume, na kwa hiyo hakumtukuza mbele ya watu. Kwa kushindwa huku kwa upande wa Musa, Mungu asingemruhusu kuwaongoza watu kwenye Nchi ya Ahadi. **{SRSw 165.3}**

Umuhimu huu wa udhihirisho wa nguvu za Mungu ulifanya tukio hilo kuwa adhimu, na Musa na Haruni walipaswa kuliboresha ili mioyo ya watu iguswe.. Lakini Musa alichochewa, na kwa kukosa subira na hasira kwa watu, kwa sababu ya manung'uniko yao, alisema, **“Sikieni sasa, enyi waasi; je! Tuwatokezee maji katika mwamba huu?” Hesabu 20:10.** Kwa kusema hivyo alikiri kwa uhakika kwa kunung'unika kwa Israeli kwamba walikuwa sahihi katika kumshtaki kwa kuwaongoza kutoka Misri. Mungu alikuwa amewasamehe watu makosa makubwa zaidi kuliko kosa hili kwa upande wa Musa, lakini hakuweza kuiona dhambi katika kiongozi wa watu Wake kuwa sawa na wale walioongozwa. Yeye Hangeweza kuisamehe dhambi ya Musa na kumruhusu kuingia katika Nchi ya Ahadi. **{SRSw 166.1}**

Bwana hapa aliwapa watu Wake uthibitisho usio na shaka kwamba Yeye ambaye alikuwa amefanya ukombozi wa ajabu kwao katika kuwaleta kutoka katika utumwa wa Misri, alikuwa malaika mwenye nguvu, na si Musa, ambaye alikuwa akitangulia mbele yao katika safari zao zote, na ambaye alisema juu yake; **“Tazama, Mimi namtuma Malaika aende mbele yako, ili akulinde njiani na kukupeleka mpaka mahali pale nilipokutengezea. Jitunzeni mbele yake, mwisikize sauti Yake; wala msimtie kasirani; maana, hatawasamehe makosa yenu; kwa kuwa Jina Langu limo ndani Yake.” Kutoka 23:20-21 {SRSw 166.2}**

Musa alijichukulia utukufu ambao ulikuwa wa Mungu tu, na kufanya iwe muhimu kwa Mungu kumfanya afanye kile alichofanya kwa ajili yake ili kuondoa mashaka ya Israeli waasi, kwamba si Musa aliyewaongoza kutoka Misri, bali Mungu Mwenyewe. Bwana alikuwa amemkabidhi Musa mzigo wa kuwaongoza watu Wake, huku malaika mwenye nguvu akiwatangulia katika safari zao zote na kuelekeza safari zao zote. Kwa sababu walikuwa tayari sana kusahau kwamba Mungu

alikuwa akiwaongoza kwa Malaika Wake, na kumhusisha mwanadamu kile ambacho nguvu za Mungu pekee zingeweza kufanya, alikuwa amewathibitisha na kuwajaribu, ili kuona kama wangemtii. Katika kila jambo walishindwa. Badala ya kuamini, na kumkiri, Mungu, ambaye alikuwa ametawanya njia yao na ushahidi wa uwezo Wake na ishara ya utunzaji na upendo Wake, hawakumwamini na kuhusisha kuondoka kwao Misri kwa uwezo wa Musa, wakimshtaki kama sababu ya maafa yao yote. Musa alikuwa amevumilia ukaidi wao kwa ustahimilivu wa ajabu. Wakati fulani walitishia kumpiga mawe. **{SRSw 166.3}**

Adhabu nzito

Bwana angeondoa kabisa mtazamo huu kutoka akilini mwao, kwa kumkataza Musa kuingia katika nchi ya ahadi. Bwana alikuwa amemtukuza sana Musa. Alikuwa amemfunulia utukufu Wake mkuu. Alikuwa amemchukua katika ukaribu mtakatifu pamoja Naye juu ya mlima, na alikuwa amejishusha na kuzungumza naye kama mtu anavyozungumza na rafiki. Aliwasiliana na Musa, na kupitia kwake kwa watu, kuhusu mapenzi Yake, sheria Zake, na maagizo Yake. Kuinuliwa kwake na kupewa heshima na Mungu kulifanya kosa lake kuwa kubwa zaidi. Musa alitubu dhambi yake na kujinyenyekeza sana mbele za Mungu. Aliwasimulia Israeli wote huzuni yake kwa ajili ya dhambi yake. Matokeo ya dhambi yake hakuyaficha, bali aliwaambia kwamba kwa kushindwa hivyo kumtukuza Mungu, asingeweza kuwaongoza kwenye Nchi ya Ahadi. Kisha aliwauliza kwamba kama kosa lake lilikuwa kubwa kiasi hicho, hata likamfanya Mungu amwadhibu hivyo, je, Mungu angewahesabuje wao kwa kunung'unika kwao mara kwa mara na kumlaumu yeye (Musa) kwa mateso yao? **{SRSw 167.1}**

Kwa tukio hili moja, Musa aliruhusu mtazamo kuenezwa kwamba aliwatolea maji kutoka kwenye mwamba, wakati alipaswa kulitukuza Jina la Bwana kati ya watu Wake. Sasa Bwana aliliweka wazi jambo

hilo mbele za watu Wake, kwamba Musa alikuwa mtu tu, aliyepaswa kufuata ushauri na mwongozo wa mwenye nguvu kuliko yeye, yaani Mwana wa Mungu. Katika hili hakuwaacha na wasiwasi. Ambapo mengi yanatolewa, mengi yanahitajika. Musa alikuwa amejaliwa kwa upendeleo mkubwa kwa maono ya pekee ya ukuu wa Mungu. Nuru na utukufu wa Mungu ulikuwa umetolewa kwake kwa kiwango kikubwa. Uso wake ulikuwa umeakisi juu ya watu utukufu ambao Bwana aliruhusu umuangazie. Wote watahukumiwa kulingana na fursa waliyokuwa nayo, na nuru na manufaa yatakayotolewa. Dhambi za watu wema, ambao mwenendo wao kwa ujumla umestahili kuigwa, ni chukizo na dhihaka kwa Mungu. Wanamfanya Shetani ashinde, na kuwadhihaki malaika wa Mungu kwa mapungufu ya vyombo vilivyochaguliwa na Mungu, na kutoa nafasi isiyo ya haki ya adui kujiinua dhidi ya Mungu. **{SRSw 168.1}**

Bwana alikuwa amemwongoza Musa kwa namna ya pekee, na akamfunulia utukufu Wake, zaidi ya mwingine juu ya nchi. Kwa kawaida hakuwa na subira, lakini alikuwa ameshikilia kwa uthabiti neema ya Mungu na kwa unyenyekevu akaomba hekima kutoka mbinguni, hivi kwamba aliimarishwa kupitia Mungu na kushinda hali yake ya kutokuwa na subira kiasi kwamba aliitwa na Mungu mnyenyekevu/mpole zaidi juu ya uso wa dunia yote. **{SRSw 168.2}**

Haruni alikufa katika Mlima Hori, kwa kuwa Bwana alikuwa amesema kwamba hataingia katika Nchi ya Ahadi, kwa sababu, alikuwa amefanya dhambi pamoja na Musa wakati wa kutoa maji kutoka kwenye mwamba huko Meriba. Musa na wana wa Haruni walimzika mlimani, ili watu wasijaribiwe kufanya sherehe kubwa sana juu ya mwili wake, na kuwa na hatia ya dhambi ya ibada ya sanamu. **{SRSw 169.1}**

SURA YA 22—KIFO CHA MUSA

Sura hii imejengwa katika Kumbukumbu la Torati 31-34.

Musa alikuwa amekaribia kufa, naye akaamrishwa kuwakusanya wana wa Israeli pamoja kabla ya kifo chake na kuwasimulia safari zote za jeshi la Kiebrania tangu kuondoka kwao kutoka Misri, na makosa yote makubwa ya baba zao, ambayo yalileta hukumu Zake juu yao, na kumlazimisha kusema kwamba wasingeingia katika nchi ya ahadi. Baba zao walikuwa wamekufa jangwani, kulingana na Neno la Bwana. Watoto wao walikuwa wamekua, na kwao ahadi ilipaswa kutimizwa ya kumiliki nchi ya Kanaani. Wengi wa hawa walikuwa watoto wadogo wakati sheria ilipotolewa, na hawakuwa na kumbukumbu/ukumbusho wa ukuu wa tukio hilo. Wengine walizaliwa jangwani, na ili wasikose kutambua ulazima wa kutii Amri Kumi na sheria zote na hukumu alizopewa Musa, aliagizwa kutoka kwa Mungu kuzirudia tena zile Amri Kumi, na hali zote zinazohusiana na utoaji wa Sheria. **{SRSw 170.1}**

Musa alikuwa ameandika katika kitabu sheria, maagizo na hukumu zote alizopewa na Mungu, na alikuwa ameandika kwa uaminifu maagizo Yake yote waliyopewa njiani, na miujiza yote ambayo alikuwa amewafanyia na manung'uniko yote ya wana wa Israeli. Musa pia alikuwa ameandika kushindwa kwake kutokana na matokeo ya manung'uniko yao. **{SRSw 170.2}**

Maelekezo ya mwisho kwa Israeli

Watu wote walikusanyika mbele yake, na alisoma matukio ya historia yao ya zamani kutoka katika kitabu alichokuwa ameandika. Aliwasomea pia ahadi za Mungu kama wangekuwa watiifu, na laana ambazo zingewajia ikiwa wangekuwa waasi. **{SRSw 171.1}**

Musa aliwaambia kwamba, kwa ajili ya uasi wao, Bwana mara kadhaa alikuwa amekusudia kuwaangamiza, lakini alikuwa amewaombea kwa bidii sana hata Mungu alikuwa amewaacha kwa neema. Aliwakumbusha juu ya miujiza ambayo Bwana aliyoifanya mbele ya Farao na nchi yote ya Misri. Akawaambia, ***"lakini macho yenu yameiona kazi kubwa ya BWANA aliyoifanya, yote. Kwa hiyo yaangalieni maagizo yote niwaagizayo leo, mpate kuwa na nguvu, na kuingia mkaimiliki nchi mwivukiayo kuimiliki"*** **Kumbukumbu la Torati 11:7-8** **{SRSw 171.2}**

Musa hasa aliwaonya wana wa Israeli dhidi ya kushawishiwa katika ibada ya sanamu. Aliwaamuru kwa bidii kutii amri za Mungu. Ikiwa wangethibitisha na kumpenda Bwana na kumtumikia kwa upendo wao usiogawanyika, angewapa mvua kwa wakati wake na kuifanya mimea yao kustawi, na kuiongeza mifugo yao. Walipaswa pia kufurahia fursa maalum zilizotukuka, na walitakiwa kuwashinda maadui zao. **{SRSw 171.3}**

Musa aliwafundisha wana wa Israeli kwa njia ya dhati na bidii na yenye kuvutia. Alijua kwamba ilikuwa fursa yake ya mwisho kuwahutubia. Kisha akamaliza kuandika katika kitabu sheria, maagizo, hukumu, na sheria zote ambazo Mungu alikuwa amempa, pia kanuni mbalimbali zinazohusu sadaka za kafara. Alikiweka kitabu hicho mikononi mwa wanadamu katika ofisi takatifu na akaomba kwamba, kwa ajili ya ulinzi, kiwekwe kando ya Sanduku la Agano, kwa maana utunzaji wa Mungu ulikuwa daima juu ya Sanduku hilo kitakatifu. Kitabu hiki cha Musa kilipaswa kuhifadhiwa, ili waamuzi wa Israeli

warejelee ikiwa jambo lolote lingetokea lililo la muhimu. Watu wanaokosea mara nyingi huelewa matakwa ya Mungu ili kukidhi kesi au ladha zao wenyewe; Kwa hiyo kitabu cha Musa kilihifadhiwa mahali Patakatifu sana, kwa kumbukumbu ya wakati ujao. **{SRSw 171.4}**

Musa alifunga maagizo yake ya mwisho kwa watu kwa hotuba yenye nguvu zaidi ya kiunabii. Ilikuwa ya kusikitisha na fasaha. Kwa uvuvio wa Mungu alibariki kila moja ya makabila ya Israeli. Katika maneno yake ya mwisho alijikita kwa kiasi kikubwa juu ya ukuu wa Mungu na ushindi wa Israeli, ambao ungeendelea kama wangemtii Mungu na kushikilia nguvu Zake. **{SRSw 172.1}**

Kufariki na Kufufuka kwa Musa

"Musa akapanda kutoka uwanda wa Moabu mpaka mlima Nebo, hata kilele cha Pisga kukabili Yeriko. BWANA akamwonyesha nchi yote ya Gileadi hata Dani; na Naftali yote, na nchi ya Efraimu na Manase, na nchi yote ya Yuda, mpaka bahari ya magharibi; na Negebu, na uwanja wa bonde la Yeriko, mji wa mitende, hata mpaka Soari. BWANA akamwambia, Hii ndiyo nchi niliyowaapia Ibrahimu, na Isaka, na Yakobo, nikisema, Nitawapa wazao wako. Basi nimekuonyesha kwa macho yako, lakini hutavuka huko. Basi Musa, mtumishi wa BWANA, akafa huko, katika nchi ya Moabu, kwa neno la BWANA. Akamzika bondeni, katika nchi ya Moabu, kukabili Beth-peori; lakini hapana mtu ajuaye kaburi lake hata leo. Musa alikuwa mtu wa miaka mia na ishirini alipokufa; jicho lake halikupofuka, wala nguvu za mwili wake hazikupunguka." Kumbukumbu la Torati 34:1-7 **{SRSw 172.2}**

Haikuwa mapenzi ya Mungu kwamba mtu yeyote apande na Musa hadi juu ya Pisga. Alisimama pale, juu ya sehemu ya juu ya Pisga, mbele za Mungu na malaika wa mbinguni. Baada ya kuiona Kanaani na

kuridhika, alijilaza, kama shujaa aliyechoka, ili apumzike. Usingizi ulimjia, lakini ulikuwa ni usingizi wa kifo. Malaika waliuchukua mwili wake na kuuzika bondeni. Waisraeli hawakuweza kamwe kupata mahali alipozikwa. Mazishi yake ya siri yalikuwa ni njia ya kuwazuia watu wasitende dhambi dhidi ya Bwana kwa kufanya ibada ya sanamu juu ya mwili wake. **{SRSw 173.1}**

Shetani alifurahi kwamba alikuwa amefaulu kumfanya Musa atende dhambi dhidi ya Mungu. Kwa kosa hili Musa alikuja chini ya utawala wa kifo. Kama angeendelea kuwa mwaminifu, na maisha yake yasingeharibiwa na kosa hilo moja, kwa kushindwa kumpa Mungu utukufu wa kutoa maji kutoka kwenye mwamba, angeingia katika nchi ya ahadi, na angenyakuliwa kwenda mbinguni bila kuona kifo. Mikaeli, au Kristo, pamoja na malaika waliomzika Musa, walishuka kutoka mbinguni, baada ya yeye kukaa kaburini kwa muda mfupi, na kumfufua na kumpeleka mbinguni. Kristo na malaika walipokaribia kaburi, Shetani na malaika zake walijitokeza kaburini na walikuwa wakiulinda mwili wa Musa, usije ukaondolewa. **{SRSw 173.2}**

Kristo na malaika Zake walipokaribia, Shetani alizuia njia yao, lakini alilazimishwa, kwa utukufu na uwezo wa Kristo na malaika zake, kurudi nyuma. Shetani aliudai mwili wa Musa, kwa sababu ya kosa lake moja; Lakini Kristo alimtaja Babaye kwa upole, akisema, ***"Bwana na akukemee." Yuda 1:9*** Kristo alimwambia Shetani kwamba alijua kwamba Musa alikuwa ametubu kwa unyenyekevu kosa hili, kwamba hakuna doa lililowekwa juu ya tabia yake, na kwamba jina lake katika Kitabu cha Kumbukumbu cha Mbinguni lilisimama bila kutiwa doa. Kisha Kristo akafufua mwili wa Musa, ambao Shetani alikuwa ameudai. **{SRSw 173.3}**

Wakati wa kubadilika sura kwa Kristo-mng'ao, Musa, na Eliya ambaye alikuwa amenyakuliwa, walitumwa kuzungumza na Kristo

kuhusiana na mateso yake, na kuwa wabebaji wa utukufu wa Mungu kwa Mwana Wake mpendwa. Musa alikuwa ameheshimiwa sana na Mungu. Alikuwa amebahatika kuzungumza na Mungu uso kwa uso, kama vile mtu anavyozungumza na rafiki yake. na Mungu alikuwa amemfunulia utukufu Wake mkuu, zaidi ya alivyowahi kumfanyia mtu mwingine yeyote. **{SRSw 174.1}**

SURA YA 23—KUINGIA KATIKA NCHI YA AHADI

Sura hii imejengwa katika Yoshua 1; 3-6; 23 na 24.

Baada ya kifo cha Musa, Yoshua alipaswa kuwa kiongozi wa Israeli, ili kuwapeleka katika nchi ya ahadi. Alikuwa waziri mkuu wa Musa wakati wa muda mrefu zaidi Waisraeli wakiwa wametangatanga jangwani. Alikuwa ameona kazi za ajabu za Mungu zilizofanywa na Musa, na alielewa vyema tabia ya watu. Alikuwa mmoja wa wale wapelelezi kumi na wawili waliotumwa kupeleleza Nchi ya Ahadi, na mmoja wa wale wawili waliotoa ripoti ya uaminifu juu ya utajiri wa hiyo nchi ya ahadi na ambaye aliwahimiza watu kupanda juu katika nguvu za Mungu kuimiliki. Alikuwa na sifa za kutosha kwa ofisi hii muhimu. Bwana alimuahidi Yoshua kuwa pamoja naye kama alivyokuwa pamoja na Musa, na kuifanya Kanaani iwe rahisi kuichukua, mradi tu angekuwa mwaminifu kushika amri Zake zote. Alikuwa na wasiwasi ni jinsi gani angetekeleza agizo lake alilopewa la kuwaongoza watu kwenye nchi ya Kanaani, lakini faraja hii iliondoa woga wake. **{SRSw 175.1}**

Yoshua aliwaamuru wana wa Israeli kujiandaa kwa ajili ya safari ya siku tatu, na kwamba watu wote wa vita watoke kwenda vitani. ***“Wakamjibu Yoshua, wakasema, Hayo yote uliyotuamuru tutayafanya, na kila mahali utakakotutuma tutakwenda” Yoshua 1:16.*** **{SRSw 175.2}**

Kuvuka kwa Waisraeli juu ya mto Yordani kulipaswa kuwa miujiza.

"Yoshua akawaambia watu, Jitakaseni; maana kesho BWANA atatenda mambo ya ajabu kati yenu. Kisha Yoshua akawaambia makuhani, akasema, Liinueni Sanduku la Agano, mkavuke mbele ya hao watu. Wakaliinua sanduku la agano, wakatangulia mbele ya watu. BWANA akamwambia Yoshua, Hivi leo nitaanza kukutukuza mbele ya Israeli wote, wapate kujua ya kuwa Mimi nitakuwa pamoja na wewe, kama nilivyokuwa pamoja na Musa." Yoshua 3:5-7 **{SRSw 176.1}**

Kuvuka Yordani

Makuhani walipaswa kwenda mbele ya watu na kubeba Sanduku la Agano lenye sheria ya Mungu. Na miguu yao ilipotumbukizwa katika ukingo wa Yordani, maji yalikatwa kutoka juu, na makuhani wakapita, wakiwa wamebeba Sanduku la Agano, ambayo ilikuwa ni ishara ya uwepo wa Mungu; Na jeshi la Kiebrania likafuata. Makuhani walipokuwa katikati ya Yordani, waliamriwa kusimama katikati cha mto mpaka jeshi lote la Israeli lilipopita. Hapa kizazi kilichokuwepo wakati huo cha Waisraeli kilisadikishwa kwamba maji ya Yordani yalikuwa chini ya nguvu zile zile ambazo baba zao walikuwa wameziona zikionyeshwa kwenye Bahari ya Shamu miaka arobaini kabla. Wengi wa hawa walikuwa wamepitia Bahari Shamu walipokuwa watoto. Sasa wanapita juu ya Yordani, watu wa vita, wakiwa na vifaa kamili kwa ajili ya vita. **{SRSw 176.2}**

Baada ya jeshi lote la Israeli kupita juu ya Yordani, Yoshua aliwaamuru makuhani watoke nje ya mto. Mara tu makuhani, wakiwa wamebeba Sanduku la Agano, walitoka nje ya mto, wakasimama kwenye nchi kavu, Yordani iliendelea kama hapo awali na kufurika kingo zake zote. Muujiza huu wa ajabu uliofanywa kwa ajili ya Waisraeli uliongeza sana imani yao. Ili muujiza huu wa ajabu usisahaulike kamwe, Bwana alimwelekeza Yoshua aamuru kwamba

watu mashuhuri, mmoja kwa kila kabila, achukue mawe kutoka kwenye mto, mahali ambapo miguu ya makuhani ilisimama wakati jeshi la Kiebrania lilikuwa likipita, na kubeba juu ya mabega yao, na kusimamisha mnara ndani yake, Gilgali, kuweka ukumbusho wa ukweli kwamba Israeli ilipita juu ya Yordani kwenye nchi kavu. Baada ya makuhani kupanda kutoka Yordani, Mungu aliondoa mkono Wake wenye nguvu, na maji yakarudi na kutiririka kwa nguvu kubwa katika mkondo wake kama maporomoko ya maji yanavyokuwa. **{SRSw 176.3}**

Wakati wafalme wote wa Waamori na wafalme wa Wakanaani waliposikia kwamba Bwana alikuwa ameyaweka maji ya Yordani mbele ya wana wa Israeli, mioyo yao iliyeyuka kwa hofu. Waisraeli walikuwa wamewaua wafalme wawili wa Moabu, na njia yao ya kimiujiza juu ya Yordani na kuvuka kwao kwa muujiza kulijaza mataifa hofu kubwa sana. Kisha Yoshua akawatahiri watu wote waliozaliwa jangwani. Baada ya sherehe hii waliitunza Pasaka katika tambarare la Yeriko. **“BWANA akamwambia Yoshua, Siku hii ya leo nimeivingirisha hiyo aibu ya Misri iondoke juu yenu.” Yoshua 5:9** **{SRSw 177.1}**

Mataifa ya kipagani yalikuwa yamemtukana Bwana na watu Wake kwa sababu Waebrania hawakuwa wamemiliki nchi ya Kanaani, ambayo walitarajia kuirithi mara tu baada ya kuondoka Misri. Maadui zao walikuwa wameshinda kwa sababu walikuwa wametanga-tanga jangwani kwa muda mrefu sana, nao wakajiinua kwa kiburi juu ya Mungu, wakitangaza kwamba Yeye hakuwa na uwezo wa kuwaongoza katika nchi ya Kanaani. Sasa walikuwa wamepita juu ya mto Yordani kwenye nchi kavu, na adui zao hawakuweza tena kuwakejeli. **{SRSw 177.2}**

Mana ilikuwa imeendelea hadi wakati huu, lakini sasa Waisraeli walipokuwa karibu kumiliki Kanaani na kula matunda ya nchi, hawakuwa na haja nayo tena, nayo ikakoma. **{SRSw 178.1}**

Mkuu wa Jeshi la Bwana

Yoshua alipoondoka katika majeshi ya Israeli, ili kutafakari na kuomba kwa ajili ya uwepo wa pekee wa Mungu ili kumhudhuria, alimwona mtu wa kimo cha juu, akiwa amevaa mavazi ya kivita, akiwa na upanga Wake mkononi Mwake. Yoshua hakumtambua kuwa mmoja wa majeshi ya Israeli, na bado hakuwa na sura ya kuwa adui. Kwa bidii yake akamwuliza kwa kumuamrisha akisema, ***Je! Wewe u upande wetu, au upande wa adui zetu? Akasema, La, lakini nimekuja sasa, Nili amiri wa jeshi la Bwana. Yoshua akapomoka kiusouso hata nchi, naye akasujudu, akamwuliza, Bwana wangu aniambia nini mimi mtumishi wake? Huyo amiri wa jeshi la Bwana akamwambia Yoshua, Vua viatu vyako miguuni mwako; kwa kuwa mahali hapo usimamapo ni Patakatifu. Yoshua akafanya vivyo. Yoshua 5:13-15*** **{SRSw 178.2}**

Huyu hakuwa malaika wa kawaida. Ilikuwa ni Bwana Yesu Kristo, yule aliyewaongoza Waebrania jangwani, aliyefunikwa na nguzo ya moto usiku na nguzo ya wingu mchana. Mahali palifanywa Patakatifu kwa uwepo Wake; Kwa hiyo Yoshua aliamriwa avue viatu vyake. **{SRSw 178.3}**

Kisha Bwana alimwelekeza Yoshua njia ya kufuata ili kuiteka Yeriko. Watu wote wa vita waliamriwa kuuzunguka mji mara moja kila siku kwa siku sita, na siku ya saba wauzunguke Yeriko mara saba. **{SRSw 178.4}**

Kutekwa kwa Yeriko

"Bali Yoshua, mwana wa Nuni, akawaita makuhani, akawaambia, Lichukueni sanduku la agano, tena makuhani saba na wachukue tarumbeta saba za pembe za kondoo waume mbele ya sanduku la BWANA. Naye akawaambia watu, Piteni mbele, mkauzunguke mji, na hao watu wenye silaha na watangulie mbele ya

Sanduku la BWANA. Basi ikawa Yoshua alipokwisha kusema na watu, wale makuhani saba, wenye kuzichukua tarumbeta saba za pembe za kondoo waume mbele za BWANA, wakatangulia, wakazipiga hizo tarumbeta; nalo Sanduku la Agano la BWANA likawafuata." Yoshua 6:6-8 **{SRSw 179.1}**

"Wale watu wenye silaha walikwenda mbele ya hao makuhani waliozipiga tarumbeta, na wale waliokuwa nyuma wakalifuata hilo Sanduku; makuhani wakizipiga tarumbeta walipokuwa wakienda. Yoshua akawaamuru watu, akasema Msipige kelele, wala sauti zenu zisisikiwe, wala neno lolote lisitoke kinywani mwenu, hata siku ile nitakapowaamuru kupiga kelele, ndipo mtakapopiga kelele. Basi akalipeleka sanduku la BWANA liuzunguke huo mji, likauzunguka mara moja, kisha wakaenda kambini wakakaa kambini." **Yoshua 6:9-11 {SRSw 179.2}**

Jeshi la Waebrania lilitembea kwa mpangilio kamili. Kwanza walikwenda kundi lililochaguliwa la watu wenye silaha, wakiwa wamevaa mavazi ya kivita, si kwa kutumia ustadi wao wa kupigana, bali kwa kuamini na kutii maagizo waliyopewa. Kisha walifuata makuhani saba wenye baragumu. Halafu likaja sanduku la Mungu, liking'aa kwa dhahabu, utukufu ukiwa juu yake, likibebwa na makuhani waliovaa mavazi yao maalumu ya utumishi mtakatifu. Jeshi kubwa la Israeli lilifuata kwa mpangilio kamili, kila kabila chini ya bendera yake. Hivyo waliuzunguka mji pamoja na Sanduku la Mungu. Hakukuwa na sauti ila hatua (nyanyo) za jeshi hilo kubwa, na sauti kuu ya baragumu, iliyosikika kando ya vilima na kusikika katika mji wa Yeriko. **{SRSw 179.3}**

Kwa mshangao na hofu, walinzi wa mji ule uliokuwa umeangamizwa walifuatilia kila hatua, na kutoa taarifa kwa watawala. Hawakuweza kuelewa maana ya maandamano hayo. Wengine

walidhihaki wazo la mji kutekwa kwa namna hiyo, huku wengine wakijawa na hofu walipoona utukufu wa Sanduku la Agano na sura ya heshima ya makuhani na jeshi la Israeli, Yoshua akiwa kiongozi wao. alikumbuka kwamba Bahari ya Shamu iliwahi kufunguka mbele yao miaka arobaini iliyopita, na kwamba njia ilikuwa imetengenezwa hivi karibuni kupitia mto Yordani. Walijawa na hofu kiasi kwamba hawakuthubutu kubeza. Walihakikisha milango ya mji imefungwa vizuri, na mashujaa hodari walilinda kila lango. **{SRSw 180.1}**

Kwa muda wa siku sita majeshi ya Israeli yalifanya mzunguko wao kuuzunguka mji. Siku ya saba waliuzunguka Yeriko mara saba [jumla 13]. Watu waliamriwa, kama kawaida, kuwa kimya. Sauti ya baragumu peke yake ndiyo iliyopaswa kusikika. Watu walipaswa kusubiri, na wakati wapiga-baragumu watakapopiga kwa nguvu kuliko kawaida, ndipo wote walipaswa kupiga kelele kwa sauti kuu, kwa maana Mungu alikuwa amewapa mji huo. ***"Ikawa siku ya saba wakaondoka asubuhi na mapema wakati wa mapambazuko, wakauzunguka mji vivyo hivyo mara saba; ila siku hiyo waliuzunguka huo mji mara saba. Hata mara ya saba makuhani walipozipiga tarumbeta, Yoshua akawaambia watu, Pigeni kelele; kwa maana BWANA amewapeni mji huu."*** **Yoshua 6:15-16** **"*Basi watu wakapiga kelele, na makuhani wakazipiga tarumbeta; hata ikawa, hapo watu waliposikia sauti ya tarumbeta hao watu wakapiga kelele kwa sauti kuu sana, na ule ukuta wa mji ukaanguka nchi kabisa, hata watu wakapanda juu, wakaingia katika mji, kila mtu akiendelea kukabili mbele; wakautwaa huo mji."*** **Yoshua 6:20** **{SRSw 180.2}**

Mungu alikusudia kuwaonyesha Waisraeli kwamba ushindi wa Kanaani haukupaswa kuhesabiwa kuwa wao wenyewe wameufanikisha. Amiri wa jeshi la Bwana Ndiye aliyeishinda Yeriko. Yeye pamoja na malaika Zake walihusika katika ushindi huo. Kristo aliyaamuru majeshi

ya mbinguni kuangusha kuta za Yeriko na kuandaa njia kwa ajili ya Yoshua na majeshi ya Israeli. Mungu, katika muujiza huu wa ajabu, hakutia nguvu tu imani ya watu Wake katika uwezo Wake wa kuwashinda maadui wao, bali pia alikemea kutokuamini kwao kwa hapo awali. **{SRSw 181.1}**

Yeriko ilikuwa imeyapinga majeshi ya Israeli na Mungu wa mbinguni. Walipoliona jeshi la Israeli likiuzunguka mji wao mara moja kila siku, waliingiwa na hofu; lakini walizitazama ngome zao imara, kuta zao nene na za juu, na walihisi kuwa wangeweza kustahimili shambulio lolote. Lakini kuta zao imara zilipotikisika ghafla na kuanguka kwa mshindo mkubwa kama ngurumo kubwa zaidi, walipooza kwa hofu na hawakuweza kutoa upinzani wowote. **{SRSw 181.2}**

Yoshua Kiongozi Mwenye Hekima na Aliyewekwa Wakfu

Hakukuwa na doa juu ya tabia takatifu ya Yoshua. Alikuwa kiongozi mwenye hekima. Maisha yake yote yaliwekwa wakfu kwa Mungu. Kabla ya kufa, alikusanya jeshi la Kiebrania, na kwa kufuata mfano wa Musa, alikumbusha safari zao jangwani na pia rehema za Mungu kwao. Kisha aliwahutubia kwa ufasaha. Aliwasimulia kwamba mfalme wa Moabu alipigana nao na akamwita Balaamu ili kuwalaani; lakini Mungu ***"hakumsikiliza Balaamu; kwa hiyo akafuliza kuwabarikia ninyi*** **Yoshua 24:10.** Kisha akawaambia, ***Nanyi kama mkiona ni vibaya kumtumikia BWANA, chagueni hivi leo mtakayemtumikia; kwamba ni miungu ile ambayo baba zenu waliitumikia ng'ambo ya Mto, au kwamba ni miungu ya wale Waamori ambao mnakaa katika nchi yao; lakini mimi na nyumba yangu tutamtumikia BWANA. Yoshua 24:16-17.*** **{SRSw 181.3}**

"Hao watu wakajibu wakasema, Hasha! Tusimwache BWANA, ili kuitumikia miungu mingine; kwa maana BWANA, Mungu wetu,

Yeye Ndiye aliyetupandisha sisi na baba zetu kutoka nchi ya Misri; kutoka nyumba ya utumwa; naye Ndiye aliyezifanya ishara zile kubwa mbele ya macho yetu, na kutulinda katika njia ile yote tuliyoiendea, na kati ya watu wa mataifa yote tuliopita katikati yao". **Yoshua 24:16-17{SRSw 182.1}**

Watu walifanya upya agano lao na Yoshua. ***Wakamwambia, BWANA, Mungu wetu, Ndiye tutakayemtumikia; na sauti Yake ndiyo tutakayoitii.*** **Yoshua 24:24.** Yoshua akaandika maneno ya agano lao katika kitabu kilichokuwa na sheria na amri alizopewa Musa. Yoshua alipendwa na kuheshimiwa na Israeli wote, na kifo chake kiliombolezwa sana nao. **{SRSw 182.2}**

SURA YA 24—SANDUKU LA MUNGU NA HATIMA YA ISRAELI

Sura hii imejengwa juu ya 1 Samweli 3-6; 2 Samweli 6 na 1 Wafalme 8.

Sanduku la Mungu lilikuwa Sanduku Takatifu, lililotengenezwa kuwa mahali pa kuhifadhia Amri Kumi, Sheria iliyomwakilisha Mungu Mwenyewe. Sanduku hili lilichukuliwa kuwa utukufu na nguvu ya Israeli. Ishara ya uwepo wa Mungu ilikaa juu yake mchana na usiku. Makuhani waliohudumu mbele yake walikuwa wamewekwa wakfu kwa huduma takatifu. Walivaa kifuko cha kifuani kilichopambwa kwa mawe ya thamani ya aina mbalimbali [naivera], sawa na yale yanayounda misingi kumi na miwili ya mji wa Mungu. Ndani ya mapambo hayo kulikuwa na majina ya makabila kumi na mawili ya Israeli, yamechorwa juu ya vito vya thamani vilivyotiwa dhahabu. Hii ilikuwa kazi ya thamani kubwa na ya kupendeza sana, iliyoning'inizwa mabegani mwa makuhani, ikifunika kifua. **{SRSw 183.1}**

Upande wa kulia na kushoto wa kifuko hicho cha kifuani kulikuwa na mawe mawili makubwa zaidi, yaliyong'aa kwa uzuri mkubwa/sana. Masuala magumu yalipoletwa kwa waamuzi na kisha wasiweze kuamua, yaliletwa kwa makuhani, nao walimuuliza Mungu, ambaye aliwajibu. Ikiwa angekubali na kuwapa mafanikio, mwanga duara wa utukufu ulikaa juu ya jiwe la upande wa kulia [halo]. Ikiwa hakukubali, ukungu au wingu ulikaa juu ya jiwe la upande wa kushoto. Walipomuuliza Mungu kuhusu kwenda vitani, jiwe la kulia lilipozungukwa na mwanga

lilisema, Kweeni, mkafanikiwe. Jiwe la kushoto lilipofunikwa na wingu lilisema, Msikwee; hamtafanikiwa. **{SRSw 183.2}**

Kuhani mkuu alipoingia Patakatifu pa Patakatifu mara moja kwa mwaka, na kuhudumu mbele ya Sanduku katika uwepo wa kutisha wa Mungu, aliuliza, na Mungu mara nyingi alimjibu kwa sauti inayosikika. Bwana alipokuwa hajibu kwa sauti, aliruhusu miale ya utukufu itue juu ya makerubi wa upande wa kulia wa Sanduku la Agano, kuonyesha kibali. Ikiwa maombi yao yalikataliwa, wingu lilikaa juu ya makerubi wa upande wa kushoto. **{SRSw 184.1}**

Malaika wanne wa mbinguni waliandamana na Sanduku la Mungu katika safari zake zote, kulilinda dhidi ya hatari na kutekeleza kazi yoyote iliyohitajika kuhusiana nalo. Yesu, Mwana wa Mungu, akifuatwa na malaika, alitangulia mbele ya Sanduku lilipofika Yordani; na maji yakakatika mbele ya uwepo Wake. Kristo na malaika walisimama karibu na Sanduku na makuhani katikati ya mto mpaka Israeli wote walipovuka. Kristo na malaika waliandamana na Sanduku lilipouzunguka Yeriko, na hatimaye wakaangusha kuta zake kubwa na kuikabidhi Yeriko mikononi mwa Israeli. **{SRSw 184.2}**

Matokeo ya Uzembe wa Eli

Wakati Eli alipokuwa kuhani mkuu aliwainua wanawe kwenye ukuhani. Eli peke yake aliruhusiwa kuingia Patakatifu pa Patakatifu mara moja kwa mwaka. Wanawe walihudumu mlangoni pa hema na waliongoza katika kuchinja wanyama na kutoa dhabihu pale madhabahuni. Walitumia vibaya sana huduma hiyo takatifu. Walikuwa wabinafsi, wenye tamaa, walafi, na wapotovu. Mungu alimkemea Eli kwa uzembe wake wa uhalifu katika nidhamu ya familia. Eli aliwakemea wanawe lakini hakuwazuia. Baada ya kuwekwa katika huduma takatifu ya ukuhani, Eli alisikia mwenendo wao wa

kuwadhulumu Waisraeli sadaka zao, pia uvunjaji wao wa sheria ya Mungu kwa ujasiri na vitendo vyao vya jeuri vilivyosababisha Israeli kutenda dhambi. **{SRSw 184.3}**

Bwana alimfunulia mtoto Samweli hukumu atakazozileta juu ya nyumba ya Eli kwa sababu ya uzembe wake… ***"BWANA akamwambia Samweli, Angalia, nitatenda tendo katika Israeli, ambalo kila atakayelisikia masikio yake yatamwasha. Siku hiyo nitayatimiza maneno yale yote niliyoyasema juu ya Eli katika habari za nyumba yake, tangu mwanzo hata mwisho. Kwa maana nimemwambia ya kwamba nitaihukumu nyumba yake milele, kwa ajili ya ule uovu alioujua; kwa kuwa wanawe walijiletea laana, wala yeye hakuwazuia. Na kwa hiyo nimeapa juu ya nyumba ya Eli, ya kwamba uovu wa nyumba ya Eli hautasafika kwa dhabihu wala kwa sadaka hata milele."*** **1 Samweli 3:11-14** **{SRSw 185.1}**

Makosa ya wana wa Eli yalikuwa ya uthubutu sana, ya kumkosea heshima Mungu mtakatifu, kiasi kwamba hakuna dhabihu iliyoweza kulipia uasi huo wa makusudi. Makuhani hawa wenye dhambi walizitia unajisi dhabihu zilizokuwa mfano wa Mwana wa Mungu. Kwa mwenendo wao wa kukufuru walikuwa wakikanyaga damu ya upatanisho, ambayo ndani yake ndimo nguvu ya dhabihu zote ilikotoka. **{SRSw 185.2}**

Samweli alimwambia Eli Maneno ya Bwana; ***Naye akasema, Ndiye BWANA; na afanye alionalo kuwa ni jema.*** **1 Samweli 3:18.** Eli alijua kwamba Mungu alikuwa amevunjiwa heshima, naye alitambua kuwa alikuwa ametenda dhambi. Alikubali kwamba Mungu alikuwa anamwadhibu kwa uzembe wake wa dhambi. Neno la Bwana kwa Samweli lilijulikana na Eli kwa Israeli wote. Kwa kufanya hivyo alidhani angeweza kurekebisha kwa kiasi fulani uzembe wake wa

zamani. Lakini hukumu iliyotangazwa juu ya Eli hata haikukawia. **{SRSw 185.3}**

Waisraeli walipigana vita na Wafilisti, nao wakashindwa, na watu elfu nne kati yao waliuawa. Waebrania wakaingiwa na hofu. Walijua kwamba mataifa mengine yakisikia kushindwa kwao yangetiwa moyo kupigana nao. Wazee wa Israeli wakaamua kwamba kushindwa kwao kulikuwa kwa sababu Sanduku la Mungu halikuwa pamoja nao. Wakatuma Shilo kulichukua Sanduku la Agano. Walikumbuka kuvuka kwao Yordani na ushindi rahisi wa Yeriko walipolibeba Sanduku, wakaamua kwamba walichohitaji ni kulileta kwao, nao wangewashinda adui zao. Hawakutambua kwamba nguvu yao ilikuwa katika utii wao kwa sheria iliyokuwa ndani ya Sanduku, ambayo ilikuwa mwakilishi wa Mungu Mwenyewe. Makuhani waliokuwa wametiwa unajisi, Hofni na Finehasi, walikuwa pamoja na Sanduku Takatifu, wakivunja sheria ya Mungu. Wenye dhambi hawa walilipeleka sanduku kambini kwa Israeli. Imani ya wapiganaji ilirejea, nao wakajiamini kwamba wangepata ushindi. **{SRSw 185.4}**

Sanduku la Agano Kuchukuliwa

"Na sanduku la agano la BWANA lilipoingia kambini, Israeli wote wakapiga kelele kwa sauti kuu, hata nchi ikavuma. Nao Wafilisti waliposikia mshindo wa zile kelele, walisema, Maana yake nini mshindo wa kelele hizi kubwa katika kambi ya Waebrania? Wakatambua ya kuwa Sanduku la BWANA limefika kambini. Wafilisti wakaogopa, maana walisema, Mungu ameingia kambini. Wakasema, Ole wetu! Kwani halijawa jambo kama hili tangu hapo. Ole wetu! Ni nani atakayetuokoa na mkono wa miungu hawa walio hodari? Hawa ndio miungu waliowapiga Wamisri kwa mapigo ya kila namna jangwani. Iweni hodari, na kufanya kiume enyi Wafilisti, msije mkawa watumwa wa Waebrania, kama wao walivyokuwa watumwa

wenu; fanyeni kiume, mkapigane nao. Wafilisti wakapigana nao, Israeli wakapigwa, wakakimbia kila mtu hemani kwake; wakauawa watu wengi sana; maana katika Israeli walianguka watu thelathini elfu wenye kwenda vitani kwa miguu. Hilo Sanduku la Mungu Likatwaliwa; na Hofni na Finehasi, wale wana wawili wa Eli, wakauawa." **1 Samweli 4:5-11** **{SRSw 186.1}**

Wafilisti walidhani Sanduku hilo ndilo lilikuwa mungu wa Waisraeli. Hawakujua kwamba Mungu aliye hai, aliyeziumba mbingu na nchi, na aliyetoa sheria Yake katika Sinai, Ndiye aliyetoa mafanikio au shida kulingana na utii au uasi wa sheria iliyokuwa ndani ya Sanduku Takatifu. **{SRSw 187.1}**

Kulikuwa na mauaji makubwa sana katika Israeli. Eli alikuwa ameketi kando ya njia, akingoja na kutazama kwa moyo unaotetemeka kupokea habari kutoka vitani (jeshi). Aliogopa kwamba Sanduku la Mungu lingechukuliwa na kutiwa unajisi na Wafilisti. Mjumbe kutoka vitani akakimbia hadi Shilo na kumwambia Eli kwamba wanawe wawili wameuawa. Aliweza kuvumilia habari hiyo kwa kiasi fulani, kwa maana alikuwa na sababu ya kutarajia hilo. Lakini mjumbe alipoongeza kusema, ***"Huo utukufu umeondoka katika Israeli; kwa sababu Sanduku la Mungu lilikuwa limetwaliwa."*** **1 Samweli 4:21.** Eli akatikisika kwa uchungu, akaanguka nyuma kutoka kitini mwake, akafa. Alishiriki ghadhabu ya Mungu iliyowapata wanawe, kwa sababu kwa kiasi kikubwa alikuwa na uhalifu na hatia ya makosa yao, kwa kuwa hakuwazuia ipasavyo. Kutekwa kwa Sanduku la Mungu na Wafilisti kulihesabiwa kuwa janga kubwa kuliko yote lililoweza kuipata Israeli. Mke wa Finehasi alipokuwa karibu kufa, *akamwita mtoto, Ikabodi, akisema,* ***"Utukufu umeondoka katika Israeli; kwa sababu Sanduku la Mungu lilikuwa limetwaliwa"*** **1 Samweli 4:21** **{SRSw 187.2}**

Katika Nchi ya Wafilisti

Mungu aliruhusu Sanduku Lake lichukuliwe na adui zao, ili kuwaonyesha Israeli jinsi ilivyokuwa bure kulitegemea Sanduku, ishara ya uwepo Wake, huku wakizivunja amri zilizokuwa ndani ya Sanduku. Mungu angewanyenyekeza kwa kuliondoa kwao Sanduku hilo Takatifu, lililokuwa nguvu na tumaini lao walilojivunia. **{SRSw 187.3}**

Wafilisti walifurahi kwa ushindi, kwa sababu walikuwa, kama walivyodhani, wamempata Mungu mashuhuri wa Waisraeli, ambaye alikuwa amewafanyia maajabu makubwa na kuwafanya kuwa tisho kwa adui zao. Walilichukua Sanduku la Mungu hadi Ashdodi na kuliweka katika hekalu zuri sana, lililojengwa kwa heshima ya mungu wao maarufu zaidi, Dagoni, na kulitia kando ya mungu wao. Asubuhi, makuhani wa miungu hiyo walipoingia hekaluni, waliingiwa na hofu walipomkuta Dagoni ameanguka kifudifudi chini mbele ya Sanduku la Bwana. Wakamwinua Dagoni na kumrudisha mahali pake pa awali. Walidhani huenda alianguka kwa bahati mbaya. Lakini asubuhi iliyofuata walimkuta ameanguka tena kifudifudi chini, kama hapo kwanza,, na kichwa cha Dagoni pamoja na mikono yake yote miwili vilikuwa vimekatika. **{SRSw 188.1}**

Malaika wa Mungu, waliokuwa wakiandamana daima na Sanduku, waliiangusha chini ile sanamu isiyo na uhai, kisha wakaivunja, ili kuonyesha kwamba Mungu, aliye hai, Yuko juu ya miungu yote, na kwamba mbele Yake kila mungu wa kipagani si kitu. Wapagani walimheshimu sana mungu wao Dagoni; walipomkuta ameharibika vibaya na amelala kifudifudi mbele ya Sanduku la Mungu, walihuzunika na wakaona kuwa ni ishara mbaya sana kwa Wafilisti. Walitafsiri kwamba Wafilisti na miungu yao yote wangeshindwa na kuangamizwa na Waebrania, na kwamba Mungu wa Waebrania angekuwa mkuu na mwenye nguvu kuliko miungu yote. Wakaliondoa Sanduku la Mungu kutoka hekaluni mwa sanamu yao na kuliweka peke yake. **{SRSw 188.2}**

Sanduku la Mungu lilikaa kwa miezi saba mikononi mwa Wafilisti. Walikuwa wamewashinda Waisraeli na kulichukua Sanduku la Mungu, ambalo walidhani nguvu yao imo ndani yake, wakafikiri wangekuwa salama daima na wasingehofia tena majeshi ya Israeli. Lakini katikati ya furaha yao kwa ushindi wao, kilio kilisikika katika nchi yote, na hatimaye sababu yake ikaelekezwa kwa Sanduku la Mungu. Lilibebwa kutoka mahali hadi mahali kwa hofu, na maangamizi kutoka kwa Mungu yakalifuata, hata Wafilisti wakachanganyikiwa sana wakijua wafanye nini nalo. Malaika waliokuwa wakiandamana nalo walililinda lisipate madhara. Wafilisti hawakuthubutu kufungua Sanduku hilo; kwa maana mungu wao Dagoni alikuwa amepata maangamizi hayo, hivyo waliogopa kuligusa au kulikaribia. Wakawaita makuhani na wabashiri, na kuwauliza wafanye nini na Sanduku la Mungu. Waliwashauri kulirudisha kwa watu wenye hii mali, na kulipeleka pamoja nalo sadaka ya hatia ya thamani, ambayo ikiwa Mungu angeipokea kwa furaha, wangepata kuponywa. Pia walipaswa kuelewa kwamba mkono wa Mungu ulikuwa juu yao kwa sababu walikuwa wamechukua Sanduku Lake, ambalo lilikuwa la Israeli peke yake. **{SRSw 188.3}**

Kurejeshwa kwa Israeli

Baadhi hawakukubali ushauri huo. Ilikuwa aibu sana kulirudisha Sanduku, na walisisitiza kwamba hakuna Mfilisti ambaye angejaribu kuhatarisha maisha yake kulibeba Sanduku la Mungu wa Israeli, ambalo lilikuwa limeleta vifo hivyo juu yao. Washauri wao waliwasihi watu wasifanye mioyo yao migumu kama Wamisri na Farao walivyofanya, na hivyo kuleta mateso na mapigo zaidi juu yao. Na kwa kuwa wote waliogopa kulichukua Sanduku la Mungu, waliwashauri wakisema, ***“Basi sasa jifanyizieni gari jipya, mtwae na ng’ombe wake wawili wakamwao, ambao hawajafungwa nira, nanyi mkawafunge hao ng’ombe garini, na kuwaondoa ndama zao na kuwatia zizini; kisha,***

litwaeni hilo Sanduku la BWANA, na kuliweka juu ya gari; na hivyo vitu vya dhahabu, mtakavyompelekea kuwa matoleo ya kosa, mvitie katika kasha kando yake; mkalipeleke Sanduku, lipate kwenda. Kisha angalieni, likikwea kwa njia ya mpakani mwake kwenda Beth-shemeshi, basi, ndiye aliyetutenda uovu huo mkuu; la, sivyo, ndipo tutakapojua ya kwamba si mkono wake uliotupiga; ilikuwa ni ajali iliyotupata. Basi watu wale walifanya hivyo; wakatwaa ng'ombe wawili wakamwao, wakawafunga garini, na ndama zao wakawafunga zizini; kisha wakaliweka Sanduku la BWANA juu ya gari, pamoja na kasha lenye panya wa dhahabu na sanamu za majipu yao. Na hao ng'ombe wakashika njia moja kwa moja kwenda Beth-shemeshi; wakaiandama njia ya barabara, wakaenda wakilia, lakini hawakugeukia upande wa kuume wala wa kushoto." **1 Samweli 6:7-12** **{SRSw 189.1}**

Wafilisti walijua kwamba ng'ombe hawawezi kuacha ndama wao nyumbani isipokuwa washurutishwe na nguvu isiyoonekana. Ng'ombe wakaenda moja kwa moja Beth-shemeshi, wakilia kwa ajili ya ndama wao, lakini wakiendelea kwenda mbali nao. Wakuu wa Wafilisti wakalifuata Sanduku la Agano mpaka mpaka wa Beth-shemeshi. Hawakuthubutu kuliacha kabisa kwa ng'ombe. Waliogopa kwamba likipatwa na jambo lolote baya, maafa makubwa zaidi yangewapata. Hawakujua kwamba malaika wa Mungu walikuwa wakiandamana na Sanduku na kuwaongoza ng'ombe hao hadi kufika mahali pake hilo Sanduku la Agano. **{SRSw 190.1}**

Kiburi Kinaadhibiwa

Watu wa Beth-shemeshi walikuwa wanavuna shambani, walipoona sanduku la Mungu juu ya gari likivutwa na ng'ombe, walifurahi sana. Walijua kwamba ilikuwa kazi ya Mungu. Ng'ombe wakaleta gari lenye Sanduku hadi kwenye jiwe kubwa, wakasimama wenyewe. Walawi

wakalishusha Sanduku la Bwana pamoja na sadaka ya Wafilisti, wakatoa sadaka ya kuteketezwa kwa Mungu kwa kutumia gari na ng'ombe waliobeba Sanduku hilo takatifu. Wakuu wa Wafilisti wakarudi Ekroni, na tauni ikakoma. **{SRSw 190.2}**

Watu wa Beth-shemeshi walitaka kujua ni nguvu gani kubwa iliyokuwa ndani ya Sanduku hilo iliyofanya mambo ya ajabu kiasi hicho. Walilitazama Sanduku lenyewe kana kwamba lina nguvu, bila kumpa Mungu utukufu wa nguvu hiyo. Hakuna mtu aliyeruhusiwa kulitazama sanduku bila vifuniko vyake isipokuwa wale walioteuliwa kwa kazi hiyo, la sivyo angeuawa, kwa maana ilikuwa kana kwamba anamwangalia Mungu Mwenyewe. Na kwa kuwa watu waliridhisha udadisi wao na kulifungua Sanduku ili kutazama ndani yake, jambo ambalo hata waabudu sanamu wa kipagani hawakuthubutu kufanya, malaika waliokuwa wakililinda waliwaua zaidi ya watu elfu hamsini. **{SRSw 191.1}**

Na watu wa Beth-Shemeshi waliliogopa Sanduku, wakasema, ***"Ni nani awezaye kusimama mbele za BWANA, Huyu Mungu Mtakatifu? Naye atapanda kwenda kwa nani kutoka kwetu? Nao wakatuma wajumbe waende kwa wenyeji wa Kiriath-yearimu, kusema, Wafilisti wamelirudisha Sanduku la BWANA; basi shukeni, mkalichukue kwenu. "1*** **Samweli 6:20-21** Watu wa Kiriath-yearimu wakalileta Sanduku la Bwana nyumbani kwa Abinadabu, na wakamtakasa mwanawe ili alilinde. Kwa muda wa miaka ishirini Waebrania walikuwa chini ya Wafilisti, na wakanyenyekezwa sana na kutubu dhambi zao; Samweli akawaombea, na Mungu akawa na rehema kwao tena. Wafilisti wakapigana nao, lakini Bwana akafanya tena kwa njia ya ajabu kwa ajili ya Israeli, nao wakawashinda adui zao. **{SRSw 191.2}**

Sanduku likakaa nyumbani kwa Abinadabu mpaka Daudi alipofanywa kuwa mfalme. Akakusanya watu wote wateule wa Israeli,

watu elfu thelathini, akaenda kulileta Sanduku la Mungu. Wakaliweka Sanduku juu ya gari jipya na kulitoa nyumbani kwa Abinadabu. Uza na Ahio, wana wa Abinadabu, wakaendesha gari. Daudi na nyumba yote ya Israeli wakacheza mbele za Bwana kwa ala za muziki za kila namna. "***Hata walipofika kwa uga ya Nakoni, Uza akalinyoshea mkono sanduku la Mungu, akalikamata kwa maana wale ng'ombe walikunguwaa. Ndipo hasira ya BWANA ikawaka juu ya Uza; Naye Mungu akampiga huko kwa kosa lake; hata akafa pale pale penye sanduku la Mungu.*** **2 Samweli 6:6-7** Uza aliwakasirikia ng'ombe kwa sababu walijikwaa. Alionyesha kutomwamini Mungu waziwazi, kana kwamba yeye aliyelileta Sanduku kutoka nchi ya Wafilisti hangeweza kulilinda. Malaika waliokuwa wakililinda Sanduku walimpiga Uza kwa kuthubutu kuligusa sanduku la Mungu kwa papara. **{SRSw 191.3}**

"*Naye Daudi akamwogopa BWANA siku ile; akasema, Litanijiaje Sanduku la BWANA? Basi Daudi hakutaka kulileta Sanduku la BWANA kwake mjini mwa Daudi; ila Daudi akalihamisha nyumbani kwa Obed-edomu, Mgiti."* **2 Samweli 6:9-10.** Daudi alijua kwamba yeye ni mwenye dhambi, akaogopa asije, kama Uza, akafanya jambo la kiburi na kuileta hasira ya Mungu juu yake. ***"Sanduku la BWANA akalitia katika nyumba ya Obed-edomu, Mgiti, muda wa miezi mitatu; naye BWANA akambarikia Obed-edomu, na nyumba yake yote."*** **2 Samweli 6:11 {SRSw 192.1}**

Mungu alitaka kuwafundisha watu Wake kwamba, ingawa Sanduku Lake lilikuwa hofu na kifo kwa wale waliovunja amri Zake zilizokuwa ndani yake, lilikuwa pia baraka na nguvu kwa wale waliotii amri Zake. Daudi aliposikia kwamba nyumba ya Obed-edomu imebarikiwa sana, na yote aliyokuwa nayo amefanikiwa kwa sababu ya Sanduku la Mungu, alitamani sana kulileta katika mji wake. Lakini kabla ya kuthubutu kulihamisha Sanduku Takatifu, alijitakasa kwa

Mungu, na pia akaamuru watu wote wenye mamlaka katika ufalme wajitenge na shughuli za kidunia na kila kitu kitakachoweza kuvuruga mawazo yao kutoka ibada takatifu. Hivyo walipaswa kujitakasa kwa ajili ya kulileta Sanduku hilo katika mji wa Daudi. ***"Daudi akaenda, akalileta Sanduku la Mungu, toka nyumba ya Obed-edomu mpaka mji wa Daudi, kwa shangwe."*** **2 Samweli 6:12** **{SRSw 192.2}**

"Wakaliingiza Sanduku la BWANA, na kuliweka mahali pake, katikati ya hema aliyoipiga Daudi kwa ajili yake, naye Daudi akatoa sadaka za kuteketezwa na sadaka za amani mbele za BWANA." **2 Samweli 6:17** **{SRSw 193.1}**

Katika Hekalu la Sulemani

Baada ya Sulemani kumaliza kujenga hekalu, aliwakusanya wazee wa Israeli na watu wenye ushawishi mkubwa miongoni mwa watu, ili kulipandisha Sanduku la agano la Bwana kutoka mji wa Daudi. Watu hawa walijitakasa kwa Mungu, na kwa heshima kubwa na unyenyekevu, waliandamana na makuhani waliobeba Sanduku hilo. ***"Wakalipandisha sanduku la BWANA, na ile hema ya kukutania, na vyombo vitakatifu vyote vilivyokuwa katika ile Hema; vitu hivyo makuhani na Walawi wakavipandisha. Mfalme Sulemani, na mkutano wote wa Israeli waliokutanika kwake, walikuwako pamoja naye mbele ya Sanduku, wakichinja sadaka kondoo na ng'ombe, wasioweza kuhesabiwa wala kufahamiwa idadi yao kwa kuwa wengi." 1 Wafalme 8:4-5*** **{SRSw 193.2}**

Sulemani alifuata mfano wa baba yake Daudi. Baada ya kila hatua sita alitoa dhabihu. Kwa kuimba na kwa muziki na kwa sherehe kubwa, ***Makuhani wakalileta Sanduku la Agano la BWANA hata mahali pake, katika chumba cha ndani cha ile nyumba, Patakatifu pa Patakatifu, naam, chini ya mbawa za makerubi. Kwa maana makerubi yalinyosha***

mbawa zao, juu ya mahali pa Sanduku, makerubi yakalifunika lile Sanduku na miti yake kwa juu. **1 Wafalme 8:6-7** **{SRSw 193.3}**

Patakatifu pa ajabu na pa utukufu mkubwa palitengenezwa, kwa mfano ulioonyeshwa kwa Musa mlimani na baadaye kuonyeshwa na Bwana kwa Daudi. Hekalu la duniani lilitengenezwa kama lile la mbinguni. Zaidi ya makerubi waliokuwa juu ya Sanduku, Sulemani alitengeneza malaika wawili wakubwa zaidi, wamesimama kila mwisho wa Sanduku, wakiwakilisha malaika wa mbinguni wanaolinda daima sheria ya Mungu. Haiwezekani kueleza uzuri na utukufu wa maskani hii. Hapo, kama ilivyokuwa katika hema la zamani, Sanduku Takatifu lilibebwa kwa mpangilio wa heshima kubwa na kuwekwa mahali pake chini ya mabawa ya makerubi wawili wakuu waliokuwa wamesimama sakafuni. **{SRSw 194.1}**

Kwaya takatifu iliunganisha sauti zao na ala za muziki za kila aina, kumsifu Mungu. Na wakati sauti hizo, zikichanganyika na muziki, ziliposikika hekaluni na kusambaa hewani kupitia Yerusalemu, wingu la utukufu wa Mungu lilichukua milki ya nyumba hiyo, kama lilivyokuwa limeijaza hapo awali hema ya kukutania. ***"Ikawa, makuhani walipotoka katika Patakatifu, nyumba ya BWANA ikajaa wingu; hata makuhani hawakuweza kusimama ili kufanya huduma yao, kwa sababu ya wingu lile; kwa kuwa nyumba ya BWANA ilikuwa imejaa utukufu wa BWANA."*** ***1 Wafalme 8:10,11*** **{SRSw 194.2}**

Mfalme Sulemani alisimama juu ya jukwaa la shaba mbele ya madhabahu na kuwabariki watu. Kisha akapiga magoti, na mikono yake ikiwa imeinuliwa juu, akamimina maombi ya dhati na ya heshima kwa Mungu huku mkutano wote ukiwa umepiga magoti na nyuso zao zikiwa chini. Baada ya Sulemani kumaliza maombi yake, moto wa kimiujiza ulitoka mbinguni na kuyateketeza matoleo ya dhabihu. **{SRSw 194.3}**

Kwa sababu ya dhambi za Israeli, janga ambalo Mungu alisema lingekuja juu ya hekalu ikiwa watu Wake wangemwacha, lilitimia miaka mia kadhaa baada ya hekalu kujengwa. Mungu aliahidi Sulemani kwamba ikiwa angeendelea kuwa mwaminifu, na watu wake wangetii amri Zake zote, hekalu hilo tukufu lingesimama milele katika utukufu wake wote, kama ushahidi wa mafanikio na baraka kuu zilizokuwa juu ya Israeli kwa utii wao. **{SRSw 194.4}**

Kuchukuliwa Mateka kwa Israeli

Kwa sababu ya uvunjaji wa Israeli wa amri za Mungu na matendo yao maovu, Mungu aliwaruhusu kwenda utumwani ili kuwanyenyekeza na kuwaadhibu. Kabla hekalu halijaharibiwa, Mungu aliwafunulia baadhi ya watumishi Wake waaminifu hatima ya hekalu hilo, ambalo lilikuwa fahari ya Israeli, na ambalo walililiheshimu kama sanamu wakati walipokuwa wakitenda dhambi dhidi ya Mungu. Pia aliwafunulia kuchukuliwa mateka kwa Israeli. Watu hawa wa haki, muda mfupi kabla ya uharibifu wa hekalu, waliliondoa Sanduku Takatifu lililokuwa na mbao za mawe, na kwa huzuni na kwa majonzi wakalificha katika pango ambapo lingefichwa mbali na watu wa Israeli kwa sababu ya dhambi zao, na halingerejeshwa kwao tena. Sanduku hilo Takatifu bado limefichwa; Nalo halijawahi kuguswa tangu lilipofichwa. **{SRSw 195.1}**

SURA YA 25—UJIO WA KWANZA WA KRISTO

Nilipelekwa hadi wakati ambapo Yesu angechukua asili ya mwanadamu, kujinyenyekeza kama mwanadamu, na kuteseka majaribu ya Shetani. **{SRSw 196.1}**

Kuzaliwa Kwake hakukuwa na utukufu wa kidunia. Alizaliwa katika zizi na kulazwa kwenye hori la kulishia mifugo; lakini kuzaliwa Kwake kuliheshimiwa zaidi kuliko kwa wana wote wa wanadamu. Malaika kutoka mbinguni waliwajulisha wachungaji juu ya kuja kwa Yesu, na nuru na utukufu kutoka kwa Mungu viliandamana na ushuhuda wao. Jeshi la mbinguni lilipiga vinubi vyao na kumtukuza Mungu. Kwa ushindi walitangaza kuja kwa Mwana wa Mungu katika ulimwengu ulioanguka ili kutimiza kazi ya ukombozi, na kwa kifo Chake kuleta amani, furaha, na uzima wa milele kwa mwanadamu. Mungu aliheshimu kuja kwa Mwana Wake. Malaika walimwabudu. **{SRSw 196.2}**

Ubatizo wa Yesu

Malaika wa Mungu walisimama juu ya tukio la ubatizo Wake; Roho Mtakatifu alishuka kwa mfano wa njiwa na kumwangukia, na watu waliposimama wakishangaa sana, macho yao yakiwa yamekazia Kwake, sauti ya Baba ilisikiwa kutoka mbinguni ikisema, ***"Wewe Ndiwe Mwanangu, mpendwa Wangu; nimependezwa Nawe." Marko 1:11*** **{SRSw 196.3}**

Yohana hakuwa na uhakika kwamba ni Mwokozi aliyekuja kubatizwa naye Yordani. Lakini Mungu alikuwa amemwahidi ishara ambayo angeweza kumtambua Mwana-Kondoo wa Mungu. Ishara hiyo ilitolewa kama njiwa wa mbinguni alipotulia juu ya Yesu na utukufu wa Mungu ukamzunguka. Yohana akanyosha mkono wake akimwelekeza Yesu, na kwa sauti kuu akapaza, "***Tazama, Mwana-Kondoo wa Mungu, aichukuaye dhambi ya ulimwengu!" Yohana 1:29*** **{SRSw 196.4}**

Huduma ya Yohana

Yohana aliwaambia wanafunzi wake kwamba Yesu Ndiye Masihi aliyeahidiwa, Mwokozi wa ulimwengu. Kazi yake ilipokuwa inakaribia mwisho, aliwafundisha wanafunzi wake kumtazama Yesu na kumfuata kama Mwalimu Mkuu. Maisha ya Yohana yalikuwa ya huzuni na kujikana nafsi. Alitangaza kuja kwa mara ya kwanza kwa Kristo lakini hakuruhusiwa kushuhudia miujiza Yake wala kufurahia nguvu aliyodhihirisha. Yesu alipoanza kujidhihirisha kama mwalimu, Yohana alijua kwamba yeye mwenyewe angekufa. Sauti yake ilisikika mara chache, isipokuwa jangwani. Maisha yake yalikuwa ya upweke. Hakuambatana na familia ya baba yake ili kufurahia ushirika wao, bali aliwaacha ili kutimiza utume wake. Makundi makubwa ya watu yalitoka miji na vijiji na kwenda jangwani kusikia maneno ya nabii huyo wa ajabu. Yohana aliweka shoka kwenye shina la mti. Alikemea dhambi bila kuogopa matokeo, na akaandaa njia kwa ajili ya Mwana-Kondoo wa Mungu. **{SRSw 197.1}**

Herode aliathirika alipomsikiliza Yohana akitoa ushuhuda wenye nguvu na wa moja kwa moja, na kwa nia ya ndani aliuliza angefanyaje ili awe mwanafunzi wake. Yohana alijua kwamba Herode alikuwa karibu kumuoa mke wa ndugu yake wakati mume wake alikuwa bado anaishi, naye alimwambia wazi kwamba hilo si halali. Herode hakutaka kujitoa dhabihu yoyote. Alimuoa mke wa ndugu yake, na kwa ushawishi

wake akamkamata Yohana na kumweka gerezani, ingawa alikusudia kumwacha huru baadaye. Akiwa gerezani, Yohana alisikia kupitia wanafunzi wake juu ya kazi kuu za Yesu. Hakuweza kusikia maneno Yake ya neema, lakini wanafunzi wake walimletea habari na kumfariji. Muda mfupi baadaye Yohana alikatwa kichwa kwa ushawishi wa mke wa Herode. Niliona kwamba wanafunzi wa kawaida waliomfuata Yesu, wakishuhudia miujiza Yake na kusikia Maneno ya faraja kutoka kinywani Mwake, walikuwa wakubwa kuliko Yohana Mbatizaji; yaani walikuwa wameinuliwa zaidi na kuheshimiwa zaidi, na walikuwa na furaha zaidi maishani mwao. **{SRSw 197.2}**

Yohana alikuja katika roho na nguvu ya Eliya kutangaza ujio wa kwanza wa Yesu. Nilielekezwa chini ya zama, hadi siku za mwisho na kuona kwamba Yohana aliwakilisha wale watakaotoka katika roho na nguvu ya Eliya kutangaza siku ya ghadhabu na ujio wa pili wa Yesu. **{SRSw 198.1}**

Majaribu

Baada ya ubatizo wa Yesu Yordani, aliongozwa na Roho kwenda nyikani ili kujaribiwa na Shetani. Roho Mtakatifu alikuwa amemwandaa kwa tukio hilo maalum la majaribu makali. Siku arobaini alijaribiwa na Shetani, na katika siku hizo hakula chochote. Kila kitu kilichomzunguka kilikuwa kisichopendeza, kiasi kwamba asili ya mwanadamu ingeweza kusukumwa kukimbia. Alikuwa pamoja na wanyama wa mwituni na Shetani katika mahali pa ukiwa na upweke. Mwana wa Mungu alikuwa amepauka na dhaifu kwa sababu ya kufunga na kuteseka. Lakini njia yake ilikuwa imepangwa, na alipaswa kutimiza kazi aliyokuja kufanya. **{SRSw 198.2}**

Shetani alitumia fursa ya mateso ya Mwana wa Mungu na akajitayarisha kumjaribu kwa majaribu tele na makubwa, akitumaini

kumshinda kwa sababu alikuwa amejinyenyekeza kama mwanadamu. Shetani alikuja na jaribu hili: ***"Ukiwa Ndiwe Mwana wa Mungu, liambie jiwe hili liwe mkate" Luka 4:***3. Alimjaribu Yesu ajidhihirishe kwa kumthibitishia Yeye kuwa Ndiye Masihi kwa kutumia nguvu Zake za Kiungu. Yesu akamjibu kwa upole, ***"Imeandikwa ya kwamba mtu hataishi kwa mkate tu." Luka 4:4*** **{SRSw 198.3}**

Shetani alitaka kubishana na Yesu kuhusu kuwa Mwana wa Mungu. Alirejea hali Yake ya udhaifu na mateso na kujisifu kwamba yeye alikuwa na nguvu kuliko Yesu. Lakini sauti iliyonenwa kutoka mbinguni, ***"Wewe Ndiwe Mwanangu, mpendwa wangu; nimependezwa Nawe." Luka 3:22*** ilitosha kumwimarisha Yesu katika mateso Yake yote. Niliona kwamba Kristo hakuwa na haja ya kumshawishi Shetani kuhusu nguvu Zake au kuwa Mwokozi wa ulimwengu. Shetani alikuwa na ushahidi wa kutosha wa cheo na mamlaka ya Mwana wa Mungu. Kukataa kwake kutii mamlaka ya Kristo kulimfanya atupwe nje ya mbingu. **{SRSw 199.1}**

Shetani, ili kudhihirisha nguvu zake, alimchukua Yesu hadi Yerusalemu na kumweka juu ya kilele cha hekalu, akamjaribu ajitose chini ili athibitishe kuwa ni Mwana wa Mungu. Shetani alikuja na Maneno ya Maandiko yaliyovuviwa: "***kwa maana imeandikwa, Atakuagizia malaika zake wakulinde; na ya kwamba,mikononi mwao watakuchukua, Usije ukajikwaa mguu Wako katika jiwe. Yesu akajibu akamwambia, Imenenwa, Usimjaribu Bwana Mungu wako. Luka 4:10-12.*** Shetani alitaka kumfanya Yesu afikirie huruma ya Baba yake na kuhatarisha maisha Yake kabla ya utimilifu wa utume Wake. Alikuwa na matumaini kwamba mpango wa wokovu ungeshindwa; Lakini mpango huo ulikuwa ulikuwa umesimikwa kwa kina sana usiweze kupinduliwa au kuharibiwa na Shetani. **{SRSw 199.2}**

Kristo ni Ndiye kielelezo kwa Wakristo wote. Wanapojaribiwa au haki zao zinapopingwa, wanapaswa kuvumilia kwa subira. Hawapaswi kumlazimisha Mungu aonyeshe nguvu Zake kwa ajili ya kuwashinda adui zao isipokuwa kwa utukufu Wake. Ikiwa Yesu angejitupa kutoka kwenye kilele cha hekalu, asingemtukuza Baba Yake, kwa maana hakuna ambaye angeshuhudia tendo hilo ila Shetani na malaika wa Mungu. Na ingekuwa ni kumjaribu Bwana, ili kuonyesha uwezo Wake kwa adui yake mwenye uchungu na hasira. Ingekuwa ni kujishusha kwa yule ambaye Yesu alikuja kumshinda. **{SRSw 199.3}**

"Akampandisha juu, akamwonyesha milki zote za ulimwengu kwa dakika moja. Ibilisi akamwambia, Nitakupa Wewe enzi hii yote, na fahari yake, kwa kuwa imo mikononi mwangu, nami humpa yeyote kama nipendavyo. Basi, Wewe ukisujudu mbele yangu yote yatakuwa Yako. Yesu akajibu akamwambia, Imeandikwa, Msujudie Bwana Mungu wako, umwabudu Yeye peke yake. Shetani kisha alimwonyesha Yesu falme zote za dunia kwa muda mfupi, akisema angezitoa Kwake ikiwa angemwabudu" Luka 4:5-8 **{SRSw 200.1}**

Shetani aliwasilisha mbele ya Yesu falme za ulimwengu katika nuru yenye kuvutia zaidi. Ikiwa Yesu angemsujudia hapo, alimpa ahadi ya kuachilia madai yake juu ya milki za dunia. Ikiwa mpango wa wokovu ungetekelezwa na Yesu, angekufa ili kumkomboa mwanadamu, Shetani alijua kwamba uwezo wake mwenyewe ungewekewa mipaka na hatimaye ungeondolewa, na kwamba yeye angeangamizwa. Kwa hiyo lilikuwa kusudi lake lililopangwa kwa makini ili kuzuia, kama ingewezekana, kukamilika kwa kazi ile kuu iliyokuwa imeanzishwa na Mwana wa Mungu. Ikiwa mpango wa ukombozi wa mwanadamu ungeshindwa, Shetani angebaki na ufalme ambao wakati huo alikuwa akiudai kuwa wake. Na kama angefanikiwa, alijisifu moyoni mwake kwamba angetawala kwa kumpinga Mungu wa mbinguni. **{SRSw 200.2}**

Mjaribu Akemewa

Shetani alishangilia alipoona Yesu ameacha utukufu Wake na kuondoka mbinguni. Alifikiri kwamba, kwa jinsi hiyo, Mwana wa Mungualiwekwa chini ya uwezo wake. Majaribu yalichukua kwa urahisi sana wanandoa watakatifu katika Edeni kiasi kwamba alitumaini kwa nguvu zake za kishetani na ujanja wa kumpindua hata Mwana wa Mungu, na hivyo kuokoa maisha yake mwenyewe na ufalme. Ikiwa angeweza kumshawishi Yesu aondoke kwenye mapenzi ya Baba Yake, lengo lake lingepatikana. Lakini Yesu aalimkabili mjaribu kwa kumkemea, ***"Nenda nyuma Yangu, Shetani"*** Ilimpaswa kumtii Baba Yake peke yake. **{SRSw 201.1}**

Shetani alidai ufalme wa dunia kuwa wake mwenyewe, na akamfahamisha Yesu kwa njia ya udokezo kwamba mateso Yake yote yangeweza kuepukwa: kwamba asingehitaji kufa ili kupata falme za ulimwengu huu; kwamba kama angekwenda kumsujudia yeye, angeweza kupata mali zote za dunia na utukufu wa kutawala juu yake. Lakini Yesu alibaki imara. Alijua kwamba wakati unakuja ambapo Yeye mwenyewe, kwa maisha Yake mwenyewe, angeukomboa ufalme kutoka kwa Shetani, na kwamba baada ya muda, vyote vilivyo mbinguni na duniani vitamtii. Alichagua maisha Yake ya mateso na kifo Chake cha kutisha kama njia iliyowekwa na Baba Yake, ili aweze kuwa mrithi halali wa falme za dunia na apate kupewa mikononi Mwake kama milki ya milele. Shetani pia atakabidhiwa mikononi Mwake ili aangamizwe kwa kifo, asimsumbue tena Yesu wala watakatifu katika utukufu. **{SRSw 201.2}**

SURA YA 26—HUDUMA YA KRISTO

Baada ya Shetani kumaliza majaribu yake, aliondoka kwa Yesu kwa muda, na malaika wakamwandalia chakula Kristo jangwani na kumtia nguvu, na baraka ya Baba Yake ikatulia juu Yake. Shetani alikuwa ameshindwa katika majaribu yake makali; Hata hivyo alitazamia kwa hamu kipindi cha huduma ya Yesu, wakati ambapo kwa nyakati tofauti angejaribu hila zake dhidi Yake. Bado alitarajia kumshinda kwa kuwachochea wale ambao hawangempokea Yesu, kumchukia na kutafuta kumwangamiza. **{SRSw 202.1}**

Shetani aliitisha baraza maalum pamoja na malaika wake. Walikuwa wamekatishwa tamaa na kuchukizwa kwa kuwa hawakufaulu chochote dhidi ya Mwana wa Mungu. Wakaamua kwamba lazima wawe wajanja zaidi na watumie nguvu zao kikamilifu kuingiza kutokuamini katika akili za taifa Lake mwenyewe kuhusu kuwa Yeye Ndiye Mwokozi wa dunia, na kwa njia hiyo kumkatisha tamaa Yesu katika utume Wake. Haijalishi Wayahudi wangekuwa makini kiasi gani katika ibada na sadaka zao, ikiwa wangefanywa vipofu kuhusu unabii na kuamini kwamba Masihi angekuja kama mfalme Mwenye nguvu wa kidunia, wangeweza kuongozwa kumdharau na kumkataa Yesu. **{SRSw 202.2}**

Nilionyeshwa kwamba Shetani na malaika wake walikuwa na shughuli nyingi wakati wa huduma ya Kristo, wakiwatia watu moyo wa kutokuamini, chuki, na dharau. Mara nyingi Yesu aliposema Ukweli halisi, akiwakemea dhambi zao, watu waliingiwa na hasira. Shetani na

malaika wake waliwachochea wamwue Mwana wa Mungu. Mara nyingi walichukua mawe ili wamrushie, lakini malaika walimlinda na kumwondoa kutoka kwa umati wenye hasira kwenda mahali salama. Tena, Ukweli ulipotoka katika midomo Yake mitakatifu, umati ulimshika na kumpeleka kwenye ukingo wa kilima, wakitaka kumtupa chini. Mabishano yalizuka miongoni mwao juu ya kile walichotaka kumfanyia, na malaika tena, wakamficha asiwaonekane machoni pa wengi, Naye akapita katikati yao akaenda Zake. **{SRSw 202.3}**

Shetani bado alitumaini kwamba mpango mkuu wa wokovu ungeanguka. Alitumia nguvu zake zote kufanya mioyo ya watu iwe migumu na hisia zao kuwa za uchungu dhidi ya Yesu. Alitumaini kwamba wachache sana wangempokea kama Mwana wa Mungu kiasi kwamba angeona mateso na dhabihu Yake kuwa kubwa mno kwa kikundi kidogo kama hicho. Lakini niliona kwamba kama kungekuwa na hata wawili tu ambao wangemkubali Yesu kama Mwana wa Mungu na kumuamini kwa wokovu wa nafsi zao, angetekeleza mpango huo. **{SRSw 203.1}**

Kuondoa Mateso

Yesu alianza kazi Yake kwa kuvunja nguvu ya Shetani juu ya mateso. Aliwaponya wagonjwa, akawapa vipofu kuona, na kuwaponya viwete, na kuwafanya waruke kwa furaha na kumtukuza Mungu. Aliwaponya waliokuwa dhaifu na waliofungwa chini ya nguvu katili ya Shetani kwa miaka mingi. Kwa maneno ya neema aliwafariji waliokuwa dhaifu, wanaotetemeka, na waliokata tamaa. Watu waliokuwa wakiteseka ambao Shetani alikuwa amewashikilia kwa ushindi, Yesu aliwanyang'anya kutoka mikononi mwake, akawapa afya ya mwili na furaha kubwa. Aliwafufua wafu, nao wakamtukuza Mungu kwa uweza Wake mkuu. Alifanya kazi kwa nguvu kwa wote waliomwamini. **{SRSw 203.2}**

Maisha ya Kristo yalijaa maneno na matendo ya wema, huruma na upendo. Daima alikuwa tayari kusikiliza na kupunguza huzuni za waliomjia. Makutano yalibeba ushahidi wa nguvu Yake ya Kiungu. Hata hivyo, baada ya kazi kufanyika, wengi wengi waliona aibu juu ya Mhubiri huyo mnyenyekevu lakini mwenye nguvu. Kwa sababu viongozi hawakumwamini, watu hawakuwa tayari kumkubali Yesu. Alikuwa mtu wa huzuni na Mwenye kujua sikitiko na maumivu. Hawakuweza kuvumilia maisha Yake ya kiasi na kujikana nafsi. Walitaka heshima ya dunia hii. Hata hivyo, wengi walimfuata Mwana wa Mungu na kusikiliza mafundisho Yake, wakifurahia Maneno yaliyotoka kwa neema midomoni Mwake. Maneno Yake yalikuwa yamejaa maana, lakini wazi sana kiasi kwamba walio dhaifu zaidi wangeweza kuyaelewa. **{SRSw 204.1}**

Upinzani Usiofanikiwa

Shetani na malaika wake walipofusha macho na na kutia giza akili za Wayahudi, na kuwachochea viongozi na watawala kutaka kumwua Mwokozi. Wengine walitumwa kumleta Yesu kwao, lakini walipokaribia mahali alipokuwa, walishangaa sana. Walimwona akiwa na huruma na upendo, akiwafariji wanaoteseka. Walimsikia akizungumza kwa upendo na upole kwa waliodhoofika. Pia walimsikia kwa mamlaka akikemea nguvu ya Shetani na kuwaachilia mateka wake. Walivutiwa na hekima ya maneno Yake, na hawakuweza kumkamata. Wakarejea kwa makuhani na wazee bila Yesu. **{SRSw 204.2}**

Walipoulizwa, “Kwa nini hamkumleta?” walieleza miujiza na maneno ya hekima waliyosikia, na wakamalizia kwa kusema: “Hakuna mtu aliyewahi kusema kama huyu Mtu.” Makuhani wakuu waliwadhihaki na kuwashutumu kuwa wamepotoshwa pia, na baadhi ya askari waliona aibu kwa kutomkamata. Makuhani waliuliza kwa dharau kama kuna yeyote wa watawala aliyemwamini. Niliona kwamba wengi

wa viongozi na wazee walimwamini Yesu, lakini Shetani aliwazuia kukiri, kwa sababu waliogopa aibu na makemeo ya watu zaidi kuliko kumwogopa Mungu. **{SRSw 204.3}**

Kufikia sasa hila na chuki ya Shetani havikuvunja mpango wa wokovu. Wakati wa kutimiza kusudi ambalo Yesu alikuja kwa ajili yake ulimwenguni ulikuwa unakaribia. Shetani na malaika wake wakaamua kuwachochea watu Wake Mwenyewe wamwombe damu Yake kwa shauku na wamletee dharau na mateso. Walitumaini kwamba Yesu angekasirika na kushindwa kudumisha unyenyekevu na upole Wake. **{SRSw 205.1}**

Shetani alipokuwa akiweka mipango yake, Yesu alikuwa akiwafungulia wanafunzi Wake mateso ambayo ni lazima apite—kwamba angesulubishwa na kwamba angefufuka tena siku ya tatu. Lakini ufahamu wao ulionekana kuwa mbaya, na hawakuweza kuelewa alichowaambia. **{SRSw 205.2}**

Kugeuka Sura

Imani ya wanafunzi iliimarishwa sana katika tukio la kugeuka sura (transfiguration), walipoona utukufu wa Kristo na kusikia sauti kutoka mbinguni ikishuhudia tabia Yake ya kiungu. Mungu aliamua kuwapa wafuasi wa Yesu uthibitisho imara kwamba Yeye Ndiye Masihi aliyeahidiwa, ili katika huzuni yao na kukata tamaa kwa kusulubiwa Kwake wasipoteze kabisa tumaini lao. Katika kugeuka sura, Bwana alimtuma Musa na Eliya kuzungumza na Yesu kuhusu mateso na kifo Chake. Badala ya kuchagua Malaika wa kuzungumza na Mwana Wake, Mungu alichagua wale waliowahi kupitia majaribu ya dunia. **{SRSw 205.3}**

Eliya alikuwa ametembea na Mungu. Kazi yake ilikuwa ya uchungu na ya majaribu, kwa maana kupitia yeye Bwana alikemea

dhambi za Israeli. Alikuwa nabii wa Mungu, lakini alilazimika kukimbia kutoka sehemu moja hadi nyingine kuokoa maisha yake. Taifa lake mwenyewe lilimwinda kama mnyama wa porini ili kumwangamiza. Lakini Mungu alimchukua Eliya mbinguni bila kuona kifo. Malaika walimbeba kwa utukufu na ushindi hadi mbinguni. **{SRSw 206.1}**

Musa alikuwa mkuu kuliko yeyote aliyeishi kabla yake. Alikuwa ameheshimiwa sana na Mungu, akipewa fursa ya kuzungumza Naye uso kwa uso kama rafiki. Aliruhusiwa kuona nuru angavu na utukufu bora uliomfunika Baba. Bwana kupitia Musa aliwakomboa wana wa Israeli kutoka katika utumwa wa Misri. Musa alikuwa mpatanishi wa watu Wake, mara nyingi akisimama kati yao na ghadhabu ya Mungu. Hasira ya Bwana ilipowaka sana dhidi ya Israeli kwa ajili ya kutokuamini kwao, manung'uniko yao, na dhambi zao kuu, upendo wa Musa kwao ulijaribiwa. Mungu alipendekeza kuwaangamiza na kumfanya kuwa taifa lenye nguvu. Musa alionyesha upendo wake kwa Israeli kwa kusihi kwa bidii kwa niaba yao. Katika dhiki yake alimwomba Mungu aache hasira Yake kali na kuwasamehe Israeli, au kulifuta jina lake katika kitabu Chake. **{SRSw 206.2}**

Musa alipitia kifo, lakini Mikaeli alishuka na kumpa uhai kabla ya mwili wake kuona uharibifu. Shetani alijaribu kuushikilia mwili huo, akidai kuwa ni wake; Lakini Mikaeli alimfufua Musa na kumchukua mbinguni. Shetani alimtukana Mungu kwa uchungu, akimshutumu kuwa dhalimu kwa kuruhusu mawindo yake kuchukuliwa kutoka kwake; Lakini Kristo hakumkemea adui Yake, ingawa ilikuwa ni kwa jaribu lake kwamba mtumishi wa Mungu alikuwa ameanguka. Alimpeleka kwa baba Yake kwa upole, akisema ***"Bwana akukemee."*** **Yuda 1:9** **{SRSw 206.3}**

Yesu alikuwa amewaambia wanafunzi Wake kwamba kuna baadhi yao waliosimama pamoja Naye ambao hawataonja mauti mpaka waone

ufalme wa Mungu ukija kwa nguvu. Katika kugeuka sura ahadi hiyo ilitimia. Uso wa Yesu ulibadilika na kung'aa kama jua, mavazi Yake yakawa meupe sana. Musa aliwakilisha wale watakaofufuliwa kutoka kwa wafu wakati wa ujio wa pili wa Yesu, na Eliya ambaye alinyakuliwa bila kuona kifo aliwakilisha wale watakaonyakuliwa bila kuona kifo. Wanafunzi waliuona kwa mshangao na kuogopa ukuu wa Yesu na wingu lililowafunika, na kusikia sauti ya Mungu katika ukuu wa kutisha, ikisema: "***Huyu ni Mwanangu mpendwa; msikieni Yeye***." **{SRSw 207.1}**

SURA YA 27—KUSALITIWA KWA KRISTO

Nilipelekwa katika zama za nyuma hadi wakati ambapo Yesu alikula mlo wa Pasaka pamoja na wanafunzi Wake. Shetani alikuwa amemdanganya Yuda na kumfanya afikiri kwamba yeye alikuwa mmoja wa wanafunzi wa kweli wa Kristo; lakini moyo wake ulikuwa wa kidunia daima- wa matendo ya kimwili. Alikuwa ameona kazi kuu za Yesu, alikuwa pamoja Naye katika huduma Yake, na alikubali ushahidi mkubwa kwamba Yeye Ndiye Masihi; lakini Yuda alikuwa mchoyo na mwenye tamaa ya mali; alipenda fedha. Alilalamika kwa hasira kuhusu marhamu ya thamani kubwa iliyomiminwa juu ya Yesu. **{SRSw 208.1}**

Mariamu alimpenda Bwana wake. Yesu alikuwa amemsamehe dhambi zake, ambazo zilikuwa nyingi, naye alimfufua ndugu yake aliyempenda sana kutoka kwa wafu, hivyo alihisi kwamba hakuna kitu kilicho cha thamani mno kumtolea Yesu. Kadiri mafuta yenye manukato (marhamu) yalivyokuwa ya thamani zaidi, ndivyo alivyoweza kuonyesha shukrani yake kwa Mwokozi wake kwa kuyatoa Kwake. **{SRSw 208.2}**

Yuda, akitafuta kisingizio cha tamaa yake, alihimiza kwamba mafuta (marhamu) hayo yangeweza kuuzwa na kupewa maskini. Lakini hakusema hivyo kwa sababu alikuwa na huruma kwa maskini; kwa maana alikuwa mbinafsi, na mara nyingi alijichukulia mali kwa matumizi yake mwenyewe sehemu ya mali iliyokuwa imekabidhiwa kwake (kile kilichowekwa mikononi mwake) kwa ajili ya maskini. Yuda

alikuwa hajali faraja na hata matakwa ya Yesu, na ili kuficha tamaa yake mara nyingi alitaja maskini. Kitendo hiki cha ukarimu cha Mariamu kilikuwa kemeo kali sana kwa tabia yake ya kutamani/uchoyo. Hivyo njia ilitengenezwa kwa majaribu ya Shetani kupokelewa kwa urahisi moyoni mwa Yuda. **{SRSw 208.3}**

Makuhani na viongozi wa Wayahudi walimchukia Yesu, lakini umati mkubwa wa watu walimiminika ili kumsikiliza akizungumza maneno ya hekima na kushuhudia matendo Yake makuu. Watu waliguswa sana na kuvutiwa na kumfuata Yesu kwa hamu kubwa ili kusikia mafundisho ya Mwalimu huyo wa ajabu. Wengi wa viongozi walimwamini, lakini hawakuthubutu kukiri imani yao, wasije wakaondolewa ushirika wa sinagogi. Makuhani na wazee wakaamua kwamba lazima wafanye jambo ili kuwageuza watu wasimfuate Yesu. Waliogopa kwamba watu wote wangemwamini. Hawakuona usalama kwao. Iliwapasa kupoteza nafasi zao (nyadhifa zao) au kumwua Yesu. Na hata baada ya kumwua, bado wangekuwepo wale waliokuwa ushahidi hai wa nguvu Zake. **{SRSw 209.1}**

Yesu alikuwa amemfufua Lazaro kutoka kwa wafu, na waliogopa kwamba ikiwa wangemuua Yesu, Lazaro angeushuhudia uweza Wake mkuu. Watu walikuwa wakimiminika kumwona yeye aliyemfufua/aliyefufuliwa kutoka kwa wafu, na viongozi waliamua pia kumuua Lazaro ili kuzima msisimko huo. Kisha wangewageuza watu wafuate mapokeo na mafundisho ya wanadamu, kutoa zaka ya mnanaa na mchicha, na tena wapate ushawishi juu yao. Walikubaliana kumkamata Yesu akiwa peke yake, kwa maana ikiwa wangejaribu kumchukua katika umati wa watu, wakati watu wote wakiwa wamemwelekezea mawazo yao, wangepigwa mawe. **{SRSw 209.2}**

Yuda alijua jinsi walivyokuwa na shauku ya kumpata Yesu na akajitolea kumsaliti kwa makuhani wakuu na wazee kwa vipande

vichache vya fedha. Upendo wake wa pesa ulimfanya akubali kumsaliti Bwana wake mikononi mwa maadui Wake wakubwa. Shetani alikuwa akifanya kazi moja kwa moja kupitia Yuda, na katikati ya tukio la kuvutia la chakula cha jioni cha mwisho, msaliti huyo alikuwa akipanga jinsi ya kumsaliti Mwalimu wake. Yesu kwa huzuni aliwaambia wanafunzi Wake kwamba wote wangemwacha usiku huo kwa sababu Yake. Lakini Petro alisisitiza kwa moyo wote kwamba hata kama wengine wote wangemwacha, yeye hatomwacha. Yesu akamwambia Petro: ***"Shetani amewataka ninyi apate kuwapepeta kama vile ngano; lakini nimekuombea wewe ili imani yako isitindike; nawe utakapoongoka waimarishe ndugu zako." Luka 22:31-32*** **{SRSw 209.3}**

Kwenye Bustani

Nilimwona Yesu akiwa bustanini pamoja na wanafunzi Wake. Kwa huzuni kubwa aliwaamuru waombe na kukesha ili wasije wakaingia katika majaribu. Alijua kwamba imani yao ingepimwa na matumaini yao yangevunjika, na kwamba wangehitaji nguvu yote waliyoweza kupata kwa kukesha na kuomba kwa bidii. Kwa kilio kikuu na machozi, Yesu aliomba: ***"Ee Baba, ikiwa ni mapenzi Yako, uniondolee kikombe hiki; walakini si mapenzi Yangu, bali Yako yatendeke."*** **Luka 22:42** Mwana wa Mungu aliomba kwa uchungu. Matone makubwa ya damu yalitoka usoni Mwake na kudondoka chini. Malaika walikuwa wakizunguka mahali pale wakishuhudia tukio hilo, lakini ni mmoja tu aliyeagizwa kwenda kumtia nguvu Mwana wa Mungu katika uchungu Wake. Hakukuwa na furaha mbinguni. Malaika walitupa taji na vinubi vyao chini, na kwa masikitiko makubwa wakamwangalia Yesu kimya kimya. Walitamani kumzunguka Mwana wa Mungu, lakini malaika wenye mamlaka/uongozi hawakuwaruhusu,

ili wasije wakamkomboa wakati wa kusalitiwa Kwake; kwa maana mpango ulikuwa umewekwa na lazima utimizwe. **{SRSw 210.1}**

Baada ya Yesu kuomba, alikuja kwa wanafunzi Wake, lakini walikuwa wamelala. Katika saa hiyo ya kutisha hakupata huruma wala maombi hata kutoka kwa wanafunzi Wake wenyewe. Petro, ambaye muda mfupi uliopita alikuwa mwenye usongo/ari, alikuwa amelala usingizi mzito. Yesu alimkumbusha maneno yake ya kujitapa na akamwambia: ***Je! Hamkuweza kukesha pamoja Nami hata saa moja?*** **Mathayo 26:40.** Mara tatu Mwana wa Mungu aliomba kwa uchungu. **{SRSw 210.2}**

Yuda Amsaliti Yesu

Kisha Yuda, pamoja na kundi lake la watu wenye silaha, akatokea. Alimkaribia Mwalimu wake kama kawaida yake ili kumsalimia. Kundi lile lilimzunguka Yesu; lakini hapo alidhihirisha uwezo Wake wa Kiungu aliposema: "Je, ni nani mnayemtafuta" "Ni mimi". Wakaanguka nyuma chini. Yesu alifanya hivyo ili waone nguvu Yake na wapate ushahidi kwamba angeweza kujikomboa kama angalitaka. **{SRSw 211.1}**

Wanafunzi walianza kuwa na matumaini walipoona umati huo ukianguka. Waliposimama tena na kumzunguka Mwana wa Mungu, Petro alichomoa upanga wake na kumkata sikio mtumishi wa kuhani mkuu. Yesu alimwamuru aweke upanga wake, akisema: ***"Ama wadhani ya kuwa Mimi siwezi kumsihi Baba Yangu, Naye atanileta sasa hivi zaidi ya majeshi kumi na mawili ya malaika?*** **Mathayo 26:53** Niliona kwamba Maneno haya yalipozungumzwa, nyuso za malaika zilijaa matumaini. Walitamani hapo hapo kumzunguka Kiongozi wao na kuusambaratisha ule umati wenye hasira. Lakini tena huzuni ilitanda juu yao, Yesu aliposema: "***Yatatimizwaje basi maandiko, ya kwamba hivyo ndivyo vilivyopasa kujiri?"*** **Mathayo 26:54** Mioyo ya wanafunzi pia

ilizama kwa kukata tamaa na kukatishwa tamaa kwa uchungu walipomwona Yesu akikubali (akiruhusu) kuchukuliwa na adui Zake. **{SRSw 211.2}**

Wanafunzi walihofia maisha yao wenyewe, na wote wakamwacha na kukimbia. Yesu akaachwa peke yake mikononi mwa umati wa wauaji. Lo, ushindi wa Shetani ulikuwa mkubwa kiasi gani hapo! Na huzuni kubwa kwa malaika wa Mungu! Makundi mengi ya malaika watakatifu, kila kundi likiwa na malaika mkuu mbele yake, walitumwa kushuhudia tukio hilo. Makundi hayo ya malaika yalitumwa ili kurekodi kila tusi na kila tendo la ukatili lililotendwa dhidi ya Mwana wa Mungu, na kila uchungu alioupata Yesu; kwa maana watu wale wale waliohusika katika tukio hili la kutisha watakuja kuuona tena wote kwa macho yao wenyewe-**Ufunuo 1:7.** **{SRSw 211.3}**

SURA YA 28—JARIBIO LA KRISTO

Malaika, walipokuwa wakitoka mbinguni, kwa huzuni waliweka kando taji zao zenye kung'aa. Hawakuweza kuzivaa wakati Kiongozi wao alikuwa akiteseka na kuvikwa taji ya miiba. Shetani na malaika zake walikuwa wakifanya kazi katika jumba la hukumu ili kuharibu hisia na huruma za wanadamu. Angahewa lilikuwa zito na kuchafuliwa na ushawishi wao. Makuhani wakuu na wazee walichochewa nao kumdhihaki na kumtukana Yesu kwa namna ambayo ilikuwa ngumu sana kwa asili ya mwanadamu kuvumilia. Shetani alitumaini kwamba kejeli na vurugu hizo zingemlazimisha Mwana wa Mungu kulalamika au kunung'unika; au kwamba angeonyesha nguvu Yake ya Kiungu na kujitoa mikononi mwa umati, na hivyo mpango wa wokovu kushindwa hatimaye. **{SRSw 213.1}**

Kukana kwa Petro

Petro alimfuata Bwana wake baada ya kusalitiwa Kwake. Alikuwa na hamu ya kuona ni nini kingefanyika kwa Yesu. Lakini aliposhutumiwa kuwa mmoja wa wanafunzi Wake, hofu ya usalama wake ilimfanya aseme kwamba hamjui huyo Mtu. Wanafunzi walijulikana kwa usafi wa lugha yao (yaani kauli/usemi wao wa heshima, Ukweli na ucha Mungu), na Petro, ili kuwathibitishia washtaki wake kwamba yeye si mmoja wa wanafunzi wa Kristo, alikanusha mara ya

tatu kwa laana na viapo. Yesu, aliyekuwa mbali kidogo na Petro, alimgeukia kwa macho ya huzuni na ya kukemea. Ndipo mwanafunzi akakumbuka Maneno aliyosema Yesu orofani, na pia kauli yake ya kujitapa: ***"Wajapochukizwa wote kwa ajili Yako, mimi sitachukizwa kamwe."*** **Mathayo 26:33** Alikuwa amemkana Bwana wake hata kwa laana na viapo; lakini mtupo huo wa jicho laYesu uliulainisha moyo wa Petro na kumwokoa. Alilia kwa uchungu na akatubu dhambi yake kubwa, na akaongoka, na kisha akawa tayari kuwaimarisha ndugu zake. **{SRSw 213.2}**

Katika Jumba la Hukumu

Umati ulikuwa ukipiga kelele wakitaka damu ya Yesu. Walimpiga mijeledi kwa ukatili, wakamvisha vazi la kifalme la rangi ya zambarau la zamani, na wakamvika taji ya miiba kichwani Mwake. Wakamwekea mwanzi mkononi Mwake, wakamsujudia na kumsalimia kwa dhihaka wakisema, ***Salamu! Mfalme wa Wayahudi! Yohana 19:3 Kisha*** wakachukua mwanzi na kumpiga nao kichwani, na miiba ikapenya pajini Mwake, damu ikatiririka usoni na kwenye ndevu Zake. **{SRSw 214.1}**

Ilikuwa vigumu kwa malaika kuvumilia wakati wa kuona vitendo hivi. Wangemkomboa Yesu, lakini malaika wenye mamlaka wakawazuia, wakisema kwamba fidia kubwa ilikuwa inalipwa kwa ajili ya mwanadamu; Lakini ingekuwa kamili na ingesababisha kifo cha Yeye ambaye alikuwa na nguvu dhidi ya kifo. Yesu alijua kwamba malaika walikuwa wakishuhudia fedheha Yake. Malaika dhaifu au mdogo kabisa, angeweza kuuangusha umati huo mara moja na kumwokoa Yesu. Lakini alijua kwamba kama angeomba kwa Baba Yake malaika, basi wangemwokoa mara moja. Lakini ililazimu kuteswa na watu waovu ili kutimiza mpango wa wokovu. **{SRSw 214.2}**

Yesu alisimama kwa upole na unyenyekevu mbele ya umati wa watu wenye hasira, huku wakimtolea matusi ya kila aina. Walimtema mate usoni Mwake—uso ule ambao siku moja watu watatamani kujificha wasiuone, uso ambao utatoa nuru katika mji wa Mungu na kung'aa zaidi kuliko jua. Kristo hakuwatazama wanadamu waliomkosea kwa jicho la hasira. Walifunika kichwa Chake kwa vazi kuukuu, Wakamfunika macho, kisha wakampiga usoni na kupiga kelele, wakimwuliza-uliza wakisema, ***"Tabiri, ni nani aliyekupiga"? (Luka 22:64)*** Kulikuwa na msisimko mkubwa miongoni mwa malaika. Malaika wangemwokoa mara moja, lakini malaika wao wakuu waliwazuia. **{SRSw 214.3}**

Baadhi ya wanafunzi walikuwa wamepata ujasiri wa kuingia pale Yesu alipokuwa na kushuhudia kesi Yake. Walitarajia kwamba angedhihirisha uwezo Wake wa Kiungu, na kujikomboa kutoka katika mikono ya adui Zake, na kuwaadhibu kwa ukatili. Lakini matumaini yao yalipanda na kushuka kadiri matukio tofauti yalivyotokea. Wakati fulani walitilia shaka, na waliogopa kwamba walikuwa wamedanganywa. Lakini sauti waliyoisikia mlimani wakati wa kubadilika sura na utukufu waliouona uliimarisha imani yao kwamba Yeye ni Mwana wa Mungu. Walikumbuka matukio ambayo walikuwa wameshuhudia, miujiza ambayo walikuwa wamemwona Yesu akifanya katika kuponya wagonjwa, akifungua macho ya vipofu, akifungua masikio ya viziwi, akikemea na kuwafukuza pepo wabaya, akiwafufua wafu na kuwapa uzima, na hata kutuliza upepo na bahari. **{SRSw 215.1}**

Hawakuweza kuamini kwamba angekufa. Walitarajia kwamba bado angeinuka kwa nguvu na kwa sauti Yake ya kuamrisha na kuwatawanya umati huo wa umwagaji damu kama vile alipoingia hekaluni na kuwafukuza wale waliokuwa wakiifanya nyumba ya Mungu kuwa mahali pa biashara, walipokimbia mbele Yake kana kwamba

wanafuatwa na kundi la askari wenye silaha. Wanafunzi walitumaini kwamba Yesu angedhihirisha uwezo Wake na kuwasadikisha wote kwamba alikuwa Mfalme wa Israeli. **{SRSw 215.2}**

Ungamo la Yuda

Yuda alijawa na majuto ya uchungu (makali) na aibu kwa kitendo chake cha hila cha kumsaliti Yesu. Aliposhuhudia mateso ambayo Mwokozi alivumilia, alishindwa. Alikuwa amempenda Yesu lakini alipenda pesa zaidi. Hakuwa amefikiri kwamba Yesu angejiachia Mwenyewe ateseke kwa kukamatwa na umati aliowaongoza. Alitarajia angefanya muujiza na kujikomboa. Lakini alipoona umati wa watu wenye hasira katika jumba la hukumu wakiwa na kiu ya damu, alihisi hatia kubwa. Na ingawa wengi walikuwa wakimshtaki Yesu vikali, Yuda alikimbia mbio katikati ya umati huo akitangaza kwamba alikuwa ametenda dhambi kwa kusaliti damu isiyo na hatia. Aliwapa makuhani pesa walizokuwa wamemlipa na na kuwasihi wamfungue Yesu, akitangaza kwamba hakuwa na hatia kabisa. **{SRSw 216.1}**

Kwa muda mfupi hasira na kuchanganyikiwa kuliwaweka makuhani kimya. Hawakutaka watu wajue kwamba walimlipa mmoja wa wale wanaojiita wafuasi wa Yesu ili amsaliti mikononi mwao. Kumwinda kwao Yesu kama mwizi na kumchukua kwa siri, walitaka kujificha. Lakini ungamo la Yuda liliwafichua mbele ya umati wa watu, ikionyesha kwamba ni chuki iliyowafanya wamchukue Yesu. Yuda alipotangaza kwa sauti kubwa kuwa Yesu hana hatia, makuhani wakasema, **“Basi, haya yatupasani sisi? Yaangalie haya wewe mwenyewe.” Mathayo 27:4**. Walikuwa wamemweka Yesu chini ya mamlaka yao, na walikuwa wameazimia kuhakikisha kwamba hatoroki mikononi mwao. Yuda, akiwa amezidiwa na uchungu mwingi, akazitupa zile fedha ambazo sasa alikuwa akizidharau miguuni pa wale waliokuwa

wamemlipa. Kisha, akiwa katika maumivu makali na hofu kuu, akaenda akajinyonga. **{SRSw 216.2}**

Yesu alikuwa na watu wengi wanaomhurumia katika umati wa watu, na kutojibu chochote kwa maswali mengi yaliyoulizwa Kwake kulishangaza umati. Chini ya dhihaka zote na vurugu za umati, Yeye hakukunja uso, wala usemi wenye utata haukuonekana. Yesu alionekana mtulivu na mwenye hadhi (asiyetetereka, wala hakupoteza kuitawala wa nafsi Yake) mbele ya matusi yote. Hakukuwa na hasira wala fadhaa usoni Mwake. Watazamaji walimtazama kwa mshangao. Alionekana kama mfalme kuliko viongozi waliomuhukumu. Walilinganisha umbo Lake kamilifu na uthabiti, wenye heshima na sura ya wale walioketi katika hukumu dhidi Yake, wakaambiana kwamba Yeye ni kama mfalme kuliko viongozi wote. Hakuwa na alama za kuwa mhalifu. Jicho Lake lilikuwa laini, wazi, na lisilo na woga, paji la uso Wake pana na juu. Kila kipengele kiliwekwa alama kwa ukarimu na kanuni bora. Uvumilivu na ustahimilivu Wake ulikuwa tofauti na mwanadamu kiasi kwamba wengi walitetemeka. Hata Herode na Pilato walifadhaika sana katika kutukuka Kwake na uungwana, kama Mungu. **{SRSw 216.3}**

Yesu mbele ya Pilato

Tangu mwanzo, Pilato alikuwa na hakika kwamba Yesu hakuwa mtu wa kawaida. Aliamini kuwa ni mtu bora na asiye na hatia kabisa ya mashtaka yaliyoletwa dhidi Yake. Malaika waliokuwa wakishuhudia tukio hilo waliiona imani ya Gavana wa Kirumi, na kumwokoa asijihusishe na tendo baya la kumtoa Kristo ili asulubiwe, malaika alitumwa kwa mke wa Pilato, na kumpa habari kupitia ndoto kwamba ni Mwana wa Mungu ambaye mume wake alihusika katika kesi Yake, na kwamba alikuwa mteswaji asiye na hatia. Mara moja alituma ujumbe kwa Pilato, akisema kwamba alikuwa ameteseka mambo mengi katika ndoto kwa sababu ya Yesu na kumwonya asifanye chochote kwa mtu

huyo mtakatifu. Mjumbe, akaingia kwa haraka katikati ya umati, akaiweka barua hiyo mikononi mwa Pilato. Alipokuwa akisoma, alitetemeka na kugeuka rangi uso, na mara moja akaamua kutokufanya lolote juu ya kumuua Kristo. Kama Wayahudi wangetaka damu ya Yesu, asingeshawishika kufanya hivyo, bali angetenda kwa ajili ya kumwokoa. **{SRSw 217.1}**

Apelekwa kwa Herode

Pilato aliposikia kwamba Herode alikuwa Yerusalemu, alifarijika sana, kwa kuwa alitumaini kujikomboa kutoka kwenye jukumu lolote la jaribu na hukumu ya Yesu. Mara moja akamtuma, pamoja na washtaki Wake, kwa Herode. Mtawala huyu alikuwa ameufanya moyo wake kuwa mgumu katika dhambi. Kisa cha mauaji ya Yohana Mbatizaji kilikuwa kimemwachia dhamiri yake doa ambalo hangeweza kujikomboa nalo. Aliposikia habari za Yesu na kazi kuu alizofanya, aliogopa na kutetemeka, akiamini kuwa Yeye ni Yohana Mbatizaji aliyefufuka kutoka kwa wafu. Yesu alipowekwa mikononi mwake na Pilato, Herode aliona tendo hilo kuwa kukiri uwezo wake, mamlaka, na hukumu. Jambo hili lilikuwa na matokeo ya kuwafanya watawala hao wawili kuwa marafiki, ambao hapo awali walikuwa maadui. Herode alifurahi kumuona Yesu akitarajia muujiza ili ajiridhishe. Lakini haikuwa kazi ya Yesu kuridhisha udadisi wa mtu au kutafuta usalama Wake Mwenyewe. Uwezo Wake wa Kiungu, wa miujiza ulipaswa kutekelezwa kwa ajili ya wokovu wa wengine, lakini si kwa niaba Yake mwenyewe. **{SRSw 218.1}**

Yesu hakujibu chochote kwa maswali mengi aliyoulizwa na Herode; Wala hakuwajibu maadui Wake, ambao walikuwa wakimshtaki vikali. Herode alikasirika kwa sababu Yesu hakuonekana kuogopa mamlaka yake, hivyo yeye, pamoja na watu wake wa vita walimdhihaki, wakamkejeli, na kumtusi Mwana wa Mungu. Hata hivyo alistaajabishwa

na sura bora ya uungwana, kama ya Mungu ya Yesu alipoteswa kwa aibu, na, akiogopa kumhukumu, alimtuma tena kwa Pilato. **{SRSw 218.2}**

Shetani na malaika zake walikuwa wakimjaribu Pilato na kujaribu kumwongoza kwenye uharibifu wake mwenyewe. Walimpendekezea kwamba ikiwa asingeshiriki katika kumhukumu Yesu, wengine wangefanya; Umati ulikuwa na kiu ya damu Yake; na kama asingemtoa ili asulubiwe, angepoteza mamlaka yake na heshima ya kidunia, na angeshutumiwa kama muumini juu ya mlaghai. Kwa kuogopa kupoteza nguvu na mamlaka yake, Pilato alikubaliana na kifo cha Yesu. Ijapokuwa aliiweka damu ya Yesu juu ya washitaki Wake, na umati wa watu wakapokea hili, wakipaza sauti na kusema. ***"Damu Yake na iwe juu yetu, na juu ya watoto wetu."*** **Mathayo 27:25** Hata hivyo Pilato hakuwa wazi; Alikuwa na hatia ya damu ya Kristo. Kwa maslahi yake ya ubinafsi, upendo wake wa heshima kutoka kwa watu wakuu wa dunia, alimtoa mtu asiye na hatia kufa. Ikiwa Pilato angefuata imani yake mwenyewe asihusika kabisa na chochote kilichohusu kumhukumu Yesu. **{SRSw 218.3}**

Mwonekano na maneno ya Yesu wakati wa kujaribiwa Kwake yaligusa sana akili za wengi waliokuwepo kwenye tukio hilo. Matokeo ya ushawishi uliotolewa yalionekana wazi baada ya ufufuo Wake. Miongoni mwa wale ambao waliongezwa kwa kanisa, kulikuwa na wengi ambao usadikisho wao ulianzia wakati wa jaribu la Yesu. **{SRSw 219.1}**

Hasira ya Shetani ilikuwa kubwa alipoona kwamba ukatili wote aliokuwa amewaongoza Wayahudi kumtendea Yesu haukumfanya awe na manung'uniko hata kidogo. Ingawa alikuwa amechukua asili ya mwanadamu, alitegemezwa na ujasiri kama wa Mungu, na alibaki kuwa

thabiti katika mapenzi ya Baba Yake na hakuyumba hata kidogo. **{SRSw 219.2}**

SURA YA 29—KUSULUBIWA KWA KRISTO

Kristo, Mwana wa Mungu mpendwa, aliongozwa mbele na kukabidhiwa kwa watu ili asulubiwe. Wanafunzi na waumini kutoka maeneo ya karibu walijiunga na umati uliomfuata Yesu kuelekea Kalvari. Mama Yake Yesu pia alikuwa hapo, akisaidiwa na Yohana, mwanafunzi mpendwa. Moyo wake ulikuwa umejeruhiwa kwa huzuni isiyoelezeka; hata hivyo yeye, pamoja na wanafunzi, walitarajia kwamba tukio hilo la uchungu lingebadilika, na Yesu angeonyesha uwezo Wake, na kujidhihirisha mbele ya adui Zake kama Mwana wa Mungu. Kisha tena moyo wa mama Yake ulizama alipokumbuka maneno ambayo alikuwa amegusia kwa kifupi kuhusu mambo yaliyokuwa yakitendeka siku hiyo. **{SRSw 220.1}**

Yesu alikuwa amepita kidogo tu karibu na lango la nyumba ya Pilato wakati msalaba uliokuwa umeandaliwa kwa Baraba ulipotolewa na kuwekwa juu ya mabega Yake yaliyojeruhiwa na kutokwa na damu. Misalaba pia iliwekwa juu ya wenzake Baraba, waliokuwa wakikabili kifo pamoja na Yesu. Mwokozi alikuwa ameubeba mzigo Wake kwa hatua chache tu, kwa sababu ya kupoteza damu na uchovu mwingi na maumivu, alianguka chini na kuzimia. **{SRSw 220.2}**

Yesu aliporejea kwenye fahamu zake tena, msalaba uliwekwa tena juu ya mabega Yake na akalazimishwa kuendelea mbele. Aliyumba kwa hatua chache, akiwa amebeba mzigo mzito, kisha akaanguka kama mtu aliyekufa. Mwanzoni alidhaniwa kuwa amekufa, lakini baadaye akapata fahamu tena. Makuhani na viongozi hawakuwa na huruma kwa mhanga wao; lakini waliona kwamba haikuwezekana Kwake kubeba kifaa hicho cha mateso zaidi. Wakati walipokuwa wakifikiria la kufanya, Simoni, Mkirene, akiwa anatokea upande mwingine, alikutana na umati, akashikwa kwa msukumo wa makuhani, na akalazimishwa kubeba msalaba wa Kristo. Wana wa Simoni walikuwa wanafunzi wa Yesu, lakini yeye mwenyewe hakuwa amewahi kuungana (kufanya ushirika/kuhusiana) Naye. **{SRSw 220.3}**

Umati mkubwa ulimfuata Mwokozi hadi Kalvari, wengi wakimdhihaki na kumkejeli; lakini wengine walikuwa wakilia na kusimulia sifa Zake. Wale aliowaponya magonjwa mbalimbali, na wale aliowafufua kutoka kwa wafu, walitangaza matendo Yake ya ajabu kwa sauti ya bidii, na kudai kujua kile ambacho Yesu alikuwa amekifanya hata atendewe namna hii, kama mkosaji. Siku chache tu kabla, walikuwa wamemfuata kwa hosana za furaha, na kutikisa matawi ya mitende alipokuwa akiingia Yerusalemu kwa ushindi. Lakini wengi waliokuwa wakipaza sauti ya sifa Zake wakati huo kwa sababu ilikuwa

umashuhuri kufanya hivyo, sasa walijiunga na kilio cha "**Msulubishe! Msulubishe!"** **{SRSw 221.1}**

Kupigiliwa Misumari Msalabani

Walipofika mahali pa kuuawa, watuhumiwa walikuwa wamefungwa kwenye vyombo vya mateso. Wakati wezi wawili walipokuwa wakipambana mikononi mwa wale waliowanyoosha msalabani, Yesu hakupinga kusulubiwa. Mama Yake Yesu alitazama kwa wasiwasi wa uchungu, akitarajia kwamba angefanya muujiza ili kujiokoa. Aliona mikono Yake ikinyooshwa msalabani—mikono ile ya thamani iliyokuwa ikitoa baraka, na iliyokuwa ikinyooshwa mara nyingi kuponya wanadamu wanaoteseka. Na sasa nyundo na misumari vililetwa, na misumari ilipigiliwa kupitia mwili laini na kufungwa msalabani, wanafunzi waliovunjika moyo walimchukua mama wa Kristo kutoka eneo hilo la ukatili. **{SRSw 221.2}**

Yesu hakutoa malalamiko; uso Wake ulibaki mweupe na tulivu, lakini matone makubwa ya jasho yalitokea kwenye paji Lake la uso. Hakukuwa na mkono wa huruma wa kufuta jasho la kifo usoni Mwake, wala maneno ya faraja na uadilifu kusisima Naye. Alikuwa akipitia shinikizo la pekee; na kati ya watu wote hakuna aliyekuwa pamoja Naye. Wakati askari walipokuwa wakifanya kazi yao ya kutisha, na akiwa anavumilia uchungu mwingi zaidi, Yesu aliomba kwa ajili ya adui Zake: "***Baba, uwasamehe, kwa kuwa hawajui watendalo."*** **Luka 23:34** Sala hiyo ya Kristo kwa ajili ya adui Zake iliukumbatia ulimwengu, ikimbeba kila mwenye dhambi anayepaswa kuishi, hadi mwisho wa wakati. **{SRSw 222.1}**

Baada ya Yesu kupigiliwa misumari msalabani, aliinuliwa na watu kadhaa wenye nguvu na kusukumwa kwa jeuri kubwa mahali palipotayarishwa kwa ajili Yake, jambo lililosababisha maumivu makali

sana kwa Mwana wa Mungu. Na sasa tukio la kutisha lilipitishwa: makuhani, viongozi, na waandishi wakaungana na kundi la kumdhihaki na kumkejeli Mwana wa Mungu anayekufa. Wakisema, ***"Kama Wewe Ndiwe mfalme wa Wayahudi, ujiokoe Mwenyewe."*** **Luka 23:37** na wengine kwa dhihaka walirudia-rudia maneno haya kati yao, wakisema, "***Aliponya wengine; hawezi kujiponya Mwenyewe."*** **Marko 15:31** Waheshimiwa wa Hekalu, askari wagumu, mwizi mwovu juu ya msalaba, na wakatili kati ya umati wa watu - wote waliungana katika kumdhihaki na kumtesa Kristo. **{SRSw 222.2}**

Wezi waliopigiliwa pamoja na Yesu waliteseka kama Yeye, lakini mmoja wao alizidi kuwa mgumu na mwenye dharau. Alichukua dhihaka za makuhani, na kumtukana Yesu, akisema, ***Je! Wewe si Kristo? Jiokoe nafsi Yako na sisi. Luka 23:39.*** Mhalifu mwingine hakuwa mhalifu mgumu. Huyu aliposikia maneno ya dharau ya mwenzake katika uhalifu, yeye ***akamjibu akamkemea, akisema, Wewe humwogopi hata Mungu, nawe u katika hukumu iyo hiyo? Nayo ni haki kwetu sisi, kwa kuwa tunapokea malipo tuliyostahili kwa matendo yetu; bali Huyu hakutenda lolote lisilofaa. Luka 23:40-41.*** Kisha, moyo wake ulipomwendea Kristo, nuru ya mbinguni ilifurika akilini mwake. Katika Yesu, aliyependeka, aliyedhihakiwa, na kuning'inia juu ya msalaba, alimwona Mkombozi wake, tumaini lake la pekee, na akamwomba kwa imani ya unyenyekevu. ***"Kisha akasema, Ee Yesu, nikumbuke utakapoingia katika ufalme Wako. Yesu akamwambia, Amin, nakuambia hivi leo, utakuwa pamoja Nami peponi." ,*** [Kwa kuweka koma baada ya neno leo, badala ya baada ya neno nakuambia (wewe), kama katika matoleo ya kawaida, maana ya Kweli ya maandishi ni dhahiri zaidi.] ***utakuwa pamoja Nami peponi."*** **Luka 23:42-43** **{SRSw 222.3}**

Kwa mshangao malaika waliona upendo usio na kikomo wa Yesu, ambaye hata katika mateso makali na uchungu mwingi wa akili na mwili aliwafikiria wengine tu, na kuitia moyo nafsi iliyotubu kuamini. Alipokuwa akimimina uhai Wake katika kifo, aliweka upendo kwa mwanadamu wenye nguvu kuliko kifo. Wengi walioshuhudia matukio hayo pale Kalvari, baadaye waliimarishwa katika imani ya Kristo. **{SRSw 223.1}**

Maadui wa Yesu sasa walingojea kifo Chake kwa tumaini lisilo na subira. Tukio hilo walilowazia lingenyamazisha milele uvumi wa uwezo Wake wa Kiungu na maajabu ya miujiza Yake. Walijidanganya kwamba hawatetemeka tena kwa sababu ya ushawishi Wake. Askari wasio na hisia ambao walikuwa wameunyoosha mwili wa Yesu msalabani, waligawana mavazi Yake kati yao wenyewe, wakagombania vazi moja, ambalo lilifumwa bila mshono. Hatimaye waliamua suala hilo kwa kulipigia kura. Kalamu ya uvuvio ilikuwa imeelezea kwa usahihi tukio hili mamia ya miaka kabla ya kutokea: ***"Kwa maana mbwa wamenizunguka; Kusanyiko la waovu wamenisonga; Wamenizua mikono na miguu. Wanagawanya nguo Zangu, Na vazi Langu wanalipigia kura." Zaburi 22:16, 18*** **{SRSw 223.2}**

Somo Katika Upendo Wa Mwana

Macho ya Yesu yalitangatanga juu ya umati wa watu ambao walikuwa wamekusanyika pamoja ili kushuhudia kifo Chake, na aliona chini ya msalaba Yohana akimsaidia Mariamu, mama wa Kristo-mahali pa kuegemea. Alikuwa amerudi kwenye eneo la kutisha, hakuweza kubaki mbali na mtoto wake. Somo la mwisho la Yesu lilikuwa la upendo wa mwana. Alitazama uso wa huzuni wa mama Yake, na kisha juu ya Yohana; Alisema, akimwambia wa mama: "***Mama, tazama, mwanao." Kisha akamwambia yule mwanafunzi, Mtunze/Tazama, mama yako."*** **Yohana 19:26-27**. Yohana alielewa vyema Maneno ya

Yesu, na dhamana-tumaini takatifu ambalo liliwekwa kwake. Mara moja alimwondoa mama wa Kristo kutoka kwenye eneo la kutisha la Kalvari. Kuanzia saa hiyo alimtunza kama vile mwana mwaminifu, akimpeleka nyumbani kwake. Mfano kamili wa upendo wa mwana kwa mama wa Kristo, unang'aa kwa mng'ao usiofifia na kikomo Katikati ya vizazi. Alipokuwa akivumilia mateso makali zaidi, Yeye hakumsahau mama Yake, lakini alifanya kila kitu kuwa muhimu kwa ajili ya maisha Yake ya baadaye. **{SRSw 224.1}**

Utume wa maisha ya Kristo duniani ulikuwa karibu kutimizwa. Ulimi Wake ulikuwa umekauka, na akasema, “Nina kiu”. Walijaza sifongo kwa siki na nyongo, wakampa anywe; Na alipokwisha kuionja, aliikataa. Na sasa Bwana wa Uzima na Utukufu alikuwa akifa, fidia ya wengi. Ilikuwa ni hisia ya dhambi, ikileta ghadhabu ya Baba juu Yake kama mbadala wa mwanadamu, ambayo ilifanya kikombe alichokunywa kuwa kichungu sana, na kuvunja moyo wa Mwana wa Mungu. **{SRSw 224.2}**

Kama mbadala wa mwanadamu na mdhamini, uovu wa wanadamu uliwekwa juu ya Kristo; Alihesabiwa kuwa mkosaji ili apate kuwakomboa kutokana na laana ya sheria. Hatia ya kila mtoto wa Adamu wa kila zama/kizazi ilikuwa ikiutesa moyo Wake; Na ghadhabu ya Mungu na udhihirisho wa kutisha wa kuchukizwa Kwake kwa sababu ya uovu, ulijaza roho ya Mwanawe kwa mshangao. Kuondolewa kwa uso wa Mungu mbele ya Mwokozi katika saa hii ya uchungu wa hali ya juu kulipenya moyo Wake kwa huzuni ambayo haiwezi kueleweka kikamilifu na mwanadamu. Kila uchungu uliovumiliwa na Mwana wa Mungu juu ya msalaba, matone ya damu yaliyotoka kichwani Mwake, mikono na miguu Yake, mishtuko ya uchungu iliyokuwa kuyumbisha-ikiyumbisha mwili wake, na uchungu usioweza kutamkwa ulioijaza nafsi Yake, kwa uso wa baba Yake kufichwa kutoka Kwake, unaongea

na mwanadamu, ukisema, Ni kwa ajili ya kukupenda wewe kwamba Mwana wa Mungu anakubali kubeba uhalifu-makosa haya mabaya juu Yake; Kwa maana anaharibu milki ya mauti, na anafungua milango ya Paradiso na uzima usioweza kufa. Yeye ambaye alituliza mawimbi ya hasira kwa Neno Lake na kutembea mawimbi yaliyofunikwa na povu, ambayo yalifanya mashetani kutetemeka na ugonjwa kutoweka mbele ya mguso Wake, ambaye aliwafufua wafu na kufungua macho ya vipofu, anajitoa juu ya msalaba kama dhabihu ya mwisho kwa mwanadamu. Yeye, mbeba dhambi, anavumilia adhabu ya mashitaka kwa ajili ya uovu na anakuwa dhambi yenyewe kwa ajili ya mwanadamu. **{SRSw 225.1}**

Shetani, pamoja na majaribu yake makali, aliuharibu moyo wa Yesu. Dhambi, yenye chuki sana mbele Yake, ilirundikwa juu Yake mpaka akaugua chini ya uzito wake. Si ajabu kwamba ubinadamu Wake ulitetemeka katika saa hiyo ya kutisha. Malaika walishuhudia kwa mshangao uchungu wa kukata tamaa wa Mwana wa Mungu, kikubwa zaidi kuliko maumivu Yake ya kimwili, ulikuwa uzito wa dhambi, kiasi kwamba yale maumivu ya pili ya mwili, hakuhisiwa Naye. Majeshi ya Mbinguni yalifunika nyuso zao dhidi ya macho ya kutisha. **{SRSw 225.2}**

Asili isiyo hai ilionyesha huruma kwa Mwanzilishi/Muumba wake aliyetukanwa na kufa. Jua lilikataa kutazama eneo hilo la kutisha. Miale yake iliyojaa, yenye kung'aa ilikuwa ikiangaza dunia wakati wa mchana, ghafla ilionekana kuwa imefutwa. Giza kamili lilifunika msalaba na maeneo yote ya karibu, kama hali ya mazishi. Giza lilidumu kwa masaa matatu kamili. Ilipofika saa tisa, giza la kutisha liliinuka kutoka kwa watu, lakini bado lilimfunika Mwokozi kama vazi. Radi kali zilionekana kurushwa kwake alipokuwa akining'inia juu ya msalaba. Kisha “Yesu akapaza sauti Yake kwa nguvu, Eloi, Eloi, lama sabakthani? Maana yake,

Mungu Wangu, Mungu Wangu, mbona umeniacha? **Marko 15:34.** **{SRSw 226.1}**

Imekwisha

Kwa ukimya watu walikuwa wakitazama mwisho wa tukio hili la kuogofya. Tena jua likiwa liaangaza, lakini msalaba umefunikwa na giza. Ghafla utusitusi unainuliwa kutoka msalabani, na kwa sauti za tarumbeta wazi, ambazo zinaonekana kuvuma wakati wote wa uumbaji, Yesu analia, “Imekwisha.” “Ee Baba, mikononi Mwako naiweka roho Yangu.” Luka 23:46 Nuru ilizunguka msalaba, na uso wa Mwokozi uliangaza kusulubiwa kwa Kristo, na uso Wake ukang’aa kwa utukufu kama jua. Kisha akainamisha kichwa Chake juu ya kifua Chake na kufa. **{SRSw 226.2}**

Wakati ambapo Kristo alikufa, kulikuwa na makuhani wakihudumu katika hekalu karibu ya pazia ambalo lilitenganisha Patakatifu na Patakatifu pa Patakatifu. Ghafla walihisi ardhi ikitetemeka chini yao, na pazia la hekalu, eneo lenye imra lenye nguvu ambalo lilikuwa limefanywa upya kila mwaka, lilipasuliwa kutoka juu hadi chini kwa mkono uleule usio na damu ambao uliandika maneno ya adhabu juu ya kuta za jumba la kifalme la Belshaza. **{SRSw 226.3}**

Yesu hakutoa uhai Wake hadi alipomaliza kazi aliyokuja kuifanya. Naye akasema kwa pumzi Yake “Imekwisha”. Malaika walifurahi Maneno yalipotamkwa, kwa maana mpango mkuu wa ukombozi ulikuwa umetekelezwa kwa ushindi. Kulikuwa na furaha mbinguni kwamba watoto wa Adamu sasa, kupitia maisha ya utii, hatimaye wanaweza kuinuliwa hadi kwenye uwepo wa Mungu. Shetani alishindwa, na alijua kwamba ufalme wake umepotea. **{SRSw 226.4}**

Mazishi ya Yesu

Yohana alishindwa kujua ni hatua gani anapaswa kuchukua kuhusiana na mwili wa bwana wake mpendwa. Alitetemeka kwa wazo la kubebwa na askari wakali na wasio na hisia, na kuwekwa mahali pa kuzikwa kwa aibu. Alijua kuwa hangeweza kupata kibali chochote kutoka kwa mamlaka ya Kiyahudi, na angeweza kutumaini kidogo kutoka kwa Pilato. Lakini Yusufu na Nikodemo walikuja mbele katika dharura hii. Wanaume hawa wote wawili walikuwa wanachama wa Sanhedrini, na walimfahamu Pilato. Wote wawili walikuwa watu wenye mali na ushawishi. Walidhamiria kwamba mwili wa Yesu unapaswa kuwa na mazishi ya heshima. **{SRSw 227.1}**

Yusufu alikwenda kwa Pilato kwa ujasiri, na akaomba kutoka kwake mwili wa Yesu kwa ajili ya mazishi. Kisha Pilato akatoa amri rasmi kwamba mwili wa Yesu apewe Yusufu. Wakati mwanafunzi Yohana alikuwa na wasiwasi na fadhaa juu ya mabaki matakatifu ya bwana wake mpendwa, Yusufu wa Arimathaya alirudi na agizo kutoka kwa gavana; Na Nikodemo, akitarajia matokeo ya mahojiano ya Yusufu na Pilato, alikuja na mchanganyiko wa gharama kubwa wa manemane na udi wa uzito wa kilo mia moja. Watu walioheshimiwa zaidi katika Yerusalemu yote hawangeweza kuonyeshwa heshima zaidi katika kifo kama Bwana alivyoonyeshwa. **{SRSw 227.2}**

Kwa upole na kwa heshima waliondoa kwa mikono yao wenyewe kutoka katika chombo cha mateso, machozi yao ya huruma yakianguka kwa kasi walipotazama umbo Lake lililopondeka na lililochanika, ambapo walimuosha kwa uangalifu na kumsafisha doa lolote la damu. Yusufu alikuwa na kaburi jipya, lililochongwa kwa mawe, ambalo alikuwa akijiwekea kwaajili yake mwenyewe; Lilikuwa karibu na Kalvari, na sasa alitayarisha kaburi hili kwa ajili ya Yesu. Mwili, pamoja na manukato ya kuwekwa na ya kuhifadhi mwili yaliyoletwa na Nikodemo, yalikuwa umefungwa kwa uangalifu katika sanda ya kitani,

na wanafunzi watatu walibeba mzigo wao wa thamani kwenye kaburi jipya, ambalo mwanadamu hakuwahi kulala humo. Huko walinyoosha ile mikono iliyoumizwa vibaya, na kukunja mikono iliyojeruhiwa kwenye kifua kisichokuwa na mapigo ya moyo. Wanawake wa Galilaya walikaribia, ili kuona kwamba yote yalikuwa yamefanywa ambayo yangeweza kufanywa kwa ajili ya umbo lisilo na uhai la Mwalimu wao mpendwa. Kisha wakaona jiwe zito likiviringishwa kwenye mlango wa kaburi, na Mwana wa Mungu akaachwa akiwa amepumzika. Wanawake walikuwa wa mwisho kutoka msalabani, na wa mwisho kutoka kwenye kaburi la Kristo. **{SRSw 227.3}**

Ijapokuwa viongozi wa Kiyahudi walikuwa wametimiza kusudi lao kali la kumuua Mwana wa Mungu, wasiwasi wao haukunyamazishwa, wala wivu wao wa Kristo haukufa. Ikichanganyikana na furaha ya kulipiza kisasi, kulikuwa na hofu iliyokuwapo daima kwamba maiti Yake, iliyolala kwenye kaburi la Yusufu, ingetokea. Kwa sababu hiyo ***"wakasema, Bwana, tumekumbuka kwamba Yule mjanja alisema, alipokuwa akali hai, Baada ya siku tatu nitafufuka. Basi amuru kwamba kaburi lilindwe salama hata siku ya tatu; wasije wanafunzi Wake wakamwiba, na kuwaambia watu, Amefufuka katika wafu; na udanganyifu wa mwisho utapita ule wa kwanza." Mathayo 27:63-64*** Pilato hakutaka Yesu ainuke kama Wayahudi walivyokuwa hawataki, kwamba Yesu ainuke akiwa na uwezo wa kuadhibu hatia ya wale waliomwangamiza, na akaweka kundi la askari wa Kirumi kwa amri ya makuhani. Alisema, ***"Pilato akawaambia, Mna askari; nendeni mkalilinde salama kadiri mjuavyo. Wakaenda, wakalilinda kaburi salama, kwa kulitia lile jiwe muhuri, pamoja na wale askari walinzi.*** **Mathayo 27:65-66 {SRSw 228.1}**

Wayahudi waligundua faida ya kuwa na walinzi kama hao kuzunguka kaburi la Yesu. Waliweka muhuri juu ya jiwe lililofunga kaburi, ili lisisumbuliwe bila ukweli kujulikana, na walichukua tahadhari zote dhidi ya wanafunzi kufanya udanganyifu wowote kuhusu mwili wa Yesu. Lakini mipango yao yote ya Kusulubiwa kwa Kristo na tahadhari zilitumika tu kufanya ushindi wa ufufuo kuwa kamili zaidi na kuthibitisha Ukweli wake kikamilifu. **{SRSw 229.1}**

SURA YA 30—UFUFUO WA KRISTO

Wanafunzi walipumzika siku ya Sabato, wakiomboleza kifo cha Bwana wao, huku Yesu, Mfalme wa utukufu, akiwa amelala kaburini. Usiku ulipozidi kusonga, askari walikuwa wamepangwa kulinda mahali pa kupumzika pa Mwokozi, huku malaika, wasioonekana, wakielea juu ya mahali Patakatifu. Usiku ulizidi kusonga polepole, na kukiwa bado giza, malaika waliokuwa wakiangalia walijua kwamba wakati wa kuachiliwa kwa Mwana mpendwa wa Mungu, Kiongozi wao mpendwa, ulikuwa umekaribia. Walipokuwa wakingojea kwa hisia kali saa ya ushindi Wake, malaika mwenye nguvu alikuja, akiruka haraka kutoka mbinguni. Uso wake ulikuwa kama umeme, na mavazi yake meupe kama theluji. Nuru yake ilitawanya giza kutoka kwenye njia yake na kusababisha malaika waovu, ambao walikuwa wamedai mwili wa Yesu kwa ushindi, kukimbia kwa hofu kutoka kwa mwangaza na utukufu wake. Mmoja wa jeshi la malaika ambaye alikuwa ameshuhudia tukio la kudhalilishwa kwa Kristo, na alikuwa akiangalia mahali Pake pa kupumzika, alijiunga na malaika kutoka mbinguni, na pamoja wakashuka kaburini. Dunia ilitetemeka na kutikisika walipokaribia, na tetemeko kubwa la ardhi likatokea. **{SRSw 230.1}**

Hofu iliwapata walinzi wa Kirumi. Sasa nguvu yao ya kuulinda mwili wa Yesu ilikuwa wapi? Hawakufikiria wajibu wao au kuhusu wanafunzi kumwiba. Huku mwangaza wa malaika ukiangaza pande zote, ukiwa mkali kuliko jua, walinzi hao wa Kirumi walianguka chini kama wafu. Mmoja wa malaika alishika jiwe kubwa na kuliviringisha kutoka mlangoni mwa kaburi na kukaa juu yake. Mwingine aliingia kaburini na kufungua kitambaa (leso) kilichokuwa kichwani mwa Yesu. **{SRSw 230.2}**

"Baba Yako Anakuita"

Kisha malaika kutoka mbinguni, kwa sauti iliyosababisha dunia kutetemeka, akapaaza sauti, "Wewe Mwana wa Mungu, Baba Yako Anakuita! Toka nje." Kifo hakingeweza kumtawala tena. Yesu alifufuka kutoka kwa wafu, mshindi Mwenye ushindi. Kwa mshangao mkuu jeshi la malaika lilitazama tukio hilo. Na Yesu alipotoka kaburini, malaika hao wanaong'aa waliinama chini wakimwabudu na kumsifu kwa nyimbo za ushindi na shangwe. **{SRSw 231.1}**

Malaika wa Shetani walikuwa wamelazimika kukimbia mbele ya mwangaza mkali, unaopenya wa malaika wa mbinguni, na walilalamika kwa uchungu kwa mfalme wao kwamba mawindo yao yalikuwa yamechukuliwa kwa nguvu, na kwamba Yeye ambaye walimchukia sana alikuwa amefufuka kutoka kwa wafu. Shetani na majeshi yake walifurahi kwamba nguvu zao juu ya mwanadamu aliyeanguka zilikuwa zimesababisha Bwana wa uzima kuzikwa kaburini, lakini ushindi wao wa kuzimu ulikuwa mfupi tu. Kwa maana Yesu alipokuwa akitoka gerezani Mwake akiwa mshindi mkuu, Shetani alijua kwamba baada ya muda fulani ni lazima afe, na ufalme wake utamkabidhi Yeye ambaye ulikuwa haki Yake. Aliomboleza na kughadhibika kwamba, licha ya juhudi zake zote, Yesu hakushindwa, bali alikuwa amefungua njia ya wokovu kwa mwanadamu, na yeyote atakayeta, ataweza kutembea ndani Yake na kuokolewa. **{SRSw 231.2}**

Malaika waovu na kiongozi wao walikutana katika baraza, ili kujadili jinsi wanavyoweza kufanya kazi dhidi ya serikali ya Mungu. Shetani aliwaagiza watumishi wake waende kwa makuhani wakuu na wazee. Alisema, "Tulifanikiwa kuwadanganya, tukiwapofusha macho yao na kuifanya mioyo yao kuwa migumu dhidi ya Yesu. Tuliwafanya

waamini kwamba alikuwa mdanganyifu. Walinzi hao wa Kirumi watabeba habari za chuki kwamba Kristo amefufuka.Tuliwaongoza makuhani na wazee kumchukia Yesu na kumwua. Sasa waambieni kwamba ikijulikana kwamba Yesu amefufuka, watapigwa mawe na watu kwa kumuua Mtu asiye na hatia." **{SRSw 231.3}**

Ripoti ya Walinzi wa Kirumi

Wakati jeshi la malaika wa mbinguni lilipoondoka kaburini na mwangaza na utukufu vikatoweka, walinzi wa Kirumi walithubutu kuinua vichwa vyao na kutazama huku na huko. Walijawa na mshangao walipoona kwamba jiwe kubwa lilikuwa limeviringishwa kutoka mlangoni mwa kaburi na kwamba mwili wa Yesu ulikuwa umetoweka. Waliharakisha kwenda mjini kuwajulisha makuhani na wazee kile walichokiona. Wauaji hao waliposikiliza ripoti hiyo ya ajabu, mpauko wa uso ulikaa juu ya kila uso. Hofu na taharuki iliwashika walipofikiria walichofanya. Ikiwa ripoti hiyo ilikuwa sahihi, walikuwa wamepotea. Kwa muda fulani walikaa kimya, wakitazamana nyuso, bila kujua la kufanya au la kusema. Kukubali ripoti hiyo kungekuwa ni kujihukumu wenyewe. Walienda kando kushauriana kuhusu la kufanya. Walifikiri kwamba ikiwa ripoti iliyoletwa na walinzi ingesambazwa miongoni mwa watu, wale waliomuua Kristo wangeuawa kama wauaji Wake. **{SRSw 232.1}**

Iliamuliwa kuwaajiri askari ili kuficha jambo hilo. Makuhani na wazee waliwapa kiasi kikubwa cha pesa, wakisema, ***“Semeni, ya kwamba wanafunzi Wake walikuja usiku, wakamwiba, sisi tulipokuwa tumelala.” Mathayo 28:13***. Na mlinzi alipouliza nini kifanyike nao kwa kulala katika lindo yao, maafisa wa Kiyahudi waliahidi kumshawishi gavana na kuhakikisha usalama wao. Kwa ajili ya pesa, walinzi wa Kirumi waliuza heshima yao na kukubali kufuata ushauri wa makuhani na wazee. **{SRSw 232.2}**

Malimbuko ya Kwanza ya Ukombozi

Yesu, alipokuwa ametundikwa msalabani, alipolia, “Imekwisha”, miamba ilipasuka, nchi ikatetemeka, na baadhi ya makaburi yakafunguka. Alipofufuka akiwa mshindi juu ya kifo na kaburi, huku dunia ikitetemeka na utukufu wa mbingu ukiangaza kuzunguka mahali Patakatifu, wengi wa wafu wenye haki, wakitii wito Wake, walitoka kama mashahidi kwamba alikuwa amefufuka. Watakatifu hao waliopata kibali, waliofufuka walitoka wakiwa wametukuzwa. Walikuwa wateule na watakatifu wa kila kizazi, tangu uumbaji hadi siku za Kristo. Hivyo, wakati viongozi wa Kiyahudi walipokuwa wakitafuta kuficha Ukweli wa ufufuo wa Kristo, Mungu alichagua kuwafufua watu kutoka makaburini mwao ili kushuhudia kwamba Yesu alifufuka, na kutangaza utukufu Wake. **{SRSw 233.1}**

Wale waliofufuka walikuwa tofauti katika kimo na umbo, wengine wakiwa na sura bora zaidi kuliko wengine. Niliarifiwa kwamba wakazi wa dunia walikuwa wakipungua, wakipoteza nguvu na uzuri wao. Shetani ana nguvu ya magonjwa na kifo, na kwa kila kizazi athari za laana zimekuwa zikionekana wazi zaidi, na nguvu ya Shetani inaonekana wazi zaidi. Wale walioishi katika siku za Nuhu na Ibrahimu walifanana na malaika katika umbo, uzuri, haiba na nguvu. Lakini kila kizazi kilichofuata kimekuwa kikizidi kuwa dhaifu na kuathiriwa zaidi na magonjwa, na maisha yao yamekuwa mafupi. Shetani amekuwa akijifunza jinsi ya kuiudhi na kuidhoofisha jamii ya ubinadamu. **{SRSw 233.2}**

Wale waliotoka baada ya ufufuo wa Yesu waliwatokea wengi, wakiwaambia kwamba dhabihu kwa ajili ya mwanadamu ilikuwa imekamilika, kwamba Yesu, ambaye Wayahudi walimsulubisha,

alikuwa amefufuka kutoka kwa wafu; na katika uthibitisho wa maneno yao walitangaza, **"Tumefufuka pamoja Naye."** Walishuhudia kwamba ilikuwa kwa nguvu Zake kuu kwamba walikuwa wameitwa kutoka makaburini mwao. Licha ya ripoti za uwongo zilizosambazwa, ufufuo wa Kristo haungeweza kufichwa na Shetani, malaika zake, au makuhani wakuu; kwa kuwa kundi hili takatifu, lililotolewa kutoka makaburini mwao, lilieneza habari njema na za furaha; pia Yesu alijionyesha kwa wanafunzi Wake wenye huzuni, waliovunjika moyo, akiondoa hofu zao na kuwasababishia furaha na shangwe. **{SRSw 233.3}**

Wanawake Kwenye Kaburi

Asubuhi na mapema ya siku ya kwanza ya juma, kabla hakujawa bado na mwanga, wanawake watakatifu walikuja kaburini, wakileta manukato mazuri ili kuupaka mwili wa Yesu. Waligundua kwamba jiwe zito lilikuwa limeondolewa mlangoni pa kaburi, na mwili wa Yesu haukuwepo. Mioyo yao ilizama ndani yao, na waliogopa kwamba adui zao walikuwa wameuondoa mwili. Ghafla waliwaona malaika wawili wakiwa wamevaa mavazi meupe, nyuso zao zikiwa zimeangaza na kung'aa. Viumbe hawa wa mbinguni walielewa kazi ya wanawake na mara moja wakawaambia kwamba Yesu hakuwepo; alikuwa amefufuka, lakini wangeweza kuona mahali alipokuwa amelala. Wakawaagiza waende wakawaambie wanafunzi Wake kwamba angewatangulia kwenda Galilaya. Kwa hofu na furaha kubwa, wanawake hao walirudi haraka kwa wanafunzi waliokuwa na huzuni na kuwaambia mambo waliyoyaona na kuyasikia. **{SRSw 234.1}**

Wanafunzi hawakuweza kuamini kwamba Kristo alikuwa amefufuka, lakini, pamoja na wanawake walioleta ripoti hiyo, walikimbilia kaburini haraka. Waligundua kwamba Yesu hakuwepo; Waliona nguo Zake za kitani, lakini hawakuweza kuamini habari njema kwamba alikuwa amefufuka kutoka kwa wafu. Walirudi nyumbani,

wakistaajabia walichokuwa wamekiona, pia ripoti waliyoletewa na wanawake. **{SRSw 234.2}**

Lakini Mariamu alichagua kukaa karibu na kaburi, akifikiria alichokuwa amekiona na kuhuzunika kwa wazo kwamba huenda alikuwa amedanganywa. Alihisi kwamba majaribu mapya yalikuwa yakimngojea. Huzuni yake ilirudishwa, na akalia kwa uchungu. Aliinama chini ili kutazama tena ndani ya kaburi, na akaona malaika wawili wamevaa nguo nyeupe. Mmoja alikuwa ameketi mahali kichwa cha Yesu kilikuwa kimelala, mwingine mahali miguu Yake ilikuwa. Walizungumza naye kwa upole na kumuuliza kwa nini alilia. Alijibu, ***"Wamemwondoa Bwana wangu, wala mimi sijui walikomweka." Yohana 20:13.*** **{SRSw 235.1}**

"Usiniguse"

Alipogeuka kutoka kaburini alimwona Yesu amesimama karibu, lakini hakumjua. Alizungumza naye kwa huruma, kujali na upendo mwanana, akiuliza chanzo cha huzuni yake na kumuuliza ni nani alikuwa akimtafuta. Akidhani kwamba Yeye alikuwa mtunza bustani, alimwomba, kama Yeye alikuwa amemchukua Bwana wake, amwambie mahali alipomweka, ili aweze kumchukua. Yesu alizungumza naye kwa sauti Yake ya mbinguni, akisema, “Mariamu!” Alikuwa akifahamu toni ya sauti hiyo tamu, na akajibu haraka, “Bwana!” na katika furaha yake alikuwa karibu kumkumbatia; lakini Yesu akasema, ***“Usinishike; kwa maana sijapaa kwenda kwa Baba. Lakini enenda kwa ndugu Zangu ukawaambie, Ninapaa kwenda kwa Baba Yangu Naye ni Baba yenu, kwa Mungu Wangu Naye ni Mungu wenu.” Yohana 20:17.*** Kwa furaha aliharakisha kwenda kwa wanafunzi Wake akiwa na habari njema. Yesu alipanda haraka kwa Baba Yake kusikia kutoka midomoni Mwake kwamba alikubali dhabihu, na kupokea mamlaka yote mbinguni na duniani. **{SRSw 235.2}**

Malaika kama wingu, walimzunguka Mwana wa Mungu na kuamuru milango ya milele iinuliwe, ili Mfalme wa utukufu aingie. Niliona kwamba Yesu alipokuwa na jeshi hilo angavu la mbinguni, mbele za Mungu, na akiwa amezungukwa na utukufu Wake, Yeye hakuwasahau wanafunzi Wake duniani, lakini alipokea nguvu kutoka kwa Baba Yake, ili aweze kurudi na kuwapa wanafunzi nguvu. Siku hiyo hiyo alirudi na kujionyesha kwa wanafunzi Wake. Aliwaruhusu wamguse, kwa maana alikuwa amepanda kwa Baba Yake na alikuwa amepokea nguvu. **{SRSw 236.1}**

Thomaso Mwenye Mashaka

Wakati huu Thomaso hakuwepo. Naye hakukubali ripoti ya wanafunzi kwa unyenyekevu, lakini kwa uthabiti na kujiamini alithibitisha kwamba hangeamini isipokuwa aweke vidole vyake kwenye alama za misumari na mkono wake ubavuni ambapo mkuki mkali ulichomwa. Katika hili alionyesha ukosefu wa imani kwa ndugu zake. Kama wote wangehitaji ushahidi huo huo, hakuna mtu ambaye angempokea Yesu sasa na kuamini katika ufufuo Wake. Lakini ilikuwa mapenzi ya Mungu kwamba ripoti ya wanafunzi ipokelewe na wale ambao hawakuweza kumuona na kumsikia Mwokozi aliyefufuka. **{SRSw 236.2}**

Mungu hakufurahishwa na kutokuamini kwa Thomaso. Yesu alipokutana tena na wanafunzi Wake, Thomaso alikuwa pamoja nao; na alipomtazama Yesu, aliamini. Lakini alikuwa ametangaza kwamba hataridhika bila ushahidi wa kuhisi, kuongezwa kwenye kuona, na Yesu akampa ushahidi alioutaka. Thomaso alilia, **"Bwana wangu na Mungu wangu!"** Lakini Yesu alimkemea kwa kutokuamini kwake, akisema, **"Wewe, kwa kuwa umeniona, umesadiki; wa heri wale wasioona, wakasadiki." Yohana 20:28, 29.** **{SRSw 236.3}**

Kutoridhika kwa Muuaji wa Kristo

Habari zilipoenea kutoka mji hadi mji na mji hadi mji, Wayahudi nao waliogopa maisha yao na kuficha chuki waliyoipenda na kuithamini dhidi ya wanafunzi. Tumaini lao pekee lilikuwa kusambaza taarifa zao za uongo. Na wale waliotaka uongo huu uwe ndio ukweli waliukubali. Pilato alitetemeka aliposikia kwamba Kristo amefufuka. Hakuweza kutilia shaka ushuhuda uliotolewa, na tangu saa hiyo amani ilimwacha milele. Kwa ajili ya heshima ya kidunia, kwa hofu ya kupoteza mamlaka yake na maisha yake, alimtoa Yesu afe. Sasa alikuwa ameshawishika kabisa kwamba haikuwa tu mtu asiye na hatia ambaye alikuwa na hatia ya damu Yake, bali Mwana wa Mungu. Maisha ya Pilato yalikuwa ya huzuni sana. Kukata tamaa na uchungu vilivunja kila hisia ya matumaini na furaha. Alikataa kufarijiwa na akafa kifo cha kusikitisha zaidi. **{SRSw 237.1}**

Siku Arobaini Pamoja na Wanafunzi

Yesu alikaa na wanafunzi Wake siku arobaini, akiwaletea furaha na furaha ya moyo alipowafunulia kikamilifu zaidi uhalisia wa ufalme wa Mungu. Aliwaagiza kutoa ushuhuda wa mambo waliyoyaona na kuyasikia kuhusu mateso Yake, kifo, na ufufuo, kwamba alikuwa ametoa dhabihu kwa ajili ya dhambi, na kwamba wote wanaotaka waweze kuja Kwake na kupata uzima. Kwa uaminifu wenye upendo mwanana, na kujali kwa dhati aliwaambia kwamba watateswa na kusumbuliwa, lakini wangepata nafuu kwa kukumbuka uzoefu wao na kukumbuka Maneno aliyowaambia. Aliwaambia kwamba Alikuwa ameshinda majaribu ya Shetani na kupata ushindi kupitia majaribu na mateso. Shetani hangeweza kuwa na nguvu zaidi juu Yake, lakini angeleta majaribu yake kuwa ya moja kwa moja zaidi kwao na kwa wote wanaopaswa kuamini katika Jina Lake. Lakini wangeweza kushinda kama alivyoshinda. Yesu alitunukia wanafunzi Wake uwezo wa

kufanya miujiza, na akawaambia kwamba ingawa wanapaswa kuteswa na watu waovu, mara kwa mara angewatuma malaika Zake kuwaokoa; maisha yao hayangeweza kuchukuliwa hadi kazi yao itimizwe; ndipo wangehitajika kutia muhuri kwa damu yao, ushuhuda waliokuwa wameutoa. **{SRSw 237.2}**

Wafuasi Wake wenye wasiwasi walisikiliza mafundisho Yake kwa furaha, wakifurahia kila Neno lililotoka kwenye midomo Yake mitakatifu. Sasa walijua hakika kwamba Yeye alikuwa Mwokozi wa ulimwengu. Maneno Yake yalizama ndani kabisa ya mioyo yao, na walihuzunika kwamba hivi karibuni wanapaswa kutenganishwa na Mwalimu wao wa mbinguni na kisha wasisikie tena Maneno ya kufariji,yenye neema kutoka kwenye midomo Yake. Lakini tena mioyo yao ilipashwa joto kwa upendo na furaha kuu, Yesu alipowaambia kwamba angeenda na kuwaandalia makao makuu na kurudi tena na kuwapokea, ili waweze kuwa pamoja Naye milele. Aliahidi pia kumtuma Mfariji, Roho Mtakatifu, kuwaongoza katika Kweli yote. “**Akainua mikono Yake, akawabariki.” Luka 24:50.** **{SRSw 238.1}**

SURA YA 31—KUPAA KWA KRISTO

Mbingu yote ilikuwa ikingojea saa ya ushindi ambapo Yesu angepanda kwa Baba Yake. Malaika walikuja kumpokea Mfalme wa utukufu na kumpeleka mbinguni kwa ushindi. Baada ya Yesu kuwabariki wanafunzi Wake, alitengwa nao na kuchukuliwa juu. Na alipokuwa akiongoza njia ya kwenda juu, umati wa mateka waliofufuliwa wakati wa ufufuo Wake ulifuata. Umati wa jeshi la mbinguni ulikuwapo, huku kundi kubwa la malaika wasiohesabika-wasio na idadi wakimngojea kuja Kwake mbinguni. **{SRSw 239.1}**

Walipopanda hadi Mji Mtakatifu, malaika waliomsindikiza Yesu walipaza sauti, ***"Inueni vichwa vyenu, enyi malango, Inukeni, enyi malango ya milele, Mfalme wa utukufu Apate kuingia.*** Malaika katika mji walipaza sauti kwa furaha, "***Ni nani Mfalme wa utukufu?*** Malaika waliokuwa wakimsindikiza walijibu kwa ushindi, ***Bwana Mwenye nguvu, hodari Bwana hodari wa vita. Inueni vichwa vyenu, enyi malango, Naam, viinueni, enyi malango ya milele, Mfalme wa utukufu apate kuingia.*** Malaika waliokuwa wakisubiri waliuliza tena, ***Ni nani huyu Mfalme wa utukufu?*** na malaika waliokuwa wakimsindikiza walijibu kwa sauti tamu ya muziki, ***Bwana wa majeshi, Yeye Ndiye Mfalme wa utukufu."*** **Zaburi 24:7-10 "** Na kundi la mbinguni likapita katika mji wa Mungu. **{SRSw 239.2}**

Kisha jeshi lote la mbinguni likamzunguka Kiongozi wao mkuu, na kwa ibada ya kina kirefu, wakainama mbele Yake na kumsujudia na kutupa taji zao zinazometameta miguuni Pake. Kisha wakagusa vinubi vyao vya dhahabu, na kwa sauti tamu za muziki zikaijaza mbingu yote

kwa muziki na nyimbo tele kwa Mwana-Kondoo aliyechinjwa, lakini anaishi tena katika ukuu na utukufu. **{SRSw 239.3}**

Ahadi ya Kurudi

Wakati wanafunzi walipotazama mbinguni kwa huzuni ili kuona mtazamo wa mwisho wa Bwana wao anayepaa, malaika wawili waliovaa mavazi meupe walisimama karibu nao na kuwaambia, wakasema, "***Enyi watu wa Galilaya, mbona mmesimama mkitazama mbinguni? Huyu Yesu aliyechukuliwa kutoka kwenu kwenda juu mbinguni, atakuja jinsi iyo hiyo mlivyomwona akienda Zake mbinguni."*** **Matendo ya Mitume 1:11** Wanafunzi na mama wa Yesu, ambaye pamoja nao walikuwa wameshuhudia kupaa kwa Mwana wa Mungu, walitumia usiku uliofuata wakizungumzia matendo Yake ya ajabu na matukio ya ajabu na ya utukufu yaliyotokea ndani ya muda mfupi. **{SRSw 240.1}**

Hasira ya Shetani

Shetani alishauriana tena na malaika zake, na kwa chuki kali dhidi ya serikali ya Mungu aliwaambia kwamba ingawa alidumisha nguvu na mamlaka yake duniani juhudi zao lazima ziwe na nguvu mara kumi dhidi ya wafuasi wa Yesu. Hawakuwa wamemshinda Kristo chochote lakini lazima wawaangamize wafuasi Wake, ikiwezekana. Katika kila kizazi lazima watafute kuwatega wale ambao wangemwamini Yesu. Aliwaambia malaika Zake kwamba Yesu alikuwa amewapa wanafunzi Wake mamlaka ya kuwakemea na kuwafukuza, na kuwaponya wale waliopaswa kuwatesa. Kisha malaika wa Shetani wakatoka kama simba wanaonguruma, wakitafuta kuwaangamiza wafuasi wa Yesu. **{SRSw 240.2}**

SURA YA 32—PENTEKOSTE

Sura hii imejengwa kwenye Matendo 2:1.

Yesu alipofungua uelewa wa wanafunzi kuhusu maana ya unabii kumhusu Yeye, aliwahakikishia kwamba alipewa mamlaka yote mbinguni na duniani, na akawaamuru waende wakahubiri Injili kwa kila kiumbe- **Mathayo 28:18,19**. Wanafunzi, wakiwa na uamsho wa ghafla wa tumaini lao la zamani kwamba Yesu angechukua mahali Pake juu ya kiti cha enzi cha Daudi huko Yerusalemu, waliuliza, **"Je Bwana, wakati huu ndipo utawarudishia Israeli ufalme?" Matendo 1:6.** Mwokozi aliweka shaka akilini mwao kuhusu mada hiyo kwa kujibu kwamba haikuwa kazi yao **"kujua nyakati au majira, Baba aliyaweka katika mamlaka Yake Mwenyewe." Matendo 1:7.** **{SRSw 241.1}**

Wanafunzi walianza kutumaini kwamba kushuka kwa ajabu kwa Roho Mtakatifu kungewashawishi Wayahudi kumkubali Yesu. Mwokozi hakutaka kuelezea zaidi, kwani alijua kwamba Roho Mtakatifu atakapowajilia kwa kipimo kamili, akili zao zingeangazwa na wataelewa kikamilifu kazi iliyokuwa mbele yao, na kuichukua pale alipoiacha. **{SRSw 241.2}**

Wanafunzi walikusanyika katika chumba cha juu, wakiungana katika maombi na wanawake waumini, pamoja na Mariamu mama Yake Yesu, na pamoja na ndugu Zake. Ndugu hawa, ambao hawakuwa waamini, sasa walikuwa wameimarika kikamilifu katika imani yao kwa

matukio yaliyoambatana na kusulubiwa na kwa ufufuo na kupaa kwa Bwana. Idadi iliyokusanyika ilikuwa kama mia moja na ishirini. **{SRSw 241.3}**

Kushuka kwa Roho Mtakatifu

"***Hata ilipotimia siku ya Pentekoste walikuwako wote mahali pamoja. Kukaja ghafula toka mbinguni uvumi kama uvumi wa upepo wa nguvu ukienda kasi, ukaijaza nyumba yote waliyokuwa wameketi. Kukawatokea ndimi zilizogawanyikana, kama ndimi za moto uliowakalia kila mmoja wao. Wote wakajazwa Roho Mtakatifu, wakaanza kusema kwa lugha nyingine, kama Roho alivyowajalia kutamka.***" **Matendo ya Mitume 2:1-4** Roho Mtakatifu, akichukua umbo la ndimi za moto zilizogawanyika nchani, na kutua juu ya wale waliokusanyika, alikuwa ishara ya kipawa walichopewa cha kuzungumza kwa ufasaha lugha kadhaa tofauti, ambazo hapo awali hawakuzifahamu. Na kuonekana kwa moto kuliashiria bidii watakayokuwa nayo wanapokuwa wakifanya kazi na nguvu ambayo ingeambatana na maneno yao. **{SRSw 242.1}**

Chini ya nuru hii ya mbinguni, maandiko ambayo Kristo alikuwa amewaelezea yalisimama akilini mwao kwa mng'ao mkali na uzuri wa ukweli ulio wazi na wenye nguvu. Pazia lililowazuia kuona mwisho wa kile kilichofutwa sasa lilikuwa limeondolewa, na lengo la utume wa Kristo na asili ya ufalme Wake vilieleweka kwa uwazi kamili. **{SRSw 242.2}**

Katika Nguvu ya Pentekoste

Wayahudi walikuwa wametawanyika karibu kila taifa, na walizungumza lugha mbalimbali. Walikuwa wamesafiri umbali mrefu

hadi Yerusalemu, na walikuwa wamekaa huko kwa muda, ili kubaki katika sherehe za kidini zilizokuwa zikiendelea wakati huo na kuzingatia mahitaji hayo ya kidini. Walipokusanyika, walikuwa wa kila lugha inayojulikana. Tofauti hii ya lugha ilikuwa kikwazo kikubwa kwa kazi za watumishi wa Mungu katika kuchapisha mafundisho ya Kristo hadi sehemu za mwisho za dunia. Kwamba Mungu aujaze upungufu wa mitume kwa njia ya kimuujiza ilikuwa kwa watu uthibitisho kamili wa ushuhuda wa mashahidi hawa wa Kristo. Roho Mtakatifu alikuwa amewafanyia kile ambacho hawangeweza kujifanyia wenyewe katika maisha yao yote; sasa wangeweza kueneza Ukweli wa injili kote, akizungumza kwa usahihi lugha ya wale ambao walikuwa wakiwafanyia kazi. Karama hii ya kimuujiza ilikuwa ushahidi wa juu zaidi ambao wangeweza kuwasilisha kwa ulimwengu kwamba agizo lao lilikuwa na muhuri wa Mbinguni. **{SRSw 242.3}**

"Na walikuwako Yerusalemu Wayahudi wakikaa, watu watauwa, watu wa kila taifa chini ya mbingu. Basi sauti hii iliposikiwa makutano walikutanika, wakashikwa na fadhaa, kwa kuwa kila mmoja aliwasikia wakisema kwa lugha yake mwenyewe. Imekuwaje basi sisi kusikia kila mtu lugha yetu tuliyozaliwa nayo?" Matendo ya Mitume 2:5-6, 8 **{SRSw 243.1}**

Makuhani na viongozi walikasirika sana kwa ufunuo huu wa ajabu, ambao uliripotiwa kote Yerusalemu na vitongojini na hapa, lakini hawakuthubutu kuonyesha chuki uovu wao, kwa kuogopa kujiweka wazi kwa chuki ya watu. Walikuwa wamemuua Bwana, lakini hapa walikuwepo watumishi Wake, watu wasio na elimu wa Galilaya, wakifuatilia utimilifu wa ajabu wa unabii na kufundisha mafundisho ya Yesu kwa lugha zote zilizozungumzwa wakati huo. Walizungumza kwa nguvu za kazi za ajabu za Mwokozi, na kuwafunulia wasikilizaji wao mpango wa wokovu katika rehema na dhabihu ya Mwana wa Mungu.

Maneno yao yaliwasadikisha na kuwabadilisha maelfu waliosikiliza. Mila na ushirikina uliofundishwa na makuhani ulifagiliwa mbali akilini mwao na wakakubali mafundisho safi ya Neno la Mungu. **{SRSw 243.2}**

Hubiri ya Petro

Petro aliwaonyesha kwamba udhihirisho huu ulikuwa utimilifu wa moja kwa moja wa unabii wa Yoeli, ambapo alitabiri kwamba nguvu kama hiyo ingewajia watu wa Mungu ili kuwastahilisha au kuwapa sifa kwa kazi maalum. **{SRSw 244.1}**

Petro alifuatilia ukoo wa Kristo moja kwa moja hadi nyumba ya Daudi yenye heshima. Hakutumia mafundisho yoyote ya Yesu kuthibitisha msimamo Wake wa Kweli, kwa sababu alijua ubaguzi wao ulikuwa mkubwa sana kiasi kwamba haungekuwa na matokeo. Lakini aliwarejelea kwa Daudi, ambaye Wayahudi walimwona kama baba mkuu wa taifa lao. Petro alisema: **{SRSw 244.2}**

"Maana Daudi ataja habari Zake, Nalimwona Bwana mbele yangu siku zote, Kwa kuwa Yuko upande wa mkono wangu wa kuume, nisitikisike. Kwa hiyo moyo wangu ukapendezewa, ulimi wangu ukafurahi; Tena mwili wangu nao utakaa katika matumaini. Kwa maana Hutaiacha roho yangu katika kuzimu; Wala hutamtoa Mtakatifu Wako aone uharibifu." Matendo ya Mitume 2:25-27 **{SRSw 244.3}**

Hapa Petro anaonyesha kwamba Daudi hangeweza kusema kwa kwa kujirejelea yeye mwenyewe, bali kwa hakika ulikuwa unabii kumhusu Yesu Kristo. Daudi alikufa kifo cha kawaida kama watu wengine; kaburi lake, pamoja na mavumbi ya heshima yaliyomo, lilihifadhiwa kwa uangalifu mkubwa hadi wakati huo. Daudi, kama

mfalme wa Israeli, na pia kama nabii, alikuwa ameheshimiwa sana na Mungu. Katika maono ya kinabii alionyeshwa maisha na huduma ya Kristo ya baadaye. Aliona kukataliwa Kwake, kujaribiwa Kwake, kusulubiwa, kuzikwa, kufufuka, na kupaa Kwake. **{SRSw 244.4}**

Daudi alishuhudia kwamba roho ya Kristo haikupaswa kuachwa kuzimu (kaburini), wala mwili Wake haukupaswa kuona uharibifu. Petro anaonyesha utimilifu wa unabii huu katika Yesu wa Nazareti. Mungu alikuwa amemfufua kutoka kaburini, kabla ya mwili Wake kuona uharibifu. Sasa alikuwa Yeye aliyeinuliwa katika mbingu za mbingu. **{SRSw 245.1}**

Katika tukio hilo la kukumbukwa, idadi kubwa ya watu ambao hapo awali walikuwa wamedhihaki wazo la mtu asiyejifanya kama Yesu kuwa Mwana wa Mungu, wakasadikishwa kabisa na Ukweli na kumkubali kama Mwokozi wao. Roho elfu tatu [3000] ziliongezwa kwenye kanisa. Mitume walinena kwa nguvu ya Roho Mtakatifu; na maneno yao hayakuweza kupingwa, kwani yalithibitishwa na miujiza mikubwa, iliyofanywa nao kupitia kumwagwa kwa Roho wa Mungu. Wanafunzi wenyewe walishangazwa na matokeo ya ziara hii, na mavuno ya haraka na mengi ya roho. Watu wote walijawa na mshangao. Wale ambao hawakusalimisha ubaguzi wao na chuki waliingiwa na hofu kubwa kiasi kwamba hawakuthubutu kwa sauti au vurugu kujaribu kuzuia kazi kuu, na, kwa wakati huo, upinzani wao ulikoma. **{SRSw 245.2}**

Hoja za mitume pekee, ingawa zilikuwa wazi na zenye kusadikisha, hazingeondoa chuki ya Wayahudi ambayo ilikuwa imepinga ushahidi mwingi. Lakini Roho Mtakatifu alituma hoja hizo nyumbani kwa nguvu ya Kiungu mioyoni mwao. Zilikuwa kama mishale mikali ya Mwenyezi, ikiwathibitishia hatia yao mbaya ya kumkataa na kumsulubisha Bwana wa utukufu. ***"Walipoyasikia haya wakachomwa mioyo yao,***

wakamwambia Petro na mitume wengine, Tutendeje, ndugu zetu? Petro akawaambia, Tubuni mkabatizwe kila mmoja kwa Jina Lake Yesu Kristo, mpate ondoleo la dhambi zenu, nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu." Matendo ya Mitume 2:37-38 **{SRSw 245.3}**

Petro aliwasisitizia watu waliosadkishwa na Ukweli kwamba walimkataa Kristo kwa sababu walikuwa wamedanganywa na makuhani na watawala; na kama wangeendelea kuwategemea kwa ushauri, na kusubiri viongozi hao wamkiri Kristo kabla hawajathubutu kufanya hivyo, hawangemkubali kamwe. Wanaume hao wenye nguvu, ingawa walikiri utakatifu, walikuwa na tamaa, na walikuwa na matamanio ya ukuu kwa ajili ya utajiri na utukufu wa kidunia. Hawangekuja kwa Kristo kamwe kupokea nuru. Yesu alikuwa ametabiri adhabu mbaya itakayowajia watu hao kwa kutokuamini kwao kugumu, licha ya ushahidi wenye nguvu zaidi waliopewa kwamba Yesu alikuwa Mwana wa Mungu. **{SRSw 246.1}**

Kuanzia wakati huu na kuendelea lugha ya wanafunzi ilikuwa safi, sahili, na sahihi katika neno na lafudhi, iwe walizungumza lugha yao ya asili au lugha ya kigeni. Wanaume hawa wanyenyekevu, ambao hawakuwa wamejifunza katika shule ya manabii, waliwasilisha Ukweli ulioinuliwa na safi, kiasi cha kuwashangaza wale waliousikia. Hawakuweza kuenda kibinafsi hadi sehemu za mwisho za dunia; lakini kulikuwa na watu kwenye karamu kutoka kila pembe ya dunia, na Ukweli uliopokelewa nao ulipelekwa kwenye nyumba zao mbalimbali na kutangazwa/kuchapishwa miongoni mwa watu wao, wakileta roho kwa Kristo. **{SRSw 246.2}**

Somo kwa Siku Zetu

Ushuhuda huu kuhusu kuanzishwa kwa kanisa la Kikristo unatolewa kwetu si tu kama sehemu muhimu ya historia takatifu bali pia

kama somo. Wote wanaokiri Jina la Kristo wanapaswa kusubiri, kukesha, na kuomba kwa moyo mmoja. Tofauti zote zinapaswa kuondolewa, na umoja na upendo mwanana wenye kujali na huruma nyororo kwa kila mmoja kuenea kwa ujumla. Kisha maombi yetu yanaweza kwenda pamoja kwa Baba yetu wa mbinguni kwa imani imara na ya dhati. Kisha tunaweza kusubiri kwa uvumilivu na kutumaini utimilifu wa ahadi. **{SRSw 246.3}**

Jibu linaweza kuja kwa kasi ya ghafla na nguvu nyingi au linaweza kucheleweshwa kwa siku na wiki, na imani yetu ikapata jaribio. Lakini Mungu anajua jinsi na wakati wa kujibu maombi yetu. Ni sehemu yetu ya kazi kujiweka katika uhusiano na njia ya Kiungu/Bwana. Mungu anawajibika kwa sehemu Yake ya kazi. Yeye ni Mwaminifu aliyeahidi. Jambo kubwa na muhimu kwetu ni kuwa na moyo mmoja na nia moja, tukiweka kando wivu wote na uovu, na, kama waombaji wanyenyekevu, kukesha na kusubiri. Yesu, Mwakilishi wetu na Kichwa chetu, Yuko tayari kutufanyia yale aliyofanya kwa ajili ya wale wanaosali na kukesha siku ya Pentekoste. **{SRSw 247.1}**

SURA YA 33—UPONYAJI WA KIWETE

Sura hii imejengwa juu ya Matendo 3 na 4.

Muda mfupi baada ya kushuka kwa Roho Mtakatifu, na mara baada ya msimu wa maombi ya dhati, Petro na Yohana, walipokuwa wakienda hekaluni kuabudu, walimwona kiwete mwenye shida na umaskini, umri wa miaka arobaini, ambaye hakujua maisha mengine zaidi ya maumivu, ugonjwa na udhaifu. Mtu huyu mwenye bahati mbaya alikuwa ametamani kwa muda mrefu kwenda kwa Yesu na kuponywa, lakini alipokuwa karibu hana msaada, na alikuwa mbali na eneo la kazi za Mganga Mkuu. Hatimaye maombi yake ya dhati yaliwafanya watu wema kumpeleka kwenye lango la hekalu. Lakini alipofika hapo aligundua kwamba Mponyaji, ambaye matumaini yake yalikuwa yameelekezwa Kwake, alikuwa ameuawa kikatili. **{SRSw 248.1}**

Kukata tamaa kwake kuliamsha huruma ya wale waliojua ni kwa muda gani alikuwa ametarajia na kutarajia kuponywa na Yesu, na walimleta kila siku hekaluni, ili wapita njia waweze kusukumwa kumpa kitu kidogo ili kupunguza mahitaji yake ya sasa. Petro na Yohana walipopita, aliwaomba msaada. Wanafunzi walimtazama kwa huruma. **“Petro, akimkazia macho, pamoja na Yohana, akasema, Tutazame sisi. Matendo ya Mitume 3:4** “***Mimi sina fedha, wala dhahabu, lakini***

nilicho nacho ndicho nikupacho. Kwa Jina la Yesu Kristo wa Nazareti, simama uende." Matendo ya Mitume 3:6 **{SRSw 248.2}**

Uso wa yule maskini ulikuwa umekunjamana wakati Petro alipotangaza umaskini wake, lakini ukang'aa kwa tumaini na imani huku mwanafunzi akiendelea. ***"Akamshika mkono wa kuume, akamwinua, mara nyayo zake na vifundo vya miguu yake vikatiwa nguvu. Akaondoka upesi akasimama, akaanza kwenda; akaingia ndani ya hekalu pamoja nao, akienda, akiruka-ruka, na kumsifu Mungu. Watu wote wakamwona akienda, akimsifu Mungu. Wakamtambua, ya kuwa yeye ndiye aliyekuwa akiketi na kuomba sadaka penye mlango Mzuri wa hekalu; wakajaa ushangao wakastaajabia mambo yale yaliyompata." Matendo ya Mitume 3:7-10*** **{SRSw 248.3}**

Wayahudi walishangaa kwamba wanafunzi waliweza kufanya miujiza kama ile ya Yesu. Yeye, walidhani, alikuwa amekufa, na walitarajia maonyesho yote ya ajabu kama hayo yangekoma na Yeye. Lakini hapa alikuwa mtu huyu ambaye alikuwa kiwete asiyejiweza kwa miaka arobaini, sasa akifurahia matumizi kamili ya viungo vyake, bila maumivu, na mwenye furaha katika kumwamini Yesu. **{SRSw 249.1}**

Mitume waliona mshangao wa watu, na wakawauliza kwa nini wanapaswa kushangazwa na muujiza ambao walikuwa wameushuhudia, na kuwachukulia kwa hofu kana kwamba ni kwa nguvu zao wenyewe walifanya jambo hili. Petro aliwahakikishia kwamba lilifanyika kupitia sifa za Yesu wa Nazareti, ambaye walikuwa wamemkataa na kumsulubisha, lakini ambaye Mungu alikuwa amemfufua kutoka kwa wafu siku ya tatu. ***"Na kwa imani katika Jina Lake, Jina Lake limemtia nguvu mtu huyu mnayemwona na kumjua; na imani ile iliyo kwake yeye imempatia huyu uzima huu mkamilifu mbele yenu ninyi nyote. Basi sasa, ndugu, najua ya kuwa mliyatenda haya kwa kutokujua kwenu, kama na wakuu wenu walivyotenda. Lakini mambo***

yale aliyohubiri Mungu tangu zamani kwa kinywa cha manabii Wake wote, ya kwamba Kristo Wake atateswa, ameyatimiza hivyo." Matendo ya Mitume 3:16-18 **{SRSw 249.2}**

Baada ya muujiza huu, watu walikusanyika pamoja hekaluni, na Petro akawahutubia katika sehemu moja ya hekalu, huku Yohana akiwahutubia katika sehemu nyingine. Mitume, baada ya kusema waziwazi kuhusu uhalifu mkubwa wa Wayahudi, kwa kumkataa na kumuua Mkuu wa uzima, walikuwa waangalifu wasiwatie wenda-wazimu au kukata tamaa. Petro alikuwa tayari kupunguza ukatili wa hatia yao iwezekanavyo, kwa kudhani kwamba walifanya tendo hilo bila kujua. Aliwatangazia kwamba Roho Mtakatifu alikuwa akiwaita watubu dhambi zao na kuongoka; kwamba hakukuwa na tumaini kwao isipokuwa kwa rehema ya Kristo ambaye walikuwa wamemsulubisha; kwa njia ya imani Kwake tu, dhambi zao zingeweza kufutwa kwa damu Yake. **{SRSw 249.3}**

Kukamatwa na Kushtakiwa kwa Mitume

Huku kuhubiri ufufuo wa Kristo, na kwamba kupitia kifo na ufufuo Wake hatimaye angewafufua wafu wote kutoka makaburini mwao, kuliwasisimua na kuwagusa sana Masadukayo [hawakuamini ufufuo au malaika]. Walihisi kwamba mafundisho yao wanayopenda yalikuwa hatarini na sifa yao iko hatarini. Baadhi ya maafisa wa hekalu, na mkuu wa hekalu, walikuwa Masadukayo. Mkuu wa jeshi, akisaidiwa na Masadukayo kadhaa, aliwakamata mitume hao wawili na kuwaweka gerezani, kwani muda ulikuwa umechelewa sana kwa kesi zao kuchunguzwa usiku huo. **{SRSw 250.1}**

Siku iliyofuata Anasi na Kayafa, pamoja na wakuu wengine wa hekalu, walikutana pamoja kwa ajili ya kesi ya wafungwa, ambao kisha

waliletwa mbele yao. Katika chumba hicho hicho, na mbele ya hao watu, Petro alikuwa amemkana Bwana Wake kwa aibu. Haya yote yalikuja waziwazi mbele ya mwanafunzi huyo alipojitokeza kwa ajili ya kesi yake mwenyewe. Sasa alikuwa na fursa ya kukomboa woga wake mwovu wa zamani. **{SRSw 250.2}**

Kundi lililokuwepo lilikumbuka sehemu ambayo Petro alitenda wakati wa kesi ya Bwana wake, na walijisifu kwa kujidanganya kwamba angeweza kutishwa na tishio la kufungwa na kifo. Lakini Petro aliyemkana Kristo katika saa ya uhitaji Wake mkubwa alikuwa mwanafunzi mwenye msukumo na kujiamini, tofauti sana na Petro aliyekuwa mbele ya Sanhedrini kwa ajili ya kuhojiwa siku hiyo. Sasa alikuwa ameongoka; hakujiamini nafsi yake, na hakuwa tena mwenye kiburi. Alijazwa na Roho Mtakatifu, na kupitia nguvu Zake alikuwa imara kama mwamba, jasiri, lakini mnyenyekevu na mwungwana, katika kumtukuza Kristo. Alikuwa tayari kuondoa doa la uasi wake kwa kuheshimu jina alilokuwa amelikana hapo awali. **{SRSw 250.3}**

Utetezi wa Ujasiri wa Petro

Hadi sasa makuhani walikuwa wameepuka kusulubiwa au kufufuka kwa Yesu kutajwa; lakini sasa, katika kutimiza kusudi lao, walilazimika kumuuliza mshtakiwa, ni kwa nguvu gani walikuwa wamekamilisha uponyaji wa ajabu wa yule mtu dhaifu. Ndipo Petro, akiwa amejawa na Roho Mtakatifu, aliwahutubia makuhani na wazee kwa heshima kamili, na kutangaza: ***"Jueni ninyi nyote na watu wote wa Israeli ya kuwa kwa Jina la Yesu Kristo wa Nazareti, ambaye ninyi mlimsulibisha, na Mungu akamfufua katika wafu, kwa Jina hilo mtu Huyu anasimama ali mzima mbele yenu. Yeye Ndiye Jiwe lile lililodharauliwa na ninyi waashi, nalo limewekwa kuwa Jiwe kuu la pembeni. Wala hakuna wokovu katika Mwingine awaye yote, kwa maana hapana Jina jingine chini ya mbingu walilopewa wanadamu***

litupasalo sisi kuokolewa kwalo." Matendo ya Mitume 4:10-12. **{SRSw 251.1}**

Muhuri wa Kristo ulikuwa juu ya maneno ya Petro, na uso wake uliangazwa na Roho Mtakatifu. Karibu naye, kama shahidi mwenye kusadikisha, alisimama mtu aliyekuwa ameponywa kimiujiza. Kuonekana kwa mtu huyu, ambaye saa chache tu zilizopita alikuwa "mlemavu asiyejiweza", sasa alikuwa amerudishwa katika utimamu wa mwili, na akiwa ameangaziwa kuhusu Yesu wa Nazareti, uliongeza uzito wa ushuhuda kwa maneno ya Petro. Makuhani, watawala, na watu walikuwa kimya. Watawala hawakuwa na uwezo wa kupinga kauli yake. Walilazimika "kusikia kile ambacho hawakutaka kusikia zaidi: Ukweli wa" ufufuo wa Yesu Kristo, na nguvu Yake mbinguni ya kufanya "miujiza kupitia njia ya mitume Wake duniani. **{SRSw 251.2}**

Utetezi wa Petro, ambapo alitangaza kwa ujasiri pale ambapo alizipata nguvu zake, uliwashtua. Alikuwa amerejelea "Jiwe lililowekwa chini ya udhibiti na wajenzi - akimaanisha mamlaka ya "kanisa, ambao wangepaswa kutambua thamani ya Yeye ambaye walimkataa - lakini ambaye hata hivyo alikuwa kichwa au Jiwe kuu la pembeni. Kwa Maneno hayo alimrejelea Kristo moja kwa moja, ambaye alikuwa Jiwe la msingi la kanisa. **{SRSw 252.1}**

Watu walishangazwa na ujasiri wa wanafunzi. Walidhani, kwa sababu walikuwa wavuvi wasio na ujuzi, wangeshangazwa na kuona aibu watakapokabiliwa na makuhani, waandishi, na wazee. Lakini waligundua kwamba walikuwa pamoja na Yesu. Mitume walizungumza kama alivyosema, kwa nguvu ya kusadikisha ambayo iliwanyamazisha wapinzani wao. Ili kuficha kuchanganyikiwa kwao, makuhani na watawala waliamuru mitume wachukuliwe, ili washauriane wao kwa wao. **{SRSw 252.2}**

Wote walikubaliana kwamba haingekuwa na maana kukataa kwamba mtu huyo alikuwa ameponywa kwa nguvu waliyopewa mitume kwa Jina la Yesu aliyesulubiwa. Wangefurahi kuficha muujiza huo kwa uongo; lakini kazi hiyo ilifanyika mchana na mbele ya umati wa watu, na tayari walikuwa wamefahamika kwa maelfu. Walihisi kwamba kazi hiyo lazima ikomeshwe mara moja, au Yesu angejipatia waumini wengi, aibu yao wenyewe ingefuata, na wangehukumiwa na hatia ya kumuua Mwana wa Mungu. **{SRSw 252.3}**

Lakini licha ya nia yao ya kuwaangamiza wanafunzi, hawakuthubutu kufanya mabaya zaidi kuliko kuwatishia adhabu kali zaidi ikiwa wangeendelea kufundisha au kufanya kazi kwa Jina la Yesu. Hapo Petro na Yohana walitangaza kwa ujasiri kwamba kazi yao walikuwa wamepewa na Mungu, na hawakuweza kujizuia kusema mambo ambayo walikuwa wameyaona na kuyasikia. Makuhani wangefurahi kuwaadhibu watu hawa bora na waungwana au mashuhuri kwa uaminifu wao usioyumba kwa wito wao mtakatifu, lakini waliwaogopa watu, "***kwa kuwa watu wote walikuwa wakimtukuza Mungu kwa hayo yaliyotendeka. Matendo ya Mitume 4:21***." Kwa hivyo, kwa vitisho na amri za mara kwa mara, mitume waliachiliwa huru. **{SRSw 253.1}**

SURA YA 34—UAMINIFU KWA MUNGU CHINI YA MATESO

Sura hii imejengwa katika Matendo 5:12-42.

Mitume waliendelea na kazi yao ya rehema na huruma, katika kuwaponya wanadamu walioteseka na katika kumtangaza Mwokozi aliyesulubiwa na kufufuka, kwa nguvu kubwa. Idadi iliongezeka kanisani kila mara kwa ubatizo, lakini hakuna aliyethubutu kujiunga nao ambao hawakuwa wameungana moyo na akili na waumini katika Kristo. Umati wa watu ulikusanyika Yerusalemu, wakiwaleta wagonjwa wao na wale waliosumbuliwa na pepo wachafu. Watesekaji wengi walilazwa mitaani wakati Petro na Yohana walipopita, ili vivuli vyao viwaangukie na kuwaponya. Nguvu ya Mwokozi aliyefufuka ilikuwa imewashukia mitume, nao walifanya ishara na miujiza ambayo kila siku iliongeza idadi ya waumini. **{SRSw 254.1}**

Mambo haya yaliwashangaza sana makuhani na watawala, hasa wale waliokuwa miongoni mwao Masadukayo. Waliona kwamba ikiwa mitume wangeruhusiwa kumhubiri Mwokozi aliyefufuka, na kufanya miujiza kwa Jina Lake, fundisho lao la imani, kwamba hakukuwa na ufufuo wa wafu lingekataliwa na wote, na dhehebu lao lingetoweka hivi karibuni. Mafarisayo waliona kwamba mwelekeo wa mahubiri yao

ungekuwa ni kudhoofisha sherehe za Kiyahudi na kufanya sadaka za dhabihu zisiwe na maana. Jitihada zao za awali za kuwakandamiza wahubiri hawa zilikuwa bure, lakini sasa walihisi wameazimia kuzima msisimko. **{SRSw 254.2}**

Kutolewa na Malaika

Mitume walikamatwa na kufungwa gerezani, na Baraza Sanhedrini iliitwa ili kusikiliza kesi yao. Idadi kubwa ya watu wasomi, pamoja na baraza, waliitwa, na wakashauriana pamoja kuhusu jambo la kufanywa na hawa wasumbufu wa amani. ***"Lakini malaika wa Bwana akafungua milango ya gereza usiku, akawatoa, akasema, Enendeni mkasimame hekaluni mkawaambie watu Maneno yote ya Uzima huu. Nao waliposikia wakaenda alfajiri hekaluni, wakaanza kufundisha" Matendo ya Mitume 5:19-21*** **{SRSw 255.1}**

Wakati mitume walipojitokeza miongoni mwa waumini na kusimulia jinsi malaika alivyowaongoza moja kwa moja kupitia kikosi cha askari waliokuwa wakilinda gereza na kuwaagiza waendelee na kazi ambayo ilikuwa imekatizwa na makuhani na watawala, ndugu walijawa na furaha, shangwe na mshangao. **{SRSw 255.2}**

Makuhani na watawala katika baraza walikuwa wameamua kuwashtaki kwa uasi na kuwashtaki kwa kuwaua Anania na Safira (Matendo 5:1-11), na kula njama ya kuwanyang'anya makuhani mamlaka yao na kuwaua. Waliamini kwamba umati ungefurahi kuchukua jambo hilo mkononi na kulishughulikia kwa kutumia mitume kama walivyomtendea Yesu. Walijua kwamba wengi ambao hawakukubali mafundisho ya Kristo walikuwa wamechoka na utawala

holela wa mamlaka ya Kiyahudi na walikuwa na hamu ya mabadiliko fulani. Ikiwa watu hawa wangependezwa na, kukubali, imani ya mitume, wakimtambua Yesu kama Masihi, waliogopa hasira ya watu wote ingeinuliwa dhidi ya makuhani, ambao wangelazimika kujibu kwa mauaji ya Kristo. Waliamua kuchukua hatua kali kuzuia hili. Hatimaye walituma wafungwa waliodhaniwa kuwa wafungwa wapelekwe mbele yao. Mshangao wao ulikuwa mkubwa walipopata ripoti kwamba milango ya gereza ilipatikana imefungwa vizuri na walinzi walikuwa wamesimama mbele yao, lakini kwamba wafungwa hawakupatikana. **{SRSw 255.3}**

Muda si mrefu ripoti hiyo ilitolewa: "***Watu wale mliowaweka gerezani wako ndani ya hekalu, wamesimama wakiwafundisha watu.***" ***Matendo ya Mitume 5:25*** Ingawa mitume waliokolewa kimiujiza kutoka gerezani, hawakuokolewa kutokana na kuhojiwa na kuadhibiwa. Kristo alikuwa amesema alipokuwa pamoja nao, **"Jihadharini nafsi zenu; maana watawapeleka ninyi mabarazani." Marko 13:9** Mungu alikuwa amewapa ishara ya utunzaji Wake na uhakika wa uwepo Wake kwa kumtuma malaika kwao; sasa ilikuwa jukumu lao kuteseka kwa ajili ya Yesu huyo waliyemhubiri. Watu walichochewa sana na kile walichokuwa wameona na kusikia hata kwa makuhani na watawala na walijua kuwa isingewezekana kuwachochea dhidi ya mitume. **{SRSw 256.1}**

Kesi ya Pili

"***Ndipo yule jemadari akaenda pamoja na watumishi, wakawaleta, lakini si kwa nguvu, kwa maana waliogopa watu wasije wakawapiga kwa mawe. Walipowaleta, wakawaweka katika baraza. Kuhani Mkuu akawauliza, akisema, Je! Hatukuwaamuru ninyi kwa nguvu, msifundishe kwa Jina hili? Nanyi, tazameni, mmeijaza Yerusalemu mafundisho yenu, na mnataka kuileta damu ya Mtu Yule***

juu yetu." Matendo ya Mitume 5:26-28. Hawakuwa tayari kubeba lawama ya kumuua Yesu kama walivyozidisha kilio pamoja na kundi lililokuwa limepotoka kimaadili: **"Damu Yake na iwe juu yetu, na juu ya watoto wetu."** **{SRSw 256.2}**

Petro, pamoja na mitume wengine, walichukua msimamo uleule alioufuata katika kesi yake ya awali: "**Petro na mitume wakajibu, wakisema, Imetupasa kumtii Mungu kuliko wanadamu. Matendo ya Mitume 5:29**." Ni malaika aliyetumwa na Mungu, ndiye aliyewatoa gerezani, na ambaye aliwaamuru kufundisha hekaluni. Kwa kufuata maagizo yake, walikuwa wakitii amri ya Mungu, ambayo ni lazima waendelee kufanya kwa gharama yoyote kwao wenyewe. Petro aliendelea: ***"Mungu wa baba zetu alimfufua Yesu, ambaye ninyi mlimwua mkimtundika katika mti. Mtu Huyo Mungu amemtukuza kwa mkono Wake wa kuume, awe Mkuu na Mwokozi, awape Waisraeli toba na msamaha wa dhambi. Na sisi tu mashahidi wa mambo haya, pamoja na Roho Mtakatifu Ambaye Mungu amewapa wote wamtiio." Matendo ya Mitume 5:30-32*** **{SRSw 256.3}**

Roho wa uvuvio alikuwa juu ya mitume, na washtakiwa wakawa washtaki, wakiwashtaki makuhani na watawala waliounda baraza kwa mauaji ya Kristo. Wayahudi walipatwa na ghadhabu sana kwa hili, kiasi kwamba waliamua, bila kesi yoyote zaidi na bila mamlaka kutoka kwa maafisa wa Kirumi, kuchukua sheria mikononi mwao wenyewe na kuwaua wafungwa. Tayari wakiwa na hatia ya damu ya Kristo, sasa walikuwa na hamu ya kumwaga damu kwa mikono yao katika damu ya mitume Wake. Lakini kulikuwa na mtu mmoja mwenye elimu na cheo cha juu ambaye akili yake safi iliona kwamba hatua hii ya vurugu ingesababisha matokeo mabaya. Mungu alimwinua mtu wa kutoka baraza lao wenyewe ili kuzuia vurugu za makuhani na watawala. **{SRSw 257.1}**

Gamalieli, Mfarisayo msomi na daktari, mtu mwenye sifa kubwa za uadilifu, alikuwa mtu wa tahadhari kubwa, ambaye, kabla ya kuzungumza kwa niaba ya wafungwa, aliomba waondolewe. Kisha akazungumza kwa mawazo mengi na utulivu: "***akawaambia, Enyi waume wa Israeli, jihadharini jinsi mtakavyowatenda watu hawa. Kwa sababu kabla ya siku hizi aliondoka Theuda, akijidai ya kuwa yeye ni mtu mkuu, watu wapata mia nne wakashikamana naye; naye aliuawa na wote waliomsadiki wakatawanyika wakawa si kitu. Baada ya mtu huyo aliondoka Yuda Mgalilaya, siku zile za kuandikiwa orodha, akawavuta watu kadha wa kadha nyuma yake, naye pia akapotea na wote waliomsadiki wakatawanyika. Basi sasa nawaambia, Jiepusheni na watu hawa, waacheni; kwa kuwa shauri hili au kazi hii ikiwa imetoka kwa binadamu, itavunjwa, lakini ikiwa imetoka kwa Mungu hamwezi kuivunja; msije mkaonekana kuwa mnapigana na Mungu.***" ***Matendo ya Mitume 5:35-39*** **{SRSw 257.2}**

Makuhani hawakuweza kujizuia kuona busara/mantiki ya maoni yake; Walilazimika kukubaliana naye, na kwa kusita sana wakawaachilia wafungwa, baada ya kuwapiga kwa fimbo na kuwaadhibu tenana tena wasihubiri tena kwa Jina la Yesu, la sivyo maisha yao yangelipa adhabu ya ujasiri wao. mitume ***"Nao wakatoka katika ile baraza, wakifurahi kwa sababu wamehesabiwa kuwa wamestahili kuaibishwa kwa ajili ya Jina hilo. Na kila siku, ndani ya hekalu na nyumbani mwao, hawakuacha kufundisha na kuhubiri habari njema za Yesu kwamba ni Kristo." Matendo ya Mitume 5:41-42*** **{SRSw 258.1}**

Watesi wa mitume walisumbuka walipoona kutokuwa na uwezo wao wa kuwaangusha mashahidi hawa wa Kristo, ambao walikuwa na imani na ujasiri wa kubadilisha aibu yao kuwa utukufu na maumivu yao kuwa furaha kwa ajili ya Bwana wao, ambaye alikuwa amevumilia aibu

na maumivu mbele yao. Hivyo wanafunzi hawa jasiri waliendelea kufundisha hadharani, na kwa siri katika nyumba za watu binafsi, kwa ombi la wenyeji ambao hawakuthubutu kukiri imani yao hadharani, kwa kuwaogopa Wayahudi. **{SRSw 258.2}**

SURA YA 35—MPANGILIO WA INJILI

Sura hii imejengwa katika Matendo 6:1-7.

"***Hata siku zile wanafunzi walipokuwa wakiongezeka hesabu yao, palikuwa na manung'uniko ya Wayahudi wa Kiyunani juu ya Waebrania kwa sababu wajane wao walisahauliwa katika huduma ya kila siku. Matendo 6:1."*** Wayunani hawa walikuwa wakazi wa nchi zingine, ambapo lugha ya Kigiriki ilizungumzwa. Idadi kubwa zaidi ya waongofu walikuwa Wayahudi waliozungumza Kiebrania; lakini hawa walikuwa wameishi katika Milki ya Kirumi, na walizungumza Kigiriki pekee. Manung'uniko yalianza kuongezeka miongoni mwao kwamba wajane wa Wayunani hawakupewa kwa ukarimu kama wahitaji miongoni mwa Waebrania. Upendeleo au ubaguzi wowote wa aina hii ungekuwa mzito kwa Mungu; na hatua za haraka zilichukuliwa ili kurejesha amani na maelewano kwa waumini. **{SRSw 259.1}**

Roho Mtakatifu alipendekeza njia ambayo mitume wangeweza kupata afueni kuhusu kazi ya kuwagawia maskini, na mizigo kama hiyo, ili waweze kuachwa huru kumhubiri Kristo. Kisha ***"Wale Thenashara***

wakawaita jamii ya wanafunzi, wakasema, Haipendezi sisi kuliacha neno la Mungu na kuhudumu mezani. Basi ndugu, chagueni watu saba miongoni mwenu, walioshuhudiwa kuwa wema, wenye kujawa na Roho, na hekima, ili tuwaweke juu ya jambo hili; na sisi tutadumu katika kuomba na kulihudumia lile Neno." Matendo 6:2-4. Kwa hiyo kanisa liliwachagua watu saba waliojaa imani na hekima ya Roho wa Mungu, ili washughulikie kazi inayohusu jambo hilo. Stefano alichaguliwa kwanza; alikuwa Myahudi kwa kuzaliwa na dini, lakini alizungumza Kigiriki, na alikuwa anafahamu vyema mila na desturi za Wagiriki. Kwa hivyo alichukuliwa kuwa mtu anayefaa zaidi kusimama kama kiongozi na kusimamia ugawaji wa fedha zilizotengwa kwaajili ya wajane, yatima, na maskini wenye sifa. Uteuzi huu uliwafikia wote, na kutoridhika na manung'uniko vilinyamazishwa. **{SRSw 260.1}**

Wale watu saba waliochaguliwa walitengwa kwa ajili ya majukumu yao kwa sala na kuwekewa mikono. Wale waliowekwa wakfu hivyo hawakutengwa kufundisha imani. Kinyume chake, imeandikwa kwamba "**Na Stefano, akijaa neema na uwezo, alikuwa akifanya maajabu na ishara kubwa katika watu. Matendo 6:8**" Mashemashi, walikuwa na sifa kamili za kufundisha ile Kweli. Pia walikuwa watu wenye busara na busara, waliopangwa vizuri kushughulikia kesi ngumu za majaribu, manung'uniko au wivu. **{SRSw 260.2}**

Uteuzi huu wa wanaume kufanya shughuli za kanisa, ili mitume waachwe huru kufanya kazi yao maalum ya kufundisha ile Kweli, ulibarikiwa sana na Mungu. Kanisa lilisonga mbele kwa idadi na nguvu. "***Neno la Mungu likaenea; na hesabu ya wanafunzi ikazidi sana katika Yerusalemu; jamii kubwa ya makuhani wakaitii ile imani." Matendo 6:7*** **{SRSw 260.3}**

Ni muhimu kwamba utaratibu na mfumo uleule uendelezwe kanisani sasa kama ilivyokuwa siku za mitume. Ustawi wa kazi unategemea sana idara zake mbalimbali zinazoendeshwa na watu wenye uwezo, ambao wana sifa za stahiki kwa nafasi zao. Wale waliochaguliwa na Mungu kuwa viongozi katika kazi ya Mungu, wakiwa na usimamizi mkuu wa maslahi ya kiroho ya kanisa, wanapaswa kupewa afueni, kwa kadiri iwezekanavyo, kutokana na wasiwasi na matatizo ya kimwili. Wale ambao Mungu amewaita kuhudumu katika neno na mafundisho wanapaswa kuwa na muda wa kutafakari, kuomba, na kujifunza Maandiko. Utambuzi wao wazi wa kiroho hupunguzwa/huhafifishwa kwa kuingia katika mambo madogo ya biashara na kushughulika na tabia mbalimbali za wale wanaokutana pamoja katika uwezo wa kanisa. Ni sawa kwa mambo yote ya kimwili kuja mbele ya maafisa wanaofaa na kurekebishwa nao. Lakini ikiwa ni wa tabia ngumu kiasi cha kutatanisha hekima yao, wanapaswa kupelekwa kwenye baraza la wale wanaosimamia kanisa zima. **{SRSw 260.4}**

SURA YA 36—KIFO CHA STEFANO

Sura hii imejengwa katika Matendo 6:8 hadi 7:60.

Stefano alikuwa mchapakazi sana katika kazi ya Mungu na alitangaza imani yake kwa ujasiri. **“Lakini baadhi ya watu wa sinagogi lililoitwa sinagogi la Mahuru, na la Wakirene, na la Waiskanderia, na la wale wa Kilikia na Asia, wakaondoka na kujadiliana na Stefano; lakini hawakuweza kushindana na hiyo hekima na huyo Roho aliyesema naye.” Matendo 6:9-10** Wanafunzi hawa wa marabi wakuu walikuwa na uhakika kwamba katika majadiliano ya hadharani wangeweza kupata ushindi kamili dhidi ya Stefano, kwa sababu ya ujinga wake uliodhaniwa. Lakini hakuzungumza tu kwa nguvu za Roho Mtakatifu, lakini ilikuwa wazi kwa mkutano wote mkubwa kwamba pia alikuwa mwanafunzi wa unabii na alijifunza katika mambo yote ya sheria. Alitetea kwa ustadi Ukweli alioutetea, na akawashinda kabisa wapinzani wake. **{SRSw 262.1}**

Makuhani na watawala walioshuhudia udhihirisho wa ajabu wa nguvu iliyoambatana na huduma ya Stefano walikuwa wamejaa chuki kali. Badala ya kukubali uzito wa ushahidi alioutoa, waliamua kumnyamazisha kwa kumuua. **{SRSw 262.2}**

Kwa hivyo walimkamata Stefano na kumleta mbele ya baraza la Sanhedrini kwa ajili ya kesi. **{SRSw 262.3}**

Wayahudi wasomi kutoka nchi jirani waliitwa kwa madhumuni ya kukanusha hoja za mshtakiwa. Sauli, ambaye alikuwa amejitambulisha kama mpinzani mwenye usongo wa mafundisho ya Kristo, na mtesaji wa wote waliomwamini, pia alikuwepo. Mwanamume huyu msomi alichukua sehemu kubwa katika kuongoza watu dhidi ya Stefano. Alileta uzito wa ufasaha na mantiki ya marabi kuibeba katika kesi hiyo, na kuwashawishi watu kwamba Stefano alikuwa akihubiri mafundisho ya udanganyifu na hatari. **{SRSw 262.4}**

Lakini Sauli aliona kuwa Stefano kama mtu mmoja aliyeelimika sana kama yeye mwenyewe, na mtu ambaye alikuwa na uelewa kamili wa kusudi la Mungu katika kueneza injili kwa mataifa mengine. Alimwamini Mungu wa Ibrahimu, Isaka, na Yakobo, na alikuwa amejiimarisha kikamilifu kuhusu mapendeleo ya Wayahudi; lakini imani yake ilikuwa pana, na alijua wakati ulikuwa umefika ambapo waumini wa Kweli hawapaswi kuabudu peke yao katika mahekalu yaliyotengenezwa kwa mikono; lakini, kote ulimwenguni, watu wangeweza kumwabudu Mungu katika Roho na Kweli. Pazia lilikuwa limeanguka kutoka kwa macho ya Stefano, naye akagundua hadi mwisho wa kile kilichofutwa na kifo cha Kristo. **{SRSw 263.1}**

Makuhani na watawala hawafua dafu dhidi ya hekima yake iliyo wazi na tulivu, ingawa walikuwa wakali katika upinzani wao. Waliazimia kumfanya Stefano mfano na, huku wakiridhika na chuki yao

ya kulipiza kisasi, wakawazuia wengine, kwa hofu, wasikubali imani yake. Mashtaka yalipendekezwa dhidi yake kwa njia ya kulazimisha sana. Mashahidi wa uongo waliajiriwa kushuhudia kwamba walikuwa wamemsikia akisema maneno ya kufuru dhidi ya hekalu na sheria. Wakasema, ***"maana tumemsikia akisema kwamba Yesu Huyo Mnazareti atapaharibu mahali hapa, na kuzibadili desturi tulizopewa na Musa." Matendo 6:14*** **{SRSw 263.2}**

Stefano aliposimama ana kwa ana na majaji wake, kujibu kosa la kufuru, mng'ao mtakatifu uliangaza usoni mwake. ***"Watu wote walioketi katika ile baraza wakamkazia macho yao, wakamwona uso wake kuwa kama uso wa malaika." Matendo 6:15*** Wengi waliouona uso uliong'aa wa Stefano walitetemeka na kufunika nyuso zao, lakini kutoamini na chuki na ukaidi wao haukurudishwa nyuma. **{SRSw 263.3}**

Utetezi wa Stefano

Stefano alihojiwa kuhusu Ukweli wa mashtaka dhidi yake, na akajitetea kwa sauti iliyo wazi na ya kusisimua iliyovuma kupitia ukumbi wa baraza. Aliendelea kukariri historia ya watu wateule wa Mungu kwa maneno yaliyofanya mkutano uvutie. Alionyesha ujuzi kamili wa uchumi wa Kiyahudi, na tafsiri yake ya kiroho ambayo sasa imedhihirishwa kupitia Kristo. Alianza na Ibrahimu na kufuatilia historia kutoka kizazi hadi kizazi, akipitia rekodi zote za kitaifa za Israeli hadi Sulemani, akichukua mambo ya kuvutia na kugusa moyo zaidi ili kutetea sababu yake. **{SRSw 264.1}**

Aliweka wazi uaminifu wake kwa Mungu na imani ya Kiyahudi, huku akionyesha kwamba sheria waliyoitegemea kwa ajili ya wokovu haikuwa na uwezo wa kuwalinda Israeli kutokana na ibada ya sanamu. Alimunganisha Yesu Kristo na historia yote ya Kiyahudi. Alirejelea ujenzi wa hekalu na Sulemani, na maneno ya Sulemani na Isaya***: "Ila***

Yeye Aliye juu hakai katika nyumba zilizofanywa kwa mikono.” Matendo 7:48 "Mbingu ni kiti Changu cha enzi, Na nchi ni pa kuwekea miguu Yangu; Ni nyumba gani mtakayonijengea? Asema Bwana, Au ni mahali gani nitakapostarehe? Si mkono Wangu uliofanya haya yote?" Matendo 7:49-50. Mahali pa ibada ya juu zaidi ya Mungu palikuwa mbinguni. **{SRSw 264.2}**

Stefano alipofikia hatua hii, kulikuwa na ghasia miongoni mwa watu. Mfungwa huyu alisoma hatima yake mbele yake. Aliona upinzani uliokutana na maneno yake, ambayo yalikuwa yakisemwa kwa amri ya Roho Mtakatifu. Alijua kwamba alikuwa akitoa ushuhuda wake wa mwisho. Ni wachache wanaosoma hotuba hii ya Stefano wanaithamini ipasavyo. Tukio, wakati na mahali, vinapaswa kukumbukwa ili maneno yake yaeleze umuhimu wake kamili. **{SRSw 264.3}**

Alipomunganisha Yesu Kristo na unabii na kusema kuhusu hekalu kama alivyofanya, kuhani, akiwa ameingiwa na hofu na kutaharuki, alirarua vazi lake. Kitendo hiki kilikuwa ishara kwa Stefano kwamba sauti yake ingenyamazishwa milele hivi karibuni. Ingawa alikuwa katikati ya mahubiri yake, alihitimisha ghafla kwa kujitenga ghafla na mnyororo wa historia, na, akiwageukia majaji wake waliokasirika, akasema, ***“Enyi wenye shingo gumu, msiotahiriwa mioyo wala masikio, siku zote mnampinga Roho Mtakatifu; kama baba zenu walivyofanya, na ninyi ni vivyo hivyo. Ni yupi katika manabii ambaye baba zenu hawakumwudhi? Nao waliwaua wale waliotabiri habari za kuja Kwake yule Mwenye Haki; ambaye ninyi sasa mmekuwa wasaliti Wake, mkamwua; ninyi mlioipokea torati kwa agizo la malaika msiishike. Matendo 7:51-53*** **{SRSw 265.1}**

Kifo cha Shahidi au Mfia Dini

Makuhani na watawala hawa walikuwa na hasira iliyopitiliza na isiyothibitika. Walikuwa zaidi kama wanyama-mwitu wanaowinda wengine kuliko wanadamu. Walimkimbilia Stefano, wakisaga meno. Lakini hakuogopa; Alitarajia hili. Uso wake ulikuwa shwari kwa utulivu, na kung'aa kwa mwanga wa kimalaika. Makuhani waliokasirika na umati wa watu wenye msisimko hawakuwa na hofu yoyote kwake. ***"Lakini yeye akijaa Roho Mtakatifu, akakaza macho yake, akitazama mbinguni, akauona utukufu wa Mungu, na Yesu akisimama upande wa mkono wa kuume wa Mungu. Akasema, Tazama! Naona mbingu zimefunguka, na Mwana wa Adamu amesimama mkono wa kuume wa Mungu." Matendo 7:55-56*** **{SRSw 265.2}**

Tukio la kuwepo kwa kimwili, kuhusu yeye lilififia kutoka kwa maono yake; Milango ya mbinguni ilikuwa wazi, na Stefano, akitazama ndani, aliona utukufu wa nyua za Mungu, na Kristo, kana kwamba amefufuka kutoka kwenye kiti Chake cha enzi, amesimama tayari kumtegemeza mtumishi Wake, ambaye alikuwa karibu kuteseka kwa kuuawa kwa ajili ya Jina Lake. Stefano alipotangaza tukio tukufu lililofunguliwa mbele yake, lilikuwa zaidi ya watesi wake wangeweza kuvumilia. Waliziba masikio yao, ili wasisikie maneno yake, na, wakipiga kelele kwa nguvu, wakamkimbilia kwa hasira pamoja. ***"Wakampiga kwa mawe Stefano, naye akiomba, akisema, Bwana Yesu, pokea roho yangu. Akapiga magoti, akalia kwa sauti kuu, Bwana, usiwahesabie dhambi hii. Akiisha kusema haya akalala- usingizi wa mauti. Matendo 7:59-60*** **{SRSw 265.3}**

Katikati ya uchungu wa kifo hiki cha kikatili zaidi shahidi mwaminifu, kama bwana wake wa Kiungu-mbinguni, aliwaombea wauaji wake. Mashahidi ambao walikuwa wamemshtaki Stefano walitakiwa kurusha mawe ya kwanza. Watu hawa waliweka nguo zao

chini ya miguu ya Sauli, ambaye alikuwa ameshiriki kikamilifu katika mabishano na akakubali kifo cha mfungwa. **{SRSw 266.1}**

Kuuawa kwa Stefano kulifanya hisia kubwa juu ya wote, kwa kugusa mioyo ya wale walioshuhudia. Lilikuwa ni jaribio gumu kwa Kanisa, lakini lilisababisha kuongoka kwa Sauli. Imani, uthabiti, na utukufu wa shahidi haukuweza kuondolewa katika kumbukumbu yake. Alama ya Mungu juu ya uso wake, maneno yake, ambayo yalifika kwenye nafsi ya wote walioyasikia, isipokuwa wale ambao walikuwa wagumu kwa kupinga nuru, yalibaki katika kumbukumbu ya mtazamaji, na kushuhudia Ukweli wa kile alichotangaza. **{SRSw 266.2}**

Hakukuwa na hukumu ya kisheria iliyotolewa kwa Stefano, lakini wenye mamlaka wa Kirumi walihongwa kwa kiasi kikubwa cha pesa ili kutofanya uchunguzi wowote wa kesi hiyo. Sauli alionekana kujazwa na wendawazimu wenye bidii katika eneo la kesi na kifo cha Stefano. Alionekana kukasirishwa na usadikisho wake mwenyewe wa siri kwamba Stefano aliheshimiwa na Mungu wakati ule ule alipovunjiwa heshima wanadamu. **{SRSw 266.3}**

Aliendelea kulitesa Kanisa la Mungu, akiwawinda, akiwakamata majumbani mwao, na kuwapeleka kwa makuhani na watawala kwa ajili ya kufungwa na kufa. Usongo wake katika kuendeleza mateso hayo ilikuwa ni hofu kwa Wakristo wa Yerusalemu. Wenye mamlaka wa Kirumi hawakufanya jitihada za pekee za kusitisha kazi hiyo ya kikatili, ya kifo cha Stefano, walikuwa na wakiwasaidia Wayahudi kwa siri ili kupata kibali chao. **{SRSw 267.1}**

Sauli msomi alikuwa chombo chenye nguvu mikononi mwa Shetani ili kutekeleza uasi wake dhidi ya Mwana wa Mungu; Lakini mwenye nguvu zaidi kuliko Shetani alikuwa amemchagua Sauli kuchukua nafasi ya Stefano aliyeuawa kishahidi-kama mfia dini, na

kufanya kazi na kuteseka kwa ajili ya jina Lake. Sauli alikuwa mtu wa kuheshimiwa sana miongoni mwa Wayahudi, kwa elimu yake na bidii/usongo wake katika kuwatesa waumini. Hakuwa mshiriki wa Baraza la Sanhedrini hadi baada ya kifo cha Stefano, alipochaguliwa katika baraza hilo kwa kuzingatia sehemu aliyokuwa ametenda katika tukio hilo. **{SRSw 267.2}**

SURA YA 37—KUONGOKA KWA SAULI

Sura hii imejengwa katika Matendo 9:1-22.

Akili ya Sauli ilichochewa sana na kifo cha ushindi cha Stefano. Alitikiswa katika chuki yake; Lakini maoni na hoja za makuhani na watawala hatimaye zilimsadikisha kwamba Stefano alikuwa mtu mwenye kukufuru; Kwamba Yesu Kristo ambaye alimhubiri alikuwa tapeli, na kwamba wale wanaohudumu katika ofisi takatifu lazima wawe sahihi. Akiwa mtu wa akili yenye kuazimia na kusudi dhabiti, alikasirika sana katika upinzani wake kwa Ukristo, baada ya kutulia kabisa akilini mwake kwamba maoni ya makuhani na waandishi yalikuwa sahihi. Bidii

yake ilimfanya ajihusishe kwa hiari katika kuwatesa waumini. Alisababisha watu watakatifu kuburutwa mbele ya mabaraza, na kufungwa au kuhukumiwa kifo bila ushahidi wa kosa lolote, isipokuwa imani yao kwa Yesu. Tabia kama hiyo, ingawa ilikuwa katika mwelekeo tofauti, ilikuwa bidii ya Yakobo na Yohana wakati walipoita moto ushuke chini kutoka mbinguni ili kuwaangamiza wale waliodharau na kumdharau bwana wao. **{SRSw 268.1}**

Sauli alikuwa karibu kusafiri hadi Dameski kwa shughuli yake mwenyewe; Lakini alikuwa amedhamiria kutimiza makusudi mawili, kwa kutafuta waumini wote katika Kristo, alipokuwa akienda. Kwa ajili hiyo alipata barua kutoka kwa Kuhani Mkuu ili kuzisoma katika masinagogi, na hizi zilimruhusu kuwakamata wale wote walioshukiwa kuwa waumini wa Yesu, na kuwatuma kwa wajumbe Yerusalemu, huko ili kuhukumiwa na kuadhibiwa. Aliondoka njiani, akiwa amejawa na msukumo na nguvu za kijana aliye mtu mzima na moto wa ari/usongo usiyo sahihi. **{SRSw 268.2}**

Wasafiri waliochoka walipokaribia Dameski, macho ya Sauli yalitulia kwa furaha juu ya ardhi yenye rutuba, bustani nzuri, miti ya matunda, na vijito vya baridi vilivyokuwa vikiendelea kuleta sauti ya kuchuruzika katikati ya vichaka vya kijani kibichi. Iliburudisha sana kutazama tukio kama hilo baada ya safari ndefu na ya kuchosha juu ya jangwe lenye ukiwa. Wakati Sauli, pamoja na wenzake walipokuwa wakitazama na kustaajabu, ghafula nuru juu ya mwangaza wa jua ilimulika pande zote, “***Akaanguka chini, akasikia sauti ikimwambia, Sauli, Sauli, mbona waniudhi? Akasema, U nani Wewe, Bwana? Naye akasema, Mimi Ndimi Yesu unayeniudhi Wewe” Matendo 9:4-5*** **{SRSw 269.1}**

Maono ya Kristo

Tukio lilikuwa mojawapo ya mkanganyiko mkubwa zaidi. Waliokuwa na Sauli waliingiwa na hofu, na karibu kupofushwa na nguvu ya nuru. Walisikia sauti, lakini hawakuona mtu, na kwao wote lilikuwa jambo lisiloleta maana au kueleweka, hakika lilikuwa fumbo. Ila Sauli alilala chini kwenye ardhi, na akayaelewa yale Maneno yaliyozungumzwa na kumwona wazi Mwana wa Mungu. Mtupo mmoja wa jicho kwa Yule Aliyekuwa Mtukufu, uliweka picha kichwani mwake milele juu ya roho ya Myahudi huyu aliyeangushwa chini. Maneno hayo yalimgusa moyoni kwa nguvu ya kutisha. Mafuriko ya nuru yalimwagika juu ya vyumba vyenye giza vya akili yake, na kufichua ujinga wake na makosa yake. Aliona kwamba, japokuwa alijiwazia kuwa alikuwa anamtumikia Mungu kwa bidii katika kuwatesa wafuasi wa Kristo, kwa kweli alikuwa akifanya kazi ya Shetani. **{SRSw 269.2}**

Aliona upumbavu wake katika kuweka imani yake juu ya uhakikisho wa makuhani na watawala, ambao ofisi yao takatifu ilikuwa imewapa ushawishi mkubwa juu ya akili yake na kumfanya aamini kwamba kisa cha ufufuo ilikuwa uzushi wa kijanja au kisanii wa wanafunzi wa Yesu. Sasa kwa kuwa Kristo alifunuliwa kwa Sauli, mahubiri ya Stefano yaliletwa kwa nguvu akilini mwake. Maneno yale ambayo makuhani walikuwa wametamka kufuru, sasa yalionekana kwake kama Ukweli na uhalisia. Katika wakati huo wa nuru ya ajabu akili yake ilitenda kwa kasi ya ajabu. Alifuatilia katika historia ya kinabii na kuona kwamba kukataliwa kwa Yesu na Wayahudi, kusulubishwa Kwake, ufufuo Wake, na kupaa Kwake kumetabiriwa na manabii, na kumthibitisha kuwa Ndiye Masihi aliyeahidiwa. Alikumbuka maneno ya Stefano: ***“Naona mbingu zimefunguka, na Mwana wa Adamu amesimama mkono wa kuume wa Mungu.” (Matendo 7:56),*** na alijua kwamba mtakatifu anayekufa alikuwa ameutazama ufalme wa utukufu. **{SRSw 269.3}**

Ni ufunuo ulioje wa haya yote kwa mtesi wa waumini. Nuru ya wazi lakini ya kutisha ilikuwa imeingia juu ya nafsi yake. Kristo alifunuliwa kwake kama Yule alikuja duniani katika kutimiza utume Wake, akikataliwa, akinyanyaswa, akihukumiwa, na kusulubiwa na wale ambao Alikuja kuwaokoa, na kuwa amefufuka kutoka kwa wafu na kupaa mbinguni. Katika wakati huo wa kutisha alikumbuka kwamba Stefano mtakatifu alikuwa ametolewa dhabihu kwa idhini yake, na kwamba kupitia maisha yake, watakatifu wengi wenye sifa/stahiki walikutana na kifo chao kwa mateso ya kikatili. **{SRSw 270.1}**

"Akatetemeka na kushangaa, akasema, Bwana, Je, unanitaka nifanye nini? Bwana akamwambia, ***Lakini simama, uingie mjini, nawe utaambiwa yakupasayo kutenda." Matendo 9:6*** Hapakuwa na shaka akilini mwake, Sauli alijua kwamba huyu alikuwa Yesu wa Nazareti ambaye alizungumza naye, na kwamba kweli alikuwa Masihi aliyetarajiwa kwa muda mrefu, Faraja na Mkombozi wa Israeli. **{SRSw 270.2}**

Wakati utukufu wenye mng'ao ulipoondolewa, na Sauli akainuka kutoka ardhini, alijikuta amenyimwa kabisa kuona. Mwangaza wa utukufu wa Kristo ulikuwa mkali sana kwa macho yake ya kibinadamu, na wakati ulipoondolewa, giza zito likatanda juu ya macho yake. Aliamini kwamba upofu wake ulikuwa adhabu ya Mungu kwa mateso yake makali dhidi ya wafuasi wa Yesu. Alipapasa-papasa gizani, na wenzake, kwa hofu na mshangao, walimshika mkono hadi Dameski. **{SRSw 271.1}**

Kuelekezwa kwa Kanisa

Jibu la swali la Sauli ni, "***simama, uingie mjini, nawe utaambiwa yakupasayo kutenda***." Yesu akamtuma Myahudi anayeuliza, kanisani

Mwake, ili kupata kutoka kwao ujuzi wa wajibu wake. Kristo alifanya kazi ya ufunuo na kusadikisha; na sasa mtu aliyetubu alikuwa katika hali ya kujifunza kutoka kwa wale ambao Mungu alikuwa amewachagua kufundisha Ukweli Wake. Hivyo Yesu alitoa idhini kwa mamlaka ya kanisa Lake lililopangwa, na kumweka Sauli katika uhusiano na wawakilishi Wake duniani. Nuru ya mwangaza wa mbinguni ilimnyima Sauli kuona, lakini Yesu, Mponyaji mkuu, hakuirejesha mara moja. Baraka zote hutoka kwa Kristo, lakini sasa alikuwa ameanzisha kanisa kama mwakilishi Wake duniani, na kazi yake ilikuwa ya kumwongoza mwenye dhambi aliyetubu katika njia ya uzima. Wanaume wale wale ambao Sauli alikuwa amekusudia kuwaangamiza wangekuwa walimu wake katika dini aliyoidharau na kuwatesa. **{SRSw 271.2}**

Imani ya Sauli ilijaribiwa vikali wakati wa siku tatu za kufunga na kuomba katika nyumba ya Yuda, huko Dameski. Alikuwa kipofu kabisa, na katika giza totoro la akili kuhusu kile kilichohitajika kutoka kwake. Alikuwa ameelekezwa kwenda Dameski, ambapo angeambiwa afanye nini. Katika kutokuwa na uhakika na dhiki yake alimlilia Mungu kwa bidii. “***Basi palikuwapo Dameski mwanafunzi jina lake Anania. Bwana akamwambia katika maono, Anania. Akasema, Mimi hapa, Bwana. Bwana akamwambia, Simama, enenda zako katika njia iitwayo Nyofu, ukaulize katika nyumba ya Yuda mtu aitwaye Sauli, wa Tarso; maana, angalia, anaomba; naye amemwona mtu, jina lake Anania, akiingia, na kumwekea mikono juu yake, apate kuona tena.” Matendo 9:10-12*** **{SRSw 271.3}**

Anania hakuweza kuamini maneno ya malaika mjumbe, kwa kuwa mateso makali ya Sauli kwa watakatifu huko Yerusalemu yalikuwa yameenea mbali na karibu. Alidhani moyoni kwa kulalamika; akisema, ***"Bwana, nimesikia habari za mtu huyu kwa watu wengi, mabaya mengi aliyowatenda watakatifu Wako Yerusalemu; hata hapa ana***

amri itokayo kwa wakuu wa makuhani awafunge wote wakuitiao Jina Lako." Matendo 9:13-14 Lakini amri kwa Anania ilikuwa lazima: ***"Nenda tu; kwa maana huyu ni chombo kiteule Kwangu, alichukue Jina Langu mbele ya Mataifa, na wafalme, na wana wa Israeli." Matendo 9:15*** **{SRSw 272.1}**

Mwanafunzi huyo, akiwa mtiifu kwa maelekezo ya malaika, alimtafuta mtu ambaye alikuwa ametishia kuua wote walioamini Jina la Yesu. Alimwambia: "***Ndugu Sauli, Bwana amenituma, Yesu, Yeye aliyekutokea katika njia uliyoijia, upate kuona tena, ukajazwe Roho Mtakatifu. Mara vikaanguka machoni pake vitu kama magamba, akapata kuona, akasimama, akabatizwa" Matendo 9:17-18*** **{SRSw 272.2}**

Hapa Kristo anatoa mfano wa jinsi alivyofanya kazi kwa ajili ya wokovu wa wanadamu. Angeweza kufanya kazi hii yote moja kwa moja kwa ajili ya Sauli; lakini hii haikuwa kulingana na mpango Wake. Baraka zake zingekuja kupitia vyombo alivyoviweka. Sauli alikuwa na jambo la kufanya katika mstari wa kukiri kwa wale ambao alikuwa amewafikiria kwaajili ya kufanya uharibifu kwao; na Mungu alikuwa na kazi ya kuwajibika kwa watu hao kufanya ambao alikuwa amewapa mamlaka ya kutenda badala yake. **{SRSw 272.3}**

Sauli anakuwa mwanafunzi wa wanafunzi. Kwa mwanga wa sheria anajiona kuwa mwenye dhambi. Anaona kwamba Yesu, ambaye kwa kutojua kwake, alimwona kama mdanganyifu, ndiye mwandishi na msingi wa dini ya watu wa Mungu tangu siku za Adamu, na mkamilishaji wa imani ambayo sasa imeeleweka kwa maono yake yaliyoangazwa; mtetezi wa Ukweli wa Kisa cha Ukombozi, na mtimizaji wa unabii. Alimwona Yesu kama asiyeifanya sheria ya Mungu kuwa na athari; lakini maono yake ya kiroho yalipoguswa na kidole cha Mungu, alijifunza kwamba Kristo alikuwa Mwanzilishi wa mfumo mzima wa

dhabihu wa Kiyahudi; kwamba alikuja ulimwenguni kwa kusudi dhahiri la kuithibitisha sheria ya Baba Yake; na kwamba katika kifo Chake sheria ya kawaida ilikuwa imekidhi mfano wake, [kivuli kimekutana na halisi]. Kwa mwanga wa sheria ya maadili, ambayo aliamini kwamba alikuwa akiishika kwa bidii, Sauli alijiona kama mwenye dhambi wa wenye dhambi. **{SRSw 273.1}**

Kutoka Kuwa Mtesaji Hadi Mtume

Paulo alibatizwa na Anania katika mto wa Dameski. Kisha akaimarishwa na chakula, na mara moja akaanza kuwahubiria waumini wa mji huo Yesu, wale aliowatoa kutoka Yerusalemu kwa kusudi la kuwaangamiza. Pia alifundisha katika masinagogi kwamba Yesu aliyeuawa, hakika alikuwa Mwana wa Mungu Kweli. Hoja zake kutoka kwa unabii zilikuwa za uhakika sana, na juhudi zake zilihudhuriwa sana na nguvu za Mungu, kiasi kwamba Wayahudi wapinzani walichanganyikiwa na hawakuweza kumjibu. Elimu ya marabi na Mafarisayo ya Paulo sasa ilitumika katika mambo mazuri, katika kuhubiri injili na katika kuunga mkono sababu aliyotumia hapo awali kwa kila juhudi kuharibu. **{SRSw 273.2}**

Wayahudi walishangazwa na kuchanganyikiwa kabisa na kubadilishwa kwa Paulo. Walijua nafasi yake Yerusalemu, na walijua ni nini ilikuwa kazi yake kuu huko Dameski, na kwamba alikuwa amepewa agizo kutoka kwa kuhani mkuu lililomruhusu kuwachukua waumini katika Yesu na kuwapeleka wakiwa wafungwa huko Yerusalemu; lakini sasa walimwona akihubiri injili ya Yesu, akiwaimarisha wale ambao tayari walikuwa wanafunzi Wake na kuendelea kuwageuza watu wapya kwenye imani ambayo hapo awali alikuwa ameipinga kwa usongo mkubwa. **{SRSw 274.1}**

Paulo aliwaonyesha wote waliomsikia kwamba mabadiliko yake ya Imani hayakutokana na msukumo wala ushabiki, bali yalisababishwa na ushahidi mwingi. Alipokuwa akifanya kazi katika masinagogi, imani yake iliongezeka kwa nguvu; bidii yake katika kusisitiza kwamba Yesu alikuwa Mwana wa Mungu iliongezeka mbele ya upinzani mkali wa Wayahudi. Hakuweza kukaa kwa muda mrefu Dameski, kwani baada ya Wayahudi kupona kutokana na mshangao wao kwa uongofu wake wa ajabu na kazi zilizofuata, waligeuka kwa uthabiti kutokana na ushahidi mwingi ulioletwa ili kupendelea mafundisho ya Kristo. Kushangazwa kwao na uongofu wa Paulo kulibadilishwa kuwa chuki kali kwake kama ile waliyoionyesha dhidi ya Yesu. **{SRSw 274.2}**

Maandalizi ya Huduma

Maisha ya Paulo yalikuwa hatarini, na alipokea agizo kutoka kwa Mungu kuondoka Dameski kwa muda. Alienda Arabia; na hapo, katika upweke ukilinganisha na maisha yake ya awali, alikuwa na fursa ya kutosha ya ushirikana Mungu na kutafakari. Alitamani kuwa peke yake na Mungu, kuchunguza moyo wake mwenyewe, kuongeza toba yake, na kujitayarisha kwa sala na kujifunza ili kushiriki katika kazi ambayo ilionekana kwake kuwa kubwa sana na muhimu sana kwake kuifanya. Alikuwa mtume, si mteule wa wanadamu, bali mteule wa Mungu, na kazi yake ilisemwa waziwazi kuwa miongoni mwa Mataifa. **{SRSw 274.3}**

Alipokuwa Arabia hakuwasiliana na mitume; alimtafuta Mungu kwa bidii kwa moyo wake wote, akiazimia kutopumzika hadi ajue kwa hakika kwamba toba yake ilikubaliwa na dhambi yake kubwa ikasamehewa. Hakuacha mzozo huo hadi apate uhakika kwamba Yesu angekuwa naye katika huduma yake ijayo. Daima angebeba alama za utukufu wa Kristo mwilini mwake, machoni pake, ambazo zilikuwa zimepofushwa na nuru ya mbinguni, na pia alitamani kubeba kila mara

uhakikasho wa neema ya Kristo inayodumisha. Paulo aliungana kwa karibu na Mbingu, na Yesu akazungumza naye, na kumtia nguvu katika imani yake, akimpa hekima na neema Yake. **{SRSw 275.1}**

SURA YA 38—HUDUMA YA AWALI YA PAULO

Sura hii imejengwa katika Matendo 9:23-31 na 22:17-21.

Paulo sasa alirudi Dameski na akahubiri kwa ujasiri kwa Jina la Yesu. Wayahudi hawakuweza kuhimili hekima ya hoja zake, na kwa hiyo wakashauriana kuinyamazisha kwa nguvu sauti yake—ambayo ndiyo hoja pekee iliyobaki kwa jambo lililokuwa likizama chini. Wakapanga kumwua. Mtume alifahamishwa kuhusu mpango wao. Milango ya mji ililindwa kwa uangalifu mkubwa, mchana na usiku, ili kumzuia asitoroke. Wasiwasi wa wanafunzi uliwapelekea kumgeukia Mungu kwa maombi; walikuwa na usingizi mchache sana, wakiwa wanajishughulisha kutafuta njia na mbinu za kumtorosha mtume mteule. Hatimaye walibuni mpango ambao kwa huo alishushwa kupitia dirishani na kuteremshwa juu ya ukuta, akiwa ndani ya kapu wakati wa usiku. Paulo alifanikiwa kutoroka kutoka Dameski, kwa njia hii ya kudhalilisha,. **{SRSw 276.1}**

Sasa alielekea Yerusalemu, akitaka kufahamiana na mitume waliokuwapo huko, hasa Petro. Alikuwa na shauku kubwa ya kukutana na wavuvi wa Galilaya waliokuwa wameishi, kuomba, na kuzungumza na Kristo alipokuwa hapa duniani. Ilikuwa kwa moyo wenye shauku kubwa kwamba alitamani kukutana na mkuu wa mitume. Paulo alipoingia Yerusalemu, aliutazama mji na hekalu kwa mtazamo uliobadilika. Sasa alijua kwamba hukumu ya adhabu ya Mungu ilikuwa ikining'inia juu yao. **{SRSw 276.2}**

Kwa sababu ya wongofu wa Paulo haikuwa na mipaka, huzuni na hasira ya Wayahudi. Lakini yeye alikuwa imara kama mwamba, na alijiaminisha kwamba alipowaeleza marafiki zake kuhusu uzoefu wake wa ajabu, wao pia wangebadili imani yao kama alivyofanya yeye, na kumwamini Yesu. Alikuwa makini sana katika dhamiri yake alipompinga Kristo na wafuasi Wake; lakini mara tu alipokamatwa na kutiwa hatiani kwa sababu ya dhambi yake, aliacha mara moja njia zake mbaya na kukiri imani katika Yesu. Sasa alikuwa na hakika kabisa

kwamba marafiki zake na washirika wake wa zamani waliposikia mazingira ya kuongoka kwake kwa ajabu, na kuona jinsi alivyobadilika kutoka kuwa Farisayo mwenye kiburi aliyewatesa na kuwaua wale waliomwamini Yesu kwamba Ndiye Mwana wa Mungu, wao pia wangesadikishwa kuhusu kosa lao na kujiunga na safu ya waumini. **{SRSw 276.3}**

Alijaribu kuungana na ndugu zake, yaani wanafunzi wa Yesu; lakini huzuni na masikitiko yake yalikuwa makubwa alipogundua kwamba hawakuwa tayari kumpokea kama mmoja wao. Walikumbuka mateso aliyowafanyia hapo awali, na walimshuku kwamba alikuwa akijifanya ameongoka ili awadanganye na kuwaangamiza. Ni kweli kwamba walikuwa wamesikia habari za kuongoka kwake kwa ajabu, lakini kwa kuwa mara tu baada ya tukio hilo aliondoka kwenda Arabia, na hawakuwa wamepata taarifa yoyote ya uhakika kumhusu tangu wakati huo, hawakuamini uvumi kuhusu mabadiliko yake makubwa. **{SRSw 277.1}**

Kukutana na Petro na Yohana

Barnaba, ambaye alikuwa ametoa kwa ukarimu mali yake ili kuendeleza kazi ya Kristo na kuwasaidia maskini katika mahitaji yao, alikuwa akimfahamu Paulo tangu alipokuwa akiwapinga waumini. Sasa alijitokeza na kufufua urafiki wao wa zamani. Alisikiliza ushuhuda wa Paulo kuhusu kuongoka kwake kwa miujiza na uzoefu wake tangu wakati huo. Barnaba alimwamini kikamilifu Paulo na akampokea. Kisha akamshika mkono na kumpeleka mbele ya mitume. Barnaba aliwasimulia mitume yale aliyokuwa amesikia kutoka kwa Paulo: kwamba Yesu Mwenyewe alikuwa amemtokea Paulo alipokuwa njiani kuelekea Dameski; kwamba alikuwa amesema naye; kwamba Paulo alipata kuona tena kutokana na maombi ya Anania; na kwamba baadaye

Paulo alikuwa amehubiri kwa ujasiri katika masinagogi ya mji huo akitangaza kwamba Yesu Ndiye Mwana wa Mungu. **{SRSw 277.2}**

Mitume hawakusita tena, kwa maana hawakuweza kuipinga kazi ya Mungu. Petro na Yakobo, ambao wakati huo ndio waliokuwa mitume pekee waliokuwapo Yerusalemu, walimpa mkono wa kuume wa ushirika Paulo, ambaye hapo awali alikuwa mtesi mkali wa imani yao. Sasa alikuwa akipendwa na kuheshimiwa kwa kiwango kile-kile ambacho zamani alikuwa akiogopwa na kuepukwa. Hapo ndipo watu hawa wawili mashuhuri wa imani mpya walipokutana: Petro, mmoja wa wafuasi waliochaguliwa wa Kristo alipokuwa duniani; na Paulo, aliyekuwa Farisayo, ambaye tangu Yesu alipopaa mbinguni alikuwa amekutana Naye uso kwa uso, akazungumza Naye, na pia akamwona katika maono pamoja na kuelewa asili ya kazi Yake huko mbinguni. **{SRSw 278.1}**

Mazungumzo haya ya kwanza kati ya mitume hawa wawili yalikuwa na umuhimu mkubwa kwao wote, ingawa hayakudumu kwa muda mrefu, kwa sababu Paulo alikuwa na shauku kubwa ya kuendelea na kazi ya Bwana wake. Muda si mrefu, sauti ile-ile ambayo hapo awali ilikuwa imebishana kwa nguvu na Stefano ikasikika tena katika sinagogi hilohilo, ikitangaza bila woga kwamba Yesu Ndiye Mwana wa Mungu, na kutetea Ukweli ule-ule ambao Stefano alikuwa ameuawa kwa kuuthibitisha. Paulo alisimulia uzoefu wake wa ajabu, na kwa moyo uliokuwa umejaa shauku kwa ajili ya ndugu zake na washirika wake wa zamani, aliwasilisha uthibitisho kutoka katika unabii, kama alivyofanya Stefano, kwamba Yesu aliyesulubiwa Ndiye Mwana wa Mungu. **{SRSw 278.2}**

Lakini Paulo alikuwa amekosea kutathmini mtazamo wa ndugu zake Wayahudi. Ghadhabu ile-ile iliyokuwa imemwangukia Stefano sasa ilimgeukia yeye pia. Alitambua kwamba ilimbidi ajitenge na ndugu

zake, jambo lililoujaza moyo wake huzuni. Alikuwa tayari hata kutoa uhai wake ikiwa kwa njia hiyo wangeweza kuifikia elimu ya ile Kweli. Wayahudi wakaanza kupanga njama za kumuua, na wanafunzi wakamsihi aondoke Yerusalemu. Lakini Paulo alikawia, kwa kuwa hakutaka kuondoka mahali pale, akiwa na hamu ya kuendelea kufanya kazi kwa muda zaidi miongoni mwa ndugu zake Wayahudi. Kwa kuwa alikuwa ameshiriki kwa bidii katika kuuawa kwa Stefano, alihisi wajibu mkubwa wa kufuta doa hilo kwa kuutetea kwa ujasiri, Ukweli ule uliomgharimu Stefano maisha yake. Kwa hiyo, kwake ilionekana kana kwamba kuikimbia Yerusalemu kungekuwa tendo la woga. **{SRSw 278.3}**

Kukimbia Kutoka Yerusalemu

Wakati Paulo, akiwa tayari kukabiliana na matokeo yote ya uamuzi huo kwa ushujaa, alipokuwa akimwomba Mungu kwa bidii hekaluni, Mwokozi alimtokea katika maono, akisema: **"Hima, utoke Yerusalemu upesi, kwa sababu hawatakubali ushuhuda wako katika habari zangu" Matendo 22:18** Hata wakati huo, Paulo bado alisita kuondoka Yerusalemu kabla hajawashawishi Wayahudi wenye ukaidi kuhusu Ukweli wa imani yake. Alifikiri kwamba, hata kama maisha yake yangetolewa kwa ajili ya kuutetea Ukweli, jambo hilo lisingekuwa zaidi ya kulipa sehemu ya deni kubwa la hatia alilohisi moyoni mwake kwa sababu ya kushiriki katika kifo cha Stefano. Ndipo akajibu: "***Bwana, wanajua hao ya kuwa mimi nalikuwa nikiwafunga gerezani wale wanaokuamini na kuwapiga katika kila sinagogi. Na damu ya Stefano shahidi wako ilipomwagwa, mimi nami nilikuwa nikisimama karibu, nikikubali, na kuzitunza nguo zao waliomwua." Matendo 22:19-21*** Lakini jibu alilopewa lilikuwa la msisitizo na uthabiti zaidi kuliko la kwanza: **"Ondoka; kwa maana nitakupeleka mbali sana kwa Mataifa." {SRSw 279.1}**

Ndugu waliposikia kuhusu maono ya Paulo na jinsi Mungu alivyokuwa akimlinda, walizidi kumhangaikia, kwa maana walitambua kwamba, ni hakika alikuwa chombo kilichochaguliwa na Bwana ili kuhubiri Ukweli kwa Mataifa. Kwa hiyo waliharakisha kumtorosha kwa siri kutoka Yerusalemu kwa kuhofu kwamba Wayahudi wangemuua. Kuondoka kwa Paulo kulisitisha kwa muda upinzani mkali wa Wayahudi, na kanisa likapata kipindi cha utulivu, ambapo watu wengi waliongezwa katika idadi ya waumini. **{SRSw 279.2}**

SURA YA 39—HUDUMA YA PETRO

Sura hii imejengwa katika Matendo 9:32 hadi 11:18.

Petro, katika kutekeleza kazi yake, aliwatembelea watakatifu huko Lida. Huko alimponya Aeneas, ambaye alikuwa amelazwa kitandani kwa muda wa miaka minane kutokana na ugonjwa wa kupooza. ***"Petro akamwambia, Ainea, Yesu Kristo akuponya; ondoka, ujitandikie kitanda chako. Mara akaondoka. Na watu wote waliokaa Lida na Sharoni wakamwona, wakamgeukia Bwana."*** ***Matendo 9:34-35*** **{SRSw 281.1}**

Yopa ilikuwa karibu na Lida, na wakati huo Tabitha—aliyeitwa Dorka kwa tafsiri nyingine—alikuwa amefariki huko. Alikuwa mwanafunzi mwema wa Yesu Kristo, na maisha yake yalijulikana kwa matendo ya huruma na wema kwa watu maskini na wenye huzuni, pamoja na bidii katika kuutetea Ukweli. Kifo chake kilikuwa hasara kubwa; kanisa changa halikuweza kustahimili kwa urahisi kupoteza juhudi zake safi na bora za ukarimu na upendo. Waumini waliposikia habari za uponyaji wa ajabu ambao Petro alikuwa amefanya huko Lida, walitamani sana afike Yopa. Wajumbe walitumwa kwake ili kumwomba aje huko. **{SRSw 281.2}**

"***Petro akaondoka akafuatana nao. Alipofika, wakampeleka juu orofani, wajane wote wakasimama karibu naye, wakilia na kumwonyesha zile kanzu na nguo alizozishona Dorkasi wakati ule alipokuwa pamoja nao. Matendo ya Mitume 9:39***. Petro aliwaamuru marafiki waliokuwa wakilia na kuomboleza watoke chumbani. Kisha akapiga magoti na kumwomba Mungu kwa bidii amrudishie Dorka uhai na afya katika mwili wake uliokuwa hauna mpigo wa moyo. "***kisha akaelekea yule maiti, akanena, Tabitha, ondoka. Naye akafumbua macho yake, na alipomwona Petro akajiinua, akaketi. Matendo 9:40***.

Kazi hii kubwa ya kumfufua mfu na kumrudisha katika uhai ilikuwa sababu iliyowafanya watu wengi huko Yopa kuamini katika imani ya Yesu. **{SRSw 281.3}**

Akida

"***Palikuwa na mtu Kaisaria, jina lake Kornelio, akida wa kikosi kilichoitwa Kiitalia, mtu mtauwa, mchaji wa Mungu, yeye na nyumba yake yote, naye alikuwa akiwapa watu sadaka nyingi, na kumwomba Mungu daima." Matendo 10:1-2.*** Ingawa Kornelio alikuwa Mrumi, alikuwa amemfahamu Mungu wa Kweli na akaachana na ibada ya sanamu. Alikuwa mtiifu kwa mapenzi ya Mungu na akamwabudu kwa moyo wa kweli. Hakuwa amejiunganisha na Wayahudi, lakini alifahamu, na kutii sheria ya maadili. Hakuwa ametahiriwa, wala hakushiriki katika matoleo ya dhabihu; Kwa hiyo alihesabiwa na Wayahudi kuwa najisi. Yeye, hata hivyo, alidumisha utume wa kusudi la Kiyahudi kwa michango huru -ya ukarimu, na alijulikana mbali na karibu kwa matendo yake ya hisani na ukarimu. Maisha yake ya haki yalimfanya kuwa na sifa njema miongoni mwa Wayahudi na Wamataifa. **{SRSw 282.1}**

Kornelio hakuwa na imani yenye ufahamu kamili kuhusu Kristo, ingawa aliamini unabii na alikuwa akimtazamia Masihi aje. Kwa sababu ya upendo wake kwa Mungu na utii wake kwa Mungu, alisogezwa karibu na Mungu na akaandaliwa kumpokea Mwokozi wakati atakapofunuliwa Kwake. Hukumu inakuja kwa kukataa nuru iliyotolewa. Akida alikuwa mtu wa familia ya waungwana wenye wadhifa na alikuwa na nafasi ya uaminifu na heshima ya juu; Lakini hali hizi hazikuwa na mwelekeo wa kupotosha sifa nzuri za tabia yake. Wema wa kweli na ukuu uliungana na kumfanya kuwa mtu wa maadili. Ushawishi wake ulikuwa wa manufaa kwa wote ambao aliletwa kwao. **{SRSw 282.2}**

Aliamini katika Mungu mmoja, Muumba wa mbingu na nchi. Alimheshimu, alitambua mamlaka Yake, na alitafuta mwongozo Wake katika shughuli zote za maisha yake. Alikuwa mwaminifu katika majukumu yake ya nyumbani kama alivyokuwa katika wajibu wake wa kikazi. Pia alikuwa ameisimamisha madhabahu ya Mungu katika familia yake. Hakuthubutu kutekeleza mipango yake wala kubeba mzigo wa majukumu yake makubwa bila msaada wa Mungu; kwa hiyo aliomba mara nyingi na kwa dhati na bidii ili apate msaada huo. Imani ilidhihirika katika matendo yake yote, na Mungu alimkubali kwa sababu ya usafi wa matendo yake na ukarimu wake. Mungu akamkaribia kwa Neno na kwa Roho. **{SRSw 283.1}**

Malaika Amtembelea Kornelio

Wakati Kornelio alipokuwa akiomba, Mungu alimtuma mjumbe wa mbinguni kwake, ambaye alimwita kwa jina. Yule akida aliogopa, lakini alijua kwamba malaika alitumwa na Mungu kumfundisha, na akasema, "***Kuna nini, Bwana? Akamwambia, Sala zako na sadaka zako zimefika juu na kuwa ukumbusho mbele za Mungu. Sasa basi, peleka watu Yafa, ukamwite Simoni, aitwaye Petro.***

Yeye ni mgeni wa mtu mmoja, jina lake Simoni, mtengenezaji wa ngozi, ambaye nyumba yake iko pwani, atakuambia yakupasayo kutenda." Matendo 10:4-6. **{SRSw 283.2}**

Hapa tena Mungu alionyesha jinsi anavyoheshimu huduma ya Injili na kanisa Lake lililoandaliwa kwa utaratibu. Malaika Wake hakuwa ndiye aliyepaswa kumweleza Kornelio habari za msalaba. Badala yake, mtu kama yeye, aliye chini ya udhaifu na majaribu ya kibinadamu, ndiye aliyepaswa kumfundisha kuhusu Mwokozi aliyesulubiwa, aliyefufuka, na aliyepaa mbinguni. Mjumbe huyo wa mbinguni alitumwa kwa kusudi mahsusi la kumunganisha Kornelio na

mtumishi wa Mungu ambaye angemfundisha jinsi yeye na watu wa nyumbani mwake wangeweza kuokolewa. **{SRSw 283.3}**

Kornelio alitii kwa furaha ujumbe huo, na mara moja akatuma wajumbe kumtafuta Petro, kama alivyoelekezwa na malaika. Ufafanuzi wa maelekezo hayo, ambayo hata kazi ya mtu ambaye Petro alikuwa akiishi nyumbani kwake ilitajwa, unaonyesha kwamba mbingu inafahamu vyema historia na shughuli za wanadamu katika kila ngazi ya maisha. Mungu anaijua kazi ya kila siku ya mfanyakazi mnyenyekevu, kama vile anavyoijua shuguli ya mfalme aliye kwenye kiti chake cha enzi. Pia tamaa ya mali, ukatili, dhambi za siri, na ubinafsi wa wanadamu unajulikana kwake, kama vile matendo yao mema, huruma, ukarimu, kuchukuliana na watu na wema. Hakuna kitu kilichofichika mbele za Mungu. **{SRSw 284.1}**

Maono ya Petro

Mara tu baada ya mahojiano haya na Kornelio, malaika alimwendea Petro, ambaye, akiwa amechoka sana na mwenye njaa kutokana na kusafiri, alikuwa akiomba juu ya dari ya nyumba. Alipokuwa akiomba, alionyeshwa maono, "***akaona mbingu zimefunuka, na chombo kikishuka kama nguo kubwa, kinatelemshwa kwa pembe zake nne hata nchi; ambayo ndani yake walikuwamo aina zote za wanyama wenye miguu minne, na hao watambaao, na ndege wa angani. Matendo ya Mitume 10:11-12."*** **{SRSw 284.2}**

"Kisha sauti ikamjia, kusema, Ondoka, Petro, uchinje ule. Lakini Petro akasema, Hasha, Bwana, kwa maana sijakula kamwe kitu kilicho kichafu au najisi. Sauti ikamjia mara ya pili, ikimwambia, Vilivyotakaswa na Mungu, usiviite wewe najisi. Jambo hili likatendeka mara tatu; kisha kile chombo kikapokewa tena mbinguni." Matendo 10:13-16 **{SRSw 284.3}**

Hapa tunaweza kutambua utendaji wa mpango wa Mungu wa kuanzisha utaratibu katika utendaji wa mambo, ili mapenzi Yake yatimizwe duniani kama yanavyotimizwa mbinguni. Petro alikuwa bado hajahubiri injili kwa mataifa. Wengi wa watu wa mataifa walikuwa wasikilizaji wenye shauku wa ile Kweli ambazo alizifundisha; lakini kiambaza cha kati kilichowatenga, ambacho kifo cha Kristo kilikuwa kimekibomoa, kilikuwa bado kipo akilini mwa mitume, na kiliwatenga wamataifa wasipate fursa za injili. Wayahudi wa Kiyunani walikuwa wamepokea huduma za mitume, na wengi wao walikuwa wameitikia juhudi hizo kwa kuikubali imani ya Yesu; lakini kuongoka kwa Kornelio lilikuwa ni jambo la kwanza lenye umuhimu mkubwa miongoni mwa mataifa. **{SRSw 284.4}**

Kwa njia ya maono ya ile nguo na vilivyokuwa ndani yake, iliyotelemshwa kutoka mbinguni, Petro alipaswa kuondolewa chuki zake za muda mrefu dhidi ya mataifa; na kuelewa kwamba, kwa njia ya Kristo, mataifa ya kipagani yalifanywa kuwa washiriki wa baraka na haki/fursa za Wayahudi, na hivyo walipaswa kunufaika sawa na wao. Baadhi ya watu wamedai kwamba maono haya yalikuwa na maana ya kuonyesha kuwa Mungu alikuwa ameondoa katazo Lake kuhusu matumizi ya nyama za wanyama ambao hapo awali alikuwa alikuwa amewaita kuwa najisi; na kwa hivyo nyama ya nguruwe au mamba, sasa ilikuwa inafaa kwa chakula. Hii ni tafsiri finyu sana na yenye makosa kabisa, na inapingwa waziwazi na maelezo ya Maandiko kuhusu maono hayo na matokeo yake. **{SRSw 285.1}**

Maono yale ya kila aina ya wanyama walio hai, waliokuwa ndani ya ile nguo (chombo), na ambao Petro aliamriwa kuwachinja na kula, huku akihakikishiwa kwamba kile Mungu alichokitakasa hakipaswi kuitwa kichafu au najisi, yalikuwa tu mfano uliowasilishwa akilini mwake ili kumfundisha nafasi ya kweli ya mataifa; kwamba kwa kifo

cha Kristo walifanywa warithi pamoja na Israeli wa Mungu. Maono hayo yalikuja kwa Petro kama karipio na mafundisho ya imani. Utendaji kazi wake hapo awali kwa ujumla ulikuwa umeelekezwa tu kwa Wayahudi; naye alikuwa akiwaona mataifa kama jamii najisi, waliotengwa na ahadi za Mungu. Sasa akili yake ilikuwa ikiongozwa kuelewa upana wa mpango wa Mungu duniani kote. **{SRSw 285.2}**

Hata alipokuwa akitafakari juu ya maono hayo, alielezwa. ***"Hata Petro alipokuwa akiona shaka ndani ya nafsi yake, maana yake ni nini maono hayo aliyoyaona, wale watu waliotumwa na Kornelio, wakiisha kuiulizia nyumba ya Simoni, wakasimama mbele ya mlango, wakaita; wakauliza kwamba Simoni aitwaye Petro anakaa humo. Na Petro alikuwa akiyafikiri yale maono. Roho akamwambia, Wako watu watatu wanakutafuta. Basi ondoka ushuke ufuatane nao, usione tashwishi, kwa maana ni mimi niliyewatuma." Matendo 10:17-20*** **{SRSw 286.1}**

Ilikuwa amri iliyomjaribu Petro sana; lakini hakuthubutu kutenda kulingana na hisia zake mwenyewe, na kwa hiyo akashuka kutoka chumbani mwake na kuwapokea wajumbe waliotumwa kwake na Kornelio. Wakamweleza mtume huyo ujumbe wao wa ajabu, na kulingana na maagizo ambayo alikuwa amepokea kutoka kwa Mungu, mara moja akakubali kwenda pamoja nao siku iliyofuata (siku ya pili). Kwa uungwana aliwakaribisha usiku huo, na asubuhi yake akaondoka pamoja nao kwenda Kaisaria, akiwa ameandamana na ndugu zake sita, ambao walipaswa kuwa mashahidi wa yote ambayo angesema au kufanya alipokuwa akiwatembelea mataifa; kwa maana alijua kwamba angeulizwa sababu ya kupingana waziwazi namna hiyo na imani na mafundisho ya Kiyahudi. **{SRSw 286.2}**

Ilichukua karibu siku mbili kufanya safari hii, na Kornelio alikuwa na furaha kubwa ya kumfungulia milango mhudumu wa injili ambaye,

ambaye kulingana na ahadi ya Mungu, angemfundisha yeye na nyumba yake jinsi ambavyo wangeweza kuokolewa. Wakati wajumbe walipokuwa katika utume wao, yule akida alikuwa amewakusanya pamoja ndugu zake wengi kadiri walivyoweza kufikiwa, ili wao pia pamoja naye wapate kufundishwa Ukweli. Petro alipofika, kundi kubwa lilikusanyika, likisubiri kwa hamu kusikiliza maneno yake. **{SRSw 286.3}**

Kutembelewa kwa Kornelio

Petro alipoingia katika nyumba ya mtu wa Mataifa, Kornelio hakumsalimu kama mgeni wa kawaida, bali kama mtu aliyeheshimiwa (aliyekirimiwa) na Mbingu na aliyetumwa kwake na Mungu. Ni desturi ya Mashariki kuinama mbele ya mkuu au mtu mwingine mwenye cheo cha juu, na kwa watoto kuinama mbele ya wazazi wao walioaminiwa kwa nafasi za heshima. Lakini Kornelio, akiwa amejawa na heshima kubwa kwa mtume ambaye alikuwa ametumwa na Mungu, alianguka miguuni pake na kumsujudia. **{SRSw 287.1}**

Petro alishtuka kwa hofu kutokana na kitendo hiki cha akida, na kumwinua miguuni pake, akisema, "**Simama, mimi nami ni mwanadamu.” Matendo 10:26** Kisha akaanza kuzungumza naye kwa urafiki, ili kuondoa hali ya hofu na heshima ya kupindukia ambayo akida huyo alimheshimu. **{SRSw 287.2}**

Kama Petro angekuwa amepewa mamlaka na nafasi ile inayodaiwa kumpa na Kanisa Katoliki la Rumi, basi angemtia moyo, badala ya kuzuia, heshima ya Kornelio Wale wanaojiita warithi wa Petro huwadai wafalme na watawala wainame miguuni pao (wapige magoti mbele yao), lakini Petro mwenyewe alikiri kuwa yeye ni mtu anayekosea na asiye mkamilifu. **{SRSw 287.3}**

Petro alizungumza na Kornelio na wale waliokusanyika katika nyumba yake kuhusu desturi ya Wayahudi; kwamba ilichukuliwa kuwa si halali (ni kinyume cha sheria) kwao kuchangamana kijamii na watu wa mataifa, na kwamba hilo lilihusisha unajisi wa kiibada. Haikuwa imekatazwa na sheria ya Mungu, bali mapokeo ya wanadamu yaliifanya kuwa desturi ya lazima. Akasema: "***Ninyi mnajua ya kuwa si halali mtu aliye Myahudi ashikamane na mtu aliye wa taifa lingine wala kumwendea, lakini Mungu amenionya, nisimwite mtu awaye yote mchafu wala najisi. Kwa sababu hiyo nalikuja nilipoitwa, nisikatae; basi nawauliza, ni neno gani mliloniitia?" Matendo 10:28-29*** **{SRSw 287.4}**

Hapo Kornelio alisimulia uzoefu wake, na maneno ya malaika aliyemtokea katika maono. Akihitimisha, kwa kusema: ***"Mara nikatuma watu kwako, nawe umefanya vyema kuja. Basi sasa sisi sote tupo hapa mbele za Mungu, tupate kuyasikiliza Maneno yote uliyoamriwa na Bwana. Petro akafumbua kinywa chake, akasema, Hakika natambua ya kuwa Mungu hana upendeleo; bali katika kila taifa mtu amchaye na kutenda haki hukubaliwa na Yeye." Matendo 10:33-35*** Ingawa Mungu alikuwa amewapendelea Wayahudi kuliko mataifa mengine yote, kama wangekataa nuru na kuishi kinyume na imani waliyoikiri, wasingepokea heshima ya juu mbele Zake kuliko mataifa mengine. Watu wa mataifa mengine ambao, kama Kornelio, walimcha Mungu na kutenda haki, wakiishi kulingana na nuru waliyokuwa nayo, walipata kibali mbele za Mungu, na huduma yao ya unyofu ilipokelewa. **{SRSw 288.1}**

Lakini imani na haki ya Kornelio havingeweza kuwa kamilifu bila kumjua Kristo; kwa hiyo Mungu alimtumia nuru na maarifa hayo kwa ajili ya kukuza zaidi tabia yake ya haki. Wengi hukataa kuipokea nuru ambayo majaliwa ya Mungu huwatumia, na kama sababu ya kufanya

hivyo, hunukuu maneno ya Petro kwa Kornelio na rafiki zake: "***bali katika kila taifa mtu amchaye na kutenda haki hukubaliwa na Yeye." Matendo 10:35.*** Wao hudai kwamba haijalishi watu wanaamini nini, mradi tu matendo yao ni mema. Watu kama hao wamekosea; imani lazima iungane na matendo yao. Wanapaswa kusonga mbele kwa kufuata nuru waliyopewa. Ikiwa Mungu atawaleta katika uhusiano na watumishi wake ambao wamepokea kweli mpya, iliyothibitishwa kwa Neno la Mungu, wanapaswa kuikubali kwa furaha. Kweli husonga mbele [endelevu daima]. Kweli huelekea juu. Kwa upande mwingine, wale wanaodai kwamba imani yao peke yake ndiyo itakayowaokoa wanategemea msingi dhaifu usio na nguvu, kwa maana imani huimarishwa na kukamilishwa kwa matendo pekee. **{SRSw 288.2}**

Watu wa Mataifa Wapokea Roho Mtakatifu

Petro alimhubiri Yesu kwa kundi lile la wasikilizaji waliokuwa makini; maisha Yake Kristo, huduma Yake, miujiza Yake, kusalitiwa Kwake, kusulubiwa Kwake, kufufuka Kwake, kupaa Kwake mbinguni, na kazi Yake huko mbinguni kama Mwakilishi na Mwombezi wa mwanadamu, akiwasemea wenye dhambi mbele za Mungu kwa niaba yao. Mtume alipokuwa akinena, moyo wake uliwaka kwa Roho wa Kweli wa Mungu aliyekuwa akimhubiri kwa watu. Wasikilizaji wake walivutiwa sana na mafundisho waliyoyasikia, kwa maana mioyo yao ilikuwa imeandaliwa kuipokea ile Kweli. Mtume alikatizwa na kushuka kwa Roho Mtakatifu, kama ilivyodhihirishwa siku ya Pentekoste. "***Na wale waliotahiriwa, walioamini, wakashangaa, watu wote waliokuja pamoja na Petro, kwa sababu Mataifa nao wamemwagiwa kipawa cha Roho Mtakatifu. Kwa maana waliwasikia wakisema kwa lugha, na kumwadhimisha Mungu. Ndipo Petro akajibu, Ni nani awezaye kuzuia maji, hawa wasibatizwe, watu waliopokea Roho Mtakatifu vile vile kama sisi? Akaamuru wabatizwe kwa Jina Lake Yesu Kristo.***

Ndipo wakamsihi azidi kukaa siku kadha wa kadha. Matendo 10:45-48 **{SRSw 289.1}**

Kushuka kwa Roho Mtakatifu juu ya Mataifa hakukuwa sawa na ubatizo. Hatua zinazohitajika katika uongofu, katika kila hali, ni imani, toba, na ubatizo. Hivyo basi, kanisa la Kweli la Kikristo linaunganishwa katika Bwana Mmoja, imani moja, na ubatizo mmoja. Tofauti za hulka/haiba za watu hubadilishwa kwa neema inayotakasa, na kanuni zilezile maalumu huongoza maisha ya wote. Petro alikubali maombi ya Mataifa walioamini, akakaa nao kwa muda, akimhubiri Yesu kwa Mataifa yote yaliyokuwa maeneo yale. **{SRSw 289.2}**

Ndugu waliokuwa Uyahudi waliposikia kwamba Petro alikuwa amewahubiria Mataifa, na kwamba alikuwa amekutana nao pamoja na kula nao katika nyumba zao, walistaajabu na kukerwa na matendo hayo ambayo kwao yalionekana ya ajabu. Waliogopa kwamba mwenendo huo, ambao kwao ulionekana kuwa wa kujiona au ujuvi, ungeweza kupingana na mafundisho yake mwenyewe. Mara tu Petro alipowatembelea, walimkabili kwa lawama kali, "***wakisema, Uliingia kwa watu wasiotahiriwa ukala nao" Matendo 11:3***. **{SRSw 290.1}**

Maono ya Kupanuka kwa Kanisa

Kisha Petro kwa uwazi aliwaeleza kikamilifu jambo hilo lote. Alisimulia uzoefu wake kuhusu ile njozi, na akasisitiza kwamba ilimwonya asiendelee tena kudumisha tofauti za kiibada au kaida kati ya ya tohara na kutotahiriwa, wala kuwachukulia Mataifa kuwa najisi, kwa kuwa Mungu hana upendeleo. Aliwaeleza kuhusu agizo la Mungu la kwenda kwa Mataifa, kuja kwa wale wajumbe, safari yake kwenda Kaisaria, na kukutana kwake na Kornelio pamoja na kikundi kilichokusanyika nyumbani kwake. Tahadhari yake ilidhihirika kwa ndugu zake kutokana na ukweli kwamba, ingawa alikuwa ameagizwa na

Mungu kwenda nyumbani kwa mtu wa Mataifa, aliambatana na wanafunzi sita waliokuwapo wakati huo kama mashahidi wa yote atakayosema au kufanya akiwa huko. Alisimulia kiini cha mazungumzo yake na Kornelio, ambapo Kornelio alimweleza kuhusu njozi yake, ambayo ndani yake alielekezwa kuwatuma wajumbe kwenda huko Yopa ili kumleta Petro kwake, ambaye angemwambia maneno ambayo yeye, na nyumba yake yote, wangeweza kuokolewa. **{SRSw 290.2}**

Alisimulia kiini cha mahojiano yake na Kornelio, ambamo yule wa pili alimwambia juu ya maono yake, ambapo alikuwa ameelekezwa kutuma wajumbe kwenda Yopa ili kumleta Petro kwake, ambaye angemwambia maneno ambayo. Alisimulia matukio ya mkutano huu wa kwanza pamoja na Mataifa, akisema, ***"Ikawa nilipoanza kunena, Roho Mtakatifu akawashukia kama alivyotushukia sisi mwanzo. Nikalikumbuka neno lile la Bwana, jinsi alivyosema, Yohana alibatiza kwa maji kweli, bali ninyi mtabatizwa kwa Roho Mtakatifu. Basi ikiwa Mwenyezi Mungu amewapa wao karama ile ile aliyotupa sisi tuliomwamini Bwana Yesu Kristo, mimi ni nani niweze kumpinga Mungu?"*** **Matendo 11:15-17** **{SRSw 290.3}**

Wanafunzi, waliposikia simulizi hilo, walinyamaza, na wakasadiki kwamba mwenendo wa Petro ulikuwa utekelezaji wa moja kwa moja wa mpango wa Mungu, na kwamba chuki na ubaguzi wao wa zamani vilipaswa kuondolewa kabisa na Injili ya Kristo. ***"Waliposikia maneno haya wakanyamaza, wakamtukuza Mungu, wakisema, Basi, Mungu amewajalia hata mataifa nao toba liletalo uzima."*** ***Matendpo 11:18*** **{SRSw 291.1}**

SURA YA 40—PETRO AOKOLEWA KUTOKA GEREZANI

Sura hii imejengwa katika Matendo 12:1-23.

Herode alidai kuwa mwongofu katika imani ya Kiyahudi, na kwa wazi alikuwa mwenye usongo sana katika kudumisha taratibu za sheria au kaida. Serikali ya Uyahudi ilikuwa mikononi mwake, akiwa chini ya Klaudio, mfalme wa Roma; pia alikuwa na cheo cha liwali wa Galilaya. Herode alitamani kupata kibali cha Wayahudi, akitumaini kwa njia hiyo kuimarisha nafasi na heshima zake. Hivyo akaanza kutekeleza matakwa ya Wayahudi kwa kutesa kanisa la Kristo. Alianza kazi yake kwa kupora nyumba na mali za waumini; kisha akaanza kuwafunga gerezani viongozi wao wakuu. Alimkamata Yakobo na kumtia gerezani, kisha akatuma mnyongaji kumuua kwa upanga, kama vile Herode mwingine alivyomfanya Yohana kwa kumkata kichwa. Baadaye akazidi kuthubutu, akiona kwamba Wayahudi walifurahia matendo yake, na akamfunga Petro gerezani. Ukatili huu ulifanywa wakati wa sikukuu takatifu ya Pasaka. **{SRSw 292.1}**

Watu walisifu kitendo cha Herode cha kusababisha kifo cha Yakobo, ingawa baadhi yao walilalamika kuhusu jinsi kifo kilivyofanywa faraghani, wakisisitiza kwamba mauaji ya hadharani yangekuwa na athari kubwa zaidi ili kuwatisha waumini wote na wanaowaunga mkono. Hivyo Herode alimshikilia Petro gerezani kwa

lengo la kuwaridhisha (kuwafurahisha) Wayahudi kwa tamasha la hadhara la kifo chake. Lakini mtawala alishauriwa kwamba haingekuwa salama kumleta mtume huyo mkongwe nje kwa ajili ya kuuawa mbele ya watu wote waliokuwa wamekusanyika Yerusalemu kwa ajili ya Pasaka. Iliogopwa kwamba muonekano wake wa heshima ungeweza kuamsha huruma na heshima kwa watu; pia waliogopa kwamba angeweza kutoa maelezo yenye nguvu ambayo mara nyingi yalikuwa yakiwachochea watu kuchunguza maisha na tabia ya Yesu Kristo, na ambayo wao, pamoja na mbinu zao zote, walishindwa kabisa kuyapinga. Katika hali kama hiyo, Wayahudi waliogopa kwamba kuachiliwa kwake kungedaiwa mikononi mwa mfalme. **{SRSw 292.2}**

Wakati utekelezaji wa hukumu ya Petro ulipokuwa ukicheleweshwa kwa visingizio mbalimbali hadi baada ya Pasaka, kanisa la Kristo lilipata muda wa kuchunguza mioyo yao kwa kina na kusali kwa bidii. Maombi makali, machozi, na kufunga vilichanganywa pamoja. Walimwomba Mungu bila kukoma kwa ajili ya Petro; walihisi kwamba hangeweza kuepushwa na kazi ya Kikristo, na waliona kwamba walikuwa wamefikia hatua ambayo, bila msaada maalum wa Mungu, kanisa la Kristo lingetoweka kabisa. **{SRSw 293.1}**

Siku ya kuuawa kwa Petro hatimaye ilipangwa; lakini bado maombi ya waumini yaliendelea kupaa mbinguni. Na wakati nguvu na hisia zao zote zilipokuwa zikielekezwa katika maombi ya dhati, malaika wa Mungu walikuwa wakimlinda mtume huyo aliyefungwa gerezani. Binadamu akifikia mwisho wa uwezo wake, ndipo Mungu huanza. Petro alikuwa amewekwa kati ya askari wawili, akiwa amefungwa kwa minyororo miwili, kila mnyororo umefungwa kwenye mkono wa mmoja wa walinzi wake. Hivyo hakuweza kusogea bila wao kutambua. Milango ya gereza ilikuwa imefungwa kwa uthabiti, na ulinzi mkali uliwekwa

mbele yake. Hivyo, kila nafasi ya kuokolewa au kutoroka kwa njia ya kibinadamu ilikuwa imezuiwa kabisa. **{SRSw 293.2}**

Mtume huyo hakutiwa hofu na hali aliyokuwa nayo. Tangu aliporejeshwa baada ya kumkana Kristo, alikuwa amekabiliana bila kuyumba na hatari, na kuonyesha ujasiri wa hali ya juu katika kuhubiri Mwokozi aliyesulubiwa, aliyefufuka, na aliyepaa mbinguni. Aliamini kwamba wakati ulikuwa umefika ambapo alipaswa kutoa maisha yake kwa ajili ya Kristo. **{SRSw 293.3}**

Usiku uliotangulia siku aliyopangiwa kuuawa, Petro, akiwa amefungwa minyororo, alikuwa amelala kati ya askari wawili kama kawaida. Herode, akikumbuka kutoroka kwa Petro na Yohana gerezani walikokuwa wamefungwa kwa sababu ya imani yao, alichukua tahadhari za ziada katika tukio hili. Askari waliokuwa wakilinda, ili kuhakikisha uangalizi wa ziada, waliwajibishwa kwa usalama wa mfungwa huyo. Alifungwa, kama ilivyoelezwa, katika chumba cha miamba makubwa, ambacho milango yake ilikuwa imefungwa kwa mapingo na vigogo. Askari kumi na sita waliwekwa kulinda chumba hicho, wakibadilishana kwa zamu za kawaida. Wanne ndio waliokuwa wakifanya zamu kwa wakati mmoja. Hata hivyo, mapingo, vigogo, na ulinzi wa Warumi, ambao kwa hakika ulizima kabisa uwezekano wa msaada wa kibinadamu kwa mfungwa huyo, ulitokana tu na kuufanya ushindi wa Mungu katika kumwokoa Petro kutoka gerezani kuwa kamili zaidi. Herode alikuwa akiinua mkono wake dhidi ya Mwenyezi Mungu, na angeaibishwa kabisa na kushindwa katika jaribio lake la kumwua mtumishi wa Mungu. **{SRSw 294.1}**

Kuokolewa na Malaika

Katika Usiku huu wa mwisho kabla ya kuuawa, malaika mwenye nguvu, aliyetumwa kutoka mbinguni, alishuka ili kumwokoa. Milango

imara ambayo ilimfungia mtakatifu wa Mungu ilifunguka bila msaada wa mikono ya binadamu; malaika wa Yeye Aliye Juu Sana aliingia, nayo ikafungwa tena kimyakimya nyuma yake. Aliingia katika chumba hicho kilichochongwa katika mwamba mgumu, ambamo Petro alikuwa amelala usingizi mtakatifu, wenye amani ya kutokuwa na hatia na imani kamili kwa Mungu, akiwa amefungwa kwa mlinzi mwenye nguvu kila upande wake. Nuru iliyomzunguka malaika ililimulika gereza, lakini haikumwamsha mtume aliyelala. Usingizi wake ulikuwa wa utulivu unaotia nguvu na kufanya upya, unaotokana na dhamiri safi. **{SRSw 294.2}**

Petro hakuamshwa, hadi alipohisi mguso wa mkono wa malaika na kusikia sauti yake ikisema, "**Ondoka upesi**." Akaona chumba chake cha gereza, ambacho hakijawahi kubarikiwa na miale ya jua, kimeangazwa na nuru ya mbinguni, na malaika mwenye utukufu mkuu amesimama mbele yake. Kwa kawaida, bila kufikiri sana, anaitii sauti ya malaika; na anapoanza kusimama, anainua mikono yake, na kugundua kwamba minyororo imevunjika kutoka mikononi mwake. Tena sauti ya malaika inasikika ikisema, "***Jifunge, kavae viatu vyako."*** **Matendo 12:8 {SRSw 295.1}**

Tena, Petro kama kawaida anatii bila kufikiri sana, akiwa amekazia macho yake yenye mshangao kwa mgeni wake wa mbinguni, na akiamini kwamba anaota, au yuko katika njozi. Askari wenye silaha wanabaki kimya na bila mwendo kama sanamu zilizochongwa kwa marumaru, malaika anapoamuru tena, ***"Jivike nguo yako, ukanifuate."*** Baada ya hapo, kiumbe huyo wa mbinguni anaelekea kwenye mlango, na Petro, ambaye kwa kawaida alikuwa mzungumzaji, anamfuata akiwa kimya kwa mshangao. Wanapita juu ya walinzi wasiosogea na kufika kwenye mlango mzito uliofungwa kwa mapingo na vigogo, ambao unafunguka wenyewe bila kuguswa na mara moja unafungwa tena; huku

mlinzi wa ndani na nje ya mlango akiwa kimya kwenye nafasi zao. **{SRSw 295.2}**

Mlango wa pili, ambao pia ulikuwa unalindwa ndani na nje, unafikiwa; unafunguka kama ule wa kwanza, bila mlio wa bawaba wala kelele ya mapingo ya chuma; wanapita, nao unafungwa tena kimyakimya. Wanapita kwenye lango la tatu kwa njia ile ile, na hatimaye wanajikuta katika barabara ya wazi. Hakuna neno lolote linalozungumzwa; hakuna sauti ya hatua za miguu; malaika anasonga mbele kama anayeelea, akiwa amezungukwa na nuru yenye mwangaza wa kupendeza mno, na Petro anamfuata mkombozi wake akiwa amechanganyikiwa, akiamini bado yuko katika ndoto. Mtaa baada ya mtaa wanapita hivyo, na kisha, kazi ya malaika inapokamilika, anatoweka ghafla. **{SRSw 295.3}**

Nuru ya mbinguni ilipofifia, Petro alijikuta katika giza nene; lakini polepole giza hilo lilianza kupungua alipokuwa akizoea hali hiyo, na akajikuta peke yake katika barabara tulivu ya mji, huku hewa ya usiku yenye baridi ikimkumbatia uso wake. Sasa alitambua kwamba haikuwa ndoto wala njozi iliyomtembelea. Alikuwa huru, katika sehemu ya mji aliyokuwa anaifahamu; alitambua mahali hapo kama sehemu ambayo alikuwa akiitembelea mara kwa mara, na ambayo alitarajia kuipita kwa mara ya mwisho kesho yake, alipokuwa akipelekwa kwenye eneo la kuuawa kwake. Alijaribu kukumbuka matukio ya dakika chache zilizopita. Alikumbuka kulala akiwa amefungwa kati ya askari wawili, akiwa amevuliwa viatu na vazi la nje. Alijichunguza na akagundua kwamba alikuwa amejivika nguo kikamilifu na amejifunga kama kawaida. **{SRSw 296.1}**

Viganja vyake, vilivyokuwa vimevimba kutokana na kuvaa minyororo ya ukatili, sasa vilikuwa huru bila pingu. Akatambua kwamba uhuru wake haukuwa udanganyifu, bali ulikuwa uhalisia wenye baraka.

Kesho yake alikuwa apelekwe kwenda kuuawa; lakini tazama, malaika alikuwa amemwokoa kutoka gerezani na kutoka mauti. “***Hata Petro alipopata fahamu akasema, Sasa nimejua yakini ya kuwa Bwana amempeleka malaika wake na kunitoa katika mkono wa Herode na katika kutazamia kote kwa taifa la Wayahudi.”*** **Matendo 12:11** **{SRSw 296.2}**

Jibu la Maombi

Mtume alielekea moja kwa moja hadi nyumbani ambapo ndugu zake walikuwa wamekusanyika kwa ajili ya maombi; akawakuta wakiendelea kumwombea kwa bidii wakati huo. ***"Naye alipobisha kilango cha lango, kijakazi, jina lake Roda, akaja kusikiliza. Alipoitambua sauti ya Petro, hakukifungua lango, kwa ajili ya furaha, bali alipiga mbio, akaingia ndani akawaambia kwamba Petro anasimama mbele ya lango. Wakamwambia, Una wazimu. Lakini yeye akakaza sana, akasema ya kwamba ndivyo hivyo. Wakanena, Ni malaika wake. Petro akafuliza kugonga, hata walipokwisha kumfungulia wakamwona, wakastaajabu. Naye akawapungia mkono wanyamaze, akawaeleza jinsi Bwana alivyomtoa katika gereza. Akasema, Kampasheni Yakobo na wale ndugu habari hizi. Akaondoka, akaenda mahali pengine.” Matendo 12:13-17*** **{SRSw 296.3}**

Shangwe na sifa vilijaa mioyoni mwa waumini waliokuwa wanafunga na kuomba, wakiamini kwamba Mungu alikuwa amesikia na kujibu maombi yao, na kumkomboa Petro kutoka mikononi mwa Herode. Asubuhi watu walikusanyika kushuhudia kuuawa kwa mtume. Herode alituma maafisa kumleta Petro kutoka gerezani kwa maandalizi makubwa ya silaha na ulinzi, ili kuhakikisha asitoroke, na kuwatisha wote waliomwonea huruma, na kuonesha uwezo wake mwenyewe. Kulikuwa na walinzi mlangoni pa gereza, makomeo na milango ikiwa

bado imara, walinzi wakiwa ndani, na minyororo ikiwa bado imefungwa mikononi mwa askari wawili; lakini mfungwa hakuwepo. **{SRSw 297.1}**

Adhabu ya Herode

Taarifa ya mambo haya ilipoletwa kwa Herode, alikasirika, na kuwatuhumu walinzi wa gereza kwa kutokuwa waaminifu. Kwa hivyo waliuawa kwa kosa linalodaiwa kama kulala kazini. Wakati huo huo Herode alijua kwamba hakuna nguvu ya kibinadamu iliyomwokoa Petro. Hata hivyo alikataa kukiri kwamba nguvu ya Mwenyezi Mungu ilikuwa imefanya kazi kuzuia mipango yake mibaya**.** Hakutaka kujidhalilisha hivyo, bali alijiweka kwa jeuri katika kumpinga Mungu. **{SRSw 298.1}**

Muda mfupi baada ya Petro kufunguliwa kutoka gerezani, Herode alishuka kutoka Yudea hadi Kaisaria na kukaa huko. Huko alifanya sherehe kubwa, iliyokusudiwa kuamsha pongezi na shangwe za watu. Wapenzi wa anasa kutoka pande zote walikusanyika pamoja, na kulikuwa na karamu nyingi na unywaji wa divai. Herode alijitokeza kwa uzuri sana mbele ya watu. Alikuwa amevaa joho/vazi, lililong'aa kwa fedha na dhahabu, ambalo lilikuwa likimeta-meta katika mikunjo yake inayong'aa, na kuwafanya watazamaji wamkodolee macho. Kwa fahari, majigambo na sherehe kubwa alisimama mbele ya umati, na kuwahutubia kwa hotuba yenye ufasaha. **{SRSw 298.2}**

Utukufu wa mwonekano wake na nguvu ya lugha yake aliyoichagua vizuri viliwashawishi watu kwa ushawishi mkubwa. Hisia zao zilikuwa tayari zimepotoshwa na karamu na divai; walishangazwa na mapambo yake yanayong'aa na kuvutiwa na tabia yake kuu na maneno ya ufasaha; na, wakiwa na shauku kubwa, walimtukuza, na kumtangaza kuwa mungu, walitangaza kwamba mwanadamu anayeweza kufa hawezi kuonyesha mwonekano kama huo au kuamuru ufasaha wa

lugha wa kushangaza kama huo. Walidai pia kwamba walikuwa wamemheshimu kama mtawala, lakini tangu sasa wanapaswa kumwabudu kama mungu. **{SRSw 298.3}**

Herode alijua kwamba hakustahili sifa na heshima hii; hata hivyo hakukemea ibada hiyo ya sanamu ya watu, bali aliikubali kama haki yake. Furaha ya kiburi cha kuridhika ilionekana usoni mwake aliposikia kelele ikipanda: ***"Ni sauti ya Mungu, si sauti ya mwanadamu." Matendo 12:22.*** Sauti zile zile ambazo sasa zilimtukuza mwenye dhambi mwovu, zilikuwa zimepaza kelele miaka michache iliyopita zikisema: "Mchukueni Yesu! Msulubishe! Msulubishe!" Herode alipokea sifa hii ambayo watu walijikomba nayo kwake na heshima kwa furaha kubwa, na moyo wake ukajaa ushindi wa kiburi; lakini ghafla mabadiliko ya haraka na ya kutisha yakamjia. Uso wake ukawa mweupe kama mauti na kupotoshwa na uchungu; matone makubwa ya jasho yakaanza kutoka kwenye vinyweleo vyake. Alisimama kwa muda kana kwamba amejawa na maumivu na hofu; kisha, akageuza uso wake uliofifia rangi ya hudhurungi na kupauka na wenye hasira kwa marafiki zake waliojaa hofu, akapaza sauti dhaifu yenye kukata tamaa akisema: "Mtu yule ambaye mmemtukuza kama Mungu amepigwa na kifo!" **{SRSw 298.4}**

Alichukuliwa akiwa katika mateso makali sana kutoka eneo hilo la starehe za uovu, furaha, na fahari, na maonyesho sasa aliyachukia nafsini mwake. Muda mfupi uliopita alikuwa amepokea sifa na ibada ya umati huo mkubwa—sasa alijihisi akiwa mikononi mwa Mtawala Mwenye nguvu kuliko yeye. Majuto yalimshika; alikumbuka amri yake ya kikatili ya kumuua Yakobo asiye na hatia; alikumbuka mateso yake yasiyokoma kwa wafuasi wa Kristo, na mpango wake wa kumuua mtume Petro, ambaye Mungu alikuwa amemwokoa mkononi mwake; alikumbuka jinsi, katika hasira yake ya kujidhalilisha na kukata tamaa,

alivyolipiza kisasi chake kisicho na sababu, kwa walinzi wa mfungwa na kuwaua bila huruma. Alihisi kwamba Mungu, ambaye alikuwa amemwokoa mtume kutoka kifo, sasa alikuwa akimshughulikia na kumhukumu, mtesaji asiye na huruma. Hakupata nafuu kutokana na maumivu ya mwili au uchungu wa roho, na hakutarajia yoyote. Herode alikuwa akiifahamu sheria ya Mungu, ambayo inasema, ***"Usiwe na miungu mingine ila Mimi." Kutoka 20:3*** na alijua kwamba kwa kukubali ibada ya watu alikuwa amejaza kipimo cha uovu wake na alikuwa amejiletea ghadhabu ya haki ya Mungu. **{SRSw 299.1}**

Malaika yule yule aliyetoka katika makao ya kifalme ya mbinguni ili kumwokoa Petro kutoka katika nguvu za mtesaji wake, alikuwa mjumbe wa ghadhabu na hukumu kwa Herode. Malaika alimpiga Petro ili kumwamsha kutoka usingizini; lakini kwa pigo tofauti, alimpiga mfalme mwovu, akimletea ugonjwa wa mauti. Mungu alidhihirisha kutoafikiana na kiburi cha Herode, na mwili wake, ambao alikuwa ameuonyesha akiwa amevaa mavazi yanayong'aa mbele ya macho ya watu, ulioliwa na minyoo, na kuoza akiwa bado hai. Herode alikufa katika maumivu makali ya akili na mwili, chini ya hukumu ya haki ya Mungu. **{SRSw 299.2}**

Onyesho hili la hukumu ya Mungu lilikuwa na ushawishi mkubwa kwa watu. Wakati mtume wa Kristo alikuwa ameokolewa kimiujiza kutoka gerezani na kifo, mtesaji wake alikuwa amepigwa chini kwa laana ya Mungu. Habari hizo zilisambazwa katika nchi zote, na zilikuwa njia ya kuwaleta wengi kumwamini Kristo. **{SRSw 300.1}**

SURA YA 41—KATIKA MAENEO YA NGAMBO

Sura hii imejengwa katika Matendo 13:1-4 na 15:1-31.

Mitume na wanafunzi walioondoka Yerusalemu wakati wa mateso makali yaliyotokea huko baada ya kifo cha Stefano, walimhubiri Kristo katika miji iliyozunguka, wakijikita kazi yao kwa Wayahudi wa Kiebrania na Kigiriki. ***"Mkono wa Bwana ukawa pamoja nao, watu wengi wakaamini, wakamwelekea Bwana."*** **Matendo 11:21.** **{SRSw 301.1}**

Waumini huko Yerusalemu waliposikia habari njema walifurahi; na Barnaba, ***"Maana alikuwa mtu mwema amejaa Roho Mtakatifu na Imani" Matendo 11:24*** alitumwa Antiokia, jiji kuu la Siria, kusaidia kanisa huko. Alifanya kazi huko kwa mafanikio makubwa. Kazi ilipoongezeka, aliomba na kupata msaada wa Paulo; na wanafunzi hao wawili walifanya kazi pamoja katika mji huo kwa mwaka mmoja, wakiwafundisha watu na kuongeza idadi ya kanisa la Kristo. **{SRSw 301.2}**

Antiokia ilikuwa na idadi kubwa ya Wayahudi na watu wa Mataifa; ilikuwa mahali pazuri pa kupumzika kwa wapenda raha na starehe, kwa sababu ya afya njema ya hali yake, mandhari yake nzuri, na utajiri, utamaduni, na uboreshaji uliokuwa katikati yake. Biashara yake kubwa iliifanya kuwa mahali pa umuhimu mkubwa, ambapo watu wa mataifa yote walipatikana. Kwa hivyo ilikuwa mji wa anasa na uovu. Hukumu ya Mungu hatimaye ilikuja juu ya Antiokia, kwa sababu ya uovu wa wakazi wake. **{SRSw 301.3}**

Hapa ndipo ilikuwa mahali ambapo wanafunzi waliitwa **Wakristo** kwa mara ya kwanza. Jina hili walipewa kwa sababu Kristo alikuwa mada kuu ya mahubiri yao, mafundisho, na mazungumzo. Walikuwa wakihesabu matukio ya maisha Yake kila mara wakati ambapo wanafunzi Wake walibarikiwa na ushirika Wake binafsi. Walizingatia mafundisho Yake bila kuchoka, miujiza Yake ya kuponya wagonjwa, kutoa pepo, na kufufua wafu. Kwa midomo inayotetemeka na macho yaliyojaa machozi walizungumza kuhusu maumivu Yake bustanini, kusalitiwa Kwake, majaribu, na kuuawa, uvumilivu na unyenyekevu unyenyekevu aliouonesha alipovumilia dharau na mateso aliyotendewa na maadui zake; na huruma yake ya Kiungu alipowaombea waliomtesa. Ufufuo Wake na kupaa Kwake mbinguni, pamoja na kazi Yake mbinguni kama Mpatanishi wa mwanadamu aliyeanguka, vilikuwa mada za furaha kwao. Wapagani wangeweza kuwaita Wakristo, kwani walihubiri kuhusu Kristo na walielekeza maombi yao kwa Mungu kupitia Yeye. **{SRSw 302.1}**

Paulo alipata, katika jiji lenye watu wengi la Antiokia, uwanja mzuri wa kazi, ambapo ujifunzaji wake mkubwa, hekima, na bidii, pamoja, vilikuwa na ushawishi mkubwa juu ya wakazi na wakazi wa mji huo wa ustaarabu. Wakati huo huo kazi ya mitume kitovu chake kilikuwa Yerusalemu, ambapo Wayahudi wa lugha zote na nchi zote

walikuja kuabudu hekaluni wakati wa sikukuu zilizotajwa. Katika nyakati kama hizo mitume walimhubiri Kristo kwa ujasiri usioyumba, ingawa walijua kwamba kwa kufanya hivyo maisha yao yalikuwa hatarini kila mara. **{SRSw 302.2}**

Watu wengi walioongoka kwa kuipokea imani, na hawa, wakitawanyika kwenda majumbani mwao katika sehemu tofauti za nchi, walitawanya mbegu za Kweli katika mataifa yote na miongoni mwa matabaka yote ya jamii. **{SRSw 302.3}**

Petro, Yakobo, na Yohana walihisi uhakika kwamba Mungu alikuwa amewateua kuhubiri Kristo miongoni mwa watu wa nchi yao wenyewe nyumbani. Lakini Paulo alikuwa amepokea agizo lake kutoka kwa Mungu, alipokuwa akisali hekaluni, na shamba lake pana la umishonari lilikuwa limewasilishwa mbele yake kwa uwazi wa ajabu. Ili kumwandaa kwa kazi yake pana na muhimu, Mungu alikuwa amemleta katika uhusiano wa karibu Naye, na akamfunulia kwa macho ya roho yake yaliyofurahi mwanga wa uzuri na utukufu wa mbinguni. **{SRSw 302.4}**

Kuwekwa wakfu kwa Paulo na Barnaba

Mungu aliwasiliana na manabii na walimu waaminifu katika kanisa la Antiokia. ***"Basi hawa walipokuwa wakimfanyia Bwana ibada na kufunga, Roho Mtakatifu akasema, Nitengeeni Barnaba na Sauli kwa kazi ile niliyowaitia."*** **Matendo 13:2**. Kwa hivyo mitume hawa walikuwa wamejiweka wakfu kwa Mungu kwa kicho kikubwa kwa kufunga na kuomba na kuwekewa mikono; nao walitumwa kwenda kwenye eneo lao la kazi miongoni mwa Mataifa. **{SRSw 303.1}**

Paulo na Barnaba wote wawili walikuwa wakifanya kazi kama wahudumu wa Kristo, na Mungu alikuwa amebariki juhudi zao kwa wingi, lakini hakuna hata mmoja wao ambaye hapo awali alikuwa

ameteuliwa rasmi kwa huduma ya injili kwa maombi na kuwekewa mikono. Sasa walikuwa wameruhusiwa na kanisa sio tu kufundisha Ukweli bali kubatiza na kupanga makanisa, wakiwa wamepewa mamlaka kamili ya kikanisa. Huu ulikuwa wakati muhimu kwa kanisa. Ingawa ukuta wa utengano kati ya Myahudi na Mmataifa ulikuwa umevunjwa na kifo cha Kristo, na kuwaruhusu Mataifa kupata haki kamili za injili, pazia lilikuwa bado halijaondolewa machoni pa Waamini wengi wa Kiyahudi, na hawakuweza kutambua waziwazi hadi mwisho wa kile ambacho kilifutwa au kuondolewea na Mwana wa Mungu. Kazi hiyo sasa ilipaswa kuendelezwe kwa nguvu miongoni mwa Mataifa, na ilitarajiwa kuimarisha kanisa kwa mkusanyiko mkubwa wa roho (waongofu). **{SRSw 303.2}**

Mitume katika kazi yao hii maalum walipaswa kukabiliwa na mashaka, chuki, na wivu. Kama matokeo ya kawaida ya kuacha msimamo wa kujitenga wa Wayahudi, mafundisho na maoni yao yangechukuliwa kama uzushi; na sifa zao kama wahudumu wa injili zingetiliwa shaka na Wayahudi wengi wenye bidii ya imani. Mungu aliona mapema matatizo haya yote ambayo watumishi Wake wangepitia, na, kwa uangalizi Wake wa busara, aliwapatia mamlaka isiyo na shaka kutoka kwa kanisa lililoanzishwa la Mungu, ili kazi yao isipingwe kwa urahisi. **{SRSw 304.1}**

Kuwekwa wakfu kwa kuwekewa mikono, baadaye, kulianza kutumiwa vibaya sana; umuhimu usio na msingi ulihusishwa na kitendo hicho, kana kwamba nguvu maalum huja mara moja kwa wale wanaowekwa mikono, na kuwafanya wawe tayari kwa kazi yoyote ya huduma, kana kwamba nguvu ipo katika tendo lenyewe la kuwekwa mikono. Katika historia ya mitume hawa wawili, tuna rekodi rahisi tu ya kuwekewa mikono, na athari yake katika kazi yao. Paulo na Barnaba walikuwa tayari wamepokea agizo lao kutoka kwa Mungu Mwenyewe;

na sherehe ya kuwekewa mikono haikuongeza neema mpya au uwezo mpya wa kiroho. Ilikuwa tu ni kuidhinishwa kwa kazi ya Mungu na kanisa, [kuweka muhuri au stempu]—alama ya utambuzi rasmi wa nafasi au ofisi, au kazi waliyopewa. **{SRSw 304.2}**

Mkutano wa Kwanza wa Konferensi Kuu

Baadhi ya Wayahudi kutoka Uyahudi (Yudea) walileta msukosuko mkubwa miongoni mwa Mataifa waliokuwa wameamini kwa kuanzisha mjadala kuhusu suala la tohara. Walisisitiza kwa ujasiri mkubwa kwamba hakuna mtu angeweza kuokolewa bila kutahiriwa na kushika sheria yote ya ibada za (sikukuu) za Kiyahudi au kaida [ceremonial laws[. **{SRSw 304.3}**

Hili lilikuwa suala muhimu sana, ambalo lililiathiri kanisa kwa kiwango kikubwa. Paulo na Barnaba walilikabili hili mara moja na kupinga kuletwa kwa jambo hilo kwa Mataifa. Hata hivyo, walipingwa na Wayahudi walioamini waliokuwa Antiokia, ambao waliunga mkono msimamo wa wale waliotoka Yudea. Jambo hilo lilisababisha mijadala mingi na ukosefu wa maelewano kanisani. Hatimaye, kanisa la Antiokia, likihofia kwamba mgawanyiko ungeweza kutokea, iwapo mjadala huo ungeendelea, liliamua kuwapeleka Paulo na Barnaba pamoja na baadhi ya watu wenye wajibu mkubwa kutoka Antiokia kwenda Yerusalemu ili kuwasilisha suala hilo mbele ya mitume na wazee. Huko walipaswa kukutana na wajumbe kutoka makanisa mbalimbali pamoja na wale waliokuwa wamekuja kuhudhuria sikukuu za kila mwaka zilizokuwa zinakaribia. Wakati huo huo, mabishano yote kuhusu suala hilo yalipaswa kusitishwa hadi uamuzi wa mwisho utakapofanywa na viongozi wenye mamlaka katika kanisa. Baada ya hapo**,** uamuzi huu ungekubaliwa na makanisa mbalimbali kote nchini. **{SRSw 305.1}**

Walipofika Yerusalemu, wajumbe kutoka Antiokia waliueleza mkutano wa makanisa mafanikio yaliyokuwa yamepatikana katika huduma yao, pamoja na mkanganyiko uliotokea kutokana na baadhi ya Mafarisayo waliokuwa wameongoka kudai kwamba waongofu wa Mataifa walipaswa kutahiriwa na kuishika Sheria ya Musa ili wapate kuokolewa. **{SRSw 305.2}**

Wayahudi walijivunia huduma na ibada zao walizopewa na Mungu. Kwa hiyo walihitimisha kwamba kwa kuwa Mungu alikuwa ameweka namna ya Kiebrania ya kuabudu, haingewezekana kamwe kwamba angeruhusu mabadiliko katika maelezo yoyote. Waliamua kwamba Ukristo lazima ujihusishe na sheria na sikukuu/taratibu/kaida za Kiyahudi. Walikuwa wepesi wa kushikilia yaliyopita, lakini walichelewa kutambua mwisho wa yale yaliyokuwa yameondolewa kwa kifo cha Kristo. Hawakuelewa kwamba sadaka zao zote zilikuwa ni kivuli na ishara ya kifo cha Mwana wa Mungu. Katika kifo hicho, mfano ulikutana na utimilifu wake, na hivyo kufanya ibada na sadaka za dini ya Kiyahudi zilizokuwa zimeagizwa na Mungu kuwa hazina thamani. **{SRSw 305.3}**

Paulo alikuwa akijivunia ukali wake wa Kifarisayo. Lakini baada ya Kristo kujifunua kwake katika njia ya kwenda Dameski, utume wa Mwokozi na kazi yake mwenyewe ya kuwaongoza Mataifa kwa Kristo alivielewa wazi. Alifahamu kikamilifu tofauti kati ya imani iliyo hai na dini ya nje yenye kufuata taratibu bila uhai wa kiroho. Paulo aliendelea kujiona kuwa mmoja wa wana wa Ibrahimu, na alizishika Amri Kumi kwa maandishi na kwa roho kwa uaminifu uleule aliokuwa nao kabla ya kuongoka na kuwa Mkristo. Hata hivyo, alijua kwamba ibada na taratibu za mfano zilipaswa kukoma kabisa hivi karibuni, kwa kuwa kile ambacho zilikuwa zikikionyesha kwa kivuli kilikuwa tayari kimetimia.

Nuru ya Injili ilikuwa ikiangaza juu ya dini ya Kiyahudi, na kuzipa maana mpya ibada na taratibu zake za kale. **{SRSw 306.1}**

Ushahidi wa Uzoefu wa Kornelio

Suala hili lililowasilishwa mbele ya baraza lilionekana kuwa na matatizo makubwa yasiyoweza kutatuliwa, bila kujali lilitazamwa kwa mtazamo gani. Hata hivyo, kwa hakika, Roho Mtakatifu alikuwa tayari amekwisha kulitatua suala hilo, ambalo juu ya uamuzi wake ustawi na hata kuwepo kwa kanisa la Kikristo kulitegemea. Mitume walipewa neema, hekima, na uwezo wa kutoa hukumu yenye mwongozo wa Mungu ili kuamua suala hilo lililokuwa linasumbua. **{SRSw 306.2}**

Petro alieleza kwamba Roho Mtakatifu alikuwa tayari ametoa uamuzi Wake kwa kushuka kwa nguvu zilezile juu ya Mataifa wasiotahiriwa kama alivyoshuka juu ya Wayahudi waliotahiriwa. Alisimulia maono yake, ambapo Mungu alimwonyesha nguo kubwa iliyojaa kila aina ya wanyama wenye miguu minne, na akamwamuru achinje na ale. Petro alieleza kwamba alipokataa, akithibitisha kwamba hajawahi kula kile kilicho kichafu au najisi, Mungu alimwambia: Mungu alisema, ***"Kile ambacho Mungu amekitakasa, usikiite najisi."*** **{SRSw 306.2}**

Alisema, "***Na Mungu, ajuaye mioyo ya watu, akawashuhudia, akiwapa Roho Mtakatifu vile vile kama alivyotupa sisi wala hakufanya tofauti kati yetu sisi na wao, akiwasafisha mioyo yao kwa imani. Basi sasa mbona mnamjaribu Mungu na kuweka kongwa juu ya shingo za wanafunzi, ambalo baba zetu wala sisi hatukuweza kulichukua?" Matendo 15:8-10*** **{SRSw 307.1}**

Nira hii haikuwa sheria ya Amri Kumi, kama wanavyodai wale wanaopinga wajibu wa kuishika sheria hiyo. Badala yake, Petro alikuwa akirejelea sheria ya kaida/taratibu na sikukuu za kidini, ambayo

ilibatilishwa/ilifutwa na kupoteza nguvu zake kupitia kusulubiwa kwa Kristo. Hotuba hii ya Petro ilileta mkutano hadi mahali ambapo wangeweza kuwasikiliza Paulo na Barnaba kwa busara, na kwa mantiki mbayo walieleza uzoefu wao katika kazi ya kuwahudumia Mataifa. **{SRSw 307.2}**

Uamuzi

Yakobo alitoa ushuhuda wake kwa msimamo thabiti, akisema kwamba Mungu alikuwa amekusudia kuwajumuisha Mataifa ili nao wafurahie haki na fursa zote ambazo Wayahudi walikuwa nazo. Roho Mtakatifu aliona kuwa si vyema kuwabebesha waongofu wa Mataifa mzigo wa sheria za taratibu na sikukuu za kidini. Vivyo hivyo, mitume na wazee, baada ya kulichunguza suala hilo kwa makini, waliliona kwa mtazamo huo huo. Mawazo yao yalipatana na mapenzi ya Roho wa Mungu. Yakobo ndiye aliyekuwa akiongoza mkutano huo wa baraza, na uamuzi wake wa mwisho ulikuwa: "***Kwa sababu hiyo mimi naamua hivi; Tusiwataabishe wale waliomgeukia Mungu katika Mataifa" Matendo 15:19*** **{SRSw 307.3}**

Uamuzi wake ulikuwa kwamba sheria za kaida/taratibu za kidini, na hasa agizo la tohara, zisilazimishwe kwa Mataifa kwa namna yoyote ile, wala hata zisipendekezwe kwao kama jambo la lazima. Yakobo alitaka kuwafahamisha ndugu zake kwamba Mataifa walipomgeukia Mungu na kuacha ibada za sanamu, walikuwa wamefanya mabadiliko makubwa katika imani yao; na kwamba tahadhari nyingi inapaswa kutumiwa kutosumbua akili zao kwa maswali yenye utata na yenye mashaka, wasije wakakata tamaa katika kumfuata Kristo. **{SRSw 307.4}**

Hata hivyo, Mataifa hawakupaswa kufanya jambo lolote ambalo lingeenda kinyume kwa kiasi kikubwa na mitazamo ya ndugu zao Wayahudi, au ambalo lingeweza kuleta chuki na upinzani akilini mwao

dhidi yao. Kwa hiyo, mitume na wazee walikubaliana kuwaandikia Mataifa barua ya kuwaagiza wajiepushe na vitu vilizotolewa sadaka kwa sanamu, uasherati, nyama zilizosongolewa, na damu. Pia walitakiwa kuzishika amri za Mungu na kuishi maisha matakatifu. Mataifa walihakikishiwa kwamba wale watu waliokuwa wakisisitiza tohara kwao hawakuwa wametumwa wala kupewa mamlaka hayo na mitume. **{SRSw 308.1}**

Paulo na Barnaba walipendekezwa kwao kama watu waliokuwa wamehatarisha maisha yao kwa ajili ya Bwana. Yuda na Sila walitumwa pamoja na mitume hawa kutangaza kwa Mataifa, kwa maneno, uamuzi wa baraza. Watumishi wanne wa Mungu walitumwa Antiokia na barua na ujumbe, ambao ulikomesha utata wote; kwani ilikuwa sauti ya mamlaka ya juu zaidi duniani. **{SRSw 308.2}**

Baraza hilo halikudai kwamba haliwezi kukosea katika maamuzi yake, bali liliongozwa na hukumu yenye nuru ya kiroho na kwa hadhi ya kanisa lililoanzishwa kwa mapenzi ya Mungu. Walitambua kwamba Mungu Mwenyewe alikuwa tayari amekwisha kuliamua suala hilo kwa kuwajalia Mataifa Roho Mtakatifu; hivyo kilichobaki kwao ilikuwa kufuata mwongozo wa Roho. **{SRSw 308.3}**

Waumini wote wa Kikristo hawakuitwa kupiga kura kuhusu jambo hilo. Mitume na wazee—watu wenye ushawishi, busara na uwezo wa kutoa maamuzi—ndio walioiweka kwenye maandishi [framed] na kutoa tamko hilo, ambalo baadaye lilikubaliwa kwa ujumla na makanisa ya Kikristo. Hata hivyo, wote hawakufurahishwa na uamuzi huu; Kulikuwa na kundi la ndugu wa uongo ambao walijipa mamlaka ya kuanzisha kazi kwa uwajibikaji wao wenyewe. Walijishughulisha na manung'uniko na kutafuta makosa kwa wengine, wakipendekeza mipango mipya na kujaribu kubomoa kazi ya wale watu wenye uzoefu ambao Mungu alikuwa amewaweka rasmi kufundisha mafundisho ya Kristo. Kanisa

limekuwa likikabiliana na vikwazo vya aina hiyo tangu mwanzo wake, na litaendelea kukutana navyo hadi mwisho wa wakati. **{SRSw 309.1}**

SURA YA 42—MIAKA YA HUDUMA YA PAULO

Paulo alikuwa mfanyakazi asiyechoka. Alisafiri kila mara kutoka sehemu hadi sehemu, wakati mwingine kupitia maeneo yasiyo na ukarimu au urafiki, wakati mwingine majini, kupitia dhoruba na tufani. Hakuruhusu chochote kumzuia kufanya kazi yake. Alikuwa mtumishi wa Mungu na lazima atekeleze mapenzi Yake. Kwa neno la mdomo na kwa barua alileta ujumbe ambao tangu wakati huo umeleta msaada na nguvu kwa kanisa la Mungu. Kwetu sisi, tukiishi mwishoni mwa historia ya dunia hii, ujumbe alioubeba unazungumza waziwazi kuhusu hatari ambazo zitatishia kanisa, na mafundisho ya uongo ambayo watu wa Mungu watalazimika kukutana nayo. **{SRSw 310.1}**

Kutoka nchi hadi nchi na kutoka mji hadi mji Paulo alikwenda, akihubiri kuhusu Kristo na kuanzisha makanisa. Popote alipoweza kupata watu wa kumsikiliza, alijitahidi kukabiliana na makosa na

kuwaongoza wanaume na wanawake katika njia ya haki. Wale ambao, kupitia huduma yake, walimkubali Kristo katika mahali popote, aliwapanga na kuwaunganisha katika kanisa. Haijalishi walikuwa wachache kiasi gani, hili lilifanyika. Na Paulo hakusahau makanisa aliyokuwa ameanzisha. Bila kujali kanisa lilikuwa dogo kiasi gani, lilikuwa lengo na sababu ya thamani kwake, na aliliangalia kwa uangalifu, upendo na kujali kwa dhati. **{SRSw 310.2}**

Wito wa Paulo ulimtaka afanye huduma za aina mbalimbali — akifanya kazi kwa mikono yake ili kujipatia riziki, akianzisha makanisa, akiandika barua kwa makanisa ambayo tayari yameanzishwa. Lakini katikati ya kazi hizi mbalimbali alitangaza, ***"ila natenda neno moja tu." (Wafilipi 3:13.)*** Lengo moja alilokuwa nalo ni kuwa thabiti mbele yake katika kazi yake yote—kuwa mwaminifu kwa Kristo, ambaye, alipokuwa akikufuru Jina Lake na kutumia kila njia katika uwezo wake kuwafanya wengine walikufuru, Alikuwa amejifunua kwake. Kusudi moja kuu la maisha yake lilikuwa kumtumikia na kumheshimu Yeye ambaye Jina Lake lilikuwa limemjaza dharau hapo awali. Tamaa yake moja ilikuwa kuwaleta watu kwa Mwokozi. Myahudi na Mmataifa wangeweza kumpinga na kumtesa, lakini hakuna kitu ambacho kingeweza kumgeuza kutoka kwenye kusudi lake. **{SRSw 310.3}**

Paulo Anaelezea Uzoefu Wake

Akiwaandikia Wafilipi, anaelezea uzoefu wake kabla na baada ya kuongoka kwake. ***"Mtu yeyote akijiona kuwa anayo sababu ya kuutumainia mwili, mimi zaidi.*** anasema **Nalitahiriwa siku ya nane, ni mtu wa taifa la Israeli, wa kabila ya Benyamini, Mwebrania wa Waebrania, kwa habari ya kuishika torati, ni Farisayo, kwa habari ya juhudi, mwenye kuliudhi Kanisa, kwa habari ya haki ipatikanayo kwa sheria sikuwa na hatia." Wafilipi 3:4-6. {SRSw 311.1}**

Baada ya kuongoka kwake, ushuhuda wake ulikuwa: **{SRSw 311.2}**

“Naam, zaidi ya hayo, nayahesabu mambo yote kuwa hasara kwa ajili ya uzuri usio na kiasi wa kumjua Kristo Yesu, Bwana wangu; ambaye kwa ajili Yake nimepata hasara ya mambo yote nikiyahesabu kuwa kama mavi ili nipate Kristo; tena nionekane katika Yeye, nisiwe na haki yangu mwenyewe ipatikanayo kwa sheria, bali ile ipatikanayo kwa imani iliyo katika Kristo, haki ile itokayo kwa Mungu, kwa Imani.” Wafilipi 3:8, 9, **{SRSw 311.3}**

Haki ambayo hapo awali alikuwa ameifikiria sana, sasa haikuwa na thamani machoni pake. Shauku ya roho yake ilikuwa***: “ili nimjue Yeye, na uweza wa kufufuka Kwake, na ushirika wa mateso Yake, nikifananishwa na kufa Kwake; ili nipate kwa njia yoyote kuifikia kiyama ya wafu. Kujitahidi Kuelekea kwa Lengo. Si kwamba nimekwisha kufika, au nimekwisha kuwa mkamilifu; la! Bali nakaza mwendo ili nipate kulishika lile ambalo kwa ajili yake nimeshikwa na Kristo Yesu. Ndugu, sijidhanii nafsi yangu kwamba nimekwisha kushika; ila natenda neno moja tu; nikiyasahau yaliyo nyuma, nikiyachuchumilia yaliyo mbele; nakaza mwendo, niifikilie mede ya thawabu ya mwito mkuu wa Mungu katika Kristo Yesu. ”Wafilipi 3:10-14.*** **{SRSw 311.4}**

Mfanyakazi Anayeweza Kubadilika

Mwone akiwa gerezani huko Filipi, ambapo, licha ya maumivu yake mwilini, wimbo wake wa sifa unavunja ukimya wa usiku wa manane. Baada ya tetemeko la ardhi kufungua milango ya gereza, sauti yake inasikika tena, kwa maneno ya furaha kwa mlinzi wa gereza mpagani, ***"Usijidhuru: kwa maana sisi sote tupo hapa" Matendo 16:28*** kila mtu mahali pake, akiwa amezuiliwa na uwepo wa mfungwa mwenzake. Na mlinzi wa gereza, akiwa amehukumiwa kwa Ukweli wa

imani hiyo inayomtegemeza Paulo, anauliza njia ya wokovu, na pamoja na nyumba yake yote inaungana na kundi linaloteswa la wanafunzi wa Kristo. **{SRSw 312.1}**

Mtazame Paulo huko Athene mbele ya baraza la Areopago, anapokutana na sayansi kwa sayansi, mantiki kwa mantiki, na falsafa kwa falsafa. Angalia jinsi, kwa busara iliyotokana na upendo wa Bwana, anavyomwelekeza Yehova kama ***"Mungu Asiyejulikana,"*** ambaye wasikilizaji wake wamemwabudu bila kujua; na kwa maneno yaliyonukuliwa kutoka kwa mshairi wao wenyewe, anamwakilisha Mungu kama Baba ambaye wao ni watoto Wake. Msikilize, katika enzi hiyo ya matabaka, wakati haki za mwanadamu kama mwanadamu hazikutambuliwa kabisa, anapoelezea ukweli mkuu wa undugu wa kibinadamu, akitangaza kwamba Mungu ***"alifanya kila taifa la wanadamu kutoka katika mmoja, wakae juu ya uso wa nchi yote" Matendo 17:26*** Kisha anaonyesha jinsi, kupitia shughuli zote za Mungu na mwanadamu, zinavyoenda kama uzi wa dhahabu, makusudi Yake ya neema na rehema. Yeye **"akiisha kuwawekea nyakati alizoziamuru tangu zamani, na mipaka ya makazi yao; ili wamtafute Mungu ingawa kwa kupapaswa-papasa, wakamwone, ijapokuwa hawi mbali na kila mmoja wetu" Matendo 17:26** **{SRSw 312.2}**

Msikilize katika mahakama ya Festo, Mfalme Agripa, alipohukumiwa na ukweli wa injili, anaposema, ***"Kwa maneno machache wadhani kunifanya mimi kuwa Mkristo." Matendo 26:28*** Kwa heshima gani ya upole, Paulo, akielekeza kwenye mnyororo wake, anajibu, "***Namwomba Mungu kwamba, ikiwa kwa machache au ikiwa kwa mengi, si wewe tu ila na hao wote wanaonisikia leo wawe kama mimi, isipokuwa vifungo hivi." Matendo 26:29*** **{SRSw 313.1}**

Hivyo ndivyo maisha yake yalivyopita, kama ilivyoelezwa katika maneno yake mwenyewe, "***katika kusafiri mara nyingi; hatari za mito;***

hatari za wanyang'anyi; hatari kwa taifa langu; hatari kwa mataifa mengine; hatari za mjini; hatari za jangwani; hatari za baharini; hatari kwa ndugu za uongo; katika taabu na masumbufu; katika kukesha mara nyingi; katika njaa na kiu; katika kufunga mara nyingi; katika baridi na kuwa uchi." 2 Wakorintho 1:26, 27. "Tukitukanwa" alisema "twabariki tukiudhiwa twastahimili; tukisingiziwa twasihi; tumefanywa kama takataka za dunia, na tama ya vitu vyote hata sasa." 1 Wakorintho 4:12, 13; 2 Wakorintho 6:10. **{SRSw 313.2}**

Huduma Katika Vifungo

Ingawa alikuwa mfungwa kwa muda mrefu, lakini Bwana aliendeleza kazi Yake maalum kupitia yeye. Vifungo vyake vilikuwa njia ya kueneza maarifa ya Kristo na hivyo kumtukuza Mungu. Aliposafirishwa kutoka mji hadi mji kwa ajili ya kesi yake, ushuhuda wake kuhusu Yesu na matukio ya kuvutia ya uongofu wake ulisimuliwa mbele ya wafalme na magavana, ili kwamba wasiwe na udhuru kuhusu Yesu. Maelfu walimwamini na kufurahi katika Jina Lake. **{SRSw 313.4}**

Niliona kwamba kusudi maalum la Mungu lilitimizwa katika safari ya Paulo baharini; Alikusudia kwamba wafanyakazi wa meli waweze kushuhudia nguvu ya Mungu kupitia Paulo, na kwamba mataifa pia waweze kusikia Jina la Yesu, na kwamba wengi waweze kuongoka kupitia mafundisho ya Paulo na kwa kushuhudia miujiza aliyofanya. Wafalme na magavana walivutiwa na hoja zake, na kwa bidii na nguvu ya Roho Mtakatifu alivyomhubiri Yesu na kusimulia matukio ya kuvutia na kugusa moyo, ya uzoefu wake, walishawishika moyoni mwao kwamba Yesu alikuwa Mwana wa Mungu. **{SRSw 314.1}**

SURA YA 43—USHAHIDI KIFO CHA PAULO NA PETRO

Mitume Paulo na Petro kwa miaka mingi walikuwa wametengana sana katika kazi zao, ikiwa ni kazi ya Paulo kupeleka injili kwa Mataifa, huku Petro akifanyia kazi hasa kwa ajili ya Wayahudi. Lakini katika imipango na majaliwa ya Mungu, wote wawili walipaswa kumshuhudia Kristo katika mji mkuu wa dunia, na juu ya ardhi yake wote wawili walipaswa kumwaga damu yao kama mbegu ya mavuno mengi ya watakatifu na mashahidi wa imani. **{SRSw 315.1}**

Karibu na wakati wa kukamatwa kwa pili kwa Paulo, Petro pia alikamatwa na kutupwa gerezani. Alikuwa amejifanya kuwa chukizo hasa kwa mamlaka kwa bidii na mafanikio yake katika kufichua udanganyifu na kushinda njama za Simon Magus, mchawi, aliyemfuata hadi Rumi kupinga na kuzuia kazi ya injili. Nero alikuwa muumini wa uchawi, na alikuwa amemfadhili/amemlinda/kumtetea Simon. Kwa hivyo alikasirika sana dhidi ya mtume huyo, na hivyo akaamuru akamatwe. **{SRSw 315.2}**

Uchungu wa mfalme dhidi ya Paulo uliongezeka kutokana na ukweli kwamba watu wa nyumba ya kifalme, na pia watu wengine wa heshima, walikuwa wameongoka na kuwa Wakristo wakati wa kifungo chake cha kwanza. Kwa sababu hii, alifanya kifungo cha pili kuwa kigumu zaidi kuliko cha kwanza, akimpa fursa ndogo ya kuhubiri injili; na akaamua kufupisha maisha yake mara tu atakapopata sababu yoyote ya kufanya hivyo. Akili ya Nero ilivutiwa na kuguswa sana na nguvu ya maneno ya mtume katika kesi yake ya mwisho kiasi kwamba aliahirisha uamuzi wa kesi hiyo, bila kumwachilia huru wala kumhukumu. Lakini hukumu hiyo iliahirishwa (ilicheleweshwa) tu. Haikuchukua muda mrefu kabla ya uamuzi uliompeleka Paulo kwenye kifo cha kishahidi-

Kufia dini. Kwa kuwa alikuwa raia wa Rumi, hangeweza kuteswa kwa mateso ya kikatili, hivyo alihukumiwa kukatwa kichwa**.** **{SRSw 315.3}**

Petro, kama Myahudi na mgeni, alihukumiwa kupigwa mijeledi na kusulubiwa. Kwa matarajio ya kifo hiki cha kutisha, mtume alikumbuka dhambi yake kubwa ya kumkana Yesu katika saa ya majaribu, na wazo lake pekee lilikuwa kwamba yeye hakustahili heshima kubwa kiasi cha kufa kwa njia sawa na Bwana wake. Petro alikuwa ametubu kwa dhati dhambi hiyo, na alikuwa amesamehewa na Kristo, kama inavyoonyeshwa na agizo kuu alilopewa la kulisha kondoo na wana-kondoo wa kundi. Lakini hakuweza kamwe kujisamehe mwenyewe. Hata mawazo ya mateso ya tukio la mwisho baya hayangeweza kupunguza uchungu wa huzuni na toba yake. Kama neema ya mwisho aliwasihi wauaji wake kwamba apigiliwe misumari msalabani huku kichwa chake kikiwa chini na miguu juu. Ombi hilo likakubaliwa, na kwa njia hii mtume mkuu Petro akafa. **{SRSw 316.1}**

Ushahidi wa Mwisho wa Paulo

Paulo aliongozwa faraghani hadi mahali pa kuuawa. Watesi wake, wakiwa na hofu kutokana na kiwango cha ushawishi wake, waliogopa kwamba waongofu wangeweza kuingizwa katika Ukristo hata kupitia eneo na tukio la kifo chake. Kwa hivyo watazamaji wachache waliruhusiwa kuwepo. Lakini askari waliosimama imara walioteuliwa kumhudhuria walisikiliza maneno yake, na kwa mshangao walimwona akiwa mchangamfu na mwenye furaha wakitarajia kifo kama hicho. Roho yake ya msamaha kwa wauaji wake na imani isiyoyumba katika Kristo hadi mwisho kabisa ilithibitika kuwa ladha ya uzima kwa baadhi ya walioshuhudia mauaji yake. Zaidi ya mtu mmoja, walimkubali Mwokozi haraka sana, ambaye Paulo alihubiri, na bila woga wakaithibitisha imani yao hata kwa kumwaga damu yao. **{SRSw 316.2}**

Maisha ya Paulo, hadi saa yake ya mwisho kabisa, yalishuhudia ukweli wa maneno yake katika waraka wa pili kwa Wakorintho: ***"Kwa kuwa Mungu, aliyesema, Nuru itang'aa toka gizani, Ndiye aliyeng'aa mioyoni mwetu, atupe nuru ya elimu ya utukufu wa Mungu katika uso wa Yesu Kristo. Lakini tuna hazina hii katika vyombo vya udongo, ili adhama kuu ya uwezo iwe ya Mungu, wala si kutoka kwetu. Pande zote twadhikika, bali hatusongwi; twaona shaka, bali hatukati tamaa; twaudhiwa, bali hatuachwi; twatupwa chini, bali hatuangamizwi; siku zote twachukua katika mwili kuuawa Kwake Yesu, ili uzima wa Yesu nao udhihirishwe katika miili yetu." 2 Wakorintho 4:6-102*** Uwezo wa utoshelevu wake haukutokana na yeye mwenyewe, bali katika uwepo na utendaji wa Roho wa Mungu aliyekuwa ameujaza moyo wake na kutiisha kila wazo chini ya mapenzi ya Kristo. Ukweli kwamba maisha yake mwenyewe yalionyesha Ukweli alioutangaza ulimpa nguvu ya kusadikisha mahubiri yake na mwenendo wake. Anasema nabii, "***Utamlinda yeye ambaye moyo wake umekutegemea Wewe, Katika amani kamilifu, kwa kuwa anakutumaini Wewe." Isaya 26:3***. Ilikuwa ni amani hii iliyotoka mbinguni, iliyoonyeshwa usoni, ambayo iliwavutia watu wengi kwa injili, na wengi wakaikubali injili. **{SRSw 317.1}**

Mtume alikuwa akitazama sehemu kubwa ya ng'ambo, si kwa kutokuwa na uhakika au kwa hofu, bali kwa tumaini la furaha na matarajio ya matumaini. Aliposimama mahali pa kuuawa kwa imani hakuona upanga unaong'aa wa muuaji wala ardhi ya kijani iliyokuwa tayari kupokea damu yake; badala yake alitazama juu kupitia anga tulivu la siku hiyo ya kiangazi hadi kwenye kiti cha enzi cha Milele. **Alisema moyoni mwake:** ***Ee Bwana, Wewe ni faraja yangu na sehemu yangu. Ni lini nitakapokukumbatia? Ni lini nitakapokuona uso kwa uso bila pazia kati yetu?*** **{SRSw 317.2}**

Paulo alibeba ndani ya maisha yake duniani angahewa ya mbinguni. Wote waliokuwa wakishirikiana naye walihisi ushawishi ya uhusiano wake na Kristo na ushirika wake na malaika. Hapa ndipo nguvu ya Ukweli ilipo—ushawishi wa maisha matakatifu usiohitaji maneno mengi ndio mahubiri yenye nguvu zaidi ya Ukristo. Hoja, hata kama haijibiki, inaweza kusababisha upinzani tu; lakini mfano wa utauwa una nguvu ambayo haiwezekani kupingwa kabisa. **{SRSw 318.1}**

Ingawa mtume alipoteza mtazamo wa mateso yake yaliyokaribia, alihisi wasiwasi mkubwa kwa wanafunzi ambao alikuwa karibu kuwaacha ili kukabiliana na ubaguzi, chuki, na mateso. Alijitahidi kuwaimarisha na kuwatia moyo Wakristo wachache walioandamana naye hadi mahali pa kuuawa, kwa kurudia ahadi za thamani kubwa zilizotolewa kwa ajili ya wale wanaoteswa kwa ajili ya haki. Aliwahakikishia kwamba hakuna kitakachoshindwa katika yote ambayo Bwana amesema kuhusu waaminifu Wake waliojaribiwa. Watainuka na kuangaza; kwa maana nuru ya Bwana itawazukia. Watavaa mavazi yao mazuri wakati utukufu wa Bwana utakapofunuliwa. Kwa muda mfupi wanaweza kuwa katika uzito kupitia majaribu mengi, wanaweza kuwa hawana faraja ya kidunia; lakini lazima wajipe moyo kwa kusema, Namjua Yeye niliyemwamini. Anaweza kulinda kile nilichomkabidhi. Adhabu yao itapita, na asubuhi ya furaha na amani kamilifu itakuja. **{SRSw 318.2}**

Kiongozi wa wokovu wetu amemwandaa mtumishi Wake kwa pambano kubwa la mwisho. Akiwa amekombolewa kwa dhabihu ya Kristo, ameoshwa kutoka kwa dhambi katika damu Yake, na amevikwa haki Yake, Paulo ana ushuhuda ndani yake kwamba roho yake ni ya thamani machoni pa Mkombozi wake. Maisha yake yamefichwa pamoja na Kristo katika Mungu, na ana hakika kwamba Yeye ambaye ameshinda kifo anaweza kutunza kile kilichowekwa chini ya amana

Yake. Akili yake inashikilia ahadi ya Mwokozi, ***"Nami nitamfufua siku ya mwisho." Yohana 6:40.*** Mawazo na matumaini yake yanalenga katika ujio wa pili wa Bwana wake. Na upanga wa mwuaji unaposhuka na vivuli vya kifo vikikusanyika kuzunguka roho ya shahidi, wazo lake la hivi karibuni linajitokeza, kama vile wazo lake la kwanza katika kuamka kwake, kukutana na Mtoa Uzima ambaye atamkaribisha kwenye furaha ya waliobarikiwa. **{SRSw 318.3}**

Karibu karne nyingi zimepita tangu Paulo alipomwaga damu yake kama shahidi wa Neno la Mungu na kwa ajili ya ushuhuda wa Kristo. Hakuna mkono mwaminifu ulioandika kwa vizazi vijavyo matukio ya mwisho katika maisha ya mtu huyu mtakatifu; lakini uvuvio umetuhifadhia ushuhuda wake wa kufa. Kama tarumbeta sauti Yake imesikika katika vizazi vyote, ikitia moyo kwa ujasiri wake maelfu ya mashahidi wa Kristo, na kuamsha katika maelfu ya mioyo yenye huzuni mwangwi wa furaha yake ya ushindi: "***Kwa maana, mimi sasa namiminwa, na wakati wa kufariki kwangu umefika. Nimevipiga vita vilivyo vizuri, mwendo nimeumaliza, Imani nimeilinda; baada ya hayo nimewekewa taji ya haki, ambayo Bwana, mhukumu Mwenye haki, atanipa siku ile; wala si mimi tu, bali na watu wote pia waliopenda kufunuliwa Kwake. 2 Timotheo 4:6-8.*** **{SRSw 319.1}**

SURA YA 44—UASI MKUU

Yesu alipowafunulia wanafunzi Wake hatima ya Yerusalemu na matukio ya ujio wa pili, alitabiri pia uzoefu wa watu Wake kuanzia wakati ambapo angechukuliwa kutoka kwao hadi kurudi Kwake kwa nguvu na utukufu kwa ajili ya ukombozi wao. Kutoka Mlima wa Mizeituni, Mwokozi aliona dhoruba zikikaribia kuangukia kanisa la mitume, na, akipenya zaidi katika siku zijazo, jicho Lake lilitambua dhoruba kali, za uharibifu ambazo zingewapiga wafuasi Wake katika nyakati zijazo za giza na mateso. Katika matamshi machache mafupi, yenye umuhimu wa kutisha, alitabiri sehemu ambayo watawala wa ulimwengu huu wangeipatia kanisa la Mungu. Wafuasi wa Kristo lazima watembee njia ile ile ya aibu, lawama, na mateso ambayo Bwana wao alikanyaga. Uadui uliozuka dhidi ya Mkombozi wa ulimwengu ungedhihirika dhidi ya wote wanaopaswa kuamini Jina Lake. **{SRSw 320.1}**

Historia ya kanisa la awali ilishuhudia utimilifu wa maneno ya Mwokozi. Nguvu za dunia na kuzimu zilijipanga dhidi ya Kristo kupitia wafuasi Wake. Upagani ulitabiri kwamba iwapo injili ingeshinda, mahekalu na madhabahu zake zingeondolewa; kwa hivyo uliita majeshi yake kuharibu Ukristo. Moto wa mateso uliwaka. Wakristo walinyang'anywa mali zao na kufukuzwa kutoka majumbani mwao. ***" wengine walijaribiwa kwa dhihaka na mapigo, naam, kwa mafungo, na kwa kutiwa gerezani;"*** **Waebrania 11:36**. Idadi kubwa ilitia muhuri ushuhuda wao kwa damu yao. Wenye heshima na watumwa, matajiri na

maskini, waungwana- wasomi na wajinga, waliuawa bila huruma. **{SRSw 320.2}**

Jitihada za Shetani za kuharibu kanisa la Kristo kwa vurugu na ukatili zilikuwa bure. Pambano kubwa ambao wanafunzi wa Yesu walijitoa maisha yao halikukoma wakati hawa wabebaji bendera waaminifu walipoanguka katika nafasi yao. Kwa kushindwa, walishinda. Watendakazi wa Mungu waliuawa, lakini kazi Yake iliendelea mbele kwa kasi. Injili iliendelea kuenea, na idadi ya wafuasi Wake kuongezeka. Ilipenya katika maeneo ambayo hata nguvu ya Rumi haikuyafikia. Alisema Mkristo mmoja, akitoa malalamiko kwa watawala wa kipagani waliokuwa wakihimiza kuendeleza mateso: Unaweza "kutuua, kututesa, kutuhukumu.... Udhalimu wako ni uthibitisho kwamba hatuna hatia.... Wala ukatili wako ... haukufaidii kitu." Ilikuwa ni mwaliko wenye nguvu zaidi wa kuwaleta wengine kwa ushawishi wao. "Kadiri mnavyotuua, ndivyo idadi yetu inavyoongezeka; damu ya Wakristo ni mbegu." **{SRSw 321.1}**

Maelfu walifungwa na kuuawa; lakini wengine walijitokeza kujaza nafasi zao. Na wale waliouawa kwa ajili ya imani yao waliwekwa salama kwa Kristo, na wakahesabiwa kuwa washindi. Walikuwa wamepigana vita vizuri, na walipaswa kupokea taji ya utukufu wakati Kristo atakapokuja. Mateso waliyoyavumilia yaliwaleta Wakristo karibu zaidi na Mkombozi wao. Mfano wao hai na ushuhuda wao wa kufa/kifo vilikuwa ushuhuda wa kudumu kwa ajili ya Ukweli; na, pale ambapo haikutarajiwa sana, raia wa Shetani walikuwa wanaacha huduma yake na kujiandikisha chini ya bendera ya Kristo. **{SRSw 321.2}**

Maelewano na Upagani

Kwa hivyo Shetani aliweka mipango yake ya kupigana vita kwa mafanikio zaidi dhidi ya serikali ya Mungu, kwa kupanda bendera Yake katika kanisa la Kikristo. Ikiwa wafuasi wa Kristo wangeweza kudanganywa na kuongozwa kumchukiza Mungu, basi nguvu zao, ushujaa, na uthabiti wao ungeshindwa, na wangeanguka kama mawindo rahisi. **{SRSw 322.1}**

Adui mkuu sasa alijitahidi kupata kwa hila kile ambacho alikuwa ameshindwa kukipata kwa nguvu. Mateso yalikoma, na badala yake yakabadilishwa na vivutio hatari vya ustawi wa muda na heshima ya kidunia. Waabudu sanamu waliongozwa kupokea sehemu ya imani ya Kikristo, huku wakikataa Ukweli mwingine muhimu. Walidai kumkubali Yesu kama Mwana wa Mungu na kuamini kifo Chake na ufufuo Wake; lakini hawakuhisi hatia ya dhambi na hawakuhisi haja ya toba au mabadiliko ya moyo. Kwa makubaliano ya ungamo la namna fulani kwa upande wao, walipendekeza kwamba Wakristo wanapaswa kufanya makubaliano, ili wote waungane kwenye jukwaa la imani katika Kristo. **{SRSw 322.2}**

Sasa kanisa lilikuwa katika hatari ya kutisha. Gereza, mateso, moto, na upanga vilikuwa baraka ikilinganishwa na hili. Baadhi ya Wakristo walisimama imara, wakitangaza kwamba hawangeweza kufanya makubaliano. Wengine walifikiri kwamba ikiwa wangekubali au kurekebisha baadhi ya vipengele vya imani yao, na kuungana na wale waliokubali sehemu ya Ukristo, inaweza kuwa njia ya uongofu wao kamili. Huo ulikuwa wakati wa maumivu makali kwa wafuasi waaminifu wa Kristo. Chini ya kivuli cha vazi la Ukristo la kujifanya [feki], Shetani alikuwa akijiingiza ndani ya kanisa, ili kuipotosha imani yao na kugeuza mawazo yao kutoka kwenye Neno la Kweli. **{SRSw 322.3}**

Hatimaye sehemu kubwa ya kundi la Wakristo walishusha kiwango chao, na muungano ukaundwa kati ya Ukristo na imani ya kipagani. Ingawa waabudu sanamu walidai kuwa wameongoka, na waliungana na kanisa, bado walishikilia ibada yao ya sanamu, wakibadilisha tu vitu vya ibada yao kuwa sanamu za Yesu, na hata za Mariamu na watakatifu. Chachu chafu ya ibada ya sanamu, iliyoingizwa kanisani, iliendelea na kazi yake mbaya. Mafundisho yasiyofaa, ibada za kishirikina, na sherehe za ibada ya sanamu ziliingizwa katika imani na ibada yake. Wafuasi wa Kristo walipoungana na waabudu sanamu, dini ya Kikristo iliharibika na kanisa likapoteza usafi na nguvu Zake. Hata hivyo, kulikuwa na baadhi ambao hawakupotoshwa na udanganyifu huu. Bado walidumisha uaminifu wao kwa Mwanzilishi wa Ukweli na kumwabudu Mungu pekee. **{SRSw 322.4}**

Daima kumekuwa na makundi mawili kati ya wale wanaodai kuwa wafuasi wa Kristo. Wakati kundi moja linajifunza maisha ya Mwokozi na kutafuta kwa bidii kurekebisha kasoro zao na kufuata Kielelezo, kundi lingine huepuka Ukweli ulio wazi na wa kivitendo unaofichua makosa yao. Hata katika hali yake bora kanisa halikuwa limeundwa kikamilifu na udhati, usafi, Ukweli [Watu, mafundisho nk]. Mwokozi wetu alifundisha kwamba wale wanaojihusisha na dhambi kimakusudi hawapaswi kupokelewa kanisani; lakini aliwaunganisha na Yeye watu waliokuwa na kasoro katika tabia, na akawapa fursa za mafundisho na mfano Wake, ili waweze kupata fursa ya kuona na kurekebisha makosa yao. **{SRSw 323.1}**

Lakini hakuna muungano kati ya Mkuu wa nuru na mkuu wa giza, na hakuwezi kuwa na muungano kati ya wafuasi wao. Wakristo walipokubali kuungana na wale waliokuwa wameongoka nusu-nusu tu kutoka kwa upagani, waliingia kwenye njia iliyoongoza mbali zaidi na zaidi kutoka kwa Ukweli. Shetani alifurahi kwamba alikuwa

amefanikiwa katika kuwadanganya idadi kubwa ya wafuasi wa Kristo. Kisha akaleta nguvu zake kuwashinikiza kikamilifu zaidi, na akawatia moyo kuwatesa wale waliobaki waaminifu kwa Mungu. Hakuna mtu ambaye angeweza kuelewa vyema jinsi ya kupinga imani ya Kweli ya Kikristo kama wale ambao walikuwa watetezi wake hapo awali; na Wakristo hawa waasi, wakiungana na wenzao wa nusu wapagani, walielekeza vita vyao dhidi ya sifa muhimu zaidi za mafundisho ya Kristo. **{SRSw 323.2}**

Ilihitaji mapambano makali kwa wale ambao wangekuwa waaminifu kusimama imara dhidi ya udanganyifu na machukizo ambayo yalijificha katika mavazi ya kikasisi na kuletwa kanisani. Biblia haikukubaliwa kama kiwango cha imani. Mafundisho ya uhuru wa kidini yaliitwa uzushi, na wafuasi wake walichukiwa na kupigwa marufuku. **{SRSw 324.1}**

Kujiondoa kwa Waaminifu

Baada ya mgogoro mrefu na mkali, waaminifu wachache waliamua kuvunja muungano wote na kanisa lililoasi ikiwa bado lilikataa kujiweka huru kutokana na uwongo na ibada ya sanamu. Waliona kwamba kujitenga kulikuwa jambo muhimu sana ikiwa wangetii Neno la Mungu. Hawakuthubutu kuvumilia makosa ambayo yangesababisha kifo kwa roho zao wenyewe na kuweka mfano ambao ungehatarisha imani ya watoto wao na watoto wa watoto wao. Ili kupata amani na umoja, walikuwa tayari kufanya makubaliano yoyote yanayoendana na uaminifu kwa Mungu; lakini walihisi kwamba hata amani ingenunuliwa kwa bei kubwa sana kwa kujitoa dhabihu au kudondosha kanuni za Mungu. Ikiwa umoja ungeweza kupatikana tu kwa makubaliano ya Ukweli na haki, basi kuwe na tofauti, na hata vita. Ingekuwa vyema kwa kanisa na ulimwengu ikiwa kanuni

zilizowasukuma roho hizo imara zingefufuliwa katika mioyo ya watu wa Mungu wanaodai. **{SRSw 324.2}**

Mtume Paulo anatangaza kwamba "***Naam, na wote wapendao kuishi maisha ya utauwa katika Kristo Yesu wataudhiwa." 2 Timotheo 3:12.*** Kwa nini basi, mateso yanaonekana kusinzia sana? Sababu pekee ni kwamba kanisa limefuata viwango vya dunia, na kwa hivyo haliamshi upinzani wowote. Dini iliyopo katika siku zetu si ya tabia safi na takatifu ambayo iliashiria imani ya Kikristo katika siku za Kristo na mitume Wake. Ni kwa sababu tu ya roho ya maelewano na dhambi, kwa sababu Ukweli mkuu wa Neno la Mungu hauzingatiwi au unapuuzwa, kwa sababu kuna uchamungu mdogo sana katika kanisa, kwamba Ukristo unaonekana kuwa unapendwa na una umaarufu sana kwa ulimwengu. Hebu kuwe na uamsho wa imani na nguvu ya kanisa la kwanza, na roho ya mateso itafufuliwa na moto wa mateso utawashwa tena. **{SRSw 324.3}**

SURA YA 45—SIRI YA KUASI

Mtume Paulo, katika barua yake ya pili kwa Wathesalonike, alitabiri uasi mkuu ambao ungesababisha kuanzishwa kwa utawala wa upapa. Alitangaza kwamba siku ya Kristo haiji ***"usipokuja kwanza ule ukengeufu; akafunuliwa yule mtu wa kuasi, mwana wa uharibifu; yule mpingamizi, ajiinuaye nafsi yake juu ya kila kiitwacho Mungu ama kuabudiwa; hata yeye mwenyewe kuketi katika hekalu la Mungu, akijionyesha nafsi yake kana kwamba yeye ndiye Mungu. Na zaidi ya hayo, mtume anawaonya ndugu zake kwamba "Maana ile siri ya kuasi hivi sasa inatenda kazi; lakini yuko azuiaye sasa, hata atakapoondolewa." 2 Wathesalonike 2:3-4, 7*** Hata katika kipindi hicho cha awali, aliona makosa yakianza kunyemelea na kuingia kanisani, ambayo yangetayarisha njia kwa maendeleo ya Upapa. **{SRSw 326.1}**

Kidogo kidogo, mwanzoni kwa siri na ukimya na kisha wazi zaidi kadri ilivyoongezeka kwa nguvu na kupata udhibiti wa akili za wanadamu, siri ya uovu iliendeleza kazi yake ya udanganyifu na ya makufuru. Taratibu, desturi za upagani ziliingia ndani ya kanisa la Kikristo bila kuonekana wazi. Roho ya maelewano na maridhiano ilizuiliwa kwa muda na mateso makali ambayo kanisa lilivumilia chini ya upagani. Lakini mateso yalipokoma, na Ukristo ulipoingia katika mahakama na majumba ya wafalme, uliweka pembeni unyenyekevu wa Kristo na mitume Wake, kwa ajili ya fahari na kiburi cha makuhani na watawala wa kipagani; na badala ya maagizo ya Mungu, mafundisho na mapokeo ya kibinadamu yalibandikwa. Uongofu wa Constantine mwanzoni mwa karne ya nne ulisababisha furaha kubwa; na ulimwengu, uliovaa mavazi ya haki, uliingia kanisani. Sasa kazi ya ufisadi iliendelea haraka. Upagani, huku ukionekana kushindwa, ukawa mshindi. Roho yake ililitawala kanisa. Mafundisho yake, sherehe zake, na ushirikina wake viliingizwa katika imani na ibada ya wale waliodai kuwa wafuasi wa Kristo. **{SRSw 326.2}**

Mapatano haya kati ya upagani na Ukristo yalisababisha ukuaji wa mtu wa kuasi aliyetabiriwa katika unabii kama mpinzani na kujiinua juu ya Mungu. Mfumo huo mkubwa wa dini ya uongo ulikuwa kazi ya ajabu hila/ugwiji ya nguvu ya Shetani—kumbukumbu ya juhudi zake za kujitwalia kiti cha enzi ili atawale dunia kwa mapenzi yake. **{SRSw 327.1}**

Ili kupata faida na heshima za kidunia, kanisa liliongozwa kutafuta kibali na usaidizi wa watu wakuu wa dunia, na baada ya kumkataa Kristo, lilishawishiwa kutoa utii kwa mwakilishi wa Shetani—Askofu wa Roma. **{SRSw 327.2}**

Ni mojawapo ya mafundisho makuu ya Urumi kwamba papa ndiye kichwa kinachoonekana cha kanisa la Kristo la ulimwengu wote,

lililopewa mamlaka kuu ya juu ya maaskofu na wachungaji katika sehemu zote za dunia. Zaidi ya hayo, papa amejinyakulia vyeo vya Uungu. **{SRSw 327.3}**

Shetani alijua vyema kwamba Maandiko Matakatifu yangewawezesha wanadamu kutambua udanganyifu wake na kupinga nguvu zake. Ilikuwa kwa Neno kwamba hata Mwokozi wa ulimwengu alipinga mashambulizi yake. Katika kila shambulio Kristo alitoa ngao ya Ukweli wa milele, akisema, **"Imeandikwa."** Kwa kila jaribu na pendekezo la adui, alijibu kwa hekima na nguvu ya Neno. Ili Shetani aendelee kuwatawala wanadamu na kuanzisha mamlaka ya mnyang'anyi-papa, lazima awaweke katika ujinga wa Maandiko. Biblia ingemtukuza Mungu na kuwaweka wanadamu wenye kikomo katika nafasi yao ya Kweli; kwa hivyo Ukweli wake mtakatifu lazima ufichwe na kukandamizwa. Mantiki hii ilipitishwa na kanisa la Kirumi. Kwa mamia ya miaka usambazaji wa Biblia ulikuwa umepigwa marufuku. Watu walikatazwa kuisoma, au kuwa nayo nyumbani mwao, na makuhani na maaskofu wasio na kanuni walitafsiri mafundisho yake ili kudumisha madai yao. Hivyo papa alikuja kutambuliwa karibu kote ulimwenguni kama msaidizi wa Mungu duniani, aliyepewa mamlaka kuu juu ya kanisa na dola/dunia. **{SRSw 327.4}**

Nyakati na Sheria Kubadilishwa

Adui wa makosa alipokuwa ameondolewa, Shetani alifanya kazi kwa uhuru. Unabii ulikuwa umetangaza kwamba Upapa uliazimu ***"kubadilisha majira na sheria" Danieli 7:25.*** Kazi hii haikuchukua muda mrefu kuanza. Ili kuwapa waongofu kutoka upagani mbadala wa ibada za sanamu na kuwafanya wakubali Ukristo kwa jina tu, kuabudiwa kwa sanamu na mabaki ya watakatifu kuliingizwa polepole katika ibada za Kikristo. Amri ya baraza kuu hatimaye ilithibitisha mfumo huu wa ibada ya sanamu ya kipapa. Ili kuwapa waongofu kutoka kwa upagani

nafasi ya ibada ya sanamu, na hivyo kukuza kukubalika kwao kwa jina kwa Ukristo, ibada ya sanamu na mabaki yaliingizwa polepole katika ibada ya Kikristo. Amri ya baraza kuu hatimaye ilianzisha mfumo huu wa ibada ya sanamu ya kipapa. Ili kukamilisha kazi hiyo ya kukufuru, Roma ilithubutu kuondoa katika Sheria ya Mungu amri ya pili inayokataza kuabudu sanamu, na kugawa amri ya kumi mara mbili, ili idadi ya amri ibaki ileile. **{SRSw 328.1}**

Roho ya kukubaliana na upagani ilifungua njia ya kupuuza zaidi mamlaka ya Mbingu. Shetani pia aliingilia kati na kuikanyaga amri ya nne, na akajaribu kuweka kando Sabato ya kale, siku ambayo Mungu alikuwa ameibariki na kuitakasa, na badala yake kuinua sikukuu iliyoadhimishwa na wapagani kama "siku ya heshima ya jua." Mabadiliko haya hayakufanywa kwa uwazi mwanzoni. Katika karne za kwanza Sabato ya Kweli ilikuwa ikitunzwa na Wakristo wote. Waaamini walikuwa na wivu kwa heshima ya Mungu, na, wakiamini kwamba sheria Yake haibadiliki, walilinda kwa bidii utakatifu wa maagizo Yake. Lakini kwa hila kubwa Shetani alifanya kazi kupitia mawakala wake ili kuleta lengo lake. Ili umakini wa watu uweze kuelekezwa kwenye siku ya Jumapili, ilifanywa kuwa sikukuu kwa heshima ya ufufuo wa Kristo. Ibada za kidini zilifanyika siku hiyo; lakini ilizingatiwa kama siku ya burudani, Sabato ikiwa bado ikitunzwa kama siku takatifu. **{SRSw 328.2}**

Constantine, akiwa bado mpagani, alitoa amri inayoamuru utunzaji wa jumla wa Jumapili kama sikukuu ya umma katika Milki ya Kirumi. Baada ya kuongoka kwake, alibaki kuwa mtetezi mkuu wa Jumapili, na amri yake ya kipagani ikatekelezwa naye kwa maslahi ya imani yake mpya. Lakini heshima iliyoonyeshwa siku hii haikuwa ya kutosha kuwazuia Wakristo kuiona Sabato ya Kweli kama siku takatifu ya Bwana. Hatua nyingine lazima ichukuliwe; sabato ya uongo lazima

iinuliwe sawa na ile ya Kweli. Miaka michache baada ya kutolewa kwa amri ya Constantine, Askofu wa Rumi aliipa Jumapili, jina la siku ya Bwana. Hivyo watu waliongozwa polepole kuiona kama yenye kiwango cha utakatifu. Bado Sabato ya awali ilitunzwa. **{SRSw 329.1}**

Mdanganyifu mkuu hakuwa amekamilisha kazi yake. Alikuwa ameazimia kukusanya ulimwengu wa Kikristo chini ya bendera yake, na kutumia nguvu zake kupitia msaidizi wake, papa mwenye kiburi aliyedai kuwa mwakilishi wa Kristo. Kupitia wapagani walioongoka nusu, maaskofu wenye tamaa, na waumini wa kanisa wanaopenda ulimwengu, alitimiza kusudi lake. Mabaraza makubwa yalifanyika, mara kwa mara, ambapo wakuu wa kanisa walikusanyika kutoka ulimwenguni kote. Katika karibu kila baraza, Sabato ambayo Mungu alikuwa ameanzisha ilikuwa chini kidogo, huku Jumapili ikiinuliwa vivyo hivyo. Hivyo sikukuu ya kipagani hatimaye ikaheshimiwa kama taasisi ya Kiungu/Bwana, huku Sabato ya Biblia ikitangazwa kuwa mabaki ya Uyahudi, na walioishika wake walitangazwa kuwa wamelaaniwa. **{SRSw 329.2}**

Mwasi mkuu alikuwa amefanikiwa kujitukuza ***"juu ya kile kiitwacho Mungu, ama kuabudiwa." 2 Wathesalonike 2:4.*** Alithubutu kubadilisha amri pekee ya sheria ya Mungu ambayo bila shaka inawaelekeza wanadamu wote kwa Mungu wa Kweli na aliye hai. Katika amri ya nne, Mungu anafunuliwa kama Muumba wa mbingu na dunia, na hivyo anatofautishwa na miungu yote ya uongo. Ilikuwa kama ukumbusho wa kazi ya uumbaji kwamba siku ya saba ilitakaswa kama siku ya kupumzika kwa mwanadamu. Ilikusudiwa kumweka Mungu aliye hai mbele ya akili za wanadamu kama Chanzo cha uwepo na wa kuheshimiwa na kuabudiwa. Shetani anajitahidi kuwageuza watu wasimtii Mungu wao na wasitii sheria Yake; kwa hivyo anaelekeza

juhudi zake haswa dhidi ya amri hiyo ambayo inamwelekeza Mungu kama Muumba. **{SRSw 330.1}**

Waprotestanti sasa wanasisitiza kwamba ufufuo wa Kristo siku ya Jumapili uliifanya Sabato ya Kikristo. Lakini ushahidi wa Maandiko unakosekana. Hakuna heshima kama hiyo iliyotolewa kwa siku hiyo na Kristo au mitume Wake. Utunzaji wa Jumapili kama taasisi ya Kikristo una asili yake katika "siri ya uasi" ambayo, hata katika siku za Paulo, ilikuwa imeanza kazi yake. Ni wapi na lini Bwana aliikubali taasisi hii ya Upapa? Ni sababu gani ya halali zinaweza kutolewa kwa mabadiliko ambayo Maandiko hayajayataja? **{SRSw 330.2}**

Katika karne ya sita Upapa ulikuwa umeimarika. Kiti chake cha mamlaka kilikuwa katika jiji la kifalme, na Askofu wa Rumi alitangazwa kuwa kichwa cha kanisa lote. Upagani ulikuwa umeupa Upapa nafasi. Joka alikuwa amempa mnyama ***"nguvu zake, kiti chake cha enzi, na uwezo mwingi." Ufunuo 13:2.*** Na sasa miaka 1260 ya ukandamizaji wa upapa iliyotabiriwa katika unabii wa Danieli na Yohana ilianza. (Danieli 7:25; Ufunuo 13:5-7.) Wakristo walilazimishwa kuchagua, ama kuacha uadilifu wao na kukubali sikukuu na ibada za upapa, au kuteseka gerezani, au kufa kwa kupigwa na rungu, kwa shoka, au kwa shoka la mkuu wa jeshi. Sasa maneno ya Yesu yalitimia, ***“Nanyi mtasalitiwa na wazazi wenu, na ndugu zenu, na jamaa zenu, na rafiki zenu, nao watawafisha baadhi yenu. Nanyi mtachukiwa na watu wote kwa ajili ya Jina Langu.” Luka 21:16, 17.*** Mateso yalifunguliwa juu ya waaminifu kwa hasira kubwa zaidi kuliko hapo awali, na ulimwengu ukawa uwanja mkubwa wa vita. Kwa mamia ya miaka kanisa la Kristo lilipata kimbilio katika upweke na giza. Hivi ndivyo nabii asemavyo: ***“Yule mwanamke akakimbilia nyikani, ambapo ana mahali palipotengenezwa na Mungu, ili wamlishe huko muda wa siku elfu na mia mbili na sitini.” Ufunuo 12:6.*** **{SRSw 330.3}**

Zama za Giza

Kuingia kwa Kanisa la Kirumi madarakani kuliashiria mwanzo wa Zama za Giza. Kadri nguvu yake ilivyoongezeka, giza likazidi kuongezeka. Imani ilihamishwa kutoka kwa Kristo, msingi wa Kweli, hadi kwa papa wa Rumi. Badala ya kumwamini Mwana wa Mungu kwa msamaha wa dhambi na wokovu wa milele, watu walimtazama papa na kwa makuhani/makasisi na maaskofu ambao aliwakabidhi mamlaka. Walifundishwa kwamba papa alikuwa mpatanishi wao, na kwamba hakuna mtu angeweza kumkaribia Mungu isipokuwa kupitia yeye, na, zaidi ya hayo, kwamba alisimama mahali pa Mungu kwao, na kwa hivyo alipaswa kutiiwa bila hata kufikiria zaidi au mashaka (automatic). Mkengeuko wowote kutoka katika maagizo yake ulitosha kuleta adhabu kali sana juu ya miili na hata roho za wakosaji. **{SRSw 331.1}**

Hivyo akili za watu ziligeuzwa kutoka kwa Mungu hadi kwa watu wanaokosea, wakosefu, na wakatili—lakini zaidi, kwa mkuu wa giza yeye mwenyewe, ambaye alitumia nguvu zake kupitia wao. Dhambi ilifichwa katika vazi la utakatifu. Maandiko yanapokandamizwa, na mwanadamu anapojiona kuwa ndiye mkuu, tunahitaji kutafuta tu ulaghai, udanganyifu, na uovu unaodhalilisha. Kwa kuinuliwa kwa sheria na mila za wanadamu, ufisadi unaotokana na kuweka kando sheria ya Mungu. **{SRSw 332.1}**

Siku za Hatari

Hizo zilikuwa siku za hatari kwa kanisa la Kristo. Washika bendera waaminifu walikuwa wachache kabisa. Ingawa ukweli haukuachwa bila mashahidi, lakini wakati mwingine ilionekana kwamba makosa na ushirikina vitashinda kabisa, na dini ya Kweli ingeondolewa duniani. Injili ilipotezwa machoni, lakini aina za dini ziliongezeka, na watu walilemewa na mizigo mikali. **{SRSw 332.2}**

Walifundishwa sio tu kumtazama papa kama mpatanishi wao na Mungu bali kuamini kazi zao wenyewe ili kulipia dhambi. Hija ndefu, vitendo vya toba, kuabudu masalio ya watakatifu, kujenga makanisa, madhabahu na makaburi, na malipo yafedha nyingi kanisani—haya na mengine mengi yaliamriwa ili kutuliza ghadhabu ya Mungu au kupata kibali Chake; kana kwamba Mungu ni kama mwanadamu, anayekasirishwa na mambo madogo au anayepatanishwa kwa zawadi na matendo yanayofwanya na watu kwaajili ya toba! **{SRSw 332.3}**

Karne zilizoendelea zilishuhudia ongezeko la makosa mara kwa mara katika mafundisho yaliyotolewa kutoka Rumi. Hata kabla ya kuanzishwa kwa Upapa, mafundisho ya wanafalsafa wapagani yalikuwa yamezingatiwa na kuwa na ushawishi katika kanisa. Wengi waliodai uongofu bado walishikilia kanuni za falsafa yao ya kipagani, na sio tu kwamba waliendelea kujifunza wenyewe bali waliihimiza haya kwa wengine kama njia ya kupanua ushawishi wao miongoni mwa wapagani. Hivyo ndivyo makosa makubwa yalivyoingizwa katika imani ya Kikristo. Jambo kuu kati ya haya lilikuwa imani katika kutokufa kwa asili kwa mwanadamu na ufahamu wake katika kifo. Fundisho hili liliweka msingi ambao Rumi ilianzisha maombi ya watakatifu na ibada ya bikira Maria. Kutoka hapa pia kulizuka uzushi wa mateso ya milele kwa wale wasiotubu, ambao uliingizwa mapema katika imani ya upapa. **{SRSw 332.4}**

Kisha njia iliandaliwa kwa ajili ya kuanzishwa kwa uvumbuzi mwingine wa upagani, ambao Roma iliuita toharani [purgatori], na kuutumia kuwatisha watu wengi wanaoamini na washirikina. Kwa uzushi huu, kunathibitishwa kuwepo kwa mahali pa mateso, ambapo roho za wale ambao hawajastahili hukumu ya milele zitapata adhabu kwa ajili ya dhambi zao, na ambazo, zikiwekwa huru kutokana na uchafu, zinruhusiwa kuingia mbinguni. **{SRSw 333.1}**

Bado uzushi mwingine ulihitajika ili kuiwezesha Roma kufaidika na hofu na maovu ya wafuasi wake. Hii ilitolewa na fundisho la msamaha. Ondoleo kamili la dhambi, zilizopita, za sasa, na zijazo, na kuachiliwa kutoka kwa maumivu na adhabu zote zilizopatikana, ziliahidiwa kwa wote ambao wangejiandikisha katika vita vya papa ili kupanua utawala wake wa muda, kuwaadhibu maadui zake, au kuwaangamiza wale waliothubutu kukataa ukuu wake wa kiroho. Watu pia walifundishwa kwamba kwa kulipa pesa kwa kanisa wangeweza kujiweka huru kutokana na dhambi na pia kuachilia roho za marafiki zao waliokufa ambao walikuwa wamefungwa kwenye moto unaotesa. Kwa njia hiyo Rumi ilijaza hazina yake na kudumisha ukuu, anasa, na maovu ya wawakilishi waliojifanya Yule Mmoja ambaye hakuwa na mahali pa kuweka kichwa Chake. **{SRSw 333.2}**

Agizo la Kimaandiko la Meza ya Bwana lilikuwa limepandwa na dhabihu ya ibada ya sanamu ya misa. Makuhani wa Kipapa walijifanya, kwa njia ya makumbusho yao yasiyo na maana, kubadilisha mkate na divai rahisi kuwa mwili na damu halisi ya Kristo. Kwa dhana ya kufuru, walidai waziwazi nguvu ya "kumuumba Muumba wao." Wakristo wote walihitajika, kwa adhabu ya kifo, kukiri imani yao katika uzushi huu mbaya, unaotukana Mbinguni. Wale waliokataa waliingizwa kwenye miale moto. **{SRSw 334.1}**

Mchana wa Upapa ulikuwa usiku wa manane wa maadili wa ulimwengu. Maandiko Matakatifu yalikuwa karibu hayajulikani, si kwa watu tu, bali pia kwa makuhani. Kama Mafarisayo wa zamani, viongozi wa Kipapa walichukia nuru ambayo ingefunua dhambi zao. Sheria ya Mungu, kiwango cha haki, baada ya kuondolewa, wanadamu walitumia nguvu bila kikomo, na wakafanya uovu bila kizuizi. Ulaghai, uchoyo, na ufisadi ulishinda. Watu hawakuepuka uhalifu wowote ambao wangeweza kupata utajiri au cheo. Majumba ya mapapa na maaskofu

yalikuwa mandhari ya ufisadi mbaya zaidi. Baadhi ya mapapa waliokuwa wakitawala walikuwa na hatia za uhalifu wa kuchukiza sana kiasi kwamba watawala wa kidunia walijaribu kuwaondoa hawa wakuu wa kanisa kama viumbe wabaya sana kuvumiliwa kwenye kiti cha enzi. Kwa karne nyingi hakukuwa na maendeleo katika elimu, sanaa, au ustaarabu. Kupooza kwa maadili na kiakili kulikuwa kumeikumba Jumuiya ya Wakristo. **{SRSw 334.2}**

SURA YA 46—WANAMATENGENEZO WA AWALI

Katikati ya giza lililotanda duniani wakati wa kipindi kirefu cha ukuu wa upapa, nuru ya Ukweli haikuweza kuzimwa kabisa. Katika kila kizazi kulikuwa na mashahidi wa Mungu—watu waliothamini imani katika Kristo kama mpatanishi pekee kati ya Mungu na mwanadamu, ambao waliichukulia Biblia kama kanuni pekee ya maisha, na ambao waliitakasa Sabato ya Kweli. Kiasi gani dunia inawiwa na watu hawa, vizazi havitajua kamwe. Walitiwa chapa kama wazushi, nia zao zilikanushwa, tabia zao zilikashifiwa, maandishi yao yalikandamizwa, yalipotoshwa, au kuharibiwa. Hata hivyo walisimama imara, na kutoka kizazi hadi kizazi walidumisha imani yao katika usafi wake, kama urithi mtakatifu kwa vizazi vijavyo. **{SRSw 335.1}**

Vita vilivyopiganwa dhidi ya Biblia vilikuwa vikali sana kiasi kwamba wakati mwingine kulikuwa na nakala chache sana; lakini Mungu hakuruhusu Neno Lake liharibiwe kabisa. Ukweli Wake haukupaswa kufichwa milele. Angeweza kufungua Maneno ya uzima kwa urahisi kama vile angeweza kufungua milango ya gereza na kufungua milango ya chuma ili kuwaweka huru watumishi Wake. Katika nchi mbalimbali za Ulaya, watu walisukumwa na Roho wa Mungu kutafuta Ukweli kama hazina iliyofichwa. Kwa mwongozo wa Mungu kwa Maandiko Matakatifu, walisoma kurasa takatifu kwa shauku kubwa. Walikuwa tayari kukubali nuru kwa gharama yoyote. Ingawa hawakuona mambo yote waziwazi, waliwezeshwa kutambua Ukweli mwingi uliofichwa kwa muda mrefu. Wakiwa wajumbe waliotumwa na Mbinguni walitoka, wakivunja minyororo ya makosa na ushirikina, na kuwaita wale waliokuwa watumwa kwa muda mrefu kuinuka na kudai uhuru wao. **{SRSw 335.2}**

Wakati ulikuwa umefika wa Maandiko kutafsiriwa na kupewa watu wa nchi tofauti katika lugha yao ya asili. Ulimwengu ulikuwa umepita kipindi cha usiku wa manane. Saa za giza zilikuwa zikiisha, na katika nchi nyingi zilionekana ishara za alfajiri inayokuja. **{SRSw 336.1}**

Nyota ya Asubuhi ya Matengenezo

Katika karne ya kumi na nne iliibuka Uingereza "nyota ya asubuhi ya Matengenezo." John Wycliffe alikuwa mhubiri/mtangazaji wa matengenezo, si kwa ajili ya Uingereza pekee, bali kwa ajili ya Ukristo wote. Alikuwa mzaliwa wa Wapuritani; enzi yake ilikuwa mahali pazuri jangwani. **{SRSw 336.2}**

Bwana aliona inafaa kukabidhi kazi ya matengenezo kwa mtu ambaye uwezo wake wa kiakili ungeipa tabia na heshima kazi yake. Hii

ilinyamazisha sauti ya dharau, na kuwazuia wapinzani wa Ukweli kujaribu kuweka aibu juu ya sababu yake kwa kudhihaki ujinga wa mtetezi. Wycliffe alipopata ujuzi wa kujifunza shule, alianza kusoma Maandiko. Katika Maandiko alipata kile alichokuwa akikitafuta bure hapo awali. Hapa aliona mpango wa wokovu ukifunuliwa, na Kristo amewekwa kama mtetezi pekee wa mwanadamu. Aliona kwamba Rumi ilikuwa imeacha njia za Biblia kwa ajili ya mila za wanadamu. Alijitoa kwa ajili ya kumtumikia Kristo, na akaazimia kutangaza Ukweli aliokuwa ameugundua. **{SRSw 336.3}**

Kazi kubwa zaidi maishani mwake ilikuwa kutafsiri Maandiko Matakatifu kwa Kiingereza. Hii ilikuwa tafsiri ya kwanza kamili ya Kiingereza kuwahi kufanywa. Sanaa ya uchapishaji ikiwa bado haijulikani, ilikuwa ni kwa kazi ya polepole na yenye kuchosha tu kwamba nakala za kazi hiyo zingeweza kuzidishwa; lakini hili lilifanyika, na watu wa Uingereza walipokea Biblia kwa lugha yao wenyewe. Hivyo nuru ya Neno la Mungu ilianza kutoa miale yake angavu dhidi ya giza. Mkono wa Bwana ulikuwa ukiandaa njia kwa ajili ya Matengenezo Makuu. **{SRSw 336.4}**

Kuvutiwa na akili za wanadamu kuliwaamsha kutoka kwenye utume wao wa chini wa mafundisho ya kipapa. Maandiko yalipokelewa kwa upendeleo na tabaka za juu, ambazo ndizo pekee katika enzi hiyo zilikuwa na ujuzi wa barua. Wycliffe sasa alifundisha mafundisho tofauti ya Uprotestanti—wokovu kupitia imani katika Kristo, na kutokuwa na makosa pekee kwa Maandiko Matakatifu. Makuhani wengi walijiunga naye katika kusambaza Biblia na katika kuhubiri injili; na athari ya kazi hizi na Maandishi ya Wycliffe yalikuwa makubwa sana kiasi kwamba imani mpya ilikubaliwa na karibu nusu ya watu wa Uingereza. Ufalme wa giza ulitetemeka. **{SRSw 337.1}**

Juhudi za maadui zake za kusimamisha kazi yake na kuharibu maisha yake hazikufanikiwa, na katika mwaka wake wa sitini na moja alikufa kwa amani katika huduma madhabahuni. **{SRSw 337.2}**

Matengenezo Yaenea

Ilikuwa kupitia maandishi ya Wycliffe kwamba John Huss wa Bohemia aliongozwa kuachana na makosa mengi ya Urumi na kuanza kazi ya matengenezo. Kama Wycliffe, Huss alikuwa Mkristo mstaarabu, mtu mwenye elimu na mwenye kujitolea bila kuyumba kwa Ukweli. Wito wake kwa Maandiko na kukemea kwake kwa ujasiri maisha ya kashfa na yasiyo ya maadili ya makasisi kuliamsha shauku kubwa, na maelfu walikubali kwa furaha imani safi zaidi. Hii ilichochea hasira ya papa na maaskofu, makuhani na watawa, na Huss aliitwa mbele ya Baraza la Constance kujibu mashtaka ya uzushi. Alipatiwa hati ya usalama wa kusafiri na mfalme wa Ujerumani, na alipofika Constance alihakikishiwa kibinafsi na papa kwamba hakutakuwa na utesi/dhuluma yoyote inayopaswa kufanywa. **{SRSw 337.3}**

Baada ya kesi ndefu, ambapo alidumisha ukweli, Huss alihitajika kuchagua kama angekana mafundisho yake au angekufa. Alichagua kufa kama shahidi, na baada ya kuona vitabu vyake vikiteketezwa kwa miale ya moto, yeye mwenyewe alichomwa moto. Mbele ya wakuu wa kanisa na serikali waliokusanyika, mtumishi wa Mungu alikuwa ametoa ushuhuda mzito na wa uaminifu dhidi ya ufisadi wa uongozi wa kipapa-hierachy. Kuuawa kwake, kwa kukiuka bila aibu ahadi nzito na ya hadharani ya ulinzi, kulionyesha kwa ulimwengu wote ukatili wa uongo wa Rumi. Maadui wa Ukweli, ingawa hawakujua, walikuwa wakiendeleza lengo ambalo walitafuta bure kuliharibu. **{SRSw 338.1}**

Licha ya hasira ya mateso, ushuhuda wa tulivu, wa uchaji Mungu, wa dhati, na wa uvumilivu dhidi ya ufisadi ulioenea wa imani ya kidini

uliendelea kutolewa baada ya kifo cha Wycliffe. Kama waumini katika siku za mitume, wengi walitoa mali zao za kidunia kwa hiari kwa ajili ya Kristo. **{SRSw 338.2}**

Juhudi kubwa zilifanywa ili kuimarisha na kupanua nguvu ya upapa, lakini huku mapapa bado wakidai kuwa wawakilishi wa Kristo, maisha yao yalikuwa yamejaa ufisadi sana kiasi cha kuwachukiza watu. Kwa msaada wa uvumbuzi wa uchapishaji* Maandiko yalisambazwa sana, na wengi waliongozwa kuona kwamba mafundisho ya upapa hayakuungwa mkono na Neno la Mungu [mashine ya kuchapa]. **{SRSw 338.3}**

Shahidi mmoja alipolazimishwa kuachilia mwenge wa Ukweli, mwingine aliunyakua kutoka mkononi mwake na kwa ujasiri usio na hofu akauinua juu. Mapambano yalikuwa yamefunguliwa ambayo yangesababisha ukombozi, si kwa watu binafsi na makanisa pekee, bali kwa mataifa. Katika pengo ya miaka mia moja watu walinyoosha mikono yao ili kushika mikono ya Walollard wa wakati wa Wycliffe. Chini ya Luther, Matengenezo yalianza Ujerumani; Calvin alihubiri injili huko Ufaransa, Zwingle huko Uswisi. Ulimwengu uliamshwa kutoka katika usingizi wa zama nyingi, kana kwamba umeamka kutoka usingizi mzito, huku kutoka nchi hadi nchi yalisikika maneno yenye nguvu na mvuto mkubwa "Uhuru wa Dini" **{SRSw 338.4}**

SURA YA 47—LUTHER NA MATENGENEZO MAKUU

Mbele ya wote walioitwa kuongoza kanisa kutoka katika giza la upapa hadi kwenye nuru ya imani safi zaidi, alisimama Martin Luther. Mwenye bidii, ari, na kujitoa kikamilifu, asiyejua hofu ila hofu ya Mungu, na asiyetambua msingi wowote wa imani ya kidini isipokuwa Maandiko Matakatifu, Luther alikuwa mtu wa wakati wake; kupitia kwake, Mungu alitimiza kazi kubwa kwa ajili ya matengenezo ya kanisa na mwangaza wa ulimwengu. **{SRSw 340.1}**

Siku moja alipokuwa akichunguza vitabu katika maktaba ya chuo kikuu, Luther aligundua Biblia ya Kilatini. Hapo awali alikuwa amesikia vipande vya Injili na Nyaraka za mitume katika ibada ya umma, na alifikiri kwamba vilikuwa Neno lote la Mungu. Sasa, kwa mara ya kwanza, aliitazama Biblia nzima. Kwa mchanganyiko wa hofu takatifu na mshangao alifungua kurasa takatifu; Kwa mapigo ya moyo yaliyoongezeka na moyo unaodunda alijisomea mwenyewe maneno ya uzima, akisimama mara kwa mara na kusema, "Laiti Mungu angenipa kitabu kama hiki kwa ajili yangu mwenyewe!" Malaika wa mbinguni walikuwa kando yake, na miale ya nuru kutoka kwenye kiti cha enzi cha Mungu ilifunua hazina za Ukweli katika ufahamu wake. Siku zote alikuwa ameogopa kumkosea Mungu, lakini sasa ufahamu wa kina kwa hali yake kama mwenye dhambi ulimshika kuliko hapo awali. Shauku ya dhati ya kuwa huru kutokana na dhambi na kupata amani na Mungu ilimpelekea hatimaye kuingia kwenye nyumba ya watawa na kujitolea maisha ya kitawa. **{SRSw 340.2}**

Kila wakati ambao angeweza kuepuka majukumu yake ya kila siku, alijishughulisha na masomo, akijinyima usingizi, na hata akichukia

wakati aliotumia kwenye milo yake yake minyenyekevu-ya kimasikini. Zaidi ya yote alifurahia kujifunza Neno la Mungu. Alikuwa amepata Biblia imefungwa kwenye ukuta wa nyumba ya watawa, na mara nyingi alikuwa akienda huko kuisoma. **{SRSw 341.1}**

Luther alitawazwa kuwa kasisi, na aliitwa kutoka nyumba za watawa Kwenda kuwa profesa katika Chuo Kikuu cha Wittenberg. Hapa alijishughulisha na kujifunza Maandiko katika lugha za asili. Alianza kutoa hotuba kuhusu Biblia; na kitabu cha Zaburi, Injili, na Nyaraka zilifunguliwa ili kueleweka na umati wa wasikilizaji waliofurahi. Alikuwa hodari katika Maandiko, na neema ilikaa juu yake. Ufasaha wake uliwavutia wasikilizaji wake, uwazi na nguvu alizotumia kuwasilisha Ukweli ziliwashawishi uelewa wao, na ari yake ya kina iligusa mioyo yao. **{SRSw 341.2}**

Katika majaliwa ya Mungu aliamua kutembelea Rumi. Msamaha ulikuwa umeahidiwa na Papa kwa wote ambao wangepanda kwa magoti kile kilichojulikana kama ngazi za Pilato. Luther siku moja alipokuwa akifanya kitendo hiki, wakati ghafla sauti kama ngurumo ilionekana kumwambia, **"Mwenye haki wataishi kwa imani!"** Aliruka kwa miguu yake kwa aibu na hofu, na akakimbia kutoka eneo la upumbavu wake. Maandishi hayo hayakupoteza nguvu zake juu ya nafsi yake. Tangu wakati huo aliona kwa uwazi zaidi kuliko hapo awali udanganyifu na upumbavu wa kuamini matendo ya wanadamu kwa ajili ya wokovu, na ulazima wa imani ya mara kwa mara katika sifa za Kristo. Macho yake yalikuwa yamefunguliwa, na hayakupaswa kufungwa tena, kwa udanganyifu wa kishetani wa upapa. **{SRSw 341.3}**

Alipogeuza uso wake kutoka Rumi alikuwa amegeuka pia moyoni, na tangu wakati huo utengano uliongezeka zaidi, hadi akakata uhusiano

wote na Kanisa la Papa. Baada ya kurudi kutoka Rumi, Luther alipokea katika Chuo Kikuu cha Wittenberg shahada ya Udaktari wa Teolojia. Sasa alikuwa na uhuru wa kujitolea, kuliko hapo awali, kwa Maandiko ambayo alipenda. Alikuwa ameweka nadhiri nzito ya kujifunza kwa makini na kuhubiri kwa uaminifu Neno la Mungu, si maneno na mafundisho ya Mapapa, siku zote za maisha yake. Hakuwa tena mtawa au profesa tu, bali mhubiri na mtangazaji aliyeidhinishwa wa Biblia. Alikuwa ameitwa kama mchungaji kulisha kundi la Mungu, ambalo lilikuwa na njaa na kiu ya Kweli. Alitangaza kwa uthabiti kwamba Wakristo hawapaswi kupokea Mafundisho ya imani mengine isipokuwa yale ambayo yanategemea mamlaka ya Maandiko Matakatifu. Maneno haya yaligusa msingi wa ukuu wa upapa. Yalikuwa na kanuni muhimu ya Matengenezo ya Kanisa. **{SRSw 342.1}**

Luther sasa aliingia kwa ujasiri juu ya kazi yake kama mtetezi wa ukweli. Sauti yake ilisikika kutoka kwenye mimbari kwa onyo la dhati. Aliweka mbele ya watu tabia ya kukera ya dhambi, na akawafundisha kwamba haiwezekani kwa mwanadamu, kwa matendo yake mwenyewe, kupunguza hatia yake au kukwepa adhabu yake. Hakuna ila toba kwa Mungu na imani katika Kristo inaweza kumwokoa mwenye dhambi. Neema ya Kristo haiwezi kununuliwa; Ni zawadi ya bure. Aliwashauri watu wasinunue hati za msamaha wa dhambi, bali wamtazame kwa imani Mkombozi aliyesulubiwa. Alisimulia uzoefu wake wa uchungu katika kutafuta bure kwa njia ya kujinyenyekeza na toba ili kupata wokovu, na akawahakikishia wasikilizaji wake kwamba alipata amani na furaha kwa kuacha kujiangalia yeye mwenyewe na kumwamini Kristo. **{SRSw 342.2}**

Mafundisho ya Luther yalivutia fikra za watu wenye kutafakari kote nchini Ujerumani. Kutoka kwenye mahubiri na maandishi yake kulitoka miale ya mwanga ambayo iliwaamsha na kuwaangazia maelfu.

Imani iliyo hai ilikuwa ikichukua nafasi ya utaratibu uliokufa ambao kanisa lilikuwa limeshikilia kwa muda mrefu. Watu walikuwa wakipoteza imani kila siku katika ushirikina wa Kirumi. Vizuizi vya ubaguzi vilikuwa vinaacha njia. Neno la Mungu, ambalo Luther alijaribu kila fundisho na kila dai, lilikuwa kama upanga wenye makali kuwili, ukikata njia yake hadi mioyoni mwa watu. Kila mahali kulikuwa na njaa na hamu ya maendeleo ya kiroho. Kila mahali kulikuwa na njaa na kiu kubwa ya haki ambayo haikuwa imejulikana kwa miaka mingi. Macho ya watu, ambayo kwa muda mrefu yalielekezwa kwa ibada za kibinadamu na wapatanishi wa kibinadamu, yalikuwa sasa yakimgeukia Kristo, kwa toba na imani, na Yeye aliyesulubiwa. **{SRSw 343.1}**

Maandishi ya Mwanamatengenezo na mafundisho yake yalikuwa yakienea hadi kila taifa katika Ukristo. Kazi ilienea hadi Uswizi na Uholanzi. Nakala za maandishi yake zilifika Ufaransa na Uhispania. Huko Uingereza mafundisho yake yalipokelewa kama neno la uzima. Huko Ubelgiji na Italia pia Ukweli ulikuwa umeenea. Maelfu walikuwa wakiamka kutoka katika usingizi wao wa mauti hadi furaha na tumaini la maisha ya imani. **{SRSw 343.2}**

Luther Aachana na Rumi

Roma ilikuwa imeazimia kumwangamiza Luther, lakini Mungu alikuwa ulinzi wake. Mafundisho yake yalisikika kila mahali—katika nyumba za watawa, katika nyumba ndogo, katika majumba ya wakuu, katika vyuo vikuu, katika majumba ya wafalme; na watu mashuhuri walikuwa wakiinuka kila upande ili kuendeleza jitihada zake. **{SRSw 343.3}**

Katika rufaa aliyoiandika kwa mfalme na wakuu wa Ujerumani kwa niaba ya Matengenezo ya Ukristo, Luther aliandika kuhusu papa: “Ni jambo baya sana kumwona mtu anayejiita kuwa mwakilishi wa

Kristo, akionyesha ukuu ambao hakuna mfalme anayeweza kulinganishwa nao. Je, hili linafana na Yesu maskini, au Petro mnyenyekevu? Wanasema kwamba yeye ndiye bwana wa ulimwengu! Lakini Kristo, ambaye anajisifu kuwa mwakilishi Wake, amesema, **'Ufalme wangu si wa ulimwengu huu.'Yohana 18:36** Je, mamlaka ya mwakilishi yanaweza kupita yale ya mkuu wake?" **{SRSw 343.4}**

Aliandika hivi kuhusu vyuo vikuu: "Ninaogopa sana kwamba vyuo vikuu vitageuka kuwa malango makubwa ya kuzimu, isipokuwa vijitahidi kwa bidii katika kuelezea Maandiko Matakatifu, na kuyachonga katika mioyo ya vijana. Simshauri mtu yeyote ampeleke mtoto wake mahali ambapo Maandiko hayatawali na kuwa ndiyo Ukuu wenyewe (supreme). Kila taasisi ambayo watu wake hawajishughushi daima na Neno la Mungu lazima iharibike." **{SRSw 344.1}**

Rufaa hii ilisambazwa kwa kasi kote Ujerumani, na kutoa ushawishi mkubwa kwa watu. Taifa zima liliamshwa kusimama chini ya bendera ya matengenezo. Wapinzani wa Luther, wakiwa na hamu ya kulipiza kisasi, walimsihi Papa kuchukua hatua madhubuti dhidi yake. Iliamriwa kwamba mafundisho yake yalaaniwe mara moja. Siku sitini zilitolewa kwa mwanamatengenezo na wafuasi wake, baada ya hapo, kama hawakukana, wote walipaswa kutengwa. **{SRSw 344.2}**

Waraka wa papa ulipomfikia Luther, alisema: "Ninaudharau na kuushambulia, kwa kuwa ni umekosa kicho na wa uongo.... ni Kristo Mwenyewe ambaye amehukumiwa humo.... Ninafurahi kuvumilia maovu kama hayo kwa sababu nzuri zaidi. Tayari ninahisi uhuru mkubwa zaidi moyoni mwangu; Oh! najua Papa ni mpinga Kristo, na kwamba kiti chake cha enzi ni kile cha Shetani mwenyewe." **{SRSw 344.3}**

Hata hivyo neno la Papa wa Rumi bado lilikuwa na nguvu. Gereza, mateso, na upanga vilikuwa silaha zenye uwezo wa kutekeleza utii. Kila kitu kilionekana kuashiria kwamba kazi ya Mwanamatengenezo ilikuwa karibu kufungwa. Wale walio dhaifu na wenye ushirikina walitetemeka mbele ya amri ya Papa, na ingawa kulikuwa na huruma ya jumla kwa Luther, wengi walihisi kwamba maisha yalikuwa ya kupendwa sana kiasi kwamba hayawezi kuhatarishwa katika sababu ya matengenezo. **{SRSw 344.4}**

SURA YA 48—KUENDELEA KWA MATENGENEZO

Mfalme mpya, Charles wa Tano, alikuwa amepanda kiti cha enzi cha Ujerumani, na wajumbe wa Rumi waliharakisha kutoa pongezi zao, na kumshawishi mfalme kutumia mamlaka yake dhidi ya Matengenezo. Kwa upande mwingine, Mteule wa Saxony, ambaye Charles alikuwa na deni kubwa kwa taji yake, alimsihi asichukue hatua dhidi ya Luther hadi atakapompa ruhusa ya kusikiliza. **{SRSw 346.1}**

Usikivu wa pande zote sasa ulielekezwa kwa mkutano wa Majimbo ya Ujerumani yaliyokutana huko Worms mara tu baada ya Charles kuingia kwenye himaya. Kulikuwa na maswali na maslahi muhimu ya kisiasa ya kuzingatiwa na baraza hili la kitaifa; lakini haya yalionekana ya madogo na ya muda mfupi yakilinganishwa na sababu ya mtawa wa Wittenberg. **{SRSw 346.2}**

Charles hapo awali alikuwa amemwelekeza mteule kumleta Luther pamoja naye kwenye Baraza, akimhakikishia kwamba Mteule anapaswa kulindwa kutokana na vurugu zote, na anapaswa kuruhusiwa hadhira ya bure na mtu mmoja mwenye uwezo wa kujadili hoja zilizobishaniwa. Luther alikuwa na hamu ya kuonekana mbele ya mfalme. **{SRSw 346.3}**

Marafiki wa Luther waliogopa na kufadhaika. Wakijua ubaguzi na uadui dhidi yake, waliogopa kwamba hata usalama wake binafsi haungeheshimiwa, na wakamsihi asihatarishe maisha yake. Alijibu: "Wafuasi wa papa hawataki nije Worms, bali hukumu yangu na kifo changu. Haijalishi. Ombeni si kwa ajili yangu, bali kwa ajili ya Neno la Mungu." **{SRSw 346.4}**

Luther Mbele ya Baraza

Mwishowe Luther alisimama mbele ya baraza la Diet of Worms. Mfalme alikaa kiti cha enzi. Alizungukwa na watu mashuhuri zaidi katika himaya. Hajawahi kutokea mtu yeyote mbele ya mkutano wa kuvutia zaidi kuliko ule ambao Martin Luther alikuwa akijibu mashtaka ya imani yake. **{SRSw 347.1}**

Ukweli wa kuonekana huko ulikuwa ushindi wa ishara kwa ukweli. Kwamba mtu ambaye papa alikuwa amemhukumu anapaswa kuhukumiwa na mahakama nyingine ilikuwa ni kukataa mamlaka ya juu ya papa. Mwanamatengenezo, aliyewekwa chini ya marufuku, na kushutumiwa dhidi ya ushirika wa kibinadamu na papa, alikuwa amehakikishiwa ulinzi, na akapewa nafasi ya kusikilizwa na watu mashuhuri wa taifa. Rumi ilikuwa imemwamuru anyamaze, lakini asaalikuwa anaenda kuzungumza mbele ya maelfu kutoka sehemu zote za Ukristo. Akiwa mtulivu na mwenye amani, lakini jasiri na mtukufu, alisimama kama shahidi wa Mungu miongoni mwa wakuu wa dunia. Luther alitoa jibu lake kwa sauti ya chini na ya unyenyekevu, bila vurugu au shauku. Tabia yake ilikuwa ya kujivuna na ya heshima; lakini alionyesha kujiamini na furaha ambayo ilishangaza mkutano. **{SRSw 347.2}**

Wale waliokataa kwa ukaidi kuupokea mwanga na waliokuwa wameamua kutosadiki Ukweli walikasirishwa sana na nguvu ya maneno ya Luther. Alipomaliza kuzungumza, msemaji wa Baraza alimwambia kwa hasira: “Hujajibu swali ulilolizwa.... Unatakiwa kutoa jibu la wazi na sahihi.... Je, utakanusha (utaondoa) mafundisho yako, au hutakana?” **{SRSw 347.3}**

Mwanamatengenezo huyo akajibu:

“Kwa kuwa Mfalme Mtukufu na Waheshimiwa Wakuu wanataka kutoka kwangu jibu lililo wazi, rahisi na sahihi, basi nitatoa jibu hili: Siwezi kuiweka imani yangu chini ya mamlaka ya papa wala ya mabaraza ya kanisa, kwa sababu ni wazi kama mchana kwamba mara nyingi yamekosea na kujipinga yenyewe. Isipokuwa nishawishwe kwa ushuhuda wa Maandiko Matakatifu au kwa hoja zilizo wazi kabisa, isipokuwa nithibitishwe kwa vifungu vya Biblia nilivyovitaja, na hivyo dhamiri yangu ifungwe na Neno la Mungu, siwezi na sitakana. Kwa maana si salama kwa Mkristo kwenda kinyume na dhamiri yake. Hapa nimesimama; siwezi kufanya vinginevyo. Mungu anisaidie. Amina.” **{SRSw 347.4}**

Hivyo ndivyo alivyosimama mtu huyu mwadilifu, juu ya msingi thabiti wa Neno la Mungu. Nuru ya Mbinguni ilimulika uso wake. Ukuu wake na usafi wa tabia, amani yake na furaha ya moyo, vilionekana kwa wote aliposhuhudia dhidi ya nguvu ya makosa na kushuhudia ukuu wa imani hiyo inayoshinda ulimwengu. **{SRSw 348.1}**

Akiwa imara kama mwamba, alisimama, huku mawimbi makali zaidi ya nguvu za kidunia yakimpiga bila madhara. Nishati sahili ya maneno yake, mwelekeo wake usio na woga, jicho lake tulivu, la kuzungumza, na mwisho usiobadilika ulioonyeshwa katika kila neno na tendo ulileta hisia kubwa juu ya mkutano. Ilikuwa dhahiri kwamba hangeweza kushawishiwa au kuuzwa, ama kwa ahadi au vitisho, kutii agizo la Roma. **{SRSw 348.2}**

Kristo alikuwa amesema kupitia ushuhuda wa Luther kwa nguvu na ukuu ambao kwa wakati huo uliwatia moyo marafiki na maadui kwa mshangao na maajabu. Roho wa Mungu alikuwapo katika baraza hilo, akivutia mioyo ya wakuu wa himaya. Wakuu kadhaa walikiri waziwazi haki ya sababu ya Luther. Wengi waliamini Ukweli, lakini kwa baadhi hisia zilizopokelewa hazikudumu. Kulikuwa na kundi lingine ambalo

wakati huo halikuonyesha imani yao, lakini ambao, baada ya kuyachunguza Maandiko kwa ajili yao wenyewe, huko mbele katika wakati ujao walitangaza kwa ujasiri mkubwa kwa Matengenezo. **{SRSw 348.3}**

Elector Frederick* alikuwa ametazamia kwa hamu kuonekana kwa Luther mbele ya Baraza, na kwa hisia kali alisikiliza hotuba yake. Alifurahi kwa ujasiri wa daktari, uthabiti, na kujitawala, na alijivunia kuwa mlinzi wake. Alitofautisha pande zilizokuwa zikishindana, na akaona kwamba hekima ya mapapa, wafalme, na maaskofu ilikuwa imebatilishwa na nguvu ya Ukweli. Upapa ulikuwa umeshindwa jambo ambalo lingehisiwa miongoni mwa mataifa yote na katika vizazi vyote. Wakati wa utawala wa Frederick the Wise (Mteule wa Saxony, 1486–1525), Watawala watakatifu wa Kirumi walikuwa Maximilian I (alitawala 1493–1519) na baadaye Charles V (alitawala 1519–1556). Frederick ndiye alisaidia kupata ushindi wa Charles V na kumlinda Martin Luther na amekuwa maarufu kwa hili katika Historia. Mteule Frederick III (Frederick the Wise) alikuwa bosi mkuu kabisa katika sehemu yake ya Saxony kuanzia 1486 hadi 1525 ambayo ndiyo baadaye ilikuwa Ujerumani Mashariki.. **{SRSw 349.1}**

Kama Mwanamatengenezo angekubali jambo moja, Shetani na majeshi yake wangepata ushindi. Lakini uthabiti wake usioyumba ulikuwa njia ya kulikomboa kanisa na kuanza zama mpya na bora zaidi. Ushawishi wa mtu huyu mmoja, aliyethubutu kufikiria na kutenda kwa ajili yake katika masuala ya kidini, ulikuwa uathiri kanisa na ulimwengu, si tu katika wakati wake, bali katika vizazi vyote vijavyo. Uthabiti wake na uaminifu wake ungewaimarisha wote, hadi mwisho wa wakati, ambao wanapaswa kupitia uzoefu kama huo. Nguvu na utukufu wa Mungu ulijitokeza waziwazi juu ya shauri la wanadamu, juu ya nguvu kuu ya Shetani. **{SRSw 349.2}**

Niliona kwamba Luther alikuwa na bidii na ari, bila woga na ujasiri, katika kukemea dhambi na kutetea Ukweli. Hakujali watu waovu au pepo; alijua kwamba alikuwa na Mmoja pamoja naye, Mwenye nguvu kuliko wote. Luther alikuwa na bidii, ujasiri, na ujasiri, na wakati mwingine alikuwa katika hatari ya kupita kiasi. Lakini Mungu alimwinua Melancthon, ambaye alikuwa kinyume kabisa katika tabia na Luther, ili kumsaidia Luther katika kuendeleza kazi ya matengenezo. Melancthon alikuwa mwoga, mwenye hofu, mwangalifu, na alikuwa na uvumilivu mkubwa. Alipendwa sana na Mungu. Ujuzi wake wa Maandiko ulikuwa mkubwa, na maamuzi na hekima yake bora. Upendo wake kwa sababu ya Mungu ulikuwa sawa na wa Luther. Mioyo ya watu hawa wa Bwana iliungana pamoja; Walikuwa marafiki wasiotenganishwa. Luther alikuwa msaada mkubwa kwa Melancthon alipokuwa katika hatari ya kuwa na hofu na kufanya mambo polepole, na Melancthon naye alikuwa msaada mkubwa kwa Luther alipokuwa katika hatari ya kusonga mbele haraka sana. **{SRSw 349.3}**

Tahadhari ya Melancthon ya kuona mbali mara nyingi iliepusha matatizo ambayo yangetokea, kama kazi ingeachwa kwa Luther peke yake; na mara nyingi kazi hiyo isingesukumwa mbele kama ingeachwa kwa Melancthon pekee. Nilionyeshwa hekima ya Mungu katika kuwachagua watu hawa wawili kuendeleza kazi ya matengenezo. **{SRSw 350.1}**

Uingereza na Scotland Kuangaziwa

Wakati Luther alipokuwa akifungua Biblia iliyofungwa kwa watu wa Ujerumani, Tyndale alisukumwa na Roho wa Mungu kufanya vivyo hivyo kwa Uingereza. Alikuwa mwanafunzi mwenye bidii wa Maandiko, na bila woga alihubiri imani yake ya Ukweli, akihimiza kwamba mafundisho yote yajaribiwe/yapimwe kwa Neno la Mungu. Bidii yake ingeweza kuchochea upinzani kutoka kwa wafuasi wa papa. Daktari

Mkatoliki msomi aliyehusika katika mabishano naye, alisema, "Ingekuwa bora kwetu kukaa bila sheria ya Mungu kuliko kukaa bila sheria ya papa." Tyndale alijibu, "Ninampinga papa na sheria zake zote; na Mungu akiniachia maisha yangu, kwa miaka mingi nitamwezesha hata mvulana anayetumia jembe la kukota (plau) kujua Maandiko zaidi kuliko wewe." **{SRSw 350.2}**

Kusudi alilokuwa ameanza kulithamini, la kuwapa watu Maandiko ya Agano Jipya kwa lugha yao wenyewe, sasa lilikuwa limethibitishwa, na mara moja akajitolea kufanya kazi hiyo. Uingereza yote ilionekana imejifunga dhidi yake, na akaazimia kutafuta makazi nchini Ujerumani. Hapa alianza kuchapisha Agano Jipya la Kiingereza. Nakala elfu tatu za Agano Jipya zilikamilika muda sio mrefu, na toleo jingine likafuata mwaka huo huo. **{SRSw 350.3}**

Hatimaye alishuhudia imani yake kwa kifo cha shahidi, lakini silaha alizoandaa zimewawezesha wanajeshi wengine kupigana vita kwa karne zote hata wakati wetu. **{SRSw 351.1}**

Huko Scotland injili ilipata ubingwa katika nafsi ya John Knox. Mwanamatengenezo huyu mwenye moyo mnyofu hakuogopa uso wa mwanadamu. Mioto ya kuuawa kishahidi, ikiwaka karibu naye, ilisaidia tu kuharakisha bidii yake kwa nguvu zaidi. Shoka la mtawala huyo likiwa limeshikiliwa kichwani mwake Knox, alisimama imara, akitoa vipigo vikali upande wa kulia na wa kushoto, ili kubomoa ibada ya sanamu. Hivyo alishikilia kusudi lake, akiomba na kupigana vita vya Bwana, hadi Scotland ilipokuwa huru {Soma ombi lake la give me Scotland or I die! Bwana nipe Scotland au nife}. **{SRSw 351.2}**

Huko Uingereza, Latimer alisisitiza kutoka mimbarini kwamba Biblia inapaswa kusomwa kwa lugha ya watu. Mwandishi wa Maandiko Matakatifu, alisema, "ni Mungu Mwenyewe;" na Maandiko haya

yanashiriki nguvu na umilele wa Mwandishi wake. "Hakuna mfalme, mwenye himaya, hakimu, na mtawala ... bali inawapasa watii ... Neno Lake takatifu." "Tusichukue njia zozote za kando, bali hebu Neno la Mungu lituongoze: tusifuate ... mababu zetu, wala tusitafute walichofanya, bali kile walichopaswa kufanya." **{SRSw 351.3}**

Barnes na Frith, marafiki waaminifu wa Tyndale, walisimama kutetea Ukweli. Akina Ridley na Cranmer walifuata. Viongozi hawa wa Matengenezo ya Uingereza walikuwa watu wa elimu, na wengi wao walikuwa wameheshimiwa sana kwa bidii au uchaji katika ushirika wa Kirumi. Upinzani wao kwa Upapa ulikuwa matokeo ya ujuzi wao wa makosa ya Holy See- [**Sancta Sedes**-Kiti Kitakatifu au serikali ya kanisa la Rumi, kama inavyojiita]. Uelewa wao wa siri za "Babeli" uliwapa nguvu zaidi katika ushuhuda wao dhidi yake**.** **{SRSw 351.4}**

Kanuni kuu iliyodumishwa na Tyndale, Frith, Latimer, na Akina Ridley ilikuwa mamlaka ya Mungu na utoshelevu wa Maandiko Matakatifu. Walikataa mamlaka yaliyodhaniwa ya mapapa, mabaraza, baba, na wafalme kutawala dhamiri katika masuala ya imani ya kidini. Biblia ilikuwa kiwango chao, na kwa hii walipima mafundisho yote na madai yote. Imani katika Mungu na Neno Lake iliwasaidia hawa watu watakatifu walipotoa maisha yao hatarini. **{SRSw 352.1}**

SURA YA 49—KUSHINDWA KUSONGA MBELE

Matengenezo hayakuishia kwa Luther, kama wengi wanavyodhani. Yataendelea hadi mwisho wa historia ya ulimwengu huu. Luther alikuwa na kazi kubwa ya kufanya katika kuwaangazia wengine nuru ambayo Mungu alikuwa ameruhusu imwangazie; lakini hakupokea nuru yote ambayo ingetolewa kwa ulimwengu. Kuanzia wakati huo hadi sasa, nuru mpya imekuwa ikiangaza Maandiko kila mara, na Ukweli mpya umekuwa ukifunuliwa kila mara. **{SRSw 353.1}**

Luther na wafanyakazi wenzake walitimiza kazi bora kwa ajili ya Mungu; lakini, wakitoka katika Kanisa la Rumi, wakiwa wameamini na kutetea mafundisho yake, haikutarajiwa kwamba wangetambua makosa haya yote. Kazi yao ilikuwa kuvunja minyororo ya Rumi na kuipatia dunia Biblia; lakini kulikuwa na Ukweli muhimu ambao walishindwa kugundua, na makosa makubwa ambayo hawakuyakataa au kuyakanusha. Wengi wao waliendelea kuadhimisha Jumapili pamoja na sherehe zingine za kipapa. Kwa kweli, hawakuiona Jumapili kama "ina mamlaka ya Kiungu/Mungu," bali waliamini kwamba inapaswa kuadhimishwa kama "siku ya ibada inayokubalika kwa ujumla." Hata hivyo, kulikuwa na baadhi yao, walioheshimu Sabato ya amri ya nne. Miongoni mwa wanamatengenezo wa kanisa, nafasi ya heshima inapaswa kutolewa kwa wale waliosimama katika kuthibitisha Ukweli ambao kwa ujumla ulipuuzwa, hata na Waprotestanti—wale waliodumisha uhalali wa amri ya nne na wajibu wa Sabato ya Biblia. Wakati Matengenezo yalifagilia mbali giza lililokuwa limetulia kwa Ulimengu wote wa Kikristo, Watunza Sabato waliletwa kwenye nuru katika nchi nyingi-{Walifunuliwa ili ulimwengu uone Fundisho hili. }**{SRSw 353.2}**

Wale waliopokea baraka kubwa za Matengenezo hawakuendelea mbele katika njia ambayo Luther aliipitia kwa ujasiri mkubwa. Watu wachache waaminifu waliinuka mara kwa mara kutangaza Ukweli mpya na kufichua makosa yaliyothaminiwa kwa muda mrefu, lakini wengi, kama Wayahudi katika siku za Kristo, au wafuasi wa papa katika wakati wa Luther, waliridhika kuamini kama baba zao walivyoamini, na kuishi kama walivyoishi. Kwa hivyo dini iliharibika tena katika hali ya kushikilia taratibu za nje tu, makosa na ushirikina ambavyo vingetupiliwa mbali kama kanisa lingeendelea kutembea katika nuru ya Neno la Mungu, uliendelea kuhifadhiwa na kuthaminiwa. Hivyo roho iliyoongozwa na Matengenezo ya Kanisa ilififia polepole na kufa, hadi kukakaribia kuwa na hitaji kubwa la matengenezo katika makanisa ya Kiprotestanti kama ilivyokuwa katika Kanisa la Kirumi wakati wa Luther. Kulikuwa na upumbavu uleule wa kiroho, kupooza, na heshima ile ile kwa maoni ya wanadamu, roho ile ile ya kuupenda ulimwengu, mbadilishano uleule wa mafundisho ya Neno la Mungu kwa nadharia za kibinadamu**.** Kiburi na ubadhirifu vilikuzwa chini ya kivuli cha dini. Makanisa yaliharibiwa kwa kujiunganisha na ulimwengu. Hivyo kanuni kuu ambazo Luther na watendakazi wenzake walizianika wazi kutoka kwenye Maandiko na kuteseka sana nazo, zilishushwa hadhi. **{SRSw 354.1}**

Shetani alipoona kwamba ameshindwa kuuangamiza Ukweli kwa mateso, aliamua tena mpango uleule wa maridhiano ambao ulikuwa umesababisha uasi mkuu na kuundwa kwa kanisa la Roma. Aliwashawishi Wakristo kujiunga, si tena na wapagani, bali na wale ambao, kwa kumwabudu mungu wa ulimwengu huu, walijithibitisha kuwa waabudu sanamu kweli. **{SRSw 354.2}**

Shetani hakuweza tena kuificha Biblia mbali na watu; Biblia sasa ilikuwa imeweza kufikiwa na wote. Lakini aliwaongoza maelfu ya watu

kukubali tafsiri za uongo na mafundisho yasiyo sahihi bila kuyachunguza Maandiko wao wenyewe ili kuujua Ukweli. Alikuwa amepotosha Mafundisho ya Biblia, na mapokeo ambayo yangewaangamiza mamilioni yalikuwa yakiaanza kuota mizizi mirefu**.** Kanisa lilikuwa likishikilia na kutetea mapokeo haya, badala ya kushindania imani ambayo mara moja ilikabidhiwa kwa watakatifu. Na huku likiwa halijui kabisa hali yao na hatari yao, kanisa na ulimwengu vilikuwa vinakaribia kwa kasi kipindi kigumu na muhimu zaidi cha historia ya dunia—kipindi cha kufunuliwa kwa Mwana wa Adamu. **{SRSw 355.1}**

SURA YA 50—UJUMBE WA MALAIKA WA KWANZA

Unabii wa ujumbe wa malaika wa kwanza, unaopatikana katika Ufunuo 14, ulitimizwa katika harakati za kuhubiri kuhusu kuja kwa Kristo kati ya miaka 1840–1844**.** Barani Ulaya na Amerika, watu wa imani na maombi waliguswa sana walipoelekezwa kwenye unabii, na, wakifuatilia Kumbukumbu Iliyovuviwa na Roho, waliona ushahidi wa kusadikisha kwamba mwisho wa mambo yote ulikuwa karibu. Roho wa Mungu aliwahimiza watumishi Wake kutoa onyo. Kila mahali, mbali na karibu, walieneza ujumbe wa injili ya milele, ***"Mcheni Mungu, na kumtukuza, kwa maana saa ya hukumu Yake imekuja." Ufunuo 14:7.*** **{SRSw 356.1}**

Popote wamishenari walipoingia, habari njema ya kurudi kwa Kristo hivi karibuni zilitangazwa. Katika nchi tofauti zilipatikana roho za Wakristo waliotengwa, ambao, kwa kujifunza Maandiko pekee, walikuwa wamefikia hitimisho kwamba ujio wa Mwokozi ulikuwa karibu. Katika baadhi ya sehemu za Ulaya, ambapo sheria zilikuwa kali sana kiasi cha kukataza kuhubiriwa kwa mafundisho ya ujio, watoto wadogo waliguswa kutangaza, na wengi walisikiliza onyo hilo zito. **{SRSw 356.2}**

William Miller na watendakazi wenzake walipewa kuhubiri ujumbe huko Amerika, na nuru iliyowashwa na kazi zao iliangaza hadi nchi za mbali. Mungu alimtuma malaika Wake kugusa moyo wa mkulima ambaye hakuamini Biblia, kumwongoza kuchunguza unabii.

Malaika wa Mungu walimtembelea mteule huyo mara kwa mara, ili kumwongoza akili yake na kufungua akili yake kwa uelewa wake unabii ambao ulikuwa giza kwa watu wa Mungu. Mwanzo wa mnyororo wa Ukweli ulifunuliwa kwake, na akaongozwa kutafuta kiungo baada ya kiungo, hadi alipotazama kwa mshangao na pongezi Neno la Mungu. Aliona hapo mnyororo mkamilifu wa Ukweli. Neno hilo, ambalo alikuwa akiliona kama lisilovuviwa, sasa lilifunguliwa mbele ya maono yake katika uzuri na utukufu Wake. Aliona kwamba sehemu moja ya Maandiko inaelezea nyingine, na kifungu kimoja kilipofungwa kwa uelewa wake, alipata katika sehemu nyingine ya Neno kile kilichoielezea. Aliliona Neno Takatifu la Mungu kwa furaha, na kwa heshima na mshangao mkubwa. **{SRSw 356.3}**

Alipokuwa akifuatilia unabii aliona kwamba wakazi wa dunia walikuwa wakiishi katika matukio ya mwisho ya kufunga historia ya ulimwengu huu; lakini hawakujua. Aliangalia makanisa, na akaona kwamba yalikuwa yamepotoka; **yalikuwa yameondoa upendo wao kwa Yesu na kuuelekeza kwa ulimwengu.** yalikuwa yakitafuta heshima ya kidunia, badala ya heshima ile inayotoka juu; walikuwa wakitafuta na kukumbatia utajiri wa kidunia, badala ya kuweka hazina yao mbinguni. Aliweza kuona unafiki, giza, na kifo kila mahali. Roho yake ilichochewa ndani yake. Mungu alimwita aondoke na kuacha shamba lake, kama alivyomwita Elisha aache ng'ombe wake na shamba lake ambayo ilikuwa kazi yake ili kumfuata Eliya. **{SRSw 357.1}**

Kwa kutetemeka, William Miller alianza kuwafunulia watu siri za ufalme wa Mungu, akiwaongoza wasikilizaji wake kupitia unabii hadi ujio wa pili wa Kristo. Ushuhuda wa Maandiko Matakatifu unaoelekeza kwenye ujio wa Kristo mwaka wa 1843, uliamsha shauku kubwa sehemu nyingi. Wengi walisadiki kwamba hoja kutoka vipindi vya unabii zilikuwa sahihi, na, na wakatoa dhabihu kiburi cha mawazo yao,

waliupokea Ukweli kwa furaha. Baadhi ya wachungaji waliweka kando mitazamo na hisia zao za kidini, wakaacha mishahara yao na makanisa yao, na wakaungana katika kutangaza ujio wa Yesu. **{SRSw 357.2}**

Hata hivyo, kulikuwa na wachungaji wachache tu ambao wangekubali ujumbe huu; kwa sababu hiyo, kazi hiyo ilikabidhiwa kwa kiasi kikubwa kwa watu wa kawaida na wale wanyenyekevu. Wakulima waliacha mashamba yao, mafundi waliacha vifaa vyao, wafanyabiashara waliacha biashara zao, wana-taaluma waliacha nafasi zao; na bado idadi ya wafanyakazi ilikuwa ndogo ikilinganishwa na kazi iliyopaswa kutimizwa. Hali ya kanisa lisilomcha Mungu na ulimwengu uliolala katika uovu ililemea roho za walinzi wa Kweli, nao walivumilia kwa hiari kazi ngumu, umaskini, na mateso, ili waweze kuwaita watu watubu kwa wokovu. Ingawa walipingwa na Shetani, kazi iliendelea mbele kwa kasi, na Ukweli wa ujio wa mara ya pili wa Yesu, ulikubaliwa na maelfu mengi. **{SRSw 358.1}**

Uamsho Mkuu wa Kidini

Kila mahali ushuhuda wenye nguvu ulisikika, ukiwaonya wenye dhambi, iwe ni watu wa ulimwengu au washiriki wa kanisa, kukimbia ghadhabu ijayo. Kama Yohana Mbatizaji, mtangulizi wa Kristo, wahubiri waliweka shoka kwenye mzizi wa mti na kuwahimiza wote kuzaa matunda yanayofaa kwa ajili ya toba. Maonyo yao yenye nguvu na kugusa moyo, yalikuwa tofauti kabisa na ujumbe wa amani na usalama uliokuwa ukisikika katika mimbari nyingi maarufu, na popote ujumbe ulipotolewa, uliwagusa watu. **{SRSw 358.2}**

Ushuhuda rahisi na wa moja kwa moja wa Maandiko, uliowekwa nyumbani kwa nguvu ya Roho Mtakatifu, ulileta uzito wa kusadikika ambao wachache waliweza kuupinga kabisa. Maprofesa wa dini **waliamshwa kutoka katika hali yao usalama wa kujidanganya**.

Waliona kurudi nyuma kwao, kupenda kwao dunia na kutoamini, kiburi na ubinafsi wao. Wengi walimtafuta Bwana kwa toba na aibu. Mapenzi ambayo yalikuwa yameshikilia kwa muda mrefu vitu vya kidunia sasa waliviweka mbinguni. Roho wa Mungu aliwakalia, na kwa mioyo iliyolainishwa na kunyenyekea waliungana kupiga kelele, "***"Mcheni Mungu, na kumtukuza, kwa maana saa ya hukumu Yake imekuja." Ufunuo 14:7.*** **{SRSw 358.3}**

Wenye dhambi waliuliza kwa kulia, "Je, nifanye nini ili niokolewe?" Wale ambao maisha yao yalikuwa yamejaa udanganyifu walitamani kurejesha kwa haki kile walichokuwa wamechukua isivyo halali. Wote waliopata amani katika Kristo walitamani kuona wengine wakishiriki baraka. Mioyo ya wazazi iligeuzwa kwa watoto wao na mioyo ya watoto kwa wazazi wao. Vizuizi vya kiburi na kujitenga vilifagiliwa mbali. Maungamo ya dhati yalifanywa, na wanafamilia walijitahidi kufanyia kazi wokovu wa wale waliokuwa karibu na wapendwa. **{SRSw 359.1}**

Mara nyingi ilisikika sauti ya maombezi ya dhati. Kila mahali kulikuwa na roho zenye uchungu mwingi, zikimsihi Mungu. Wengi walipigana mieleka usiku kucha katika maombi kwa ajili ya uhakikisho kwamba dhambi zao wenyewe zimesamehewa, au kwa ajili ya kuongoka kwa jamaa zao au majirani. Imani hiyo ya dhati, iliyoazimia, ilipata lengo lake. Kama watu wa Mungu wangeendelea kuwa na bidii katika maombi yasiyochoka, wakisisitiza maombi yao kwenye kiti cha rehema, wangekuwa na uzoefu mwingi zaidi kuliko walio nao sasa. Kuna maombi machache sana, imani ndogo sana ya usadikisho wa dhambi; na ukosefu wa imani hai huwaacha wengi wakiwa hawana neema iliyotolewa kwa wingi na Mkombozi wetu Mwenye neema. **{SRSw 359.2}**

Matabaka yote yalimiminika kwenye mikutano ya Waadventista. Matajiri na maskini, wakuu na watu wa vyeo vya chini, watu walikuja kutokana na sababu mbalimbali, wakitamani kusikia mafundisho ya ujio wa pili. Bwana alizuia roho ya upinzani huku watumishi Wake wakielezea sababu za imani yao. Wakati mwingine chombo kilikuwa dhaifu; lakini Roho wa Mungu aliipa nguvu Kweli Yake. Uwepo wa malaika watakatifu ulihisiwa katika makusanyiko haya, na wengi waliongezwa kila siku kwa waumini. Ushahidi wa kuja kwa Kristo hivi karibuni uliporudiwa, umati mkubwa wa watu walisikiliza kwa ukimya ambao ulikuwa kana kwamba hakuna mtu aliyekuwa akipumua, kwasababu ya maneno mazito. Mbingu na dunia zilionekana kukaribiana. Nguvu ya Mungu ingehisiwa kwa wazee, vijana na watu wa makamo. Watu walirejea majumbani mwao huku nyimbo za sifa zikiwa midomoni mwao, na sauti ya furaha ilisikika kwenye hewa tulivu ya usiku. Hakuna aliyehudhuria mikutano hiyo anayeweza kusahau matukio hayo ya kuvutia sana. **{SRSw 359.3}**

Upinzani

Tangazo la wakati sahihi wa kuja kwa Kristo lilisababisha upinzani mkubwa kutoka kwa watu wengi wa tabaka zote, kuanzia mhudumu aliyekuwa jukwaani hadi kwa mtu mwenye dhambi asiyejali na mwenye kutoa uthubutu kwa mbingu. "**Hakuna mtu anayejua siku wala saa**!" lilisikika kwa wote, yaani kutoka kwa mhudumu mnafiki na mdhihaki jasiri. Walifunga masikio yao kwa maelezo yaliyo wazi na yenye upatano ya maandishi kutoka kwa wale waliokuwa wakielekeza kumalizika kwa vipindi vya unabii na ishara ambazo Kristo Mwenyewe alikuwa ametabiri kama ishara za kuja Kwake. **{SRSw 360.1}**

Wengi waliodai kumpenda Mwokozi walitangaza kwamba hawakuwa na upinzani wowote kwa mahubiri ya kuja Kwake; walipinga tu wakati uliobainishwa. Jicho la Mungu linaloona yote lilisoma mioyo

yao. Watu hawakutaka kusikia kuhusu kuja kwa Kristo kuhukumu ulimwengu kwa haki. Walikuwa watumishi wasio waaminifu, kazi zao hazingestahimili ukaguzi wa Mungu anayechunguza mioyo, na waliogopa kukutana na Bwana wao. Kama Wayahudi wakati wa kuja kwa Kristo kwa mara ya kwanza, hawakuwa tayari kumkaribisha Yesu. Shetani na malaika zake walifurahi na kurusha dhihaka mbele ya Kristo na malaika watakatifu, kwamba watu wanaodai kuwa Wake, walikuwa na upendo mdogo sana Kwake kiasi kwamba hawakutamani kuonekana Kwake. **{SRSw 360.2}**

Walinzi wasio waaminifu walizuia maendeleo ya kazi ya Mungu. Watu walipoamshwa, na kuanza kuuliza njia ya wokovu, viongozi hawa waliingilia kati yao na Ukweli, wakitafuta kutuliza hofu zao kwa kutafsiri Neno la Mungu kwa uongo. Katika kazi hii Shetani na wahudumu wasiojiweka wakfu waliungana, wakilia, Amani, amani, wakati Mungu hakuwa amesema amani. Kama Mafarisayo katika siku za Kristo, wengi walikataa kuingia katika ufalme wa mbinguni wenyewe, na wale waliokuwa wakiingia walizuia. Damu ya roho hizi itahitajika mikononi mwao. **{SRSw 361.1}**

Popote ujumbe wa Ukweli ulipotangazwa, watu wanyenyekevu na waliojitolea zaidi makanisani walikuwa wa kwanza kuupokea. Wale waliojifunza Biblia wenyewe wangeweza kuona tabia isiyo ya Kimaandiko ya mitazamo maarufu ya unabii, na popote ambapo watu hawakudanganywa na juhudi za makasisi za kupindisha na kupotosha imani, popote walipotafuta Neno la Mungu wenyewe, mafundisho ya ujio yalihitaji tu kulinganishwa na Maandiko ili kuthibitisha mamlaka yake ya Kiungu. **{SRSw 361.2}**

Wengi waliteswa na ndugu zao wasioamini. Ili kudumisha nafasi zao kanisani, baadhi walikubali kunyamaza kuhusu tumaini lao, lakini wengine waliona kwamba uaminifu kwa Mungu uliwazuia hivyo

kuficha Ukweli ambao alikuwa amewakabidhi kwa amana yao. Si wachache walikatiliwa mbali na ushirika wa kanisa kwa sababu nyingine isipokuwa kuonyesha imani yao katika kuja kwa Kristo. Maneno ya nabii yalikuwa ya thamani sana kwa wale waliovumilia majaribu ya imani yao, "***Ndugu zenu wawachukiao ninyi, waliowatupa kwa ajili ya jina langu, wamesema, Na atukuzwe Bwana, tupate kuiona furaha yenu; lakini watatahayarika." Isaya 66:5.*** **{SRSw 361.3}**

Malaika wa Mungu walikuwa wakiangalia kwa hamu kubwa matokeo ya onyo hilo. Wakati makanisa yote yalipoukataa ujumbe huo, malaika waliwaacha kwa huzuni. Hata hivyo, kulikuwa na wengi katika makanisa ambao hawakuwa wamejaribiwa kuhusu Ukweli wa ujio wa Kristo. Wengi walidanganywa na waume, wake, wazazi, au watoto, na walifanywa waamini kuwa ni dhambi hata kusikiliza mafundisho potofu kama hayo ambayo Waadventista walifundisha. Malaika waliagizwa kuwa waaminifu kulinda roho hizi; kwa maana nuru nyingine bado ilikuwa haijawaangazia kutoka kiti cha enzi cha Mungu. **{SRSw 362.1}**

Kujiandaa Kukutana na Bwana

Kwa hamu isiyoelezeka wale waliokuwa wamepokea ujumbe huo walitazamia kuja kwa Mwokozi wao. Wakati waliotarajia kukutana Naye ulikuwa umekaribia. Walikaribia saa hii kwa kicho na utulivu. Walipumzika katika ushirika mtamu na Mungu, na amani ya dhati ambayo ingekuwa yao katika ulimwengu unaong'aa wa baadaye. Hakuna aliyepata tumaini na uaminifu huu anayeweza kusahau saa hizo za thamani za kusubiri. Shughuli za kidunia kwa sehemu kubwa ziliwekwa kando kwa wiki chache. Waumini walichunguza kwa makini kila wazo na hisia za mioyo yao kana kwamba wako kwenye vitanda vyao vya mauti na baada ya saa chache kufunga macho yao kwenye mandhari za kidunia. Hakukuwa na utengenezaji wa "mavazi ya kupaa nayo juu kwenda mbinguni-ascension robes," lakini wote waliona hitaji

la ushahidi wa ndani kwamba walikuwa tayari kukutana na Mwokozi; mavazi yao meupe yalikuwa usafi wa roho, tabia zilizosafishwa kutoka kwa dhambi kwa damu ya upatanisho ya Kristo. **{SRSw 362.2}**

Mungu alikusudia kuwathibitisha watu Wake. Mkono Wake ulifunika kosa katika kuhesabu vipindi vya unabii. Waadventista hawakufunua kosa hilo, wala halikugunduliwa na wapinzani wao walioelimika zaidi. Wale wapinzani walisema, "Hesabu yyenu ya vipindi vya unabii ni sahihi. Tukio kubwa linakaribia kutokea, lakini si kile ambacho Bw. Miller anatabiri; ni uongofu wa ulimwengu, na si ujio wa pili wa Kristo." **{SRSw 362.3}**

Wakati wa matarajio ulipita, na Kristo hakutokea kwa ajili ya ukombozi wa watu Wake. Wale ambao kwa imani na upendo wa dhati walikuwa wamemtafuta Mwokozi wao walipitia huzuni kubwa ya kukatishwa tamaa. Lakini Bwana alikuwa ametimiza kusudi Lake: Alikuwa amejaribu mioyo ya wale waliokuwa wamedai kusubiri ujio Wake. Kulikuwa na wengi miongoni mwao ambao walikuwa wamechochewa na nia isiyo ya juu zaidi ya hofu. Kukiri kwao imani hakukuathiri mioyo yao au maisha yao. Tukio lililotarajiwa liliposhindwa kutokea, watu hawa walitangaza kwamba hawakukata tamaa; kwamba hata hivyo walikuwa hawajaamini kuwa Kristo angekuja. Hawa ndio walikuwa miongoni mwa wa kwanza kudhihaki huzuni ya waumini wa kweli. **{SRSw 363.1}**

Lakini Yesu na jeshi lote la mbinguni waliwatazama kwa upendo na huruma wale waliojaribiwa na waaminifu, lakini waliokatishwa tamaa. Kama pazia linalotenganisha ulimwengu unaoonekana na usioonekana lingeondolewa, malaika wangeonekana wakikaribia roho hizo za wale wasioyumbayumba, wenye kutegemeka na waaminifu, wakizilinda dhidi ya mishale ya Shetani. **{SRSw 363.2}**

SURA YA 51—UJUMBE WA MALAIKA WA PILI

Makanisa yaliyokataa kupokea ujumbe wa malaika wa kwanza yalikataa nuru kutoka mbinguni. Ujumbe huo ulitumwa kwa rehema ili kuwaamsha ili waone hali yao halisi ya udunia na kurudi nyuma, na kutafuta maandalizi ya kukutana na Bwana wao. **{SRSw 364.1}**

Ilikuwa ni kutenganisha kanisa la Kristo na ushawishi unaoharibu maadili na uovu wa ulimwengu ndipo ujumbe wa malaika wa kwanza ulitolewa. Lakini pamoja na umati, hata wa wanaodai kuwa Wakristo, vifungo vilivyowafunga duniani vilikuwa na nguvu kuliko vivutio vya mbinguni. Walichagua kusikiliza sauti ya hekima ya kidunia, na wakageuka kutoka kwa ujumbe wa Kweli unaochunguza mioyo. **{SRSw 364.2}**

Mungu hutoa nuru ili itunzwe, ithaminiwe na kutii, isidharauliwe na kukataliwa. Nuru anayotuma inakuwa giza kwa wale wanaoipuuza.

Roho wa Mungu anapoacha kuigusa Kweli kwenye mioyo ya wanadamu, kusikia kote ni bure, na mahubiri yote pia ni bure. **{SRSw 364.3}**

Makanisa yalipokataa ushauri wa Mungu kwa kukataa ujumbe wa marejeo, Bwana aliwakataa. Malaika wa kwanza alifuatwa na wa pili, akitangaza, ***"Umeanguka, umeanguka Babeli, mji ule ulio mkubwa, maana ndio uliowanywesha mataifa yote mvinyo ya ghadhabu ya uasherati wake." Ufunuo 14:8.*** Ujumbe huu ulieleweka na Waadventista kuwa tangazo la anguko la kimaadili la makanisa kutokana na kukataa kwao ujumbe wa kwanza. Tangazo, "**Babeli umeanguka**," lilitolewa katika kiangazi cha 1844, na matokeo yake, watu wapatao elfu hamsini walijiondoa kutoka kwa makanisa haya. **{SRSw 364.4}**

Wale waliohubiri ujumbe wa kwanza hawakuwa na kusudi au matarajio ya kusababisha mgawanyiko katika makanisa, au kuunda taasisi tofauti. **"**Katika kazi zangu zote, sikuwahi kuwa na wazo wala shauku ya kuanzisha kundi tofauti na madhehebu yaliyokuwapo, wala kulinufaisha dhehebu moja kwa hasara ya jingine." Nilidhani kuwanufaisha wote. Tukidhani kwamba Wakristo wote wangefurahi katika matarajio ya kuja kwa Kristo, na kwamba wale ambao hawangeweza kuona kama nilivyofanya, hawangewapenda hata wale wanaopaswa kukubali mafundisho haya, sikufikiria kwamba kungekuwa na umuhimu wowote wa mikutano tofauti. Lengo langu lote/haswa, lilikuwa ni hamu ya kuongoa roho kwa Mungu, kuijulisha dunia kuhusu hukumu ijayo, na kuwashawishi wanadamu wenzangu kufanya maandalizi ya moyo ambayo yatawawezesha kukutana na Mungu wao kwa amani. Wengi wa wale waliongoka chini ya kazi zangu waliungana na makanisa mbalimbali yaliyopo. Watu walipokuja kwangu kuuliza kuhusu wajibu wao, siku zote niliwaambia waende mahali ambapo

wangejisikia nyumbani; na sikulipendelea kamwe dhehebu lolote katika ushauri wangu kwa hayo." **{SRSw 365.1}**

Kwa muda fulani makanisa mengi yalipokea huduma yake. Lakini yalipoamua kuukataa Ukweli wa ujio wa Kristo, yalianza kuzuia mjadala wowote kuhusu somo hilo. Wale waliokuwa wamekubali fundisho hilo waliwekwa katika hali ya majaribu na mkanganyiko mkubwa. Walipenda makanisa yao, na hawakutaka kujitenga nayo; lakini walipodhihakiwa na kukandamizwa, wakanyimwa fursa ya kuzungumzia matumaini yao, au kuhudhuria mahubiri kuhusu ujio wa Bwana, wengi mwishowe waliinuka na kutupa nira iliyokuwa imewekwa juu yao. **{SRSw 365.2}**

Waadventista, walipoona kwamba makanisa yalikataa ushuhuda wa Neno la Mungu, hawakuweza tena kuyaona makundi hayo kama yale yanayounda kanisa la Kristo, "nguzo na msingi wa Ukweli;" na ujumbe, "Babeli umeanguka," ulipoanza kutangazwa, walijiona wana haki ya kujitenga na uhusiano wao wa awali. **{SRSw 366.1}**

Tangu kukataliwa kwa ujumbe wa kwanza, mabadiliko ya kusikitisha yametokea makanisani. Ukweli unapokataliwa, makosa yanapokelewa na kuthaminiwa. Upendo kwa Mungu na imani katika Neno Lake vimepoa. Makanisa yamemhuzunisha Roho wa Bwana, na kwa kiasi kikubwa Yeye ameondolewa. **{SRSw 366.2}**

Wakati wa Kukawia

Mwaka 1843 ulipopita kabisa bila kutambuliwa na ujio wa Yesu, wale waliokuwa wametazamia kwa imani kuonekana Kwake, walibaki kwa muda katika mashaka na hali ya kuchanganyikiwa. Lakini licha ya kukata tamaa kwao, wengi waliendelea kuchunguza Maandiko, wakichunguza upya ushahidi wa imani yao, na kusoma kwa makini unabii ili kupata mwanga zaidi. Ushuhuda wa Biblia unaounga mkono

msimamo wao ulionekana wazi na kuleta hitimisho. Ishara ambazo hazingeweza kuwa na makosa ziliashiria kuja kwa Kristo kuwa karibu. Waumini hawakuweza kuelezea kukata tamaa kwao; lakini walihisi uhakika kwamba Mungu alikuwa amewaongoza katika uzoefu wao wa zamani. **{SRSw 366.3}**

Imani yao iliimarishwa sana na matumizi ya moja kwa moja na ya utendaji wenye nguvu wa Maandiko hayo ambayo yanaeleza wakati wa kukawia. Mapema kama mwaka wa 1842, Roho wa Mungu alikuwa amemsukuma Charles Fitch kubuni chati ya unabii, ambayo kwa ujumla ilionekana kwa Waadventista kama utimilifu wa amri iliyotolewa na nabii Habakuki, **"Iandike njozi na ukaifanye iwe wazi sana katika vibao**." Hata hivyo, hakuna hata mtu mmoja, hata hivyo aliyeona wakati wa kukawia ambao ulionyeshwa katika unabii uleule. Baada ya kukatishwa tamaa, maana kamili ya andiko hili ikawa dhahiri. Hivi ndivyo asemavyo nabii: "***Iandike njozi ukaifanye iwe wazi sana katika vibao, ili aisomaye apate kuisoma kama maji. Maana njozi hii bado ni kwa wakati ulioamriwa, inafanya haraka ili kuufikilia mwisho wake, wala haitasema uongo; ijapokawia, ingojee; kwa kuwa haina budi kuja, haitakawia. Habakuki 2:2-3*** **{SRSw 366.4}**

Wale waliokuwa wakingoja walifurahi kwamba Yeye ajuaye mwisho tangu mwanzo alikuwa ametazama chini kupitia vizazi, na, akiona mapema kukata tamaa kwao, alikuwa amewapa maneno ya ujasiri na matumaini. Kama isingekuwa sehemu kama hizo za Maandiko, zinazoonyesha kwamba walikuwa katika njia sahihi, imani yao ingekuwa imeshindwa katika saa hiyo ya majaribu. **{SRSw 367.1}**

Katika mfano wa wanawali kumi, Mathayo 25, uzoefu wa Waadventista unaonyeshwa na matukio ya ndoa ya Mashariki. “**Ndipo ufalme wa mbinguni utakapofanana na wanawali kumi, waliotwaa taa zao, wakatoka kwenda kumlaki bwana arusi.” Mathayo 25:1**

“***Hata bwana arusi alipokawia, wote wakasinzia wakalala usingizi.” Mathayo 25:5*** **{SRSw 367.2}**

Harakati kubwa iliyotokana na kutangazwa kwa ujumbe wa kwanza ilifananishwa na kutoka kwa wanawali kwenda kumlaki bwana arusi. Kupita kwa wakati uliotarajiwa, kukatishwa tamaa, na kuchelewa kwa tukio hilo, kulifananishwa na kukawia kwa bwana arusi. Baada ya muda uliowekwa kupita, waumini wa Kweli waliendelea kuamini kwamba mwisho wa mambo yote ulikuwa karibu. Lakini baada ya muda ilionekana kwamba walikuwa wakipoteza kwa kiwango fulani bidii yao ari, na kujitoa kwao kwa Mungu, na walikuwa wanaingia katika hali ile iliyoelezwa katika mfano wa wanawali waliosinzia wakati wa kuchelewa kwa bwana arusi. **{SRSw 367.3}**

Karibu na wakati huo, ushabiki wa kidini ulianza kujitokeza. Baadhi ya watu waliodai kuwa waumini wenye bidii wa ujumbe huo walilikataa Neno la Mungu kama mwongozo pekee usiokosea. Wakidai kwamba walikuwa wanaongozwa na Roho, walijikabidhi chini ya utawala wa hisia zao wenyewe, mawazo yao, na fikra zao binafsi. Kulikuwa na baadhi walioonyesha bidii isiyo na kifani na ya ubaguzi, wakiwashutumu wote ambao hawakukubali mwendo wao. Mawazo na mazoezi yao ya ushabiki yaliyopitiliza, hayakupata huruma yoyote kutoka kwa kundi kubwa la Waadventista; lakini yalitumika kuleta lawama kwa sababu ya Ukweli. **{SRSw 368.1}**

Mahubiri ya ujumbe wa kwanza mwaka wa 1843, na kilio cha usiku wa manane mwaka wa 1844, yalilenga moja kwa moja kukandamiza ushabiki na mgawanyiko. Wale walioshiriki katika harakati hizi nzito, walikuwa katika maelewano; mioyo yao ilijaa upendo kwa kila mmoja, na kwa ajili ya Yesu, ambaye walitarajia kumuona hivi karibuni. Imani moja, tumaini moja lililobarikiwa,

viliwainua juu ya udhibiti wa ushawishi wowote wa kianadamu na ikawa ngao dhidi ya mashambulizi ya Shetani. **{SRSw 368.2}**

SURA YA 52—KILIO CHA USIKU WA MANANE

"***Hata bwana arusi alipokawia, wote wakasinzia wakalala usingizi. Lakini usiku wa manane, pakawa na kelele, Haya, bwana arusi; tokeni mwende kumlaki. Mara wakaondoka wanawali wale wote, wakazitengeneza taa zao." Mathayo 25:5-7***. **{SRSw 369.1}**

Katika majira ya joto ya mwaka 1844, Waadventista waligundua kosa lililokuwa katika hesabu yao ya awali ya vipindi vya unabii, na wakafikia ufahamu sahihi. Siku 2300 za Danieli 8:14, ambazo wote waliamini zilihusu kuja kwa pili kwa Kristo, zilidhaniwa kuisha katika majira ya kuchipua ya mwaka 1844. Lakini sasa ilionekana kwamba kipindi hicho kilifikia mwisho wake katika majira ya kupukutisha majani, mwaka huo huo. Kwa hiyo mawazo ya Waadventista yalielekezwa kwenye wakati huo kama muda wa kuonekana kwa Bwana. Kutangazwa kwa ujumbe huu wa wakati maalumu kulikuwa hatua nyingine katika utimilifu wa mfano wa arusi, ambao matumizi yake kwa

uzoefu wa Waadventista yalikuwa tayari yameonekana wazi. **{SRSw 369.2}**

Kama katika mfano huo, kilio kilitolewa usiku wa manane kikitangaza kuwasili kwa bwana arusi, ndivyo ilivyokuwa katika utimilifu wake. Katikati ya kipindi kati ya majira ya kuchipua ya mwaka 1844—wakati ilidhaniwa kwanza kwamba siku 2300 zingekwisha—na majira ya vuli ya mwaka huo, wakati ilipogunduliwa baadaye kwamba ndicho kipindi halisi cha mwisho wake, kilio hiki kilitangazwa kwa maneno yale yale ya Maandiko: ***"Haya, bwana arusi; tokeni mwende kumlaki." Mathayo 25:6*** **{SRSw 369.3}**

Harakati hiyo ilienea nchini kote kama wimbi kubwa la bahari. Ilisafiri kutoka mji hadi mji, kutoka kijiji hadi kijiji, na kufika hata maeneo ya mbali kabisa ya mashambani, mpaka watu wa Mungu waliokuwa wakingoja wakaamshwa kikamilifu. Kabla ya tangazo hili, ushabiki wa kidini ulitoweka kama barafu ya asubuhi kwenye majani, inavyoyeyuka mbele ya jua linalochomoza. Waumini walipata tena msimamo wao, na tumaini pamoja na ujasiri vikajaza mioyo yao. **{SRSw 370.1}**

Kazi hii haikuwa na misimamo mikali ambayo mara nyingi huonekana pale ambapo kuna msisimko wa kibinadamu usiodhibitiwa na Neno la Mungu na Roho Wake. Hali hii ilifanana na vipindi vya unyenyekevu na kurudi kwa Bwana ambavyo vilitokea katika Israeli ya kale baada ya ujumbe wa karipio kutoka kwa watumishi wa Mungu. Ilikuwa na sifa zile zile zinazotambulisha kazi ya Mungu katika kila kizazi. Hakukuwa na furaha ya kihisia isiyo na msingi, bali kulikuwa na uchunguzi wa kina wa moyo, maungamo ya dhambi, na kuacha mambo ya ulimwengu. Maandalizi ya kukutana na Bwana ndiyo yaliyokuwa mzigo mkubwa wa nafsi zilizokuwa na shauku kubwa. Kulikuwa na maombi ya kudumu na kujitoa kwa Mungu bila masharti. **{SRSw 370.2}**

Kilio cha usiku wa manane hakikuenezwa sana kwa hoja za kibinadamu, ingawa ushahidi wa Maandiko ulikuwa wazi na wenye nguvu. Kiliambatana na nguvu ya kiroho iliyogusa nafsi za watu. Hakukuwa na mashaka wala kusitasita. Katika tukio la kuingia kwa ushindi kwa Kristo Yerusalemu, watu waliokuwa wamekusanyika kutoka sehemu zote za nchi kusherehekea sikukuu, walikusanyika hadi Mlima wa Mizeituni, na walipojiunga na umati uliokuwa ukimsindikiza Yesu, walipata msukumo wa saa hiyo na kusaidia kuongeza sauti, ***"Ndiye mbarikwa, Yeye ajaye kwa Jina la Bwana." Mathayo 21:9***. Vivyo hivyo, wasioamini waliokusanyika kwenye mikutano ya Waadventista—baadhi kwa udadisi, wengine kwa dhihaka tu—walihisi nguvu ya kushawishi iliyoambatana na ujumbe, **"Tazama, Bwana Arusi Anakuja!"** **{SRSw 370.3}**

Wakati huo kulikuwa na imani iliyoleta majibu ya maombi—imani iliyotazamia thawabu iliyoahidiwa. Kama manyunyu ya mvua juu ya nchi yenye kiu, Roho wa neema alishuka juu ya wale wanaotafuta kwa bidii. Wale waliotarajia kusimama ana kwa ana na Mkombozi wao walihisi furaha kubwa ambayo haikuweza kutamkwa. Nguvu ya Roho Mtakatifu ya kulainisha, ya kutiisha, iliyeyusha mioyo, huku wimbi baada ya wimbi la utukufu wa Mungu likiwafunika waaminifu, waaminio. **{SRSw 371.1}**

Kwa uangalifu na kwa kicho, wale waliopokea ujumbe walifika hadi wakati walipotarajia kukutana na Bwana wao. Kila asubuhi walihisi kwamba ilikuwa jukumu lao la kwanza kupata uthibitisho wa kukubalika kwao na Mungu. Mioyo yao ilikuwa imeungana kwa karibu, na waliomba sana pamoja na kwa ajili ya kila mmoja. Mara nyingi walikutana pamoja katika sehemu zilizotengwa ili kuwasiliana na Mungu, na sauti ya maombezi ilipanda mbinguni kutoka mashambani na vichakani. Uhakika wa idhini ya Mwokozi ulikuwa muhimu zaidi kwao

kuliko chakula chao cha kila siku, na ikiwa wingu lingetia giza akili zao, hawakupumzika hadi lilipoondolewa. Walipohisi ushuhuda wa neema ya msamaha, walitamani kumwona Yeye ambaye roho zao zilimpenda. **{SRSw 371.2}**

Wakiwa Wamekata Tamaa, ila Hawakuachwa

Lakini tena walikabiliwa na kukatishwa tamaa. Wakati uliotarajiwa ulipita, na Mwokozi wao hakuonekana. Kwa ujasiri usioyumba walikuwa wametarajia kuja Kwake, na sasa walihisi kama Mariamu, alipofika kwenye kaburi la Mwokozi na kulikuta tupu, akalia akisema: ***"Kwa sababu wamemwondoa Bwana wangu, wala mimi sijui walikomweka." Yohana 20:13.*** **{SRSw 371.3}**

Hisia ya hofu, hofu kwamba ujumbe huo unaweza kuwa wa Kweli, ilikuwa kizuizi kwa muda kwa ulimwengu usioamini. Baada ya kupita kwa wakati huu haukutoweka mara moja; Hawakuthubutu kushinda wale waliokatishwa tamaa, lakini kwa kuwa hakuna dalili za ghadhabu ya Mungu zilizoonekana, walirudi kutoka kwenye hofu zao na kuanza tena lawama na dhihaka zao. Kundi kubwa lililokuwa limedai kuamini katika kuja kwa Bwana hivi karibuni lilikana imani yao. Baadhi ya waliokuwa na ujasiri sana walikuwa wamejeruhiwa sana katika kiburi chao kiasi kwamba walihisi kama kukimbia kutoka duniani. Kama Yona, walimlalamikia Mungu, na kuchagua kifo badala ya uzima. Wale ambao walikuwa wameweka imani yao juu ya maoni ya wengine, na si juu ya Neno la Mungu, walikuwa tayari sasa kubadilishana maoni yao tena. Wadhihaki walivutia walio dhaifu na waoga kujiunga nao, na wote wakaungana kusema kwamba hakuna tena hofu wala matarajio yoyote. Wakati ulikuwa umepita, Bwana hakuwa amekuja, na dunia ingeweza kubaki vile vile kwa maelfu ya miaka. **{SRSw 371.4}**

Waumini wenye bidii na waaminifu walikuwa wameacha yote kwa ajili ya Kristo, na walikuwa wameshiriki uwepo Wake zaidi kuliko hapo awali. Kwa imani yao, walikuwa wametoa onyo lao la mwisho kwa ulimwengu, na kutajaria hivi karibuni, kupokelewa na Bwana wao pamoja na malaika wa mbinguni, kwa kiasi kikubwa walikuwa wamejitenga na umati usioamini. Kwa hamu kubwa walikuwa wameomba, "Njoo, Bwana Yesu,na uje haraka." Lakini hakuwa amekuja. Na sasa kuchukua tena mzigo mzito wa wasiwasi na matatizo ya maisha, na kuvumilia dhihaka na kejeli za ulimwengu unaodhihaki, kwa kweli ilikuwa jaribu baya la imani na uvumilivu. **{SRSw 372.1}**

Lakini huku kukatishwa tamaa hakukuwa sana kama kule kuliowapata wanafunzi wakati wa ujio wa kwanza wa Kristo. Yesu alipopanda punda kwa ushindi kuingia Yerusalemu, wafuasi Wake waliamini kwamba Yeye alikuwa karibu kupanda na kukikalia kiti cha enzi cha Daudi na kuwakomboa Israeli kutoka kwa watesi wake [Kilio cha Usiku wa manane]. Kwa matumaini makubwa na matarajio ya furaha walishindana katika kuonyesha heshima kwa Mfalme wao. Wengi walitandaza mavazi yao kama zulia katika njia Yake, au walitandaza matawi ya mitende mbele Yake. Katika furaha yao ya shauku waliungana katika kelele za furaha, "Hosana kwa Mwana wa Daudi!" **{SRSw 372.2}**

Wakati Mafarisayo, wakiwa wamefadhaishwa na kughadhibishwa na mlipuko huu wa furaha, walipomtaka Yesu awakemee wanafunzi Wake, alijibu, ***"Wakinyamaza hawa, mawe yatapiga kelele." Luka 19:40.*** Unabii lazima utimizwe. Wanafunzi walikuwa wakitimiza kusudi la Mungu; lakini walikuwa wamekabiliwa na kukatishwa tamaa. Lakini siku chache zilikuwa zimepita toka hapo waliposhuhudia kifo cha uchungu cha Mwokozi na kumlaza kaburini. Matarajio yao hayakutimizwa kwa katika jambo hili moja, na hivyo matumaini yao

yalikufa pamoja na Yesu. Hawakuweza kuelewa kwamba yote yalikuwa yametabiriwa mpaka Bwana wao alipotoka nje ya kaburi kwa ushindi, ndiyo waliweza kuelewa unabii uliotabiriwa na kwamba "***ilimpasa Kristo kuteswa na kufufuka katika kwa wafu." Matendo 17:3.*** Vivyo hivyo unabii ulitimizwa katika ujumbe wa malaika wa kwanza na wa pili. Ujumbe huu ulitolewa kwa wakati unaofaa na kukamilisha kazi ambayo Mungu alikusudia kuitimiza kupitia kwao. **{SRSw 373.1}**

Ulimwengu ulikuwa ukitazama, ukitarajia kwamba ikiwa wakati ungepita na Kristo hangeonekana, mfumo mzima wa Uadventista ungeachwa. Lakini ingawa wengi, chini ya majaribu makali, waliacha au kuisalimisha imani yao, kulikuwa na baadhi waliosimama imara. Hawakuweza kugundua kosa lolote katika hesabu yao ya vipindi vya unabii. Wapinzani wao hodari hawakufanikiwa kupindua nafasi yao. Ni kweli, kulikuwa na kushindwa kuhusu tukio lililotarajiwa, lakini hata hili halikuweza kutikisa imani yao katika Neno la Mungu. **{SRSw 373.2}**

Mungu hakuwaacha watu Wake; Roho Wake bado alikaa na wale ambao hawakukataa nuru waliyopokea kwa kurupuka, bila ya tafakari , na kukemea harakati za ujio wa Yesu kwa mara ya pili. Mtume Paulo, akiangalia chini katika vizazi vyote, alikuwa ameandika maneno ya kutia moyo na onyo kwa wale waliojaribiwa, wakingoja katika mgogoro huu: "***Basi msiutupe ujasiri wenu, kwa maana una thawabu kuu. Maana mnahitaji saburi, ili kwamba mkiisha kuyafanya mapenzi ya Mungu mpate ile ahadi. Kwa kuwa bado kitambo kidogo sana, Yeye Ajaye atakuja, wala hatakawia. Lakini mwenye haki wangu ataishi kwa imani; Naye akisita-sita, roho Yangu haina furaha naye. Lakini sisi hatumo miongoni mwao wasitao na kupotea, bali tumo miongoni mwa hao walio na imani ya kutuokoa roho zetu." Waebrania 10:35-39.*** **{SRSw 374.1}**

Njia yao pekee salama ilikuwa ni kuthamini nuru ambayo walikuwa wameipokea kutoka kwa Mungu, kushikilia ahadi Zake kwa bidii, na kuendelea kuchunguza Maandiko, na kusubiri kwa uvumilivu na kutazama ili kupokea nuru zaidi. **{SRSw 374.2}**

SURA YA 53—PATAKATIFU

Andiko ambalo, zaidi ya mengine yote, lililokuwa msingi na nguzo kuu ya imani ya ujio wa Kristo lilikuwa tangazo lisemalo: ***"Hata nyakati za jioni na asubuhi elfu mbili na mia tatu; ndipo Patakatifu patakapotakaswa." Danieli 8:14.*** Haya yalikuwa maneno yanayojulikana kwa waumini wote katika kuja kwa Bwana hivi karibuni. Kwa midomo ya maelfu unabii huu ulirudiwa kwa furaha kama kama Neno la kauli-mbiu ya imani yao. Wote walihisi kwamba juu ya matukio yaliyofunuliwa katika unabii huu ndiko kulitegemea matumaini yao makuu na matarajio yao ya thamani zaidi. Siku hizi za kinabii zilieleweka kuishia katika majira ya kupukutisha majani ya mwaka 1844. Kama ilivyokuwa katika ulimwengu wote wa Kikristo, Waadventista kwa wakati huo waliamini kwamba dunia, au sehemu fulani yake, ndiyo Patakatifu, na kwamba kusafishwa kwa Patakatifu kulimaanisha kutakaswa kwa dunia kwa mioto ya siku ya mwisho kuu. Walielewa

kwamba jambo hilo lingetokea wakati wa kuja mara ya pili kwa Kristo. Kwa hiyo wakahitimisha kwamba Kristo angerudi duniani mwaka 1844. **{SRSw 375.1}**

Lakini wakati uliowekwa ulifika, na Bwana hakuonekana. Waumini walijua kwamba Neno la Mungu haliwezi kushindwa; tafsiri yao ya unabii lazima iwe na kosa; lakini kosa lilikuwa wapi? Wengi kwa haraka walikata fundo la ugumu kwa kukataa kwamba siku 2300 ziliishia mwaka wa 1844. Hakuna sababu iliyoweza kutolewa kwa msimamo huu, isipokuwa kwamba Kristo hakuja wakati waliotarajia. Walibishana kwamba ikiwa siku za kinabii zingeisha mwaka wa 1844, Kristo angekuja kutakasa Patakatifu kwa kutakasa dunia kwa moto; na kwamba kwa kuwa hakuja, siku hizo hazingeweza kuwa kuisha. **{SRSw 375.2}**

Ingawa Waadventista wengi waliacha kukorokotoa kwao kwa zamani vipindi vya kinabii, na kwa hivyo wakakataa usahihi wa harakati iliyotegemea, wachache hawakuwa tayari kukataa hoja za imani na uzoefu ambazo ziliungwa mkono na Maandiko na kwa ushuhuda maalum wa Roho wa Mungu. Waliamini kwamba walikuwa wamechukua kanuni nzuri za tafsiri katika kujifunza kwao Maandiko, na kwamba ilikuwa ni wajibu wao kushikilia Kweli ambazo tayari zilikuwa zimepatikana, na bado kufuata njia ile ile ya Utafiti wa Biblia. Kwa maombi ya dhati na bidiim walipitia msimamo wao, na kusoma Maandiko ili kugundua kosa lao. Kwa kuwa hawakuweza kuona kosa lolote katika maelezo yao ya vipindi vya unabii, waliongozwa kuchunguza kwa undani zaidi mada ya Patakatifu. **{SRSw 376.1}**

Patakatifu pa Duniani na Mbinguni

Katika uchunguzi wao walijifunza kwamba Patakatifu pa dunia, palipojengwa na Musa kwa amri ya Mungu kulingana na mfano

ulioonyeshwa mlimani, palikuwa katika "Waebrania 9:9, ambako ndiyo mfano wa wakati huu uliopo sasa; wakati huo sadaka na dhabihu zinatolewa"; kwamba mahali Pake Patakatifu palikuwa "**nakala za mambo yaliyo mbinguni**"; kwamba Kristo, Kuhani wetu Mkuu, ni ***"mhudumu wa Patakatifu, na wa ile hema ya Kweli, ambayo Bwana aliiweka wala si mwanadamu."*** kwamba "***Kristo hakuingia katika Patakatifu palipofanyika kwa mikono, ndio mfano wa Patakatifu halisi; bali aliingia mbinguni hasa, aonekane sasa usoni pa Mungu kwa ajili yetu" Waebrania 9:9, 23; 8:2; Waebrania 9:24.*** **{SRSw 376.2}**

Patakatifu pa mbinguni, ambapo Yesu anahudumu kwa niaba yetu, ndipo Patakatifu pa asili (original), ambapo Patakatifu palipojengwa na Musa palikuwa nakala. Kama Patakatifu pa duniani palivyokuwa na vyumba viwili—Patakatifu, na Patakatifu pa Patakatifu—vivyo hivyo kuna sehemu mbili katika Patakatifu pa mbinguni**.** Na Sanduku la Agano lenye sheria ya Mungu, Madhabahu ya Uvumba, na vyombo vingine vya huduma vilivyopatikana katika Patakatifu chini, vina kielelezo pia katika Patakatifu hapo juu. Katika maono matakatifu, mtume Yohana aliruhusiwa kuingia mbinguni, na hapo akaona kinara na madhabahu ya uvumba, na "**hekalu la Mungu lilipofunguliwa,**" aliona pia **"Sanduku la Agano Lake." Ufunuo 4:5; 8:3; Ufunuo 11:19.** **{SRSw 377.1}**

Wale waliokuwa wakitafuta Ukweli walipata uthibitisho usiopingika wa kuwepo kwa Patakatifu mbinguni. Musa alitengeneza Patakatifu pa duniani kwa mfano alioonyeshwa. Paulo alitangaza kwamba mchoro huo ulikuwa Patakatifu pa Kweli pa mbinguni. (Waebrania 8:2, 5.) Yohana alishuhudia kwamba aliliona mbinguni. **{SRSw 377.2}**

Mwishoni mwa siku 2300, ambayo ilikuwa katika mwaka wa 1844, hakuna Patakatifu palikuwa hapa duniani kwa karne nyingi; Kwa hivyo Patakatifu pa mbinguni lazima pawe ndio lile lililoonekana na kuelezwa

katika tangazo la Danieli 8:14, “Hadi siku elfu mbili na mia tatu; ndipo Patakatifu patakapotakaswa.” Lakini Patakatifu pa mbinguni pangewezaje kuhitaji kutakaswa? Tukigeukia tena kwenye Maandiko Matakatifu, wanafunzi wa unabii walijifunza kwamba kutakaswa hakukuwa kuondolewa kwa uchafu wa kimwili, kwani kutakaswa kungefanywa kwa damu, na kwa hivyo lazima kuwe kutakaswa kutoka kwa dhambi. Hivi ndivyo mtume asemavyo: “***Basi ilikuwa sharti nakala za mambo yaliyo mbinguni zisafishwe kwa hizo, lakini mambo ya mbinguni yenyewe yasafishwe kwa dhabihu zilizo bora kuliko hizo.*** [Naam, damu ya thamani ya Kristo Mwenyewe***].” Waebrania* 9:23.** **{SRSw 377.3}**

Ili kupata ufahamu zaidi wa utakaso ambao unabii unaelekeza, ilikuwa muhimu kuelewa huduma ya Patakatifu pa mbinguni. Hili lingeweza kujifunzwa tu kutoka kwa huduma ya Patakatifu pa duniani; Kwa maana Paulo anatangaza kwamba makuhani waliohudumu hapo walihudumu ***"mfano na kivuli cha mambo ya mbinguni." Waebrania 8:5.*** **{SRSw 378.1}**

Kutakaswa kwa Patakatifu

Kama vile dhambi za watu zilivyohamishiwa hapo awali, kwa mfano, hadi Patakatifu pa duniani kwa damu ya sadaka ya dhambi, vivyo hivyo dhambi zetu, kwa Kweli, zinahamishiwa hadi Patakatifu pa mbinguni kwa damu ya Kristo. Na kama vile utakaso wa kawaida wa Patakatifu pa duniani ulivyokamilika kwa kuondolewa kwa dhambi ambazo zilichafuliwa, vivyo hivyo utakaso halisi wa Patakatifu pa mbinguni utakamilika kwa kuondolewa, au kufutwa, kwa dhambi zilizoandikwa hapo. Hii inahitaji uchunguzi wa vitabu vya kumbukumbu ili kubaini ni nani, kupitia toba ya dhambi na imani katika Kristo, wanastahili kupata faida za upatanisho Wake. Kwa hivyo, utakaso wa Patakatifu unahusisha kazi ya hukumu ya upelelezi. Kazi hii lazima

ifanyike kabla ya kuja kwa Kristo kuwakomboa watu Wake, kwani Yeye atakapokuja, atakuja na ujira Wake mkononi, kumlipa kila mtu kulingana na matendo yake. (Ufunuo 22:12.) **{SRSw 378.2}**

Hivyo wale waliofuata katika nuru iliyoendelea mbele ya Neno la unabii waliona kwamba badala ya kuja duniani mwishoni mwa siku 2300 mwaka wa 1844, Kristo kisha aliingia Patakatifu pa Patakatifu pa mbinguni, mbele za Mungu, kufanya hitimisho au kufunga kazi ya upatanisho, akijiandaa kwa kuja Kwake. **{SRSw 378.3}**

SURA YA 54—UJUMBE WA MALAIKA WA TATU

Kristo alipoingia katika Patakatifu pa Patakatifu pa hekalu la mbinguni, ili kufanya kazi ya mwisho ya upatanisho, aliwakabidhi watumishi Wake ujumbe wa mwisho wa rehema utakaotolewa kwa ulimwengu. Hilo ndio onyo la malaika wa tatu wa Ufunuo 14. Mara tu baada ya kutangazwa kwake, Mwana wa Adamu anaonekana na nabii akija katika utukufu ili kuvuna mavuno ya dunia. **{SRSw 379.1}**

Kama ilivyotabiriwa katika Maandiko, huduma ya Kristo katika Patakatifu pa Patakatifu ilianza mwishoni mwa zile siku za unabii mwaka 1844. Kwa wakati huo yanatumika Maneno ya Yohana katika Ufunuo: ***"Kisha Hekalu la Mungu lililoko mbinguni likafunguliwa, na Sanduku la Agano Lake likaonekana ndani ya hekalu Lake." Ufunuo 11:19.*** Sanduku la Agano la Mungu liko katika chumba cha pili cha Patakatifu. Kristo alipoingia humo, kuhudumu kwa niaba ya mwenye

dhambi, hekalu la ndani lilifunguliwa, na Sanduku la Mungu likaonekana. Kwa wale ambao kwa imani walimwona Mwokozi katika kazi Yake ya maombezi, ukuu na nguvu za Mungu zilifunuliwa. Pindo za vazi la utukufu Wake zikalijaza hekalu, nuru kutoka Patakatifu pa Patakatifu ilimwagika juu ya watu Wake waliokuwa wakimngojea duniani. **{SRSw 379.2}**

Kwa imani walikuwa wamemfuata Kuhani wao Mkuu kutoka Patakatifu, hadi Patakatifu pa Patakatifu, na walimwona akisihi kwa kutumia damu Yake mbele ya Sanduku la Mungu. Ndani ya Sanduku hilo Takatifu kuna sheria ya Baba, ile ile ambayo ilinenwa na Mungu Mwenyewe katikati ya ngurumo za Mlima Sinai, na kuandikwa kwa kidole Chake Mwenyewe kwenye mbao za mawe. Hakuna amri hata moja ambayo imefutwa; hakuna nukta au chembe iliyobadilishwa. Ingawa Mungu alimpa Musa nakala ya sheria Yake, alihifadhi ile nakala halisi katika Patakatifu pa juu. Wakifuatilia maagizo Yake matakatifu, watafutaji wa Ukweli walikuta, katikati kabisa ya Amri Kumi, amri ya nne, kama ilivyotangazwa kwanza: "***Ikumbuke siku ya Sabato uitakase. Siku sita fanya kazi, utende mambo yako yote; lakini siku ya saba ni Sabato ya Bwana, Mungu wako, siku hiyo usifanye kazi yo yote, wewe, wala mwana wako, wala binti yako, wala mtumwa wako, wala mjakazi wako, wala mnyama wako wa kufuga, wala mgeni aliye ndani ya malango yako. Maana, kwa siku sita Bwana alifanya mbingu, na nchi, na bahari, na vyote vilivyomo, akastarehe siku ya saba; kwa hiyo Bwana akaibarikia siku ya Sabato akaitakasa." Kutoka 20:8-11.*** **{SRSw 379.3}**

Roho wa Mungu aligusa mioyo ya wanafunzi hawa wa Neno Lake. Imani iliwajia kwamba walikuwa wamevunja amri ya nne kwa kutojua, kwa kupuuza siku ya pumziko ya Muumba. Walianza kuchunguza sababu za kuadhimisha siku ya kwanza ya juma badala ya siku ambayo

Mungu alikuwa ameitakasa. Hawakuweza kupata ushahidi wowote katika Maandiko kwamba amri ya nne ilikuwa imefutwa, au kwamba Sabato ilikuwa imebadilishwa; Baraka ambayo iliitakasa siku ya saba kwa mara ya kwanza haikuwahi kuondolewa. Walikuwa wakitafuta kwa uadilifu kujua na kufanya mapenzi ya Mungu, na sasa, walipojiona kuwa wavunja sheria Yake, huzuni ilijaza mioyo yao. Mara moja walithibitisha uaminifu wao kwa Mungu kwa kuishika na kuitakasa Sabato Yake. **{SRSw 380.1}**

Juhudi nyingi na za dhati zilifanywa ili kuipindua imani yao. Hakuna ambaye angeweza kushindwa kuona kwamba ikiwa Patakatifu pa duniani palikuwa mfano wa mbinguni, sheria iliyowekwa ndani ya Sanduku duniani ilikuwa nakala halisi ya sheria ndani ya Sanduku mbinguni, na kwamba kukubali Ukweli kuhusu Patakatifu pa mbinguni kulihusisha kukiri madai ya sheria ya Mungu, na wajibu wa Sabato ya amri ya nne. **{SRSw 380.2}**

Wale waliokubali nuru kuhusu upatanishi wa Kristo na umilele wa sheria ya Mungu, waligundua kwamba hizi ndizo zilikuwa Kweli zilizoonyeshwa katika ujumbe wa tatu. Malaika anatangaza, ***"Hapa ndipo penye subira ya watakatifu, hao wazishikao amri za Mungu, na imani ya Yesu." Ufunuo 14:12.*** Kauli hii inatanguliwa na onyo zito na la kutisha: ***"Mtu awaye yote akimsujudu huyo mnyama na sanamu yake, na kuipokea chapa katika kipaji cha uso wake, au katika mkono wake, yeye naye atakunywa katika mvinyo ya ghadhabu ya Mungu iliyotengenezwa, pasipo kuchanganywa na maji, katika kikombe cha hasira Yake." Ufunuo 14:9, 10.*** Tafsiri ya alama zilizotumika zilikuwa muhimu kwa uelewa wa ujumbe huu. Ni nini kilichowakilishwa na mnyama, sanamu, na chapa? Tena wale waliokuwa wakitafuta Ukweli walirudi kwenye utafiti wa unabii. **{SRSw 381.1}**

Mnyama na Sanamu Yake

Mnyama wa kwanza anawakilisha Kanisa la Rumi—mfumo wa kidini ulio na mamlaka ya serikali, wenye uwezo wa kuwaadhibu wote wanaopinga. Sanamu ya mnyama inawakilisha mfumo mwingine wa kidini unaofanana naye, pia ukiwa na nguvu za serikali. Kuundwa kwa sanamu hii ni kazi ya mnyama huyo mwingine, ambaye kuibuka kwake kwa amani na madai yake ya upole huifanya iwe ishara inayowakilisha Marekani-[Soma Ufunuo 13, mnyama wa kwanza na wa pili]. Hapa ndipo kunapatikana mfano wa Upapa. Wakati makanisa ya nchi yetu, yakiungana juu ya mambo kama hayo ya imani ambayo yanashikilia kwa pamoja, yatakapoishawishi Serikali kutekeleza amri zao na kudumisha taasisi zao, ndipo Amerika ya Kiprotestanti itakapounda sanamu ya uongozi wa Kirumi. **Ndipo kanisa la Kweli litakapokabiliwa na mateso kama walivyokumbana nayo watu wa Mungu wa kale.** **{SRSw 381.2}**

Mnyama mwenye pembe kama za mwana-kondoo anawaamuru "***Naye awafanya wote, wadogo kwa wakubwa, na matajiri kwa maskini, na walio huru kwa watumwa, watiwe chapa katika mkono wao wa kuume, au katika vipaji vya nyuso zao; tena kwamba mtu awaye yote asiweze kununua wala kuuza, isipokuwa ana chapa ile, yaani, jina la mnyama yule, au hesabu ya jina lake" Ufunuo 13:16, 17.*** Hii ndiyo chapa ambayo malaika wa tatu anatamka onyo lake. Ni chapa ya mnyama wa kwanza, au Upapa, na kwa hivyo inapaswa kutafutwa miongoni mwa sifa zinazotofautisha nguvu hiyo. Nabii Danieli alitangaza kwamba Kanisa la Kirumi, linalowakilishwa na pembe ndogo, lingefikiria kubadilisha **majira na sheria** (Danieli 7:25), huku Paulo akiiita **mtu wa kuasi** (2 Wathesalonike 2:3, 4), ambaye angejiinua juu ya Mungu. Ni kwa kubadilisha sheria ya Mungu pekee ndipo Upapa

ungejiinua juu ya Mungu; yeyote anatakayeitunza sheria kwa uelewa kwamba imebadilishwa, angekuwa akiipa heshima kuu nguvu hiyo ambayo mabadiliko yalifanyika. **{SRSw 382.1}**

Amri ya nne, ambayo Roma imejitahidi kuiweka kando, ndiyo amri pekee katika Amri Kumi, inayomtaja Mungu kama Muumba wa mbingu na dunia, na hivyo kumtofautisha Mungu wa Kweli na miungu yote ya uongo. Sabato ilianzishwa ili kukumbuka kazi ya uumbaji, na hivyo kuelekeza akili za wanadamu kwa Mungu wa Kweli na aliye hai. Ukweli wa nguvu Zake za uumbaji unatajwa katika Maandiko yote kama uthibitisho kwamba Mungu wa Israeli ni mkuu kuliko miungu ya kipagani. Kama Sabato ingekuwa imetunzwa wakati wote, mawazo na mapenzi ya mwanadamu yangeongozwa kwa Muumba wake kama lengo la kicho na heshima na ibada, na kusingekuwa kamwe mwabudu sanamu duniani, wala mtu asiyeamini Mungu, au kafiri. **{SRSw 382.2}**

Taasisi hiyo inayomtaja Mungu kama Muumba ni ishara ya mamlaka Yake halali juu ya viumbe alivyoviumba. Mabadiliko ya Sabato ni ishara, au alama, ya mamlaka ya Kanisa la Kirumi. Wale wanaoyaelewa madai ya amri ya nne lakini wakachagua siku nyingine badala ya ile ya Kweli, wanakuwa wanaitambua fika mamlaka iliyofanya mabadiliko hayo. **{SRSw 383.1}**

Ujumbe wa Kutisha

Onyo kali kuliko yote lililowahi kutolewa kwa wanadamu liko katika ujumbe wa malaika wa tatu. Dhambi hii ni kubwa kiasi kwamba inaleta ghadhabu ya Mungu isiyo na rehema. Watu hawapaswi kuachwa gizani kuhusu jambo hili; onyo lazima litangazwe ili wote wapate kuelewa na kuwa na nafasi ya kuepuka hukumu. **{SRSw 383.2}**

Katika suala la pambano kuu, Maoni na Ibada za makundi mawili tofauti, yanayopingana yameendelezwa. Kundi moja "linamwabudu

mnyama na sanamu yake, na kupokea alama yake," na hivyo kujiletea hukumu mbaya zinazotolewa na malaika wa tatu. Kundi lingine, tofauti kabisa na ulimwengu, "linazishika amri za Mungu, na imani ya Yesu." Ufunuo 14:9, 12. **{SRSw 383.3}**

Hizo ndizo Kweli muhimu zilizofunguliwa mbele ya wale waliopokea ujumbe wa malaika wa tatu. Walipopitia uzoefu wao kuanzia tangazo la kwanza la ujio wa pili, hadi kupita kwa wakati mnamo 1844, waliona kukata tamaa kwao kukiwa kumeelezewa sababu yake, na matumaini na furaha vikaamsha tena mioyo yao. Nuru kutoka Patakatifu iliangaza yaliyopita, ya sasa, na yajayo, na walijua kwamba Mungu alikuwa amewaongoza kwa mipango na majaliwa Yake yasiyo na makosa. Sasa kwa ujasiri mpya na imani thabiti, walijiunga katika kutoa onyo la malaika wa tatu. Tangu 1844, katika kutimiza unabii wa ujumbe wa malaika wa tatu, umakini wa ulimwengu umeelekezwa kwa Sabato ya Kweli, na idadi inayoongezeka kila mara inarudi kwenye utunzaji wa hii siku takatifu ya Mungu. **{SRSw 383.4}**

SURA YA 55—JUKWAA IMARA

Niliona kundi la watu waliokuwa wamesimama vizuri, wakilindwa na kuwa imara, bila kutoa nafasi kwa wale ambao wangeweza kutikisa imani iliyowekwa ya kundi hilo. Mungu aliwaangalia kwa kibali. Nikaonyeshwa hatua tatu—ujumbe wa malaika wa kwanza, wa pili, na wa tatu. Malaika aliyeandamana nami alisema: “Ole wake yeye atakayesogeza tofali/jiwe au pini au kuvuruga thamani ya ujumbe huu. Uelewa wa Kweli wa ujumbe huu ni muhimu sana. Hatima ya roho hutegemea jinsi Jumbe hizi zinavyopokelewa.” **{SRSw 385.1}**

Nilirudishwa tena kupitia ujumbe huu, na nikaona jinsi watu wa Mungu walivyolipia kwa gharama uzoefu wao. Uzoefu huu ulipatikana

kupitia mateso mengi na migogoro mikali. Mungu alikuwa amewaongoza hatua kwa hatua, hadi alipowaweka kwenye jukwaa imara lisiloweza kuhamishika. Niliona watu karibu wote wakikaribia jukwaa na kuchunguza msingi. Baadhi kwa furaha waliukanyaga mara moja. Wengine walianza kupata makosa kwenye msingi. Walitamani maboresho yafanyike, na kisha jukwaa lingekuwa kamili zaidi na watu wawe na furaha zaidi. **{SRSw 385.2}**

Baadhi walitoka kwenye jukwaa ili kulichunguza, na kutangaza kuwa limewekwa vibaya. Lakini niliona kwamba karibu watu wote walisimama imara kwenye jukwaa na kuwahamasisha wale waliokuwa wametoka kuacha malalamiko yao; kwa maana Mungu alikuwa Mjenzi Mkuu, nao walikuwa wakipigana Naye. Walisimulia kazi ya ajabu ya Mungu, ambayo iliwaongoza kwenye jukwaa imara, na kwa umoja waliinua macho yao mbinguni na kwa sauti kubwa wakamtukuza Mungu. Hili liliathiri baadhi ya wale waliokuwa wamelalamika na kuondoka kwenye jukwaa, nao kwa mtazamo wa unyenyekevu wakarudi na kukanyaga tena ule msingi-jukwaa. **{SRSw 385.3}**

Uzoefu wa Wayahudi Ulirudiwa

Nilielekezwa nyuma kwenye tangazo la ujio wa kwanza wa Kristo. Yohana alitumwa kwa roho na nguvu ya Eliya kuandaa njia kwa ajili ya Yesu. Wale waliokataa ushuhuda wa Yohana hawakufaidika na mafundisho ya Yesu. Upinzani wao kwa ujumbe uliotabiri kuja Kwake uliwaweka mahali ambapo hawangeweza kupokea kwa urahisi ushahidi wenye nguvu zaidi kwamba Yeye alikuwa Masihi. Shetani aliwaongoza wale waliokataa ujumbe wa Yohana kwenda mbali zaidi, kumkataa na kumsulubisha Kristo. Kwa kufanya hivi walijiweka mahali ambapo hawangeweza kupokea baraka siku ya Pentekoste, ambayo ingewafundisha njia ya kuingia Patakatifu pa mbinguni. **{SRSw 386.1}**

Kupasuka kwa pazia la hekalu, kulionyesha kwamba dhabihu na maagizo ya Kiyahudi hayangepokelewa tena. Dhabihu kubwa ilikuwa imetolewa na ilikuwa imekubaliwa, na Roho Mtakatifu aliyeshuka siku ya Pentekoste aliwageuza wanafunzi kutoka Patakatifu pa duniani hadi pa mbinguni, ambapo Yesu alikuwa ameingia kwa damu Yake Mwenyewe, kumwaga juu ya wanafunzi Wake faida za upatanisho Wake. Lakini Wayahudi waliachwa gizani kabisa. Walipoteza nuru yote ambayo wangeweza kuwa nayo juu ya mpango wa wokovu, na bado waliamini katika dhabihu na sadaka zao zisizo na maana. Patakatifu pa mbinguni palichukua nafasi ya Patakatifu pa dunia, lakini hawakuwa na ufahamu wa mabadiliko hayo. Kwa hivyo hawangeweza kufaidika na upatanishi wa Kristo katika mahali Patakatifu. **{SRSw 386.2}**

Wengi wanaangalia kwa hofu na kushtuka mwenendo wa Wayahudi katika kumkataa na kumsulubisha Kristo; na wanaposoma historia ya matusi Yake ya aibu, wakifikiri kwamba wanampenda sana, na hawangemkana kama Petro, au kumsulubisha kama Wayahudi. Lakini Mungu, anayesoma mioyo ya wote, ameupima na kuuleta kuujaribu upendo huo kwa Yesu, ambao watu walidai kuuhisi. **{SRSw 387.1}**

Mbingu yote ilitazama kwa shauku kubwa upokeaji wa ujumbe wa malaika wa kwanza. Lakini wengi waliodai kumpenda Yesu, na ambao walitoa machozi waliposoma kisa cha msalaba, walidhihaki habari njema za kuja Kwake. Badala ya kupokea ujumbe huo kwa furaha, waliutangaza kuwa ni udanganyifu. Waliwachukia wale waliopenda kuonekana Kwake Kristo, na kuwafungia nje ya makanisa. Wale waliokataa ujumbe wa kwanza hawakuweza kufaidika na ujumbe wa pili; wala hawakufaidika na kilio cha usiku wa manane, ambacho kilikuwa cha kuwaandaa kuingia na Yesu kwa imani katika Patakatifu pa Patakatifu pa mbinguni. Na kwa kukataa jumbe hizo mbili za awali,

wametia giza uelewa wao kiasi kwamba hawawezi kuona nuru katika ujumbe wa malaika wa tatu, ambao unaonyesha njia ya kuingia Patakatifu pa Patakatifu. **{SRSw 387.2}**

SURA YA 56—UDANGANYIFU WA SHETANI

Shetani alianza udanganyifu wake Edeni. Alimwambia Hawa, "**Hakika hamtakufa**." Hili lilikuwa somo la kwanza la Shetani kuhusu kutokufa kwa roho, na ameendeleza udanganyifu huu tangu wakati huo hadi sasa, na ataendelea nao hadi utumwa wa watoto wa Mungu utakapogeuzwa. Nilielekezwa kwa Adamu na Hawa katika bustani ya Edeni. Walikula matunda ya mti uliokatazwa, kisha upanga wa moto ukawekwa kuzunguka mti wa uzima, nao wakafukuzwa kutoka bustanini, wasije wakala matunda ya mti wa uzima, na kuwa wenye dhambi

wasiokufa. Tunda la mti huu lilikuwa kwa ajili ya kuendeleza kutokufa. Nilimsikia malaika akiuliza, “Ni nani wa familia ya Adamu aliyepitisha upanga huo wa moto na kushiriki matunda ya mti wa uzima?” Nilimsikia malaika mwingine akijibu, “Hakuna hata mmoja wa familia ya Adamu aliyepitisha upanga huo wa moto na kushiriki matunda ya mti huo; kwa hivyo hakuna mwenye dhambi asiyekufa.” Roho inayotenda dhambi, itakufa kifo cha milele—kifo ambacho hakitakuwa na tumaini la ufufuo; na ndipo ghadhabu ya Mungu itatulizwa. Ilikuwa ajabu kwangu kwamba Shetani angeweza kufanikiwa vizuri sana katika kuwafanya wanadamu waamini kwamba Maneno ya Mungu, “**Roho ile itendayo dhambi, itakufa” (Ezekieli 18:4),** yanamaanisha kwamba roho inayotenda dhambi haitakufa, bali itaishi milele katika taabu na huzuni. Malaika alisema, “Uzima ni uzima, iwe ni katika maumivu au furaha. Kifo hakina maumivu, bila furaha, bila chuki.” **{SRSw 388.1}**

Shetani aliwaambia malaika zake wafanye juhudi maalum ya kueneza uwongo ambao kwanza ulirudiwa kwa Hawa huko Edeni, “Hakika hamtakufa.” Na kadri kosa lilivyopokelewa na watu, na wakaongozwa kuamini kwamba mwanadamu hakufa, Shetani aliwaongoza kuamini kwamba mwenye dhambi angeishi katika taabu ya milele. **{SRSw 388.2}**

Kisha njia iliandaliwa kwa Shetani kufanya kazi kupitia wawakilishi wake na kumsimamisha Mungu mbele ya watu kama mtawala wa kisasi—mtu anayewatumbukiza wote kuzimuni ambao hawampendezi, na kuwafanya wahisi ghadhabu yake; na huku wakiteseka kwa uchungu usioelezeka, na kugaagaa katika moto wa milele, Yeye anawakilishwa kama yule ambaye anawatazama chini kwa kuridhika. Shetani alijua kwamba ikiwa kosa hili lingepokelewa, Mungu angechukiwa na wanadamu wengi, badala ya kupendwa na kuabudiwa; na kwamba wengi wangeongozwa kuamini kwamba vitisho vya Neno la

Mungu havingetimizwa kihalisi, kwani itakuwa kinyume cha tabia Yake ya ukarimu, fadhili na upendo kutumbukiza katika mateso ya milele ya viumbe alivyoviumba. **{SRSw 389.1}**

Kuna upotovu mwingine uliopitiliza ambao Shetani amewaongoza watu kuufuata ni kupuuza kabisa haki ya Mungu na vitisho vya Neno Lake, na kumwakilisha Yeye kama Mwenye rehema yote, hivi kwamba hakuna hata mtu mmoja atapotea, bali wote, watakatifu na wanadamu wote wenye dhambi, hatimaye wataokolewa katika ufalme Wake. **{SRSw 389.2}**

Kwa sababu ya makosa maarufu ya kutokufa kwa roho na mateso yasiyo na mwisho, Shetani anatumia kundi lingine na kuwaongoza kuiona Biblia kama kitabu kisicho na mwongozo. Wanafikiri inafundisha mambo mengi mazuri, lakini hawawezi kuitegemea na kuipenda, kwa sababu wamefundishwa kwamba inatangaza Fundisho la mateso ya milele [Doctrine of eternal misery]. **{SRSw 389.3}**

Kundi jingine Shetani analiongoza kupitiliza zaidi, na hata kukana uwepo wa Mungu. Hawawezi kuona uthabiti au mwendelezo [consistency] wowote katika tabia ya Mungu wa Biblia, endapo ataleta mateso mabaya kwa sehemu ya familia ya wanadamu milele. Kwa hivyo wanaikana Biblia na Mwandishi Wake, na wanaona kifo kama usingizi wa milele. **{SRSw 390.1}**

Bado kuna kundi lingine ambalo ni waoga na hawana ujasiri[timid],. Shetani hawa huwajaribu kutenda dhambi, na baada ya kutenda dhambi, anawaonyesha mbele yao kwamba mshahara wa dhambi si mauti bali ni uzima katika mateso makali, ambayo watayavumilia katika vizazi visivyo na mwisho vya umilele. Kwa kuinua mbele ya akili zao dhaifu hofu za kuzimu isiyo na mwisho, anazichota akili zao, nao wanapoteza busara na akili zao. Kisha Shetani

na malaika zake wanashangilia, na wasioamini Mungu na makafiri wanajiunga na kutukana Ukristo. Wanadai kwamba maovu haya ni matokeo ya kawaida ya kuamini Biblia na Mwandishi Wake, ilhali ni matokeo ya kupokea uzushi maarufu. **{SRSw 390.2}**

Maandiko ni Mlinzi na Usalama Wetu

Niliona kwamba jeshi la mbinguni lilijawa na hasira kwa kazi hii ya ujasiri ya Shetani. Niliuliza kwa nini udanganyifu huu wote uachiliwe ili kuathiri akili za wanadamu wakati malaika wa Mungu walikuwa na nguvu, na ikiwa wangeagizwa, wangeweza kuvunja kwa urahisi nguvu ya adui. Kisha nikaona kwamba Mungu alijua kwamba Shetani angejaribu kila sanaa kumwangamiza mwanadamu; kwa hivyo alikuwa amesababisha Neno Lake liandikwe, na alikuwa ameweka makusudi Yake kuhusu jamii ya wanadamu wazi sana kiasi kwamba hata mtu dhaifu zaidi hawezi kukosea. Baada ya kumpa mwanadamu Neno Lake, alikuwa ameilinda kwa uangalifu kutokana na uharibifu na Shetani au malaika zake, au na yeyote kati ya mawakala au wawakilishi wake. Ingawa vitabu vingine vinaweza kuharibiwa, hiki kingekuwa kisichokufa-cha milele. Na karibu na mwisho wa wakati, wakati udanganyifu wa Shetani unaongezeka, Neno la Mungu litakuwa likiongezeka sana kiasi kwamba wote wanaoitaka wangeweza kuwa na nakala, na, kama wangetaka, wangeweza kujihami dhidi ya udanganyifu na maajabu ya uongo ya Shetani. **{SRSw 390.3}**

Niliona kwamba Mungu alikuwa ameilinda Biblia hasa; lakini nakala zake zilipokuwa chache, watu wenye elimu katika baadhi ya matukio walikuwa walibadilisha maneno, wakifikiri kwamba walikuwa wakilifanya liwe wazi zaidi, wakati kwa kweli walikuwa wakificha kile kilicho wazi na kukifanya kiwe fumbo, kwa kufanya Neno liegemee mitazamo yao waliyoianzisha, ambayo ilitawaliwa na mapokeo. Lakini niliona kwamba Neno la Mungu, kwa ujumla, ni mnyororo mkamilifu,

sehemu moja ikiunganisha na kuelezea nyingine. Watafutaji wa ile Kweli kiukweli hawapaswi kukosea, kwani sio tu kwamba Neno la Mungu ni wazi na rahisi katika kutangaza njia ya uzima, lakini Roho Mtakatifu ametolewa kama mwongozo katika kuelewa njia ya uzima iliyofunuliwa ndani yake. **{SRSw 391.1}**

Niliona kwamba malaika wa Mungu hawapaswi kamwe kudhibiti mapenzi ya mtu. Mungu huweka mbele ya mwanadamu uzima na kifo. Mtu anaweza kuwa na chaguo lake. Wengi wanatamani uzima, lakini bado wanaendelea kutembea katika njia pana. Wanachagua kuasi serikali ya Mungu, licha ya rehema na huruma Yake kubwa katika kumtoa Mwanawe afe kwa ajili yao. Wale ambao hawakubali wokovu ulionunuliwa kwa thamani kubwa, lazima waadhibiwe. Lakini niliona kwamba Mungu hangewafunga kuzimu ili kuvumilia mateso yasiyo na mwisho, wala hatawapeleka mbinguni; kwani kuwaleta katika kundi la wale walio safi na watakatifu kungewafanya wawe na huzuni kubwa. Lakini atawaangamiza kabisa na kuwafanya wawe kama hawakuwapo; ndipo haki Yake itatoshelezwa. Aliumba mwanadamu kutoka katika mavumbi ya nchi, na wasiotii na wasio watakatifu watateketezwa kwa moto na kurudi mavumbini tena. Niliona kwamba wema na huruma ya Mungu katika jambo hili inapaswa kuwaongoza wote kuipenda na kuitamani tabia Yake na kuliabudu Jina Lake takatifu. Baada ya waovu kuangamizwa kutoka duniani, jeshi lote la mbinguni litasema, “Amina!” **{SRSw 391.2}**

Shetani anawatazama kwa kuridhika sana wale wanaokiri Jina la Kristo, lakini bado wanashikilia kwa karibu udanganyifu ambao yeye mwenyewe ameanzisha. Kazi yake bado ni kubuni udanganyifu mpya, na nguvu na sanaa yake katika mwelekeo huu inaongezeka kila mara. Aliwaongoza wawakilishi wake, mapapa na makuhani, kujitukuza, na kuwachochea watu kuwatesa kwa uchungu na kuwaangamiza wale

ambao hawakuwa tayari kukubali udanganyifu wake. Jamani! mateso na maumivu ambayo wafuasi wa thamani wa Kristo walilazimishwa kuvumilia! Malaika wameweka rekodi ya uaminifu ya yote. Shetani na malaika wake waovu kwa furaha aliwaambia malaika waliowahudumia watakatifu hawa wanaoteseka kwamba wote watauawa, ili asibaki Mkristo wa kweli duniani. Niliona kwamba kanisa la Mungu lilikuwa safi wakati huo. Hakukuwa na hatari ya watu wenye mioyo miovu kuingia humo, kwani Mkristo wa Kweli, aliyethubutu kutangaza imani yake, alikuwa katika hatari ya kutundikwa kwenye mti wa kuunguza waamini, na kila mateso ambayo Shetani na malaika wake waovu wangeweza kubuni au kuhamasisha akilini mwa mwanadamu. **{SRSw 392.1}**

SURA YA 57—UMIZIMU

Fundisho la kutokufa kwa asili limeandaa njia kwa ajili ya umizimu wa enzi hizi. Ikiwa wafu wanakubaliwa mbele ya Mungu na malaika watakatifu, na kupewa ujuzi unaozidi sana kile walichokuwa nacho hapo awali, kwa nini basi wasirudi duniani kuwaangazia na kuwafundisha walio hai? Wale wanaoamini katika ufahamu wa mwanadamu katika kifo, wanawezaje kukataa kile kinachowajia kama

nuru ya Kiungu inayowasilishwa na roho zilizotukuzwa? Hapa kuna njia inayoonekana kama takatifu, ambayo Shetani hufanya kazi kwa ajili ya kutimiza makusudi yake. Malaika walioanguka wanatenda maagizo yake huonekana kama wajumbe kutoka ulimwengu wa roho. Huku wakidai kuwaleta walio hai katika mawasiliano na wafu, Shetani hutumia ushawishi wake wa kuroga akilini mwao. **{SRSw 393.1}**

Adui ana uwezo hata wa kuleta mbele ya watu mwonekano wa marafiki zao walioondoka. Hiyo bandia ya mtu aliyekufa inaonekama kama vile kamilifu, kama vile ndiye mwenyewe; mwonekano unaojulikana, maneno, sauti, toni, huzalishwa kwa uwazi wa ajabu. Wengi wanafarijika na uhakika kwamba wapendwa wao wanafurahia furaha ya mbinguni, na bila shaka ya hatari wanasikiliza roho zinazodanganya na mafundisho ya mashetani. **{SRSw 393.2}**

Wanapoongozwa kuamini kwamba wafu kweli hurudi kuwasiliana nao, Shetani husababisha wale walioingia kaburini bila kujiandaa [kuonekana kwa namna ya mizimu]. Wanadai kuwa na furaha mbinguni, na hata kuchukua nafasi za juu huko; na hivyo kosa hilo linafundishwa sana, kwamba hakuna tofauti kati ya wenye haki na waovu. Wageni wa kujifanya kutoka ulimwengu wa roho wakati mwingine hutoa tahadhari na maonyo ambayo yanathibitika kuwa sahihi. Kisha, kadri ujasiri unavyopatikana, wanawasilisha mafundisho ambayo yanadhoofisha moja kwa moja imani katika Maandiko. Kwa mwonekano wa kupendezwa sana na ustawi wa marafiki zao duniani, wanazua makosa hatari zaidi. Ukweli kwamba wanasema Ukweli fulani, na wakati mwingine wanaweza kutabiri matukio yajayo, huipa kauli zao mwonekano wa kuaminika; na mafundisho yao ya uongo yanakubaliwa na umati wa watu kwa urahisi, na yanaaminika bila kuficha, kana kwamba yalikuwa zile Kweli takatifu zaidi za Biblia. Sheria ya Mungu inawekwa kando, Roho wa neema anadharauliwa, damu ya agano

inahesabiwa kuwa kitu kisicho kitakatifu. Mizimu hukataa Uungu wa Kristo na kumweka hata Muumba katika kiwango sawa na wao wenyewe. Kwa hivyo, chini ya umbo jipya, mwasi mkuu bado anaendelea na vita vyake dhidi ya Mungu, vilivyoanza mbinguni na kwa karibu miaka elfu sita viliendelea duniani. **{SRSw 393.3}**

Wengi hujitahidi kuhesabu udhihirisho wa kiroho kwa kuuhusisha kabisa na ulaghai na hila ya kutumia mkono [kama watu wafanyavyo kwenye mazingaombwe, uchawi au ushirikina]. Ingawa ni kweli kwamba matokeo ya ujanja huu wa mazingaombwe yamechukuliwa kama udhihirisho wa kweli, pia kumekuwa na maonyesho dhahiri ya nguvu isiyo ya kawaida. Udanganyifu wa ajabu ambao umizimu wa kisasa ulianza nao haukuwa matokeo ya ujanja au hila za kibinadamu, bali kazi ya moja kwa moja ya malaika waovu, ambao kwa jinsi hiyo, walianzisha mojawapo ya udanganyifu uliofanikiwa zaidi wa kuharibu roho. Wengi watanaswa kupitia imani kwamba umizimu ni udanganyifu wa kibinadamu tu; watakapoletwa ana kwa ana na udhihirisho ambao hawawezi kuuona kama usio wa kawaida, au wa kimiujiza, basi watadanganywa, na wataongozwa kuukubali kama nguvu kuu ya Mungu. **{SRSw 394.1}**

Watu hawa hupuuza ushuhuda wa Maandiko kuhusu maajabu yaliyofanywa na Shetani na mawakala wake. Ilikuwa kwa msaada wa Shetani kwamba wachawi wa Farao waliwezeshwa kuiga kazi ya Mungu. Mtume Yohana, akielezea nguvu ya kufanya miujiza ambayo itadhihirishwa katika siku za mwisho, anatangaza: ***"Naye afanya ishara kubwa, hata kufanya moto kushuka kutoka mbinguni uje juu ya nchi mbele ya wanadamu. Naye awakosesha wale wakaao juu ya nchi, kwa ishara zile alizopewa kuzifanya mbele ya huyo mnyama, akiwaambia wakaao juu ya nchi kumfanyia sanamu yule mnyama, aliyekuwa na jeraha la upanga naye akaishi." Ufunuo 13:13, 14.*** Huu siyo

udanganyifu mdogo au kujifanya tu, bali ni jambo zito zaidi ya hapo. Wanadamu wanadanganywa na miujiza ambayo mawakala wa Shetani wana uwezo wa kufanya, si ambayo wanaigiza kuifanya. **{SRSw 395.1}**

Uchawi Katika Umbo la Kisasa

Jina lenyewe la uchawi, sasa linachukuliwa kuwa jambo la kudharau. Dai kwamba wanadamu wanaweza kufanya ngono na pepo wabaya linachukuliwa kama hekaya za Zama za Giza. Lakini umizimu, ambao unahesabu watu wake walioongoka kwa mamia ya maelfu, naam, kwa mamilioni, ambao umeingia katika duru za kisayansi, ambao umevamia makanisa umepata kibali katika vyombo vya sheria, na hata katika mahakama za wafalme—udanganyifu huu mkubwa ni uamsho katika uficho mpya au barakoa mpya. **{SRSw 395.2}**

Shetani anawadanganya watu sasa, kama alivyomdanganya Hawa huko Edeni, kwa kuchochea hamu ya kupata maarifa yaliyokatazwa au kupigiwa marufuku. "Mtakuwa kama miungu," anatangaza, "mkijua mema na mabaya." Mwanzo 3:5. Lakini hekima ambayo umizimu hutoa ni ile iliyoelezwa na mtume Yakobo, ambayo ***"siyo ile ishukayo kutoka juu, bali ni ya dunia, ya tabia ya kibinadamu, na Shetani."*** **Yakobo 3:15.** **{SRSw 395.3}**

Mkuu wa giza ana akili timamu, na kwa ustadi hubadilisha majaribu yake kwa watu wa kila aina ya hali na utamaduni. Anafanya kazi "kwa udanganyifu wote wa udhalimu" ili kupata udhibiti wa wanadamu, lakini anaweza kutimiza lengo lake tu wanapokubali kwa hiari majaribu yake. Wale wanaojiweka katika uwezo wake kwa kujiingiza katika tabia zao mbaya, hawajui hata kidogo mahali ambapo njia yao itaishia. Mjaribu hutimiza uharibifu wao, na kisha huwatumia kuwaangamiza wengine. **{SRSw 396.1}**

Hakuna Anayepaswa Kudanganywa

Lakini hakuna anayehitaji kudanganywa na madai ya uwongo ya umizimu. Mungu ameupa ulimwengu nuru ya kutosha kuwawezesha kugundua mtego. Kama hakukuwa na ushahidi mwingine, habari hizi zinapaswa kutosha kwa Mkristo kwamba mmizimu hatofautishi kati ya haki na dhambi, kati ya mitume wa Kristo walio watukufu na safi zaidi na watumishi wa Shetani walio wafisadi zaidi. Kwa kuwawakilisha wanadamu wa chini kabisa kama wapo mbinguni, na walioinuliwa sana huko, Shetani hutangaza kwa ulimwengu, Haijalishi wewe ni mwovu kiasi gani; haijalishi iwe unaamini au huamini Mungu na Biblia. Wewe ishi unavyotaka; mbinguni ni nyumbani kwako. **{SRSw 396.2}**

Zaidi ya hayo, mitume wanaodaiwa na roho hizi hufanywa kupingana na yale waliyoandika kwa amri ya Roho Mtakatifu wanapokuwa duniani. Wanakana asili ya Kiungu ya Biblia, na hivyo kubomoa msingi wa tumaini la Mkristo, na kuizima nuru inayofunua njia ya kwenda mbinguni. **{SRSw 396.3}**

Shetani anaufanya ulimwengu kuamini kwamba Biblia ni riwaya tu, au angalau kitabu kinachofaa kwa jamii ya wanadamu wachanga tu, lakini sasa kichukuliwe vyepesi tu au kutupwa kando kuwa kimepitwa na wakati. Na anaweka wazi maonyesho ya kiroho kuchukua nafasi ya Neno la Mungu. Hapa kuna njia/uchawi ilio chini ya udhibiti wake kabisa; Kwa njia hii anaweza kuifanya dunia iamini atakavyo. Kitabu ambacho ni cha kumhukumu yeye na wafuasi wake anakiweka kwenye kivuli, pale anapotaka; na Mwokozi wa dunia anamweka kama mtu wa kawaida tu. Na kama vile walinzi wa Kirumi waliolilinda kaburi la Yesu walivyoeneza ripoti ya uwongo ambayo makuhani na wazee waliweka vinywani mwao ili kukanusha ufufuo Wake, ndivyo waumini wa udhihirisho wa umizimu wanavyojaribu kufanya ionekane kwamba hakuna kitu cha ajabu katika hali ya maisha Mwokozi wetu. Baada ya

kutafuta hivyo kumweka Yesu huko nyuma (usuli), wanaleta umakini wa watu kwenye miujiza yao wenyewe, wakitangaza kwamba hii miujiza yao, inazidi kabisa, kazi za Kristo. **{SRSw 396.4}**

Nabii Isaya asema hivi: ***"Na wakati watakapokuambia, Tafuta habari kwa watu wenye pepo na kwa wachawi; waliao kama ndege na kunong'ona; je! Haiwapasi watu kutafuta habari kwa Mungu wao? Je! Waende kwa watu waliokufa kwa ajili ya watu walio hai? Na waende kwa sheria na ushuhuda; ikiwa hawasemi sawasawa na Neno hili, bila shaka kwa hao hapana asubuhi." Isaya 8:19, 20*** Kama watu wangekuwa tayari kupokea Ukweli uliosemwa waziwazi katika Maandiko, kwamba wafu hawajui lolote, wangeona katika madai na maonyesho ya umizimu utendaji wa Shetani kwa nguvu na ishara na maajabu ya uongo. Lakini badala ya kutoa uhuru unaokubalika sana kwa moyo wa kimwili, na kukataa dhambi wanazozipenda, umati wa watu hufunga macho yao dhidi ya nuru, na kutembea moja kwa moja, bila kujali maonyo, huku Shetani akisuka mitego yake juu yao, na kisha wanakuwa mawindo yake. ***"Kwa sababu hawakukubali kuipenda ile Kweli, wapate kuokolewa. Kwa hiyo Mungu awaletea nguvu ya upotevu, wauamini uongo." 2 Wathesalonike 2:10, 11.*** **{SRSw 397.1}**

Wale wanaopinga mafundisho ya Umizimu wanashambulia, si watu peke yao, bali Shetani na malaika zake. Wameingia kwenye mashindano dhidi ya falme na mamlaka na roho mbaya katika mahali pa juu. Shetani hatatoa sentimeta moja ya ardhi isipokuwa kama anavyorudishwa nyuma na uwezo wa wajumbe wa mbinguni. Watu wa Mungu wanapaswa kukutana naye adui, kama alivyofanya Mwokozi wetu, kwa maneno, "Imeandikwa." Shetani anaweza kunukuu Maandiko sasa kama katika siku za Kristo, na atapotosha mafundisho Yake ili kudumisha udanganyifu wake. Lakini maamshi au taarifa za wazi za Biblia zitatoa silaha zenye nguvu katika kila pambano. **{SRSw 397.2}**

Wale ambao wangesimama katika wakati wa hatari lazima waelewe ushuhuda wa Maandiko kuhusu asili ya mwanadamu na hali ya wafu, kwa kuwa katika siku za usoni wengi watakabiliwa na roho za mashetani wanaojifanya jamaa wapendwa au marafiki na kutangaza uzushi hatari zaidi. Wageni hawa watavutia huruma zetu za dhati na watafanya miujiza ili kuendeleza majivuno yao. Ni lazima tuwe tayari kuwastahimili kwa Ukweli wa Biblia kwamba wafu hawajui lolote, na kwamba wale wanaoonekana hivyo ni roho za mashetani. **{SRSw 398.1}**

Kwa muda mrefu Shetani amekuwa akijiandaa kwa juhudi zake za mwisho za kudanganya ulimwengu. Msingi wa kazi yake uliwekwa na uhakikisho aliopewa Hawa katika Edeni, ***"Hakika hamtakufa, kwa maana Mungu anajua ya kwamba siku mtakayokula matunda ya mti huo, mtafumbuliwa macho, nanyi mtakuwa kama Mungu, mkijua mema na mabaya." Mwanzo 3:4, 5.*** Kidogo kidogo ametayarisha njia kwa ajili ya kazi yake bora ya udanganyifu katika maendeleo ya umizimu. Bado hajafikia utimilifu kamili wa miundo yake; Lakini itafikiwa katika masalio ya mwisho ya wakati, na ulimwengu utafagiliwa katika safu ya udanganyifu huu. Wanaingizwa kwa haraka katika usalama mbaya, ili kuamshwa tu na kumwagwa kwa ghadhabu ya Mungu. **{SRSw 398.2}**

SURA YA 58—KILIO KIKUU

Niliona malaika wakiharakisha huku na huko, wakishuka duniani, na tena wakipanda mbinguni, wakijitayarisha kwa ajili ya kutimizwa kwa tukio fulani muhimu. Kisha nikaona malaika mwingine mwenye nguvu aliyeagizwa kushuka duniani, kuunganisha sauti yake na malaika wa tatu, na kutoa nguvu na nguvu kwa ujumbe wake. Nguvu kuu na utukufu vilitolewa kwa malaika, na aliposhuka, dunia iliangazwa kwa utukufu Wake. Nuru iliyokuwa juu ya malaika huyu ilipenya kila mahali, huku akilia kwa nguvu, kwa sauti kuu, ***"Akalia kwa sauti kuu, akisema, Umeanguka, umeanguka Babeli ule mkuu; umekuwa maskani ya mashetani, na ngome ya kila roho mchafu, na ngome ya kila ndege mchafu mwenye kuchukiza;" Ufunuo 18:2.*** **{SRSw 399.1}**

Ujumbe wa anguko la Babeli, kama ulivyotolewa na malaika wa pili, unarudiwa, na kutajwa kwa ziada kwa ufisadi ambao umekuwa ukiingia makanisani tangu 1844. Kazi ya malaika huyu inakuja kwa wakati ufaao ili kujiunga katika kazi kuu ya mwisho ya ujumbe wa malaika wa tatu, inapoongezeka na kuwa kilio kikuu. Na watu wa Mungu hivyo wako tayari kusimama katika saa ya majaribu, ambayo watakutana nayo hivi karibuni. Niliona nuru kubwa ikikaa juu yao, nao wakaungana kutangaza ujumbe wa malaika wa tatu bila woga. **{SRSw 399.2}**

Malaika walitumwa kumsaidia malaika mwenye nguvu kutoka mbinguni, na nikasikia sauti ambazo zilionekana kusikika kila mahali, **"Tokeni kwake, enyi watu wangu, msishiriki dhambi zake, wala msipokee mapigo yake. Kwa maana dhambi zake zimefika hata mbinguni, na Mungu amekumbuka maovu yake." Ufunuo 18:4,5** Akitangaza anguko la Babeli na kuwaita watu wa Mungu watoke ndani yake, ili waepuke adhabu yake ya kutisha. **{SRSw 399.3}**

Nuru iliyokuwa juu ya wale wanaongoja ilipenya kila mahali, na wale katika makanisa ambao walikuwa na nuru yoyote, ambao

hawakuwa wamesikia na kukataa jumbe hizo tatu, walitii wito na kuyaacha makanisa yaliyoanguka. Wengi walikuwa wamefikia miaka mingi ya uwajibikaji tangu jumbe hizi zilipotolewa, na nuru ikamulika, na walikuwa na fursa la kuchagua uzima au kifo. Wengine walichagua uzima na wakachukua msimamo wao pamoja na wale waliokuwa wakimtafuta Mungu wao na kushika amri Zake zote. Ujumbe wa tatu ulikuwa ufanye kazi yake; wote walipaswa kujaribiwa nao, na wale walio wa thamani walikuwa watoke katika taasisi za kidini. **{SRSw 400.1}**

Nguvu inayobidisha iliwasukuma waaminifu, wakati udhihirisho wa uwezo wa Mungu ulileta hofu na kizuizi juu ya jamaa na marafiki zao wasioamini ili wasithubutu, wala hawakuwa na uwezo wa kuwazuia wale waliohisi kazi ya Roho wa Mungu juu yao. Wito wa mwisho ulichukuliwa hata kwa watumwa maskini; na wachamungu miongoni mwao wakamimina nyimbo zao za furaha zilizorindima kwa tazamio la ukombozi wao wenye furaha. [Kumbuka.—Kwamba kutakuwa na utumwa wakati wa Majilio ya Pili- hili linawekwa wazi na Nabii Yohana katika Ufunuo 6:15, 16, katika maelezo yake ya wazi ya “kila mtumwa, na kila mtu huru” akiita “milima na miamba”kuwaangukia na kuwaficha. “Kutoka katika uso wa Yeye aketiye juu ya kiti cha enzi.”—Wakusanyaji.] Mabwana zao hawakuweza kuwachunguza; Hofu na mshangao viliwaweka kimya. Miujiza yenye nguvu ilifanyika, wagonjwa waliponywa, na ishara na maajabu yakawafuata waumini. Mungu alikuwa katika kazi, na kila mtakatifu, bila woga wa matokeo, alifuata usadikisho wa dhamiri yake mwenyewe na kuunganishwa na wale waliokuwa wakizishika amri zote za Mungu; Na kwa nguvu walitangaza ujumbe wa tatu nje ya nchi. Niliona kwamba ujumbe huu utafungwa kwa nguvu na nguvu ukizidi sana kilio cha usiku wa manane. **{SRSw 400.2}**

Watumishi wa Mungu, waliojaliwa uwezo kutoka juu, na nyuso zao zikiwa zimeng'aa, na kung'aa kwa kuwekwa wakfu, wakatoka kutangaza ujumbe kutoka mbinguni. Nafsi ambazo zilitawanyika katika mifumo yote ya kidini ziliitikia wito huo, na wale wa thamani walitolewa haraka kutoka kwa makanisa yaliyoangamizwa, kwa kuwa Luti aliharakishwa kutoka Sodoma kabla ya kuangamizwa kwake. Watu wa Mungu waliimarishwa na utukufu ulio bora ambao ulikaa juu yao kwa wingi na kuwatayarisha kuvumilia saa ya majaribu. Nilisikia kila mahali sauti nyingi zikisema, ***"Hapa ndipo penye subira ya watakatifu, hao wazishikao amri za Mungu, na imani ya Yesu." Ufunuo 14:12.*** **{SRSw 401.1}**

SURA YA 59—KUFUNGWA KWA MLANGO WA REHEMA

Nilielekezwa chini hadi wakati ambapo ujumbe wa malaika wa tatu ulikuwa unafungwa. Nguvu za Mungu zilikuwa zimekaa juu ya watu Wake; Walikuwa wamekamilisha kazi yao na walikuwa wamejitayarisha kwa saa iliyojaribu mbele yao. Walikuwa wamepokea mvua ya masika, au kuburudishwa na uwepo wa Bwana, na ushuhuda ulio hai ulikuwa umehuishwa. Onyo kuu la mwisho lilikuwa limesikika kila mahali, na lilikuwa limewachochea na kuwakasirisha wakaaji wa dunia ambao hawangepokea ujumbe. **{SRSw 402.1}**

Niliona malaika wakiharakisha huku na huko Mbinguni. Malaika aliye na kalamu ya wino kando yake alirudi kutoka duniani na kuripoti kwa Yesu kwamba kazi yake imefanywa, na watakatifu walihesabiwa na kutiwa muhuri. Kisha nikamwona Yesu, ambaye alikuwa akihudumu mbele ya safina iliyokuwa na Amri Kumi, akiitupa chini kwenye chetezo. Aliinua mikono Yake, na kwa sauti kubwa akasema, "Imekwisha." Na jeshi lote la malaika liliondoa taji zao kama Yesu alivyosema tamko zito, ***"Mwenye kudhulumu na azidi kudhulumu; na mwenye uchafu na azidi kuwa mchafu; na mwenye haki na azidi kufanya haki; na mtakatifu na azidi kutakaswa." Ufunuo 22:11.*** **{SRSw 402.2}**

Kila kesi ilikuwa imeamuliwa kwa maisha au kifo. Wakati Yesu alipokuwa akihudumu katika Patakatifu, hukumu ilikuwa ikiendelea kwa wafu wenye haki, na kisha kwa walio hai. Kristo alikuwa amepokea ufalme Wake, baada ya kufanya upatanisho kwa ajili ya watu Wake na kufuta dhambi zao. Raia wa ufalme walikuwa tayari. Ndoa ya mwana-kondoo ilifungwa. Na ufalme, na ukuu wa ufalme chini ya mbingu yote, ulitolewa kwa Yesu na warithi wa wokovu, na Yesu alipaswa kutawala kama Mfalme wa wafalme na Bwana wa mabwana. **{SRSw 402.3}**

Yesu alipotoka katika Patakatifu pa Patakatifu, nilisikia mlio wa kengele kwenye vazi Lake; na alipoondoka, wingu la giza lilifunika wakaaji wa dunia. Wakati huo hapakuwa na mpatanishi kati ya mtu

mwenye hatia na Mungu Mwenye aliyekosewa na Aliye na ghadhabu. Wakati Yesu alikuwa amesimama kati ya Mungu na mtu mwenye hatia, kulikuwa na kizuizi juu ya watu; Lakini alipotoka kati ya mwanadamu na Baba, kizuizi kiliondolewa na Shetani alikuwa na udhibiti kamili wa wale ambao hawakutubu. **{SRSw 403.1}**

Haikuwezekana kwa mapigo kumiminwa wakati Yesu akihudumu katika Patakatifu; Lakini kazi Yake inapokwisha, na maombezi Yake yanapofungwa, hakuna kitu cha kuzuia ghadhabu ya Mungu, na ghadhabu inapasuka kwa hasira juu ya kichwa kisicho na makazi cha mwenye dhambi mwenye hatia, ambaye amedharau wokovu na kuchukia karipio. Katika wakati huo wa kutisha, baada ya kufungwa kwa upatanishi wa Yesu, watakatifu walikuwa wakiishi machoni pa Mungu mtakatifu bila mwombezi-mpatanishi. Kila kesi iliamuliwa, kila kito kilihesabiwa. Yesu alikaa kwa muda katika nyumba ya nje ya Patakatifu pa mbinguni, na dhambi ambazo zilikuwa zimeungamwa alipokuwa katika mahali Patakatifu Pa patakatifu ziliwekwa juu ya Shetani, mwanzilishi wa dhambi, ambaye lazima apate adhabu yao. [Kumbuka.—Mateso haya ya Shetani si kwa maana yoyote ya upatanisho wa urithi. Kama inavyoonyeshwa katika sura iliyotangulia: “Kama mbadala wa mwanadamu na mdhamini, uovu wa wanadamu uliwekwa juu ya Kristo.” (Ona uk. 225.) Lakini baada ya wale wanaokubali dhabihu ya Kristo kukombolewa, hakika ni kwamba Shetani, mwanzilishi wa dhambi, anapaswa kupata adhabu ya mwisho. Kama alivyosema Ellen White “Uovu ambao amewafanya waufanye.”—The Great Controversy, 658.—Wakusanyaji.] **{SRSw 403.2}**

Umechelewa Sana! Umechelewa Sana!

Kisha nikamwona Yesu akivua mavazi Yake ya kikuhani na kujivika mavazi Yake ya kifalme. Juu ya kichwa Chake kulikuwa na taji nyingi, taji ndani ya taji. Akiwa amezungukwa na jeshi la malaika, aliondoka mbinguni. Mapigo yalikuwa yakiwaangukia wakaaji wa dunia. Wengine walikuwa wakimshutumu Mungu na kumlaani. Wengine walikimbilia kwa watu wa Mungu na kusihi sana wafundishwe jinsi wanavyoweza kuepuka hukumu Zake. Lakini watakatifu hawakuwa na chochote kwa ajili yao. Chozi la mwisho kwa wenye dhambi lilikuwa limemwagika, sala ya mwisho yenye uchungu imetolewa, mzigo wa mwisho umebebwa, onyo la mwisho limetolewa. Hapakuwa tena na sauti tamu ya rehema ya kuwaalika. Wakati watakatifu na mbingu yote walipokuwa na hamu ya wokovu wao, wao hawakuwa na hamu kwa ajili yao wenyewe. Uzima na kifo vilikuwa vimewekwa mbele yao. Wengi walitamani uzima, lakini hawakufanya juhudi kuupata. Hawakuchagua uzima, na sasa hapakuwa na damu ya upatanisho ya kuwasafisha wenye hatia, hakuna Mwokozi mwenye huruma kuwasihi na kulia, “Okoa, mrehemu, mwenye dhambi kwa kumpa muda mrefu zaidi.” Mbingu zote zilikuwa zimeungana na Yesu, waliposikia maneno ya kutisha, “Imekwisha. Imekwisha.” Mpango wa wokovu ulikuwa umetimizwa, lakini ni wachache waliokuwa wamechagua kuukubali. Na sauti tamu ya rehema ilipotoweka, woga na hofu viliwashika waovu. Kwa utofauti wa kutisha walisikia maneno, "Umechelewa sana! Umechelewa sana!" **{SRSw 404.1}**

Wale ambao hawakuwa wamelithamini Neno la Mungu walikuwa wakiharakisha huku na huko, wakimangamanga kutoka bahari hadi bahari, na kutoka kaskazini hadi mashariki, kutafuta Neno la Bwana. Malaika akasema, “Hawatalipata. Kuna njaa katika nchi; sio njaa ya chakula, wala kiu ya maji, bali kwa ajili ya kusikia maneno ya Bwana.

Kiu siku baada ya siku wamedharau wokovu, wakithamini utajiri wa kidunia na starehe za kidunia kuliko hazina yoyote ya mbinguni au kishawishi. Wachafu lazima wabaki wachafu milele. "Wamemkataa Yesu na kuwadharau watakatifu Wake. Aliye mchafu na aendelee kuwa mchafu milele." **{SRSw 404.2}**

Wengi wa waovu walikasirika sana walipopata madhara ya tauni. Ilikuwa ni eneo la uchungu wa kutisha. Wazazi walikuwa wakiwalaumu sana watoto wao, na watoto wazazi wao, ndugu zao, na dada zao, na dada zao. Vilio vikali, na mayowe yalisikika kila upande, “Ni wewe uliyenizuia kupokea Ukweli ambao ungeniokoa na saa hii ya kutisha.” Watu waliwageukia wachungaji wao kwa chuki kali na kuwakemea, wakisema, “Ninyi hamkutuonya. Mlisema dunia yote itaongoka, mkasema amani, amani, mkituliza hofu zetu. Hamkutueleza kuhusu saa hii.” Na wale waliowatahadharisha mliwaita watu shupavu waliopitiliza na waovu. Lakini niliona kwamba wachungaji hawakuepuka ghadhabu ya Mungu. Mateso yao yalikuwa makubwa mara kumi kuliko yale ya washiriki wao. **{SRSw 405.1}**

SURA YA 60—WAKATI WA TAABU YA YAKOBO

Niliona watakatifu wakiondoka mijini na vijijini, na kushirikiana pamoja katika makundi, na kuishi katika sehemu za upweke zaidi. Malaika waliwapa chakula na maji, huku waovu wakiteseka kwa njaa na kiu. Kisha nikaona watu wakuu wa dunia wakishauriana pamoja, na Shetani na malaika zake wakiwa na shughuli nyingi karibu nao. Niliona maandishi, ambayo nakala zake zilitawanyika katika sehemu mbalimbali za nchi, zikitoa amri kwamba pasipo watakatifu kubadili imani yao ya kipekee, waache Sabato na kushika siku ya kwanza ya juma, watu watakuwa huru, baada ya muda fulani, kuwaua. Lakini katika saa hii ya majaribu watakatifu walikuwa watulivu na wakijithibiti nafsi zao vyema, wakimtumaini Mungu na kuegemea juu ya ahadi Yake kwamba njia ya kutoroka ingefanywa kwa ajili yao. **{SRSw 406.1}**

Katika baadhi ya maeneo, kabla ya muda wa kutekelezwa kwa amri hiyo, waovu walikimbilia kuwashambulia watakatifu ili kuwaua; lakini malaika katika umbo la wanajeshi waliwapigania. Shetani alitamani kupata ruhusa ya kuwaangamiza watakatifu wa Aliye Juu, lakini Yesu aliwaamuru malaika Wake kuwachunga. Mungu ataheshimiwa kwa kufanya Agano na wale waliolishika sheria Yake, mbele ya mataifa yaliyo karibu nao; na Yesu ataheshimiwa kwa kuwabadilisha na kuwachukua mbinguni, bila wao kuona mauti, wale waaminifu waliokuwa wakisubiri na waliomtarajia kwa muda mrefu. **{SRSw 406.2}**

Punde nikaona watakatifu wakiteseka sana kiakili. Walionekana kuzungukwa na wakaaji waovu wa dunia. Kila mwonekano ulikuwa dhidi yao. Wengine walianza kuogopa kwamba hatimaye Mungu aliwaacha waangamie kwa mkono wa waovu. Lakini kama macho yao

yangeweza kufunguliwa, wangejiona wamezungukwa na malaika wa Mungu. Kisha ukaja umati wa waovu wenye hasira, na umati wa malaika waovu uliofuata, wakiharakisha juu ya waovu kuwaua watakatifu. Lakini kabla hawajafika kwa watu wa Mungu, waovu walipaswa kwanza wapite katikati ya kundi hili la malaika wenye nguvu na watakatifu**.** Hii ilikuwa haiwezekani. Malaika wa Mungu walikuwa wakiwafanya warudi nyuma na pia kuwafanya malaika waovu waliokuwa wakiwakandamiza kuanguka nyuma. **{SRSw 407.1}**

Kilio cha Ukombozi

Ilikuwa ni saa moja ya uchungu wa kutisha, wa kutisha kwa watakatifu. Mchana na usiku walimlilia Mungu kwa ajili ya ukombozi. Kwa mwonekano wa nje, hakukuwa na uwezekano wa kutoroka. Mwovu alikuwa tayari ameanza kushinda, akipiga kelele, "Kwa nini Mungu wako hakuokoi kutoka kwenye mikono yetu? Kwa nini usiende juu na kuokoa maisha yako?" Lakini watakatifu hawakuyawekea umakini maneno hayo. Kama Yakobo, walikuwa wakipigana mieleka na Mungu. Malaika walitamani kuwakomboa, lakini lazima wangojee kwa muda mrefu zaidi; Watu wa Mungu lazima wanywee kikombe na wabatizwe kwa ubatizo. Malaika, wakiwa waaminifu kwa amana yao, waliendelea kukesha. Mungu hangeruhusu Jina Lake litukanwe kati ya wapagani. Wakati ulikuwa karibu kufika ambapo alipaswa kudhihirisha uwezo Wake mkuu na kuwakomboa watakatifu Wake kwa utukufu. Kwa ajili ya utukufu wa Jina Lake, Yeye angemwokoa kila mmoja wa wale waliomngoja kwa subira na ambao majina yao yaliandikwa katika kitabu. **{SRSw 407.2}**

Nilielekezwa nyuma kwa Nuhu mwaminifu. Mvua iliponyesha na gharika ikaja, Nuhu na familia yake walikuwa wameingia ndani ya safina, na Mungu akawafungia ndani. Nuhu alikuwa amewaonya kwa uaminifu wakaaji wa ulimwengu wa kabla ya gharika, wakati wao

walikuwa wamemdhihaki na kumkejeli. Na maji yaliposhuka juu ya nchi, na mmoja baada ya mwingine alikuwa akizama, waliiona ile safina, ambayo walikuwa wameifanyia mchezo mwingi sana, ikiendelea salama juu ya maji, ikimhifadhi Nuhu mwaminifu na familia yake. Kwa hiyo nikaona kwamba watu wa Mungu, ambao walikuwa wameuonya ulimwengu kwa uaminifu juu ya ghadhabu yake inayokuja, wangekombolewa. Mungu hangewaruhusu waovu kuwaangamiza wale waliokuwa wakitarajia unyakuo na ambao hawangesujudia amri ya mnyama au kupokea alama yake. Niliona kwamba ikiwa waovu wangeruhusiwa kuwaua watakatifu, Shetani na jeshi lake baya, na wote wanaomchukia Mungu, wangeridhika. Na oooh, ingekuwa ushindi wa hali ya juu ulioje kwa Ukuu wake wa Kishetani kuwa na nguvu, katika pambano la mwisho, juu ya wale ambao walikuwa wamengoja kwa muda mrefu kumtazama Yeye ambaye walimpenda! Wale ambao wamekejeli wazo la watakatifu kupanda juu watashuhudia utunzaji wa Mungu kwa watu Wake na kuona ukombozi wao kwa utukufu. **{SRSw 407.3}**

Watakatifu walipoondoka katika miji na vijiji, walifuatwa na waovu, ambao walitaka kuwaua. Lakini panga zilizoinuliwa ili kuua watu wa Mungu zilivunjika na kuanguka bila, zikakosa nguvu kama majani. Malaika wa Mungu waliwalinda watakatifu. Walipokuwa wakilia mchana na usiku kwa ajili ya ukombozi, kilio chao kilikuja mbele za Bwana. **{SRSw 408.1}**

SURA YA 61—UKOMBOZI WA WATAKATIFU

Mungu alichagua kuwakomboa watu Wake katika usiku wa manane ambapo. Waovu walipokuwa wakiwadhihaki, ghafla jua lilitokea, likiangaza kwa nguvu Zake, na mwezi ukasimama tuli. Waovu walitazama eneo lile kwa mshangao, huku watakatifu wakiangalia kwa furaha tele ishara za ukombozi wao. Ishara na maajabu vilifuatana kwa mfululizo wa haraka. Kila kitu kilionekana kuwa nje ya mkondo wake wa asili. Vijito vilikoma kutiririka. Mawingu meusi na mazito yalikuja na kugongana. Lakini palikuwa na sehemu moja ya utukufu iliyotulia, ambapo sauti ya Mungu ilitoka kama maji mengi, ikitikisa mbingu na nchi. Kulikuwa na tetemeko kubwa la ardhi. Makaburi yalifunguliwa, na wale waliokufa kwa imani chini ya ujumbe wa malaika wa tatu, wakiitunza Sabato, wakatoka katika vitanda vyao vyenye vumbi, wakitukuzwa, ili kusikia Agano la Amani ambalo Mungu angefanya na wale walioshika sheria Yake. **{SRSw 409.1}**

Anga lilifunguka na kufungwa na kulikuwa na machafuko. Milima ilitikisika kama mwanzi kwenye upepo na kutupa miamba iliyochakaa pande zote. Bahari ilichemka kama chungu na kutupa mawe juu ya nchi. Na Mungu aliponena siku na saa ya kuja kwa Yesu na kutoa Agano la Milele kwa watu Wake, alizungumza sentensi moja, kisha akatulia, wakati Maneno yakizunguka duniani. Israeli wa Mungu walisimama huku macho yao yakiwa yameelekezwa juu, wakisikiliza Maneno yalipokuwa yakitoka katika kinywa cha Yehova na kuzunguka-zunguka

katika nchi kama sauti mbambali za ngurumo kubwa zinazofuatana. Ilikuwa ya kusikitisha sana. Mwishoni mwa kila sentensi, Watakatifu walipiga kelele, “Utukufu! Haleluya!” Nyuso zao ziliangazwa kwa utukufu wa Mungu, na ziling'aa kwa utukufu kama uso wa Musa aliposhuka kutoka Sinai. Waovu hawakuweza kuwatazama kwa ajili ya utukufu. Na baraka isiyokoma ilipotamkwa kwa wale waliomheshimu Mungu katika kuitakasa Sabato Yake, palikuwa na sauti kuu ya ushindi juu ya mnyama na juu ya sanamu yake. **{SRSw 409.2}**

Kisha ilianza Yubile/Jubilee, wakati ambapo nchi ingepumzika. Niliona mtumwa mcha Mungu akiinuka kwa ushindi na furaha, akavunja minyororo iliyomfunga, huku bwana wake mwovu akiwa katika kuchanganyikiwa, hajui afanye nini, kwa maana waovu hawakuweza kuelewa maneno ya sauti ya Mungu. **{SRSw 410.1}**

Ujio wa Pili Wa Kristo

Mara likatokea wingu kubwa jeupe, ambalo juu yake aliketi Mwana wa Adamu. Lilipoanza kuonekana kwa mbali, wingu hilo lilionekana dogo sana. Malaika akasema kwamba ilikuwa ni ishara ya Mwana wa Adamu. Lilipokaribia dunia, tuliweza kuona utukufu na ukuu wa Yesu alipokuwa akija akiwa amepanda farasi ili kushinda. Msafara wa malaika watakatifu, wenye taji angavu, zinazometa vichwani mwao, walimsindikiza alipokuwa njiani kuja. Hakuna lugha inayoweza kueleza utukufu wa tukio hilo. Wingu la utukufu lisilo na kifani lilizidi kukaribia, na tukauona uso mzuri wa Yesu waziwazi. Kristo, Hakuvikwa taji ya miiba, bali taji ya utukufu ilikuwa juu ya kipaji Chake kitakatifu. **{SRSw 410.2}**

Hakuna lugha inayoweza kuelezea utukufu wa tukio. Wingu lililo hai la ukuu na utukufu usio na kifani ulikaribia zaidi, na tuliweza kuuuona kwa uwazi uso mzuri wa Yesu. Hakuvaa taji ya miiba, bali taji

ya utukufu ilikaa juu ya uso Wake mtakatifu. Juu ya vazi Lake na paji lilikuwa limeandikwa, Mfalme wa wafalme, na bwana wa mabwana. Uso Wake ulikuwa unang'aa kama jua la adhuhuri, macho Yake yalikuwa kama mwali wa moto, na miguu Yake ilikuwa na mwonekano wa shaba nzuri. Sauti Yake ilisikika kama vyombo vingi vya muziki. Nchi ilitetemeka mbele Yake, mbingu zikaondoka kama gombo linavyokunjwa, na kila mlima na kisiwa vikahamishwa kutoka mahali pake. ***"Na wafalme wa dunia, na wakuu, na majemadari, na matajiri, na wenye nguvu, na kila mtumwa, na mwungwana, wakajificha katika pango na chini ya miamba ya milima, wakiiambia milima na miamba, Tuangukieni, tusitirini, mbele za uso Wake Yeye aketiye juu ya kiti cha enzi, na hasira ya Mwana-Kondoo. Kwa maana siku iliyo kuu, ya hasira yao, imekuja; naye ni nani awezaye kusimama? Ufunuo 6:15-17.*** **{SRSw 410.3}**

Wale ambao muda mfupi uliopita wangewaangamiza watoto waaminifu wa Mungu kutoka duniani, sasa walishuhudia utukufu wa Mungu uliokuwa juu yao. Na katikati ya hofu yao yote walisikia sauti za watakatifu walio hai katika mikazo ya shangwe, wakisema, "***Tazama, Huyu Ndiye Mungu wetu, Ndiye tuliyemngoja atusaidie" Isaya 25:9.*** **{SRSw 411.1}**

Ufufuo wa kwanza Dunia

Dunia ilitikisika kwa nguvu wakati sauti ya Mwana wa Mungu ilipowaita watakatifu waliolala. Waliitikia wito huo na wakatoka makaburini wakiwa wamevikwa kutokufa kwa utukufu, wakipaza "Ushindi, ushindi, juu ya kifo na kaburi! Ku wapi, Ewe mauti, kushinda kwako? U wapi, Ewe mauti, uchungu wako? (Tazama 1 Wakorintho 15:55.) Kisha watakatifu walio hai na wale waliofufuka waliinua sauti zao katika shangwe ndefu ya ushindi wenye furaha isiyoelezeka. Miili iliyokuwa imeshuka kaburini ikiwa na alama za ugonjwa na mauti

ilitoka ikiwa katika afya na nguvu ya kutokufa. Watakatifu walio hai wanabadilishwa kwa muda mfupi, kwa kufumba na kufumbua, na kunyakuliwa na wale waliofufuka, na kwa pamoja wanakutana na Bwana wao angani. Jamani, ni mkutano mtukufu kama nini! Marafiki ambao kifo kilikuwa kimewatenganisha walikuwa wameungana, wa wasiachane tena milele. **{SRSw 411.2}**

Kila upande wa gari la mawingu kulikuwa na mbawa, na chini yake kulikuwa na magurudumu hai; Na gari lilipokuwa likipanda juu, magurudumu yalilia, “Mtakatifu,” na mbawa, zilipokuwa zikisogea, zililia, “Mtakatifu,” na kundi la malaika watakatifu kuzunguka wingu likalia, “Mtakatifu, mtakatifu, mtakatifu, Bwana Mungu Mwenyezi!” Na watakatifu katika wingu walilia, "Utukufu! Aleluya!" Na gari likapanda kwenda juu mpaka mji mtakatifu. Kabla ya kuingia jijini, watakatifu walipangwa katika umbo kamili la mraba, na Yesu akiwa katikati. Alisimama kichwa na mabega juu ya watakatifu na juu ya malaika. Umbo Lake lenye utukufu na uso Wake wa kupendeza ulionekana mbele za wote waliokuwa kwenye mraba. **{SRSw 412.1}**

SURA YA 62—TAJI KWA WATAKATIFU

Kisha nikaona idadi kubwa sana ya malaika wakileta kutoka katika jiji, taji tukufu—taji kwa kila mtakatifu, na jina lake likiwa limeandikwa juu yake. Yesu alipoyaita majina ya mhusika mwenye taji, malaika walimkabidhi, na kwa mkono Wake wa kuume Yesu mpendwa, aliweka taji juu ya vichwa vya watakatifu. Vivyo hivyo malaika walileta vinubi, na Yesu akawakabidhi watakatifu. Malaika kiongozi au mwenye amri kwanza walipiga noti hiyo, na kisha kila sauti ikapazwa kwa shukrani, sifa ya furaha, na kila mkono ulipiga kwa ustadi nyuzi za kinubi, ukitoa muziki wenye melodi ya kupendeza katika mikazo mingi na kamilifu. **{SRSw 413.1}**

Kisha nikamwona Yesu akiongoza kundi lililokombolewa hadi kwenye lango la jiji. Alilishika geti na kulirudisha nyuma kwenye bawaba zake zinazometa na kuamuru mataifa yaliyokuwa yameshika Ukweli yaingie ndani. Ndani ya jiji hilo kulikuwa na kila kitu cha kupendezesha macho na kuyafanya macho yawe na karamu. Utukufu mwingi na wa ajabu ulionekana kila mahali. Kisha Yesu akawaangalia watakatifu Wake waliokombolewa; nyuso zao zilikuwa zinang'aa kwa utukufu. Alipowatazama kwa macho Yake ya upendo, akasema kwa sauti Yake tamu na ya muziki: "Nimeona taabu ya nafsi yangu, na nimeridhika. Utukufu huu mkuu ni wako kufurahia milele. Huzuni zako zimekwisha. Hakutakuwa na kifo tena, wala huzuni wala kilio, wala maumivu hayatakuwapo tena. Niliona jeshi la waliokombolewa wakipiga magoti na kutupa taji zao zenye kung'aa miguuni pa Yesu, kisha mkono Wake wa kupendeza ukiwainua, wakagusa vinubi vyao vya

dhahabu na kujaza mbingu yote kwa muziki mtamu na nyimbo kwa Mwana-Kondoo. **{SRSw 413.2}**

Kisha nilimwona Yesu akiwapeleka watu Wake kwenye mti wa uzima, na tena tukasikia sauti Yake ya kupendeza, tamu kuliko muziki wowote uliowahi kusikika duniani, ikisema: “Majani ya mti huu ni kwa ajili ya kuponya mataifa. Kuleni ninyi yote.” Juu ya mti wa uzima kulikuwa na matunda mazuri sana, ambayo watakatifu waliweza kula kwa uhuru. Katika mji kulikuwa na kiti cha enzi cha utukufu sana, ambacho ulitoka mto safi wa maji ya uzima, ulio wazi kama kioo. Kando ya mto huo kulikuwa na mti wa uzima, na kando ya kingo za mto kulikuwa na miti mingine mizuri iliyokuwa na matunda mazuri kwa chakula. **{SRSw 414.1}**

Lugha ni dhaifu kabisa kujaribu kuelezea mbingu. Wakati tukio hili linajitokeza mbele yangu, ninashikwa na mshangao. Nikishindwa na utukufu wake wa kupita kiasi na fahari ya ajabu, ninaweka kalamu yangu chini na kusema: “Jamani ni upendo ulioje! upendo wa ajabu ulioje!” Lugha ya juu kabisa kwa misamiati inashindwa kueleza utukufu wa mbingu wala kina kisichoelezeka cha upendo wa Mwokozi. **{SRSw 414.2}**

SURA YA 63—MILENIA

Nilikielekeza tena macho yangu duniani. Waovu walikuwa wameangamizwa, na maiti zao zilikuwa zimelala juu ya uso wa dunia. Ghadhabu ya Mungu katika mapigo saba ya mwisho ilikuwa imewajilia wakazi wa dunia, kiasi kwamba walijitafuna ndimi zao kwa maumivu na kumlaani Mungu. Wachungaji wa uongo walikuwa walengwa wakuu wa ghadhabu ya Yehova. Macho yao yalikuwa yameteketea ndani ya matundu yao, na ndimi zao ziliyeyuka vinywani mwao, huku wakiwa wamesimama kwa miguu yao. Baada ya watakatifu kutolewa kwa sauti ya Mungu, umati wa watu waovu waligeuza hasira yao juu ya mtu mwingine. Dunia ilionekana kufunikwa na damu, na maiti zilionekana kutoka mwisho mmoja, hadi mwingine. **{SRSw 415.1}**

Dunia ilionekana kama nyika isiyo na watu. Miji na vijiji, vilivyotikiswa na tetemeko la ardhi, vililala kwenye lundo. Milima ilikuwa imehamishwa kutoka mahali pake, na kuacha mapango makubwa. Miamba chakavu, iliyotupwa nje na bahari, au kung'olewa kutoka kwa ardhi yenyewe, ilitawanyika juu ya uso wake. Miti mikubwa ilikuwa imeng'olewa na kutawanyika juu ya ardhi. Hapa ndipo itakuwa makazi ya Shetani pamoja na malaika wake waovu kwa miaka elfu moja. Hapa adui atafungwa, akizunguka juu ya uso wa dunia uliovunjika na

kuona matokeo ya uasi wake dhidi ya sheria ya Mungu. Kwa miaka elfu moja atapata nafasi ya kufurahia matunda ya laana aliyosababisha. **{SRSw 415.2}**

Akiwa amewekewa mipaka akae duniani peke yake, hatakuwa na fursa ya kwenda sayari nyingine, kuwajaribu na kuwaudhi wale ambao hawajaanguka. Wakati huu Shetani atakuwa anateseka sana. Tangu kuanguka kwake sifa zake mbaya zimekuwa katika mazoezi ya mara kwa mara. Lakini basi atanyimwa uwezo wake na kuachwa kutafakari juu ya sehemu ambayo ametenda tangu anguko lake, na kutazamia kwa kutetemeka na hofu kwa siku zijazo za kutisha, wakati ambapo lazima ateseke kwa uovu wote aliofanya na kuadhibiwa kwa dhambi zote alizozifanya. **{SRSw 416.1}**

Nilisikia kelele za ushindi kutoka kwa malaika na kutoka kwa watakatifu waliokombolewa ambazo zilisikika kama ala elfu kumi za muziki, kwa sababu hawakupaswa kuudhiwa na kujaribiwa na Shetani na kwa sababu wakaaji wa walimwengu wengine walikombolewa kutoka kwa uwepo wake na majaribu yake. **{SRSw 416.2}**

Kisha nikaona viti vya enzi, na Yesu na watakatifu waliokombolewa wakaketi juu yao; Na watakatifu walitawala kama wafalme na makuhani kwa Mungu. Kristo, akiwa pamoja na watu Wake, alihukumu wafu waovu, akilinganisha matendo yao na Kitabu cha Sheria—Neno la Mungu—na kuamua kila kesi kulingana na matendo yao walipokuwa hai. Kisha wakawapa waovu adhabu waliyostahili kulingana na matendo yao; na hilo likaandikwa dhidi ya majina yao katika kitabu cha mauti. Shetani pia na malaika zake walihukumiwa na Yesu na watakatifu. Adhabu ya Shetani ilipaswa kuwa kubwa zaidi kuliko ile ya wale ambao alikuwa amewadanganya. Mateso yake hadi sasa yangezidi yao kiasi cha kutoweza kulinganishwa nayo. Baada ya

wale wote aliokuwa amewadanganya kuangamia, Shetani bado alipaswa kuishi na kuteseka kwa muda mrefu zaidi. **{SRSw 416.3}**

Baada ya hukumu ya wafu waovu kukamilika, mwishoni mwa miaka elfu moja, Yesu aliondoka katika jiji hilo, na msafara wa jeshi la watakatifu na la malaika likamfuata. Yesu alishuka juu ya mlima mkubwa, ambao, mara tu miguu yake ilipougusa, uligawanyika na kuwa tambarare kubwa. Kisha tukatazama juu na kuuona ule mji mkubwa na mzuri, wenye misingi kumi na miwili na milango kumi na miwili, mitatu kila upande, na malaika kwenye kila lango. Tukapiga kelele, “Mji! Mji mkuu! Unashuka kutoka kwa Mungu kutoka mbinguni!” Nao ulishuka katika fahari yake yote na utukufu unaong'aa, na kukaa katika uwanda wenye nguvu ambao Yesu alikuwa ameutayarisha kwa ajili yake. **{SRSw 416.4}**

SURA YA 64—UFUFUO WA PILI

Kisha Yesu na msafara wote wa Malaika Watakatifu, na Watakatifu wote waliotajwa, waliondoka jijini. Malaika walimzunguka kiongozi wao na kumsindikiza njiani, na msururu wa watakatifu waliokombolewa ukafuata. Kisha, kwa utukufu wa kutisha na wa ajabu, Yesu aliwaita wafu waovu; nao wakafufuka wakiwa na miili ile ile dhaifu na yenye ugonjwa waliyoingia nayo kaburini. Ni tukio la kushangaza namna gani! Ni mandhari ya kutisha! Katika ufufuo wa kwanza wote walitokea wakiwa na uzima wa kutokufa na utukufu, lakini katika ufufuo wa pili alama za laana zilionekana kwa wote. Wafalme na wakuu wa dunia, wa hali ya chini na wa vyeo vya juu, wasomi na wasio na elimu, wote wakatokea pamoja. Wote wakamwona Mwana wa Adamu; na wale wale waliomdharau na kumdhihaki, waliomwekea taji ya miiba kichwani na kumpiga kwa mwanzi, wakamwona katika utukufu Wake wa kifalme. Wale waliomtemea mate alipokuwa akihukumiwa sasa wakageuza uso wao kutoka katika mtazamo Wake wa kupenya na kutoka katika utukufu wa uso wWake. Wale waliopigilia misumari kwenye mikono na miguu Yake sasa wanatazama alama za kusulubiwa Kwake. Wale waliotupia mkuki ubavuni Mwake wanaona alama za ukatili wao juu ya mwili Wake. Na wanajua kwamba Yeye Ndiye Yule Yule waliyemsulubisha na kumdhihaki katika uchungu wake alipokuwa anakata roho. Na kisha kunatokea kilio kimoja cha muda mrefu cha uchungu, huku wakikimbia kujificha kutoka kwenye uwepo wa Mfalme wa wafalme na Bwana wa mabwana. **{SRSw 418.1}**

Wote wanatafuta kujificha kwenye miamba, ili kujikinga na utukufu wa kutisha wa Yule ambaye walimdharau huko nyuma. Na, wakiwa wamezidiwa na kuumizwa na ukuu Wake na utukufu mwingi, wao kwa nia moja wanapaza sauti zao, na kwa uwazi wa kutisha, "Amebarikiwa Yeye Ajaye kwa Jina la Bwana!" **{SRSw 419.1}**

Kisha Yesu na malaika watakatifu, wakifuatana na watakatifu wote, wanakwenda tena mjini, na maombolezo makali na vilio vya waovu walioangamizwa vinajaa hewani. Kisha nikaona kwamba Shetani alianza tena kazi yake. Alipita kati ya raia wake na kuwafanya walio dhaifu kuwa na nguvu, na kuwaambia kwamba yeye na malaika zake wana nguvu. Aliwaelekeza kwa mamilioni waliokuwa wamefufuliwa. Kulikuwa na wapiganaji hodari na wafalme ambao walikuwa na ujuzi wa kutosha katika vita na ambao walikuwa wameshinda falme. Na kulikuwa na majitu yenye nguvu na watu mashujaa ambao hawakuwahi kushindwa vita. Kulikuwa na Napoleon mwenye kiburi, mwenye matamanio y aukuu, ambaye mbinu yake ilikuwa imesababisha falme kutetemeka. Walisimama watu wa kimo cha juu na wenye wenye heshima, ambao walikuwa wameanguka vitani huku wakiwa na kiu ya kushinda. **{SRSw 419.2}**

Walipofufuka kutoka makaburini mwao, waliendeleza mawazo yao pale yalipoishia walipokufa. Walibeba tamaa zile zile za ushindi walizokuwa nazo walipokufa. Shetani anashauriana na malaika zake, na kisha na wale wafalme na washindi na watu wenye nguvu. Kisha analitazama jeshi kubwa, na kuwaambia kwamba kundi la jiji ni dogo na dhaifu, na kwamba wanaweza kupanda na kulichukua, na kuwafukuza wakaaji wake, na kumiliki mali na utukufu Wake wenyewe. **{SRSw 419.3}**

Shetani anafanikiwa kuwadanganya, na wote mara moja wanaanza kujitayarisha kwa ajili ya vita. Kuna watu wengi wenye ujuzi katika

jeshi hilo kubwa, na wanaunda kila aina ya zana za vita. Kisha Shetani akiwa kiongozi wao, umati huo wa watu unasonga mbele. Wafalme na wapiganaji hufuata kwa karibu baada ya Shetani, na umati unafuata katika makundi. Kila kundi lilikuwa na kiongozi wake, na utaratibu ulizingatiwa walipokuwa wakimachi juu ya dunia iliyoharibiwa kuelekea Mji Mtakatifu-wakipiga gwaride. Yesu anafunga milango ya jiji, na jeshi hili kubwa linaizunguka, na kujiweka katika safu ya vita, wakitarajia mapambano makali. **{SRSw 419.4}**

SURA YA 65—KUTAWAZWA KWA KRISTO

Sasa Kristo anaonekana tena mbele ya maadui Zake. Juu kabisa ya mji, juu ya msingi wa dhahabu iliyosafishwa, kuna kiti cha enzi kilichoinuliwa juu na kilicho tukufu. Kwenye kiti hicho ameketi Mwana wa Mungu, na karibu Naye wapo raia wa ufalme Wake. Nguvu na ukuu wa Kristo hakuna lugha inayoweza kuueleza, wala kalamu kuuelezea. Utukufu wa Baba wa Milele unamfunika Mwana Wake. Mwangaza wa uwepo Wake unajaza mji wa Mungu na kusambaa nje ya malango, ukifurika dunia yote kwa nuru Yake. **{SRSw 421.1}**

Karibu na kiti cha enzi ni wale ambao hapo awali walikuwa na bidii katika kazi ya Shetani, lakini ambao, walinyakuliwa kama kijinga au chuma kutoka motoni, wamemfuata Mwokozi wao kwa upendo wa kina na wa dhati. Kisha wanakuja wale waliokamilisha tabia ya Kikristo katikati ya uongo na upotovu, walioiheshimu sheria ya Mungu wakati ulimwengu wa Kikristo ulipotangaza kuwa imebatilishwa, na mamilioni wa kila kizazi waliouawa kwa ajili ya imani yao. Na zaidi ya hayo ni "***mkutano mkubwa sana ambao hapana mtu awezaye kuuhesabu, watu wa kila taifa, na kabila, na jamaa, na lugha, wamesimama mbele ya kile kiti cha enzi, na mbele za Mwana-Kondoo, wamevikwa mavazi meupe, wana matawi ya mitende mikononi mwao." Ufunuo 7:9.*** Vita vyao vimeisha, ushindi wao umenyakuliwa. Wamevipiga vita na kufikia tuzo. Tawi la mitende mikononi mwao ni ishara ya ushindi wao, vazi jeupe ni nembo ya haki isiyo na doa ya Kristo, ambayo sasa ni yao. **{SRSw 421.2}**

Waliokombolewa huinua wimbo wa sifa unaorudia na kusikika tena kupitia vyumba vya mbinguni, ***"Wokovu una Mungu wetu aketiye katika kiti cha enzi, na Mwana-Kondoo Ufunuo wa Yohana 7:10."*** Na Malaika na Serafi wanaunganisha sauti zao kwa kuabudu. Kama vile waliokombolewa wameona nguvu na uovu wa Shetani, wameona, kuliko wakati mwingine wowote, kwamba hakuna uwezo ila ule wa Kristo ungeweza kuwafanya washindi. Katika umati huo wote unaong'aa hakuna wa kumpa sifa kwa kuwapatia wokovu kwao wenyewe, kana kwamba wameshinda kwa uwezo wao wenyewe na wema wao. Hakuna kinachosemwa juu ya yale waliyofanya au kuteseka; Lakini mzigo wa kila wimbo, neno kuu la kila wimbo, ni, "***"Wokovu una Mungu wetu aketiye katika kiti cha enzi, na Mwana-Kondoo Ufunuo wa Yohana 7:10."*** **{SRSw 422.1}**

Mbele ya wakaaji waliokusanyika wa dunia na mbingu hufanyika kutawazwa kwa mwisho kwa Mwana wa Mungu. Na sasa, akiwa amewekeza kwa ukuu na uwezo mkuu, Mfalme wa wafalme anatoa hukumu juu ya waasi dhidi ya serikali Yake, na kutekeleza haki juu ya wale ambao wamevunja sheria Yake na kuwakandamiza watu Wake. Nabii wa Mungu asema hivi: ***"Kisha nikaona kiti cha enzi, kikubwa, cheupe, na Yeye aketiye juu yake; ambaye nchi na mbingu zikakimbia uso Wake, na mahali pao hapakuonekana. Nikawaona wafu, wakubwa kwa wadogo, wamesimama mbele ya hicho kiti cha enzi; na vitabu vikafunguliwa; na kitabu kingine kikafunguliwa, ambacho ni cha uzima; na hao wafu wakahukumiwa katika mambo hayo yaliyoandikwa katika vile vitabu, sawasawa na matendo yao." Ufunuo 20:11, 12.*** **{SRSw 422.2}**

Mara tu vitabu vya kumbukumbu vinapofunguliwa, na jicho la Yesu linawatazama waovu, wanatambua kila dhambi ambayo wamewahi kufanya. Wanaona pale ambapo miguu yao ilijitenga na njia

ya usafi na utakatifu, jinsi kiburi na uasi vimewabeba katika uvunjaji wa sheria ya Mungu. Majaribu yaliyowavutia ambayo walijipa moyo kwa kujiingiza katika dhambi, baraka zilipotoshwa, mawimbi ya rehema yaliyorudishwa nyuma na moyo mkaidi, usiotubu—yote yanaonekana kana kwamba yameandikwa kwa herufi za moto. **{SRSw 422.3}**

Sinema ya Pambano Kuu

Juu ya kiti cha enzi unaonekana msalaba; na kama picha ya mandhari ya mfululizo yaani panorama, yanaonekana matukio ya jaribu na anguko la Adamu, pamoja na hatua zote zinazofuatana za mpango mkuu wa ukombozi. Kuzaliwa kwa Mwokozi kwa unyenyekevu; maisha Yake ya utoto ya usahili na utii; ubatizo Wake katika Yordani; kufunga na kujaribiwa nyikani; huduma Yake ya hadharani, ikifunua kwa wanadamu baraka za thamani zaidi za mbinguni; siku zilizojazwa na matendo ya upendo na rehema, usiku wa maombi na kukesha katika upweke wa milima; mipango ya husuda, chuki na uovu uliolipizwa kwa wema Wake; uchungu wa ajabu na wa kutisha katika Gethsemane, chini ya mzigo mzito wa dhambi za ulimwengu wote; kusalitiwa Kwake mikononi mwa umati wa wauaji; matukio ya kutisha ya usiku ule wa huzuni: Mfungwa asiyepinga, aliyetelekezwa na wanafunzi Wake waliompenda zaidi, akipelekwa kwa jeuri kupitia mitaa ya Yerusalemu; Mwana wa Mungu akionyeshwa kwa dhihaka mbele ya Anasi, akihukumiwa katika jumba la kuhani mkuu, katika mahakama ya Pilato, mbele ya Herode mwoga na katili, akidhihakiwa, akitukanwa, akiteswa, na kuhukumiwa kufa—yote yanaonyeshwa kwa uwazi mkubwa. **{SRSw 423.1}**

Na sasa mbele ya umati unaoyumbayumba kwa kutikiswa, yanafunuliwa matukio ya mwisho: Mteswa mvumilivu akitembea njia ya

Kalvari; Mfalme wa mbinguni akining'inia msalabani; makuhani wenye kiburi na umati wa watu wenye kejeli wakidhihaki uchungu wake wa kufa; giza lisilo la kawaida; tetemeko la dunia, miamba iliyopasuka, makaburi yaliyofunguka—yote yakiashiria wakati ambapo Mkombozi wa ulimwengu alikata roho. **{SRSw 423.2}**

Mandhari hiyo ya kutisha inaonekana kama ilivyokuwa. Shetani, malaika wake, na wafuasi wake hawana uwezo wa kugeuka au kuondoka kwenye picha ya kazi yao wenyewe. Kila mhusika anakumbuka sehemu aliyoshiriki. Herode, aliyewaua watoto wasio na hatia wa Bethlehemu ili amwangamize Mfalme wa Israeli; Herodia mbaya, ambaye juu ya nafsi yake yenye hatia ipo damu ya Yohana Mbatizaji; Pilato asiye na msimamo, aliyekuwa dhaifu na mwenye kujipendekeza; askari waliodhihaki; makuhani na viongozi, pamoja na umati uliopagawa uliopiga kelele, "Damu Yake na iwe juu yetu na juu ya watoto wetu"—wote wanaona ukubwa wa hatia yao. Wanajaribu bure kujificha kutoka kwa utukufu wa uso Wake wa Kiungu unaong'aa zaidi kuliko mwangaza wa jua ila ni kazi bure, wakati waliokombolewa wanatupa taji zao mbele ya Mwokozi wakisema, "Alikufa kwa ajili yangu!" **{SRSw 424.1}**

Miongoni mwa umati wa waliokombolewa wapo mitume wa Kristo, Paulo jasiri, Petro mwenye ari, Yohana aliyependwa na mwenye upendo, na ndugu zao waaminifu; pamoja na umati mkubwa wa wafia-imani. Wakati nje ya kuta, pamoja na kila kitu kichafu na cha kuchukiza, wapo wale waliowatesa, kuwafunga gerezani, na kuwaua. Humo pia yupo Nero, yule zimwi wa ukatili na uasherati, akiona furaha na utukufu wa wale aliowatesa zamani na katika mateso yao makali zaidi alifurahia kwa nguvu za kishetani. Mama yake yumo hapo pia kushuhudia matokeo ya kazi yake mwenyewe; kuona jinsi alivyomwacha mwanawe athari mbaya ya tabia, na jinsi tamaa mbaya zilivyokuzwa kupitia

ushawishi na mfano wake zilivyozaa matunda ya uhalifu ambao ulisababisha ulimwengu kutetemeka. **{SRSw 424.2}**

Wapo mapapa wenye kiburi waliojiinua juu ya Mungu na kudhania kubadilisha sheria ya Aliye Juu. Kwa kuchelewa sana wanaona kwamba Yeye Ajuaye yote ana wivu juu ya sheria Yake, na kwamba hatamhesabia haki mtu mwenye hatia. Sasa wanatambua kwamba Kristo huunganisha maslahi Yake na yale ya watu Wake wanaoteseka; na wanahisi nguvu ya maneno Yake mwenyewe: Kuna mapadre wa Kipapa na maaskofu, ambao walidai kuwa mabalozi wa Kristo, lakini walitumia mateso, gereza la kifungo, na kuchomea moto (stake) ili kudhibiti dhamiri za watu wa Mungu. shimo, Kuna mapapa wenye kiburi waliojiinua juu ya Mungu na kudhania kubadili sheria ya Aliye Juu. Wale waliojifanya kuwa "mababa wa kanisa" watawajibika mbele ya Mungu kwa yale yote na watatoa hesabu, ijapokuwa watajaribu kuepuka uwajibikaji huo. Wakiwa wamechelewa sana kuona kwamba Yeye anayejua yote ana wivu juu ya sheria Yake, na kwamba Yeye hatamhesabia yeyote kuwa hana hatia kwa njia yoyote. Wanajifunza sasa kwamba Kristo anabainisha kupendezwa Kwake na yale ya watu Wake wanaoteseka; Nao wanahisi nguvu ya maneno Yake Mwenyewe, "***Kadiri mlivyomtendea mmojawapo wa hao ndugu zangu walio wadogo, mlinitendea Mimi." Mathayo 25:40.*** **{SRSw 424.3}**

Kwenye Kiti cha Hukumu

Ulimwengu wote wa waovu unasimama ukishtakiwa mbele ya kiti cha hukumu cha Mungu, kwa kosa la uhaini mkuu dhidi ya serikali ya mbinguni. Hawana mtetezi; hawana udhuru au kisingizio; na hukumu ya kifo cha milele inatolewa juu yao. **{SRSw 425.1}**

Sasa kwa wote inakuwa dhahiri kwamba mshahara wa dhambi si uhuru mtukufu wala uzima wa milele, bali ni utumwa, uharibifu, na

mauti. Waovu wanaona kile walichokikosa kwa maisha yao ya uasi. Utukufu ule wa milele ulio mkuu sana na wa thamani isiyopimika ulidharauliwa ulipowekwa mbele yao; lakini sasa unaonekana kuwa siyo kupendeza mno. "Yote haya," roho iliyopotea inalia, "ningeweza kuwa nayo, lakini nilichagua kuweka mambo haya mbali na mimi. Ee upumbavu wa ajabu na uzuri wa kufikirika tu! Nimebadilisha amani, furaha na heshima kwa taabu, fedheha na kukata tamaa.” Wote wanaona kwamba kutengwa kwao mbinguni ni haki. Katika maisha yao walitangaza: Hatutaki huyu Yesu atutawale. **{SRSw 425.2}**

Kama waliokuwa wamezama katika mshangao au njozi, waovu wameutazama kutawazwa kwa Mwana wa Mungu. Wanaona mikononi Mwake mbao za sheria ya Mungu, amri ambazo walizidharau na kuzivunja. Wanashuhudia mlipuko wa ajabu wa mshangao, furaha na ibada kutoka kwa waliokombolewa; na wimbi la wimbo linaposambaa juu ya umati ulio nje ya mji, wote kwa sauti moja wanapaza sauti “Ni makuu, na ya ajabu, matendo Yako, Ee Bwana Mungu Mwenyezi; Ni za haki, na za Kweli, njia Zako, Ee Mfalme wa mataifa.” (Ufunuo 15:3), Kisha wakianguka kifudifudi, wanamwabudu Mfalme wa uzima. **{SRSw 425.3}**

SURA YA 66—MAUTI YA PILI

Shetani anaonekana kupooza anapotazama utukufu na ukuu wa Kristo. Yeye ambaye hapo awali alikuwa kerubi anayefunika anakumbuka alikotoka. Serafi anayeng'aa, "Mwana wa Asubuhi"; Jinsi alivyobadilika, jinsi alivyoshushwa na kuhafifia! **{SRSw 427.1}**

Shetani anaona kwamba uasi wake wa hiari haujamfaa kwenda mbinguni. Amezoeza nguvu zake kupigana na Mungu waje; Usafi, amani, na maelewano ya mbinguni yangekuwa kwake mateso makubwa zaidi. Mashtaka yake dhidi ya rehema na haki ya Mungu sasa yamenyamazishwa. Adhabu ambayo amejitahidi kumtupia Yehova inakaa juu yake mwenyewe. Na sasa Shetani anainama chini na kukiri haki ya hukumu yake. **{SRSw 427.2}**

Kila swali la Ukweli na makosa katika mabishano ya muda mrefu linawekwa wazi. Haki ya Mungu imethibitishwa kikamilifu. Kabla ya ulimwengu wote kutolewa dhabihu kuu iliyotolewa na Baba na Mwana kwa niaba ya mwanadamu. Saa imefika ambapo Kristo anashika nafasi yake halali, na anatukuzwa juu ya enzi na mamlaka na kila jina linaloitwa. **{SRSw 427.3}**

Ijapokuwa Shetani amelazimishwa kukiri haki ya Mungu, na kuinamia ukuu wa Kristo, tabia yake bado haijabadilika. Roho ya uasi, kama mto wenye nguvu, inachipuka tena. Akiwa amejawa na wenda-wazimu, anaamua kutokubali kushindwa katika pambano hilo kuu. Wakati umefika wa mapambano ya mwisho ya kukata tamaa dhidi ya Mfalme wa mbinguni. Anakimbilia katikati ya raia wake na kujitahidi kuwatia moyo kwa ghadhabu yake mwenyewe na kuwaamsha kwenye vita vya papo hapo. Lakini kati ya mamilioni yasiyohesabika ambayo amewavutia katika uasi, hakuna sasa wa kukiri ukuu wake. Nguvu yake imefikia mwisho. Waovu wamejawa na chuki ile ile ya Mungu inayomtia jazba Shetani; Lakini wanaona kwamba kesi yao haina tumaini, kwamba hawawezi kumshinda Yehova. Hasira zao zimewashwa dhidi ya Shetani, na wale ambao wamekuwa mawakala wake katika udanganyifu. Kwa ghadhabu ya mapepo wanawageukia, na kunafuata tukio la ugomvi wa ulimwengu wote. **{SRSw 427.4}**

Moto Kutoka Mbinguni

Kisha yanatimizwa Maneno ya nabii: "***Maana Bwana ana ghadhabu juu ya mataifa yote, na hasira kali juu ya jeshi lao lote; amewaangamiza kabisa, amewatoa waende kuchinjwa. Isaya 34:2. "Awanyeshee wasio haki mitego, Moto na kiberiti na upepo wa hari, Na viwe fungu la kikombe chao." Zaburi 11:6***. Dunia inapasuka vipande-vipande. Silaha zilizofichwa ndani ya vilindi vyake zinatolewa. Miali ya moto inayomeza inatokea kutoka kila ufa unaofunguka. Miamba yenyewe inawaka moto. Siku imefika ambayo "itawaka kama tanuri." Malaki 4:1. Vitu vyote vya asili vinayeyuka kwa joto kali, na dunia pamoja na kazi zilizo ndani yake zinateketezwa. (2 Petro 3:10) Moto wa Tofeti umetayarishwa kwa ajili ya mfalme, mkuu wa uasi; Rundo lake ni la kina na kubwa, na **"Pumzi ya Bwana, kama mto wa kiberiti, huiwasha." Isaya 30:33.** Uso wa dunia unaonekana kuwa na

wingi wa kuyeyushwa—ziwa kubwa la moto linalowaka moto. Ni wakati wa hukumu na uharibifu wa watu wasiomcha Mungu— ***"Maana ni siku ya kisasi cha Bwana, mwaka wa malipo, ili kushindania Sayuni." Isaya 34:8.*** **{SRSw 428.1}**

Waovu wanapokea malipo yao duniani. "***Watakuwa makapi; na siku ile inayokuja itawateketeza, asema Bwana wa majeshi." Malaki 4:1***. Wengine wanaangamizwa ghafla, huku wengine wakiteseka kwa siku nyingi. Wote wanaadhibiwa kulingana na matendo yao. Dhambi za wenye haki zimehamishwa kwa Shetani, mwanzilishi wa uovu, ambaye lazima achukue adhabu yao. [Angalia maelezo ya chini uk. 403.] Hivyo anafanywa kuteseka, si kwa ajili ya uasi wake tu, bali kwa ajili ya dhambi zote alizowafanya watu wa Mungu kutenda. Adhabu yake inapaswa kuwa kubwa zaidi kuliko ile ya wale ambao amewadanganya. Baada ya yote kuangamia ambaye alianguka kwa udanganyifu wake, bado anapaswa kuishi na kuteseka. Katika moto huu wa utakaso, waovu wanaangamizwa hatimaye—mizizi na matawi: Shetani akiwa mzizi, wafuasi wake wakiwa matawi. Haki ya Mungu inaridhishwa, na watakatifu pamoja na jeshi lote la malaika, wanakiri kwa sauti kuu, Amina. **{SRSw 429.1}**

Wakati dunia imefunikwa na moto wa kisasi cha Mungu, waadilifu wanakaa salama katika Mji Mtakatifu. Kwa wale waliofufuliwa katika ufufuo wa kwanza, kifo cha pili hakina mamlaka juu yao. (Ufunuo 20:6). Wakati Mungu, kwa waovu ni moto ulao, kwa watu Wake, Yeye ni jua na ngao. (Zaburi 84:11). **{SRSw 429.2}**

SURA YA 67—DUNIA MPYA

"Kisha nikaona mbingu mpya na nchi mpya; kwa maana mbingu za kwanza na nchi ya kwanza zimekwisha kupita, wala hapana bahari tena." Ufunuo 21:1. Moto unaowaangamiza waovu huitakasa dunia. Kila alama ya laana imeondolewa kabisa. Hakutakuwa na Jehanamu inayowaka milele itakayowakumbusha wanadamu waliokombolewa matokeo ya kutisha ya dhambi. Kumbukumbu moja tu itabaki: Mkombozi wetu ataendelea kubeba alama za kusulubiwa Kwake. Juu ya kichwa Chake kilichojeruhiwa, na mikono na miguu yake, kuna alama pekee za kazi ya kikatili ambayo dhambi imetenda/imeweka. **{SRSw 430.1}**

"Na wewe, Ee mnara wa kundi, kilima cha binti Sayuni, utajiliwa; naam, mamlaka ya kwanza. "Mika 4:8. Ufalme uliopokonywa kwa dhambi, Kristo ameurejesha, na waliokombolewa wanapaswa kuumiliki pamoja Naye. "***Wenye haki watairithi nchi, Nao watakaa humo milele." Zaburi 37:29.*** Hofu ya kufanya urithi wa watakatifu uonekane kuwa wa kimwili sana umewafanya wengi kuzipunguza na kupotosha zile Kweli za Neno la Mungu kwa kuzifanya

baraka hizo zinazofundishwa za dunia mpya kama makazi yetu, kuonekana kama baraka za kiroho tunazifagilia mbali baraka za kimwili kama uzuri wa mandhari, maua, mito, vito, wanyama, kwa kukita kwenye baraka za kiroho peke yake *ili tusionekana kama watu tunaopenda vitu au mali sana. Kristo aliwahakikishia wanafunzi Wake kwamba alikwenda kuwatayarishia makazi kabambe-majumba haswa. Wale wanaokubali mafundisho ya Neno la Mungu hawatakuwa wajinga kabisa kuhusu makao ya mbinguni. Na bado Mtume Paulo anatangaza, ***"jicho halikuyaona wala sikio halikuyasikia, (Wala hayakuingia katika moyo wa mwanadamu,) Mambo ambayo Mungu aliwaandalia wampendao.1 Wakorintho 2:9.*** Lugha ya binadamu haitoshi kuelezea malipo/thawabu ya wenye haki. Itajulikana kwa wale tu wanaoitazama thawabu hiyo. Hakuna akili yenye ukomo, inayoweza kufahamu utukufu wa Paradiso ya Mungu (*A fear of making the saints' inheritance seem too material has led many to spiritualize away the very truths which lead us to look upon the new earth as our home.). **{SRSw 430.2}**

Katika Biblia, urithi wa waliokombolewa unaitwa nchi. **(Waebrania 11:14-16.)** Huko Mchungaji Mkuu huongoza kundi Lake kwenye chemchemi za maji ya uzima. Mti wa uzima hutoa matunda yake kila mwezi, na majani ya mti ni kwa ajili ya huduma ya mataifa. Kuna vijito vinavyotiririka kila mara, vilivyo wazi kama kioo, na kando yake miti inayopeperushwa hutupa vivuli vyake juu ya njia zilizotayarishwa kwa ajili ya kukombolewa kwa Bwana. **Huko tambarare pana zinainuka na kuwa vilima vya uzuri, na milima ya Mungu inainua vilele vyake vya juu. Juu ya tambarare hizo za amani, kando ya mito hiyo iliyo hai, watu wa Mungu, waliokuwa mahujaji na wasafiri kwa muda mrefu, watapata makao. {SRSw 431.1}**

Yerusalemu Mpya

Humo ndimo mna Yerusalemu Mpya, ***“wenye utukufu wa Mungu, na mwangaza wake ulikuwa mfano wa kito chenye thamani nyingi kama kito cha yaspi, safi kama bilauri” Ufunuo 21:11.*** Bwana asema, ***“Nami nitaufurahia Yerusalemu, nitawaonea shangwe watu Wangu” Isaya 65:19. “maskani ya Mungu ni pamoja na wanadamu, Naye atafanya maskani Yake pamoja nao, nao watakuwa watu Wake. Naye Mungu Mwenyewe atakuwa pamoja nao. Naye atafuta kila chozi katika macho yao, wala mauti haitakuwapo tena; wala maombolezo, wala kilio, wala maumivu hayatakuwapo tena; kwa kuwa mambo ya kwanza yamekwisha kupita." Ufunuo 21:3, 4.*** **{SRSw 431.2}**

Katika mji wa Mungu “hakutakuwa na usiku.” Hakuna atakayehitaji au kutamani kupumzika. Hakutakuwa na uchovu katika kufanya mapenzi ya Mungu na kutoa sifa kwa Jina Lake. Tutaanza kuhisi uchangamfu wa asubuhi, na tutakuwa mbali na mwisho wake. ***“wala hawana haja ya taa wala ya nuru ya jua; kwa kuwa Bwana Mungu huwatia nuru, nao watatawala hata milele na milele.” Ufunuo 22:5.*** Nuru ya jua itazidiwa na mwangaza ambao haupigi macho kwa uchungu na kutia kiwi, lakini unaozidi sana mwangaza wa adhuhuri yetu. Utukufu wa Mungu na wa Mwana-Kondoo huujaza mji mtakatifu kwa nuru isiyokoma. Waliokombolewa hutembea katika utukufu wa mwanga wa milele usio na jua. **{SRSw 431.3}**

“Nami sikuona hekalu ndani yake; kwa maana Bwana Mungu Mwenyezi na Mwana-Kondoo, ndio hekalu lake.” Ufunuo 21:22. Watu wa Mungu watapewa fursa ya kuwa na ushirika wa wazi na Baba na Mwana. Sasa ***"tunaona kwa kioo kwa jinsi ya fumbo." 1 Wakorintho 13:12.*** Sasa tunaona sura ya Mungu ikionyeshwa, kama katika kioo, katika kazi za asili na katika shughuli Zake na wanadamu; Lakini basi tutamwona uso kwa uso, bila pazia la giza katikati yetu. Tutasimama mbele Zake na kuutazama utukufu wa uso Wake. **{SRSw 432.1}**

Hapo akili zisizoweza kufa zitasoma kwa furaha isiyo na kikomo, furaha isiyoisha ya maajabu ya nguvu za ubunifu, mafumbo ya upendo wenye kukomboa. Hakutakuwa na adui mkatili wala mdanganyifu wa kutushawishi kumsahau Mungu. Kila kipawa na kitivyo cha akili kitakuzwa, kila uwezo utaongezwa. Kupata maarifa hakutachosha akili wala kumaliza nguvu. Humo, shughuli kuu na za utukufu zaidi zinaweza kuendelezwa, matamanio ya juu zaidi kufikiwa, na malengo makubwa zaidi ya matarajio kutimizwa; na bado kutazuka viwango vipya vya kupanda, maajabu mapya ya kushangaa, Kweli mpya za kuelewa, na mambo mapya ya kuchochea nguvu za akili, roho, na mwili. **{SRSw 432.2}**

Na kadiri miaka ya umilele inavyoendelea kupita, italeta ufunuo mpya, wenye utajiri zaidi na utukufu zaidi kuhusu Mungu na Kristo. Kadiri maarifa yanavyoendelea kukua, ndivyo upendo, heshima, na furaha navyo vitakavyoongezeka. Kadiri wanadamu wanavyozidi kumjua Mungu, ndivyo mshangao wao kwa tabia Yake utakavyokuwa mkubwa zaidi. Yesu anapowafunulia utajiri wa ukombozi na mafanikio ya ajabu katika pambano kuu dhidi ya Shetani, mioyo ya waliokombolewa itadunda kwa uaminifu mkubwa zaidi, nao watapiga vinubi vya dhahabu kwa mkono ulio imara zaidi; na elfu kumi mara elfu kumi na maelfu ya maelfu ya sauti zitaungana kuujaza wimbo mkuu wa sifa [10.000 x 10,000 x 10,000]. **{SRSw 432.3}**

"Na kila kiumbe kilichoko mbinguni na juu ya nchi na chini ya nchi ya juu ya bahari, na vitu vyote vilivyomo ndani yake, nalivisikia, vikisema, Baraka na heshima na utukufu na uweza una Yeye aketiye juu ya kiti cha enzi, na Yeye Mwana-Kondoo, hata milele na milele. Ufunuo 5:13. **{SRSw 433.1}**

Dhambi na wenye dhambi hawatakuwa tena; ulimwengu wote wa Mungu utakuwa safi, na pambano kuu litakuwa limekamilika milele. **{SRSw 433.2}**

MASOMO YA BIBLIA

Shukrani kwa Mwenyezi Mungu, Muumbaji, Mdumishaji, na Mkombozi. Pia Wasomaji na Waombezi, Watafsiri, Wahariri, Waandishi, Mafundi, na Wachoraji, nk:

1. Gerard Sakumi Nyafanga-Rorya, Tanzania

2. Grace Momadi-Masaka-Jersey, Marekani

3. Musa Budodi-Shinyanga, Tanzania

UTANGULIZI

Nimewiwa kuandika kitabu hiki kwa kuwa nyakati tunazoishi, na zinazotujia mbeleni, ni nyakati ambazo inatubidi tujielimishe na kujiaanda kikamilifu, tusije tukashtukishwa kwa mambo ya dharura yanayojujia ulimwengu. Matukio haya hayatamjia muamini tu au yule asiyeamini, la! Bali kila mwenye mwili. Kuacha kukuambia mambo haya, itakuwa ni ukatili kwangu. Hivyo weka umakini na uyasome mambo haya taratibu

Kitabu hiki kimeandaliwa kwa njia rahisi sana kukusaidia wewe msomaji kufamu Kweli za Maandiko matakatifu na baadhi ya mafundisho ambayo yameachwa na wengi. Basi kubali Neno la Mungu likuongoze sio wewe kuliongoza Neno la Mungu. Pia ukubali Maandiko matakatifu kujieleza yenyewe sio wewe kuieleza maandiko matakatifu kwa tafsiri yako mwenyewe.

Yohana 8:32 tena mtaifahamu Kweli, nayo hiyo Kweli itawaweka huru.

Katika maisha ya kila siku bila kuelezana Ukweli hakuna uhuru, Kweli za Neno la Mungu ndio linatuweka huru. Kitabu hiki kimekusanya baadhi ya Kweli za Maandiko ambayo yameachwa. Kweli ana dada yake aitwaye Upendo, na yote yanapaswa kwenda sambamba, Upendo bila Ukweli utakuwa unafiki, na Ukweli bila upendo utakuwa ukatili tu.

UWEPO WA MUNGU NA KWELI ZA MANENO YAKE

Ufunuo 22:12

Tazama Naja upesi na ujira wangu u pamoja Nami kumlipa kila mtu kama kazi yake ilivyo

1. Neno la Mungu
2. Chimbuko la dhambi na Matokeo yake
3. Yesu ni nani?
4. Ukombozi wa mwanadamu
5. Katikati ya vita
6. Kimbilio kwa wote
7. Njia ya wokovu kabla ya kifo cha Yesu
8. Sheria ya Mungu
9. Amri za Mungu
10. Sabato ya Kweli
11. Kwanini mkanganyiko katika ibada?
12. kuzaliwa ukubwani
13. Ibada ya Kweli ni ipi?
14. Vita dhidi ya Kweli za Mungu
15. Kuna tumaini gani makaburini.
16. Ibada bandia ilitoka wapi?
17. Utii wangu mbele za Mungu (uwakili)
18. Mwili wangu ni mtakatifu
19. Familia yangu ni ya thamani
20. Miaka 1000 ina maana gani?
21. Njia ya wokovu kabla ya kifo cha Yesu (Patakatifu)
22. Ujio wa Yesu mara ya pili ni wa hakika
23. Mwisho wa dhambi
24. Nchi mpya na mbingu mpya.

Sura 1

NENO

Yohana 17:17 Uwatakase kwa ile Kweli; Neno Lako ndiyo Kweli.

Acha Neno la Mungu litupatie Kweli Zake maana kupitia Neno twapata utakaso.

Neno au Neno ni nani?

Yohana 1:1

Hapo mwanzo kulikuwako Neno, Naye Neno alikuwako kwa Mungu, ***Naye Neno alikuwa Mungu.***

Unapozungumzia Neno unazungumzia uwepo wa Mungu. Maeneo mengine Neno la Mungu ikisomwa watu huamriwa kuvua kofia au kuamriwa watu wasimame.

NENO ni uwepo wa Mungu, maana Neno ni Mungu.

Yesu ni Neno la Mungu.

Ufunuo19:13. Naye amevikwa vazi lililochovywa katika damu, na Jina Lake aitwa, Neno la Mungu.

Neno la Mungu lina mamlaka kiasi gani?

Zaburi 33:6 Kwa Neno la Bwana mbingu zilifanyika, Na jeshi Lake lote kwa pumzi ya kinywa Chake.

Neno ni uwepo wa Mungu katikati yetu.

Mwanzo moja yote Mungu anaumba mbingu na nchi na vyote vilivyomo kwa uwezo wa Neno Lake, hivyo ndani ya Neno kuna uungu.

Biblia yaani Neno la Mungu

Biblia ina vitabu 66,

Agano la kale vitabu 39,

Agano jipya vitabu 27.

Biblia ina sura 1189, na mafungu 32,102 ambayo watu wamehesabu ahadi zake, Wengi wamepata kuwa zipo zaidi ya 8100, ila wengine wamehesabu na kupata 30,000, inategemea unavyofafanua ahadi. Kwa kawaida kila agizo la Mungu ni ahadi! Katika Kutoka 20, kuna ahadi zaidi ya 11! Na Zaburi 23 ina ahadi zaidi ya 14

Takribani watu 45+ wameandika Biblia, watu wa tasnia mbalimbali

Biblia iliandikwa kama ifuatavyo:

1. Musa aliandika kitabu cha Mwanzo, Kutoka, Mambo ya Walawi, Hesabu, Kumbukumbu la Torati 1-33, Ayubu na Zaburi 90.
2. Joshua ameandika kitabu cha Kumbukumbu la Torati 34 na Joshua 1-24:28.

3. Eleazari ameandika kitabu cha Joshua 24:29-32.
4. Finehas ameandika kitabu cha Yoshua 24:33.
5. Samweli ameandika kitabu cha Waamuzi, Ruthu, 1 Samweli 1-24.
6. Nathani na Gadi wameandika kitabu cha 1 Samweli 25- 31 na 2 Samweli
7. Daudi ameandika kitabu cha Zaburi 1-9, Zaburi 11-32, Zaburi 34- 41, Zaburi 51- 65, Zaburi 68-70, Zaburi 86, Zaburi 95, Zaburi 101, Zaburi 103, Zaburi 108-110, Zaburi 122, Zaburi 124, Zaburi 131, Zaburi 133, Zaburi 138-145
8. Asafu ameandika kitabu cha Zaburi 50, Zaburi 73-83.
9. Watoto wa Kora: Asiri, Elikana, Abiasafu, hawa waliandika kitabu cha Zaburi 42, Zaburi 44-49, Zaburi 84, Zaburi 85 na Zaburi 87.
10. Ethani ameandika kitabu cha Zaburi 89.
11. Hemani ameandika kitabu cha Zaburi 88.
12. Musa ameandika Zaburi 90
13. Sulemani ameandika kitabu cha Wimbo ulio Bora, Mithali 1-29, Zaburi 72, Zaburi 127 na Mhubiri.
14. Aguri ameandika kitabu cha Mithali 30.
15. Lemueli ameandika kitabu cha Mithali 31.
16. Ezra, Yeremia, Ahiya, Yehu, Shemaya na Ido wameandika cha kitabu 1 Wafalme na 2 Wafalme na 1 Mambo ya Nyakati na 2 Mambo ya Nyakati.
17. Obadia ameandika kitabu cha Obadia.
18. Yoeli ameandika kitabu cha Yoeli.
19. Yona ameandika kitabu cha Yona.
20. Amosi ameandika kitabu cha Amosi.
21. Hosea ameandika kitabu cha Hosea.
22. Mika ameandika kitabu cha Mika.
23. Isaya ameandika kitabu cha Isaya.
24. Hezekia amehusishwa sana kwenye uandishi wa kitabu cha Zaburi 42-89 na sehemu ya kitabu cha Mithali 30 akishirikiana na wengine waliokwisha kutajwa.
25. Nahumu ameandika kitabu cha Nahumu.
26. Zefania ameandika kitabu cha Zefania.
27. Yeremia ameandika kitabu cha Yeremia 1-51 na Yeremia 52:1-30 na Maombolezo.
28. Baruku ameandika kitabu cha Yeremia 52:31-34.
29. Habakuki ameandika kitabu cha Habakuki.
30. Danieli ameandika kitabu cha Danieli.
31. Ezekieli ameandika kitabu cha Ezekieli.
32. Hagai ameandika kitabu cha Hagai.
33. Zakaria ameandika kitabu cha Zakaria.
34. Modekai ameandika kitabu cha Esta.
35. Ezra ameandika kitabu cha Ezra, Nehemia pia amehariri kitabu cha Zaburi 90-150.

36. Nehemia ameandika kitabu cha Nehemia 1-7:5 na Nehemia 11:27 na Nehemia 12:43, Nehemia 13:4-31.
37. Malaki ameandika kitabu cha Malaki.
38. Kuna baadhi ya sura za vitabu waandishi wake hawajulikani kama 2 Wafalme 25, Zaburi 1, 10, 33, 43, 66, 67, 71, 91-94, 96 – 100, 102, 104- 107, 111 – 121, 123, 125, 126, 128 – 130, 132, 134 – 137, 146-150.
39. Mathayo ameandika kitabu cha Mathayo.
40. Marko ameandika kitabu cha Marko.
41. Luka ameandika kitabu cha Luka na Matendo ya Mitume.
42. Yakobo ameandika kitabu cha Yakobo.
43. Paulo ameandika kitabu cha Warumi, 1 Wakorintho, 2 Wakorintho Wagalatia, Waefeso, Wakolosai, 1 Timotheo, 2 Timotheo, Wafilipi, Tito, Filemon.
44. Petro ameandika kitabu cha 1 Petro na 2 Petro.
45. Yuda ameandika kitabu cha Yuda. Huyu ni Yuda ndugu yake Yakobo na mtumishi wa Yesu.
46. Yohana ameandika kitabu cha Yohana, 1 Yohana, 2 Yohana 3 Yohana na Ufunuo wa Yohana.

Kitabu cha Waebrania mwandishi hajulikani.

Kwa sababu Biblia ni uwepo wa Mungu, hivyo biblia ina mamlaka na uwezo mbinguni na duniani, na ndiyo sauti ya Mungu kwetu, na tunapaswa kuichukua kama Yeye anazungumza nasi mbashara au uso kwa uso.

Waebrania 4:12

Maana Neno la Mungu li hai tena lina nguvu tena lina ukali kuliko upanga uwao wote, ukatao kuwili, tena lachoma hata kuzigawanya nafsi na roho na viungo na mafuta yaliyomo ndani yake, tena li jepesi kuyatambua mawazo na makusudi ya moyo.

Neno la Mungu linapokaa ndani yako mawazo potofu na hisia chafu hukatwa-katwa ndipo Kristo hukaa ndani yako. Dhambi hutupwa motoni kwa uweza wa Neno la Mungu. Ndio maana wanadamu wanajitahidi kuipinga Biblia maana Biblia inawasonda na kuchoma mioyo iliyojaa dhambi.

Je, nani aliongoza uandishi wa Maandiko matakatifu?

Tumia Neno la Mungu kwa hekima toka mbinguni kuonya watu na kuwaweka kwenye mstari wa Mungu.

Wakolosai 3:16.

Neno la Kristo na likae kwa wingi ndani yenu katika hekima yote, mkifundishana na kuonyana kwa Zaburi, na nyimbo, na tenzi za rohoni; huku mkimwimbia Mungu kwa neema mioyoni mwenu.

2 Petro 1:21

Maana unabii haukuletwa popote kwa mapenzi ya mwanadamu, bali wanadamu walinena yaliyotoka kwa Mungu wakiongozwa na Roho Mtakatifu.

Neno la Mungu halibadiliki wala halitapitwa na wakati bali litadumu milele.

Mathayo 24:35

Mbingu na nchi zitapita, lakini Maneno Yangu hayatapita kamwe.

Neno lilisababisha Yohana aende kisiwa cha Patimo.

Ufunuo1:9. Mimi Yohana, ndugu yenu na mwenye kushiriki pamoja nanyi katika mateso na ufalme na subira ya Yesu Kristo, nalikuwa katika kisiwa kiitwacho Patmo, kwa ajili ya Neno la Mungu, na ushuhuda wa Yesu.

Biblia inawachoma watu mioyo yao pia ndio maana watu wanaona imepitwa na wakati hivyo wanataka ifanyiwe marekebisho. Lakini Neno la Mungu limekamilika, akili ya Mungu au maamuzi ya Mungu hayakosolewi na mwanadamu aliyechakazwa na dhambi.

1 Wakorintho 1:25

Kwa sababu upumbavu wa Mungu una hekima Zaidi ya wanadamu, na udhaifu wa Mungu una nguvu Zaidi ya wanadamu.

Mungu ni Zaidi ya mzazi mwenye hekika, hivyo Yeye anaona mwisho kabla haijafika.

Hakuna kiumbe chenye mawazo ya kumkosoa Mungu wala kusema Neno la Mungu limepitwa na wakati.

Mungu hapitwi na wakati wala Neno Lake halipitwi na wakati.

Mathayo 24:35. Mbingu na nchi zitapita; lakini Maneno Yangu hayatapita kamwe.

Kila Andiko la Mungu lina makusudi yake maalum kwangu na siku zote Maneno ya Mungu hayatamkwi bure.

Isaya 55:10, 11. Maana kama vile mvua ishukavyo, na theluji, kutoka mbinguni, wala hairudi huko; bali huinywesha ardhi, na kuizalisha na kuichipuza, ikampa mtu apandaye mbegu, na mtu alaye chakula;

Ndivyo litakavyokuwa Neno Langu, litokalo katika kinywa Changu; halitanirudia bure, bali litatimiza mapenzi Yangu, nalo litafanikiwa katika mambo yale niliyolituma.

Kuhubiri injili ni agizo sio ombi, jinsi ulivyookolewa nawe nenda ukaokoe. Neno hili litumike kwa upendo kuonya watu makosa yao.

2Timotheo 4:1 Nakuagiza mbele za Mungu, na mbele za Kristo Yesu, atakayewahukumu walio hai na waliokufa; kwa kufunuliwa Kwake na kwa ufalme Wake;

2 Timotheo 4:2 lihubiri Neno, uwe tayari, wakati ukufaao na wakati usiokufaa, karipia, kemea, na kuonya kwa uvumilivu wote na mafundisho.

Popote Neno la Mungu linapotajwa kuna sababu ya msingi na ni mpango wa Mungu hivyo Neno la Mungu halitajwi bure na usijaribu kutaja Neno la Mungu bure wala usilitaje Neno takatifu kwa mizaha.

Bwana Atubariki tunapoheshimu Neno takatifu.

Sura 2

Chimbuko la Dhambi na Matokeo yake

Dhambi ni nini?

1 Yohana 3:4 Kila atendaye dhambi, afanya uasi; kwa kuwa dhambi ni uasi.

Mwanzo 2:16, 17

Bwana Mungu akamwagiza huyo mtu, akisema matunda ya kila mti wa bustani waweza kula.

Walakini matunda ya mti wa ujuzi wa mema na mabaya, usile, kwa maana siku utakapokula matunda ya mti huo utakufa hakika.

Mungu anachodai kwa watu Wake ni utii. Serikali kinachodai kwa wananchi wake ni utii.

Usipotii sheria ya nchi kuna siku tu utajikuta upo gerezani. Sio salama kukaidi sheria.

Usipotii sheria ya Mungu kuna siku tu utakuta yale ambayo Mungu alikuandalia anayaondoa, hapa duniani hasa ule uzima wa milele.

Namna Lusifa alivyoanguka mpaka akaitwa Shetani

Ezekiel 28:14-19

Wewe ulikuwa kerubi mwenye kutiwa mafuta afunikaye, nami nalikuweka ukawa ukawa juu ya mlima mtakatifu wa Mungu umetembea huko na huko kati ya mawe ya moto.

Ulikuwa mkamilifu katika njia zako tangu siku ile ulipoumbwa hata uovu ulipoonekana ndani yako.

Kwa wingi wa uchuuzi wako watu walikujaza udhalimu ndani yako, nawe umetenda dhambi, kwasababu hiyo nimekutoa kwa nguvu katika mlima wa Mungu kama kitu kilicho najisi, Nami nimekuangamiza ewe kerubi ufunikaye, utoke katika mawe hayo ya moto.

Moyo wako uliinuka kwasababu ya uzuri wako, umeiharibu hekima yako kwasababu ya mwangaza wako, Nimekutupa chini, nimekulaza mbele ya wafalme wapate kukutazama.

Kwa wingi wa maovu yako, katika uovu wa uchuuzi wako, umepatia unajisi patakatifu pako, basi nimetokeza moto kutoka ndani yako, nao umekuteketeza, Nami nimekufanya majivu juu ya nchi, machoni pa watu wote wakutazamao.

Wote wakujuao kati ya kabila za watu watakustajabia, umekuwa kitu cha kutisha, wala hautakuwapo tena hata milele.

I. Ukiona mawazo yako ndio ya thamani kuliko ya wengine, tena wewe ni bora kuliko wengine elewa tayari wewe ni mateka ya Shetani.
II. Shetani alikuwa na utukufu na aliheshimika maana hakuwa na dhambi
III. Ukiwa mwaminifu Mungu anakuheshimu na kukuinua juu
IV. Mungu hakuumba dhambi wala mdhambi bali aliumba viumbe vilivyo vikamilifu
V. Shetani aliridhia kujidanganya kupitia uzuri wake.
VI. Ukitenda dhambi utukufu wa Mungu unatoweka.
VII. Uwezo uliokuwa nao katika Jina la Yesu hutoweka, na sasa ukiliita Jina la Yesu, Naye Yesu hunyamaza.
VIII. Mema ambayo Mungu alikuandalia Mungu anaondoa.
IX. Chanzo cha anguko la mwanadamu ni kiburi, majivuno, mashindano.
X. Kujiona mzuri au bora kuliko wengine, kunaleta uasi
XI. Ukianguka dhambini hekima uliyokuwa nayo pia inaanguka.
XII. Ukianguka hata watu wanakuzomea na kukudhihaki.
XIII. Huwezi kuwepo tena katika maeneo matakatifu.

Mwanzo 3:4, 5.

Nyoka akamwambia mwanamke hakika hamtakufa.

Kwa maana Mungu anajua ya kwamba siku mtakayokula matunda ya mti huo mtafumbuliwa macho nanyi mtakuwa kama Mungu mkijua mema na mabaya.

Mwanadamu alidhani kuna jambo zuri amefichwa na Mungu na kuona Shetani ni mkweli kuliko Mungu

Mungu amemaliza hubiri Lake, kisha Shetani naye anaanza kupotosha hubiri la Mungu.

Mwanadamu alipewa uhuru wa kutii au kutotii hubiri la Mungu, aliambiwa madhara ya kutotii na faida ya kutii. Mwanadamu akamwamini Shetani kuliko Muumba Wake

Dhambi ikaingia mwanadamu, naye akaanza kuvuna matunda ya dhambi.

Mwanzo 3:16-19

Akamwambia mwanamke hakika nitakuzidishia uchungu wako na kuzaa kwako kwa utungu utazaa watoto na tamaa yako itakuwa kwa mumeo, naye atakutawala.

Akamwambia Adamu, kwa kuwa umeisikiliza sauti ya mke wako, ukala matunda ya mti ambao nalikuagiza nikisema, usiyale, ardhi imelaaniwa kwa ajili yako. Kwa uchungu utakula mazao yake siku zote za maisha yako.

Michongoma na miiba itakuzalia, nawe utakula mboga za kondeni,

Kwa jasho la uso wako utakula chakula hata utakapoirudia ardhi, ambayo katika hiyo ulitwaliwa, kwa maana u mavumbi wewe nawe mavumbini utaru.

Leo tunakula kwa jasho jingi tena kwa machozi

Leo mama zetu wanazaa kwa uchungu mwingi, tena wakati mwingine wanapasuliwa kwa kisu. Baada ya dhambi, mwanamke anatawaliwa na mwanamume, hata kama mataifa wanajaribu kuiondoa lakini halitaisha. Wanawake wengi pia hula kwa jasho jingi kwa vile mwanamume ndiye mtawala, mara zingine ameacha majukumu ya kutokwa na jasho kwenda kwa mkewe au binti zake, au dada zake.

Hata kauli iliyozoeleka kuwa jembe halimtupi mkulima, leo jembe kuna wakati linawatupa wakulima, ndio maana tunaangaika na mbolea za aina zote. Katika yote haya, Neno la Mungu limetimia, kwamba ardhi imelaaniwa kwaajili yako.

Mwanadamu ameanza kutumikia dhambi aliyoichagua na matunda ya dhambi ni taabu na mwisho wa taabu ni mauti.

Shetani hakuwa na uwezo wa kuwaokoa wanadamu maana yeye ndiye mwasisi wa dhambi na anasubiri mauti ya milele.

Ufunuo 20:10. Na yule ibilisi mwenye kuwadanganya akatupwa katika ziwa la moto na kiberiti alimo yule mnyama na yule nabii wa uongo. Nao watateswa mchana na usiku hata milele na milele.

Shetani alifanya kazi gani ya kumdhoofisha mwanadamu?

Warumi 1:25 Kwa maana waliibadili ile Kweli ya Mungu kuwa uongo, wakakisujudia kiumbe na kukiabudu badala ya Muumba anayehimidiwa milele. Amina.

Warumi 6:23

Kwa maana mshahara wa dhambi ni mauti bali karama ya Mungu ni uzima wa milele katika Kristo Yesu Bwana wetu.

Hauwezi ukatenda dhambi ukabaki salama. Hata kama unadhani upo salama lakini ukweli ni kwamba, haupo salama. Mwisho wa dhambi ni mauti ya milele. Dhambi inaondoa usalama wa mtu.

Isaya 57:21

Hapana Amani kwa wabaya asema Mungu wangu.

Mtu mbaya hana amani siku zote vifo vyao ni kwa mateso mengi.

Warumi 6:23. Kwa maana mshahara wa dhambi ni mauti; bali karama ya Mungu ni uzima wa milele katika Kristo Yesu Bwana wetu.

Daniel 12:10

Wengi watajitakasa na kujifanya weupe na kusafika, bali wabaya watenda mabaya, wala hataelewa mtu mbaya awaye yote bali wao walio na hekima ndio watakaooelewa.

Wengi leo wanajificha kwenye kichaka au kivuli cha dini na kujitakasa katikati ya watu ili waonekane wacha-Mungu, kumbe ni kuficha dhambi katikati ya watu.

Kumbuka

- Mungu hachanganywi,
- Mungu hadhihakiwi,
- Mungu hadanganywi,
- Mungu haongwi,
- Mungu habadiliki Malaki 3:6.

Acha kujadili dhambi maana dhambi haijadiliwi kuwa nitende au niache, dhambi ni kuacha. Naam dawa ya dhambi ni kuacha mara moja.

1 Wakorintho 6:18

Ikimbieni zinaa kila dhambi aitendayo mwanadamu ni nje ya mwili wake ila yeye afanyaye zinaa hutenda dhambi juu ya mwili wake mwenyewe.

Dawa ya dhambi ni kuikimbia, usifanye urafiki na dhambi.

1 Samweli 15:23 Kwani kuasi ni kama dhambi ya uchawi, Na ukaidi ni kama ukafiri na vinyago; Kwa kuwa umelikataa Neno la Bwana, Yeye Naye amekukataa wewe usiwe mfalme.

Madhara ya kucheza dhambini ni makubwa hugarimu hata maisha. Jisalimishe kwa Yesu ili upate kuondolewa dhambi zako.

Yakobo 1:15 Halafu ile tamaa ikiisha kuchukua mimba huzaa dhambi, na ile dhambi ikiisha kukomaa huzaa mauti.

Sura 3

YESU NI NANI?

Mathayo1:23

Tazama bikira atachukua mimba, naye atazaa mwana, Nao watamwita jina lake Imanueli, yaani Mungu pamoja nasi.

1) Anayemzaa Yesu ni bikira, yaani kitu kilicho kisafi.
2) Anayezaliwa ni mwanaume yaani kiongozi
3) Imanueli yaani Mungu pamoja nasi
4) Imanueli ni kudhihirisha Uungu wa Yesu

Isaya 9:6

Maana kwaajili yetu Mtoto amezaliwa, tumepewa Mtoto mwanaume, na uweza wa kifalme utakuwa begani Mwake, Naye ataitwa Jina Lake,Mshauri wa ajabu, Mungu Mwenye nguvu, Baba wa milele, Mfalme wa Amani.

Miaka Zaidi ya 400 nabii Isaya alionyeshwa habari za Yesu

1. Kuzaliwa kwake ni kwaajili yetu, Yesu hakuzaliwa kwa matakwa Yake alikuja ili tupate uzima.
2. Amezaliwa kwa mamlaka ya aliye juu sio kwa mbegu za mwanaume
3. Yesu ni mshauri mzuri kuliko washauri wote, mshauri wa ajabu!
4. Yesu ni Mungu, jibu tumepata kuwa Yesu ni nani kuanzi leo elewa Yesu ni Mungu.
5. Yesu ni Baba (mathayo 23:9, *wala msimwite mtu baba duniani, maana Baba yenu ni Mmoja, aliye wa mbinguni.* Yesu ni Baba wa mbinguni Uungu Wake hauna mashaka).
6. Yesu ni mtawala wa vyote tunavyoviona ni mfalme wa wafalme.

Kama Yesu ni Mungu Je! Alitenda kazi za Kiungu?

Luka 5:20

Naye alipoona Imani yao alimwambia, Ee rafiki umesamehewa dhambi zako.

1. Yesu anauwezo wa kusoma mioyo, alisoma mioyo ya watu akaona imani yao.
2. Yesu alisamehe dhambi. Ni Mungu tu ndiye Mwenye mamlaka ya kusamehe dhambi.

Yohana 8:51

Amin, amin, nawaambia mtu akilishika neno langu hataona mauti milele.

1. Yesu anatoa uhakika kwa watu Wake
2. Yesu neno Lake lina mamlaka ya kuondoa mauti maishani mwetu.

Pamoja na yote aliyofanya Yesu hapa duniani walio Wake hawakumwamini ndio maana mpaka leo baadhi ya watu wana mashaka na Uungu wa Yesu.

Marko 6:4

Yesu akawaambia, nabii hakosi heshima isipokuwa katika nchi yake mwenyewe na kwa jamaa zake na nyumbani mwake.

Hii ndio sababu Yesu alionekana wa kawaida

1. Wale wanaooishi pamoja huwa wanadharauliana, mpaka wakamdharau Yesu.
2. Mitume walitamani kumfahamu Mungu lakini hata wao walikuwa na mashaka mpaka Yesu alipowaambia wazi wazi kuwa Yeye ni Mungu.

Yohana 14:8,9

Filipo akamwambia Bwana, utuonye Baba yatutosha.

Yesu akamwambia, Mimi nimekuwapo pamoja nanyi siku hizi zote wewe usinijue Filipo? Aliyeniona Mimi amemwona Baba, Basi wewe wasemaje utuonyeshe baba.

Uungu wa Yesu hauna mashaka.

1. Yesu ni kiongozi …….. Isaya 55:4
2. Yesu ni Mungu wa milele. Isaya 40:28
3. Yesu ni mfalme wa wafalme. Ufunuo 17:14
4. Yesu ni mfalme wa utukufu. Zaburi 24:10
5. Yesu ni tumaini letu. 1 Timotheo 1:1
6. Yesu ni nyota ya asubuhi. Ufunuo 2:28
7. Yesu ni mtakatifu. Isaya 6:3
8. Yesu ni masihi. Yohana 4:25, Danieli 9:25

9. Yesu ni mchungaji mwema. Yohana 10:11
10. Yesu ni muumbaji. Wakolosai 1:16
11. Yesu ni mkombozi wetu. Isaya 59:20
12. Yesu ni ufufuo na uzima. Yohana 11:25
13. Yesu ni haki yetu. 1 Yohana 2:1
14. Yesu ni mlango wa kuingia mbinguni. 1 Yohana 1:7.

Warumi 14:11

Kwa kuwa imeandikwa kama niishivyo anena Bwana, kila goti litapigwa mbele zangu na kila ulimi utamkiri Mungu.

Wa kupigiwa magoti ni Yesu.

Wafilipi 2:10

Ili kwa Jina la Yesu kila goti lipigwe, la vitu vya mbinguni na duniani na vya chini ya nchi.

1. Kila mwanadamu ili aingie mbinguni ni lazima amkiri Yesu Kristo kuwa Bwana na mwokozi wa maisha yake.
2. Biblia haisemi utaokolewa kwasababu ya kutii dini yako bali utii kwa Maaandiko matakatifu.
3. Biblia inadai kila mtu amkiri Yesu.
4. Kila goti lipigwe mbele Zake

Yohana 12:42

Walakini hata katika wakuu walikuwamo wengi waliomwamini, lakini kwa sababu ya mafarisayo hawakumkiri wasije wakatengwa na sinagogi.

1. Wengi walishindwa kumpokea Yesu kwa sababu ya kulinda vyeo vyao.
2. Wengi walishindwa kumpokea Yesu kwasababu ya kuogopa kutengwa na makanisa yao.

Yohana 11:28

Njoni kwangu ninyi nyote msumbukao na wenye kulemewa na mizigo Nami nitawapumzisha.

Twendeni kwa Yesu ili tuweze kupata raha nafsini mwetu. Mungu wetu ni mkuu, Yeye hashindwi na jambo lolote.
Mitume walimkiri Yesu kuwa Bwana na Mwokozi wa maisha yao
Mathayo 16:15, 16
Akawaambia, Nanyi mwaninena Mimi kuwa ni nani?
Simoni Petro akajibu akasema, Wewe Ndiwe Kristo, Mwana wa Mungu aliye hai.

Sura 4

UKOMBOZI WA MWANADAMU

Ukombozi ni kuokolewa toka dhambini au hatari fulani. Ukombozi ni zawadi ya Mungu kwa wanadamu walioanguka dhambini kupitia Yesu Kristo.

Yohana 3:16

Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu hata akamtoa Mwana wake wa pekee ili kila mtu amwaminiye asipotee bali awe na uzima wa milele.

1. Kilichomsukuma Yesu kuja duniani ni upendo.
2. Mungu anamtoa Mtoto Wake wa pekee kuwa sadaka ya kuuawa msalabani.
3. Kila anayemwamini Yesu na kuishi sawasawa na Neno Lake ataokolewa
4. Na atapata uzima wa milele.
5. Pamoja na dhambi kumchakaza mwanadamu, bado Mungu alimpenda mwanadamu na kuweka mpango mahususi ya kumuokoa mwanadamu huyo

Je! Kuna dhambi mtu akitenda hawezi kuokolewa hata akitubu?

Isaya 1:18 Haya, njoni, tusemezane, asema Bwana. Dhambi zenu zijapokuwa nyekundu sana, zitakuwa nyeupe kama theluji; zijapokuwa nyekundu kama bendera, zitakuwa kama sufu.

Fungu hili la Isaya linampa kila mdhambi tumaini ya kusogea miguuni Pake Yesu upya.

Kukombolewa kuna masharti ya kufuata Neno la Mungu. Mtunga Zaburi amesisitiza akisema.

Zaburi 25:5 Uniongoze katika Kweli Yako, Na kunifundisha. Maana Wewe Ndiwe Mungu wa wokovu wangu, Nakungoja Wewe mchana kutwa.

Mathayo 1:23

Tazama bikira atachukua mimba naye atazaa Mwana, Nao watamwita Jina Lake Imanueli yaani Mungu pamoja nasi

1. Baada ya anguko la mwanadamu Mungu alianza mapema hatua za kumkomboa mwanadamu
2. Mkombozi lazima afanane na wanaokombolewa ndio maana Yesu alivaa ubinadamu

Yohana 1:29

Siku ya pili yake, Yohana anamwona Yesu anakuja kwake, akasema, Tazama Mwana-Kondoo wa Mungu aichukuaye dhambi ya ulimwengu

1. Yesu ndio aliyekuja kwetu kutukomboa
2. Yesu amebeba dhambi zetu akisukumwa na upendo
3. Yeye Alibeba adhabu yetu

Isaya 7:14

Kwa hiyo Bwana Mwenyewe atawapa ishara,Tazama bikira atachukua mimba atazaa mtoto mwanamume naye atamwita Jina Lake Imanueli.

1. Kuzaliwa kwa Yesu kulipangiliwa kwa muda mrefu sana.
2. Kuzaliwa Kwake ni mianzo ya sisi kukombolewa.
3. Anayezaliwa ni Mungu aliyevaa ubinadamu yaani Imanueli.

Isaya 53:5

Bali alijeruhiwa kwaajili ya makosa yetu, Alichubuliwa kwa maovu yetu, Adhabu ya Amani yetu ilikuwa juu Yake, Na kwa kupigwa Kwake sisi tumepona.

1. Kila mtu atalipwa kwa alichokipanda
2. Yesu kwa upendo mkuu anavaa ubinadamu, ili alipe dhambi aliyopanda mwanadamu
3. Yesu alidharauliwa kwa ajili ya dhambi zangu
4. Alijeruhiwa kwaajili ya dhambi zangu
5. Alipigwa kwaajili ya dhambi zangu
6. Mateso Yake ni ukombozi wangu
7. Mbadilishano wa ajabu, alibeba dhambi zetu, na tukapewa haki na maisha Yake matakatifu!

Wafilipi 2:9,10

Kwa hiyo tena Mungu alimwadhimisha mno akamkirimia Jina lile lipitalo kila jina, ili kwa Jina la Yesu kila goti lipigwe la vitu vya mbinguni na vya duniani na chini ya nchi.

1. Mungu anamjali mno mwanadamu ndio maana hata baada ya dhambi bado, anatufuatilia na kuturudisha
2. Jina la Yesu ndilo Jina la kutuokoa na sio majina mengine wala sio kitu kingine.
3. Hivyo Yesu sharti apewe heshima na utukufu kwa kile anachowatendea wanadamu.

Ufunuo 12:7-12

8. *Kulikuwa na vita mbinguni, Mikael na malaika Zake wakapigana na yule joka, yule joka naye akapigana nao pamoja na malaika zake.*
9. *Nao hawakushinda wala mahali pao hapakuonekana tena mbinguni.*

10. Yule joka akatupwa, yule mkubwa, nyoka wa zamani, aitwaye ibilisi na shetani, audanganyaye ulimwengu wote, akatupwa hata nchi, na malaika zake wakatupwa pamoja naye.
11. Nikasikia sauti kuu mbinguni, ikisema, sasa kumekuwa wokovu, na nguvu, na ufalme wa Mungu wetu, na mamlaka ya Kristo Wake, kwa maana ametupwa chini mshitaki wa ndugu zetu, yeye awashitakiye mbele za Mungu wetu, mchana na usiku.
12. Nao wakamshinda kwa damu ya Mwana-Kondoo na kwa Neno la ushuhuda wao, ambao hawakupenda maisha yao hata kufa.

1. Vita vinavyopiganwa kati ya Yesu na Shetani ni vita ya kumgombania mwanadamu, Shetani anataka tuwe upande wake, na Mwenyezi Mungu ambaye alituumba, anataka tuwe upande Wake.
2. Yesu alishinda vita hivyo na ushindi Wake ndio ukombozi wetu
3. Shetani alifukuzwa mbinguni, hivyo hana nafasi tena mbinguni, yeye na malaika zake
4. Shetani alitupwa katika sayari yetu dunia
5. Pamoja na malaika zake wapo kwenye hii sayari dunia
6. Yesu anatoa tangazo kutoka mbinguni.
7. Wokovu na nguvu na ufalme wa Mungu wetu na mamlaka wa Kristo Wake
8. Nguvu zipo kwa Yesu
9. Hakuna mwanadamu anayeweza kumshinda Shetani kwa nguvu zake isipokuwa amemvaa Kristo
10. Kuna watu hawakuona hasara juu ya miili yao, nayo iliteswa kwaajili ya Kristo hata wakafa, baada ya kutambua kafara ya Kristo.
11. Maisha ya umilele ni bora kuliko maisha haya ya taabu na yenye maumivu makali, vilio, vifo na hakika ni mafupi.
12. Tazama maisha ya umilele ndio bora Zaidi.

1 Petro 2:24

Yeye Mwenyewe alizichukua dhambi zetu katika mwili Wake juu ya mti, tukiwa wafu kwa mambo ya dhambi, tuwe hai kwa mambo ya haki na kwa kupigwa Kwake mliponywa.

Mwilini Mwake Yesu amebeba dhambi zangu. Yesu amebeba dhambi zetu na kupona kwetu ni kukimbilia Kwake.

Maombolezo 3:22

Ni huruma za Bwana kwamba hatuangamii, kwa kuwa rehema Zake hazikomi.

1. Mungu ni mwingi wa huruma na upendo anajishugulisha kwa ajili ya maisha yetu
2. Rehema za Bwana ni za milele na hazibagui
3. Mungu ni wa upendo.

Isaya 45:4

Kwaajili ya Yakobo, Wangu, na Israeli, mteule Wangu, nimekuita kwa jina lako, nimekupa jina la sifa, ijapokuwa hukunijua.

Katika dunia ya dhambi kiongozi anajulikana na wengi anaowaongoza na asiowangoza ila kwa Mungu ni kinyume Yeye anawajua wote kwa jina na Yupo wakati wote na watu Wake. Mungu anatujali japo sisi wanadamu hatumjali,

Mungu ametupa jina la sifa japo hatukustahili sifa.

Waebrania 13:12

Kwa ajili hii Yesu Naye, ili awatakase watu kwa damu Yake Mwenyewe, aliteswa nje ya lango.

Tumeokolewa kupitia mateso ya Yesu Kristo hata akamwaga damu Yake ili tuweze kuokolewa. Nje ya Kristo hakuna utakaso, nje ya Kristo hakuna wokovu, nje ya Kristo hakuna mbingu

Sura 5

KATIKATI YA VITA

Ufunuo 12:7

Kulikuwa na vita mbinguni,Mikaeli na malaika Zake,wakapigana na yule joka, yule joka naye akapigana nao pamoja na malaika zake.

1. Vita sio kitu kigeni masikioni mwa wengi lakini sio jambo zuri.
2. Vita sio jambo lelema.
3. Ukisikia vita ni wazi kuwa kuna chuki baina ya pande mbili tofauti.
4. Vita vifupi kupita vyote, vilipiganwa kule Zanzibari, mwaka 1896 kwa masaa 38, Uingereza ilitaka kisiwa hicho, na Sultani wa Omani pia alitaka kisiwa hicho. Baada ya masaa hayo 38, Sultani alijisalimisha kwa Uingereza, nao wakachukua kisiwa hicho. Vita refu kupita zote ilianzia mbinguni, zaidi ya miaka 6000 iliyopita, na inaendelea kupiganwa hata leo nawe umo katika vita hivi kila siku, kichwani mwako utasikia makombora-Waefeso sita yasema tuvae silaha za vita!

Ufunuo 12:12

Kwa hiyo shangilieni enyi mbingu, nanyi mkaao humo.

Ole wa nchi na bahari! Kwa maana yule ibilisi ameshuka kwenu mwenye ghadhabu nyingi, akijua ya kuwa ana wakati mchache tu.

1. Shetani ameshuka kwetu duniani, adui wake namba moja ni mwanadamu

2. Hata kama wakati mwingine mwanadamu ameridhika na maisha na kuwa na amani dhambini.
3. Lakini mwanadamu hayupo salama bila Yesu.
4. Nguvu ya Mkristo na ushindi katika vita ni maombi, kukaa na Yesu karibu.

Silaha kubwa ya mkristo itakayompa ni ipi?

Waefeso 6:11

Vaeni silaha zote za Mungu, mpate kuweza kuzipinga hila za shetani.

Silaha ya Mkristo ni kuishi maisha matakatifu

Waefeso 6:13

Kwa sababu hiyo twaeni silaha zote za Mungu, mpate kuweza kushindana siku ya uovu, na mkiisha kuyatimiza yote kusimama.

Basi simameni, hali mmefunga Kweli viunoni, na kuvaa dirii ya haki kifuani,

Na kufungiwa miguu utayari tupatao kwa Injili ya amani,

Zaidi ya hayo mkitwa ngao ya Imani, ambayo kwa hiyo mtaweza kuizima mishale yote yenye moto ya yule mwovu.

Tena ipokeeni chapeo ya wokovu, na upanga wa Roho ambao ni Neno la Mungu.

Kwa sala zote na maombi mkisali kila wakati katika Roho, mkikesha kwa jambo hilo na kudumu katika kuwaombea watakatifu wote.

Mwili wote uwe tayari kwa Yesu kwa maombi na usomaji wa Biblia.

Unyenyekevu, Uaminifu, Upendo, Furaha, Amani, Uvumilivu, Utu wema, Fadhili, Uaminifu, Upole, Kiasi.

Vita kuu uk 93

Jambo lingine la ajabu ni jinsi ambavyo Shetani amewafanya wanadamu waisahau kabisa haki ya Mungu na maonyo ya Neno Lake na kusema ya kwamba Mungu ni Mwenye neema hata hakuna yeyote atakayepotea bali wote watakatifu na wenye dhambi mwisho wataokolewa katika ufalme Wake.

1. John Wycliffe Mwiingereza aliyehubiri sana Ulaya na mfia Imani aliyejifunza Ukweli na kuuishi

2. Askofu alipomvisha John Huss kofia iliyoandikwa mwasi mkuu; huyu mfia dini alisema, kwa furaha nyingi, nitaivaa taji hii ya aibu kwa ajili Yako, Ewe Yesu ambaye ulivikwa taji ya miiba kwa ajili yangu
3. Martin Luther aliposimama bila hofu mbele ya adui zake wengi katika baraza la Worms, alisema, Sitaikana Imani yangu kamwe wala siwezi kufanya hivyo kwa kuwa Mkristo anajihatarisha kama akiyakiri mambo yafarakanayo na dhamiri yake. Hapa nimesimama MUNGU NISAIDIE
4. 1. William Miller hakuweza kuondosha thibitisho ilikuwa kazi yake kutoa ujumbe wa kurudi kwa Kristo mara ya pili na katika mwaka 1831 alionyesha wazi mbele ya watu sababu za Imani yake ya unabii uliokuwa ukitimilika. Wakristo wengi walizuiliwa kupokea Kweli za Mungu, na wale waliolazimisha waliuawa kikatili sana.

Katika zama zote kweli za biblia zimepigwa vita hata sasa.

Mkristo anayependwa na dunia na ameridhika anapaswa atafakari upya imani yake maana ni rahisi kuanguka.

Mithali 30:6

Usiongeze neno katika Maneno Yake; Asije akakulaumu, ukaonekana u mwongo.

Kwasababu tupo kwenye vita wakaongeza vitabu saba jambo ambalo watu wasiozoea kusoma Biblia mara kwa mara hawashituki. Tupo kwenye pambano Shetani anatumia ushawishi wa kumteka mwanadamu, hamu Ya neno la Mungu leo halipo kwenye mioyo ya watu wengi.

Vitabu kama Tobiti, Yudithi, Hekima ya Sulemani, Sira, Baruku, 1 Wamakabayo, 2 Wamakabayo vinaitwa Deuterokanoni.

Pia kitabu cha Danieli kimeishia sura 12, lakini wanadamu wakaongeza ya kwao, kama vile sura kumi na tatu kisa cha Susana mke wa Yoakimu na kumi na nne.

Sura 6
KIMBILIO KWA WOTE

Warumi 5:12

Kwa hiyo kama kwa mtu mmoja dhambi iliingia ulimwenguni na kwa dhambi hiyo mauti, na hivyo mauti ikawafika watu wote kwa sababu wote wamefanya dhambi.

1. Ikiwa dhambi iliingia kupitia kwa mtu basi huyo mtu hawezi kuleta wokovu.
2. Mwanadamu aliyeanguka dhambini hawezi kuwa kimbilio.
3. Mwanadamu hana uzima wa kudumu ndani yake
4. Alihitajika mtu asiyeathiriwa na dhambi ili kumwokoa mwanadamu.

1Timotheo 2:14

Wala Adamu hakudanganywa ila mwanamke, alidanganywa kabisa akaingia katika hali ya kukosa.

Adamu na Hawa wametenda dhambi, Je! Waendelee na utaratibu wa kutuokoa?

Kwa nani kuna usalama na nani tuliyemkosea?

Wakolosai 1:13,14

Naye alituokoa katika nguvu za giza akatuamisha na kutuingiza katika ufalme wa Mwana wa pendo Lake, ambaye katika Yeye tuna ukombozi yaani msamaha wa dhambi

1. Anayesamehe dhambi Ndiye ana mamlaka ya kuokoa
2. Je, tupitie kwa nani tunapoenda Kwake?
3. Tulipozingirwa na nguvu za giza, Yeye alituokoa tusiangamizwe na Shetani
4. Alituokoa gizani na kutupeleka nuruni Mwake

Yohana 14:13,14

Nanyi mkiniomba lolote kwa Jina Langu hilo nitalifanya, ili Baba atukuzwe ndani ya mwana.

Mkiniomba lolote kwa Jina Langu nitalifanya

1. Ili kwenda kwa Yesu tunaenda moja kwa moja
2. Yesu hana katibu muhtasi wala dalali wa kukutafutia Yesu
3. Viongozi wengi wamechukua utukufu kwa kukaa katikati ya waumini na Yesu, Na Yesu jambo ambalo ni la uongo ni pale wachungaji wanapokuzuia usimwone Yesu
4. Hakuna Nabii wala bikira Maria wala Mtume wa kukuombea kwa Yesu, ila Yesu ametupatia ujasiri wa kwenda kwake moja kwa moja.
5. Baada ya kifo cha Yesu, hatuna makuhani tena, wanaosimama kati ya Mungu na mtu

1Yohana 2:1

Watoto Wangu wadogo nawaandikia haya ili kwamba msitende dhambi, na kama mtu akitenda dhambi tunaye mwombezi kwa Baba, Yesu Kristo Mwenye haki.

1. Yohana huonyesha wazi Mwenye haki ni Yesu pekee
2. Yesu ndio kimbilio kwa wanadamu wote.
3. Acha kupeleka dhambi zako kwa kiongozi wako wa kanisa bali peleka kwa Yesu.

Isaya 1:18, 19

Haya, njoni tusemezane asema Bwana. Dhambi zenu zijapokwa nyekundu sana, zitakuwa nyeupe kama theluji, zijapokuwa nyekundu kama bendera, zitakuwa kama sufu. Kama mkikubali na kutii mtakula mema ya nchi.

1. Mungu anatualika twende Kwake tukitenda dhambi
2. Yeye Ndiye Mwenye dawa ya dhambi. Mwambie akukumbushe dhambi za kuungama kila siku
3. Usiangalie wingi wa dhambi zako nenda tu kwa Yesu
4. Mkubali Yesu na kutii Neno Lake.

Matendo 2:28

Petro akawaambia, tubuni mkabatizwe kila mmoja kwa Jina Lake Yesu Kristo, mpate ondoleo la dhambi zenu, nanyi mtapokea kipawa cha Roho mtakatifu

1. Yesu anahitaji kuona toba zetu
2. Anahitaji kuwa na moyo ulionyenyekea Kwake Mwenyezi Mungu.
3. Utiifu kwa Neno Lake na kumkiri Yeye kama Bwana na mwokozi wa maisha yetu

Sura 7

NJIA YA WOKOVU KABLA YA KIFO CHA YESU (PATAKATIFU)

Kutoka 25:8

Nao na wanifanyie Patakatifu ili nipate kukaa katikati yao.

1. Baada ya anguko la mwanadamu Mungu anamsogeza mwanadamu karibu ili asizidi kuanguka
2. Patakatifu katika Agano la Kale Palikuwa kivuli cha huduma ya Yesu duniani. Waebrania 8:5
3. Yaani Mungu pamoja nasi, Mungu alimwonyesha Musa.

Nje ya patakatifu.

1. *Beseni ya shaba*

   Yohana 7:37- 39

   Hata siku ya mwisho, siku ile kubwa ya sikukuu, Yesu akasimama, akapaza sauti sauti Yake akisema, mtu akiona kiu, na aje Kwangu anywe.

   Aniaminiye Mimi, kama vile Maandiko yalivyonena, mito ya maji yaliyo hai itatoka ndani yake.

   Na Neno hilo alilisema katika habari ya Roho, ambaye wale wamwaminio watampokea baadaye, kwa maana Roho alikuwa hajaja, kwa sababu Yesu alikuwa hajatukuzwa.

2. *Madhabahu ya kafara*

Waefeso 5:2

Mkaenende katika upendo, kama Kristo Naye alivyowapenda ninyi tena kajitoa kwa ajili yenu, sadaka na dhabihu kwa Mungu kuwa harufu ya manukato

3. *Lango.*

Ndani ya patakatifu

4. *Patakatifu pa Patakatifu*
5. *Sanduku la Agano*
6. *Pazia la Patakatifu pa Patakatifu.*
7. *Madhabahu ya Uvumba*
8. *Kinara cha Taa*
9. *Patakatifu*
10. *Mikate ya Wonyesho*
11. *Pazia la Patakatifu-Veil of the Holy place*
12. *Pazia la Nje*
13. *Kifuniko cha mkono wa ngozi*
14. *Pazia la manyoya ya mbuzi*
15. *Pazia la mistari*

Mambo ya Nyakati 22:19

Basi sasa jitieni moyo na nia kumtafuta Bwana, Mungu wenu; inukeni basi, mkamjengee Bwana Mungu mahali Patakatifu, ili kulileta Sanduku la Agano la Bwana, na vyombo vitakatifu vya Mungu, ndani ya nyumba itakayojengwa kwa ajili ya Jina la Bwana.

Ikiwa patakatifu pa zamani paliheshimiwa sana na watu walifanya utakaso mkubwa ili kuingia. Basi baada ya Yesu kuingia mbinguni Patakatifu pa Patakatifu twapaswa kujitakasa zaidi sasa.

Waebrania 10:1- Basi torati, kwa kuwa ni kivuli cha mema yatakayokuwa, wala si sura yenyewe ya mambo hayo, kwa dhabihu zile zile wanazozitoa kila mwaka daima, haiwezi wakati wowote kuwakamilisha wakaribiao.

Waebrania 8:5-watu watumikiao mfano na kivuli cha mambo ya mbinguni, kama Musa alivyoagizwa na Mungu, alipokuwa tayari kuifanya ile hema; maana asema, Angalia ukavifanye vitu vyote kwa mfano ule ulioonyeshwa katika mlima.

Njia aliyoelekezwa Musa na Mungu kufanya iliwakilisha kile alichokifanya Yesu baada ya kuja duniani kwa mara ya kwanza.

Wakolosai 2:17 -Mambo hayo ni kivuli cha mambo yajayo; bali Mwili ni wa Kristo.

Mathayo 27:50, 51.

Kafara ya Yesu iliondoa kafara zote za wanyama, maana sasa Yesu ndiye kafara ya ulimwengu. Yesu Ndiye Mwana-Kondoo wa Mungu aliyechinjwa kwaajili yetu.

Naye Yesu akiisha kupaza sauti tena kwa nguvu, akaitoa roho Yake.

51 Na tazama, Pazia la Hekalu likapasuka vipande viwili toka juu hata chini; nchi ikatetemeka; miamba ikapasuka;

Kitabu cha Tumaini la Vizazi Vyote Uk 429:

"Makuhani, askari, wanyongaji na watu wote waliokuwapo hapo walianguka kifudi fudi. Wakati sauti ya kilio "Imekwisha" iliposikika kutoka mdomoni mwa Kristo, ilikuwa ni wakati wa kutoa dhabihu ya jioni. Kondoo aliyemwakilisha Kristo alikuwa ameletwa kuchinjwa. Kuhani alisimama na kisu tayari hali watu wakiangalia. Lakini nchi ilitetemeka kwasababu Bwana Mwenyewe alikaribia karibu. Kwa sababu ya mpasuko, Pazia la Hekalu likapasuliwa kwa mkono usioonekana vipande viwili toka juu hata chini; na kukifungua wazi kwa macho ya watu chumba cha Patakatifu pa Patakatifu palipokuwa pakijaa utukufu wa Mungu. Mahali Patakatifu mno pa hekalu la dunia hapakuwa patakatifu tena".

Tunapozungumzia patakatifu pa dunia hii aliyoifanya Musa imebaki kuwa historia ya ukombozi kabla ya kifo ya Yesu Kristo, ila sasa tunaye Yesu Kristo Kuhani wetu mkuu ambaye anatuhudumia akiwa Patakatifu pa Patakatifu mbinguni.

1 Yohana 2:1 Watoto wangu wadogo, nawaandikia haya ili kwamba msitende dhambi. Na kama mtu akitenda dhambi tunaye Mwombezi kwa Baba, Yesu Kristo Mwenye haki,

Kila afundishaye Patakatifu pa dunia hii na katika fundisho lake, Yesu haonekani fundisho hilo halijakamilika. Soma zaidi Waebrania 8 mpaka 10.

Sura 8

JE, LIPO KANISA LA MUNGU?

Yesu analo kanisa?

Mathayo 16:18

Nami nakuambia, Wewe ndiwe Petro, na juu ya mwamba huu nitalijenga kanisa Langu; wala milango ya kuzimu haitalishinda.

Waefeso 4:4, 5.

Mwili mmoja na Roho moja kama na mlivyoitwa katika tumaini moja la wito wenu.

Bwana mmoja, Imani moja na ubatizo mmoja.

1. Mungu hajagawanyika wala sio kigeugeu.
2. Mungu aliacha Imani moja, mitume wote walikuwa na imani moja, hawakugawanyika.
3. Bwana hakugawanyika

Matendo 2:1

Hata ilipotimia siku ya petentekoste walikuwako wote mahali pamoja.

1. Yesu aliacha mitume wote 11 wakiwa kitu kimoja
2. Mitume nao walidumisha umoja wao siku zote, mpaka walipolala mauti hapakuwepo na mtume aliyeingiwa na tamaa ya kuanzisha Imani yake.
3. Leo kila kukicha mtu anaibuka na imani tofauti, au yake.
4. Leo kila siku watu wanaibuka, mara huyu ni nabii wengine mitume, wengine askofu mtukufu-reverend, wengine wachungaji.

Waebrania 13:8

Yesu Kristo ni Yeye Yule Yule jana na leo na hata milele.

1. Yesu siku zote habadiliki
2. Wala Yesu hawezi kugawa watu Wake
3. Chuki na hila na vijembe kwa viongozi wa ibada na kuona huyu ni bora kuliko huyu imekuja pale upendo ulipotoweka na kila mmoja kuwa na tamaa ya vitu vinavyoonekana.

Je, Yesu ana kundi Lake yaani kanisa Lake?

Yohana 10:16

Na kondoo wengine ninao, ambao si wa zizi hili; na hao nao imenipasa kuwaleta; na sauti yangu wataisikia; kisha kutakuwako kundi moja na mchungaji Mmoja

1. Walio waaminifu kwa Mungu ni wengi sana wapo kila sehemu wengine wanaabudu miungu ya kipagani bila wao kujua, na wamekuwa waaminifu kwa kile wanachoamini.
2. Yesu atawaita waje katika kanisa Lake maana Yeye hajagawanyika
3. Leo kuna umoja mwingi, mara umoja wa madhehebu, ni kweli umoja huu unasaidia sana kimwili lakini kiroho hatuna umoja.

4. Kwenye ibada hatuna umoja.
5. Watakaofuata imani ya Yesu watakuwa kitu kimoja na kuingia katika kanisa la Yesu ndio watakaookolewa. Leo tuna zaidi ya madhehebu 49,000 ya Kikristo.

Ufunuo 14:6-12

Kisha nikaona malaika mwingine akiruka katikati ya mbingu mwenye injili ya milele, awahubiri hao wakaao juu ya nchi na kila taifa na kabila na lugha na jamaa,

Akasema kwa sauti kuu mcheni Mungu na kumtukuza kwa maana saa ya hukumu Yake imekuja, Msujudieni Yeye aliyezifanya mbingu na nchi na bahari na chemchemi za maji.

kisha nikaona mwingine malaika wa pili akafuata, akisema, Umeanguka umeanguka Babeli mji ule ulio mkubwa maana ndio uliowanywesha mataifa yote mvinyo ya ghadhabu ya uwasherati wake.

Na mwingine malaika wa tatu akawafuata, akisema kwa sauti kuu, Mtu awaye yote akimsujudia huyo mnyama na sanamu yake na kuipokea chapa katika kipaji cha uso wake au katika mkono wake,

Yeye naye atakunywa katika mvinyo ya ghadhabu ya Mungu iliyotengenezwa pasipo kuchanganywa na maji, katika kikombe cha hasira yake naye atateswa kwa moto na kiberiti mbele ya malaika watakatifu na mbele za Mwana-Kondoo.

Na moshi ya maumivu yao hupanda juu hata milele na milele, wala hawana raha mchana wala usiku, hao wamsujuduo huyo mnyama na sanamu yake na kila aipokeaye chapa ya jina lake.

Hapa ndipo penye subira ya watakatifu, hao wazishikao amri za Mungu na imani ya Yesu.

1. Katika ujumbe wa malaika wa kwanza, Mungu Anataka tumtambue Yeye kama muumba wa mbingu na nchi. Hii ndiyo ibada ya Kweli peke yake.
2. Mungu anadai ibada Yake Kwake, Yeye pekee Ndiey anastahili apewe ibada na ibada Yake asipewe mungu mwingine
3. Mungu anataka ategemewe Yeye tu na sio mwanadamu au kitu kingine
   Yeremia 17:5
   Bwana asema hivi, Amelaaniwa mtu yule amtegemeaye mwanadamu, amfanyaye mwanadamu kuwa kinga yake Na moyoni mwake amemwacha Bwana.
4. Kanisa la Mungu lazima limtambue Mwenye kanisa na kuacha ibada za sanamu maana sanamu haiwezi kumiliki kanisa la Kweli
5. Kanisa la Mungu lazima lishike amri za Mungu
6. Kanisa la Mungu lazima Yesu ainuliwe na sio mwanadamu.

Ufunuo 22:17

Na Roho na bibi arusi wasema njoo! Naye asikiaye na aseme njoo! Naye mwenye kiu na aje na yeye atakaye na ayatwae maji ya uzima bure.

1. Mungu anaita watu mbalimbali kutoka makabila yote. Kuna makundi 14,700 duniani na 7400 bado kufikiwa, ikiwemo Waislamu, Hindu, Budha, Wakomunisti, Wayahudi, Shinto, Waabudu mizimu, Confusious na wengineo

Zakaria 13:8,9

Hata itakuwa ya kwamba katika nchi yote mafungu mawili yatakatiliwa mbali na watakufa asema Bwana, lakini fungu la tatu litabaki humo.

Nami nitalileta fungu lile la tatu na kulipitisha kati ya moto, nami nitawasafisha kama fedha isafishavyo, Nami nitawajaribu kama dhahabu ijaribiavyo, wataliita Jina Langu Nami nitawasikia, Mimi nitasema, watu hawa ndio Wangu, nao watasema, Bwana ndiye Mungu Wangu.

1. Leo katika dunia yote kuna makundi matatu makuu ya ibada, jumapili, ijumaa, na jumamosi
2. Kundi la Mungu, Mungu Mwenyewe ana namna ya kutengeneza watu Wake.
3. Kati ya makundi yote matatu, Mungu ana kundi moja tu (kanisa moja tu).

Kanisa linafananishwa na nyumba

Ezekiel 12:2,3

Mwanadamu wewe unakaa kati ya nyumba iliyoasi watu ambao wana macho ya kuona ila hawaoni, wana masikio ya kusikia ila hawasikii, kwa maana ni nyumba iliyoasi.

Basi mwanadamu funga tayari vyombo kwa uhamisho, ukahame wakati wa mchana mbele ya macho yao, nawe ukahame toka mahali pako hapa mpaka mahali pengine mbele ya macho yao, labda watafahamu, wajapokuwa ni nyumba iliyoasi.

1. Kanisa ambalo linafundisha Kweli za Biblia nusu nusu ama haraka
2. Usiogope kuhama, maana kwa kuhama kwako wengi watapokea injili ya Kweli.
3. Kanisa lililoacha amri za Mungu kwa madai kuwa ziligongomelewa msalabani, hilo kanisa limeasi maana mtu huyo kwenye kanisa lake amejiwekea utaratibu wa kufuata, ila inapokuja kwenye Neno la Mungu anadai ziligongomelewa msalabani
4. Hakuna nyumba inayokosa amri, amri ni mwongozo wa nyumba, amri za Mungu ni mwongozo wa kanisa.

Habakuki 2:20

Lakini Bwana Yumo ndani ya hekalu Lake takatifu; dunia yote na inyamaze kimya mbele Zake.

Zaburi 122:1

Nalifurahi waliponiambia, Na twende nyumbani kwa Bwana.

Mungu analo kanisa moja tu ndio maana Mungu hajagawanyika wala hawezi kugawa watu Wake katika imani nyingi zinazotofautiana ni kuendekeza maslahi ya dunia na sio kusaidia watu kwenda mbinguni.

Sura 9

AMRI ZA MUNGU

Ufunuo 14:12

Hapa ndipo penye subira ya watakatifu, hao wazishikao amri za Mungu na imani ya Yesu

1. Amri za Mungu zinaendana na imani ya watakatifu wa Mungu

Yakobo 1:25

Lakini aliyetazama sheria kamilifu iliyo ya uhuru na kukaa humo asiwe msikiaji msahaulifu, bali mtendaji wa kazi, huyo atakuwa heri katika kutenda kwake.

1. Maisha yetu ya uadilifu na uaminifu, Mungu anahitaji tuweke kwenye utendaji
2. Sheria ya Mungu ni ya iari na uhuru, ila ni muhimu sana.

Amri kumi za Mungu ni zipi?

Kutoka 20:1-17

Mungu Akanena maneno haya yote akasema,

Mimi ni Bwana Mungu wako niliyekutoa katika nchi ya Misri katika nyumba ya utumwa.

1

Usiwe na miungu mingine ila Mimi.

2

Usijifanyie sanamu ya kuchonga wala mfano wa kitu chochote kilicho juu mbinguni, wala kilicho chini duniani wala kilicho majini chini ya dunia

Usivisujudie wala kuvitumikia, kwa kuwa Mimi, Bwana, Mungu wako, ni Mungu Mwenye wivu, nawapatiliza wana maovu ya baba zao hata kizazi cha tatu na cha nne cha wanichukiao, Nami nawarehemu maelfu wanipendao na kuzishika amri Zangu.

3

Usilitaje bure Jina la Bwana Mungu wako, maana Bwana hatamhesabia kuwa hana hatia mtu alitajaye Jina Lake bure.

4

Ikumbuke siku ya Sabato, uitakase

Siku sita fanya kazi utende mambo yako yote

Lakini siku ya saba ni Sabato ya Bwana Mungu wako, siku hiyo usifanye kazi yoyote, wewe, wala mwana wako, wala binti yako, wala mtumwa wako, wala mjakazi wako, wala mnyama wako wa kufuga, wala mgeni aliye ndani ya malango yako.

Maana kwa siku sita Bwana alifanya mbingu, na nchi na bahari na vyote vilivyomo, akastarehe siku ya saba kwa hiyo Bwana akaibarikia siku ya Sabato akaitakasa.

5

Waheshimu baba yako na mama yako, siku zako zipate kuwa nyingi, katika nchi upewayo na Bwana Mungu wako.

6

Usiue

7

Usizini

8

Usiibe

9

Usimshuhudie jirani yako uongo

10

Usitamani nyumba ya jirani yako, usimtamani mke wa jirani yako, wala mtumwa wake, wala mjakazi wake, wala ng'ombe wake, wala punda wake, wala chochote alicho nacho jirani yako.

Tazama Amri za Mungu katika katekisimu ya kanisa katoliki ukurasa wa 459

Katekisimu hueleza amri za Mungu katika Biblia kitabu cha kutoka 20:1-17, na kumbukumbu la torati 5:6-21, na Fomula ya mapokeo.

Warumi 14:12

Basi ni hivyo kila mtu miongoni mwetu atatoa habari zake mwenyewe mbele za Mungu

1. Leo hii unasikiliza ya watu lakini siku ya mwisho hakuna atakaye kutetea siku ya hukumu
2. Mbele za Mungu hakuna wakili wala mtetezi
3. Hukumu ya Mungu ni kamilifu.

2 Wakorintho 5:10

Ili kila mtu apokee ijara ya mambo aliyotenda kwa mwili, kadiri alivyo tenda, kwamba ni mema au mabaya.

1. Haya tunayofanya sasa duniani, yote yana mshahara wake.
2. Zuri au baya utalipwa
3. Chochote ufanyalo yatakuja mbele ya kiti cha enzi liwe la utani au sio la utani. Mungu hana utani.
4. Kabla haujaongea na wenzako fikiria kwani hunena yale yaujazayo moyo.

Yakobo 2:10

Maana mtu awaye yote atakayeishika sheria yote, ila akajikwaa katika neno moja, amekosa juu ya yote.

Kushika sheria za Mungu nusu, ni utambulisho wa kuendelea kuupenda dunia,

Yohana 12:32 Nami nikiinuliwa juu ya nchi, nitawavuta wote Kwangu.

Mwinue Yesu juu na sio sanamu ya Yesu.

Aliyetuokoa msalabani ni Yesu na sio msalaba hivyo sio salama kubeba msalaba na kumwacha Yesu.

Matendo ya Mitume 5:29, Petro na mitume wakajibu, wakisema, Imetupasa kumtii Mungu kuliko wanadamu.

Kwanini wewe unang'ang'ania mapokeo ya wanadamu badala ya Neno la Mungu?

Imetupasa kumheshimu Mungu sio na kanisa linalokanyaga Neno la Mungu na kubaki na kubaki kushika mapokeo.

Sura 10

SABATO YA KWELI KATIKA BIBLIA

Mwanzo 2:2

Na siku ya saba alimaliza kazi Yake yote aliyoifanya, akastarehe siku ya saba, akaacha kufanya kazi Yake yote aliyoifanya.

1. Mbingu na nchi na vyote vilivyomo vilifanyika siku ya kwanza mpaka ya siku ya sita
2. Siku ya saba Mungu alipumzika akaacha kazi Zake zote
3. Uumbaji ulikamilika kwa 100%
4. Mungu alibariki siku ya saba
5. Tangu mwanzo wa uumbaji Mungu alianzisha Sabato yaani pumziko siku ya saba

Waebrania 4:1-11

1.Basi ikiwa ikaliko ahadi ya kuingia katika raha Yake, na tuogope mmoja wenu asijeakaonekana ameikosa.

2.Maana ni Kweli sisi nasi, tumehubiriwa habari njema vilevile kama hao, lakini Neno lile lililosikiwa halikuwafaa hao, kwa sababu halikuchanganyika na imani ndani yao waliosikia.

3.Maana sisi tulioamini tunaingia katika raha ile kama vile alivyosema, kama nilivyoapa kwa hasira Yangu hawataingia rahani Mwangu ijapokuwa zile kazi zilimalizika tangu kuwekwa misingi ya ulimwengu.

1. Mungu ametangaza raha kwa watu Wake. Raha ya Mungu sio ya muda mfupi.
2. Kila mtu ajitahidi kuipata
3. Raha hiyo imetangazwa na wahubiri mbalimbali ili watu wasikie sauti ya Mungu.
4. Wengi wanahubiriwa habari njema lakini kwa sababu ya vivutio kwa yale yanayoonekana, basi wanaamua kumtii Shetani kuliko kuliko Mungu.
5. Hili ni agizo sio hiari, mtawala anapotoa agizo, cha kufanya ni kutekeleza na sio kujadili, na mtawala wetu ni Mungu
6. Ikiwa sisi ni watiifu kwa mamlaka ya dunia hii ambayo ina ukomo, basi imetupasa kuwa watiifu zaidi kwa utawala wa mbinguni ambao ni wa milele.

4.Kwa maana imenenwa siku ya saba mahali fulani hivi, Mungu alistarehe siku ya saba, akaziacha kazi Zake zote.

1. Biblia haipingani
2. Kwa kusisitiza utunzaji wa Sabato Paulo ananukuu kauli ya Mungu wakati akiitimisha uumbaji. Mwanzo 2:2.
3. Sabato ni kumbukumbu la uumbaji, inatukumbusha wanadamu asili yetu kuwa tuliumbwa. Ndio maana ni agizo na ni amri na sio ombi la kutii au kutotii.

5.Na hapa napo, hawataingia rahani Mwangu.

6. Basi, kwa kuwa Neno hili limebaki kwamba wako watu watakaoingia humo, na wale waliohubiriwa habari ile zamani walikosa kuingia kwa sababu ya kuasi kwao.

7.Aweka tena siku fulani, akisema katika Daudi baada ya muda mwingi namna hii, Leo, kama ilivyonenwa tangu zamani,

8. Maana kama Yoshua angaliwapa raha, asingalinena siku nyingine baadaye.

1. Wote tumeandikiwa uzima wa milele lakini kuungia katika uzima huo ni hiari
2. Mbele yetu kuna uzima na mauti. Uamuzi ni wako kuchagua.

9. Basi imesalia raha ya Mungu kwa watu wa Mungu.

1. Sabato iliwekwa kwaajili ya watu wa Mungu, na sio watu wengine.
2. Hivyo kila mtu anayejitambua kuwa ni mtu wa Mungu lazima aitunze Sabato.
3. Kutunza Sabato ni kumtangaza Mungu kuwa Yeye Ndiye Muumbaji na Mdumishaji.
4. Sabato iliwekwa kwaajili ya mwanadamu na sio mwanadamu kwaajili ya Sabato.
5. Marko 2:27, 28 *Akawaambia Sabato ilifanyika kwaajili ya mwanadamu, si mwanadamu kwaajili ya sabato. 28. Basi Mwana wa Adamu Ndiye Bwana wa Sabato pia.*
6. Mungu ni mtakatifu, Naye ametuwekea Sabato tuitii.

10. Kwa maana yeye aliyeingia katika raha yake amestarehe mwenyewe katika kazi yake, kama vile Mungu alivyopumzika katika kazi Zake.

11. Basi, na tufanye bidii ya kuingia katika raha ile, ili kwamba mtu yeyote asije akaanguka kwa mfano uo huo wa kuasi.

1. Kuacha kuituinza Sabato ni uasi.
2. Kuacha kutunza sabato ni dhambi kama dhambi zingine katika Amri 10, nakala ya tabia ya Mungu Mwenyewe
3. Ikiwa tunakataa kuwa Sabato ni ya Wayahudi huku tunajiita ni Waisraeli wa kiroho na Wairaeli ndio Wayahudi, basi tunakuwa wanafiki. Warumi 9:6-8

Katekisimu ya kanisa katoliki ukurasa wa 483. Sabato katika utakatifu wake.

Katekisimu ya kanisa katoliki ukurasa wa 484. Badiliko toka Sabato ya Kweli ya Bwana Yesu Kristo kwenda siku ya kwanza ya juma.

Ni miongoni mwa machukizo mbele za Mungu.

Je! Wakolosai 2:16 ina maana gani?

Basi, mtu asiwahukumu ninyi katika vyakula au vinywaji, au kwa sababu ya sikukuu au mwanadamo wa mwezi au Sabato.

1. Kazi ya kuhukumu ni ya Mungu.

2. Kazi yetu tuliyopewa na Mungu ni kufundisha Kweli, kama usipofuata utaukumiwa.

Mitume walifanyaje ugenini?

Matendo 13:44

Hata Sabato ya pili, watu wengi karibu mji wote, wakakusanyika walisikie Neno la Mungu.

1. Mitume na waongofu wapya walikutanika kila sabato kusikiliza Neno la Mungu.
2. Waliendesha ibada zao siku ya Sabato pia.

Mbinguni hali itakuwaje?

Matendo 16:13

Hata siku ya Sabato tukatoka nje ya lango, tukaenda kando ya mto, ambapo tukadhani kuwa pana mahali pa kusali, tukaketi tukasema na wanawake waliokutana pale.

1. Mitume waliitunza Sabato baada ya Yesu kupaa mbinguni.
2. Hata mahali ambapo hakuna kanisa wao walijikusanya siku ya Sabato na kuendesha ibada.
3. Wanawake kwa wanaume waliheshimu ibada takatifu.

Je, Yesu aliitunza Sabato?

Luka 4:16

Akaenda Nazareti hapo alipolelewa na siku ya Sabato akaingia katika sinagogi kama ilivyokuwa desturi Yake, akasimama ili asome.

1. Yesu aliitunza Sabato takatifu
2. Aliendesha ibada siku ya Sabato kanisani.
3. Kawaida ya Yesu tangu utoto wake alikuwapo ibadani siku ya sabato.

Ezekieli 20:12 Tena naliwapa Sabato Zangu, ziwe ishara kati ya Mimi na wao, wapate kujua ya kuwa Mimi, Bwana, Ndimi niwatakasaye.

Ezekieli 20:20 zitakaseni Sabato Zangu; zitakuwa ishara kati ya Mimi na ninyi, mpate kujua ya kuwa Mimi Ndimi Bwana, Mungu wenu.

Sabato ni linki/kiunganishi cha Mungu na watu Wake.

Sabato ni ishara kati ya Mungu na wanadamu.

Mungu anadai uatakaso na heshima kwa Sabato Zake.

Isaya 66:23

Na itakuwa, mwezi mpya hata mwezi mpya, na Sabato hata sabato, wanadamu wote watakuja kuabudu mbele Zangu, asema Bwana.

1. Mbinguni tutaabudu siku ya Sabato.
2. Sabato itaendelea mbinguni.

Matendo ya Mitume 5:29 Petro na mitume wakajibu, wakisema, Imetupasa kumtii Mungu kuliko wanadamu.

Sura 11

IMANI NDANI YA TUFANI (siku ya Sabato)

Imani ni nini?

Waebrania 11:1

Basi imani ni kuwa na hakika ya mambo yatarajiwayo, ni bayana ya mambo yasiyoonekana.

Wale ambao wanamtafuta Yesu japo kwa kupapasa, hebu na watambue mwokozi Yupo karibu nao japo wakati mwingine tunaona Yesu Yupo mbali kwasababu ya tufani tunazopitia.

Matendo ya Mitume 17:27

ili wamtafute Mungu, ingawa ni kwa kupapasa-papasa, wakamwone, ijapokuwa hawi mbali na kila mmoja wetu.

Yesu akikanyaga sehemu, lazima kitu fulani kizuri kitokee

Yesu alipokanyaga Yeriko wokovu ulitokea

Yeriko ni eneo la Palestina, magharibi ya bonde la mto Yordani, mashariki kuna Yerusalemu.

Maana ya Neno Yeriko ni manukato yenye kunukia vizuri.

Luka 19:1-7

Naye alipoingia Yeriko alipita katikati yake.

1. Katikati ya umati Yesu Yupo. Yesu alijichanganya na watu Wake.

2. Yeriko ilikaliwa na wapagani wanaojua dini mafarisayo, waliojiona bora kuliko wengine. Bora ukutane na mpagani asiyejua dini kuliko kukutana na mpagani anayejua dini.

3. Waliweka mpaka kwa watu watakaoingia mbinguni

Luka 19:2- Na tazama palikuwa na mtu, jina lake Zakayo, mkubwa mmoja katika watoza ushuru, naye ni tajiri.

1. Zakayo maana yake ni usafi au mwadilifu.

2. Zakayo alikuwa mtu maarufu katika serikali ya Kiyahudi, fisadi, asiye na huruma.

3. Zakayo alikuwa mkubwa wa umri lakini alikuwa amedumazwa na dhambi.

Huyu alikuwa akitafuta kumwona Yesu ni Mtu wa namna gani, asiweze kwa sababu ya umati wa watu, maana ni mfupi wa kimo.

1. Roho Mtakatifu aliingia ndani yake.

2. Akaanza kumtafuta Yesu kwa bidii.

3. Umati, yaani waumini wenzake walimzuia asiende kwa Yesu maana yeye ni mdhambi sana.

4. Pamoja na kuzuiliwa bado alibuni njia zingine za kumwona Yesu.

5. Imani yake na Roho mtakatifu aliyekuwa ndani yake Zakayo ndio vilimwongoza cha kufanya.

Akatangulia mbio, akapanda juu ya mkuyu apate kumwona, kwa kuwa atakuja kupitia njia ile.

1. Zakayo akaenda mbio mbele akijuaYesu anapatikana wapi.

2. Waliompokea Yesu hawakatishwi tamaa na washiriki au na mtu yeyote

3. Usiogope umati, Yesu Yupo

4. Wakati wenzako wanang'ang'ania dunia, hii wewe tazama juu.

5. Wakimtafuta Yesu chini wewe mtafute Yesu juu. Zaburi 121:1. Nitayainua macho yangu nitazame milima, Msaada wangu utatoka wapi?

6. Ukikatishwa tamaa na watu, Yesu atakutia moyo

Na Yesu, alipofika mahali pale, alitazama juu, akamwambia, Zakayo, shuka upesi, kwa kuwa leo imenipasa kushinda nyumbani mwako.

1. Kamwe anayemtafuta Yesu hawezi kuachwa.
2. Yesu atakufuata ulipo
3. Yesu anakutembelea bila kuangalia hali yako
4. Wakati watu wanaangalia ulivyochafuka Yesu anaangalia utakavyokuwa msafi
5. Yesu analeta utakaso kwa watu Wake, Yesu Yupo kutakasa watu Wake.

Akafanya haraka, akashuka, akamkaribisha kwa furaha

Hata watu walipoona, walinung'unika wote, wakisema, Ameingia kukaa na mtu mwenye dhambi.

1. Kilichotawala ni chuki na wivu dhidi ya Zakayo.
2. Sio kila mtu atafurahia ubatizo wako, hata wa nyumbani mwako wanaweza wasifurahi.
3. Wakitazama dhambi zako, Yesu ana tazama utakatifu wako.

Kumbukumbu la Torati 3:23, 24.

23 Nikamnyenyekea Bwana wakati huo, nikamwambia,

24 Ee Bwana Mungu, umeanza kumwonyesha mtumishi wako ukubwa wako, na mkono wako wa nguvu; kwani kuna mungu gani mbinguni au duniani awezaye kufanya mfano wa kazi zako, na mfano wa matendo yako yenye nguvu?

Sura 12

SHERIA ZA MUSA NA ZA MUGU

Warumi 10:4

Kwa maana Kristo ni mwisho wa sheria ili kila aaminiye ahesabiwe haki.

1. Neno 'mwisho' kwa lugha ya asili ya Biblia kilatini ni 'telos' ambayo ina maana kiini au lengo.
2. Hivyo sasa twaweza kusema Kristo ni kiini cha sheria. Kristo ni Mwasisi wa sheria
3. Hivyo Yesu hawezi kuipinga sheria Yake Mwenyewe.

Warumi 7:7

Tusemeje basi torati ni dhambi? Hasha nisingalitambua dhambi ila kwa njia ya sheria, kwa kuwa nisingalijua kutamani kama torati isingalisema usitamani.

1. Kama tukichunguza Maandiko matakatifu, hasa wakati Yesu Mwenyewe anazungumzia kuhusu sheria, haitakuwa ngumu kuelewa lengo
2. Kuikataa sheria ni kumkataa Mwenye sheria ambaye ni Yesu
3. Dhambi ipo kwasababu ya sheria
4. Bila sheria hakuna dhambi

Yesu anasemaje kuhusu sheria?

Mathayo 5:17

Msidhani ya kuwa nalikuja kuitangua sheria au manabii la sikuja kutangua bali kuitimiliza.

1. Shida yetu leo tunasoma Biblia kwa kulinda maslahi yetu au kulinda yale tuliyopandikiziwa zamani.
2. Biblia inajitosheleza haihitaji kukosolewa na kitabu cha ziada

Yohana 14:15

Mkinipenda mtazishika amri Zangu

1. Upendo wa Kristo watusukuma/watubidisha kujua sheria za Mungu na kuziishi.
2. Kipimo chetu Kwake huonekana kwa namna tunavyompenda.

Zaburi 19:7

Sheria ya Bwana ni kamilifu huiburudisha nafsi. Ushuhuda wa Bwana ni amini, humtia mjinga hekima.

1. Jambo kutoka mbinguni hatujadili.
2. Yesu akiwa ndani yako, sheria Yake huwa laini kwetu
3. Mjinga aliyeshika sheria ya Bwana, ujinga hutoweshwa na hekima kutawala, anakuwa na akili mahiri kuliko mtu yeyote anayeaminika kwamba ana akili nyingi duniani-genius.

Yakobo 4:12

Mtoa sheria na Mwenye kuhukumu ni Mmoja tu, Ndiye awezaye kuokoa na kuangamiza, u nani wewe uukumuye mtu mwingine.

1. Mhukumu ni Mungu pekee
2. Hakuna mwanadamu mwenye nafasi ya kuhumu

Danieli 9:11

Naam, Israeli wote wameihalifu sheria Yako, kwa kugeuka upande, wasiisikilize sauti Yako, basi kwa hiyo laana imemwagwa juu yetu, na uapo ule ulioandikwa katika sheria ya Musa mtumishi wa Mungu, kwa sababu tumemtenda dhambi.

1. Kuacha sheria ya Mungu ni kuleta laana katika jamii
2. Dunia yetu leo imechafuka sana kwa sababu sheria ya Mungu imeachwa
3. Sheria za Musa zilikuwepo ili kulinda sheria ya Mungu.

Zaburi 119:1

Heri walio kamili katika njia zao, waendao katika sheria ya Bwana

1. Heri kwa washikao sheria ya Bwana, imeandikwa mara nyingi katika Biblia.

Wagalatia 6:2

Mchukuliane mizigo na kuitimiza hivyo sheria ya Kristo

1. Kristo alikuwa na sheria Zake
2. Sheria ina umuhimu maishani.
3. Kuchukuliana mizigo ni pamoja na kusaidiana kwa kufundishana na kukumbushana sheria ya Mungu

Wagalatia 2:19

Maana mimi kwa njia ya sheria naliifia sheria ili nimwishie Mungu.

Ishi kwa mpango wa Mungu na kwa utaratibu wa Mungu.

Sura 13

KUZALIWA UKUBWANI

Yohana 3:3, 4

Yesu akajibu, akamwambia, amin, amin, nakuambia, mtu asipozaliwa mara ya pili, hawezi kuuona ufalme wa Mungu.

Nikodemo akamwambia, Awezaje mtu kuzaliwa akiwa mzee? Aweza kuingia tumboni mwa mamaye mara ya pili akazaliwa?

Yohana 3:5 Yesu akajibu, Amin, amin, nakuambia, Mtu asipozaliwa kwa maji na kwa Roho, hawezi kuuingia ufalme wa Mungu.

1. Yesu anatoa utaratibu wa kuingia mbinguni.
2. Sharti uzaliwe mara ya pili

3. Kuzaliwa mara ya pili wapaswa uzaliwe ukiwa na utambuzi, na ufanye maamuzi mwenyewe ya kuzaliwa tena.
4. Mungu Ana uwezo wote.
5. Ubatizo ni muhimu ili tuweze kuingia mbinguni.

Ubatizo ina maana gani?

Warumi 6:3, 4.

Hamfahamu kuwa ya kuwa sisi sote tuliobatizwa katika Kristo Yesu tulibatizwa katika mauti Yake?

Basi tulizikwa pamoja Naye kwa njia ya ubatizo katika mauti Yake, kusudi kama Kristo alivyofufuka katika wafu kwa njia ya utukufu wa Baba, vivyo hivyo na sisi tuenende katika upya wa uzima.

1. Tunabatizwa katika Kristo Yesu
2. Maana ya ubatizo ni kushiriki mauti ya Kristo Yesu
3. Maana ya pili ya ubatizo ni alama ya kuzikwa pamoja na Kristo
4. Tunapozamishwa ndani ya maji, tunazika dhambi, na kutoka ndani ya maji tukiwa kiumbe kipya
5. Maana nyingine ya ubatizo ni kuzaliwa mara ya pili.
6. Maana ya ubatizo ni kuzamisha.

Matendo ya mitume 22:16

Basi sasa, unakawilia nini? Simama, ubatizwe, ukaoshe dhambi zako, ukiliitia Jina Lake.

1. Maana nyingine ya ubatizo ni kuosha dhambi.
2. Tunapobatizwa tunabatizwa kwa Jina la Yesu.
3. Ubatizo ni wewe mwenyewe ufanye maamuzi usimame ukabatizwe

Marko 16:15, 16.

Akawaambia, Enendeni ulimwenguni mwote, mkahubiri injili kwa kila kiumbe.

Aaminiye na kubatizwa ataokoka, asiyeamini ataukumiwa.

1. Kwanza mtu ajifunze aelewe kwanini anabatizwa ndipo abatizwe
2. Injili ihubiriwe kote ili watu wamjue Yesu.
3. Mwenye sifa ya kubatizwa ni aliyeamini tu.
4. Asiyeamini ataukumiwa maana ubatizo ina umuhimu wake.

Matendo 2:38 Petro akawaambia, Tubuni mkabatizwe kila mmoja kwa Lina Lake Yesu Kristo, mpate ondoleo la dhambi zenu, nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu.

Ubatizo unafuatana na toba. Ili tupate uwezo wa Roho Mtakatifu sharti tukubaliane na ubatizo

Matendo 8:35-38

Filipo akafunua kinywa chake, naye, akianza na andiko lilo hilo, akamhubiri habari njema za Yesu.

Wakawa wakiendelea njiani, wakafika mahali penye maji, yule towashi akasema, Tazama, maji haya, ni nini kinachonizuia nisibatizwe?

Filipo akasema, ukiamini kwa moyo wako wote, inawezekana, Akajibu akanena, Naamini ya kwamba Yesu Kristo Ndiye mwana ya Mungu.

Akaamuru lile gari lisimame, wakatelemka wote wawili majini, Filipo na yule towashi, naye akambatiza.

1. Kabla ya ubatizo mtu aelezwe kweli za Biblia
2. Mungu anamtuma Filipo kwenda kumhubiri towashi
3. Towashi anahubiriwa wakiwa safarini ndani ya gari
4. Towashi alipoamini walifika kwenye maji akaomba ubatizo
5. Kabla ya ubatizo sharti uamini
6. Towashi alimkiri Yesu kuwa ni Bwana na mwokozi wa maisha yake akabatizwa
7. Walishuka chini wakaingia ndani ya maji, na akabatizwa
8. Filipo akawa amemaliza kazi yake

Yesu ni kielelezo chetu maishani, Yeye alibarikiwa akiwa mtoto.

Luka 2:25-34

Natazama pale Yerusalemu palikuwa na mtu, jina lake Simeoni, naye ni mtu mwenye haki, mcha Mungu, akitarajia faraja ya Israeli, na Roho Mtakatifu alikuwa juu yake.

Naye alikuwa ameonywa na Roho Mtakatifu ya kwamba hataona mauti kabla ya kumwona Kristo wa Bwana.

Basi akaja hekaluni ameongozwa na Roho, na wale wazazi walipomleta mtoto ndani, ili wamfanyie kama ilivyokuwa desturi ya sheria.

Yeye mwenyewe alimpokea mikononi mwake, akamshukuru Mungu akisema,

Sasa, Bwana wamruhusu mtumishi wako, kwa amani, kama ulivyosema,

Kwa kuwa macho yangu yameuona Wokovu wako.

Uliouweka tayari machoni pa watu wote,

Nuru ya kuwa mwangaza kwa mataifa, na kuwa utukufu wa watu Wako Israeli

Na babaye na mamaye walikuwa wakistaajabia hayo yaliyonenwa juu yake.

Simeoni akawabariki, akamwambia Mariamu mama yake, tazama, huyu amewekwa kwa kuanguka na kuinuka kwa wengi walio katika Israeli, na kuwa ishara itakayonenewa.

1. Simeoni alikuwa kuhani aliyejitoa kikamilifu kumtumikia Yesu.
2. Simeoni alipata kibali machoni pa Mungu
3. Aliahidiwa kumwona Masihi kabla ya kufa kwake.
4. Mungu alimwandaa kwa njia maalum, kwaajili ya kazi yake kabla ya kufa.
5. Wewe hautakufa mpaka Yesu atimize mapenzi Yake ndani yako.
6. Simeoni aliandaliwa kwa kazi ya kumbariki Yesu tu, kisha akalala usingizi wa mauti.
7. Mstari wa 34, Simeoni alimweka Yesu wakfu akiwa mtoto mchanga
8. Watoto hawabatizwi bali wanabarikiwa wakiwa wachanga.

Yesu alibariki watoto

Marko 10:15, 16.

Amin, nawaambieni, Yeyote asiyeukubali ufalme wa Mungu kama mtoto mdogo hatauingia kabisa.

Akawakumbatia, akaweka mikono Yake juu yao, akawabarikia.

1. Yesu alibariki watoto
2. Hakuwabatiza maana watoto hawabatizwi.
3. Watoto hawajui jambo lolote baya wala zuri, hawawezi kufundishwa mambo na kuyashika yote.

Ubatizo wa Yesu.

Mathayo 3:13-16

Wakati huo Yesu akaja kutoka Galilaya mpaka Yordani kwa Yohana ili abatizwe.

Lakini Yohana alitaka kumzuia, akisema, Mimi nahitaji kubatizwa na wewe, Nawe waja kwangu?

Yesu akajibu akamwambia, kubali hivi sasa kwakuwa ndivyo itupasavyo kuitimiza haki yote. Basi akamkubali.

Naye Yesu alipokwisha kubatizwa mara akapanda kutoka majini na tazama, mbingu zikamfunukia, akamwona Roho wa Mungu akishuka kama hua, akija juu Yake.

1. Ubatizo wa Yesu ulifanyika akiwa ameshakuwa mtu mzima.
2. Yesu alienda mwenyewe kufuata ubatizo.
3. Ubatizo ni kuzika dhambi Yesu alienda kutuonyesha kielelezo ili tufuate.
4. Baada ya ubatizo Roho mtakatifu huja juu yako.

Yohana 3:23

Yohana naye alikuwa akibatiza huko Ainoni, karibu na Salimu kwasababu huko kulikuwa na maji tele, na watu wakamwendea, wakabatizwa.

1. Yohana aliendelea kubatiza sehemu mbalimbali
2. Ubatizo sio lazima mto Yordani bali popote penye maji mengi.
3. Ubatizo ni kukiri imani yako adharani.

Katekisimu ya kanisa katoliki.

Uk 297, 298, 300, 303, 304

Sakramenti Hii Inaitwaje?

1214 Huitwa *ubatizo* kutokana na madhehebu ya msingi ambayo kwayo unafanyika: kubatiza (kwa Kigiriki *baptizein)* humaanisha ‘kutumbukiza’ au ‘kuzamisha’ ndani ya maji alama ya maziko mkatekumeni katika mauti ya Kristo ambamo anafufuka pamoja naye ambaye ni kiumbe kipya.

Sura 14

Vita dhidi ya kweli za Mungu

Dunia imepiga hatua kubwa ya kimaendeleo, mavumbuzi juu ya anga, mavumbuzi hapa duniani, mavumbuzi chini ya dunia, mavumbuzi ndani ya maji, yote hayo yanamfanya mwanadamu ajione yeye ni bora zaidi na mwanadamu kwa sababu ya maendeleo hayo anajitafutia utukufu wake mwenyewe.

Danieli 12:4

Lakini wewe, Ee Danieli, yafunge maneno haya, ukakitie muhuri kitabu, hata wakati wa mwisho, wengi wataenda mbio huko na huko, na maarifa yataongezeka.

Kiburi na chuki vitatawala kila kona, tetesi ya vita pande zote.

Mathayo 24:6

Nanyi mtasikia habari za vita na matetesi ya vita, angalieni msitishwe, maana hayo hayana budi kutukia lakini ule mwisho bado.

1. Maendeleo hayo ya mwanadamu yatapelekea kiburi na majivuno kutawala.
2. Jambo litakalofanya vita katika kona zote za dunia
3. Msumbji, Somalia, Congo, Nigeria, Sudan, Chad, makundi ya kigaidi vimekuwa tishio ulimwenguni mwote.
4. Matukio yote hayo ni sababu ya kiburi cha maendeleo.

Danieli 7:25

Naye atanena kinyume chake Aliye juu, naye atawadhoofisha watakatifu wake Aliye juu, naye ataazimu kubadili majira na sheria, nao watatiwa mikononi mwake kwa wakati na nyakati mbili, na nusu wakati.

1. Mwanadamu hujikweza na kujifananisha na Mungu.
2. Leo sabato imebadilishwa na kuwa jumapili, ni sehemu ya kiburi cha mwanadamu.
3. Miungu mingine itapewa kipaumbele badala ya Mungu wa mbinguni.
4. Shetani anashambulia sheria ya Mungu na kuakikisha anabadilisha kila kitu.

kuna maneno katika biblia yakupasa ufahamu maana yake.

Babeli ni dini ya machafuko.

Ufunuo 18:1-4

1. *Mnyama ni utawala, ufalme, serikali, nguvu ya kisiasa. Danieli 7:17.*
2. *Upepo ni vita au misuguano. Yeremia 49:32.*
3. *Namba 3 ni namba ya ukamilifu au umoja. Mathayo 28:19.*

Danieli 2:1-3

Hata katika mwaka wa pili wa kumiliki kwake Nebukadreza aliota ndoto na roho yake ikamwacha.

Ndipo mfalme akatoa amri ya kuwaita waganga, na wachawi na wasihiri, na wakaldayo, wapate kumweleza mfalme ndoto zake, basi wakaingia wakasimama mbele ya mfalme.

Mfalme akawaambia nimeota ndoto na roho yangu imefadhaika hata niijue tafsiri yake

1. Shetani hajui yaliyomo ndani yako mpaka umruhusu akutawale
2. Mfalme anahitaji tafsiri ya ndoto ambayo hajaisimulia anataka wenye nguvu giza wamweleze

Utawala wa kidini ulioshikamana na utawala wa serikali.

Ndio uliobadilisha sabato ya Mungu na kuacha sabato ya Bwana

Danieli 7:25

Naye atanena maneno kinyume chake Aliye juu, naye atawadhoofisha watakatifu wake Aliye juu, naye ataazimu kubadili majira na sheria, nao watatiwa mikononi mwake kwa wakati, na nyakati mbili, na nusu wakati.

1. Mafundisho mengi potofu yanafundishwa katika nyumba nyingi za ibada.
2. Mafundisho hayo yamekaa kana kwamba ni ya kiroho, kumbe ni silaha ya yule mwovu shetani.

Wameliacha sheria ya Mungu yaliyowasonda dhambi.

Amri ya pili ya Mungu wameiacha na amri ya kumi wameigawa mara mbili.

Kutoka 20:4-6 imeachwa kabisa.

Kutoka 20:17 imegawanywa mara mbili.

Sheria ya Mungu imeachwa kando. Na viongozi wamejitengenezea sheria zao

Vita kubwa ni sheria ya Mungu.

Ubatizo umebadilishwa na watu kujitengenezea ubatizo wao.

Wakaldayo wakajibu mbele ya mfalme, wakasema, hapana mtu duniani awezaye kulionyesha neno hili la mfalme, kwa maana hapana mfalme, wala bwana wala liwali, aliyetaka neno kama hili kwa mganga, wala kwa mchawi, wala kwa mkaldayo.

Ni neno la ajabu, hili analotaka mfame, wala hapana mwingine awezaye kumwonyesha mfalme neno hilo, ila miungu, wasiona na kikao pamoja na wenye mwili.

1. Mfalme alitegemea waganga wa kienyeji, jambo ambalo halikumsaidia.
2. Kuna mambo hayawezekani kwa nguvu za kibinadamu wala kwa nguvu za mwovu shetani.
3. Hekima ya mwanadamu ni upumbavu mbele za Mungu 1Wakorintho 1:25

Danieli 2:16.

Basi Danieli akaingia, akamwona mfalme ampe muda, kisha yeye atamwonyesha mfalme tafsiri ile.

Sura ya 15

MAOMBI NA UMUHIMU WAKE

Maombi ni njia ya sisi wanadamu kuongea na Mungu kwa kueleza haja zetu, kumsifu, kujitakasa. Maombi ya mara kwa mara ni njia ya kufanya mahusiano ya karibu na Mungu.

Ili maombi yako yawe ya hakika na uwe mtu aliyekomaa kiroho basi usomaji wa neno la Mungu (Biblia) lazima ziendane na kama hujui kusoma au una matatizo ya macho una paswa kutenga muda wa kusikiliza Neno mara kwa mara. Usomaji wa Neno na maombi ni mapacha.

Siri ya ushindi wa Yesu ilikuwa ni kuomba sana.

Marko 1:35

Hata alfajiri na mapema sana akaondoka, akatoka akaenda zake mahali pasipokuwa na watu, akaomba huko.

Yesu pamoja na uungu aliokuwa na akaja duniani kama mwanadamu akaomba tena alijinyima usingizi ili aombe kwa bidi.

Kuomba wakati mwingine inagharimu kama ilivyomgharimu Yesu akaomba mpaka jasho la damu.

Luka 22:44

Naye kwa vile alivyokuwa katika dhiki, akazidi sana kuomba; hari yake ikawa kama matone ya damu yakidondoka nchini.

Mwisho wa ombi malaika walishuka kumfariji. Kwa tukio kubwa lililokuwa mbele yake yaani msalaba.

Ushindi dhidi ya dhambi sio kwasababu tuna msimamo dhabiti ila kwa kukubali kuomba kwa bidi ili Mungu atushindie.

Mathayo 26:41

Kesheni, mwombe, msije mkaingia majaribuni; roho i radhi, lakini mwili ni dhaifu.

Njia ya kushinda majaribu ya adui Shetani ni kuomba.

Niombe mpaka lini ili Mungu anijibu?

1 Wathesalonike 5:17

Ombeni bila kukoma;

Omba sana hata kama unaona Mungu amenyamaza kimya wewe omba bila kukoma.

Manabii na mitume waliomba.

1 Wafalme 18:36-39 Eliya aliomba moto ukashuka toka mbinguni.

Sio lazima Mungu ajibu maombi yetu tunavyotaka, maana hata Daudi aliomba na kufunga ili mtoto apone lakini mtoto alikufa.

Kila anapoomba kubali pia mapenzi ya Mungu yatimizwe.

2 Samweli 12:16. Basi Daudi akamwomba Mungu kwa ajili ya mtoto; Daudi akafunga, akaingia, akalala usiku kucha chini.

2 Samweli 12:19. Lakini alipoona ya kuwa watumishi wake wananong'onezana, Daudi alitambua ya kuwa mtoto amekufa; basi Daudi akawauliza watumishi wake, Je! Mtoto amekufa? Nao wakasema, Amekufa.

Daudi alipokea kitu ambacho hakutaka kabisa maishani mwake.

Katika kuomba tukumbuke sala ya Bwana inayosema mapenzi yako yatimizwe. Mungu kunyamaza bila kujibu ombi lako wakati mwingine sio kwamba hauna imani bali hekima ya jibu la Mungu ni kunyamaza kimya kwaajili ya faida yako wewe mwombaji.

Mathayo 26:39 Akaendelea mbele kidogo, akaanguka kifulifuli, akaomba, akisema, Baba yangu, ikiwezekana, kikombe hiki kiniepuke; walakini si kama nitakavyo mimi, bali kama utakavyo wewe.

Yesu akiwa katika mateso makali akielekea Goligotha akaumia sana, kama binadamu akaomba akitaka Baba amwondoe kwenye yale maumivu. Lakini hayo maumivu na kifo chake ndio ukombozi wetu. Kama Mungu angemjibu Yesu alivyoomba basi hadi leo huduma ya kupeleka wanyama kwaajili ya ondoleo la dhambi ingeendelea.

Ukimya wa Mungu ndio ukombozi wa mwanadamu.

Yesu anasema sio nitakavyo mimi bali kama utakavyo wewe. Tusimlazimishe Mungu kufanya kile ambacho hataki kufanya.

Kumbuka Yeye anatazama mwisho kabla ya mwanzo.

Ayubu 41:34 Yeye hutazama kila kitu kilicho juu; Ni mfalme juu ya wote wenye kiburi.

Kumlazimisha Mungu kufanya Yetu ni kiburi hivyo maombi mengi Mungu hasikii kwasababu ya kiburi.

Nani aniombee ili Mungu asikie?

Waebrania 10:19 Basi, ndugu, kwa kuwa tuna ujasiri wa kupaingia patakatifu kwa damu ya Yesu,

Kwenda kwa Yesu kuomba ni kila mtu anakibali cha kuombambele za Yesu Kristo kwani Yeye ndiye kuhani wetu, swala la kusema lazima tuombe kupitia kwa kiongozi wangu wa dini ni kumtukuza mwanadamu kuliko Yesu.

Kuomba kupitia wazee wa imani walikwisha lala mauti au mtu yoyote aliyekufa hata kama alilala katika Kristo basi hayo maombi ni kuomba katika umizimu na sio kwa katika Kristo.

Ili maombi yetu yajibiwe Yesu anasemaje?

Yohana 14:13,14 Nanyi mkiomba lo lote kwa jina langu, hilo nitalifanya, ili Baba atukuzwe ndani ya Mwana.

14 Mkiniomba neno lo lote kwa jina langu, nitalifanya.

Maombi ni sehemu ya mahusiano na Mungu hivyo Mungu anahitaji twende kwake tumwombe kwa jina lake Yesu. Wale wanaotegemea siku zote kuombewa na wenzao wanajinyima nafasi ya kukaribia msalaba wa Yesu wao wenyewe na kukosa urafiki na Yesu.

NDOA NA FAMILIA

Ndoa ni fundisho la biblia linalohitaji umakini mkubwa kwani maana ya ndoa imeondolewa katika familia nyingi.

Ndoa ni ya watu gani?

Marko 10:6 Lakini tangu mwanzo wa kuumbwa ulimwengu, aliwafanya mume na mke.

Ndoa lazima iwe ya jinsia mbili tofauti. Mume na mke hao wawili ndio ndoa. Biblia haisemi aliwafanya waume na wake au mume na wake.

Mwanzo 2:21 Bwana Mungu akamletea Adamu usingizi mzito, naye akalala; kisha akatwaa ubavu wake mmoja, akafunika nyama mahali pake,

Mwanzo 2:22 na ule ubavu alioutwaa katika Adamu Bwana Mungu akaufanya mwanamke, akamleta kwa Adamu.

1. Huduma ya upasuaji wa kwaza ilifanywa na Mungu ili kukamilisha kumuumba mwanadamu.
2. Mungu aliumba wawili jinsia mbili tofauti na hii ndio ndoa ya kwanza iliyofungwa na Mungu mwenyewe.
3. Mungu alimuumba Adamu akiwa mtu mzima na Hawa akiwa mtu mzima na hivyo hakuna ndoa ya utotoni wala manabii na mitume na wazee wa imani hakuna waliofunga ndoa za utotoni

Mwanzo 2:23 Adamu akasema, Sasa huyu ni mfupa katika mifupa yangu, na nyama katika nyama yangu, basi ataitwa mwanamke, kwa maana ametwaliwa katika mwanamume.

1. Adamu alimpokea Hawa kama mke wake maana walifanana kila kitu isipokuwa mfumo wa uzazi.
2. Kila mmoja aliumbwa kuwa mvuto kwa mwenzake ili kuimarisha upendo wao kwa wao.
3. Baada ya kuoana wanandoa wanakuwa mwili mmoja ndio maana ya kusema ni mifupa katika mifupa yangu na nyama katika nyama yangu.

Mwanzo 2:24 Kwa hiyo mwanamume atamwacha baba yake na mama yake naye ataambatana na mkewe, nao watakuwa mwili mmoja.

1. Wale wanaoanzisha ndoa ina maana wanaanzisha maisha wao wawili bila wazazi wala walezi wala waangalizi wa ndoa.
2. Sababu ya msingi ya kuingia kwenye ndoa ni kuwa wote wawili mmekomaa kiakili, kimaumbile, hivyo wanapaswa waondoke kwenye imaya ya wazazi au walezi wakaanzishe maisha yao hata kama wakikaa jirani na wazazi basi wawe na maisha yao.
3. Wazazi na walezi fundisheni vijana wa kike na wa kiume kazi za mikono na namna ya kuja kutunza ndoa kabla ya ndoa maana baada ya ndoa hautakuwa na muda wa kuwafundisha.
4. Mara nyingi wanaume hawawachi wazazi wao bali wanawapeleka wake zao kukaa na wazazi wao jambo ambalo Mungu amekataa.
5. Mama mkwe kamwe hauwezi kumfundisha mke wa kijana wako kama hakufundishwa kwao.

Mwanzo 2:25 Nao walikuwa uchi wote wawili, Adamu na mkewe, wala hawakuona haya.

1. Wanandoa waliooana kwa utaratibu hawapaswi kuoneana aibu kwa sababu Mungu anabariki ndoa yao.
2. Ndoa ni takatifu ikichukuliwa kwa utaratibu, usafi, na utukufu wa Mungu.

2 Wakorintho 6:14 Msifungiwe nira pamoja na wasioamini, kwa jinsi isivyo sawasawa; kwa maana pana urafiki gani kati ya haki na uasi? Tena pana shirika gani kati ya nuru na giza?

Funga ndoa na mtu mnaye fanana kwa imani ili kuondoa migogoro isiyo ya lazima pia kuepuka uasi kati yenu.

Kubadilisha imani kwaajili ya mwenzi sio kusudi la injili. Ila kubadilisha imani kwaajili ya Kristo ndio kusudi la injili.

Waebrania 13:4 Ndoa na iheshimiwe na watu wote, na malazi yawe safi; kwa maana waasherati na wazinzi Mungu atawahukumia adhabu.

1. Jamii inapaswa iheshimu ndoa zinazowazunguka na wanandoa wenyewe waheshimu ndoa yao.
2. Mwanandoa usiruhusu uzinzi wala usiruhusu viashiria vya uzinzi katika ndoa yako.
3. Matumizi ya ndoa uasherati usiruhusiwe.
4. Migogoro mingi ndani ya ndoa ni uzinzi na viashiria vya uzinzi.
5. Jambo lingine kubwa linaloleta migogoro ndani ya ndoa ni kuleta kunyimana tendo la ndoa. *1 Wakorintho 7:5 Msinyimane isipokuwa mmepatana kwa muda, ili mpate faragha kwa kusali; mkajiane tena, Shetani asije akawajaribu kwa kutokuwa na kiasi kwenu.*

Warumi 1:26 Hivyo Mungu aliwaacha wafuate tamaa zao za aibu, hata wanawake wakabadili matumizi ya asili kwa matumizi yasiyo ya asili;

1. Ni kosa na chukizo mbele za Mungu kumgeuza mwanamke kinyume na maumbile yake, hata kama ni wanandoa na hii ni uchafu mkubwa ndani ya ndoa.
2. Mwanamke anapaswa kumtii mume wake ila sio katika kuingiliwa kinyume na maumbile yake wewe mwanamke kataa, na kukataa kwako itakusaidia kuondoa laana ndani ya familia yako.
3. Kila kiungo Mungu ameumba ndani ya miili yetu ikiwa na kazi yake, hivyo acha kubadilisha kazi ya viungo vyako.

Hakuna ndoa ya jinsia moja.

Warumi 1:27 wanaume nao vivyo hivyo waliyaacha matumizi ya mke, ya asili, wakawakiana tamaa, wanaume wakiyatenda yasiyopasa, wakapata nafsini mwao malipo ya upotevu wao yaliyo haki yao.

Kamwe hakuna ndoa ya jinsia moja, ndoa ya jinsia moja ni kumvaa shetani ndani ya miili ya hao wanaoendekeza ndoa hiyo.

1 Wakorintho 6:9 Au hamjui ya kuwa wadhalimu hawataurithi ufalme wa Mungu? Msidanganyike; waasherati hawataurithi ufalme wa Mungu, wala waabudu sanamu, wala wazinzi, wala wafiraji, wala walawiti,

Mithali 5:18 Chemchemi yako ibarikiwe; Nawe umfurahie mke wa ujana wako.

1. Fanya ndoa yako iwe na furaha,
2. Fanya ndoa yako iwe kituo cha ibada.
3. Fanya ndoa yako kuwa kituo cha malezi ya familia.
4. Baba mfanye mke wako awe mwenye furaha na mama mfanye mume wako awe mwenye furaha.
5. Mpeane faraja hata kama kuna maumivu makubwa ndani ya ndoa basi kila mmoja aone faraja ni mwenzi wako.

Malaki 2:15 Hakuna mtu mmoja aliyetenda hivi, ambaye alikuwa na ufahamu kidogo. Au je! Kuna mtu mmoja atafutaye mzao mwenye kumcha Mungu? Kwa hiyo jihadharini roho zenu; mtu awaye yote asimtende mke wa ujana wake mambo ya hiana.

Mthamini mke wako hata kama amezeeka, hata kama hajabahatika kupata mtoto hata kama amepata ugonjwa utakaodumu maisha yake yote, bado Mungu ni shahidi kwa mke wa ujana wako.

Mke ni zawadi toka kwa Bwana.

Mithali 18:22 Apataye mke apata kitu chema; Naye ajipatia kibali kwa Bwana.

Anayempiga mke wake sio tu kwamba anamdhalilisha mke wake lakini pia anamkosea Mungu.

Anayempiga mume wake sio tu kwamba anamdhalilisha mume wake lakini pia anamkosea Mungu.

Usimpige mke maana yeye sio mtoto, ndio maana mlioana wote ni watu wazima.

Katika ndoa Mungu anaweza kuwajalia watoto kama sehemu ya familia yenu.

Watoto hao wanapaswa walelewe vizuri kiroho na kimwili wazazi wakiwa kielelezo bora kwa familia yao.

Sasa mtoto afundisheje kiroho?

Kumbukumbu la Torati 6:4-9. Sikiza, Ee Israeli; Bwana, Mungu wetu, Bwana ndiye mmoja.

5 Nawe mpende Bwana, Mungu wako, kwa moyo wako wote, na kwa roho yako yote, na kwa nguvu zako zote.

6 Na maneno haya ninayokuamuru leo, yatakuwa katika moyo wako;

7 nawe uwafundishe watoto wako kwa bidii, na kuyanena uketipo katika nyumba yako, na utembeapo njiani, na ulalapo, na uondokapo.

8 Yafunge yawe dalili juu ya mkono wako, nayo yatakuwa kama utepe katikati ya macho yako.

9 Tena yaandike juu ya miimo ya nyumba yako, na juu ya malango yako.

1. Mungu anatoa sheria, amri, na hukumu zake kwa taifa lake Israeli.
2. Maagizo wanalopewa ni kuzitunza na kuzishika lakini pia kuwafundisha watoto maagizo ya Mungu.
3. Wayahudi tangu mwanzo walijua kurithisha watoto wao neno la Mungu katika mioyo yao.
4. Anaposema yaandikwe juu ya miimo ya nyumba ni kwamba hata wageni wanaotutembelea katika nyumba zetu wamwone Yesu kupitia familia zetu.
5. Mzazi au mlezi ana nafasi kubwa ya kumfundisha mtoto wake kuliko mwalimu wake.

Mithali 4:13. Mkamate sana elimu, usimwache aende zake; Mshike, maana yeye ni uzima wako.

Elimu ya hapa duniani ni muhimu sana kwa mtoto.

Mafanikio yake ya kiroho na kimwili inachangiwa pia na elimu ya dunia.

Kumnyima mtoto elimu ya dunia ni kumdhulumu mtoto huyo maendeleo yake ya kimwili na kiroho.

Wale wanaokazania watoto wao elimu ya kiroho na kupuuza elimu ya duniani anamtayarisha mtoto wake kuwa manamba yaani kuja kutumikishwa maisha yake yote maana una elimu ya kiroho lakini bado unaishi duniani.

Pia wale wanaowapa watoto wao elimu ya kiduni na kupuuza elimu ya kiroho wanamtarisha mtoto huyo kuwa mpagani na kukosa dira ya mbinguni.

Yesu anaporudi mara ya pili nitadaiwa nini?

Yeremia 13:20 Inua macho yako, Ee Yerusalemu, ukawatazame hawa wanaokuja kutoka kaskazini; liko wapi kundi lako ulilopewa, kundi lile.

Yesu atakapokuja atakuuliza iko wapi familia niliyokupa?

Kabla ya kudaiwa makundi mengine ya watu kumbuka Mungu atakudai familia ya maana ndio upo nao karibu kuliko wote. Na familia Mungu amekupa kwa agano.

Linda na kuhudumia familia yako kuliko kitu kingine chochote.

1 Timotheo 5:8 Lakini mtu ye yote asiyewatunza walio wake, yaani, wale wa nyumbani mwake hasa, ameikana Imani, tena ni mbaya kuliko mtu asiyeamini.

Sura 16

KILA NENO TOKA KWA MUNGU NA MANABII WAKE KITATIMIA

Ufunuo 22:12

Tazama naja upesi na ujira wangu u pamoja nami kumlipa kila mtu kama kazi yake ilivyo.

1. Kila ovu chini ya jua Mungu atakilipa na kila zuri chini ya jua Mungu atakilipa.
2. Hakuna siri mbele zake.
3. Mipango yote ya shetani anayotimiza kupitia watu wake dhidi ya watu wa Mungu anaijua.

Mathayo 12:36

Basi, nawaambia, kila neno lisilo maana, watakalolinena wanadamu, watatoa hesabu ya neno hilo siku ya hukumu.

1. Mungu hana mizaha chochote kile tutendalo litaletwa ukumuni.
2. Yeye anachunguza mioyo ya watu wake
3. Maovu yanayoendelea leo kote duniani hakuna iliyojificha mbele zake.

Ufunuo 14:8

Kisha mwingine malaika wa pili akafuata akisema, Umeanguka, Umeanguka Babeli, mji ule ulio mkubwa, maana ndio uliowanywesha mataifa yote mvinyo ya ghadhabu ya uasherati wake.

1. Mvinyo ni mafundisho ya kidini yaliyo changanyika na uongo ndani yake
2. Babeli ambayo ni machafuko yaliyo shamiri kwenye majengo mengi ya ibada.
3. Viongozi wakubwa wa serikali washauri wao wakubwa ni viongozi wa dini
4. Dini nyingi leo zina jaribu kushikamana na dola ili kuwa na mamlaka ndani dini
5. Serikali nyingi na zenye nguvu duniani ina tumia vitabu vya kidini kuweka viongzi wao madarakani wakiapishwa ikiwemo Tanzania
6. Hii ina maana viongozi wa dini hizo wana mchango mkubwa serikalini
7. Amri ya utunzaji wa jumapili itakapotolewa yaani utunzaji wa sabato bandia.
8. Siku moja ya kuabudu jumapili inakuja kwa kasi kuanzia mataifa yenye nguvu
9. Wakati serikali inashughulikia bidhaa bandia TBS. Pia kuna kuna ibada bandia hakuna serikali ya kudhughulikia.

Ufunuo 14:9-12

Na mwingine malaika wa tatu, akawafuata akasema, kwa sauti kuu, mtu awaye yote akimsujudia huyo mnyama na sanamu yake, na kuipokea chapa katika kipaji cha uso wake, au katika mkono wake,

Yeye naye atakunywa katika kikombe kilichochanganywa na hasira ya Mungu iliyotengenezwa, pasipo kuchanganywa na maji, katika kikombe cha hasira yake, naye atateswa kwa moto na kiberiti mbele ya malaika watakatifu, na mbele ya mwana-kondoo.

Na moshi ya maumivu yao hupanda juu hata milele na milele, wala hawana raha mchana wala usiku, hao wamsujuduo huyo mnyama na sanamu yake na kila apokeaye chapa ya jina lake.

Hapa ndipo penye subira ya watakatifu, hao wazishikao amri za Mungu na kuwa na imani ya Yesu.

1. Ole wake mwenye kumwabudu mwanadamu mwenzake
2. Ole wake mwenye kuabudu mnyama na sanamu yake
3. Ole wake mwenye kuabudu vitu vinavyoonekana badala ya Mungu wa mbinguni.
4. Hasira ya Mungu inawaka pale ambapo Uungu wake anapewa mwanadamu,
5. Wana heri wazitunzao amri za Mungu na kuwa na imani ya Yesu.
6. Utukufu wa Mungu apewe Mungu.

Sura 17

KWANINI MKANGANYIKO KATIKA IBADA? (kunena kwa lugha)

1wakorintho 14:26-33

26.Basi ndugu imekuwaje? Mkutanapo pamoja kila mmoja ana zaburi ana fundisho, ana ufunuo, ana lugha, ana tafsiri. Mambo yote na ya tendeke kwa kusudi la kujenga.

27.kama mtu akinena kwa lugha wanene wawili au watatu, si Zaidi, tena zamu kwa zamu, na mmoja afasiri

28.Kama asipokuwapo mwenye kufasiri, na anyamaze katika kanisa aseme na nafsi yake tena na Mungu.

29.Na manabii wanene wawili au tatu na wengine wapambanue

30.Lakini mwingine aliyeketi akifunuliwa neno, yule wa kwanza na anyamaze.

31.Kwa maana ninyi nyote mwaweza kuhutubu mmoja mmoja, ili wote wapate kujifunza, na wote wafarijiwe.

32.Na roho za manabii huwatii manabii.

33.Kwa maana Mungu si Mungu wa machafuko, bali wa amani, vilevile kama ilivyo katika makanisa yote ya watakatifu.

1. Mungu anahitaji umoja na mawelewano katika ibada.

2. Kila mtu ndani ya kanisa ana karama yake hivyo hata mchungaji ana karama yake. Sio kwamba mchungaji ana karama zote
3. Kila jambo lifanyike kwa sudi la kujenga yaani kwa utukufu wa Mungu.
4. Kwa habari ya kunena kwa lugha waumini wasipige kelele ibadani wanene zamu kwa zamu na mmoja atafsiri.
5. Mungu ni Mungu wa utaratibu. Hivyo ibada zetu zinahitaji utaratibu.
6. Ukizungumza na Mungu lieleze kanisa ili isiwe ni ujumbe wako mwenyewe lugha za mbinguni nipi?
7. Mungu anafahamu lugha zote

1Wakorintho 13:1

Nijaposema kwa lugha za wanadamu na za malaika, kama sina upendo, nimekuwa shaba iliayo na upatu uvumao.

1. Mbinguni wanaongea lugha gani?
2. Kwanini Mungu azungumze nasi lugha za mbinguni? Hapo lazima udanganyifu iwepo
3. Kwanini saa ya maombi tunaongea lugha zetu alafu Mungu atujibu kwa lugha ya mbinguni?
4. Hapa kuna kuchezeana kiini macho, shetani hutawala maombi ya wengi bila kujua.

Wakolosai 3:17

Na kila mfanyalo, kwa neno au kwa tendo, fanyeni yote katika jina la Bwana, wala si kwa wanadamu.

1. Sio salama kutenda kwa mapenzi ya kanisa bali ni salama kutenda kwa mapenzi ya Mungu.
2. Kila tulitendalo tutende kwa usimamizi wa Roho mtakatifu.
3. Vingozi wengi wanachezea roho za watu katika mikono yao.

Wengi unena kwa lugha zisizojulikana na kusisitiza ubatizo wa Roho mtakatifu, ni kweli ubatizo wa Roho mtakatifu ni muhimu

Lakini matunda ya Roho mtakatifu ni yapi?

Wagalatia 5:22,23.

Lakini tunda la Roho ni upendo, furaha, Amani, uvumilivu, utu wema, fadhili, uaminifu, upole, kiasi, juu ya mambo kama hayo hakuna sheria.

Wakati Yesu anataka kupaa mbinguni alituachia msaidizi

Yohana 14:26 Lakini huyo Msaidizi, huyo Roho Mtakatifu, ambaye Baba atampeleka kwa jina langu, atawafundisha yote, na kuwakumbusha yote niliyowaambia.

1. Matunda ya Roho mtakatifu ni tabia njema na utii wa sheria ya Mungu.
2. Aliyejazwa na Roho mtakatifu maisha yake lazima yabadilike na kuwa makamilifu

Mitume walipojazwa na Roho mtakatifu walifanyeje?

Matendo 2:1,4

Hata ilipotimia siku ya Pentekoste walikuwako wote mahali pamoja.

Wote wakajazwa Roho mtakatifu, wakaanza kusema kwa lugha nyingine, kama Roho alivyowajalia kutamka.

1. Siku ya pentekoste maana yake ni siku ya 50 baada ya Yesu kupaa mbinguni.
2. Baada ya Yesu kupaa mbinguni mitume walibaki wakiwa wamoja sana walishikamana na kuondoa tofauti zao.
3. Roho mtakatifu hukaa pale ambapo watu wameacha tofauti zao na kuwa kitu kimoja.
4. Mitume hawa na waongofu walianza kunena kwa lugha ngeni?

Je! Hiyo lugha ngeni ilitoka mbinguni?

Matendo 2:7,8

Wakashangaa wote, wakastaajabu wakiambiana, Tazama hawa wote wasemao si Wagalilaya?

Imekuwaje basi sisi kuwasikia kila mtu lugha yetu tuliyozaliwa nayo?

1. Lugha zilizosikika ni za binadamu walizozaliwa nazo sio lugha ya mbinguni
2. Ukitaka kujua Mungu ni kabila gani basi hao wanaonena kwa lugha waeleze kwa kutumia maandiko matakatifu lugha waliowasiliana na Mungu.
3. Wanadamu wadhambi walielewa lugha iliyozungumzwa
4. Mungu aliwapa njia ya mwasiliano

Katika siku za mwisho shetani atabuni njia mbalimbali za ibada Wakristo wengi wakidhani wanamwabudu Mungu kumbe ni njia ya kumwadu adui.

Isaya 52:10

Bwana ameweka wazi mkono wake mtakatifu machoni pa mataifa yote, Na ncha zote za dunia, Zitauona wokovu wa Mungu wetu.

Niangalieni mkaokolewe, enyi ncha zote za dunia, maana mimi ni Mungu hapana mwingine.

Kutoka 32:19 Hata alipoyakaribia marago akaiona ile ndama, na ile michezo. Hasira ya Musa ikawaka, akazitupa zile mbao mikononi mwake, akazivunja chini ya mlima.

Wana wa Israeli walipotengeneza ndama, ibada zao zilikuwa mchanganyikeni

Ibada zetu ni za thamani sana mbele za Mungu. Hivyo ibada inahitaji utulivu na hekima toka mbinguni.

Waebrania 12:28 Basi kwa kuwa tunapokea ufalme usioweza kutetemeshwa, na mwe na neema, ambayo kwa hiyo tumtolee Mungu ibada ya kumpendeza, pamoja na unyenyekevu na kicho;

Sura 18

KUNA TUMAINI GANI MAKABURINI

Kama kuna kitu kimechanganya wengi ni habari ya kifo.

Hata sasa wengi wamechanganyikiwa juu ya kifo.

Wasomi na wasio na elimu hapa wamechanganyikiwa kwa habari kifo.

Hofu hutanda tunaposimama mbele ya maiti.

Kauli nyingi hutamkwa mbele ya jeneza hata katika vyombo vya habari.

1. Mungu ailaze roho ya marehemu mahali pema peponi amina.
2. Mungu amempenda zaidi.
3. Tangulia mbinguni tunakufuata.
4. Katuombee.

Mwanzo 2:17

Walakini matunda ya mti wa ujuzi wa mema na mabaya usile, kwa maana siku utakapokula matunda ya mti huo utakufa hakika.

1. Kabla ya kifo kuingia duniani Mungu alitoa taadhari ili kuepuka kifo
2. Mwanadamu hakujua maana ya kufa hivyo hawakuchukulia agizo la Mungu kwa uzito
3. Alicho kisema Mungu hakibadiliki hata kama ni mwingi wa rehema na huruma.

Mwanzo 3:4, 5

Nyoka akamwambia mwanamke hakika hamtakufa.

Kwa maana Mungu anajua ya kwamba siku mtakayokula matunda ya mti huo mtafumbuliwa macho nanyi mtakuwa kama Mungu mkijua mema na mabaya.

1. Mwanadamu alimwamini shetani kuliko Mungu
2. Shetani alidhamiria kuteka dunia yote na wakazi wake.
3. Kusudi lake asife mwenyewe bali awandae wengi kwaajili ya kwenda nao motoni
4. Shetani anamweleza mwanadamu hakika hamtakufa bali Mungu ni mwongo.

Mwanzo 3:19

Kwa jasho la uso wako utakula chakula, hata utakapo irudia ardhi ambayo, katika hiyo, ulitwaliwa, kwa maana u mavumbi wewe, nawe mavumbini utarudi.

1. Baada ya anguko mwanadamu ameanza kuteseka,
2. Chakula na mahitaji yake mengine ameanza kupata kwa shida.
3. Tangazo la kifo likatolewa rasim ila bado hawakuona kifo

Mwanzo 4:8. Kaini akamwambia Habili nduguye, Twende uwandani Ikawa walipokuwapo uwandani,Kaini akamwinukia Habili nduguye,akamwua.

1. Adamu na Hawa kwa mara ya kwanza walisimama mbele ya mtoto wao aliyekufa wakiwa hawana uzoefu wa kuona mwanadamu aliyekufa.
2. Yawezekana walidhani amelala tu.
3. Kifo hiki cha kwanza kilikuwa na maumivu makubwa sana.
4. Kifo cha kwanza baada ya dhambi kuingia na kabla ya hapo hapakuwahi kutokea kifo.
5. Hakuna kitu chenye maumivu makubwa duniani kama kifo.
6. Hata hivyo maumivu makali kuliko yote ni kifo ingawa aliyekufa hana maumivu kwani hajui neno lolote
7. Maumivu yote yanaishia kwenye kifo.

1 Wathesalonike 4:13-18.

Lakini, ndugu, hatutaki msijue habari zao waliolala mauti, msije mkahuzunika kama na wengine wasio na matumaini.

14 Maana, ikiwa twaamini ya kwamba Yesu alikufa akafufuka, vivyo hivyo na hao waliolala katika Yesu, Mungu atawaleta pamoja naye.

15 Kwa kuwa twawaambieni haya kwa neno la Bwana, kwamba sisi tulio hai, tutakaosalia hata wakati wa kuja kwake Bwana, hakika hatutawatangulia wao waliokwisha kulala mauti.

16 Kwa sababu Bwana mwenyewe atashuka kutoka mbinguni pamoja na mwaliko, na sauti ya malaika mkuu, na parapanda ya Mungu; nao waliokufa katika Kristo watafufuliwa kwanza.

17 Kisha sisi tulio hai, tuliosalia, tutanyakuliwa pamoja nao katika mawingu, ili tumlaki Bwana hewani; na hivyo tutakuwa pamoja na Bwana milele.

18 Basi, farijianeni kwa maneno hayo.

Mungu ametuweka wazi kwa habari ya wafu.

Yesu atakuja tena kufufua watakatifu wake kwaajili ya uzima wa milele kisha waovu kwaajili hukumu.

1 Wathesalonike 4:15 inaeleza hakuna anayewatangulia wengine mbinguni.

Bwana atashuka kuchukua watakatifu wake hivyo hakuna mtakatifu anayekufa na kuingia mbinguni.

Hakuna unyakuo wa siri kwamba kuna watu wataingia mbinguni kwa siri, wala kaburi sio lango la kuingia mbinguni.

Faraja kamili ya mkristo anaye kwenda mbinguni ni kujua hali ya wafu na kifo cha mkristo ipoje.

Mhubiri 9:5

Kwa sababu walio hai wanajua ya kwamba watakufa, lakini wafu hawajui neno lolote, wala hawana ijara tena, maana kumbukumbu lao limesauliwa.

1. Walio hai wanajitambua lakini wafu hawajui neno lolote.
2. Aliyekufa hajui neno lolote.
3. Wafu hawana msaada kwetu.
4. Hatuwezi kuomba msaada kwao, maana hawana utambuzi.

Zaburi 146:4 Pumzi yake hutoka, huurudia udongo wake, Siku hiyo mawazo yake yapotea.

Hatuwezi kutegemea aliyekufa kwa lolote hata kama alikuwa na uwezo kiasi gani.

1 Samweli 28:3-15

1. Samweli amefariki na kuzikwa
2. Taifa la Israeli lilishambuliwa na Wafilisti na mfalme aliye mwasi Bwana, akakimbilia kwa mashetani.
3. Bwana alikataa kumpa Sauli maono kwa sababu ya uasi.

Mtu akifa amekufa yupo kaburini mpaka siku ya kurudi kwa Yesu mara ya pili.

Matendo 2:29.

Daudi alikufa mtume Paulo anashuhudia hata hivi leo kaburi lake lipo katikati ya jamii.

Waume, ndugu zangu, mniwie radhi, niseme kwa ujasiri mbele yenu habari za baba yetu mkuu, Daudi, ya kuwa alifariki akazikwa, na kaburi lake liko kwetu hata leo.

1. Daudi alikufa kaburi lake lipo mpaka sasa.
2. Daudi anasubiri ufufuo wa kurudi kwa Yesu mara ya pili.
3. Daudi alikuwa rafiki wa karibu wa Yesu lakini yupo kaburini mpaka Yesu atakapokuja.

Musa alikufa ila hakuna mwanadamu aliyehusika kwenye mazishi yake wala kuona kaburi lake.

Kumbukumbu la torati 34:5, 6. Basi Musa, mtumishi wa Bwana, akafa huko, katika nchi ya Moabu, kwa neno la Bwana.

6 Akamzika bondeni, katika nchi ya Moabu, kukabili Beth-peori; lakini hapana mtu ajuaye kaburi lake hata leo.

Luka 9:29,30. Ikawa katika kusali kwake sura ya uso wake ikageuka, mavazi yake yakawa meupe, yakimeta-meta.

Na tazama, watu wawili walikuwa wakizungumza naye, nao ni Musa na Eliya;

Ayubu 27:3

Kwa kuwa uhai wangu ukali mzima ndani yangu, na roho ya Mungu I katika pua yangu

Roho inayosemwa kwenye kitabu cha Ayubu ni pumzi.

Mwanzo 2:7 Bwana Mungu akamfanya mtu kwa mavumbi ya ardhi, akampulizia puani pumzi ya uhai; mtu akawa nafsi hai.

Mwisho wa kifo ni nini?

1 Wakorintho 15:53-57. Maana sharti huu uharibikao uvae kutokuharibika, nao huu wa kufa uvae kutokufa.

Basi huu uharibikao utakapovaa kutokuharibika, na huu wa kufa utakapovaa kutokufa, hapo ndipo litakapokuwa lile neno lililoandikwa, Mauti imemezwa kwa kushinda.

Ku wapi, Ewe mauti, kushinda kwako? U wapi, Ewe mauti, uchungu wako?

Uchungu wa mauti ni dhambi, na nguvu za dhambi ni torati.

Lakini Mungu na ashukuriwe atupaye kushinda kwa Bwana wetu Yesu Kristo.

Sote tutabadilishwa maana uharibifu hautarithi uzima wa milele.

Kifo ni matokeo ya dhambi maana dhambi.

Yesu atakapokuja na kukomesha dhambi moja kwa moja kifo haitakuwa na nafasi.

wito

Isaya 26:19

Wafu wako wataishi, maiti zangu watafufuka, amkeni, kaimbeni, ninyi mnaokaa mavumbini, kwa maana umande wako ni kama umande wa mimea, nayo ardhi itawatoa waliokufa.

1. Wanaomtumani Yesu Kristo kuwa Bwana na Mwokozi wao wajapokufa wataishi tena.
2. Mungu atafufua watakatifu wake
3. Saa itafika mavumbi haitaweza kubeba watakatifu wa Mungu tena.
4. Waliokufa katika Kristo wataamka kwa furaha kuu.

Sura 19
MWILI WAKO NI HEKALU LA ROHO MTAKATIFU

Afya ni kitu muhimu sana katika maisha ya mwanadamu.

Wengi ambao hawaoni umuhimu wa afya zao wakiugua wanateseka sana.

Hivyo wanaona umuhimu wa afya zao pale wanapougua.

Hata hivyo elimu juu ya afya sio kwaajili ya kuishi maisha marefu na afya nzuri tu, bali elimu juu ya afya ni mausiano na Mungu.

1 Wakorintho 6:19

Au hamjui ya kuwa mwili wenu ni hekalu la Roho mtakatifu aliye ndani yenu, mliyepewa na Mungu? Wala ninyi si mali yenu wenyewe.

1. Mmiliki wako ni Mungu wewe hauwezi kujimiliki mwenyewe.
2. Mungu ambaye ni mmiliki wako anataka atawale mwili wako anavyotaka sio unavyotaka wewe.
3. Mungu pekee ndiye anajua kilicho bora zaidi kwa ajili ya miili yetu.
4. Anatupenda anajishugulisha kwa ajili ya miili yetu ili tuwe na afya njema.

Mwanazo 1:29

Mungu akasema, tazama, nimewapa kila mche utoao mbegu, ulio juu ya uso wa nchi yote pia, na kila mti, ambao matunda yake yana mbegu vita kuwa ndivyo chakula chenu.

Na chakula cha kila mnyama wa nchi, na cha kila ndege wa angani, na cha kila kitu kitaambacho juu ya nchi, chenye uhai, majani yote ya miche,ndiyo chakula chenu, ikawa hivyo.

1. Vyakula bora kwaajili ya miili yetu anayejua ni Mungu pekee naye Mungu ameturithisha.
2. Chakula cha awali kilikuwa ni mboga za majani, matunda na mizizi na mbegu.
3. Mwanadamu hakuwahi kuona damu imemwagika.
4. Ulaji wa nyama Mungu aliruhusu baadae sana baada ya dhambi kuingia.
5. Mpaka wanyama nao wote walikula hivyo

Mwanzo 9:3

Kila kiendacho kilicho hai kitakuwa chakula chenu, kama nilivyowapa mboga za majani, kadhalika nawapeni hivi vyote.

1. Baada ya dhambi kuingia na sasa Nuhu na familia yake wanatoka ndani ya safina Mungu akaruhusu watu wale nyama
2. Vyakula havikuwepo katika maeneo hayo.
3. Watu waliendelea kusikiliza sauti ya Mungu hata wakati wa Nuhu.

Walawi 11:2-8

2.Neneni na wana wa Israeli, mkiwaambia, wanyama hawa ndio wanyama wenye uhai mtakaowala, katika hayawani wote walio juu ya nchi.

3.Kila mnyama mwenye kwato katika miguu yake, mwenye miguu ya kupasuka kati, mwenye kucheua, katika hayawani, hao ndio mtakaowala.

4.Pamoja na hayo, wanyama hawa hamtawala katika wale wenye kucheua, na katika wale walio na kwato, ngamia kwa sababu yuacheua lakini hana kwato, yeye ni najisi kwenu.

5.Na wibari kwa sababu yeye hucheua lakini hana kwato, yeye ni najisi kwenu.

6.Na sungura kwa sababu hucheua lakini hana kwato, yeye ni najisi kwenu.

7.Na nguruwe kwa sababu yeye anazo kwato, ni mwenye miguu iliyopasuka kati, lakini hacheui, yeye ni najisi kwenu.

8.Msile nyama yao, wala msiguse mizoga yao, hao ni najisi kwenu.

1. Mungu anajua miili yetu ili tuwe na afya bora ina hitaji nini?
2. Ikiwa Muumbaji wetu ndiye amesema basi nasi twapaswa kufuata.
3. Bila kupinga kwa lolote lile.

4. Nguruwe na sungura na vitu vingine najisi ni chukukizo kutumika kwa matumizi ya chakula.
5. Sio kila mnyama aliyeumbwa na Mungu ameumbwa kwa matumizi ya chakula.

Walawi 11:9

Katika hao wote walio ndani ya maji mtakula hawa, kila aliye na mapezi na magamba ndani ya maji, na ndani ya bahari, na ndani ya mito, mtakula hao.

1. Mungu ametoa utaratibu mzuri wa kula vilivyomo ndani ya maji.
2. Kipi kinafaa kipi hakifai.

Isaya 65:3, 4

Watu wanikasirishao mbele za uso wangu daima, wakitoa dhabihu katika bustani zao, na kufukiza uvumba juu ya matofali,

Waketio kati ya makaburi, na kulala katika mahali pao pa siri, walao nyama ya nguruwe, na mchuzi wa vitu vinichukiavyo u katika vyombo vyao.

1. Mungu anachukia utaratibu wake unapoachwa.
2. Ulafi na tamaa chafu vimetawala mioyo ya watu wengi leo.
3. Mungu anahitaji neno lake tulitii kwa kila anchotamka.
4. Tamaa chafu na vikome ndani ya makanisa yetu.

Walawi 17:14

Kwa maana kuliko huo uhai wa mnyama, hiyo damu yake ni moja na uhai wake, kwa hiyo naliwaambia wana wa Israeli, msile damu ya mnyama wa aina yoyote, kwa kuwa uhai wa wanyama wote ni katika hiyo damu yake, atakayeila awaye yote atakatiliwa mbali.

1. Usile damu.
2. Wale wanyama ambao Mungu ameruhusu tule, damu zao tusile
3. Chinja mnyama kisha damu imwagike ndipo ule nyama yake.
4. Wala usinyonge mnyama

Walawi 22:8

Nyamafu au mnyama aliyeraruliwa na wanyama asile asijitie unajisi kwa hiyo nyama, mimi ndimi Bwana.

1. Usile kibudu
2. Wengi waliokula kibudu wamejiletea madhara makubwa sana maishani mwao na Mungu alijua hilo.
3. Hata hivyo usiache kwa sababu ina madhara bali acha kwa sababu Mungu amekataa.
4. Mungu ana akili kuliko mwanadamu.

5. Kilichokufa ni chukizo mbele za Mungu wa mbinguni.

Mungu anasema nini kuhusu pombe?

Mithali 20:1 Mvinyo hudhihaki, kileo huleta ugomvi; Na akosaye kwa vitu hivyo hana hekima.

Mambo ya aibu hutendwa baada ya kuondoa ufahamu kwa njia ya pombe.

Matukio mengi ya kutisha ya aibu hutokana na pombe na madawa mengine ya kulevya

Mwanzo 19:34-36. Ikawa siku ya pili, mkubwa akamwambia mdogo, Tazama, nimelala jana na baba yangu, tumnyweshe mvinyo tena usiku huu, ukaingie ukalale naye.

Wakamnywesha tena baba yao mvinyo usiku ule, akaondoka mdogo akalala naye, wala yeye hana habari alipolala wala alipoondoka.

Basi hao binti wote wawili wa Lutu wakapata mimba kwa baba yao.

Matendo 10:14

Lakini Petro akasema, Hasha, Bwana, kwa maana sijakula kamwe kitu kilicho kichafu au najisi.

1. Mitume hawakula vitu ambavyo Mungu amekataza.
2. Walifundishwa maadili bora na Yesu mwenyewe wakiwa naye hapa duniani.

Matendo 10:28

Akawaambia, Ninyi mnajua ya kuwa si halali mtu aliye Myahudi ashikanane na mtu aliye wa taifa lingine wala kumwendea, lakini Mungu amenionya, nisimwite mtu awaye yote mchafu wala najisi.

1. Katika njozi ya vyakula haikuwa vyakula halisi bali Mungu alikuwa anavunja ukuta kati ya mataifa na wayahudi
2. Pazi lililoshuka na vitu najisi Petro hakuchukuwa hata kimoja na kula.
3. Mungu wakati mwingine alizungumza na watu wake kwa mifano na kuwafafanulia

Matendo10:34, 35

Petro akafumbua kinywa chake, akasema, Hakika natambua ya kuwa Mungu hana upendeleo,

Bali katika kila taifa mtu amchaye na kutenda haki hukubaliwa na yeye.

1. Mungu ni mwingi wa rehema hana ubaguzi wala upendeleo
2. Mungu hawezi mwekea mtoto wake kinyongo.
3. Mpango wa Mungu ni kumwokoa kila mtu asipotee
4. Mungu alitafuta na anaendelea kutafuta watu wake katika kona zote.
5. Makabila yote na mataifa yote ni watoto wa Mungu.

Mathayo 15:10, 11.

Akawaita makutano akawaambia,

Sikilizeni, mfahamu, sicho kiingiacho kinywani kimtiacho mtu unajisi, bali kitokacho kinywani ndicho kimtiacho mtu unajisi.

1. Mfano huu wanafunzi wa Yesu hawakuelewa ndipo Yesu akaanza kuwafafanulia.
2. Ndipo Yesu akaanza kuwafafanulia
3. Hata leo Yesu alishafafanua lakini watu hawaelewi kitu.

Mathayo 15:17-20

Hamfahamu bado ya kuwa kila kiingiacho kinywani hupitia tumboni, kikatupwa chooni?

Bali vitokavyo kinywani vyatoka moyoni, navyo ndivyo vimtiavyo mtu unajisi

Kwa maana moyoni hutoka mawazo mabaya, uuaji, uzinzi, uasherati, wivi, ushuhuda wa uongo, na matukano.

Hayo ndiyo yamtiacho mtu unajisi, lakini kula kabla ya kunawa hakumtii mtu unajisi.

1. Yesu alikuwa akizungumzia maneno na sio vyakula.
2. Mawazo machafu.
3. Vyakula vitabaki kuwa vyakula na vitu najisi vitabaki kuwa najisi mwanadamu anapaswa kuelewa na kuheshimu hilo.
4. Aliyetoa tusi ndiye ananajisika, bali ayesikia tusi hawezi kunajisika.

1 Wakorintho 10:31 Basi, mlapo, au mnywapo, au mtendapo neno lo lote, fanyeni yote kwa utukufu wa Mungu.

Sura 20

UTII WANGU MBELE ZA MUNGU (UWAKILI)

Sifa ya wakili awe mwaminifu, mwenye Busara.

Luka 12:42 Bwana akasema, Ni nani, basi, aliye wakili mwaminifu, mwenye busara, ambaye bwana wake atamweka juu ya utumishi wake wote, awape watu posho kwa wakati wake?

Swala la kujitoa na kutoa kwa Mungu hekima toka mbinguni hutambulisha kuwa Mungu ni vyote hivyo mwaminifu toa kila kitu mikononi mwa Mungu kama mpaji na mlinzi wa mali. Mwenye Busara hakumbushwi wajibu wake wa kutoa zaka na sadaka bali hekima toka mbinguni humwongoza. Asiye na Roho Mtakatifu uhoji utoaji kwa mpango.

Zaburi 24:1

Nchi na vyote viijazavyo ni mali ya Bwana, Dunia na wote wakaao ndani yake.

1. Mwanadamu hatuna chochote chini ya jua vyote ni vya Mungu
2. Tulivyo navyo tumeazimwa na Mungu tuvitunze

Mithali 3:9 Mheshimu Bwana kwa mali yako, Na kwa malimbuko ya mazao yako yote

Ukimtambua aliyekupa mali kwamba ni Mungu basi utamheshimu Mungu na swala la kutoa zaka na sadaka haiwezi kuwa mgogoro kwako.

Haghai2:8. Fedha ni mali yangu, na dhahabu ni mali yangu, asema Bwana wa majeshi.

kwa mali zako Fedha ni mali yangu, na dhahabu ni mali yangu, asema Bwana wa majeshi..

Walawi 27:30

Tena zaka yote ya nchi, kama ni mbegu ya nchi, au kama ni matunda ya nchi, ni ya Bwana, ni takatifu kwa Bwana.

Mwanzo 28:22 Na jiwe hili nililolisimamisha kama nguzo litakuwa nyumba ya Mungu; na katika kila utakalonipa hakika nitakutolea wewe sehemu ya kumi.

Zaka ni moja ya kumi au sehemu ya kumi ya faida ya mapato yako na sadaka ni moja ya kumi ya faida ya mapato yako.

1. Zaka ni mali takatifu ya Bwana.
2. Chochote upatacho toa zaka maana sio yako bali ni ya Bwana.

3. Zaka hutangaza mahusiano kati ya Mungu na mwanadamu.
4. Zaka ni kiini ya maafanikio ya wanadamu.

Waliofanikiwa walitoa, siku zote wachoyo hawafanikiwa wanapata pesa nyingi lakini hawafanikiwi. Wachoyo siku zote hawafikii malengo yao.

Malaki 3:7

Tokea siku za baba zenu mmegeuka upande, mkayaacha maagizo yangu, wala hamkuyashika. Nirudieni mimi, nami nitawarudia ninyi, asema Bwana wa majeshi. Lakini ninyi mwasema, Turudi kwa namna gani?

1. Baada ya mwanadamu kwenda mbali na upendo wa Mungu, Mungu anataka turudi kwake.
2. Uasi ni kupotea na sio kupona
3. Maagizo ya Yesu yameachwa mbali sasa watu wanaenda kwa desturi tu.
4. Mungu kwa kuwa bado anapenda watoto wake hivyo anasema turudi kwake.
5. Yupo tayari kutupokea.

Malaki 3:8, 9

Je! Mwanadamu atamwibia Mungu? Lakini ninyi mnaniibia mimi. Lakini ninyi mwasema, tumekuibia kwa namna gani? Mmeniibia zaka na dhabihu.

Ninyi mmelaaniwa kwa laana, maana mnaniibia mimi, naam, taifa hili lote.

1. Kushindwa kutoa zaka mbele za Mungu ni wizi.
2. Kushindwa kutoa zaka mbele za Mungu ni kujiletea laana kwako na kwa familia yako
3. Watoto wengi wamelaaniwa hata hawana msimamo kanisani na walishashindwa masomo yao.
4. Ukila zaka takatifu ya Bwana kwa tamaa zako elewa umekaribisha matatizo mwenyewe nyumbani mwako.

Malaki 3:10-12

Leteni zaka kamili galani, ili kiwemo chakula katika nyumba yangu, mkanijaribu kwa njia hiyo, asema Bwana wa majeshi, mjue kama sitawafungulia madirisha ya mbinguni, na kuwamwigieni baraka, hata isiwepo nafasi ya kutosha au la.

Nami kwa ajili yenu nitakemea yeye alaye, wala hataharibu mazao ya ardhi yenu, wala mzabibu wenu hautapukutisha matunda yake kabla ya wakati wake katika mashamba, asema Bwana wa majeshi.

Na mataifa yote yatawaiteni heri, maana mtakuwa nchi ya kupendeza sana, asema Bwana wa majeshi.

1. Toa zaka kwa uaminifu ili Mungu akubariki.
2. Mungu anatangaza tumjaribu kwenye kitabu cha Malaki tu biblia nzima.
3. Mibaraka ni mingi mno ikiwemo na kulindwa dhidi ya magonjwa, kulindwa dhidi ya watu wabaya, kulindwa katika masomo, kulindwa mashambani, kulindwa katika biashara, kupata mwenzi wa maisha, kulindwa katika ndoa, kulindwa katika safari, kulindwa katika ajira, kulindwa katika kazi, na mengine mengi.
4. Taifa lililojikabidhi mikononi mwa Mungu litalindwa.
5. Kila aliyepata nafasi ya kumtumikia Mungu kwa matoleo fanya hivyo saa inakuja utatamani kutoa chochote hautaweza tena
6. Waliomtii Mungu, Mungu anawapenda sana na Mungu hujishugulisha na maisha yao.

Mashauri juu ya uwakili uk 13

Kama tunavyoendelea kupokea mibaraka ya Mungu, ndivyo inavyotupasa kuendelea kutoa. Wakati mtoaji wa mbinguni atakapokoma kutoa kwetu, ndipo nasi tutaacha kutoa, kwa sababu nasi tutakuwa hatuna cha kutoa. Kamwe Mungu hajatuacha bila kutuonyesha wazi upendo wake, kwa maana alitutendea mema.

Mungu anatulinda kila dakika na kutusaidia kwa uwezo wake. Hutupatia vyakula kwenye meza zetu. Hutupatia Amani na kutuburudisha na usingizi. Kila juma utupatia sabato ili tupate kupumzika katika kazi zetu za kawaida, na kumwabudu Mungu katika nyumba yake. Katika kurasa za maandiko matakatifu tunapata mashauri ya hekima,

Mwanzo 14:18-20.

Na Melkizedeki mfalme wa Salemu, akaleta mkate na divai, naye alikuwa kuhani wa Mungu aliye juu sana.

Akambariki, akasema, Abramu na abarikiwe Mungu aliye juu sana muumba wa mbingu na nchi.

Ahimidiwe aliye juu sana, adui zako mikononi mwako. Abramu akampa fungu la kumi la vitu vyote.

1. Waumini wenye imani walijua thamani ya wachungaji wao.
2. Kabla hajajineemesha walineemesha viongozi wa kanisa.
3. Wachungaji waliojitoa kikamilifu kwa kazi ya Mungu hufanya kazi ya kubariki watu wote
4. Hivyo tunapaswa kuhudumia wachungaji na waatendakazi waliojitoa kwa moyo
5. Wengi unakuta wana neemeka na watendakazi wao wanalia.

Matendo 16:14. 15

Mwanamke mmoja, jina lake Lidia, mwenye kuuza rangi ya zambarau, mwenyeji wa Thiatira, mcha Mungu, akatusikiliza ambaye moyo wake ulifunguliwa na Bwana, ayatunze maneno ya Paulo.

Hata alipokwisha kubatizwa, yeye na nyumba yake, akatusihi akisema

Sadaka ambayo Yesu aliutolea ulimwengu ni uhai wake ili tupate uzima wa milele.

Yohana 10:15 kama vile Baba anijuavyo, nami nimjuavyo Baba. Nami nautoa uhai wangu kwa ajili ya kondoo

Yohana 3:16. Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa Mwanawe pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele.

Mwanzo 18:3-10. Ukarimu wa Ibrahimu ulimpatia mwana anayeitwa Isaka

Waebrania 13:2 Msisahau kuwafadhili wageni; maana kwa njia hii wengine wamewakaribisha malaika pasipo kujua.

Malaika wengi hutembelea watu kwa sura za watu tena wakati mwingine wanakuja kama watu duni ambao wanadharaulika katikati ya jamii nawe ukamdharau kumbe unamdharau malaika.

Ikiwa unafikiri kuwa Roho Mtakatifu anakuongoza kutenda yaliyomema na hajakuongoza kutoa zaka na sadaka basi huyo sio Roho Mtakatifu. Maana Roho aliyesema ikumbuke siku ya sabato uitakase ndiye Roho aliyesema leteni Zaka na dhabihu ghalani, na ndiye Roho aliyesema atakayeishika sheria yote akajikwa katika moja amekosa juu ya yote.

21

KWANINI WAADVENTISTA WASABATO HATUVAI HELENI MASIKIONI AU MIKUFU SHINGONI

Mwanzo35:1-5

Mungu akamwambia Yakobo, Ondoka, panda uende Betheli, ukakae huko; ukamfanyie Mungu madhabahu huko; yeye aliyekutokea ulipomkimbia Esau, ndugu yako.

2 Yakobo akawaambia watu wa nyumbani mwake, na wote waliokuwa pamoja naye, Ondoeni miungu migeni iliyoko kwenu, mjisafishe mkabadili nguo zenu.

3 Tuondoke, tupande kwenda Betheli, nami nitamfanyia Mungu madhabahu huko; yeye aliyenisikia siku ya shida yangu, akawa pamoja nami katika njia yote niliyoiendea.

4 Nao wakampa Yakobo miungu migeni yote iliyokuwa mikononi mwao, na pete zilizokuwa masikioni mwao, naye Yakobo akaificha chini ya mwaloni ulioko Shekemu.

5 Wakashika njia, hofu ya Mungu ikaishika miji iliyowazunguka, wala hawakuwafuata wana wa Yakobo.

1. Mungu anapomwita Yakobo, anahitaji Yakobo afanye matengenezo katika nyumba yake kabla ya kukutana na Mungu.
2. Matengenezo aliyofanya ni kukabidhi bangili walizovaa mikononi mwao na pete zilizokuwa masikioni mwao (heleni zilizokuwa masikioni mwao).

Wakinanani walivaa pete za masikio?

Waamuzi 8:24

24Kisha Gideoni akawaambia, Mimi nina haja yangu niitakayo kwenu, ni ya kila mtu kunipa hizo pete za masikio ya mateka yake. (Kwa maana walikuwa na pete za masikio za dhahabu, kwa sababu walikuwa ni Waishmaeli.)

25 Wakajibu, Tutakupa kwa mioyo. Basi wakatandika nguo chini, wakatia humo kila mtu pete za masikio ya mateka yake.

1. Waishmaeli walivaa pete za masikio
2. Kumbuka Ibrahimu alizaa watoto wawili mtoto wa ndoa Isaka kwa Sara na Isaka ndiye mtoto wa ahadi na mtoto mwingine ni Ishmaeli kwa mjakazi Hajiri.
3. Kupitia Isaka wote tunafanywa wana wa Mungu hivyo sio salama kuiga tamaduni nje ya wana wa Isaka. Wokovu watoka kwa Wayahudi.
4. Unapozungumzia Wayahudi unamzungumzia Yakobo na Yakobo ndio Israeli na Israeli ni mtoto wa Isaka. Isaya 2:3.

Utoboaji wa masikio ilianzia wapi?

Kutoka 21:5,6

5 Lakini huyo mtumwa akisema waziwazi, Mimi nampenda bwana wangu, na mke wangu na watoto wangu; sitaki mimi kutoka niwe huru;

6 ndipo hapo huyo bwana wake atamleta mbele ya Mungu na kumleta mlangoni, au penye mwimo wa mlango; na bwana wake atalitoboa sikio lake kwa uma; ndipo atamtumikia sikuzote.

1. Watumwa walioiari kuwa watumwa wa kudumu walitobolewa masikio.
2. Baada ya Yesu kufa msalabani sisi sio watumwa tena hivyo hakuna sababu ya kutoboa masikio.

3. Yohana 15:15 Siwaiti tena watumwa; kwa maana mtumwa hajui atendalo bwana wake; lakini ninyi nimewaita rafiki; kwa kuwa yote niliyoyasikia kwa Baba yangu nimewaarifu.
4. Aliyetobolewa masikio akitembea popote alijulikana kuwa ni mali ya mtu fulani ni mtumwa wa mtu fulani. Hivyo alikuwa hawezi kusumbuliwa na mtu mwingine ata akitoroka atarudishwa kwa Bwana wake.
5. Leo hatuwezi toboa masikio wala kuvaa pete za masikio.

Sura 22

YESU ATAKUJA TENA

Mathayo 24:6

Nanyi mtasikia habari za vita na matetesi ya vita, angalieni msitishwe, maana hayo hayana budi kutukia, lakini ule mwisho bado.

1. Dalili za kurudi kwa Yesu ni vita katika pande zote za dunia.
2. Chuki itaongezeka kati mtu na mtu taifa na taifa kabila kwa kabila,
3. Watu wa Mungu hawatapendwa kabisa.
4. Ukweli wa neno la Mungu litaachwa.
5. Dhiki itaongezeka kwa watu wengi.

Isaya 25:9

Katika siku hiyo watasema, Tazama huyu ndiye Mungu wetu, ndiye tuliyemgoja atusaidie, huyu ndiye Bwana tuliyemngoja, na tushangilie na kuufurahia wokovu wake.

1. Waliokombolewa na Yesu watamkiri mwokozi.
2. Msaada wa watu wa Mungu ni kwa Bwana na Bwana atafungua njia.
3. Furaha ya watakatifu ni uwepo wa Mungu maishani mwao.
4. Watakatifu wa Mungu kimbilio lao ni kwa Yesu tu.

1 Yohana 3:2

Wapenzi, sasa tu wana wa Mungu, wala haijadhihirika bado tutakavyokuwa, lakini twajua ya kuwa atakapodhihirishwa, tutafanana naye, kwa maana tutamwona kama alivyo.

1. Sasa tunamwona Yesu kwa mbali na katika Roho saa inakuja tutamwona uso kwa uso.
2. Tutafanana naye Yesu.
3. Tutamwona kama alivyo.

Ufunuo 1:7

Tazama, yuaja na mawingu na kila jicho litamwona, na hao waliomchoma, na kabila zote za dunia wataomboleza kwaajili yake. Naam. Amina.

1. Ujio wa Yesu ni wa hakika
2. Wote watamwona Yesu hivyo hakuna ujio wa siri.
3. Waovu wote wataomboleza kwaajili ya ujio wa Yesu siku ya mwisho ndio maana.

Ufunuo 16:6

Kwa kuwa walimwaga damu ya watakatifu na ya manabii, nawe umewapa damu wainywe, nao, wamestahili.

1. Waovu watalipwa sawasawa na matendo yao.
2. Wauaji wengi hawatumii silaha, bali wanatumia maneno.
3. Wote waliomwaga damu zisizo na hatia kesi yao itasimamiwa na Mungu mwenyewe.

Yohana 14:1-3

Msifadhaike mioyoni mweni, mnamwamini Mungu, niaminini na mimi.

Nyumbani mwa Baba yangu mna makao mengi, kama sivyo, ningaliwambia, maana naenda kuwaandali mahali.

Mimi nikienda kuwaandalia mahali, nitakuja tena niwakaribishe kwangu, ili nilipo mimi nanyi mwepo.

Kwanini hapa duniani tusiridhike nako?

Waebrania 13:14 Maana hapa hatuna mji udumuo, bali twautafuta ule ujao.

1 Yohana 3:2

Wapenzi, sasa tu wana wa Mungu, wala haijadhihirika bado tutakavyokuwa; lakini twajua ya kuwa atakapodhihirishwa, tutafanana naye; kwa maana tutamwona kama alivyo

Yesu atakuja lini?

Katikati ya ulimwengu uliochanganyikiwa kiroho wahubiri wengi wameacha neno la Mungu na kutengeneza mafundisho yao kwa kuweka tarehe ya kuja kwa Bwana Yesu.

Mathayo 24:36. Walakini habari ya siku ile na saa ile hakuna aijuaye, hata malaika walio mbinguni, wala Mwana, ila Baba peke yake.

Kauli ya Yesu mwenyewe anasema hatujui siku wala saa.

Tumaini la Vizazi Vyote Uk 355, 356 Karne za giza za mateso haya ya pili.

Kwa muda zaidi ya miaka elfu moja wafuasi wa Kristo watapata mateso ambayo ulimwengu haujayayona. Kama mkono wa Mungu usingalinyoshwa ili kuwalinda watu wake, wote wangalipotea kabisa.

Sasa, Bwana akazungumzia kurudi kwake kwa usemi wa wazi ‘’Mathayo 24:23 Wakati huo mtu akiwaambia, Tazama, Kristo yupo hapa, au yuko kule msisadiki

Mathayo 24:24 Kwa maana watatokea makristo wa uongo, na manabii wa uongo, nao watatoa ishara kubwa na maajabu; wapate kuwapoteza, kama yamkini, hata walio wateule.

Mathayo24:25 Tazama, nimekwisha kuwaonya mbele.

Mathayo 24:26 Basi wakiwaambia, Yuko jangwani, msitoke; yumo nyumbani, msisadiki.

Mathayo 24:27. Kwa maana kama vile umeme utokavyo mashariki ukaonekana hata magharibi, hivyo ndivyo kutakavyokuwa kuja kwake Mwana wa Adamu.

Katika mikutano ya maelfu wanaodai kuongea na wafu, je hapasikiki wito wa Tazama Kristo yumo nyumbani? Haya ndiyo madai yanayofanywa na roho za mizimu. Lakini Kristo anasemaje? “msisadiki”

Mawakala wengi wa shetani wanatangaza Yesu ameonekana wengine wanaweka tarehe mwezi na mwaka wa kuja kwa Bwana Yesu. Lakini wana wa Nuru watoto wa Mungu wanabaki na neno moja. Hatujui siku wala saa hivyo hujiandaa wakati wote. Maisha ya waaminifu siku zote uishi kwa kumngoja Mfalme wa Amani wakimpendeza Mungu.

Tukio la kuja kwa Bwana Yesu ni tukio la hakika. Tutamwona alivyo, maana alisema mwenyewe, manabii walitabiri kwamba anakuja tena, mitume walisema, dalili zinaonyesha kwamba Yesu yupo mlangoni, hivyo hatupaswi kuwa na mashaka na ujio wa Bwana wetu Yesu Kristo.

Isaya 26:21 Kwa maana, tazama, Bwana anakuja kutoka mahali pake, ili kuwaadhibu wakaao duniani, kwa sababu ya uovu wao; ardhi nayo itafunua damu yake, wala haitawafunika tena watu wake waliouawa.

1 Yohana 3:2 Wapenzi, sasa tu wana wa Mungu, wala haijadhihirika bado tutakavyokuwa; lakini twajua ya kuwa atakapodhihirishwa, tutafanana naye; kwa maana tutamwona kama alivyo.

Mungu kamwe hasemi uongo aliahidi atatimiza ahadi yake.

Tito 1:2 katika tumaini la uzima wa milele, ambao Mungu asiyeweza kusema uongo aliuahidi tangu milele;

Sura 23

MAPUMZIKO NYUMBANI

Ufunuo 20:1-15. 1 Kisha nikaona malaika akishuka kutoka mbinguni, mwenye ufunguo wa kuzimu, na mnyororo mkubwa mkononi mwake.

2 Akamshika yule joka, yule nyoka wa zamani, ambaye ni Ibilisi na Shetani, akamfunga miaka elfu;

3 akamtupa katika kuzimu, akamfunga, akatia muhuri juu yake, asipate kuwadanganya mataifa tena, hata ile miaka elfu itimie; na baada ya hayo yapasa afunguliwe muda mchache.

4 Kisha nikaona viti vya enzi, wakaketi juu yake, nao wakapewa hukumu; nami nikaona roho zao waliokatwa vichwa kwa ajili ya ushuhuda wa Yesu, na kwa ajili ya neno la Mungu, na hao wasiomsujudia yule mnyama, wala sanamu yake, wala hawakuipokea ile chapa katika vipaji vya nyuso zao, wala katika mikono yao; nao wakawa hai, wakatawala pamoja na Kristo miaka elfu.

5 Hao wafu waliosalia hawakuwa hai, hata itimie ile miaka elfu.

6 Huo ndio ufufuo wa kwanza. Heri, na mtakatifu, ni yeye aliye na sehemu katika ufufuo wa kwanza; juu ya hao mauti ya pili haina nguvu; bali watakuwa makuhani wa Mungu na wa Kristo, nao watatawala pamoja naye hiyo miaka elfu.

7 Na hiyo miaka elfu itakapokwisha, Shetani atafunguliwa, atoke kifungoni mwake;

8 naye atatoka kuwadanganya mataifa walio katika pembe nne za nchi, Gogu na Magogu, kuwakusanya kwa vita, ambao hesabu yao ni kama mchanga wa bahari.

9 Wakapanda juu ya upana wa nchi, wakaizingira kambi ya watakatifu, na mji huo uliopendwa. Moto ukashuka kutoka mbinguni, ukawala.

10 Na yule Ibilisi, mwenye kuwadanganya, akatupwa katika ziwa la moto na kiberiti, alimo yule mnyama na yule nabii wa uongo. Nao watateswa mchana na usiku hata milele na milele.

11 Kisha nikaona kiti cha enzi, kikubwa, cheupe, na yeye aketiye juu yake; ambaye nchi na mbingu zikakimbia uso wake, na mahali pao hapakuonekana.

12 Nikawaona wafu, wakubwa kwa wadogo, wamesimama mbele ya hicho kiti cha enzi; na vitabu vikafunguliwa; na kitabu kingine kikafunguliwa, ambacho ni cha uzima; na hao wafu wakahukumiwa katika mambo hayo yaliyoandikwa katika vile vitabu, sawasawa na matendo yao.

13 Bahari ikawatoa wafu waliokuwamo ndani yake; na Mauti na Kuzimu zikawatoa wafu waliokuwamo ndani yake. Wakahukumiwa kila mtu kwa kadiri ya matendo yake.

14 Mauti na Kuzimu zikatupwa katika lile ziwa la moto. Hii ndiyo mauti ya pili, yaani, hilo ziwa la moto.

15 Na iwapo mtu ye yote hakuonekana ameandikwa katika kitabu cha uzima, alitupwa katika lile ziwa la moto.

1 Wathesalonike 4:13-18

13 Lakini, ndugu, hatutaki msijue habari zao waliolala mauti, msije mkahuzunika kama na wengine wasio na matumaini.

14 Maana, ikiwa twaamini ya kwamba Yesu alikufa akafufuka, vivyo hivyo na hao waliolala katika Yesu, Mungu atawaleta pamoja naye.

15 Kwa kuwa twawaambieni haya kwa neno la Bwana, kwamba sisi tulio hai, tutakaosalia hata wakati wa kuja kwake Bwana, hakika hatutawatangulia wao waliokwisha kulala mauti.

16 Kwa sababu Bwana mwenyewe atashuka kutoka mbinguni pamoja na mwaliko, na sauti ya malaika mkuu, na parapanda ya Mungu; nao waliokufa katika Kristo watafufuliwa kwanza.

17 Kisha sisi tulio hai, tuliosalia, tutanyakuliwa pamoja nao katika mawingu, ili tumlaki Bwana hewani; na hivyo tutakuwa pamoja na Bwana milele.

18 Basi, farijianeni kwa maneno hayo.

1. Hapa ndipo Mungu anapokea watakatifu wake walioshinda dunia.
2. Mianzo ya miaka 1000 nitakutana na wapendwa wetu
3. Tutakutana na ndugu zetu, watoto wetu wazazi wetu, dada zetu kaka zetu, marafiki zetu, washiriki wetu, wapendwa wetu.
4. Wakati mwingine wachungaji tunasimama mbele ya majeneza ya washiriki wetu kwa huzuni tukivumilia tu lakini moyoni machozi mengi yakimwagika.
5. Mianzo ya siku 1000 tutakutana nao tena.
6. Hapa ndipo tutahukumu makabila 12 ya wana wa Israeli.
7. Hapa ndipo yaliyofichwa sasa yatawekwa wazi mbele ya umati wa wote waliokombolewa.

Amos 8:3, 4

3 Tena nyimbo za hekaluni zitakuwa vilio siku ile, asema Bwana MUNGU; mizoga itakuwa mingi; kila mahali wataitupa, wakinyamaza kimya.

4 Lisikieni hili, ninyi mnaopenda kuwameza wahitaji, na kuwakomesha maskini wa nchi,

1. Hapa Mungu atakomesha maovu yote.

2. Wanaonyanyasa wenzao sasa na kununua haki ya wenzao sasa watakoma pamoja asema Bwana wa majeshi.

Ufunuo 14:1-5

1 Kisha nikaona, na tazama, huyo Mwana-Kondoo amesimama juu ya mlima Sayuni, na watu mia na arobaini na nne elfu pamoja naye, wenye jina lake na jina la Baba yake limeandikwa katika vipaji vya nyuso zao.

2 Nami nikasikia sauti kutoka mbinguni, kama sauti ya maji mengi, na kama sauti ya radi kuu. Na hiyo sauti niliyoisikia ilikuwa kama sauti ya wapiga vinubi, wakivipiga vinubi vyao;

3 na kuimba wimbo mpya mbele ya kile kiti cha enzi, na mbele ya wale wenye uhai wanne, na wale wazee; wala hapana mtu aliyeweza kujifunza wimbo ule, ila wale mia na arobaini na nne elfu, walionunuliwa katika nchi.

4 Hawa ndio wasiotiwa unajisi pamoja na wanawake, kwa maana ni bikira. Hawa ndio wamfuatao Mwana-Kondoo kila aendako. Hawa wamenunuliwa katika wanadamu, malimbuko kwa Mungu na kwa Mwana-Kondoo.

5 Na katika vinywa vyao haukuonekana uongo. Maana hawana mawaa.

Sura 24

MAKAO YA WALIOKOMBOLEWA

2 Wafalme 2:1, 2

Ikawa hapo Bwana alipopenda kumpandisha Eliya mbinguni kwa upepo wa kisulisuli, Eliya alitoka Gilgali pamoja na Elisha.

Eliya akamwambia Elisha, Tafadhali, kaa hapa, maana Bwana amenituma niende mpaka Betheli.

1. Saa itafika Mungu hata ruhusu kuona watoto wake wanateseka pia.
2. Kikombe cha uovu kimejaa sasa Mungu hatamvumilia tena shetani na wanadamu waliomchagua.
3. Mungu ni upendo na mwaminifu kwa watakatifu wake.

2 Wafalme 2:3

Elisha akaseam, kama Bwana aishivyo, na roho yako iishivyo, sitakuacha, Basi wakashuka mpaka Betheli. Basi wana wa manabii walikuwako Betheli, wakatoka kuonana na Elisha, wakamwambia je! Unajua ya kuwa Bwana atamwondoa bwana wako leo, asiwe mkubwa wako? Akasema, naam najua nyamazeni.

1. Ukitaka kuingia mbinguni kwanza kubali kutoka Gilgali.
2. Bwana kupenda uingie mbinguni kwanza ni utayari wako.
3. Utayari wako ni kukomesha dhambi maishani mwako.
4. Kaa karibu na watu wenye mausiano na Yesu itakusaidia kiroho.
5. Acha kusikiliza umati hata kama wanaonekana kushika dini.
6. Wanaokuona ona watakumaliza, sikiliza neno la Mungu sio watu.
7. Ukisikiliza watu utakufa kiroho, na kukosa uzima wa milele.

Ufunuo 22:11,12

Mwenye kudhulumu na azidi kudhulumu, na mwenye uchafu na azidi kuwa mchafu, na mwenye haki na azidi kufanya haki, na mtakatifu na azidi kutakaswa.

Tazama naja upesi na ujira wangu u pamoja nami kumlipa kila mtu kama kazi yake ilivyo.

1. Tunapaswa kuishi maisha matakatifu tangu sasa
2. Tuanze kufanya mazoezi ya maisha ya mbinguni mapema,
3. Maisha ya unyenyekevu, maisha matakatifu, tukunyenyekeana. Acha kujiinua.
4. Maana watakatifu tutakuwepo mbinguni
5. Yesu anakuja na ujira mkononi.
6. Jiandae kumlaki mawinguni.

Mbinguni tutawaona Adamu, Nuhu, Enoko, Ibrahimu,Isaka, Yakobo, Rahabu, Yusufu, Musa, Daudi, Eliya, Elisha, Danieli, Petro, Yohana, na wengine wengi hata waliolala mauti katika kizazi chetu tutawaona ikiwa walilala katika Kristo Yesu.

Wahubiri wa injili tuwe kielelezo ili watu wamwone Yesu ndani Yetu ili wamwone Kristo ndani yetu.

1 Wakorintho 11:1 Mnifuate mimi kama mimi ninavyomfuata Kristo.

Wito

Isaya 45:22 Niangalieni mimi, mkaokolewe, enyi ncha zote za dunia; maana mimi ni Mungu; hapana mwingine.

Bwana anahitaji tumtazame yeye ili tupate kuokolewa, hivyo kwa fungu hili hatuna nafasi ya kumtazama mwanadamu.

Kwanini niendelee kuabudu katika nyumba ya ibada isiyofuata maagizo ya Mungu? Nifanye nini ili niokolewe?

Ezekieli 12:1-3

Neno la Bwana likanijia tena, kusema,

2 Mwanadamu, wewe unakaa kati ya nyumba iliyoasi, watu ambao wana macho ya kuona, ila hawaoni, wana masikio ya kusikia, ila hawasikii; kwa maana ni nyumba iliyoasi.

3 Basi, mwanadamu, funga tayari vyombo kwa uhamisho, ukahame wakati wa mchana mbele ya macho yao; nawe utahama toka mahali pako hapa mpaka mahali pengine mbele ya macho yao; labda watafahamu, wajapokuwa ni nyumba iliyoasi.

Usiogope kubadilisha imani baada ya kufahamu kweli za maandiko. Mungu atakushika mkono.

Isaya 41:10 usiogope, kwa maana mimi ni pamoja nawe; usifadhaike, kwa maana mimi ni Mungu wako; nitakutia nguvu, naam, nitakusaidia, naam, nitakushika kwa mkono wa kuume wa haki yangu.

Yesu anatuita tumfuate.

Yohana 1:43 Siku ya pili yake alitaka kuondoka kwenda Galilaya, naye akamwona Filipo. Yesu akamwambia, Nifuate.

Ikiwa una jambo lolote zito gumu liwe la kimwili au la kiroho peleka kwa Yesu maana anatuita tulio na mizigo twende kwake.

Mathayo11:28 Njoni kwangu, ninyi nyote msumbukao na wenye kulemewa na mizigo, nami nitawapumzisha.

Yesu anahitaji wote walio na uhitaji wa kumfahamu.

Mathayo 5:6 Heri wenye njaa na kiu ya haki; Maana hao watashibishwa.

Usione aibu kwenda kwa Yesu maana Yeye ni uzima wetu na anayemwonea Yesu aibu saa itafika Yesu atamkataa

Tujifunze miguuni pake Yesu. Anatuita tujifunze kwake.

Mathayo 11:29 Jitieni nira yangu, mjifunze kwangu; kwa kuwa mimi ni mpole na mnyenyekevu wa moyo; nanyi mtapata raha nafsini mwenu;

HISTORIA YA KANISA LA KUKUTANA SABATO.

Kanisa la Kukutana Sabato lilianzishwa na Mungu tangu Edeni pale Mungu alipoumba kila kitu kisha akamkabidhi mwanadamu vitu vyote ambavyo ni mahitaji ya mwanadamu na aliumba kila kitu kikiwa kimekamilika.

Mwanzo 1:31 Mungu akaona kila kitu alichokifanya, na tazama, ni chema sana. Ikawa jioni ikawa asubuhi, siku ya sita.

Mwanadamu alikuwa wa mwisho kuumbwa, Mungu anapomuumba mwanadamu, anampa jukumu la kutawala vyote vilivyo umbwa kabla yake, pia akaonyeshe taswira ya Mungu maishani mwake.

Mwanzo 1:26 Mungu akasema, Na tumfanye mtu kwa mfano wetu, kwa sura yetu; wakatawale samaki wa baharini, na ndege wa angani, na wanyama, na nchi yote pia, na kila chenye kutambaa kitambaacho juu ya nchi.

Ibada ifanywe kwa Mungu mwenyewe.

Ufunuo 14:7 akasema kwa sauti kuu, Mcheni Mungu, na kumtukuza, kwa maana saa ya hukumu yake imekuja. ***Msujudieni yeye aliyezifanya mbingu na nchi na bahari na chemchemi za maji.***

Ili mwanadamu aabudu alikabidhiwa sabato kama pumziko na siku ya kutafakari neno la Mungu na uumbaji wake.

Waebrania 4:9, 10 Basi, imesalia raha ya sabato kwa watu wa Mungu.

Kwa maana yeye aliyeingia katika raha yake amestarehe mwenyewe katika kazi yake, kama vile Mungu alivyostarehe katika kazi zake.

Baada ya uumbaji na maagizo ya awali kwa watu wake. Bwana alipitisha watu wake ndani ya safina, Safina ilikuwa chujio ya kupitisha watiifu kwa Mungu na wakaidi kuangamia, hivyo Mungu alianzisha tena kanisa lake kupitia Nuhu.

Nuhu na mkewe, Shemu na mkewe, Hamu na mkewe, Yafethi na mkwewe hili ndilo kanisa la Mungu lililonusurika kwenye garika.

Kanisa lilisafiri likiongozwa na Mungu kupitia Makuhani, Manabii, Wazee na Wafalme. Wafalme hawakufanya jambo lolote bila kuuliza kiongozi wa kanisa makuhani au manabii hivyo walifanya kazi kama timu moja.

Katika agano jipya hapakuwepo na dini mbali mbali wala madhehebu ila walikuwepo Wakristo ambao waliabudu siku ya saba ya juma na kuitunza sabato takatifu.

Matendo ya Mitume 16:13 Hata siku ya sabato tukatoka nje ya lango, tukaenda kando ya mto, ambapo tukadhani ya kuwa pana mahali pa kusali; tukaketi, tukasema na wanawake waliokutana pale.

Paulo uliona umuhimu wa utunzaji wa sabato hata wakiwa ugenini walitafuta eneo la ibada.

Hata hivyo utunzaji wa sabato tu haitoshi kulitambulisha kanisa la Mungu.

Isaya anasemaje?

Isaya 8:20 Na waende kwa sheria na ushuhuda; ikiwa hawasemi sawasawa na neno hili, bila shaka kwa hao hapana asubuhi.

Ufunuo 14:12 Hapa ndipo penye subira ya watakatifu, hao wazishikao amri za Mungu, na imani ya Yesu.

Dunia imesafiri kwa miaka mingi na mambo hubadilika na vizazi hutoweka na kuibuka vizazi vipya. Kanisa ilipitia matatizo mbali mbali yaliyojaa mateso Rumi ilitawala dunia kwa miaka mingi na kujaribu kuzima nuru ya Yesu ila haikuwezekana. Watakatifu wa Mungu walidhoofishwa lakini Mungu aliendelea kulinda neno lake lisipotee wala kweli za maandiko matakatifu yasibadilishwe.

Baada ya miaka kupita Mungu anainua watu kama William Miller, Martin Luther na wengine kuanza kuelekeza watu kufanya matengenezo ya dhati.

Mwaka 1843 Mungu aliwainua wahubiri wengi kama William Miller, Joshua Himes, Josepeh Bates, James White na mke wake Ellen White wakahubiri kwa nguvu zao zote wakiongozwa na Roho Mtakatifu.

Mungu anamwita Ellen G. White kama nabii wake ili kuonyesha dira kipindi ambacho giza lilitanda duniani na muda mfupi baada ya kilio cha usiku wa manane na njozi yake ya kwanza ilijulikana kama njia nyembamba (Narrow path).

Kupitia maandiko ya Ellen White ni udhibitisho kuwa Mungu hakuliacha kanisa lake gizani.

Maandiko yote ya Ellen White yamejaa ushuhuda wa Yesu Kristo. Na ndio Roho ya unabii Ufunuo 19:10 sehemu ya mwisho.

Nina kualikaumpokee Yesu Kristo kama Bwana na mwokozi wa maisha yako ili upate kuokolewa Yesu anaporudi tena.

SHUKRANI

1. Niwashukuru sana kwa mwaliko wenu, upendo wenu kwa kuniruhusu kurudi Kiserian.

2. Niwashukuru kwa huduma nzuri na ushirikiano mlionipa wakati wote wa mahubiri.

3. Niwashukuru viongozi wa kundi na washiriki wa Kiserian.

4. Niwashukuru wapishi wote wa nilipokuwa ninaishi, na mkutanoni.

5. Niwashukuru Rehema Baraka na Baraka Mbalazi kwa ukarimu wao na kunipokea nyumbani mwao kwangu nimeona upendo mkuu.

6. Suhukrani kwa wale watu wawili walionikatia tiketi ya ndege ili niwahi mkutano mwingine.

7. Niwashukuru uongozi wa Kiserian kwa ushirikiano na umoja, ulinzi mlionipa.

8. Niwashukuru viongozi wa kanisa la Njiro bila kuwasahau: wazee wa kanisa, mzee Kitururu, Mzee Manjale, Dr Mabula, Chimwejo, Pr Mwamkonda na Pr Nyakirere.

9. Niwashukuru wahudumu wenzangu, wainjilisti waliokuwa wanaenda nyumba kwa nyumba, Ev Japhet Magoti, Pr Benjamin Kola.

10. Nishukuru pia familia yangu kwa maombi wanayoniombea nikiwa huku.

11. Nishukuru pia uongozi wa Mara conference kuniruhusu kuja huku.

12. Nimshukuru sana Mungu kwa afya na ulinzi alionipa kipindi chote.

Kitabu hiki kimeandaliwa kwa kusudi la kufundishia biblia kwa mlei ili afikie hatua ya kufahamu biblia. Unaweza ukakitumia kufundishia darasa la ubatizo, mahubiri ya hadhara na nyumba kwa nyumba, kumtia moyo mgonjwa au mtu yoyote anayepitia matatizo mbalimbali.

Naamini maisha ya kila mtu ni ushuhuda kwa namna yake. Kila Mkristo ana jambo la kumshudia Yesu maishani mwake.

Wasifu wa mwandishi.

Kitabu hiki kimeandaliwa na mchungaji Gerald Yusufu Nyafanga.

Mchungaji Gerald Nyafanga amekuwa mwinjilisti kwa miaka mingi mwenye uzoefu katika nyanja mbalimbali katika uinjilisti akitumika maeneo tofauti tofauti.

Mchungaji Gerald Nyafanga alihitimu katika chuo kikuu cha Bugema kilichopo nchini Uganda mwaka 2017 Bachelor of Religious Studies in Evangelism and Church Growth. Shahada ya dini uinjilisti na ukuaji wa kanisa.

Mchungaji Gerald Nyafanga ni mchungaji mwenye uzoefu wa kuchunga mitaa mbalimbali na amewekewa mikono ya uchungaji katika kanisa la Waadventista Wasabato katika jimbo dogo la Mara.

Shukrani

Nina kila sababu ya kumshukuru Mungu Muumba wa mbingu na nchi kwa namna anavyonitunza na kunilea miguuni pake.

Shukrani kwa familia yangu, mke wangu Joyce kwa ushauri na maombi yake kwangu na kunitia moyo ninapomtumikia Mungu. Maana kila ninapokutana na magumu na hila za adui Shetani yeye hunitia moyo na kuniombea.

Shukrani kwa watoto wangu Jemimah na Abigail ambao huniombea na kunitia moyo kila wakati.

Mungu awabariki.

Ulawiti

Warumi 1:27 wanaume nao vivyo hivyo waliyaacha matumizi ya mke, ya asili, wakawakiana tamaa, wanaume wakiyatenda yasiyopasa, wakapata nafsini mwao malipo ya upotevu wao yaliyo haki yao.

Sabato ilianza lini?

Mwanzo 1:1, 2 Basi mbingu na nchi zikamalizika, na jeshi lake lote.

2 Na siku ya saba Mungu alimaliza kazi yake yote aliyoifanya; akastarehe siku ya saba, akaacha kufanya kazi yake yote aliyoifanya.

Kucheza wakati wa kuimba

Zaburi 47:7 Maana Mungu ndiye mfalme wa dunia yote, Imbeni kwa akili.

1 Wakorintho 10:31 Basi, mlapo, au mnywapo, au mtendapo neno lo lote, fanyeni yote kwa utukufu wa Mungu.

2 Samweli 6:16 Ikawa, sanduku la Bwana lilipoingia mji wa Daudi Mikali, binti Sauli, akachungulia dirishani, akamwona mfalme Daudi akiruka-ruka na kucheza mbele za Bwana; akamdharau moyoni mwake

2Samweli 6:20 Ndipo Daudi akarudi ili awabarikie watu wa nyumbani mwake. Na Mikali, binti Sauli, akatoka nje aende kumlaki Daudi, naye akasema, Mfalme wa Israeli alikuwa mtukufu leo namna gani, akijifunua mwili wake mbele ya vijakazi vya watumishi wake, mfano wa watu baradhuli mmojawapo, ajifunuavyo mwili wake mbele ya watu, asipokuwa na haya!